# FASIRI YA BIBLIA ISIYOGHARAMIWA

UNAWEZA KUIELEWA BIBLIA!

*Tumaini Katika Siku za Dhiki-Pazia la Mwisho*

*Ufunuo*

Na Dr. Bob Utley, Profesa mstaafu wa kanuni za ufasiri (utafasili wa Biblia)

**ORODHA YA YALIYOMO**

Vifupisho Vilivyotumika Katika Fasiri Hii

Neno Toka kwa Mwandishi: Ni kwa Namna Gani Fasihi Inaweza Kukusaidia

Mwongozo Mzuri wa Usomaji wa Biblia:Utafiti Binafsi kwa Ukweli Uliothibitika

**Fasiri:**

Kiambata Muhimu Cha Utangulizi (ni yupi Mkristo Mwenye Tafasiri za Mfumo wa Imani ya Kitabu Cha Ufunuo

Utangulizi wa Unabii wa Agano la Kale

Utangulizi wa Kitabu cha Ufunuo

Ufunuo 1

Ufunuo 2 & 3

Ufunuo 4 & 5

Ufunuo 6 & 7

Ufunuo 8 & 9

Ufunuo 10 & 11

Ufunuo 12 - 14

Ufunuo 15 & 16

Ufunuo 17 & 18

Ufunuo 19

Ufunuo 20

Ufunuo 21 & 22

**Viambatisho:**

Maelezo Mafupi ya Muundo wa Kisarufi wa Kiyunani.

Uhakiki wa Tofauti wa Kiuandishi

Ufafanuzi/Faharasa

Maelezo ya Kimaandiko

Orodha Juu ya Maoni ya Millenia: Ukurasa 1 2 3

Ushairi Juu ya Kitabu Cha Ufunuo

Copyright © 2013 Bible Lessons International. Haki zote zimehifaziwa. Nukuu au usambazaji wowote wa sehemu ya maandishi haya lazima utolewe pasipo malipo yoyote. Nukuu au usambazaji huo lazima pongezi zimwendee mwandaaji Dr. Bob Utley na ikijumuisha nukuu toka www.freebiblecommentary.org

Msingi wa Mandiko ya Kibiblia yaliyotumika katika fasihi hii yametoka katika toleo la: New American Standard Bible (lililoboreshwa, 1995) Copyright ©1960, 1962, 1963, 1968, 1971, 1972, 1973, 1975, 1977, 1995 by The Lockman Foundation, P. O. Box2279, La Habra, CA 90632-2279

# VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA KATIKA FASIRI HII

| | |
|---|---|
| AB | Anchor Bible Commentaries, ed. William Foxwell Albright and David Noel Freedman |
| ABD | Anchor Bible Dictionary (6 vols.), ed. David Noel Freedman |
| ABPS | American Baptist Publication Society |
| AKOT | Analytical Key to the Old Testament by John Joseph Owens |
| ANE | Ancient Near East |
| ANET | Ancient Near Eastern Texts, James B. Pritchard |
| ASV | American Standard Version |
| AV | Authorized Version |
| BAGD | A Greek-English Lexicon of the New Testament and Early Christian Literature, Walter Bauer, 2nd ed. by F. W. Gingrich and Fredrick Danker |
| BDB | A Hebrew and English Lexicon of the Old Testament by F. Brown, S. R. Driver and C. A. Briggs |
| BHS | Biblia Hebraica Stuttgartensia, GBS, 1997 |
| DSS | Dead Sea Scrolls |
| EJ | Encyclopedia Judaica |
| IDB | The Interpreter's Dictionary of the Bible (4 vols.), ed. George A. Buttrick |
| ISBE | International Standard Bible Encyclopedia (5 vols.), ed. James Orr |
| JB | Jerusalem Bible |
| JPSOA | The Holy Scriptures According to the Masoretic Text: A New Translation (The Jewish Publication Society of America) |
| KB | The Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament by Ludwig Koehler and Walter Baumgartner |
| KJV | King James Version |
| LAM | The Holy Bible From Ancient Eastern Manuscripts (the Peshitta) by George M. Lamsa |
| LXX | Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1970 |
| MOF | A New Translation of the Bible by James Moffatt |
| MT | Masoretic Hebrew Text |
| NAB | New American Bible Text |
| NASB | New American Standard Bible |
| NEB | New English Bible |
| NET | NET Bible: New English Translation, Second Beta Edition |
| NIDNTT | New International Dictionary of New Testament Theology (4 vol.s), by Colin Brown |
| NIDOTTE | New International Dictionary of Old Testament Theology and Exegesis (5 vols.), ed. Willem VanGemeren |
| NIV | New International Version |
| NJB | New Jerusalem Bible |

| | |
|---|---|
| NKJV | New King James Version |
| NRSV | New Revised Standard Bible |
| OTPG | Old Testament Passing Guide by Todd S. Beall, William A. Banks and Colin Smith |
| REB | Revised English Bible |
| RSV | Revised Standard Version |
| SEPT | The Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1970 |
| TCNT | The Twentieth Century New Testament |
| TEV | Today's English Version from United Bible Societies |
| $UBS^4$ | United Bible Societies' The Greek New Testament, fourth revised edition |
| YLT | Young's Literal Translation of the Holy Bible by Robert Young |
| ZPEB | Zondervan Pictorial Encyclopedia of the Bible (5 vols.), ed. Merrill C. Tenney |

# NENO TOKA KWA MWANDISHI
# NI KWA NAMNA GANI FASIHI HII ITAKUSAIDIA?

Kutafasiri Biblia ni uwiano wa wastani na wa kiroho ambao unajaribu kumwelewa mwandishi wa kale aliyevuviwa kuandika ili kuwezesha ujumbe wa Mungu uweze kueleweka na kutumiwa katika zama hizi.

Mchakato wa kiroho ni muhimu sana lakini mugumu sana kuelezea. Unahusisha kujitoa na kuwa wazi kwa Mungu. Lazima pawepo na njaa (1) kwa ajili yake (2) ya kumjua yeye na (3) kumtumkia yeye. Mchakato huu unahusisha maombi, ukiri na kuwa tayari kubadili mfumo wa kuishi. Roho Mtakatifu ni wa muhimu sana katika mchakato wa utafasiri, lakini kwa nini wakiristo waminifu, wanaompenda Mungu wanaielewa Biblia tofauti kabisa na kuitafasiri visivyo.

Mchakato wa uwiano huu ni rahisi kuuelezea. Lazima tuwe na msimamo na haki kwa maandiko badala ya kuathiriwa na hali ya upendeleo binafsi au wa ki-madhehebu. Sote tumefungamanishwa ki-historia. Hakuna yeyote mtafasiri miongoni mwetu awezae kubisha. Fahiri hii inatoa kwa uangalifu uwiano ulio sahihi wenye kanuni tatu za tafasiri zilizoundwa kusaidia kudhibiti hali zetu za upendeleo.

## KANUNI YA KWANZA

Kanuni ya kwanza ni kuona muundo wa kihistoria ambao kwayo Biblia iliandikwa na tukio zima la kihistoria katika uandishi wake. Mwandishi wa mwanzo alikuwa na kusudi, ujumbe wa kuwakilisha. Andiko haliwezi kumaanisha kitu kwetu ambacho hakikumaanishwa na ile asili, na mwandishi aliyevuviwa wa zama hizo. Kusudi lake na wala sio mahitaji yetu ki-historia, ki-musisimko, ki-tamaduni na mapokeo ya ki-madhehebu yetu ni—ufunguo.

Matumizi ni mbia mkubwa wa tafasiri, lakini tafasiri sahihi lazima ipate kipaumbele kwa matumizi. Lazima isisitizwe kwamba, kila andiko la Biblia lina tafasiri moja tu, na si vinginevyo. Maana hii ndiyo mwandishi wa mwanzo wa Biblia alivyokusudia akiongozwa na roho kuiwasilisha katika enzi zake. Maana hii moja yaweza kuwa na matumizi anwai, katika tamaduni na mazingira tofauti. Matumizi haya lazima yaambatane na ukweli halisi wa mwandishi wa awali. Kwa sababu hii, mwongozo wa fasiri hii imetayalishwa kwa namna ya kutoa utangulizi kwa kila kitabu cha Biblia.

## KANUNI YA PILI

Kanuni ya pili ni kuibainisha fasihi moja. Kila kitabu cha Biblia ni hati ya kumbukumbu iliyounganishwa. Wafasiri hawana haki ya kutenganisha hoja moja ya ukweli kwa nyingine. Kwa hiyo hatuna budi kujaribu kuelewa kusudi la kitabu kizima cha Biblia kabla ya kutafari fasihi ya kitabu kimoja kimoja. Sehemu moja—sura, aya, au mistari haiwezi kumaanisha ambacho kitabu kizima hakimaanishi. Tafsiri sharti iwiane na mtizamo mzima kuelekea mtimzamo wa sehemu ya vifungu vya Biblia. Kwa hiyo mwongozo huu wa fasiri ya mafunzo haya umelenga kuwasaidia wanafunzi kuchambua muundo wa kila andiko ki-aya. Mgawanyo wa ibara na sura havikuvuviwa bali ni kutusaidia tu ili kubaini mawazo.

Kutafasiri katika ngazi ya aya na sio sentesi, ibara,kifungu au ngazi ya neno ndio ufunguo katika kufuata maana ya mwandishi aliyokusudia. Aya zimejengwa kwenye mada iliyounganishwa pamoja, mara nyingi huitwa sentesi yenye dhamira au mada. Kila neno, kifungu, ibara na sentesi katika aya kwa kiasi fulani vinahusiana na dhamira iliyo pamoja. Aidha haya huweka ukomo, inapanua , kuieleza na/ au kuihoji. Maelekezo sahihi (ufunguo) kwa tafsiri sahihi ni kufuata wazo la mwandishi wa awali aya kwa aya kufuatana na fasihi binafsi ambayo inatengeneza Biblia nzima..Tafsiri hizi zimechaguliwa kwa sababu zinatumia nadharia mbalimbali za tafsiri.

1. Andiko la Kiyunani la United Bible Society ni rekebisho la chapisho la Nne la (UBS$^4$). Andiko hili liliandikwa ki-aya na wasomi wa maandiko ya kisasa.

2. Toleo la New King James Version (NKJV) ni utafsiri wa fasihi wa neno kwa neno uliosimamia kwenye mapokeo ya machapisho ya Kiyunani yaliyojulikana kama “Upokeaji wa Maandishi”. Mgawanyo wa aya zake ni mrefu kuliko tafasiri zinginezo. Urefu wa aya hizi unamwezesha wasomi kuona mada zilizo pamoja.
3. Toleo la New Revised English Version(NRSV) ni tafsiri ya neno kwa neno lililoboreshwa. Inatengeneza pointi ya kati baina ya matoleo mawili ya kisasa yanayofuata. Mgawanyo wa aya zake ni wa msaada mkubwa katika kubainisha masomo.
4. Toleo Today’s English Version(TEV) ni utafsiri sawia wenye nguvu uliyochapishwa na muungano wa vyama vya Biblia. Unajaribu kutafasiri Biblia kwa njia ya kumwezesha msomaji au mnenaji wa kingereza cha kisasa kuelewa maana iliyomo katika andiko la Kigiriki. Mara nyingi, hasa hasa katika injili, inagawanya aya kufuatana na mnenaji hata kuliko somo lenyewe, sawa na NIV. Kwa kusudi la mtafsiri, hili halina msaada. Inapendeza kuona kuwa vitabu vya UBS[4] na TEV vimechapishwa na mtu yule yule lakini aya zake zinatofautiana.
5. The Jerusalem Bible(JB) nii tafsiri sawia yenye mlinganyo wa nguvu iliyosimamia kwenye tafasiri ya Katoriki ya Ufaransa. Ni nzuri mno katika kufanya ulinganifu wa aya kutoka katika mtizamo wa ki-Ulaya.
6. Chapisho la andiko ni uboreshaji wa mwaka 1995 wa toleo la Biblia New American Standard Bible (NASB) ambalo ni tafasili ya neno kwa neno. Pia maoni ya mstari kwa mstari yanafuata aya hizi.

## KANUNI YA TATU

Kanuni ya tatu ni kusoma Biblia tofauti tofauti ili kupata uwezekano mpana wa maana (somo la maana ya maneno) kwamba maneno ya Kibiblia au vifungu yanaweza kuwa nayo. Daima, neno au fungu la maneno katika Kiyunani yanaweza kueleweka kwa njia mbalimbali. Tafsiri hizi tofauti husaidia kubaini na kuelezea utofauti uliopo katika maandiko ya awali ya Kiyunani. Lakini haya hayaathiri mafundisho, bali husaidia katika kujaribu kurejerea maandiko asili yalioandikwa na mwandishi wa kwanza aliyevuviwa.

Fasiri hii humpa mwanafunzi njia ya haraka ya kuchunguza fasiri zake. Hii haina maana kuwa ni ya kumalizia, bali ni ya utoaji taarifa na udadisi kimawazo. Mara nyingi tafsiri nyingine hutusaidia tusiwe ving’ang’anizi na wafinyu wa mawazo na mapokeo ya kimadhehebu. Watafasili wanapaswa kuwa na upana mkubwa wa kuelewa tafsiri tofauti tofauti na kuweza kubaini ni kwa ugumu upi maandiko ya kale yanaweza kuwa. Inashangaza kuona ni kwa kiasi kidogo kilioje cha makubaliano yaliopo kati ya wakristo ambao wanadai kuamini biblia kama chanzo chao pekee cha ukweli. Kanuni hizi zimenisaidia kushinda hali yangu ya kufungwa kihistoria na kunifanya nipambane na maandiko ya zama hizo. Ni matumaini yangu kuwa kanuni hizi zitakuwa za Baraka kwako.

Bob Utley
June 27, 1 996
Haki Miliki © 2013 Bible Lessons International

# MWONGOZO KWA USOMAJI MZURI WA BIBLIA:

# UTAFITI BINAFSI KWA UKWELI ULIOTHIBITIKA

Kinachofuata ni maelezo mafupi ya Dr. Bob Utley mwana falsafa wa kanuni za ufasili na njia alizotumia katika fasihi yake.

Tunaweza kuufahamu ukweli? Unapatikana wapi? Tunaweza kuuthibitisha kimantiki? Kweli, kuna mamlaka ya kimsingi? Kuna imani kamili inayoweza kulinda maisha yetu, na ulimwengu wetu tuliomo? Kuna maana yeyote katika maisha? Kwa nini tuko hapa? Tunakwenda wapi? Maswali haya yanauliza kwa watu wote wenye tafakuri zenye uwiano—wameyatawala maarifa ya binadamu tangu mwanzoni mwa nyakati (Mhu. 1:13-18; 3:9-11). Naweza kukumbuka utafiti wangu binafsi kwa ajili ya ungamanisho la maisha yangu. Nimekuwa mwamini katika Kristo kwenye umri mdogo, awali kabisa nikizingatia juu ya ushahidi wa watu wengine muhimu kwenye familia yangu. Nilivyokuwa kufikia utu uzima, maswali juu yangu na ulimwengu ninamoishi nayo yalikuwa.Tamaduni za kawaida na dini hazikuleta maana yeyote kwenye uzoefu niliousoma au kukutana nao. Ulikuwa ni muda wa kuchanganyikiwa, kutafuta, kutamani, na mara nyingi fikra zisizokuwa na tumaini katika uso wa ulimwengu mgumu, usiojali nilimoishi.

Wengi walidai kuwa na majibu kwa maswali haya ya msingi, lakini baada ya utafiti na kufikiri nikapata majibu yao yamelenga juu ya (1) falsafa binafsi, (2) hadithi za kubuniwa za kale, (3) uzoefu binafsi, au (4) Saikolojia zilizojichomoza. Nilihitaji digrii Fulani ya uthibitisho, baadhi ya vielelezo, kiasi cha busara ambamo ningelenga mtazamo wangu wa kidunia, kiini cha uzima wangu, sababu yangu ya kuishi.

Niliyapata haya katika usomaji wangu wa biblia. Nilianza kutafuta ushahidi wa udhamini nilioupata katika (1) utegemezi wa historia ya biblia kama ulivyothibitishwa na elimu kale, (2) usahihi wa Nabii za Agano la Kale, (3) umoja wa jumbe za Biblia zaidi ya miaka 1600 ya kutolewa kwake na (4) shuhuda binafsi za watu ambao maisha yao yalibadilika moja kwa moja baada ya kusoma biblia. Ukristo, kama mfumo wa imani na kuamini ulioунganishwa, una uweo wa kukabiliana na maswali magumu ya maisha ya mwanadamu. Siyo haya tu yanaweza kutoa muundo kazi, lakini mwelekeo unaotokana na uzoefu wa imani za kibiblia uliniletea furaha zenye hisia na ustahimili.

Nilijiridhisha ya kuwa nimepata kiini cha uzima wa maisha yangu-Kristo, kama ninavyoelewa kupitia maandiko.Ulikuwa ni uzoefu mgumu, msukumo wenye kuweka huru. Ingawa, naweza kukumbuka mshutuko na maumivu yalipoanza kunifahamisha juu ya tafasiri ngapi tofauti ya kitabu hiki zimetetewa, wakati mwingine hata ndani ya makanisa hayo ya aina moja. Nikithibitisha mwongozo wa Ki-Mungu na uaminifu wa biblia haukuwa mwisho, lakini ni mwanzo pekee. Ni kwa vipi naweza kuthibitisha au kukataa tafsiri zinazotofautiana na kugongana za kurasa nyingi ngumu ndani ya maandiko kwa wale waliokuwa wakidai mamlaka yake na uaminifu?

Kazi hii imekuwa lengo la maisha yangu na hija ya imani. Nilifahamu ya kuwa imani katika Kristo imeniletea furaha na amani kubwa. Mawazo yangu yametamani baadhi ya imani kamili katikati ya nadharia ya utamaduni wangu na mfumo wa imani gonganishi wa dini na majivuno ya kimadhehebu. Katika utafiti wangu wa mitazamo halali kwenye utafsiri wa fasihi ya kale, nilishangaa kuvumbua historia yangu, ya kitamaduni, ya kimadhehebu na uzoefu wa kipendeleo. Kwa kawaida kabisa, mara nyingi, nimesoma Biblia ili kuuimarisha mtizamo wangu. Nimeutumia kama chanzo cha mfumo wa imani kuvamia imani nyingine wakati nikijihakikishia usalama wangu na utoshelevu. Ni kwa namna gani utambuzi wa maumivu haya yalikuwa kwangu!

Ingawa siwezi kuwa kipingamizi moja kwa moja, naweza kuwa msomaji mzuri wa biblia. Naweza kuweka ukomo wa upendeleo kwa kutambua na kukubali uwepo wao. Sijawaweka huru,lakini nimeukabiri udhaifu wangu. Mtafsiri mara nyingi ndio adui mbaya wa usomaji mzuri wa biblia! Ngoja nitaje baadhi ya dhanio nilizoleta kwenye usomaji wa biblia ili, msomaji, aweze kuzichunguza pamoja nami:


## I. DHANIO

1. Ninaamini biblia ni uvuvio wa ki-pekee wa ufunuo binafsi wa Mungu mmoja na aliye wa kweli. Kwa hiyo, ni lazima itafsiriwe katika mwanga wa kusudi la Kiuungu la mwandishi wa mwanzo (yaani Roho) kupitia mwandishi wa kibinadamu katika muundo wa historia uliokusudiwa.
   - Wapokeaji wa mwanzo
   - Ujumbe ulioandikwa
   - Kusudi la mwandishi wa mwanzo
2. Ninaamini biblia iliandikwa kwa ajili ya mtu wa kawaida—kwa watu wote! Mungu alilazimika mwenyewe kuongea kwetu waziwazi kupitia historia na tamaduni zilizomo. Mungu hakuuficha ukweli, anatutaka sisi kuelewa! Kwa hiyo, inalazimika kutafsiriwa katika (uwazi) katika siku hizo, na siku hizi tulizomo. Biblia haitakiwi kumaanisha kwetu yale ambayo hayakumaanisha kwa wale wa mwanzo walioisoma au kuiisikia. Inaeleweka kwa wastani wa mawazo ya kibinadamu na kutumia aina ya njeo mbadala za kawaida za mawasiano ya ki-binadamu.
3. Ninaamini Biblia inakusudi na ujumbe uliowekwa pamoja. Haina mkanganyiko ndani yake, ingawa inajumuisha (njia ngumu na zinazokinzana). Hivyo basi, mtafsiri mzuri wa biblia ni biblia yenyewe.
4. Ninaamini kwa kila kurasa (pasipo kujumuisha unabii) ina maana moja iliyosimama kwenye kusudi la mwanzo la mwaandishi aliyevuviwa. Ingawa hatuwezi kutia shaka kutambua kusudi la mwandishi wa mwanzo, viashirio vingi daima vimeelekeza katika uelekeo wake;
   a. Aina ya fasihi tanzu uliochaguliwa kuelezea ujumbe
   b. Mtindo wa kihistoria na/au muda maalumu ulioshawishi maandiko kuandikwa
   c. Muundo wa fasihi wa kitabu husika pamoja na kila fasihi moja
   d. Muundo wa maandishi (elezewa kwa fasaha) wa fasihi moja kama zinavyo husiana na ujumbe
   e. Umbo la kisarufi husika lililowekwa kuwasilisha ujumbe
   f. Maana zilizochaguliwa kuwakilisha ujumbe


Mafunzo ya kila eneo hili liwe chanzo cha mafunzo yetu katika aya. Kabla sijaelezea njia zangu za usomaji mzuri wa biblia, hebu nielezee angalau njia zisizosahihi zinazotumiwa siku hizi zilizopelekea kuwepo kwa tafsiri tofauti nyingi na hivyo basi zinatakiwa kuepukika.

## II. Mbinu zisizofaa

1. Kutojali mazingira ya fasihi ya vitabu vya Biblia na kutumia kila sentesi, ibara, au maneno binafsi kama maelezo ya kweli yasiohusiana na kusudi la mwandishi wa mwanzo au mtindo mpana. Hii mara nyingi huitwa “uhakiki wa andiko”
2. Kutoujali muundo wa ki-hisoria wa vitabu kwa kubadilisha muundo wa ki-historia unaodhaniwa kuwa ni mdogo au usiosaidika kutoka kwenye andiko lenyewe.
3. Kutojali muundo wa kihistoria wa vitabu na kusoma kama gazeti la mtaani lililoandikwa asili kwa wakristo binafsi wa kisasa.
4. Kuupa muundo wa kihistoria wa vitabu kwa kuliistiari andiko ndani ya ujumbe wa falsafa/theolojia isioendana na wasikiaji wa kwanza na kusudi la mwandishi wa mwanzo.
5. Kutojali muundo wa mwanzo kwa kubadilisha mtindo wa theolojia ya mtu, mafundisho yanayopendeka, au mambo ya kisasa yasiyoendana na kusudi la mwandishi wa mwanzo na ujumbe uliotolewa. Tabia hii mara nyingi hufuata usomaji wa mwanzo wa biblia kama kigezo cha kuanzisha mamlaka ya mnenaji. Hii mara nyingi hurejewa kama “mwitikio wa msomaji” (utafsiri wa-andiko-lililomaanisha-kwangu). Kwa wastani, vitu vitatu vinavyoendana vinaweza kupatikana katika mawasiliano ya binadamu yalioandikwa.



Siku za nyuma, mbinu tofauti za usomaji zimenitazamisha juu ya moja kati ya vitu vitatu. Lakini kweli tunatamka kwa dhati uhuisho wa Biblia wa kipekee na mchora uliofanyiwa mabadiliko unaofaa zaidi:




Kwa kweli vitu hivi nyote vitatu lazima vijumulishwe katika mchakato wa ufasihi. Kwa kusudi la uthibitisho, ufasiri wangu unalenga juu ya moja kati ya vitu viwili: muandishi wa mwanzo na maandiko. Ninayamkinika kujibu matusi mabaya niliyoyachunguza (1) shutumu au kutakasa maandiko na (2) tafasili ya "mwitikio wa msomaji" (unamaanishwa nini kwangu).Matusi yanaweza kutokea katika kila hatua. Ni lazima kila mara tuchunguze mienendo yetu, upendeleo wetu, mbinu na matumizi. Lakini ni kwa jinsi gani tunaweza kuyachunguza kama hapatakuwepo na mipaka ya ufasihi, ukomo au kigezo? Hapa ni pale kusudi la mwandishi na muundo wa maandiko yaliponipa baadhi ya vigezo kuzuia maeneo ya fasiri zilizo halali. Katika kuangazia hizi mbinu za usomaji zisizofaa, zipi ni baadhi ya mitazamo mizuri ya usomaji mzuri wa biblia ambao unatoa digri ya uthibitisho na misimamo?

## III. Mitazamo inayofaa katika usomaji mzuri wa Biblia

Katika hatua hii sijadili mbinu pekee za ufasiri wa namna mahususi lakini kwa pamoja kanuni halali kwa aina yote ya maandiko ya kibiblia. Kitabu kizuri kwa namna ya mitazamo mahususi ni *How To Read The Bible For All Its Worth*, ya Gordon Fee na Douglas Stuart, kilichochapishwa na Zondervan.

Utaratibu wangu mwanzoni ulinitizamisha juu ya msomaji aliyemruhusu Roho Mtakatifu kuangaza biblia kupitia kwa miduara minne ya usomaji binafsi. Hii inamfanya Roho, andiko na msomaji wawe kiwango cha mwanzo, na siyo cha juu. Vile vile hii inamlinda msomaji kutokua na mwanya wa kushawishiwa na mtoa maoni. Nimesikia ikisemwa: "Biblia inaangazia zaidi katika fasihi". Hii haimaanishi kukashifu maoni juu ya msaada wa usomaji lakini ni ombi kwa muda unaofaa kwa matumizi yao. Tunalazimika kuusaidia ufasiri wetu kutoka katika andiko lenyewe. Maeneo matatu yanatoa angalau ukomo wa uthibitisho:

1. muundo wa kihistoria
2. mazingira ya fasihi
3. muundo wa kisarufi (vipashio)
4. matumizi ya maneno ya kisasa
5. milango muhimu iliyo sambamba
6. namna au tanzu

Tunahitajika kuweza kutoa sababu na mantiki zilizo nyuma ya ufasii wetu. Biblia ndiyo chanzo pekee cha imani yetu na mazoezi. Kwa huzuni, mara nyingi wakristo hawakubali juu ya kile kinachofundishwa au kukiri. Ni kushindwa kudai uhuisho juu ya Biblia na kupelekea waamini washindwe kukubali juu ya kile kinachofundishwa na kutakiwa! Miduara mine ya usomaji imeundwa kutupatia utambuzi wa ufasili ufuatao:

### 1. Mduara wa kwanza wa usomaji

a. Soma kitabu katika mkao mmoja. Soma tena katika fasili tofauti , kwa matumaini kutoka katika fasili tofauti za nadharia
   1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
   2) Mlinganyo wenye nguvu (TEV, JB)
   3) Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
b. Angalia kiini cha kusudi la uandishi mzima. Tambua dhamira yake.

c. Tenga (ikiwezekana) fasihi moja, sura, ibara au sentesi inayoelezea waziwazi Kiini cha kusudi au dhamira
d. Tambua fasihi tanzu yenye nguvu
   1) Agano la kale
      a) Simlizi za waebrania
      b) Mashahiri ya waebrania (fasihi za hekima, zaburi)
      c) Unabii wa ki-Ebrania (lugha ya mjazo, shairi)
      d) Alama za siri za ki-sheria
   2) Agano jipya
      a) Simlizi (Injili, matendo)
      b) Hadithi za mafumbo (Injili)
      c) Barua/nyaraka
      d) Fasihi za mafunuo

## 2. Mduara wa pili wa usomaji

a. Soma kitabu kizima tena, ukitafuta kufahamu mada muhimu au masomo.
b. Elezea kwa muhtasari wa mada muhimu na elezea kwa kifupi yaliomo kwa maelezo rahisi
c. Angalia kusudi la maelezo yako na eleza kwa mapana kwa msaada wa usomaji.

## 3. Mduara wa tatu wa usomaji.

a. Soma tena kitabu kizima, ukitafuta kutambua muundo wa ki-historia na Matukio lengwa kwa ajili ya uandishi kutoka katika kitabu cha Biblia yenyewe.
b. Taja vipengele vya ki-historia ambavyo vinatajwa katika kitabu cha Biblia.
   1) Mwandishi
   2) Tarehe
   3) Wapokeaji
   4) Kusudu mahsusi la uandishi
   5) Mwelekeo muundo wa kitamaduni unaorandana na kusudi la mwandishi
   6) Marejeo toka kwenye matukio na watu wa kihistoria/ kale
c. Panua maelezo yako kwa kiwango cha aya kutoka katika sehemu ya kitabu cha biblia unayotafasiri. Mara nyingi tambua na kuelezea fasihi. Inaweza kuwa na vifungu na aya nyingi. Hii inakuwezesha wewe kufuata wazo na muundo wa maandiko ya mwandishi wa mwanzo.
d. Angalia muundo wako wa kihistoria kwa kutumia msaada wa usomaji

## 4. Mduara wa nne wa usomaji

a. Soma tena bayana fasihi moja katika tafasiri nyinginezo nyingi
   1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
   2) Mwenendo linganifu (TEV, JB)
   3) Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
b. Angalia fahisi au muundo wa kisarufi
   1) Misemo ya kujirudia Waefeso.1:6, 12, 14
   2) Muundo wa kisarufi unaojirudia Warumi 8:31
   3) Mbinyo wa mawazo (dhana zinazoafikiana)
c. Taja vipengele vifuatavyo:-
   1) Isahili muhimu
   2) Istahili zisizo za kawaida
   3) Muundo muhimu wa kisarufi
   4) Maneno magumu, ibara, na sentesi
d. Angalia njia muhimu zilizosambamba
   1) Angalia njia za wazi za ufundishaji kwenye somo lako kwa kutumia
      a) Vitabu vya thiolojia
      b) Biblia za marejeo
      c) Itifaki

2) Angalia maneno mawili yanayokinzana katika somo lako. Kweli nyingi za ki-Biblia zinatolewa katika rahaja mbili zinazofanana. Migongano mingi ya ki-madhehebu hutokea kutokana na uthibitisho nusu wa maandiko ya Biblia. Biblia zote zimevuviwa. Ni lazima tutafute ujumbe mzima ili kutoa mlinganyo wa ki-maandiko katika tafasiri zetu.
3) Angalia milinganisho ndani ya kitabu, kilekile, mwandishi Yule Yule, au namna ileile, Biblia ina mfasiri wake mzuri kwa sababu ina mwandishi mmoja ambaye ni Roho Mtakatifu.

e. Tumia misaada ya kusoma kuangalia uchunguzi wako wa muundo wa kihistoria na tukio.
1) Soma biblia
2) Ensaikolopidia za biblia, vitabu vya mkononi na kamusi
3) Tangulizi za biblia
4) Fasihi za biblia (katika hatua hii kwenye usomaji wako ruhusu jamii ya waamini, waliopita na waliopo, kusaidia na kusahihisha usomaji wako binafsi)

## IV. Matumizi ya utafasiri wa Biblia.

Katika hatua hii tunageukia matumizi, umechukua muda kuelewa andiko katika muundo wake, sasa lazima utumie katika maisha yako, utamaduni wako, na elezea mamlaka ya Ki-biblia kama "uelewa ule mwandishi wa ki-biblia wa mwanzo alivyosema katika zama zake na kutumia ukweli huo katika zama hizi". Matumizi lazima yafuate utafasiri wa kusudi la mwandishi wa mwanzo katika muda na mantiki.

Hatuwezi kutumia njia ya Biblia katika zama zetu mpaka pale tutakapo fahamu kile alichokuwa akikisema katika zama hizo. Njia ya Biblia isimaanishe kile asicho kimaanisha!
Maelezo yako kwa kirefu, kwa kiwango cha aya (mzunguko wa usomaji≠3) yatakuwa mwongozo wako. Matumizi lazima yafanyike katika kiwango cha aya, na sio kiwango cha neno, maneno yana maana pekee katika mazingira, ibara zina maana pekee katika mazingira na sentensi zina maana pekee katika mazingira. Mtu pekee aliyevuviwa ambaye amejumuishwa katika mchakato wa utafsiri ni mwandishi wa mwanzo. Kipekee unafuata utangulizi wake kwa mwanga wa Roho Mtakatifu. Lakini nuru sio uvuvio. Kusema "asema Bwana"lazima, tufungamane na kusudi la mwandishi wa mwanzo. Matumizi lazima yaendane bayana na kusudi lote la uandishi mzima, maandishi bayana, na muendelezo wa kiwango cha aya.

Usiruhusu mambo ya zama hizi yatafasiri Biblia, iruhusu Biblia ijiongee yenyewe. Hii itatuhitaji kuvuta kanuni kutoka kwenye andiko. Hii itakubalika kama andiko litaiwezesha kanuni. Bahati mbaya wakati mwingi kanuni zetu ni "zetu" na si kanuni za ki-maandiko.

Katika kutumia Bibilia, ni muhimu kukumbuka kuwa (isipokuwa katika unabii) maana moja na moja pekee itakubalika kwa andiko la Kibiblia pekee. Maana hiyo iendane na kusudi la mwandishi wa mwanzo kama alivyo eleza tatizo au hitaji katika zama zake. Mengi ya matumizi yanayowezekana yanaweza kutolewa kutoka katika maana hii moja. Matumizi yatategemea mahitaji ya wapokeaji lakini ni lazima yaendane na maana ya mwandishi wa mwanzo.

## V. Sura ya utafasiri wa kiroho.

Zaidi ya hapo nimejadili mantiki na mchakato wa ki-maandiko uliojumuishwa kwenye utafasiri na matumizi. Sasa ngoja nijadili kwa kinaga ubaga mwelekeo wa kiroho wa utafasiri. Mfuatano ufuatao umekuwa wa msaada sana kwangu.

1. Omba kwa ajili ya msaada wa Roho (kama vile 1Kor. 1:26-2:16)
2. Omba kwa ajili ya msaada binafsi na kusafishwa kutoka katika dhambi inayojulikana (rkama vile 1 Yohana 1:9)
3. Omba kwa ajili ya hamu kubwa ya kumjua Mungu (kama vile Zab. 19:7-14, 42:1, 119:1)
4. Tumia utambuzi wowote mpya mara moja katika maisha yako.
5. Baki mnyenyekevu na anayefundishika.

Ni vigumu kuweka mlinganyo kati ya mchakato wa kimantiki na uongozi wa kiroho wa Roho Mtakatifu. Dondoo zifuatazo zimesaidia kulinganisha hizi mbili:

1. Kutoka kwa mwandishi James W.Sire, *scripture twisting*,kr. 17-18
   "Nuru huja kwenye mawazo ya watu wa Mungu na sio tabaka la watu wa kiroho. Hakuna daraja la ualimu katika ukristo wa kibiblia. Hakuna kuongoza, hapana mtu awaye yote ambaye tafsiri zote nzuri zitoke kwake. Na hivyo, wakati roho mtakatifu anatoa karama maalumu ya hekima, maarifa na utambuzi wa kiroho huwa pamoja. Hakutoa hizi kwa wakristo waliokirimiwa kuwa wao ndo pekee watafsiri wenye mamlaka ya Neno lake. Ni juu ya kila watu wake kujifunza, kuamua na kutambua kwa kufanya marejeo kwenye Biblia ambayo inasimama kama yenye mamlaka hata kwa wale ambao Mungu amewapa uwezo pekee. Kwa kufupisha, wazo mnalofanya kupitia kitabu kizima ni kuwa Biblia ni ufunuo wa kweli wa Mungu kwa watu wote, ya kuwa ni mamlaka yetu ya mwisho katika mambo yote ambayo inayaongelea, kuwa sio fumbo lote lakini inaweza kueleweka vya kutosha na watu wa kawaida kwa kila tamaduni."
2. Juu ya Kierkegaard, inayopatikana toka kwa Benard Ramm, *Protestant Biblical Interpretation (tafsiri ya biblia ya ki-protestanti*) Uk.75:
   Kutokana na Kierkegaard, kisarufi, misamiati na usomaji wa kihistoria wa Biblia ulikuwa ni muhimu lakini utangulizi wa usomaji wa kweli wa Biblia na kusoma Biblia kama neno la Mungu mmoja lazima alisome kwa moyo wake wote mdomoni mwake, kutoka ncha ya kidole, na shauku ya matarajio katika mazungumzo na Mungu. Usomaji wa Biblia pasipo tafakari, kutojali au kielimu, au weledi sio usomaji wa Biblia kama neno la Mungu, kama mmojawapo asomavyo barua ya mapenzi isemavyo, tena mmoja asoma kama neno la Mungu.
3. H.H Rawley katika *The Relevance of the Bible*, Uk.19:
   Hakuna uelewa mdogo wa kisomi wa Biblia, ingawa yote, inaweza kumiliki hazina yote. Haidharau uelewa huo, kwa kuwa ni muhimu kwa uelewa wote. Lakini ni lazima iongeze uelewa wa kiroho wa hazina ya kiroho ya kitabu hiki kwa ujumla. Kwa huo uelewa wa kiroho kitu Fulani ambacho ni zaidi ya hadhari ya kiroho ni muhimu. Mambo ya kiroho ni utambuzi wa kiroho, na wanafunzi wa Biblia wanahitaji fikra za upokeaji wa kiroho. Ile hamu ya kumtafuta Mungu ambayo inaweza kumsababisha ajitoe kwake. Ni kama kupita zaidi ya usomaji wa kisayansi kuingia kwenye urithi wa utajiri wa hiki kitabu kikubwa kuliko vyote.

## VI. Njia hizi za Fasiri

*Study Guide Commentary (Mwongozo wa usomaji) wa* fasihi umeundwa kusaidia njia zako za utafsiri katika njia zifuatazo:

1. Maelezo fasaha ya kihistoria yanayotambulisha kila kitabu baada ya kufanya "mduara wa usomaji #3" angalia taarifa hizi.
2. Utambuzi wa ki-mazingira unapatikana katika kila kurasa. Hii itakusaidia kuona jinsi gani maandishi/fasihi imeundwa.
3. Katika kila mwanzo wa kifungu au fasihi kubwa inaunganisha mgawawanyo wa aya na maelezo ya kichwa cha makala yanatolewa kutoka katika tafsiri za kisasa.
   a. United Bible Society Greek Text.Toleo la nne lililobadilishwa (UBC)
   b. The New American Standard Bible 1995 ya kisasa (NASB)
   c. The New King James Version (NKJV)
   d. The New Revised Standard Version (NRSV)
   e. Today's English Version (TEV)
   f. The Jerusalem Bible (JB)

Aya zilizogawanywa hazikuvuviwa. Lazima ziyakinishwe kutoka katika mazingira fulani. Kwa kulinganisha tafsiri nyingi za kisasa kutoka tafsiri nyingi za ki-nadharia na mitizamo ya kitheolojia, tunaweza kuchanganua muundo unaokusudiwa wa mawazo ya mwandishi wa mwanzo, kwani kila aya ina ukweli mmoja mkubwa. Huu uliitwa "mada ya sentensi" au wazo la kati la andiko, hilo wazo lililounganishwa ni ufunguo kwa tafsiri nzuri ya kihistoria na kisarufi. Mmojawapo asitafsiri, kuhubiri au kufundisha chini ya aya, vilevile ukumbuke ya kuwa kila aya inahusiana na aya zingine. Hii ndo maana kiwango cha aya kinachoelezea kitabu kizima ni muhimu. Ni lazima tuweze kufuata mtiririko wa kimantiki wa somo lililotolewa na mwandishi wa mwanzo aliyevuviwa.

4. Muhtasari wa Bob unafuata mtazamo wa kifungu kwa kifungu kwa utafsiri wake. Hii inatulazimisha kufuata mawazo ya mwandishi wa mwanzo. Muhtasari unatoa habari kutoka sehemu nyingi.
   a. Mazingira ya fasihi

   b. Utambuzi wa kihistoria na tamaduni
   c. Habari za kisarufi
   d. Usomaji wa neno
   e. Njia muhimu zilizo sambamba
5. Mahali Fulani katika fasihi, andiko lililochapishwa toka toleo jipya la Marekani (1995 mpaka sasa hivi) litaongezewa na tafsiri za matoleo mbalimbali ya kisasa.
   a. New King James Version (NKJV) ambayo unafuata mswaada wa "Upokeaji wa Maandiko halisi".
   b. The New Revised Standard Version (NRSV) ambayo ni rudio la neno-kwa-neno Kutoka katika Umoja makanisa asili ya Revised Standard Version
   c. The Today's English Version (TEV) ambayo ni tafsiri ya mlinganyo wa nguvu Kutoka American Bible Society.
   d. The Jerusalem Bible (JB) ambayo ni tafsiri ya Kiingereza inayotegemea kutoka tafsiri ya Mlinganyo wa nguvu wa Katoriki ya Ufaransa.
6. Kwa wale wote ambao hawasomi ki-giriki, ukilinganisha na tafsiri za kiingereza inaweza kusaidia kutambua matatizo katika andiko:
   a. Tofauti za mswada
   b. Maana ya maneno mbadala
   c. Muundo na maandiko magumu ya kisarufi Ingawa tafsiri za kiingereza haziwezi kuleta suluhu kwenye matatizo hayo yanayalenga kama sehemu ya ndani na usomaji kamili.
   d. Karibia kila kifungu, maswali muhimu ya majadiliano yanatolewa ambayo yanajaribu kulenga maswala muhimu ya utafsiri wa kifungu hicho

# MADA MAALUMU: UTABIRI WA BAADAE WA AGANO LA KALE DHIDI YA UTABIRI WA AGANO JIPYA ("UTANGULIZI WA MUHIMU" WA UFUNUO)

Katika miaka ya masomo yangu ya elimu juu ya siku za mwisho wa nchi nimegundua kwamba Wakristo wengi hawana au hawapendi mtiririko, ulioboreshwa, ulioendelea unaoonesha nyakati za mwisho. Kuna Wakristo wenye mlengo mkubwa wa eneo hili la Ukristo kwa ajili ya theolojia, saikolojia, au sababu ya kidhehebu. Wakristo hawa wanaonekana kusumbuliwa sana na namna gani jambo hili litaisha, na kwa namna fulani kukosa ule umaana wa Injili! Waamini hawawezi kuathiri ajenda ya Mungu juu ya mwisho wa nchi, lakini wanaweza kushiriki katika mamlaka ya Injili (rejea Mathayo. 28:19-20; Luka 24:46-47; Matendo ya Mitume 1:8). Waamini wengi wanakiri kuja kwa mara ya Pili kwa Kristo na kule kutimilizwa kwa mwisho kwa ahadi za Mungu. Tatizo la kiutafsiri linainuka kutoka katika namna ya kuelewa kutimilizwa huku kutoka katika utata kadhaa wa kibiblia (rejea Mada Maalum: Utata katika Maandiko ( Special Topic: Paradox in Scripture)

1. Mvutano kati ya mifano ya kinabii ya Agano la Kale na mifano Mipya ya Kitume ya Agano jipya.
2. Mvutano kati ya Uungu mmoja wa Biblia (Mungu mmoja kwa ajili ya wote) na kuchaguliwa kwa Israeli (watu maalumu)
3. Mvutano baina ya kipengele cha sharti cha agano na ahadi za kibiblia ("ikiwa…basi") na uaminifu usio na masharti wa Mungu kwa ukombozi wa binadamu aliyeanguka
4. Mvutano kati ya aina ya uandishi wa Mashariki ya Karibu na mifano ya uandishi wa kimagharibi
5. Mvutano kati ya Ufalme wa Mungu wa sasa na ujao.
6. Mvutano kati ya imani katika kurudi kwa Kristo na imani kwamba matukio kadhaa lazima yatokee kwanza.

Naomba tujadili mivutano hii moja baada ya nyingine.

**MVUTANO WA KWANZA** (Agano la Kale, kabila, utaifa na kipengele cha jiografia dhidi ya waamini wote dunia nzima).Manabii wa Agano la Kale walitabiri juu ya urejesho wa Ufalme wa Kiyahudi katika Palestina iliyo katikati ya Yerusalemu ambapo mataifa yote ya dunia yatakusanyika kumsifu na kuutumikia utawala wa Daudi, lakini si Yesu wala Mtume yoyote wa Agano jipya aliwahi kuweka msisitizo katika ajenda hii. Si uvuvio wa Agano la Kale (rejea Mathayo 5:17-19)? Je waandishi wa agano jipya wameondoa sehemu matukio muhimu yanyakati za mwisho?

Kuna vyanzo kadhaa vya taarifa kuhusu mwisho wa ulimwengu.

1. Manabii wa Agano la Kale (Isaya, Mika, Malaki)
2. Waandishi wa mambo ya mwisho wa nchi wa Agano la Kale (rejea Ezekieli 37-39; Daniel 7-12; Zakaria)
3. Waandishi wa kati ya maagano, waandishi wayahudi wa siku za mwisho wasio wakanoni (kama I Enoch kinachosemekana kilitakiwa kifuate baada ya Yuda)
4. Yesu mwenyewe (rejea Mathayo 24; Marko 13; luka 21)
5. Nyaraka za Paulo (rejea 1 Wakorintho 15; 2 Wakorintho 5; 1 Wathesalonike 4-5; 2 Wathesalonike 2)
6. Nyaraka za Yohana (1 Yohana na Ufunuo)

Je haya yote yanatufundisha kwa hakika ajenda ya mwisho wa nchi (matukio, mfululizo, watu)? Kama sio kwanini? Je si yote kuwa yamevuviwa (isipokuwa maandishi ya kati ya maagano ya Kiyahudi).Roho alifunua ukweli kwa waandishi wa Agano la Kale kwa namna na sehemu ambayo wangeelewa. Hata hivyo, kupitia ufunuo endelevu roho alipanua dhana hii ya Agano la Kale juuya siku za mwisho wan chi katika namna pana ("maajabu ya Kristo," rejea Waefeso 2: 11-3:13). Ifuatayo ni baadhi ya mifano inayoendana:

1. Jiji la Yerusalemu katika Agano la Kale imetumika kama ulinganifu kwa watu wa Mungu (Sayuni),lakini inatajwa katika Agano Jipya kama neno linaloelezea kupokelewa na Mungu kwa watubuo wote, wanadamu waaminio ("Yerusalemu Mpya" ya Ufunuo 21-22). Maana kubwa zaidi ya kithiolojia iliyokuzwa ya jiji linavyoonekana kuwa watu wapya wa Mungu (Wayahudi waaminio na Mataifa) inatajwa kwa mbele katika ahadi za Mungu kukomboa binadamu aliyeanguka katika Mwanzo 3:15, kabla hata hapajawa na

Muyahudi yoyote au Mji mkuu wa Kiyahudi. Hata wito wa Ibrahimu (rejea 12:1-3) ulihusisha mataifa (rejea Mwanzo 12:3; Kutoka 19:5) angalia Mada Maalumu: Mpango wa Ukombozi wa Milele wa YHWH.

2. Katika Agano la Kale, maadui wa watu wa Mungu ni mataifa yaliyozunguka Mashariki ya karibu, lakini katika Agano Jipya wamekuza kwa wasioamini wote, wampingao Mungu, watu wenye uvuvio wa kishetani. Vita imehamishwa kutoka kijiografia, migogoro ya kikanda kwenda ulimwenguni kote, mgogoro wa kiulimwengu (rejea Wakolosai).
3. Ahadi ya ardhi ambayo ni sehemu ya Agano la Kale ( ahadi ya Mwanzo, rejea 12:7 13:15; 15:7,15, 16; 7:8) sasa imekuwa dunia nzima. Yerusalemu mpya inashuka chini kwa nchi iliyoumbwa tena, sio Mashariki ya Karibu tu au kinginecho (rejea Ufunuo 21-22).
4. Baadhi ya mifano mingine ya ya dhana za kinabii ya Agano la Kale inayokuzwa
   a. Mbegu ya Ibrahimu sasa imetahiriwa kiroho (Warumi 2:28-29)
   b. (rejea Hosea 1:10; 2:23, ikinukuliwa kutoka Warumi 9:24-26; pia Walawi. 26:12; Kutoka 29:45, imenukuliwa kutoka 2 Wakorintho 6:16-18 and Kutoka 19:5; Kumbukumbu la torati 14:2, imenukuliwa katika Tito 2:14)
   c. Hekalu sasa ni Yesu (rejea Mathayo 26:61; 27:40; Yohana 2:19-21) na kupitia yeye kanisa la nyumbani (rejea 1 Wakorintho 3:16) au kwa mwamini mmoja mmoja (rejea 1 Wakorintho 6:19)
   d. Hata Israel na tabia za zinazofunua maneno ya Agano la Kale sasa zinamaanisha watu wote wa Mungu (kama vile “Israeli,” rejea Warumi 9:6 Wagalatia 6:16, kama “Ufalme wa Makuhani," rejea 1 Petro 2:5, 9-10; Ufunuo 1:6)

Mifano ya kinabii imekuwa ikitimizwa, ikikuzwa, na sasa ikujumuisha. Yesu na waandishi wa Kitume hawawasilishi nyakati za mwisho kama ile ya manabii wa Agano la Kale (rejea Martin Wyngaarden, *The Future of The Kingdom in Prophecy and Fulfillment)* watafsiri wa kisasa wanaojaribu kutengeneza mifano ya Agano la Kale au kugeuza kimaarifa ya kitabu cha Ufunuo kwenda katika kitabu cha Kiyahudi na kulazimisha maana isiyoeleweka, yenye utata kauli za Yesu na Paulo! Waandishi wa Agano Jipya hawawakatai manabii wa Agano la Kale,lakini huonesha kilele cha walichomaanisha kwa ujumla. Hakuna mfumo uliopangwa katika mwisho wan chi kunakozungumzwa na Yesu au Paulo. Kusudi lao kimsingi kabisa ni kiukombozi au kichungaji.

Hata hivyo ndani ya Agano Jipya kuna mvutano. Hakuna mfumo rasmi wa wazi wa matukio ya siku za mwisho. Katika namna nyingi kwa mshangao mkubwa Ufunuo unatumia dhana za Agano la Kale katika kuelezea mwisho badala ya mafundisho ya Yesu (rejea Mathayo 24; Marko 13)! Inafuata namna ya uandishi ulioanzishwa na Ezekieli, Danieli, na Zakaria, lakini ilikua wakati wa katia ya Agano la Kwanza na Jipya (fasihi ya Kiyahudi ya nyakati za mwisho wa nchi). Hii ilikuwa najia ya Yohana ya kuunganisha Agano la Kale na Jipya. Inatazama taratibu za nyakati za kale ya uasi wa mwanadamu na kujithatiti kwa Mungu katika ukombozi! Lakini hata hivyo lazima izingatiwe kwamba ingawa Ufunuo unatumia lugha ya Agano la Kale, watu na matukio, inayatafsiri katika ufahamu wa karne ya kwanza ya Rumi(rejea Ufunuo 17).

## **MVUTANO WA PILI** (Hali ya uwepo wa Mungu mmoja dhidi ya watu wateule)

Msisitizo wa Kibiblia upo kwa my mmoja, roho, muunmbaji-mkombozi, Mungu(rejea Kutoka 8:10; Isaya 44:24; 45:5-7,14,18,21-22; 46:9; Yeremia 10:6-7). Upekee wa Agano la Kale katika siku zake lenyewe ilikuwa ni hali ya Mungu mmoja (angalia Mada Maalumu: Hali ya Uwepo wa Mungu mmoja( Special Topic: Monotheism).Mataifa yote yazungukayoyalikuwa yakiabudu miungu mingi. Umoja wa Mungu ndio moyo wa Ufunuo wa Agano la Kale (rejea Kumbukumbu la Torati 6:4) uumbaji ni eneo kwa ajili ya kusudi la ushirika kati ya Mungu na mwanadamu, aliyeumbwa kwa sura na mfano wake(rejea Mwanzo 1:26-27). Hata hivyo, mwanadamu aliasi, atatenda dhambi dhidi ya upendo wa Mungu, uongozi, na kusudi (rejea Mwanzo 3). Upendo wa Mungu na kusudi lilikuwa kubwa sana na hakika kuwa alihaidi kukomboa uanadamu ulioanguka (rejea Mwanzo 3:15)!

Mvutano unaanza pale Mungu anapochagua kumtumia mtu mmoja, familia moja, taifa moja kufikia wanadamu wengineo. Uchaguzi wa Mungu wa Ibrahimu (Mwanzo 12; 15; 17; 18) na Wayahudi kama ufalme wa Makuhani (rejea Kutoka 19:4-6) ulisababisha kiburi badala ya huduma, kubaguana badala ya kujumuika kwa pamoja. Wito wa Mungu kwa Ibrahimu ulijumuisha kusudio la kubariki wanadamu wote (Mwanzo 12:3). Lazima ikukmbukwe na

isisitizwe kwamba kuchaguliwa kwa Agano la Kale ilikuwa ni huduma, sio wokovu. Waisraeli wote hawakuwa sawa machoni pa Mungu, kamwe si kuokolewa kwa msingi wa haki ya uzaliwa (rejea Yohana 8:31-59; Mathayo 3:9), lakini kwa imani binafsi na utii (Mwanzo. 15:6, imenukuliwa kutoka Warumi. 4:3,9,22; Wagalatia 3:6). Israeli ilipoteza kusudi lake (kanisa kwa sasa ndio ufalme wa makuhani, rejea Ufunuo 1:6; 1Petro 2:5,9) na kugeuza mamlaka katika neema, huduma katika msimamo maalumu! Mungu alichagua mmoja kuchagua wote!

## **MVUTANO WA TATU** (maagano yenye masharti dhidi ya maagano yasiyo na masharti)

Kuna mvutano wa kithiolojia au kugawanyika kati ya maagano yasiyo na masharti na yenye masharti. Ni kweli hakika kabisa kuwa kusudi/mpango wa ukombozi wa Mungu si wa masharti (rejea Mwanzo 15:12-21). Hata hivyo, mwitikio wa kimamlaka wa mwanadamu siku zote huwa ni wa masharti! Ule utaratibu wa "iwapo…ndipo"inaonekana katika vitabu vyote Agano la Kale na Agano Jipya. Mungu ni mwaminifu; mwanadamu si mwaminifu.Mvutano huu umesababisha hali ya kutoelewana isiyo ya kawaida. Watafsiri wamejifanya kuegemea upande mmoja tu "pembe ya kutoelewa vizuri," uaminifu wa Mungu au juhudi za mwanadamu, Ukuu wa Mungu au utashi huru wa mwanadamu. Zote ni za Kibliblia na muhimu. Angalia Mada Maalumu: Kuchaguliwa/kuandaliwa kabla kwa Hatima na Uhitaji wa Ulali Sawa wa Kithiolojia (Special Topic: Election/Predestination and the Need of Theological Balance)

Hii ina husiana na siku za mwisho wa nchi, kwenda kwenye ahadi za Mungu za Agano la Kale kwa Waisraeli. Iwapo Mungu alihaidi, basi hiyo inatosha! Mungu anafanya kazi kwa ahadi zake; heshima yake huusika (rejea Ezekieli 36:22-38). Maagano yenye masharti na yale yasiyo na masharti hukutana na Kristo (rejea Isaya 53), sio Israeli! Kilele cha uaminifu wa Mungu kiko katika wa ukombozi wa wote watakao tubu na kuamini, si kwa kigezo cha nani alikuwa baba yako au mama yako! Kristo, sio Israeli ndio msingi wa Maagano yote ya Mungu na ahadi. Kama kuna sehemu ya mabano katika thiolojia katika Biblia, sio Kanisa, bali Israeli (Matendo ya Mitume 7 na Wagalatia 3).

Kusudi la ulimwengu la kutangaza Injili limekabidhiwa kwa Kanisa (rejea. Mathayo 28:19-20; Luka 24:47; Matendo ya Mitume 1:8). Hili ni sharti na kiagano! Hii haimaanishi Mungu amewakataa kabisa Wayahudi (rejea Warumi 9-11). Kunawezekana kukawa na sehemu na kusudi kwa ajili ya siku za Mwisho, kuamini kwa Israeli (rejea Zakaria 12:10)

## **MVUTANO WA NNE** (mifano ya kiuandishi ya Mashariki ya karibu dhidi ya ile ya Kimagharibi)

Aina ya uandishi ni kipengele muhimu sana katika kuitafsiri Biblia kwa usahihi (angalia Fee and Stuart, *How To Read the Bible For All Its Worth*). Kanisa lilikua katika mazingira ya kiutamaduni wa kimagharibi (Kigiriki). Fasihi ya Mashariki ina mafumbo mengi sana zaidi, inatumia ulinganifu wa vitu visivyofanana, na yenye ishara kuliko ya kisasa, mifano ya utamaduni wa Kimagharibi (angalia Mada Maalumu: Fasihi ya ki-Mashariki (Utata wa Kibiblia(Special Topic: Eastern Literature(Biblical Paradoxes) Inaweka mkazo kwa watu, makabiliano, na matukio zaidi ya ukweli kamili unaopendekezwa. Wakristo wamekuwa katika hukumu ya kutumia historia yao wenyewe na mifano ya kiunadishi kutafsiri unabii wa Kibiblia (yote Agano la Kale na Agano Jipya). Kila kizazi na ujumla ya kijiografia umetumia desturi, historian a ukawaida kutafsiri Ufunuo. Kila mmoja wao alikosea! Ni majivuno kufikiria kuwa desturi ya kimagharibi ndio mahali pa kuanzia pa unabii wa kibiblia.

Aina ya uandishi ambayo kwa asili, imevuviwa mwandishi kuchagua kuitumia kuandika ni mkataba na msomaji (Bruce Corley). Kitabu cha Ufunuo sio hadithi ya Kihistoria. Ni mkusanyiko wa barua (Sura ya 1-3), unabii, na zaidi sana maandishi yanayozungumza juu ya mwisho wa nchi. Ni makosa kuifanya Biblia iseme zaidi ya kilichokusudiwa na mwandishi wa asili ambayo ni sawa na kuifanya iseme chini ya yale yaliyokuwa yamekusudiwa! Majivuno wa Watafsiri na misingi yao ya kiimani si ya kuweka kabisa katika kitabu kama cha Ufunuo.

Kanisa halijawahi kukubaliana kuhusu tafsiri sahihi ya Ufunuo. Ninachotamani ni kusikia na kujishughulisha na biblia nzima, si vijisehemu tu. Ufahamu wa Biblia wa Kimashariki unawasilisha ukweli katika namna za safu za mivutano. Hali yetu ya Kimagharibi kuelekea ukweli unaopendekezwa sio kwamba haufai, bali hauna ulali wa usawa! Nafikiri inawezekana saa nyingine kuondoa angalau baadhi ya vifuniko katika kutafsiri Ufunuo kwa kuzingatia kusudi la kubadilika kwake kwenda kwa vizazi vinavyofuata vya waaminio. Ni wazi kwamba watafsiri

wengi kuwa Ufunuo lazima utafsiriwe katika ufahamu wa siku zake na aina ya uandishi wake. Namna ya kihistoria ya kuelezea Ufunuo lazima izingatie nini wasomaji wa kwanza wangekuwa nacho, na wangeelewa. Kwa namna nyingi watafsiri wa kisasa wamepoteza maana ya ishara nyingi za kitabu. Lengo la kwanza la Ufunuo ilikuwa ni kuwatia moyo waamini wanaopitia dhiki. Inaonesha namna Mungu anavyoshughulikia Historia (kama alivyofanya kwa manabii wa Agano la Kale); ilikubali kuwa historia inaelekea kwenye muda ulioteuliwa, hukumu au Baraka (kama ilivyokuwa kwa Manabii wa Agano la Kale). Ilikubalika katika namna ya karne ya kwanza ya kiyahudi ya siku za mwisho za upendo wa Mungu, uwepo, nguvu na ukuu.

Inafanya kazi kwa namna hiyohiyo kithiolojia kwa kila kizazi cha waaminio. Inaelezea mapambano ya kiulimwengu ya wema na uovu. Maelezo ya karne ya kwanza yanaweza yakawa yalitupoteza, lakini si kweli zenye nguvu na zifarijizo. Pale watafsiri wa kisasa wa kimagharibi wanapojaribu kulazimisha maelezo ya Ufunuo kwenda kwenye historia yao ya sasa, utaratibu wa tafsiri za uongo huendelea!

Inawezekana kwamba maelezo ya kitabu yanaweza yakarudi kwa kasi kuwa kawaida (kama ilivyokuwa Agano la Kale ikilinganisha kuzaliwa, maisha na kifo cha Kristo) kwa kizazi cha mwhisho cha waaminio wanapokabiliana na kutishiwa kifo na kiongozi mpinga Mungu (rejea 2 Wathesalonike 2) na desturi. Hakuna anayefahamu kutimilizwa kwa kawaida kwa Ufunuo mpaka maneno ya Yesu (rejea. Mathayo 24; Marko 13; and Luka 21) na Paulo (rejea. 1 Wakorintho 15; 1 Wathesalonike 4-5; na 2 Wathesalonike 2) pia yatapokuwa halisi kihistoria. Kubashiri, kubuni buni na kukaa katika imani za kidhebehu si sawa. Fasihi ya mwisho wa nchi inaruhusu huku kubadilika. Mshukuru Mungu kwa ajili ya taswira na ishara zinazopita hadithi za kihistoria! Mungu yupo kazini; Yeye anatalawa; Anakuja!

Watoa maoni wengi wa kisasa wanakosa sehemu muhimu ya aina hii ya uandishi! Watafsiri wa kimagharibi wa Kisasa mara nyingi hutafuta mtiririko mzuri wa kueleweka wa kithiolojia badala ya kuwa sawa na utata, ishara na aina ya uandishi ya kitamthiliya ya Kiyahudi ya fasihi ya siku za mwisho. Kweli hii inaelezwa vizuri na Ralph P. Martin katika makala yake, "Approaches to New Testament Exegesis," katika kitabu *New Testament Interpretation*, kilichohaririwa na I. Howard Marshall:

“Mpaka tutakapotambua ubora wa kitamthiliya wa maandiko haya na kurejea katika namna ambayo lugha inavyotumika kama njia ya kuelezea ukweli wa kidini, tutakosea sana katika kufahamu mambo ya siku za mwisho, na kimakosa tunajaribu kutafsiri maono yake kama vile sasa noo kitabu cha mabo ya kawaida tu na chenye lengo la kufunua matukio yanayojulikana na historia yenye taarifa. Kujaribu kufanya jambo hili la mwisho ni kuingia katika kila namna ya matatizo ya kiutafsiri. Na zaidi sana inapelekea upotevu wa maana muhimu ya siku za mwisho na hivyo kuppotea thamani kubwa ya ukuu wa Mungu katika sehemu ya Agano jipya kama tamko la Kitamthiliya katika lugha ya kishairi ya uungu ya Uungu wa Mungu na Kristo na mgongano wa utawala wake unaochanganya ukuu na upendo (Ufunuo 5:5,6; the Lion is the Lamb)" (ukurasa wa 235).

W. Randolph Tate katika kitabu chake cha *Biblical Interpretations* (Tafsiri za Kibiblia):

“Hakuna aina ya uandishi mwingine wa Biblia iliyosomwa kwa dhati sana kwa matokeo yanatokatisha tama kama vitabu vinavyoongelea mwisho wan chi kama vitabu vya Danieli na Ufunuo. Aina hii ya uandishi ilidhoofika kutokana na historia mbovu ya tafsiri zisizo sahihi kutokana na kukosa uelewa wa msingi wa aina yake ya kifasihi, muundo na kusudi. Kwasababu ya tamko hilo kufunua kile kinachotakiwa kutokea kwa muda mfupi, siku za mwisho zimekuwa zikichukuliwa kama ramani ya njia na mpango wa siku zijazo. Kosa baya ya kuchukuliwa huku ni ile dhana kwamba namna ya rejea ya vitabu iko katika nyakati anazoishi msomaji wa wakati huo badala ya wakati anaoishi mwandishi. Kwenda kwa namna hii kwa bila muongozo kwa siku za mwisho (haswa Ufunuo) inazifanya kazi kana kwamba ni lugha ya siri au fumbo ambalo matukio ya sasa yanaweza kutumiak kutafsiri ishara za maandiko. Kwanza, mtafsiri lazima atambue kwamba vitabu vya siku za mwhisho vinawasilisha ujumbe wake kupitia viwakilishi vya kiishara. Kutafsiri viwakilishi kikawaida wakati inalinganisha vitu ni kukosea katika kutafsiri. Jambo kubwa sio kama matukio katika siku za mwisho ni ya kihistoria. Matukio yanaweza yakawa ya kihistoria;yanaweza yakawa kuwa yalitokea, au yatatokea lakini mwandishi anawasilisha matukio na anazungumza maana kupitia taswira na namna hizo” (ukurasa wa 137).

Kutoka katika *Dictionary of Biblical Imagery*, edited by Ryken, Wilhost and Longman III:

“waasomaji wa leo mara nyingi wamefumbwa na wanachanganyikiwa na aina hiii ya uandishi. Taswira isiyotarajiwa na mambo yaliyo nje ya ulimwengu huu yanaleta giza na kutoka nje katika maandiko mengi. Ukichukulia maandiko haya kwa thamani ya usoni inawaacha wasomaji wengi wakihangaika kutafuta kujua ‘itatokea nini iwapo,’ kwahiyo kupoteza lengo la ujumbe wa siku za mwisho” (ukurasa wa 35)

## **MVUTANO WA TANO** (ufalme wa Mungu kwa sasa na baadaye)

Ufalme wa Mungu ni sasa, na baadaye. Hali hii ya mtafaruku wa kithiolojia inalengwa katika siku za mwisho wa nchi. Kama hakuna anayetegemea kutimilizwa kwa nabii zote za Agano la Kale kwa Waisraeli hivyo Ufalme unakuwa haswa kurejeshwa kwa Israeli katika eneo lao la Kijiografia na kuheshimiwa kabla kwa thiolojia! Hii ingesababisha kuwa kanisa lingekuwa limetwaliwa katika Sura ya 5 na Sura zinazobaki zihusiane na Israeli (ila zingatia Ufunuo 22:16).

Hatahivyo kama lengo ilikuwa katika ufalme kuanzishwa na Mesiya aliyahaidiwa na Agano la Kale, halafu ipo na kuja kwa Kristo kwa mara ya kwanza, na alafu lengo linakuwa kuwa hai tena, maisha, mafundisho, mauti, na ufufuo wa Kristo. Mkazo wa kithiolojia upo katika wokovu wa sasa. Ufalme umekuja, Agano la Kale linatimilizwa kwa Kristo kujitoa kwa jili ya wokovu kwa wote, siyo Yeye kutawala milele juu ya wengine!

Ni kweli ya uhakika kuwa Biblia inazungungumzia kuja kote kuwili kwa Kristo, lakini msisitizo unawekwa wapi zaidi? Inaonekena kwangu kwamba unabii mwingi wa Agano la Kale linalenga kwenya kuja kwa mara ya kwanza, kuanzishwa kwa ufalme wa kimasiya (rejea Daniel 2). Katika Agano la Kale mkazo upo kwenye kutawala milele kwa Mungu, na namna ya kushihirishwa huko kwa utawala ni huduma ya Masiya (rejea 1 Wakorintho 15:25-27). Sio swali la kipi ni kweli; yote ni kweli, lakini mkazo upo wapi? Lazima isemwe kwamba baadhi ya Watafsiri wanajikita sana kwenye kutawala milele kwa Masiya (rejea ufahamu wa kumuktadha kwenye Ufunuo 20) kwamba wamepoteza shabaha ya kibiblia kwenye kutawala milele kwa Baba. Kutawala kwa Kristo ni tukio la utangulizi. Kuja kwa Kristo kote hakukuwa wazi katika Agano la Kale, wala kutawala kwa muda kwa Masiya!

Msingi wa kuhubiri kwa Yesu na kufundisha ni ufalme wa Mungu. Ni vyote (wokovu na huduma), na baadae (katika kuendelea na nguvu). Ufunuo kama shabaha yake ni utawala wa kimelenia wa Masiya (rejea Ufunuo 20), ni utangulizi, sio kilele (Ufunuo 21-22). Haiku wazi katika Agano la Kale kwamba utawala wa Muda ni muhimu; kwa kusema kweli, kutawala kwa Masiya kwa Danieli 7 ni milele, si kwa kwa millennia.

## **MVUTANO WA SITA** (kurudi kwa Kristo kunakotarajiwa dhidi ya kuchelewa kurudi mara ya pili)

Waaminio wengi wamefundishwa kwamba Yesu anakuja hivi karibuni, punde na bila kutegemea (rejea. Mathayo 10:23; 24:27,34,44; Marko 9:1; 13:30; Ufunuo 1:1,3; 2:16; 3:11; 22:7,10,12,20; angalia Mada Maalumu: Kurudi Punde (Special Topic: Soon Return). Lakini kila kizazi kilichotegemea kilikuwa kimekosea! Uharaka (mapema) wa kuja kwa Yesu ahadi yenye nguvu ya tumaini la kila kizazi, lakini uhalisia ni kwa mmoja (na huyo ni Yule apitiaye dhiki). Waaminio laziima waishi kama vile Anakuja kesho, lakini waweke mipango na kufanyia kazi Agizo Kuu (rejea Mathayo 28:19-20) kama akikawia. Baadhi ya vifungu katika Injili na Wathesalonike wa 1 na 2 yamejikita kwenye kukawia kwa Kuja kwa Mara ya Pili (Parousia). Kuna matukio ya kihistoria ambayo lazima yatimie kwanza;

1. Kuhubiriwa kwa ulimwengu wote ( rejea Mathayo 24:14; Marko 13:10)
2. Kufunuliwa kwa “mwanadamu mwenye dhambi” (rejea Mathayo 24:15; 2 Wathesalonike 2; Ufunuo 13)
3. Dhiki kuu (Mathayo 24:21,24; Ufunuo 13)

Kuna utata wa kimakusudi (rejea Mathayo 24:42-51; Marko 13:32-36)! Ishi kila siku kama vile ndiyo siku yako ya mwisho ila panga na pata mafunzo kwa ajili ya huduma ya baadaye!

## UTHABITI NA USAWA

Lazima isemwe kwamba shule mbalimbali za utafsiri wa matukio ya siku za mwisho yote yana ukweli nusu. Wanaelezea na kutafsiri vyema baadhi ya vifungu. Tatizo linakuja katika kuendelea na kutafuta ulali wa usawa.

Mara nyingi kuna mapendekezo yanayotumia vifungu vya Biblia kujazilizia katika mifupa ya kithiolojia zilizoandaliwa. Biblia haifunui mfuatano mzuri, mpangilio wa siku za mwisho. Ni kama albamu ya picha ya familia. Picha zile ni za kweli ila haziko katika mpangilio, mazingira na katika mfuatano. Baadhi ya picha zimeanguka kutoka nje ya albamu na kizazi kingine cha wanafamilia hawajui namna ya kuzirudisha tena. Msingi wa kupata tafsiri sahihi ya Ufunuo ni lengo na mwandishi wa awali kama ilivyofunuliwa katika aina ya uandishi wake. Watafsiri wengi sana wanajaribu kubeba vifaa vyao na taratibu zao kutoka katika aina ya uandishi wa Agano Jipya kwenda katika Tafsiri zao za Ufunuo. Wanaweka shabaha zao katika Agano la Kale badala ya kuruhusu mafundisho ya Yesu na Paulo kutengeneza muundo wao wa kithiolojia na kuacha Ufunuo uwe kama kielelezo.

Lazima ni kubali kuwa nakabili maoni haya ya Ufunuo kwa hofu na uoga, si kwasababu ya laana ya Ufunuo 22:18-19, lakini kwasababu ya kiwango cha mgongano na kutofautiana kwa tafsiri ya kitabu hiki uliosababishwa na kuendelea kusababisha katika ya watu wa Mungu. Napenda Ufunuo wa Mungu. Ni kweli pale ambapo wanadamu wote ni waongo (rejea Warumi 3:4)! Tafadhali tumia Maoni haya kama jaribio la kuamsha mawazo na sio kutoa maana, kama kibao cha kukuonesha uendapo na sio ramani ya barabara, kama "vipi ingekuwa," nana sio "hilo ndilo neno la Bwana." Nimekutana uso kwa uso na mapungufu yangu mimi mwenyewe, upendeleo na ajenda za kithiolojia. Nimeona pia zile za Watafsiri wengine. Inakuwa inaonekana watu wanatafuta katika Ufunuo wanachokitegemea kikipata. Aina yenyewe ya uandishi inapelekea matumizi mabaya! Hata hivyo, ipo katika Biblia kwa makusudi. Kimewekwa kama "neno" la hitimisho na sio kwa ajali au bahati mbaya. Kina ujumbe wa Mungu kwa watoto Wake wa kila kizazi. Mungu anataka tuelewe! Hebu tuungane, sio kutengeneza vijiwe; tukubali yale yaliyo ya kweli, wazi na yenye dhamira kuu, sio yale yanayoweza kuwa au kufanyika kuwa ya kweli. Mungu atusaidie sisi sote!

# MADA MAALUMU: UNABII WA AGANO LA KALE

## I. UTANGULIZI

A. Maelezo ya Ufunguzi

1. Jamii ya waaminio haiamini namna ya ya kutafsiri unabii. Kweli zingine zimekwisha weka wekwa bayana kama ilivyo kwa nafasi ya Waorthodox katika karne nyingi, lakini si katika karne hii.
2. Zipo hatua kadhaa za unabii wa Agano la Kale
   a. Premornarchial (Kabla ya utawala wa Kifalme)
      (1) Watu binafsi walioitwa manabii
         (a) Abraham – Mwanzo 20:7
         (b) Musa – Hesabu 12:6-8; Kumbukumbu la Torati 18:15; 34:10
         (c) Aaron – Kutoka 7:1 (Msemaji wa Musa)
         (d) Miriam – Kutoka 15:20
         (e) Medad na Eldad – Hesabu 11:24-30
         (f) Deborah – Waamuzi 4:4
         (g) Wasiokuwa na majina – Waamuzi 6:7-10
         (h) Samweli - 1 Samweli 3:20
      (2) Rejea ya manabii kama kundi – Kumbukumbu la Torati 13:1-5; 18:20-22
      (3) Kundi la Kinabii au ushirika – 1 Samweli 10:5-13; 19:20; 1 Wafalme 20:35, 41; 22:6, 10-13; 2 Wafalme 2:3,7; 4:1, 38; 5:22; 6:1, nakadhalika.
      (4) Masiya aitwaye nabii – Kumbukumbu la Torati 13:1-5; 18:20-22
         a. utawala wa kifalme usioandikwa (wakimlenga mfalme);
            (1) Gadi – 1 Samweli 22:5; 2 Samweli 24:11; 1 Mambo ya Nyakati 29:29
            (2) Nathan – 2 Samweli 7:2; 1 Wafalme 1:22
            (3) Ahijah – 1 Wafalme 11:29
            (4) Yehu – 1 Wafalme 16:1, 7, 12
            (5) Wasiotajwa – 1 Wafalme 18:4, 13, 22
            (6) Eliya – 1 Wafalme 18- 2 Wafalme 2
            (7) Mikaya – 1 Wafalme 22
            (8) Elisha 2 Wafalme 2:9, 12-13
         b. Maandiko ya kale ya manabii (yanayo lenga taifa pamoja na mfalme); Isaya – Malaki (isipokuwa Danieli)

## B. ISTILAHI ZA KIBIBLIA

1. *Ro'eh* = "muonaji" (BDB 906, KB 1157), 1 Samweli 9:9. Rejea hii yenyewe inatuonesha mpito kutoka katika neno nabi. Ro'eh inatokana na istilahi ya jumla "kuona." Mtu huyu alizielewa njia za Mungu na mipango yake na aliulizwa kutambua mapenzi ya Mungu katika jambo lolote.
2. *Hozeh* = "muonaji"(BDB 302, KB 3011), 2 Samweli 24:11. Ni jamii ya neon lenye maana sawa na Ro'eh. Inatokana na neno "kuona." Njeo ya wakati uliopita ya neno hili ni"tazama" ambalo limetumika mara nyingi ikimaanisha manabii.
3. Nabi' = "nabii" (BDB 611, KB 661), inayohusiana na lugha ya Akkadia ya kitenzi *Nabu* = "kuita" na kiarabu *Naba'a* = "kutangaza". Hili ni neon limetajwa mara nyingi katika Agano la kale kumaanisha nabii. Limetumika zaidi ya mara 300. Asili kabisa haijulikana kwa hakika japo "kuita" kwa wakati huu inaonekana kama mbadala mzuri zaidi. Yawezekana uelewa mzuri zaidi unatoka YHWH's yanayoeleza mahusiano ya Musa kwa Farao kupitia Haruni. (rejea kutoka 4:10-16; 7:1; Kumbukumbu la torati 5:5). Nabii ni mtu anayezungumza kwa niaba ya Mungu kwa watu wake. (Amosi 3:8; Jeremia 1:7,17; Ezekieli 3:4).
4. Istilahi zote tatu zinatumika katika huduma ya Nabii katika 1 Mambo ya Nyakati 29:29; Samueli – *Ro'eh*; Nathan – *Nabi*' and Gadi – *Hozeh.*

5. Kifungu cha maneno, *'ish ha – 'elohim*, "Mtu wa Mungu" pia ni namna pana ya kumaanisha msemaji wa Mungu. Inatumika mara 76 katika Agano la Kale kwa kumaanisha "nabii"
6. Neno "Nabii" kwa asili ni la Kigiriki. Inatokana na neno (1) *pro* = "kabla" au "kwa niaba ya" na (2) *phemi* = "kuzungumza."

## II. MAANA YA UNABII

A. Neno unabii lilikuwa pana kimaana katika lugha ya kiebrania kuliko Kingereza. Vitabu vya historia vya Yoshua, Wafalme (isipokuwa Ruth) vinatajwa na Wayahudi kama "Manabii waliopita". Wote Ibrahimu (Mwanzo 20:7; Zaburi. 105:15) and Moses (Kumbukumbu la Torati 18:18) wanatajwa kama Manabii (pia Miriam, Kutoka 15:20). Kwahiyo kuwa makini unapokuwa unatazama maana kutoka katika lugha ya Kingereza!

B. "Unabii kisheria kabisa waweza kusema ni ule uelewa wa historia unaokubali maana zile tu zinazohusiana na uungu, kusudi la kiungu, ushirika wa kiungu," *Interpreter's Dictionary of the Bible*, toleo la. 3, ukurasa wa. 896.

C. "Nabii si mwanafalsafa au mwana taaluma ya Theolojia, bali msaidizi wa agano aletaye neno la Mungu kwa watu wake ili kutengeneza hatima zao kwa kufanya mageuzi ya siku zao za sasa," <u>Prophets and Prophecy</u>, *Encyclopedia Judaica* toleo la. 13 ukurasa wa. 1152.

## III. KUSUDI LA UNABII

A. Unabii ni njia ya Mungu kuzungumza na watu wake, kuwapa miongozo katika mazingira yao ya sasa na tumaini katika kuyaendesha maisha yao na matukio ya duniani. Ujumbe wao ulikuwa wa jumla. Ilikusudiwa kuonya, kutia moyo, kuhamasisha imani na toba, na kuwafahamisha watu wa Mungu kuhusu Mungu mwenyewe na mipango yake. Iliwashikilia watu wa Mungu katika maagano na Mungu. Katika hili inatakiwa iongezwe kuwa mara nyingi imekuwa ikitumika kufunua uchaguzi wa Mungu wa wasemaji (Kumbukumbu la Torati 13:1-3; 18:20-22). Hii ukiipa umaanani kabisa utagundua ilimaanisha Mesiya

B. Mara nyingi nabii aliichukua historia na migongano ya kithiolojia ya siku zake na kuangazia hayo katika mazingira ya matukio ya siku za mwisho. Namna ya muono huu wa siku za mwisho kihistoria katika Israel ni wa kipekee na katika hali yakeya uchaguzi wa kiungu na ahadi za kiagano.

C. Ofisi ya nabii inaonekana kutengeneza usawa (Yeremia 18:18) na kuchukua ofisi ya Kuhani Mkuu kama njia ya kufahamu mapenzi ya Mungu. Urimm na Thummim inabadilika katika ujumbe wa mdomo kutoka kwa msemaji wa Mungu. Ofisi ya nabii inaonekana pia kupita mbali katika Israeli baada ya Malaki. Haitokei mpaka baada ya miaka 400 baadae kwa Yohana Mbatizaji. Haieleweki namna ambavyo kipawa cha "unabii" kwa Agano Jipya kinavyoshabihiana na Agano la Kale. Manabii wa Agano Jipya (Matendo ya Mitume 11:27-28; 13:1; 15:32; 1 Wakorintho. 12:10,28-29; 14:29,32,37; Waefeso. 4:11) sio vifunuo vya ufunuo mpya au maandiko, bali wasimulizi wa yajayo na wazungumzaji wa mambo ya mbele ya mapenzi ya Mungu katika hali za agano.

D. Unabii hauna msingi sana au hausisitizi katika utabiri kwa asili. Utabiri ni njia mojawapo ya kutthibitisha ofisi yake na ujumbe wake, ila lazima izingatiwe "chini ya asilimia 2% ya unabii wa Agano la Kale ni kuhusu wa kimasiya". Chini ya asilimia 5% kiuhalisia inafunua nyakati za Agano Jipya. Chini ya asilimia 1% inahusu matukio yajayo. "fee na Stuart, *How to Read the Bible For All Its Worth*, ukurasa wa 166).

E. Manabii wanamwakilisha Mungu kwa watu, wakati Makuhani wanawawakilisha watu kwa Mungu. Haya ni maelezo ya jumla. Kuna utofauti kwa kama Habakkuki, ambaye anauliza maswali kwa Mungu.

F. Sababu moja inayoleta ugumu kuwaelewa manabii ni kwasababu hatujui muundo wa vitabu vyao. Havina mfuatano unaoeleweka. Vinaonekana ni vyenye hoja na mada kweli lakini si kama vile mtu angetegemea. Mara nyingi hakuna mazingira ya wazi ya kihistoria wala muda maalumu, au mgawanyiko wa wazi wa mambo ya kiungu. Vitabu hivi ni vigumu
   1. Kuvisoma kwa mara moja
   2. Kufafanua kwa mada

3. Kug’amua kweli kuu au kusudio la mwandishi katika kila uungu.

## IV. TABIA ZA UNABII

A. Katika Agano la Kale inaonekana kukua kwa dhana ya “nabii” na “unabii”. Hapo mwanzo katika Israeli kulitokea ushirika wa manabii, ukiongozwa na viongozi shupavu wenye uvuvio wa Mungu kama Eliya na Elisha. Kuna wakati neno “wana wa manabii,” ilitumika kuzungumzia kundi hili (II Wafalme 2). Manabii walikuwa na tabia ya kujawa na furaha ya kupiliza (1 Samweli 10:10-13; 19:18-24)

B. Hata hivyo kipindi hiki kilipita mara kwa manabii mmmoja mmoja. Kulikuwa manabii (wa kweli na waongo) waliojitambulisha pamoja na mfalme, na waliishi katika Kasri la Kifalme (Gad, Nathan). Pia, kulikuwa na wale waliojitegemea, wakati mwingine wasiokuwa na hadhi kabisa za jamii ya ki-Israeli (Amos) walijumuisha wote wanawake na wanaume (2 Wafalme 22:14)

C. Nabii mara nyingi alikuwa mfunuaji ya hatima, anayefanya katika mazingira ya mwanadamu yanavyoenda. Mara nyingi jukumu la nabii ilikuwa ni kufunua mpango wa Mungu kwa uumbaji wake ambao hauathiriwi na mwitikio wa kibinadamu. Huu mpango wa wa ulimwengu wa matukio ya mwisho wa nchi ni wa kipekee katika manabii wa Mashariki ya Karibu ya kale. Utabiri na Agano ni mapacha waendao pamoja katika ujumbe wa kinabii (rejea Fee na Stuart, ukurasa wa 150). Hii inamaanisha manabii husisitiza ujumuishwaji katika lengo. Siku zote, japo si kila eneo, hujielekeza katika kuambia taifa.

D. Mambo mengi ya kinabii yakitolewa kwa njia ya kinywa. Baadae iliunganishwa kwa njia ya mada, mfululizo, au namna nyingine ya uandishi wa Mashariki ya Karibu ambao imepotea huku kwetu. Kwakuwa ilikuwa kwa njia ya kinywa, haikuwa na muundo kama unaokuwa katika kazi iliyo andikwa. Hii inafanya vitabu kuwa vigumu kusoma na ngumu kuelewa bila kuwa na historia ya mazingira halisi.

E. Manabii walitumia namna kadhaa kuwasilisha jumbe zao
   1. Matukio ya kimahakama – Mungu anawapeleka watu wake mahakamani, mara nyingi ni kesi ya kutalikiana ambapo YHWH anamkataa mke wake (Israeli) kwasababu ya kukosa uaminifu wake (Hosea 4; Micah 6).
   2. Mazingira ya msiba – mzani haswa kwa jaili ya ujumbe wa namna hii na tabia zake “ole” inajitenga kama aina yake kivyake vyake (Isaiah 5; Habbakkuk 2)
   3. Matamko ya Agano la Baraka - asili ya masharti ya Baraka imesisitizwa na madhara yake, yote ya wema na ubaya, yanatajwa kwa ajili ya baadae (Kumbukumbu la Torati 27-28).

## V. MIONGOZO YA KUKUSAIDIA KATIKA KUTAFSIRI UNABII

A. Tafta kujua lengo la kwanza la nabii (mwandishi) kwa kuzingatia mazingira ya kihistoria na muktadha wa maandishi ya kiungu.

B. Soma na tafsiri mambo yote, sio sehemu tu; fafanua na yaliyomo. Angalia inavyoshabihiana na mazingira ya unabii. Jaribu kufafanua kitabu kizima.

C. Endelea na kufanya makisio ya utafsiri wa kawaida wa hadithi mpaka vitu katika habari vikuelekeze katika matumizi yaliyofichwa kimaana; hivyo badili lugha iliyofichwa katika maandishi.

D. Fafanua matendo ya kiishara katika ufahamu wa mazingira ya kihistoria na usambamba wa hadithi. Kuwa na uhakika wa kukumbuka maanadishi ya kale ya Mashariki ya Karibu si kama yale ya kisasa ya kimagharibi.

E. kuwa mwangalifu wa utabiri
   1. Je unahusisha siku za mwandishi?
   2. Je uliwahi kutimia katika historia ya Israeli?
   3. Je ni kweli yamekwisha kuwa matukio yajayo?
   4. Je yana kutimizwa kwa sasa nab ado yanasubiri kutimizwa siku zijazo?
   5. Waruhusu waandishi wa Biblia wakuongoze katika majibu na sio waandishi wa kisasa.

F. Vitu vya kuzingatia
   1. Je utabiri umekidhi kigezo cha sharti la mwitikio

2. Kuna uhakika kwa Yule ambaye unabii umemlenga? (Na kwa nini)?
3. Je kuna uwezekano, wa kibiblia na/au kihistoria, wa kutimia mara mbili?
4. Waandishi wa Agano Jipya, chini ya uvuvio waliweza kumuona mesiya katika sehemu nyingi katika Agano la Kale kiasi ambacho hakipo kwetu. Wanaonekana kutumia aina hii ya mchezo. Kwakuwa hatujavuviwa basi ni bora tukawaachia utaratibu huu wao.

## VI. VITABU VYA KIMSAADA


A. *A Guide to Biblical Prophecy* by Carl E. Amending and W. Ward Basque
B. *How to Read the Bible for All Its Worth* by Gordon Fee and Douglas Stuart
C. *My Servants the Prophets* by Edward J. Young
D. *Plowshares and Pruning Hooks: Rethinking the Language of Biblical Prophecy and Apocalyptic* by D. Brent Sandy
E. *New International Dictionary of Old Testament Theology and Exegesis*, vol. 4, pp. 1067-1078
F. *The Language and Imagery of the Bible* by G. B. Caird

# UTANGULIZI WA UFUNUO

## Maelezo ya ufunguzi

A. Wakati mwingi wa maisha yangu ya utu uzima ya taaluma/thiolojia nilikuwa na dhana kuwa wale wanaoiamini Biblia huichukulia "kawaida" (na huo ndo ukweli wa masimulizi ya kihistoria). Ingawa imekuwa wazi zaidi kwamba kwangu kuufanya unabii, ushairi, maandiko yanayotabiri mwisho wa dunia kawaida ni kukosa uvuvio uliokusudiwa wa andiko hilo. Kusudio la Mwandishi na sio ukawaida wa maandiko ndio ufunguo wa kuielewa Biblia katika usahihi wake. Kuifanya Biblia iseme zaidi (kubainisha mafundisho ya kidhehebu) ni hatari sana na ni upotoshaji kuitafsiri katika namna ambayo itafanya iseme kidogo kuliko ilivyokusudiwa mwanzoni na mwandishi aliyevuviwa. Lengo linatakiwa kuwa na muktadha mpana, mazingira ya kihistoria na lile kusudio lililoainishwa na mwandishi katika andiko na katika uchaguzi wake wa mbinu ya uwasilishaji. Namna ya uwasilishaji ni makubaliano ya kifasihi kati ya mwandishi na msomaji. Kutolielewa jambo hili hakika hupelekea katika upotoshaji wa tafsiri sahihi.

> Kitabu cha ufunuo sio masimulizi ya kihistoria bali ukweli wa uhakika ambao hautakiwi kuchukuliwa kawaida kawaida. Namna ya uwasilishaji wenyewe kinapaza sauti kutwambia jambo hili iwapo tutakuwa tayari kusikia tu. Hii haina maana kuwa hakina uvuvio au kuwa si kweli bali ni vile tu kiko kitamathali, kimefumbwa kimaana, kimetumia lugha ya ishara, chenye ulinganifu na taswira. Wayahudi na wakristo wa karne ya kwanza walielewa sana aina hii ya maandiko kuliko sisi! Ishara za ukristo katika *"The Lord of the Rings"* au "*The Chronicles of Narnia"* zinaweza zikawa sambamba na zile za kisasa.

B. Ufunuo kipekee kabisa ni fasihi yenye uwasilishaji wa maandishi ya Kiyahudi juu ya mambo yajayo. Namna hii ilikuwa ikitumika mara nyingi nyakati zilizojaa mivutano (kama vile Israeli ilipokuwa ikitawaliwa na mataifa) kuelezea imani kuwa Mungu anashughulika na mambo yao na historia yao na kuwa angeleta ukombozi kwa watu wake. Aina hii ya uandishi ina tabia zifuatazo;

1. Hisia kali ya kutambua kwa dhati ukuu wa Mungu (Imani kwa Mungu mmoja na udhabiti)
2. Mashindano kati ya wema na uovu, zama hizi za uovu na zama za haki zitakazokuja (kuwepo kwa pande mbili)
3. Matumizi ya alama katika maneno ya siri (mara nyingi kutoka katika agano la kale au, kutoka miongoni mwa maandiko ya Kiyahudi ya nyakati zijazo kati ya agano la kale na agano jipya.
4. Matumizi ya rangi, wanyama, na wakati mwingine binadamu.
5. Matumizi ya namba za tarakimu (kama 4, 6, 7, 10, 12)
6. Matumizi ya upatanisho wa kimalaika kwa njia za maono na ndoto lakini mara nyingi kupitia tafsiri za malaika
7. Kuweka msisitizo na mkazo katika matukio ya hali ya hewa ya siku za mwisho au nyakati mpya zijazo punde.
8. Matumizi ya seti za alama za kudumu pasipo uhalisia kuzungumza ujumbe wa Mungu juu ya siku/nyakati za mwisho.
9. Baadhi ya mifano ya aina hii ya uwasilishaji ni kama
   - (a) Agano la Kale
     - (1) Isaya 13-14, 24-27, 56-66
     - (2) Ezekieli 1:26-28, 33-48
     - (3) Danieli 7-12
     - (4) Joeli 2:28 – 3:21
     - (5) Zakaria 1-6, 12-14
   - (b) Agano jipya
     1. Mathayo 24, Marko 13, Luka 21 na I Wakorintho 15 (katika baadhi ya maeneo)
     2. II Wathesalonike 2 (katika namna nyingi zaidi)
     3. Ufunuo (Sura 4-22)
   - (c) Danieli 7-12 na ufunuo 4-22 ni mfano halisi wa aina hii ya uandishi katika Biblia

10. Vitabu visivyopitishwa visivyohusu sheria za kanisa (imechukuliwa kutoka kwa D.S. Russel, The Method and Message of Jewish Apocalyptic, ukurasa wa 37 – 38
    a. I Enoch, II Enoch (The Secrets of Enoch)
    b. The Book of Jubilees
    c. The Sibelline Oracles III, IV, V
    d. The Testament of The Twelve Patriarchs
    e. The Assumptions of Moses
    f. The Martyrdom of Isaiah
    g. The Apocalypse of Moses (Life of Adam and Eve)
    h. The Apocalypse of Abraham
    i. The Testament of Abraham
    j. II Esdras (IV Esdras)
    k. II & III Baruch
11. Kuna hali ya kuwepo kwa pande mbili katika namna ya uandishi huu. Inauangalia ukweli katika mfuatano wa pande mbili, kwa kuonyesha utofauti kwa kulinganisha, au kuvutana (hii imeonekana sana katika maandiko ya Yohana) kati ya;-
    a. Mbingu na nchi
    b. Zama za uovu (binadamu waovu na malaika waovu) – zama mpya za haki (wanadamu wacha Mungu na malaika wenye hofu ya Mungu)
    c. Ulimwengu wa sasa - ulimwengu ujao

    Haya yote yanaelekea katika kilele na ukamilisho unaoletwa na Mungu. Hii si nchi amabayo Mungu alikusudia iwe bali yeye anapanga na kufanya kazi kukamilisha mapenzi yake ya uhusiano wake wa karibu aliouasisi katika bustani ya ya Eden. Tukio la Kristo ni alama na kiashiria muhimu cha mpango wa Mungu lakini vitu hivyo viwili vinaletwa na hali ya kuwepo kwa pande mbili.

C. Kazi hizi za utabiri juu ya mwisho wa nchi hazijawahi kuwasilisha kwa njia ya mdomo; bali siku zote ziliandikwa. Ni kazi za fasihi zenye muundo madhubuti sana. Muundo wake ni muhimu sana ili kupata tafsiri sahihi. Sehemu kubwa ya mpango uliopangwa wa kitabu cha ufunuo ni vipengele saba vya fasihi ambavyo vina uelekeo unaofanana katika baadhi ya maeneo (kama vile mihuri saba, baragumu saba, na vitasa saba). Katika kila mzunguko hukumu inaongezeka; mihuri, ½ uharibifu; baragumu, ⅓ uharibifu, vitasa, uharibifu kamili; katika kila kipengele cha kuja kwa mara ya pili kwa Kristo au matukio ya vifo, kuzimu, hukumu na mbingu vinatokea; (1) muhuri wa 6, ufunuo 6:12-17; (2) baragumu saba, ufunuo 11:15-18, hukumu ya malaika ya mwisho katika ufunuo 14:14-20; (3) vitasa saba, ufunuo 16:17-21 na tena katika ufunuo 19:11-21, na pia katika ufunuo 22:6-16 (pia chunguza sehemu tatu katika cheo cha Mungu) katika ufunuo 1:4, 8 na Kristo katika ufunuo 1:17, 18, "Yeye aliyeko, "Yeye aliyekuwako" na utagundua sehemu ya ajaye imeachwa katika ufunuo 11:17 na ufunuo 16:5 jambo hili likimaanisha kuwa milele imekwisha kuja (kuja kwa mara ya pili) hii ina maanisha kitabu hakifuati utaratibu wa kupanga miaka na matukio kwa mfuatano au mfululizo bali ni tamthiliya katika vipengele kadhaa vinavyoonesha nyakati zijazo kwa wakati mmoja kwa kuendelea kwa nguvu na kwa namna ya hukumu ya Agano la kale la kurudiarudia (kutoka kwa James Blems, Revelation as Drama and *"The Genre of Revelation"* in Review and Expositor, Septemba. 1980, ukurasa 393-408)

Kuna sehemu saba za fasihi ukijumlisha sehemu ya utangulizi na hitimisho

1. Utangulizi ufunuo 1:1-84
2. Ufunuo 1:9-3 (Kristo na Makanisa saba)
3. Ufunuo 4-8:1 (Mbingu na mihuri saba[Ufunuo 2:1-17 baada ya muda kati ya muhuri wa 6 na 7])
4. Ufunuo 8:2-11(Malaika saba wenye baragumu[Ufunuo 10:1-11:13 baada ya muda kupita kati ya baragumu cha 6 na saba])
5. Ufunuo 12-14 (Jamii mbili na viongozi wake)
6. Ufunuo 15-16 (Malaika saba na vitasa)
7. Ufunuo 17_19(Babylon na hukumu yake)
8. Ufunuo 20-22:5 (Hukumu na mbingu mpya na nchi)

9. Hitimisho, ufunuo 22:6-21

Mwandishi mwingine aliyeamini katika dhana ya kurudiarudia kwa muhtasari na ufupisho ni William Hendriksen. Katika kitabu chake, *More Than Conquerors*, anafafanua kitabu ifuatavyo;

1. Ufunuo 1-3 (Kristo katikati ya vinara vya taa)
2. Ufunuo 4-7 (kitabu chenye mihuri saba)
3. Ufunuo 8-11 (baragumu saba za hukumu)
4. Ufunuo 12-14 (Mwanamke na mwana wa binadamu ateswavyo na joka na wasaidizi wake[mnyama na kahaba])
5. Ufunuo 15-16 (vitasa saba za ghadhabu)
6. Ufunuo 17-19 (anguko la kahaba na mnyama)
7. Ufunuo 20-22 (hukumu juu ya joka ikifuatiwa na mbingu mpya na nchi, Yerusalemu mpya, ukurasa wa 28)

   Katika *More Than Conquerors,* William Hendriksen anasema kuwa Ufunuo una sehemu saba: Ufunuo 1-3;4-7;8-11; 12-14; 15-16; 20-22 na kila sehemu hii inaenda sambamba na kuchukua kipindi kati ya kuja kwa Kristo kwa mara ya kwanza na kuja kwa Kristo kwa mara ya pili. Kila kimoja kinaisha na sehemu inayohusiana na hukumu na kuja kwa mara ya pili (ukurasa wa 22-31).

   Ingawa naamini kwa hakika katika usambamba wa tamthiliya ya mihuri, baragumu, na vitasa na pia navutiwa sana na 17-19 vile ilivyo sambamba na 20-22 (kuna kuja kwa mara ya pili katika ufunuo 19:11-21 na kuja kwa mara ya pili tena katika Ufunuo 22:6-15; angalia kwa umakini mstari wa 15; uovu haujaondolewa bado, kama vile katika Ufunuo 19:14-15), sioni mahali vipengele hivi vinapoishia katika kurudi kwake mara ya pili (*Parousia)*, hasa katika sura 1-3, labda kuwepo na kipengele cha hukumu kinachoonekana kama tukio la mwisho wa nchi (linganisha Ufunuo 2:5, 7, 11, 16-17, 25-26; 3:5, 10, 12, 18-21). Hata hivyo, kwangu mimi, kurudia rudia kwa namna ya sehemu saba inatengeneza zaidi na zaidi uwezekano wa uelewa sambamba na muundo wa kitabu chote.

D. Ni wazi kuwa namba “saba” inachangia sehemu kubwa katika muundo wa kitabu kama ambayo inaweza kuonekana kutoka katika makanisa saba, mihuri saba, baragumu saba, na vitasa saba. Mifano mingine yenye “saba” ni:
   1. Baraka saba, Ufunuo 1:3; 14;13 16:15; 19:9; 20:6; 22:7, 14
   2. Vinara vya taa saba, Ufunuo 1:12
   3. Roho saba za Mungu, Ufunuo 1:4; 3:1 4:5; 5:6
   4. Nyota saba, Ufunuo 1:16, 20; 2:1
   5. Taa saba za moto, Ufunuo 4:5
   6. Mihuri saba katika kitabu, Ufunuo 5:1
   7. Pembe saba, macho saba ya mwana kondoo, Ufunuo 5:6
   8. Sifa saba ya Yesu kusifiwa, Ufunuo 5:12
   9. Ishara saba za kiasili, Ufunuo 6:12-14
   10. Aina saba za watu, Ufunuo 6:15
   11. Sifa saba za Mungu anayesifiwa, Ufunuo 7:12
   12. Malaika saba wakaao mbele za Mungu, Ufunuo 8:2, 6
   13. Baragumu saba zibebwazo na malaika saba, Ufunuo 8:6 (Ufunuo 15:1, 6, 7, 8; 17:1; 21:9)
   14. Ishara saba, Ufunuo 12: 1, 3; 13: 13, 14, 15:1; 16:14; 19:20
   15. Vichwa saba, vilemba saba vya joka mwekundu, Ufunuo 12:3
   16. Vichwa saba vya mnyama wa majini, Ufunuo 13:1; 17:3, 7
   17. Malaika saba, Ufunuo 14:6-20
   18. Mapigo saba, Ufunuo15:1; 21:9
   19. Milima saba, Ufunuo 17:9
   20. Wafalme saba, Ufunuo 17:10
   21. Vitu saba visivyokuwepo tena katika sura ya 21-22 (Ufunuo 21:1, 4 [mara nne]; Ufunuo 21:25; 22:3)

E. Tafsiri ya kitabu hiki inaweza changiwa sana na elimu ya thiolojia. Dhana za mtu zinaweza kupelekea maelezo yaliyo na maana zaidi ya moja. Dhana hizi za kithiolojia zinafanya kazi katika viwango Fulani
   1. Asili ya ishara
      a. Dokezo za Agano la kale
         (1) Mada za agano la Kale kama uumbaji, anguko,, gharika, kutoka, urejesho wa Israeli
         (2) Mamia ya madokezo (yasiyonukuliwa moja kwa moja ) kutoka katika Agano la kale la Manabii
      b. Maandiko ya Kiyahudi ya kati ya maagano (I Enoch, II Baruch, Sibylline Oracles, II Esdras)
      c. Karne ya kwanza ya kipindi cha Wagiriki-Waroma
      d. Hesabu ya kuumbwa kwa ulimwengu ya Near Eastern ya kale (haswa Ufunuo 12)

   2. Muda wa kuanza na kumalizika kwa kitabu
      a. Karne ya kwanza
      b. Kila karne
      c. Kizazi cha mwisho
   3. Utaratibu wa vipimo vya ki-thiolojia (angalia maana katika ukurasa wa 14, "Historical Theories of Interpretation" C; a good summary, *Four Views on the Book of Revelation*, Ed. C. Marvin Pate)
      a. Wenye mlengo wa kuwa matukio haya yalishatimia (Preterist)
      b. Wanye mlengo kuwa matukio yanayotokea yako juu ya uwezo wa binadamu. (Historicist)
      c. Wenye mlengo wa mambo yajayo (Futurist)
      d. Wenye mlengo wa nadharia (idealist)
   4. Nafasi ya Theolojia katika sura ya 20 (angalia jedwali katika ukurasa wa 193; good summaries: (1) *The Meaning of the Millennium: Four Views*, ed. Robert G Clouse and *Three Views of the Millennium and Beyond,* ed. Darrell L. Bock)
      a. Milenia
      b. Baada ya Millenia
      c. Kabla ya Millenia
      d. Mgawanyo wa kabla ya millennia

         Katika mwanga wa kugawanyika kwa katika elimu ya kutafsiri maandiko (mbinu tofauti za kutafsiri) na imani zisizo sahihi (mtazamo wa kujua kila kitu), mtafsiri anawezaje kuendelea?
   5. Tukubaliane kuwa wakristo wa kisasa hawana uelewa wa namna ya kutambua dhana za kihistoria kama waliyokuwa nayo wakristo wa kwanza namna ambavyo wangeelewa.
   6. Tukubaliane kuwa kila kizazi cha Wakristo kimelazimisha Ufunuo katika mazingira yao wenyewe ya kihistoria na wote wamekosea mpaka hapo.
   7. Tujitahidi kusoma Biblia zetu kabla ya kusoma mifumo na utaratibu wa ki-thiolojia. Angalia muktadha ama mazingira ya maandiko ya kila maono na hali ya ukweli mkuu katika tamko moja la andiko. Ukweli utabaki na kusimama kwa kila kizazi wakati umaalumu wa maelezo yanaweza kuwa ya kwa jili ya kizazi cha kwanza tu na au kizazi cha mwisho cha waamini. Maelezo yanaweza kuwa na mahusiano, lakini historia, itafunua utimilifu wake.
   8. Tukumbuke kwamba kitabu hiki kimekusudiwa hasa kuwa neno la faraja na kutia moyo katika uaminifu katikati ya dhiki wanazofanywa na wasioamini kwa waaamini. Kitabu hiki hakijakusudiwa kutoa majibu ya shauku ya kila kizazi cha waaminio, hakikusudiwa kutoa ufafanuzi wa kina wa matukio ya siku za mwisho.
   9. Ni salama kukiri kuwa jamii iliyoanguka ya binadamu ipo katika mgongano na ufalme wa Mungu. Mwanzoni yaweza kuonekana kama uli wengu umeshinda (kama Kalvari), lakini subiri; Mungu ni mwenye uwezo wote, yeye ndiye anaye endesha historia, ya maisha na mauti. Watu wake ni washindi ndani yake!

F. Licha ya ugumu na utata wa tafsiri, kitabu hiki kina ujumbe na ni neno la Mungu lililovuviwa kwa ajili ya watu wake katika kila kizazi. Kitabu hiki cha kipekee kinastahili kuwekewa nguvu ya ziada ya makusudi kukisoma. Nafasi yake katika azimio la kikanoni la Agano Jipya ni alama ya ujumbe wake. Alan Johnson, *The Expositor's Bible Commentary,* Vol. 12, kinasema

> " Hakika, inawezekana kabisa kuwa ukiacha vitabu vya Injili, vitabu vinavyoonyesha mwisho wa nchi vimejaa mafunzo mengi ya msingi katika mafundisho ya Ukristo na uanafunzi kuwahi kuwepo katika Maandiko Matakatifu. Haitakiwi hata ulokole wa baadhi ya watu walioweka mkazo wao mkubwa katika unabii zaidi ya Kristo, bila hata kuzingatia mgawanyiko uliopo wa namna ya kinavyotafsiriwa unatakiwa utukatishe tamaa sisi ya kuutafuta ukweli wa ukristo wetu katika kitabu hiki kizuri sana kwa namna yake" (ukurasa wa 399).

Kumbuka, hakika haya ndiyo maneno ya Yesu kwa kanisa lake! Kanisa la leo halitakiwi kujaribu kuyapuuza au kuyapunguza! Yamekusudiwa kuwaandaa waaminio kwa ajili ya dhiki na mgogoro katika ufahamu wa uweza wa Mungu (imani kwa Mungu mmoja), uhalisia wa Yule muovu (upili wenye kikomo), hali inayoendelea ya anguko (uasi wa binadamu), na ahadi za Mungu kumkomboa mwanadamu (agano lisilo na masharti, angalia Mwanzo 3:15; 12:1-3; Kutoka 19:5-6; Yohana 3:16; 2 Wakorintho 5:21).

## MWANDISHI

A. Ushahidi wa ndani wa uandishi wa Mtume Yohana
   1. Mwandishi mwenyewe amejitaja mwenyewe mara nne kama Yohana (rejea Ufunuo 1:1, 4, 9; 22:8)
   2. Pia alijiita mwenyewe
      a. Mtumwa mwaminifu (rejea Ufunuo 1:1; 22:6)
      b. Ndugu yenu na mwenye kushiriki dhiki (rejea Ufunuo 1:9)
      c. Nabii (angalia Ufunuo 22:9), na akakiita kitabu chake unabii (rejea Ufunuo 1:3; 22:7, 10, 18, 19)
   3. Analijua Agano la kale (hatumii LXX, bali Targums) na nyikani kama kipindi cha upotevu, Sanduku la agano na taratibu za ibada za kisinagogi za wakati huu.

B. Ushahidi wa nje wa uandishi wa Mtume Yohana kutoka kwa waandishi wa kwanza wa Kikristo
   1. Mtume Yohana, mwana wa Zebedayo
      a. Justin Martyr (Rumi, baada ya Kristo mwaka 110-165) katika *Dialogue with Trypho* 81.4)
      b. Ireneus (Lyons, baada ya Kristo mwaka 120-202) katika *Against Heresies* IV.14.;17.6; 21.3; V.16.1; 28.2; 30.3; 34.6;35.2
      c. Tertullian (Africa Kaskazini, kabla ya Kristo mwaka 145-220) katika *Against Prexeas* 27
      d. Origen (Alexandria, baada ya Kristo mwaka 181-252) katika
         (1) *On the Soul*, L:8:1
         (2) *Against Marcion*, II:5
         (3) *Against Heretics*, III:14, 25
         (4) *Against Celsus*, IV:6, 32; VIII:17
      e. Orodha ya kale ya vitabu vya kanuni za kikanisa vya karne ya pili (Muratorian Canon) (Rumi , baada ya Kristo 180-200)
   2. Wengineo
      a. Yohana Marko – Hii ilitajwa kwanza na Dionysius, Askofu wa Mji wa Alexandria (baada ya Kristo mwaka 247-264), yeye alikataa uandishi wa Mtume Yohana lakini akaendelea kuiweka kazi yake katika azimio la Kanoni. Sababu kuu aliyoitoa kwa nini akatae ilijikita katika misamiati na staili yake pamoja na maandiko mengine ya Yohana yasiyoeleweka asili yake. Alimshawishi pia Eusebius wa Kaisaria.
      b. Yohana mzee – Hii inatokana na nukuu za Eusebius kutoka kwa Papias (*Eccl. Hist*. 3.39. 1-7). Ingawa nukuu ya Papia yumkini ilitumia cheo hiki badala ya Mtume Yohana ili isije ikamaanisha mwandishi mwingine.
      c. Yohana Mbatizaji – (ikiwa na maboresho ya kiuandishi mengine) imependekezwa na J. Massyngberde Ford katika Anchor Bible Commentary, ikiweka msisitizo wa Yohana Mbatizaji kumuita Yesu "mwanakondoo". Sehemu nyingine ambapo neon hili linaitwa ni katika kitabu cha Ufunuo.

C. Dionysius, Askofu wa Alexandria (baada ya Kristo mwaka 247-264) na mwanafunzi wa Origen, alikuwa wa kwanza kuonesha mashaka (kitabu chake kilipotea lakini ananukuliwa na Eusebius wa Kaisaria anayekubaliana nae) kwamba uandishi wa Mtu Yohana umejikita katika

1. Mtume Yohana hajitaji kuwa yeye ndiye Yohana Yule wa Injili wala barua zake hazioneshi hivyo lakini Ufunuo unatoka kwa "Yohana"
2. Muundo wa Ufunuo ni tofauti na Injili na barua zingine
3. Misamiati ya Ufunuo ni tofauti na Injili na barua zake.
4. Staili ya kisarufi ya Ufunuo ni ya kinyonge na isiyo na ubora ukilinganisha na ile ya Injili na barua zake

A. Yawezekana changamoto kubwa kabisa ya kisasa inayokabili uandishi wa Mtume Yohana inatoka kwa R.H.Charles katika Saint John, Vol I p. xxxixff.

B. Waandishi wengi wa kisasa wamekataa uandishi wa kienyeji wa vitabu vingi vya Agano Jipya. Mfano mzuri wa jambo hili unaohusiana na Ufunuo anaweza akawa Raymond E. Brown, Mtaaluma maarufu wa KIkatoliki wa Johannine. Mfululizo wa toleo la utangulizi la Anchor Bible Commentary linasema, "imeandikwa na Nabii Mkristo wa Kiyahudi aitwaye Yohana ambaye hakuwa Yohana mwana wa Zebedayo wala hakuwa Yohana wa Injili, wala si yule wa Waraka" (ukurasa 774).

C. Katika namna nyingi uandishi una tiliwa shaka. Kuna mgongano wa usambamba na Maandiko mengine ya Mtume Yohana pia kutofautina sana. Msingi wa kukielewa kitabu hiki haipo katika kujua ubinadamu wa mwandishi bali katika Uungu wa Mwandishi! Mwandishi mwenyewe anajiamini kuwa nabii aliyevuviwa (rejea Ufunuo 1:3; 22:7, 10, 18, 19).

## TAREHE

A. Hii kwa hakika inatengeneza muunganiko katika ya uandishi na dhana ya utafsiri (rejea Nadharia za Kihistoria)
B. Uwezekano wa baadhi ya tarehe
   1. Tarehe za kienyeji ni wakati wa utawala wa Domitia (baada ya Kristo mwaka 81-96) kwakuwa inarandana na ushahidi wa ndani wa dhiki.
      a. Irenaeus (alinukuliwa na Eusebius) katika *Against Heresies,* 5.30.3 "Hii dhiki ilionekana si miaka mingi iliyopita karibu na kizazi chetu, karibu na utawala wa Domitia"
      b. Clement wa Alexandria
      c. Asili ya Alexandria
      d. Eusebius wa Kaisaria, *Church History,* iii.23.1
      e. Victorinus,*Apocalypse* x.11
      f. Jerome
   2. Epiphanius, mwandishi wa karne ya tatu, katika *Haer*, 51.12, 32, inasema kuwa Yohana aliandika baada ya kutolewa Patmos wakati wa utawala wa Klaudio (baada ya Kristo mwaka 41-54).
   3. Wengine yawezekana kuwa wakati wa utawala wa Nero (baada ya Kristo mwaka 54-68) kwasababu ya:
      a. Historia ya mateso ya kidini Mfalme
      b. *Caesar Nero,* kimeandikwa kwa lugha ya Kiebrania, ikitaja namba za mnyama, 666
      c. Kama wenye mlengo wa kuwa matukio haya yalishatokea wako sawa kuwa Ufunuo wa Yohana unamaanisha uharibifu wa Yerusalemu, kwahiyo ili kitabu kuwa cha Unabii, lazima kiwe kimeandikwa mwaka 70 baada ya Kristo

## WAPOKEAJI

A. Kutoka Ufunuo 1:4 ni wazi kuwa wapokeaji wa asili yalikuwa makanisa saba katika Jimbo la Rumi huko Asia. Makanisa haya yanaambiwa ujumbe katika namna inayomaanisha ramani ya muwasilishaji wa barua.
B. Ujumbe wa Ufunuo kipekee una uhusiano na makanisa yote na waaminio wanaopitia hali ya dhiki kutoka katika mfumo ulioanguka wa utawala wa kidunia.
C. Kama hitimisho la Kikanoni kwa Agano Jipya, kitabu hiki ni ukamilisho wa waaminio wote wa vizazi vyote.

## MAZINGIRA

A. Mazingira yalikuwa ni ya dhiki iliyosababishwa na kuachana kwa makanisa kutoka katika ulinzi wa kisheria wa Rumi uliorasmishwa kwa dini ya Kiyahudi. Mgawanyiko huu ulitokea rasmi katika miaka ya 70 baada ya Kristo wakati walimu kutoka Jamnia walirasmisha utaratibu wa kiapo kilichokuwa na sharti la waaminio wa masinagogi kumlaani Yesu wa Nazareti.
B. Nyaraka za Kirumi zinaonyesha kuwa kumwabudu Mfalme kulileta mtafaruku mkubwa na makanisa kutoka katika kipindi cha utawala wa Nero (mwaka 54-68 baada ya Kristo) mpaka kipindi cha Domitia (81-96 baada ya Kristo). Ingawa hakuna nyaraka zinazoonesha kuenea rasmi kwa dhiki katika ufalme. Kwa uwazi kabisa Ufunuo unaaksi kichocheo cha kitendo cha dini cha kuabudu Mfalme katika Majimbo ya Mashariki ya ufalme wa Rumi (rejea "Biblical Archaeology Review", Mei/Juni 1993 ukurasa wa 29-37)

## SARUFI YA MANENO

A. Kuna matatizo mengi ya kisarufi katika maandiko ya Kigiriki
B. Baadhi ya sababu za matatizo haya.
   1. Mpangilio wa mawazo ya Yohana katika lugha ya Ki-aramaiki.
   2. Hakuwa na kitabu cha kuandikia huko Patmos.
   3. Alikuwa na msisimko wa kupitiliza wa maono.
   4. Yalikuwa na kusudi ya kutokea kwake
   5. Staili ya uwasilishaji wake (juu ya matukio ya mwisho wa nchi) ilijaa sana mafumbo.
C. Sarufi inayofanana kitabia zinapatikana katika maandiko mengine ya Kiyahudi juu ya mwisho wa nchi. Hivyo, Ufunuo haukuandikwa katika staili dhaifu ya kisarufi bali katika namna pekee kisarufi.

## MWONGOZO WA KIKANONI

A. Kilikataliwa mapema na kanisa la Mashariki; kitabu hakipatikani katika Peshitta (toleo la tano la Ki-Ashuru)
B. Mwanzoni mwa karne ya nne ya Eusebius, akifuatiwa na Dionysius wa Alexandria mwishoni kabisa mwa karne ya tatu, ilisemekana kuwa Ufunuo haukuandikwa na Mtume Yohana. Alikitaja kama moja ya vitabu vuisivyoeleweka japo alinijumuisha katika idadi ya vitabu vya Kikanoni (rejea Eccesiastical History, III.24.18; III.39.6).
C. Baraza la Laodikia (miaka ya 360 baada ya Kristo) ilikiondoa katika orodha ya vitabu vya kikanoni. Jerome alikikataa kuwa hakiwezi kuwa kikanoni, lakini baraza la Carthage (mwaka 397 baada ya Kristo) likiingiza katika orodha. Ufunuo kiliingizwa na kukubaliwa kwa mapatano ya kishingo upande kati ya makanisa ya Mashariki na Magharibi ambapo vitabu vyote vya Waebrania na Ufunuo vilikubaliwa kuingia katika Agano Jipya kama azimio la Kikanoni.
D. Lazima tutambue kuwa ni dhana ya imani ya Waaaminio kwamba Roho Mtakatifu alisimamia na kuongoza mchakato wa kihistoria wa kutengeneza Kanoni ya Kikristo.
E. Wanathiolojia wakubwa wa mwanzo wa Mageuzi ya Kiprotestant walikataa nafasi yake katika mafundisho ya Kikristo.
   1. Martin Luther alikitaja kuwa hakikuwa cha kinabii wala kitume, kiuhalisia akikataa uvuvio wake.
   2. John Calvin, aliyeandika Mwongozo katika kila kitabu cha Agano Jipya isipokuwa Ufunuo, kiuhalisia alikataa uhusika wake.

## DHANA ZA KIHISTORIA ZA UTAFSIRI

A. Kinasifika kwa kuwa kigumu kutafsiri; hivyo, kulazimisha imani fulani ni jambo lisilofaa!
B. Ishara zake zimetolewa kutoka
   1. Aya za siku za mwisho wa ulimwengu katika
      a. Daniel
      b. Ezekiel
      c. Zakaria
      d. Isaya

2. Maandiko ya kiyahudi ya siku za mwisho wa nchi ya maagano.
3. Mazingira ya kihistoria ya karne ya kwanza ya Wagiriki-Warumi (hasa Ufunuo 17)
4. Maelezo ya hadithi za kubuni za uumbaji katika Near Eastern kongwe (hasa Ufunuo 12).

C. Kwa ujumla kuna dhana nne za utafsiri
1. WENYE MLENGO KUWA MATUKIO HAYA YAMEKWISHA TOKEA – kundi hili linakiona kitabu hiki kama chenye kuweka msingi sana wa mahusiano na makanisa ya kwanza katika majimbo ya Kirumi ya Asia. Maelezo mengi na unabii ulitimilizika katika karne ya kwanza (angalia John L. Bray, *Matthew 24 Fulfilled)*
2. WENYE MLENGO KUWA MATUKIO YANAYOTUKIA YAKO JUU YA UWEZO WA BINADAMU – kundi hili linaangalia kitabu kama mapitio tu ya Kihistoria, kikazo ustaarabu wa Magharibi na katika hali Fulani pia Kanisa la Kirumi la Kikatolic. Mara zote barua kwa makanisa saba kwa sura za pili na tatu zinatumika kama kufunua vipindi fulani vya muda. Wengine wanaliona hili kama uonishaji wa muda mfupi tu na wengine wakitazama kuwa zinatoa utaratibu mzuri wa mpangilio wa matukio.
3. WENYE MLENGO WA BAADAE – kundi hili linaona kitabu hiki kuwa kinayazungumzia zaidi matukio yajayo yatakayotangu;lia na yatayofuatia *Parousia* (Kuja kwa Kristo mara ya pili) ambayo kimaandiko na kihistoria lazima itimie (rejea *Progressive Dispensationalism*, kilichoandikwa na Craig A. Blaising na Darrell Bock).
4. WENYE MLENGO WA NADHARIA – kundi hili linakitazama kitabu kama ishara kabisa ya mashindano kati ya wema na uovu kisicho na rejea za kihistoria (angalia Ray Summers, *Worthy Is the Lamb*; William Hendriksen, *More Than Conquerors*).

   Wote hawa wanazungumza ukweli, ila wanashindwa kuuona utata wa kimakusudi unaosababishwa na taswira na aina ya njia aliyoichagua Yohana katika uwasilishaji wa ujumbe. Tatizo hapa ni uwasa wa kimizani, na sio nani yuko sahihi.

## KUSUDI YA KITABU HIKI

A. Kusudi la kitabu cha Ufunuo ni kuonesha ukuu wa Mungu katika historia na ahadi ya kilele cha mambo yote katika Yeye. Waaminifu wanatakiwa kudumu katika imani na matumaini katikati ya dhiki na uchokozi wa mfumo wa dunia hii ulioanguka. Lengo la kitabu ni dhiki (kuabudu mfalme katika majimbo ya Mashariki) na uaminifu (walimu wa uongo na maridhiano ya kiutamaduni) wa waaminio katika karne ya kwanza na katika kila karne (rejea Ufunuo 2:10). Kumbuka, manabii walizungumza juu ya mambo yajayo katika jitihada za kufanya mageuzi ya wakati uliopo. Ufunuo haujajikita tu juu ya itakavyomalizika, ila pia jinsi inavyoendelea. Katika makala yake katika The Expositors Bible Commentary, Vol I yenye kichwa cha habari "The Eschalotological of The Bible," Robert L. Sancy alisema,

> "Manabii wa kibiblia hawakujali sana kuhusu muda na upangiliaji mzuri wa matukio yajayo. Kwao hali ya kiroho waliyokuwa nayoo wakati huo ndiyo iliyobeba umuhimu mkubwa na kutembelewa na Mungu kwa ajili ya siku za mwisho na hukumu ya wasio haki na Baraka za Wacha Mungu zinachachawizwa kwa matokeo yake ya kimaadili ya wakati tulionao"( ukurasa wa 104).

B. Kusudi kuu linawekwa vyema ki-muhtasari katika utambulisho mfupi wa matoleo ya tafsiri ya TEV na NJB.
1. TEV, ukurasa wa 1122, "Ufunuo wa Yohana uliandikwa wakati ambapo Wakristo walikuwa wanapitia dhiki kwasababu imani ya kumkiri kwao Kristo Yesu kama Bwana. Kusudi kuu la mwandishi ni kuwapa wasomaji wake tumaini nakuwatia moyo, na pia kuwasihi kuendelea kuwa waaminifu wakati wa mateso na dhiki"
2. NJB, ukurasa wa 1416, "Biblia inajumuishwa katika muhtasari katika ujumbe wa tumaini na utajiri mkubwa wa ishara wa kitabu hiki. Ni maono ya ukombozi kutoka katika majaribu ambayo yanawapata watu wa Mungu, na ahadi ya utukufu ujao. Ujumbe unawasilishwa kwa namna ya taswira zinazotokana na Biblia nziama, ili kila sifa ya mnyama, rangi, tarakimu, zinaamsha hisia na zimejaa vidokezo halisi kwa msomaji wa Agano la Kale. Katika namna hii ni siri na ni Ufunuo wa kudokeza yajayo, licha ya ishara ya asili kuwa ishara kubwa ya matendo yakuabudu na maono ya mwisho ya mg'ao wa kimasiya wa Mji Mpya Mtakatifu kuwa dhahiri kabisa. Kuliwahi kuwa na desturi ya uandishi

wa namna hii katika Uyahudi kutoka kwa Daniel na kuendelea, hii ni kuimarisha watu wa Mungu katika dhiki kwa uhakika wa hatimaye kupata ukombozi na ushindi"

C. Ni muhimu sana kuwa mtafsiri atoe kipaumbele cha hoja ya ukombozi.
   1. Mungu ameleta wokovu wa mtu, watu na ulimwengu mzima kupitia Kristo.
   2. Ukombozi wa Mungu ni wa vyote yaani roho na mwili. Kanisa linaokolewa lakini si salama! Siku moja litakuwa salama!
   3. Mungu bado anawapenda walioanguka, wakaidi, wabinafsi. Gadhabu ya Mungu katika muhuri na baragumu ni kwa ajili ya Ukombozi (rejea Ufunuo 9:20-21; 14:6-7; 16:9, 11; 21:6b-7; 22:17).
   4. Sio tu kwamba Mungu anarejesha mwanadamu, lakini pia uumbaji ulioanguka (rejea Warumi 8:18-25). Uovu katika kiwango chochote kitasafishwa!

      Hali ya Mungu kujaribu tena na tena kumfikia mwanadamu aliyepotea kwa Injili kunakuza tabia ya Kurehemu aliyonayo Mungu. Hukumu ya Kitasa ni matokeo ya uovu usiovumilika, na si kwamba Mungu amekosa upendo. Mungu yeye hutoa hukumu na kuutenga uovu pale tunapokataa kutubu tena na tena. Katika namna nyingi kitabu kinahalalisha hukumu ya Mungu kwa walioanguka, binadamu wasiokubali kupatanishwa! Kitabu kinahitimisha kwa ukaribisho wa Injili (rejea 22:17).

D. Kitabu hiki <u>hakitakiwi</u> kuonekana kama mchoro wa utaratibu wa matukio, nyakati, na namna ya Kuja kwa Mara ya Pili. Imekuwa mara kwa mara ikitafsiriwa kama "siri" kwa historia ya Magharibi (makanisa saba kuonekena kama nyakati). Kila kizazi kimelazimisha historia yake yenyewe kuwa ishara ya mwisho wan chi; mpaka hapa kila mmoja amekosea.

   Maelezo ya unabii huu yatakuwa dhahiri zaidi katika kizazi cha mwisho cha waaminio watakaoteseka chini ya Mpinga Kristo (rejea 2 Wathesalonike 2). Tafsiri za kawaida umesababisha kitabu hiki kususiwa na baadhi (Calvin), kutopewa thamani na wengineo (Luther, "si cha kitume wala cha kinabii"), na kupewa msisitizo uliopitiliza na baadhi (wenye mlengo wa kimelenia)

## MWONGOZO WA BOB WA UTAFSIRI

A. Tunahitajika kuangalia baadhi ya vipengele vya Agano la kale
   1. Aina ya uandishi kuhusu mwisho wa nchi wa Agano la Kale umejaa ishara nyingi.
   2. Vidokezo kadhaa vimepakuliwa kutoka katika Agano la Kale (wengine wanakadiria kuwa ni kati ya mistari 404, mistari 275 inajuisha madokezo kutoka katika Agano la Kale); maana ya ishara hizi zimetafsiriwa tena katika namna ya ufahamu wa hali ya karne yya Kwanza ya Kirumi.
   3. Dalili ya unabii inachukua matukio ya sasa kuonyesha dalili ya matukio yajayo ya mwisho wa nchi. Mara nyingi kutimilizwa kwa matukio haya ya kihistoria ya karne ya kwanza kunapelekea kutimilizwa kwa siku za mwisho kihistoria.

B. Muundo mzima wa kitabu unatusaidia kuona makusudi ya mwandishi
   1. Mihuri, baragumu, vitasa kimsingi vinachukua muda ule ule (Ufunuo 6-16). Ufunuo ni hadithi ya matendo yanayofululiza.
   2. Inawezekana kuwa Ufunuo 17-19 ni sambamba na Ufunuo 20-22. Sehemu za sura ya 19 (kama vile 19:11-21) zinarudiwa katika Ufunuo 20: 7-10.
   3. Angalia vipengele vya uandishi katika Maelezo ya Ufunguzi, C.

C. Muktadha wa kihistoria lazima uzingatiwe katika kila tafsiri ya kitabu
   1. Uwepo wa kumuabudu Mfalme
   2. Dhiki katika Majimbo ya Mashariki.
   3. Biblia haiwezi kuwa na maana ambayo haikukusudiwa. Tafsiri ya Ufunuo lazima iwe na uhusiano na nyakati za kwanza za Yohana. Inaweza kutimilizwa kwa namna mbalimbali au kutumiwa, lakini lazima ijikite katika karne ya kwanza.

D. Maana za baadhi ya maneno ya kimafumbo hatuyafahamu na yamepoteza maana kwetu kwasababu ya utamaduni, lugha na mazingira yetu. Inawezekana matukio ya mwisho yenyewe yatatupatia ufahamu juu ya tafsiri sahihi ya ishara hizi. Kuwa mwangalifu usije ukasukumia maelezo yote katika tamthiliya ya kutukia kwa mwisho wa nchi. Watafsiri wa kisasalazima watafute kweli kuu katika kila maono.

E. Naomba nijumuishe baadhi ya vipengele vya miongozo ya kutafsiri
   1. Historia ya asili ya ishara
      a. Mada za Agano la kale, madokezo ya Agano la Kale
      b. Visasili vya Near Eastern ya kale
      c. Maandiko kati ya agano la kale na agano jipya ya siku za mwisho
      d. Mazingira ya karne ya kwanza ya Wagiriki-Warumi
   2. Njia za mwandishi za kutoa maana za ishara
      a. Mazungumzo na malaika waongozaji
      b. Tenzi za kwaya za kimbingu
      c. Maana zinazotolewa na mwandishi mwenyewe
   3. Muundo wa kitabu (usambamba wa kitamthiliya)

F. Msaada zaidi
   *1.* Watoa maoni wawili wa Ufunuo ninaowapendelea zaidi ni George Eldon Ladd na Alan F. Johnson. Hawakubaliani. Kuna kutoelewana kwingi kati ya watu wa Mungu, wasomi, wanataaluma kuwa neno la tahadhari ni muhimu. Naomba kumnukuu Alaan Johnson katika kazi yake ya *Commentary on Revelation,*iliyochapishwa na Zondervan:

   "Katika maoni ya utumizi wa taswira na maono kutoka Ufunuo 4:1 mpaka mwisho wa Ufunuo na namna jambo hili linavyofanana na sura 1-3, haishangazi kwamba watoa maoni wanatofautiana sana wanavyozitazama sura hizi. Tatizo moja linalojitokeza ni utafsiri. Taswira na maono humaanisha *nini*? Tatizo lingine linahusisha mpangilio wa wa nyakati. *Lini* mambo haya yanatukia? Zaidi sana, je Yohana anatafsiri taswira zakke za Agano la Kale katika mfanano uleule wa vyanzo vyake vya Agano la Kale, au anatoa tafsiri zake huru tu kwa taswira hizi? Kipi ni ishara na kipi sio? Majibu ya maswali hayo itaamua mtazamo wa mtafsiri. Kwakuwa baadhi ya maswali haya machache yana uwezekano wa kupewa majibu ya kidini, kuna umuhimu wa kuvumiliana katika kugawanyika huku kwa mitazamo ya tumaini kuwa Roho anaweza kutumia majadiliano huru ya kiakili kutufikisha mali zaidi hata katika maana za nyakati za mwisho" (ukurasa wa 69).

   *2.* Kwa Utangulizi wa jumla wa uhusiano wa Ufunuo na Agano la Kale, napendekeza *Prophecy Interpretend* cha John P. Milton na The *Authority of The Old Testament* cha John Bright. Kwa ajili ya mjadala mzuri wa uhusiano wa Ufunuo na Paulo, napendekeza *A Man In Christ* cha James S. Stewart.

## MZUNGUKO WA KWANZA WA USOMAJI (kutoka "Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia")

Huu ni <u>mwongozo</u> wa maoni, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mtoa maoni.

Kwahiyo, soma Biblia nzima kwa mara moja. Taja mada kuu ya kitabu kizima kwa maneno yako mwenyewe
   1. Mada ya kitabu kizima
   2. Aina ya fasihi (namna ya uwasiilishaji)

## MZUNGUKO WA PILI WA USOMAJI (kutoka "Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia")

Huu ni <u>mwongozo</u> wa maoni, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mtoa maoni.
Kwahiyo, soma Biblia nzima kwa mara ya pili kwa mara moja. Ainisha mada kuu na zieleze kwa sentensi moja.
*1.* Mada ya kipengele cha kwanza cha maandiko
*2.* Mada ya kipengele cha pili cha maandiko
*3.* Mada ya kipengele cha tatu cha maandiko
*4.* Mada ya kipengele cha nne cha maandiko
*5.* Nakadhalika

# UFUNUO 1:1-20

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA* | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Utambulisho na Salamu | Utambulisho na dua baada ya ibada | Dibaji | Utambulisho | Dibaji |
| 1:1-3 | 1:1-3 | 1:1-2<br>1:3 | 1:1-3 | 1:1-3 |
| | Salamu kwa makanisa saba | Salamu za utambulisho | Salamu kwa makanisa saba | Hotuba na Salamu |
| 1:4-5a | 1:4-8 | 1:4-5a | 1:4-5a | 1:4-8 |
| 1:5b-7 | | 1:5b-7 | 1:5b-6<br>5:7 | |
| 5:8 | | 5:8 | 5:8 | |
| Maono ya Kristo mwanzo | Maono ya<br><br>Mwana wa Adamu | Maono ya<br><br>maandalio | Maono ya Kristo | Maono ya |
| 1:9-11 | 1:9-20 | 1:9-11 | 1:9-11 | 1:9-16 |
| 1:12-16 | | 1:12-16 | 1:12:20 | |
| 1:17:20 | | 1:17:20 | | 1:17-20 |

* Ingawa hazijavuviwa, migawanyo ya aya ndiyo ufunguo wa kuelewa na kufuata kusudi la mwandishi. Kila tafsiri ya kisasa imegawanya na kufanya muhtasari wa aya kila aya ina mada kuu, kweli kuu au au wazo kuu kila tafsiri hufupisha mada ile kwa namna yake iliyo dhahiri. Unaposoma maandishi ya mwandishi jiulize ni tafsiri ipi inawiana na uelewa wako wa somo na mgawanyo wa aya. Katika kila sura lazima tusome Biblia kwanza na kujaribu kutambua somo (aya), kasha tulinganishe uelewa wetu na tafsiri za kisasa. Ni pale tunapoelewa kusudi la asili la mwandishi kwa kufuata mantiki yake na jinsi alivyojieleza tunaielewa kwa Biblia kiukweli. Ni Yule mwandishi aliyevuviwa —wasomaji hawana haki ya kubadiliana kuboresha ujumbe. Wasomaji wa biblia wana wajibu wa kutumia ukweli uliovuviwa kwenye siku na maisha yao. Fahamu kwamba maneno yote ya kiufundi na vifupisho vimefafanuliwa kwa kirefu kwenye nyaraka zifuatazo: Maelezo Fasaha Ya Muundo Wa Sarufi Za Kiyunani, Uhakiki Wa Tofauti Za Kiandishi Ufafanuzi na Maelezo ya Kimaandiko

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Angalia **"Semina ya Ukalimani wa Biblia"["Bible Interpretation Seminar")**

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili

3. Aya tatu
4. N.k

## UTAMBUZI WA KIMUKTADHA KWA UFUNUO 1:1-3:22

A. Ufu. 1:1-3 inaunda utangulizi wa unabii wote. Aya tatu za kwanza zinamtambulisha mwandishi, muda, aina ya fasihi na mibaraka.
   1. Mwandishi ni Yohana (jina la kawaida la Kiyunani).
   2. Wakati u-karibu (Ufu. 1:1b, 3c).
   3. Ujumbe ni mawasiliano kwa njia ya maono, yakifasiriwa kwa namna ya upatanisho wa kimalaika na huitwa "unabii" (Ufu. 1:3). Sura tatu za mwanzo zinafanana na namna ya kawaida ya barua za karne ya kwanza.
   4. Baraka ni kwa wale ambao husikia maneno yake na kutii ushawishi wake kwa wale waaminifu katikati ya mateso.

B. Aya nne zifuatazo zinawaelezea wapokeaji katika muundo wa makanisa saba (4-7) sehemu hii imezingatiwa na (Ufu. 1:11) na roho saba (kama vile Ufu. 1:4,20; 3:1; 4:5; 5:6). Sehemu hii imezingatiwa na
   1. YHWH akielezewa kitofauti (ufu. 1:4)
   2. Yesu akielezewa kitofauti (Ufu. 1:5,6b,7)
   3. Waaminio wanafanywa kuwa sifa stahili (Ufu. 1:6a)
   4. YHWH anazungumza (Ufu. 1:8)

C. Aya ya 1:9-3:22 ni maneno ya mwisho kwa makanisa yake. Katika Ufu. 1:9-20 na mwanzoni mwa mahubiri kwa kila kanisa miongoni mwa makanisa saba, Yesu ametambulishwa kwa sifa za vyeo vya Agano la Kale na utambulisho uliotumika kwa YHWH.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 1:1-3**

**1 Ufunuo wa Yesu Kristo, aliopewa na Mungu awaonyeshe watumwa wake mambo ambayo kwamba hayana budi kuwako upesi; naye akatuma kwa mkono wa malaika akamwonyesha mtumwa wake Yohana; 2 aliyelishuhudia Neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu Kristo, yaani, mambo yote aliyoyaona. 3 Heri asomaye na wao wayasikiao maneno ya unabii huu, na kuyashika yaliyoandikwa humo; kwa maana wakati u karibu.**

**1:1"Ufunuo"** Neno hili la Kiyunani *apocalypsis* linapatikana hapa tu kitabuni. Lilitokana na maneno mawili yaliyomaanisha "kutoka mahali pa maficho" ama “kudhihilisha” au kufunua kitu Fulani." Lilitumika katika dhana nyingi (BAGD uk. 92).

1. Ufunuo wa ukweli – Luka 2:32; Rum. 16:25; 1 Kor. 14:6,26; Gal. 1:12; Efe. 1:17
2. Siri kuwekwa wazi – Efe. 2:11-3:13
3. Ufunuo kwa njia ya maono/ndoto – 2 Kor. 12:1,7; Gal. 2:2
4. Siri zinazohusiana na nyakati za mwisho – Luka 17:30; 1 Kor. 1:7; 2 The. 1:7; 1 Pet. 1:7,13; 4:13; 5:1

Katika kitabu hiki, inamaanisha ukweli kutoka kwa Mungu kwa njia ya Yesu Kristo umepatanisha kwa njia ya maono na tafsiri za kimalaika. Unalenga uovu uliopo na ushindi unaokuja wa haki kwa njia ya nguvu ya ajabu ya Mungu Baba!

◙**"wa Yesu Kristo"** Hiki chaweza kuwa KISHAMIRISHO MILIKISHI kinachohusiana na ujumbe kuhusu Yesu Kristo (kama vile Gal. 1:12), au KIIMA MILIKISHI, kinachohusu ujumbe uliotolewa na Yesu Kristo .

◙**"Yesu"** Neno hili la Kiebrania lilimaanisha "YHWH anaokoa," "YHWH ni wokovu," "YHWH huleta wokovu." Linafanana na jina la Agano la Kale la "Yoshua." Jina"Yesu"limepatikana kutoka neno la Kiebrania wokovu, neno "*hosea*," ni kiambishi kwenye jina la Agano kwa Mungu, "YHWH" (tazama Mada Maalum: Majina ya Uungu (Special Topic: Name of Deity) D. Ni jina lililosanifiwa na Mungu kupitia malaika wa Bwana (kama vile Mt. 1:21).

◙ **"Kristo"** Hili ni jina la Kiyunani ambalo linafanana na jina la Kiebrania "*messiah,*" ambalo linamaanisha "aliyetiwa mafuta." Lilimaanisha "mtu aliyeitwa na kutengenezwa kwa ajili ya shughuli maalum." Katika Agano la Kale makundi matatu ya viongozi ndio walipakwa mafuta: makuhani, wafalme, na manabii,. Yesu alitimiza ofisi zote hizi tatu za kuwa mpakwa mafuta (kama vile Hebr. 1:2-3). Tazama Mada Maalum: Masihi hapa chini.

MADA MAALUM: MASIHI (SPECIAL TOPIC: MESSIAH)

◙ **"aliopewa na Mungu"** Yesu hakufundisha wala hakufanya lolote bila ufunuo ama ruhusa kutoka kwa Baba (Kama vile Yohana 3:11-13, 31-36; 4:34; 5:19-23,30; 6:38; 7:16; 8:26,28-29,40; 12:49-50; 14:10,24; 15:15). Kithiolojia hii ndio tabia ya Yohana.

◙ **"awaonyeshe watumwa wake mambo ambayo kwamba hayana budi kuwako upesi"** Angalia jinsi ibara hii ya ufunguzi inavyofanana katika Ufu. 22:6-21. Hii ilikuwa mbinu ya kifasihi (yaani, jumuisho) ya karne ya kwanza.

**NASB, NKJV "mambo ambayo lazima yatendeke hivi karibuni"**
**NRSV "ambacho lazima kitokee siku za karibu"**
**TEV "kitakachotokea mapema sana"**
**NJB "kitu ambacho sasa kitatokea mapema sana"**

Kipengele cha muda ni cha muhimu sana kwenye kutafsiri kitabu hiki kwa sababu kinaelezea dhahiri kwamba ujumbe wa Yohana ulikuwa wa muhimu katika siku zake pamoja na siku zijazo. Neno "lazima" (*dei*) lilimaanisha "kile ambacho kinalazimisha, kile kilicho muhimu kimaadili, kile ambacho ni stahiki ama kisicho epukika" (kama vile Ufu. 22:6). Angalia Mada Maalum: Ujio wa mapema hapa chini.

MADA MAALUM: UJIO WA MAPEMA (SPECIAL TOPIC: NEAR RETURN)

◙ **"akamwonyesha"** Hii kikawaida neno (*semainō*) linamaanisha "onyesha" (kama vile kwenye toleo la NKJV). "Ishara" ni mojawapo ya maumbo ya ki-fasihi ambayo Yohana hutumia kuwasilisha ujumbe wake katika injili yake *(semeion*, kama vile Ufu. 12:33; 18:32; 21:19). Hii yaweza kuwa na uhusiano wa agano la kale juu ya manabii wa Agano la Kale(kama vile Isa. 7:11,14; 8:18; 19:20; 20:3; 37:30; 38:7,22; 55:13; 66:19; Yer. 10:2; 32:20-21; 44:29 na Ezek. 4:3; 14:8; 20:12,20). Ukweli kwamba kitabu hiki kinaitwa "ufunuo" kwa njia ya "ishara" na "unabii" kinatupatia mwanga kwenye namna ya uwasilishaji wa fasihi ya kitabu hiki. Neno la fasihi ya leo "kiyama" lililometumika kuelezea namna ya uwasilishaji halikujulikana kwa Yohana.

◙ **"mtumwa wake"** Cheo kina matumizi kadhaa katika kitabu hiki.

1. Kwa namna ya utambulisho wa aya, kifungu hiki kinarejea juu ya mwandishi wa kitume wa kitabu hiki.
2. Sehemu nyingine ndani ya kitabu hiki UWINGI umetumika kwa wahubiri/manabii/wapeleka habari wa Mungu (kama vile Ufu. 10:7; 11:18; 22:6).
3. Hata hivyo, katika sehemu nyingine ndani ya kitabu cheo kimetumika kwa waamini wote (kama vile Ufu. 7:3; 19:2,5; 22:3), ikimaanisha waaminio wote lazima wawe mashahidi (kama vile Mt. 28:18-20; Kol. 4:6; 2 Tim. 2:24-25; 1 Pet. 3:15). Yesu ndiye mfano wa kufuatwa (kama vile. Ufu. 1:5; 3:14; Yohana 20:21)! Wengi watauawa kama Yesu alivyouawa (kama vile Ufu. 6:9; 12:17; 17:6; 18:24; 20:4). Kumbuka dhamira ya kitabu hiki ni kuwa mwaminifu hata kufa! Mimi (Yesu) nimeyashinda!

Mada Maalum: Mtumishi Wangu (Special Topic My Servant)

◙**"Yohana"** Tofauti na waandishi wengine wa matukio ya siku ya mwisho, Yohana alijitambulisha mwenyewe na kuunda ufunguzi wa ushuhuda wake wa kinabii katika mfumo wa barua saba (sura ya 1-3). Baadhi hawakukubali kwamba mtume Yohana ndiye mwandishi wa kitabu cha ufunuo kwa sababu yeye hajulikani katika maandiko yake

mengine ( “anajiita mwanafunzi mpendwa" kwenye injili yake na "mzee” katika II na 3 Yohana), lakini anajiita katika Ufu. 1:4, 9; 22:8.

**1:2 "ushuhuda wa Yesu Kristo"** Kama ilivyo Ufu. 1:1, hiki chaweza kuwa KIIMA, ushuhuda kuhusu Yesu, ama KIIMA MILIKISHI, ushuhuda uliotolewa na Yesu. Wakati mwingine katika maandiko ya Yohana kunakuwa na utata wa makusudi ambao unajumuisha vidokezo vyote.

**1:3"Amebarikiwa"** Hii ni moja kati ya Baraka saba katika kitabu hiki (kama vile Ufu 1:3; 14:13; 16:15; 19:9; 20:6; 22:7,14).kweli kwamba wale waliousoma walibarikiwa haionyeshi si tu asili yake ya uvuvio bali pia uhusika wake kwa watu wa siku hizo na kila siku.

Mada Maalum: Baraka (AGANO LA KALE) (Special Topic: Blessing (OT)

◙**"Heri asomaye"** Toleo la NRSV linaongeza "kwa sauti” ikimaanisha kusoma hadharani," (kama vile 1 Tim. 4:13). Kusoma maandiko mbele ya kusanyiko kulifanyika kwanza na washirika wa kanisa waliofunzwa katika sinagogi (kiongozi wa waimbaji). Kanisa lilianzisha miundo ya kuabudu ndani ya masinagogi ya awali (kama vile Luka 4:16; Matendo 13:15; Kol. 4:16; 1 Thes. 5:27). Tunao uthibitisho wa kihistoria wa kusoma maandiko mbele ya watu kutoka kwa Justin Martyr, B.K. 167, aliyetamka kwamba kanisa lilisoma fungu kutoka kwenye injili na fungu jingine kutoka kwa manabii.

◙ **"wao wayasikiao. . . na kuyashika"** Huku kusikia na kufanya (yote yakiwa katika KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO) ni kiini cha neno la Kiebrania "*Shema*" (kama vile Kumb. 5:1; 6:4-6; 9:1; 20:3; 27:9-10; Luka 11:28). Tazama asili ya kimasharti ya baraka. Wale wanaosikia lazima waitikie. Hili neno" ikiwa. . .halafu" lenye Kielezo cha kimaagano lipo pote Agano la Kale na Agano Jipya. Baraka imeunganishwa sio tu kwenye maarifa bali hata kwenye mtindo wa maisha.

◙ **“ya unabii huu"** Neno hili linatambulisha maudhui yote ya ki-Uungu ndani ya kitabu hiki na namna ya uwasilishaji wa fasihi hii. Kitabu hiki ni mchanganyiko wa nyaraka (sura ya 1-3), na matukio ya siku ya mwisho (Mihuri, baragumu, na mabakuli), na unabii (kama vile Ufu. 22:7,10,18,19). Ni muhimu kukumbuka kwamba “unabii” ulikuwa na vidokezo viwili:

1. Kuwahubiria wasikilizaji wa sasa na ujumbe wa Mungu
2. Kuonyesha jinsi imani ya sasa ilivyoathiri matokeo ya baadaye

Yote haya ni kuwatangazia na kuwatabiria.Tazama makala ya utambulisho.

◙ **"wakati u karibu"**Hii pia inaonyesha uhusika wa unabii kwa siku zake (kama vile Ufu. 22:10, mfano mwingine upo katika Rum. 16:20).

Mada Maalum: Ujio wa Mapema (Special Topic: Soon Return)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 1: 4-7**

**[4] Yohana, kwa yale makanisa saba yaliyoko Asia; Neema na iwe kwenu na amani, zitokazo kwake yeye aliyeko na aliyekuwako na atakayekuja; na zitokazo kwa roho saba walioko mbele ya kiti chake cha enzi; [5] tena zitokazo kwa Yesu Kristo, shahidi aliye mwaminifu, mzaliwa wa kwanza wa waliokufa, na mkuu wa wafalme wa dunia. Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake, [6] na kutufanya kuwa ufalme, na makuhani kwa Mungu, naye ni Baba yake; utukufu na ukuu una Yeye hata milele na milele. Amina. [7] Tazama, yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona, na hao waliomchoma; na kabila zote za dunia wataomboleza kwa ajili yake. Naam. Amina.**

**1:4"kwa yale makanisa saba"** Kwa uhakika sababu ya yale makanisa saba tu kuyatambulisha haijulikani. Zipo nadharia kadhaa:

1. Baadhi wamesema kwamba haya yalikuwa makanisa ambayo Yohana alikuwa nayo uhusiano maalumu wa ki-huduma
2. Wengine wanadai kwamba walitengeneza njia mbadala katika jimbo la Kirumi huko Asia
3. Namba saba ilikuwa na umuhimu kwa Wayahudi hasa katika mwingiliano wa fasihi ya matukio ya mwisho kati ya kipindi cha agano la kale na agano jipya.

Ilikuwa ni hesabu ya utimilifu kutokana na matumizi yake ya siku hizo kwenye Mwanzo 1. Kwahiyo pengine ilitumiwa kwa maana iliyo wazi —Yohana aliyaandikia makanisa kadhaa yaliyotengeneza njia mbadala ya Kirumi huko Asia ndogo—na kiishara ilikuwa ni namna ya kurejea makanisa yote ya siku hizo. Angalia Mada Maalum hapa chini.

## MADA MAALUM: HESABU ZA KIISHARA KATIKA MAANDIKO (SPECIAL TOPIC: SYMBOLIC NUMBERS IN SCRIPTURE)

## MADA MAALUM: KANISA (*EKKLESIA*), (SPECIAL TOPIC: CHURCH *(EKKLESIA*)

◙ **"yaliyoko Asia"** Hii inarejea kwenye miisho iliyoko Magharibi mwa taifa la Uturuki ya leo, iliyokuwa, sehemu kubwa, taifa la kale liitwalo Phrygia, Iliyokuja kuwa jimbo la Kirumi la "Asia Ndogo."

◙ **"Neema na iwe kwenu na amani"** Huu ulikuwa mfumo wa utamaduni wao wa salamu ambao unaonekana mara kwa mara katika maandiko ya Paulo. Wengi wanadai kwamba Wakristo walibadili fasihi ya ki-tamaduni ya salamu ya Kiyunani kutoka "*charein*" (kama vile Yakobo 1:1) kwenda kwenye sauti inayofanana ya salamu ya Kikristo *charis*, ambayo ilimaanisha "neema." Neno "amani" pengine lilihusiana na neno la Kiebrania "*shalom,*" hivyo kuunganisha salamu za KIyunani na Kiebrania ili kuhusianisha makundi yote mawili makanisani. Hata hivyo, hili ni kisio tu.

◙ **"zitokazo kwake yeye aliyeko na aliyekuwako na atakayekuja"** Bila shaka hii ni sifa ya Mungu wa Agano asiyebadilika (kama vile Zab. 102:7; Mal. 3:6; Yakobo 1:17). Muundo wake ki-fasihi ni usio eleweka Kiyunani lakini unaweza kuakisi mazingira ya lugha ya ki-Arama. Kifungu cha maneno halisi ni " kutoka kwake Yeye aliyepo, kutoka kwake Yeye aliyekuwepo, na kutoka kwake Yeye ajaye" (kama vile Ufu. 4:8). Kifungu hiki kinaaksi cheo cha Agano Jipya "MIMI NIKO" (YHWH, kama vile Kut. 3:14, angalia MADA MAALUM: MAJINA YA UUNGU (SPECIAL TOPIC: NAMES FOR DEITY). Kifungu hiki cha maneno kinatumika kumaanisha Mungu Baba katika Ufu. 1:4 na 8, na wa Yesu Kristo katika Ufu. 1:17 na 18 (kama vile Ebr. 13:8). Kuhamisha kwa makusudi kwa vyeo kutoka YHWH kwenda Yesu ilikuwa njia mojawapo ya waandishi wa Agano Jipya ya kutetea Uungu wa Yesu .
Kifungu hiki cha fungamano la utatu wa Mungu yaani aliyekuwako, aliyeko, na atakayekuwako inarekebishwa katika Ufu. 11:17 (yaani, baragumu) na 16:5 (yaani, bakuli), ambako ni Kuja mara ya Pili mwishoni mwa baragumu, kuuthibitisha wakati uliopo na uliopita kwa sababu wakati ujao (nyakati za mwisho) umeanza kudhihirika.

◙ **"na zitokazo kwa Roho saba walioko mbele ya kiti Chake cha enzi"** Angalia Mada Maalum hapa chini.

## MADA MAALUM: ROHO SABA (SPECIAL TOPIC: SEVEN SPIRITS)

**1:5"tena zitokazo kwa Yesu Kristo, shahidi aliye mwaminifu"** Hiki ni kimoja kati ya vifungu vitatu vinavyomwelezea Yesu Masihi. Aya hizi za ufunguzi zinafananishwa na Ufu. 20:6-21. Neno "Mwaminifu" lilikuwa na kidokezo cha Agano La Kale cha mtu ambaye ni mwaminifu, mkweli, na anayetegemewa (kama vile Isa. 55:3-5). Kama neno la Mungu lilivyoandikwa (Biblia) ni lenye kuaminiwa, ndivyo ulivyo ufunuo wake wa ndani, neno liishilo Yesu, (kama vile Ufu. 3:14). Injili ni ujumbe wa kuaminiwa, mtu wa kupokelewa, na maisha yakimfuatishae mtu huyo kuyaishi kwayo.

Kifungu cha Kiyunani, "shahidi wa kweli," kinaweza kumaanisha

1. "Shahidi wangu, Mwaminifu wangu" – kama vifungu viwili, angalia Ufu. 2:13 (pamoja na nyongeza ya KIWAKILISHI CHA NAFSI)
2. "Mwaminifu na shahidi wa kweli," angalia Ufu. 3:14 (pamoja na nyongeza ya "na kweli")

◙ **"mzaliwa wa kwanza wa waliokufa"** Angalia MADA MAALUM: MZALIWA WA KWANZA (SPECIAL TOPIC: FIRST BORN)

◙ **"na mkuu wa wafalme wa dunia"** Kifungu hiki cha maneno, kama kilichotangulia, ni dokezo kwa Zab. 89:27 (kama vile Zab. 72:11; Isa. 48:23), linazungumzia Yesu kama Masihi aliyeahidiwa. Pia kinaaksi mwitikio wa Yohana kwa

1. Kumwabudu mfalme wa majimbo ya mashariki kwenye himaya ya Kirumi "Mfalme wa Wafalme" (kama vile Ufu. 1:15; 17:14; 19:16)
2. Matumizi ya kifungu cha kifalme wa Mesopotamia "Mfalme wa Wafalme" (kama vile Ufu. 11:15; 17:14; 19:16)

Angalia Mada Maalum: Vyeo vya Agano la Kale kwa Yule Mahsusi Ajaye (Special Topic: Old Testament Titles of the Special Coming One)

◙ **"Yeye atupendaye"** Hii ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO, ikimaanisha"Yesu kuendelea kutupenda sisi." Uthibitisho huu ni wa muhimu sana machoni mwa walio wadhaifu na kushindwa kwa yale makanisa matano kati ya saba (kama vile Aya 2-3).

◙ **"na kutuosha dhambi zetu"** Hii ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Tafsiri ya matoleo ya Vulgate na Coptic, pamoja na baadhi ya machapisho ya herufi ndogo ya Kiyunani, na King James Version zina KITENZI"lioshwa" (*louō*) iliyotamkwa sawasawa kama neno "achiliwa" (*luō*). Waandishi wa Kale waliandaa maandiko ya Agano Jipya kwa njia ya mtu mmoja kusoma andiko kwa sauti kubwa wakati wengine waliandika.
Neno hili "achiliwa" (pamoja na vilivyoongezwa) laonekana kwenye machapisho ya Kiyunani ya Kale P[18], א[*] (yakiwa na KIHUSISHI), א[2], A, na C wakati neno "safishwa" linapatikana baadaye kwenye machapisho ya herufi kubwa P (karne ya sita) na 046, kama vile ilivyo baadaye kwenye machapishi ya herufi ndogo (mswada wa Kiyunani uliopo).Hatimaye, neno "achiliwa" ama"funguliwa" ndio likawa limependekezwa.Toleo la UBS[4] hulipatia neno "achiliwa" daraja "lenye uhakika".
Mada Maalum: Uhakiki wa Tofauti za Kiuandishi Kwenye Machapisho (Special Topic: Textual Criticism)

◙ **"katika damu yake"** Hiki ni kidokezo kilicho dhahiri kwa sadaka ya utakaso wa kuwakilishwa na Yesu Kristo (kama vile Mambo ya walawi 1-7), (kama vile Ufu. 5:9; 7:14; 12:11; Marko 10:45; 2 Kor 5:21; Isa. 52:13-53:12). "Kwa damu yake" ni ukweli wa injili unaojirudia jirudia (kama vile Rum. 3:25; Efe. 1:7; 2:13; Kol. 1:20; 1 Pet. 1:18-19. Kwa namna Fulani fumbo la Mungu, Haki yake na sehemu kwa wanadamu wote walioanguka vilikutana katika kifo cha mbadala cha Yesu Kristo (kama vile Hebr. 9:11-28). Angalia Mada Maalum hapa chini.

**MADA MAALUM: MAFUNDISHO YA KANISA LA MWANZO (SPECIAL TOPIC: THE *KERYGMA* OF THE EARLY CHURCH)**

**1:6"na kutufanya kuwa"** Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Kama vile Yesu alivyotufungua kutoka katika dhambi zetu (Ufu. 1:5), Pia ametufanya sisi kuwa ufalme wa makuhani kumwakilisha Yeye!

**NASB "makuhani wa Ufalme kwa Mungu Wake "**

**NKJV** **"wafalme na makuhani kwa Mungu Wake"**

**NRSV** **"ufalme, makuhani wamtumikiao Mungu Wake"**

**TEV, NJB** **" ufalme wa makuhani wamtumikiao Mungu Wake"**

Hiki ni kidokezo kwa neno la Agano la Kale lililotumika kwa Israeli katika Kut. 19:6 na Isa. 61:6, ambapo taifa lilichukuliwa kama ufalme wa makuhani. Mungu alimchagua Ibrahimu aichagua Israeli ili kuuchagua ulimwengu uliopotea (kama vile Mwa. 3:15; 12:3). Israeli ilikusudiwa kuwa taifa la mashahidi (yaani, makuhani) lakini walishindwa kwenye jukumu hili la kiinjilisti walilokabidhiwa (kama vile Ezek. 36:22-38). Kwa hiyo Mungu akalichagua kanisa kuufikia ulimwengu (kama vile Mt. 28:19-20; Luka 24:47; Matendo 1:8). Vifungu hivyohivyo ambavyo vilitumiwa kwa Israeli sasa inatumiwa kwa kanisa (kama vile Gal. 3:29; 6:16; Flp 3:3; 1 Pet. 2:5,9; Ufu. 1:6; 5:10; 20:6).

Ni muhimu kutambua msisitizo wa kibiblia wa kuwa kitu kimoja wa “ukuhani wa waaminio." Ukristo wa kimagharibi umesisitiza kupindukia mahali na jukumu la mtu binafsi na kushusha msisitizo wa muunganiko wa kibiblia. Sitiari ya mwili wa Kristo katika Agano Jipya (kama vile 1 Wakorintho 12) ni sitiari inayofanana. Cheo cha Agano la Kale kamwe hakikumaanisha kuwa kisingizio kwa waaminio kuthibitisha uhuru wao. Msisitizo huu uliendelea kutoka kwenye mapambano kati ya Martin Luther na *the Catholic Church of his day*. Lengo la muktadha huu ni uinjilisti (kama vile Ufu. 1:7), likihusisha kila aaminiye, likidiriki kumfikia mtu yeyote aliyepotea na mhitaji aliyeumbwa kwa mfano wa Mungu ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake (kama vile Yohana 3:16; 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:2; 4:14). Angalia Mada Maalum hapo chini.

**MADA MAALUM: UKRISTO NI USHIRIKA (SPECIAL TOPIC: CHRISTIANITY IS CORPORATE)**

◙ **"Mungu, naye ni Baba yake"** Kifungu hiki chaweza kuonekana kushusha hadhi ya Uungu mtimilifu wa mwana, lakini hakika ni njia ya kuthibitisha kujishusha kwa Yesu alipofanywa mwanadamu. Kifungu hiki kimetumiwa na Paulo katika Rum. 15:6. Hali ya usawa inaweza kuonekana katika Ufu. 3:21; 14:1.

Mada Maalum: Utatu (Special Topic: The Trinity)

Mada Maalum: Ubaba wa Mungu (Special Topic: The Father Hood of God)

◙**"utukufu na ukuu una Yeye"** Neno " utukufu" ni neno la kibiashara la Agano la Kale (kutumia mizani kwa manunuzi) lililomaanisha "kuwa kizito"; kile ambacho kilikuwa kizito (yaani, dhahabu) kilikuwa cha thamani. Neno lilikuja kutumika kwa kuangaza ukuu, utakatifu wa Mungu kutoka kwenye wingu la utukufu, *Shekinah* katika kitabu cha Kutoka. Utukufu ulipatiwa Mungu Baba katika Agano Jipya (kama vile Rum. 11:36; 16:27; Efe. 3:21; Flp. 4:20; 1 Tim. 1:17; 2 Tim. 4:18; 1 Pet. 4:11; 5:11; 2 Pet. 3:18; Yuda 25; Ufu. 1:6; 5:13; 7:12). Angalia Mada Maalu: Utukufu (*doxa*, Agano Jipya [See Special Topic: Groly (*doxa*, NT).

Neno hili "utawala" lililoelezewa kwa Mungu Baba, lafanana kithiolojia na msaidizi wa Mwana (kama vile Yohana 17). Yesu ni wakala wa Baba katika mambo yote, lakini lengo ni utukufu wa ndani wa Baba (kama vile 1 Kor. 15:27-28).

◙**"milele na milele"** Kikawaida hii ni kusema “kwa vizazi na vizazi." Huku kutumia mara mbili kwa *aiōnos*,UMOJA baadaye UWINGi, ni kwa kawaida katika Ufunuo (kama vile Ufu. 1:18; 4:9,10; 5:13; 7:12; 10:6; 11:15; 15:7; 19:3; 20:10; 22:5). Inashangaza kuona kwamba mashahidi wa Kiyunani waliondoa lile la Pili (MSS $P^{18}$, A, P). toleo la $UBS^4$ haziwezi kuamua. Angalia Mada Maalum hapa chini.

**MADA MAALUM: MILELE (NAHAU YA KIYUNANI) SPECIAL TOPIC: FOREVER (GREEK IDIOM)**

**MADA MAALUM: MILELE *('OLAM)* SPECIAL TOPIC: FOREVER ('OLAM)**

◙ **"Amina"** Huu ni muundo wa neno la Kiebrania la agano la kale kwa neno " imani" (kama vile Hab. 2:4).Maana yake ya asili ilikuwa "kuwa imara na hakika." Hata hivyo, kidokezo kilibadilika na kuwa kile kinachopaswa kuthibitishwa (kama vile 2 Kor. 1:20). Kilitumika kimafumbo kwa mtu aliyekuwa mwaminifu, mtii, mwaminifu, thabiti wa kutumainiwa (cheo kwa ajili ya Yesu katika Ufu. 3:14, 2 Kor. 1:20). Angalia Mada Maalum hapa chini.

**MADA MAALUM: AMINA (SPECIAL TOPIC: AMEN)**

**1:7"TAZAMA, YUAJA NA MAWINGU"** Msitari huu ungeweza kuwa ni mshangao wa malaika kwenye Ufu. 1:1. Ni mrejeo dhahiri wa kuja kwa Kristo mara ya pili. Angalia Mada Maalum hapa chini.

**MADA MAALUM: KUJA KATIKA MAWINGU (SPECIAL TOPIC: COMING ON THE CLOUDS)**

◙ **"na kila jicho litamwona"** Hii inaonekana kumaanisha kurudi kwa Yesu kimwili, kisura, kwa wazi, na kwa watu wote, sio kunyakuliwa kwa waaminio. Kwa maoni yangu Biblia kamwe haifundishi unyakuo au kuja kwa siri. Zile aya katika injili (kama vile Mt. 24:37-44; Luka 17:22-37) ambazo mara nyingi hutumika kutetea unyakuo wa siri, ki-muktadha zinahusu ulinganisho na siku za Nuhu. Maandiko haya huonyesha kuja kwake kwa ghafla kusiko tazamiwa. Katika siku ya Nuhu Yule aliyechukuliwa aliangamizwa! Kuwa mwangalifu kutafsiri maandiko kwa kuchukua mafungu madogo ya maandiko kutoka kwenye mpangilio wa asili uliovuviwa na kuyatumia kutetea utaratibu wako wa yale unayoyafasiri kuhusu theolojia juu ya mambo ya kifo hukumu na mwisho wa nafsi!

◙ **"na hao waliomchoma na kabila zote za dunia wataomboleza kwa ajili yake."** Hiki ni kidokezo kwa Zek. 12:10,12 (kama vile Yohana 19:37). Huu ni mfano mzuri wa jinsi Yohana anavyoyachukua maandiko ya Agano la Kale na kuyafanya yaweze kutumika kwenye mazingira yake ya Kirumi (aina ya Kiyahudi ya kutafsiri upya iitwayo *pesher*). Maandiko ya Zekaria ni kichocheo kwenda kwenye matumizi mapya ya Yohana. Katika Zekaria andiko linahusu wakazi wa Yerusalemu wanaoomboleza juu ya "mtu aliyechomwa," lakini hapa Yohana alilitumia kwa viongozi wa Kirumi na Wayahudi waliomsulubisha (kama vile Yohana 19:37). KIWAKILISHI NOMINO cha neno"wao" katika maandiko ya Kiebrania cha Masoretic kimebadilishwa kuwa "makabila yote ya dunia" (kama vile Mt. 24:30, kifungu hiki hakitoki kwenye maandiko ya kale ya Kiyunani). Pia, neno "omboleza," kwenye muktadha wa maandiko ya Zekaria mara nyingi imetafsiriwa kama inayohusiana na Warumi 11, Pale Wayahudi wanapotubu na kumwamini Yesu kama Masihi. Hata hivyo, katika Ufu. 1:7 maombolezo sio kwa ajili ya toba, bali kwa sababu hukumu ya Mungu imeanguka juu ya wasio amini kutoka makabila yote (kama vile Mt. 24:30). Muktadha wa Zekaria unarejerea hukumu ya nyakati za mwisho ya mataifa yaliyotajwa "bonde la Megiddo," katika Kiebrania laitwa Armageddon (kama vile Zek. 12:11; 2 Nya. 35:22 na Zaburi 2; Ufu. 16:16), eneo la vita dhidi ya Mungu na watu wake na shetani na watu wake, mataifa wasio amini. Angalia Mada Maalum hapa chini.

**MADA MAALUM: IBADA KWA WALIO KATIKA HUZUNI (SPECIAL TOPIC: GRIEVING RITES)**

◙ **"Naam, Amina."** Hili ni neno la kiyunani kwa kuthibitisha (*nai*) na neno la Kiebrania kwa kuthibitisha (*amen*) yamewekwa yakiwa sambamba kwa ajili ya msisitizo (kama vile Ufu. 22:20).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 1: 8**

8 **Mimi ni Alfa na Omega, mwanzo na mwisho, asema Bwana Mungu, aliyeko na aliyekuwako na atakayekuja, Mwenyezi.**

**1:8** YHWH Mwenyewe hutamka aya hii akithibitisha ukweli wa maelezo ya awali kuhusu Yesu. Inajumuisha vyeo vinne kwake Yeye pamoja na kidokezo cha tano na cha sita. Yaonekana, Ufu. 1:8 ulikuwa ukiongezea uthibitisho wake mwenyewe kwenye maelezo kwa matumizi ya majina haya matukufu.

1. "MiMI NDIMI," ambalo ni dokezo kwenye jina la Agano YHWH (kama vile Kut. 3:14), muundo wa KITENZI"kuwa." Yesu alitumia hili kwa nafsi yake (kama vile Yohana 8:56-59).

2. "Alfa na Omega" ndio herufi za kwanza na mwisho za alfabeti ya Kiyunani ambazo inasadiki bila ushahidi kwamba Mungu ndiye mwanzo na mwisho mtawala wa historia, (kama vile Isa. 44:6; Ufu. 21:6); cheo hiki pia kinatumiwa kwa Yesu katika Ufu. 1:17 na 22:13.
3. "Bwana" ndio njia ya kisasa ya kutafsiri YHWH (cheo "Bwana" [*kurios*] katika Agano Jipya huakisi cheo hiki cha Agano la Kale.).
4. "Mungu" katika Mwa. 2:4, YHWH, na *Elohim* yameunganishwa (BWANA Mungu) kama jina kwa uungu. *El* ndilo jina la jumla kwa Mungu wa Mashariki ya karibu, kutoka katika mzizi wa neno"kuwa mwenye nguvu."
5. "Yeye aliyepo na Yeye aliyekuwako, Yeye ajaye" ni kirai kilichotumika mapema katika Ufu. 1:4, kinayozungumzia, Mungu asiye badilika aishiye daima (kama vile Zab. 102:27; Mal. 3:6; Yakobo 1:17). Kirai hiki kinatumika kwa Mungu Baba, YHWH, katika Ufu. 1:4 na 8 na kwa Yesu, Mungu Mwana, katika Ufu. 1:17,18 na 22:13 (kama vile Ebr. 13:8).
6. "Mkuu" ambalo lilikuwa jina la Agano la Kale, (a) "*El-Shaddai,*" jina la Baba wa Familia kwa Mungu (kama vile Kut. 6:3) au (b) "YHWH *Sabaoth*," kutoka LXX "Bwana Mungu mwenye enzi. Linapatikana mara nyingi kitabuni humu (yaani, *pantokratōr*, kama vile Ufu. 4:8; 11:17; 15:3; 16:7,14; 19:6,11; 21:22), lakini mara moja tu katika vitabu vingine vya Agano Jipya (yaani, 2 Kor. 6:18). Angalia Mada Maalum: Shaddai (Special Topic: Shadai

Chapisho moja la kale la Kiyunani, *aleph* (א[*]), na maandiko kadhaa ya badae yanaongeza kirai "mwanzo na mwisho " " baada ya Alfa na Omega." Waandishi waliingiza kutoka Ufu. 21:6, lakini pengine halitoki kwenye sehemu ya asili ya maandiko ya asili yaliyovuviwa ya Kiyunani. toleo la UBS[4] hupima kuondolewa kwake kama "chenye uhakika." Angalia Mada Maalum hapa chini.

**MADA MAALUM: MAJINA YA UUNGU (SPECIAL TOPIC: DEITY),** C. na D.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 1: 9-11**
**9 Mimi Yohana, ndugu yenu na mwenye kushiriki pamoja nanyi katika mateso na ufalme na subira ya Yesu Kristo, nalikuwa katika kisiwa kiitwacho Patmo, kwa ajili ya Neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu. Nalikuwa katika Roho, siku ya Bwana; nikasikia sauti kuu nyuma yangu, kama sauti ya baragumu, ikisema, Haya uyaonayo uyaandike katika chuo, ukayapeleke kwa hayo makanisa saba: Efeso, na Smirna, na Pergamo, na Thiatira, na Sardi, na Filadelfia, na Laodikia.**

**1:9-20** Haya ni maono ya Kristo aliyefufuka, aliyepaa mbinguni, aliyeinuliwa. Maelezo haya yana tumika kutambulisha makanisa saba (sura 2-3). Yohana huonyesha utambulisho wake na wasomaji kwa (1) kutumia neno "ndugu yenu" na (2) kutamka uzoefu wake mwenyewe wa mateso, na ufalme wa ustahimilivu. Maneno haya makuu— mateso, ufalme wa uvumilivu — pia ni mifano ya maisha ya Yesu ambayo wasomaji, kama Yohana wanalazimika kuyafanya kwa ubora zaidi (Kama vile Yohana 16:33; Matendo 14:22; Rum. 8:17).
Sababu moja inayowafanya wafasiri wa magharibi wa leo kutokielewa kitabu cha ufunuo ni kwa sababu hatujawahi kupitia mateso na majaribu ya ulimwengu wa Warumi wa karne ya kwanza. Ufunuo ni neno kwa waaminio wanaoteswa,wanaokufa, wanaotishwa.

**1:9 "kushiriki pamoja nanyi katika mateso"** Angalia angalizo katika Ufu. 7:14.

Mada Maalum: Mateso (Special Topic: Tribuation)

◙ **"ufalme"**Angalia MADA MAALUM: UFALME WA MUNGU (SPECIAL TOPIC: THE KINGDOM OF GOD)

◙ **"subira"** Neno hili limetumika katika Ufu. 2:2,3,19; 3:10; 13:10; 14:12.

MADA MAALUM: USTAHIMILIVU (SPECIAL TOPIC: PERSEVERANCE)

◙ **"katika kisiwa kiitwacho Patmo"** Warumi walitumia visiwa vidogo mbali kidogo kutoka pwani ya Asia ndogo kuwapeleka uhamishoni wafungwa wa kisiasa (kama vile Tacitus' *Annals*, 3.68; 4.30; 15.71).Yawezekana Yohana alikuwa uhamishoni kwenye kisiwa hiki kidogo, maili 37 kutoka mileto. Kisiwa kilikuwa na umbile la mwezi mchanga, kikielekea mashariki, maili sita.

◙ **"kwa ajili ya Neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu"** Kuna tafsiri mbili za kirai hiki ambazo zinaweza kukubalika. Inaweza kuhusu (1) kuhubiri injili kwa Yohana ama (2) kupokea ufunuo kwa Yohana. Tunayo marejeo kadhaa ya kihistoria ya kupelekwa uhamishoni.

1. Tertullian, *On the Prescription of Heretics,* 36
2. Origen, *Homilies on Matthew*
3. Clement of Alexandria, *The Rich Man's Salvation,* 47
4. Eusebius, *Ecclesiastical History*, III.20.8-9; and (4) Jerome, *Concerning Illustrious Men,* 9.

**1:10 "nalikuwa katika roho"** Hiki ni kifungu cha maneno chenye kuweka alama kwenye maono tofauti ambayo yohana aliyapokea (kama vile ufu. 1:10; 4:2; 17:3; 21:10). Inaonekana kurejea juu ya hali kama ya kupagawa ama kuzubaa wakati ufunuo ulipotolewa (kama vile matendo 10:10; 22:17; 2 kor. 12:1na kuendelea). Hii ni tabia ya Kiyahudi juu ya matukio ya siku ya mwisho.

Mada Maalum: Roho (*pneuma*) katika Agano Jipya (Special Topic: Spirit (*Pneuma*) In the NT)

◙ **"siku ya Bwana"** Hii ndiyo nukuu pekee ndani ya Biblia, ikirejea jumapili, inayotumia kirai hiki. Jumapili ilirejea “siku ya kwanza ya juma” katika Yohana 20:19; Matendo 20:7 na 1 Kor. 16:2.

◙ **"kama sauti ya baragumu"** Kirai hiki kilitumika katika muktadha wa Mungu kutoa amri kumi kwenye mlima Sinai (kama vile Kut. 19:16). Hata hivyo kwasababu ya Ufu. 1:12a na 4:1, inaweza kuhusu sauti ya malaika. Upatanisho wa malaika unaashiria kwenye fasihi ya maangamizi ya mwisho wa ulimwengu.

MADA MAALUM: PEMBE ZILIZOTUMIWA NA WAISRAEL (SPECIAL TOPIC: HORNS USED BY ISRAEL)

**1:11"katika kitabu"** Hili ni neno la Kiyunani *biblion.* Lilitumika katika maana ya kijitabu ama gombo. Baadaye likawa neno la kutumika mahali pa miswaada ya kale ama kitabu. Yohana alilazimishwa kuandika maono yake. Maono hayo yanajifunua Ki-Ungu. Hayapo kwa manufaa binafsi ya Yohana bali kwa kanisa. Tabia Mojawapo ya maandiko juu ya matukio ya siku ya mwisho ni kwamba ilikuwa aina maalum ya fasihi iliyoandikwa, kwa mpangilio wa hali ya juu, ambayo haikutolewa kwa maneno ya kinywani kama unabii wa Agano la Kale. Kitabu ama gombo hutokea mara nyingi kwenye maandiko ya Kiyahudi juu ya matukio ya siku ya mwisho wa ulimwengu kama njia ya kupitisha ujumbe kwa ajili ya wasomaji.

◙ **"ukayapeleke kwa hayo makanisa saba"** Amri kwa haya makanisa ilikuwa ni kuifuata njia kuu ya Kirumi iliyoanza na kuishia Efeso. Kitabu cha Paulo chenye kuzunguka miongoni mwa watu kijulikanacho kama “Waefeso” yawezekana nacho kilisafilishwa kwa njia hii moja. Ufunuo wa Mungu sio kwa ajili ya mtu mmoja tu, bali ni kwa ajili ya watu wa Mungu, ambao ni mwili wa Kristo!

Mada Maalum: Mifano ya Namba katika Maandiko (Special Topic: Symbolic Numbers In Scripture), #4

◙ Tafsiri ya King James inaongeza kifungu "Mimi ni Alpha na Omega" tena, lakini hakuna machapisho ya Kiyunani ya Kale yoyote yanayotetea kifungu hiki kuwa ndani ya aya hii

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 1: 12-16**

[12] **Nikageuka niione ile sauti iliyosema nami. Na nilipogeuka, niliona vinara vya taa saba vya dhahabu;** [13] **na katikati ya vile vinara nikaona mtu mfano wa Mwanadamu, amevaa vazi lililofika miguuni, na kufungwa mshipi wa dhahabu matitini.** [14] **Kichwa chake na nywele zake zilikuwa nyeupe kama sufu nyeupe, kama theluji; na macho yake kama mwali wa moto;** [15] **na miguu yake kama shaba iliyosuguliwa sana, kana kwamba imesafishwa katika tanuru; na sauti yake kama sauti ya maji mengi.** [16] **Naye alikuwa na nyota saba katika mkono wake wa kuume; na upanga mkali, wenye makali kuwili, ukitoka katika kinywa chake; na uso wake kama jua liking'aa kwa nguvu zake.**

**1:12"niliona vinara vya taa saba vya dhahabu"** Hii hairejei vinara saba vya dhahabu vilivyokuwa ndani ya hema takatifu lilitumiwa na Wayahudi (kama vile Kut. 25:31-40) wala kinara cha taa cha Zek. 4:2. Hivi kinara kimoja kilikuwa ishara ya kurejerea, kwa makanisa saba (kama vile Ufu. 1:20; 2:1).

Mada Maalum: Roho Saba katika Ufunuo (Special Topic: Seven Spirits in Revelation)

**1:13-18** Katika maelezo haya ya Yesu sehemu kubwa ya taswira yake ina historia mbili za Agano la kale: (1) YHWH, lakini pia (2) malaika wa Daniel 10.

**1:13**

**NASB "mtu mfano wa mwanadamu"**

**NKJV "mtu mfano wa mwanadamu"**

**NRSV "mtu mfano wa mwanadamu"**

**TEV "akifanana kama mwanadamu"**

**NJB "mtu kama Mwana wa Adamu"**

Tambua namna ya utumiaji wa herufi kubwa. Sababu ni utata wa neno. Katika Agano la Kale kilikuwa ni kifungu kinachomwelezea mwanadamu (kama vile Zab. 8:4; Ezek. 2:1 na nyingine nyingi). Hata hivyo,kimetumika katika Dan. 7:13 na ikiwezekana Ezek. 1:26 kikirejea juu ya Masihi aliyekuwa mwanadamu, ambaye Uungu wake (kama vile Ufu 2:18, ambaye kwa maana nyingine huitwa "Mwana wa Mungu") unasadikiwa kwasababu

1. Anajiwasilisha mbele za Mungu
2. Huruka juu ya mawingu mbinguni
3. Amepewa ufalme wa milele.

Yesu alitumia neno hili kujirejea Mwenyewe kwa sababu halikuwa na matumizi ya Kiualimu wa dini ya Kiyahudi, halikuwa na vidokezo vya kiutaifa wala kijeshi. Linaunganisha kipengele cha ubinadamu na Uungu wa Yesu kama mwanadamu (kama vile 1 Yohana 4:1-3; Yohana 1:1-2,14).

Tambua kwamba matoleo ya NKJV na NRSV yana neno"wale” wakati NASB, TEV, na JB yana neno“yule.” Hakuna KIBAINISHI CHENYE UKOMO katika maandiko ya Kiyunani (kama vile Dan. 7:13; Ebr. 1:2; 3:6; 5:8; 7:28). Hata hivyo, ukweli kwamba sifa yake zinakifanya kiwe na ukomo. Utata wake ni wa kimakusudi. (mwonekano wa maandiko ya Yohana). Yesu ni Mwanadamu halisi na pia Masihi wa Ki-Ungu.

Mada Maalum: Mwana wa Adamu (Special Topic: Son of Man)

◙**"amevaa vazi lililofika miguuni, na kufungwa mshipi wa dhahabu matitini"** Kifungu hiki kinaeleweka kwa njia kadhaa.

1. Kama rejeo la kuhani mkuu (kama vile Kut. 28:4; 29:5; Law. 16:4 na Zek. 3:4)
2. kama rejeo la mtu mtawala, tajili (kama vile 1 Sam. 18:24; 24:12 na Ezek. 26:16)
3. kama maono ya malaika mfasiri mwenye utukufu wa Dan. 10:5-21, ambavyo ingeweza kumaanisha Yesu kama mleta ujumbe wa Mungu.

Josephus, kwenye kitabu chake, *Antiquities of the Jews* III.7.2,4, alisema kwamba kuhani mkuu alivaa vazi la dhahabu. Kwahiyo, Yesu ni Kuhani Mkuu (kama vile Zab. 110:4-7; Zekaria 3) (kama vile Ebr. 8:1-13; Zaburi 110).

**1:14"Kichwa chake na nywele zake zilikuwa nyeupe kama sufu nyeupe"** Hiki ni kidokezo cha siku za kale katika Dan. 7:9. Huu ndio mfano wa waandishi wa Agano Jipya wakidhani ndio sababu ya sifa zake na ufafanuzi wa YHWH kwa Yesu, kusisitiza Utatu wa Yesu.

◙ **"na macho yake kama mwali wa moto"** Hii inaashiria maarifa yake yanayopenya (kama vile Dan. 10:6; Ufu. 2:18; 19:12).

**1:15**

**NASB "kama shaba iliyosuguliwa sana kana kwamba imesafishwa katika tanuru"**

**NKJV "kama shaba nyeupe, kama kwamba imesafishwa kwenye tanuru"**

**NRSV " kana shaba safi, imesafishwa katika tanuru"**

**TEV "kama shaba iliyosuguliwa na kusafisha"**

**NJB "Kama shaba inayosuguliwa na kusafishwa"**

Neno lililotumika kwenye shaba (*chalkolibanon*) halijulikani. Shaba inahusiana na neno, *chalkos* (kama vile Mt. 10:9; 1 Kor. 13:1; ufu. 18:22). Lililotumika katika Ezek. 1:7 ikimaanisha miguu ya Kerubi na katika Dan. 10:6 kwa malaika mpeleka habari. Miguu ya Yesu inaelezwa katika neno hilo hilo (kama vile Ufu. 1:15; 2:18) kuonyesha asili yake huko mbinguni ama tabia ya ukuu.

**NASB, NKJV, NRSV "sauti ilikuwa kama sauti ya maji mengi"**

**TEV "sauti ilitoka kama maporomoko ya maji mengi"**

**NJB "sauti kama sauti ya bahari"**

Hili lilitumika kwa ajili ya

1. YHWH katika Ezek. 1:24; 43:2
2. Mbawa za Makerubi wa Ezek. 1:24
3. Kwa malaika wa kupeleka habari (yumkini) katika Dan. 10:6

Yaonekana ilikuwa ishara ya sauti ya mtu mwenye mamlaka kutoka mbinguni (kama vile Ufu. 14:2; 19:6).

**1:16 "Naye alikuwa na nyota saba katika mkono wake wa kuume"** Kifungu hiki kimerudiwa katika Ufu. 1:16,20; 2:1; 3:1. Hii inaonyesha uangalizi binafsi wa Yesu kwa makanisa yake ya mahali.

◙ **na upanga mkali, wenye makali kuwili, ukitoka katika kinywa chake"** *Hromphaia* inarejea upanga wa Kirumi waliubeba, huu upanga mpana huonekana kwenye Agano la Kale katika Isa. 11:4; 49:2. Unaashiria vita (kama vile ufu. 2:16; 6:8). Nguvu ya neno la Mungu, (kama vile Ufu. 2:12; 19:15,21; 2 The. 2:8).
Waebrania 4:12 hutumia aina nyingine ya upanga (*machaira*), lakini katika dhana ya aina ile ile—nguvu ya neno la Mungu.

◙ **"na uso wake kama jua liking'aa kwa nguvu zake"** Kifungu kama kile kile kimetumika kuelezea malaika anayepeleka habari wa Dan. 10:6 na ufu. 10:1. Katika Dan. 12:3 (kama vile Mt. 13:43) ilikuwa ni ishara ya wale wenye haki waliofufuliwa. Yesu anaelezewa kwa maneno yafananayo na hayo wakati ule wa kubadilika kwake sura (kama vile. Mt. 17:2).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 1: 17-20**

**[17] Nami nilipomwona, nalianguka miguuni pake kama mtu aliyekufa. Akaweka mkono wake wa kuume juu yangu, akisema, Usiogope, Mimi ni wa kwanza na wa mwisho, [18] na aliye hai; nami nalikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na milele. Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu. [19] Basi, uyaandike mambo**

**hayo uliyoyaona, nayo yaliyopo, na yale yatakayokuwa baada ya hayo. [20] Siri ya zile nyota saba ulizoziona katika mkono wangu wa kuume, na ya vile vinara saba vya dhahabu. Zile nyota saba ni malaika wa yale makanisa saba; na vile vinara saba ni makanisa saba.**

**1:17 "nalianguka miguuni pake kama mtu aliyekufa."** Aina hii ya ufunuo kila wakati imekuwa ikisababisha mshangao mkubwa wa kuvunjika moyo kwa watu wanaoupokea (kama vile Dan. 8:17; 10:9; Ezek. 1:28; 3:23; II Baruk 21:26; IV Ezra 5:14). Ni kitu cha kusababisha mshangao kwa ulimwengu wa kiroho usio wa kawaida kujifunua wenyewe kwa mwanadamu.

◙ **"Akaweka mkono wake wa kuume juu yangu"** Kitendo hiki kinaonyesha kujali pamoja na umakini wa Yesu kwa watu wake (kama vile Dan. 8:18; 10:10, 18).

◙ **"Usiogope"** Hii ni KAULI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ikiwa na KIAMBATA HASI, kwa kawaida ikiwa na maana kuzuia kitendo ambacho kipo kwenye mchakato. Wanadamu wanauhofu ulimwengu ule usio wa kawaida (kama vile maneno ya Yesu katika Mt. 14:27; 17:7; 28:10; Marko 6:50; Luka 5:10; 12:32; Yohana 6:20 na maneno ya malaika katika Mt. 28:5; Luka 1:13,30; 2:10).

◙ **"Mimi ni wa kwanza na wa mwisho"** Hii kawaida ilikuwa nukuu inayomhusu YHWH (kama vile Isa. 41:4; 44:6; 48:12), Lakini hapa ilitumika kwa Kristo aliyeinuliwa (kama vile Ufu. 1:8; 2:8; 22:13). Hii inafanana na kifungu "Alfa na Omega." Angalia nukuu katika Ufu. 1:4 na 8.

**1:18**

| | |
|---|---|
| **NASB, NRSV** | **"yeye aishiye"** |
| **NKJV** | **"mimi ndimi yule aishiye"** |
| **TEV** | **"mimi ndiye aishiye"** |
| **NJB** | **"Mimi ndiye aishiye"** |

Hili ni dokezo la jina la agano la Mungu, YHWH, linalotokana na KITENZI cha Kiebrania "kuwa" (kama vile kut. 3:14). Yeye ni yule aishiye nyakati zote, pekee aishiye (kama vile Dan. 12:7; Yohana 5:26). Yohana 8:58.

Mada Maalum: Majina Ya Uungu (Special Topic: Names for Deity), D.

◙ **"nami nalikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na milele"** Ufufuo ulikuwa:

1. Mhuri wa ukubalifu wa Baba (kama vile Matendo 2:24; 3:15; 4:10; 5:30; 10:40; 13:30,33,34,37; 17:31; Rum. 4:24; 10:9; 1 Kor. 6:14; 15:15; Efe. 1:20; Col. 2:12; Ebr. 13:20; 1 Pet. 1:21)
2. Udhihirisho wa nguvu ya Roho (kama vile Rum. 8:11)
3. Udhihirisho wa nguvu binafsi za Yesu (kama vile Yohana 10:11,15,17,18)

Haya marejeo ya kifo cha Yesu yangeweza kuwa njia ya kuwekea pingamizi kwa walimu wenye mafunuo ya uongo waliokataa ubinadamu wake.

◙ **"Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu"** Wayahudi waliona kifo kama gereza lenye malango (kama vile Ayubu 38:17; Zab. 9:13; 107:18; Isa. 38:10; Mt. 16:19). Funguo ni msemo wa fumbo kwa mamlaka ya Yesu juu ya kifo chake mwenyewe na cha wafuasi wake. (kama vile Ufu. 5:9-10; 1 Kor. 15).

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV, NRSV, NJB** | **"Kuzimu"** |
| **TEV** | **"ulimwengu wa wafu"** |

Toleo la King James linaitafasiri hili kama “kuzimu,” lakini huu ni mkanganyiko wa tafasiri ya Kiingereza ya maneno ya Kiyunani *Hades* na *Gehenna.*neno *Hades* linafanana na lile lililoko agano la kale *sheol* (k.v. Ufu. 6:8; 20:13-14). Katika Agano la Kale wanadamu walionekana kama wanaoshuka kuja duniani pale walipokusanyika kutengeneza

familia nyingi. Ni maisha yaliyotambulika lakini yasiyo na raha. Pole pole Mungu alianza kufunua zaidi na zaidi (ufunuo endelevu) kuhusu maisha baada ya kifo. Waalimu wa dini ya Kiyahudi walieleza kwamba kulikuwepo na sehemu ya haki (Paradiso) na sehemu ya uovu (shimoni) kule Shiro (kama vile Luka 23:43). Biblia hutoa vielelezo vya picha katika habari za maisha baada ya kifo. Inazungumzia mafumbo ya mbinguni (yaani, mabarabara ya dhahabu, mji maili 1500 urefu, upana na kimo hakuna malango yanayofungwa etc.) (moto, giza, funza, n.k.)

**MADA MAALUM: Wako Wapi Waliokufa? (SPECIAL TOPIC: Where Are the Dead?,** I. B. and II. B.

**1:19** Kifungu hiki kimekuwa kikitumika kama sehemu ya ufasiri wa kitabu hiki cha Ufunuo. Unaonekana kama maono yenye sehemu mbili ama tatu. Yanaonekana kuwa maono mojawapo ama mara mbili zaidi au tatu zaidi. Kifungu cha Kiyunani ni maelezo mara mbili zaidi ya kile kilchopo na kile kitakachotokea.Yohana alikuwa anazungumza kuhusu siku zake na siku zilizokuwa zinafuata. Kitabu hiki kinaunganisha mionekano yote miwili katika dhana ya unabii wa kimapokeo wa matukio ya wakati huo ikiashiria matukio ya siku ya mwisho ya mpinga Kristo (kama vile Dan. 9:24-27; 2 Thessalonike 2).

**1:20"Siri ya zile nyota"** Neno hili (*mustērion*) linatumiwa na Paulo kwa maana mbali mbali, lakini zote zinahusu umilele, mpango wa Mungu uliojificha kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu, ambapo Wayahudi na watu wa mataifa waaminio watafanywa kuwa mwili mpya katika Kristo (kama vile Efe. 2:11-3:13). Hapa, hata hivyo, laonekana kutumika kwenye yale makanisa saba ambayo Yesu anayatambulisha katika sura ya 2 na 3. Kutoka aya 20 ni dhahiri kwamba roho saba, nyota saba, vinara saba vya dhahabu, na malaika saba yote ni mifanao kwa namna moja kumaanisha yale makanisa saba.neno hili limetumika kwa namna ile ile ya maana ya siri ya alama katika Ufu. 17:7. Angalia maelezo na Mada Maalum: Fumbo (Special Topic: Mystery).

◙ **"malaika"** Neno la Kiyunani (*aggelos*) na Kiebrania (*malak*) yanaweza kutafsiriwa "wapeleka habari" au "malaika." Kumekuwepo nadharia kadhaa yenye kufanana kwayo.

1. Baadhi wanasema kulikuwepo roho saba ambazo zimetajwa katika aya ya 4.
2. Wengine wanasema walikuwa wachungaji wa makanisa haya (kama vile Mal. 2:7).
3. Wengine wanasema inahusu malaika alindaye makanisa haya (kama vile Dan. 10:13,20,21).

Yaonekana vizuri zaidi kwamba wao wanahusika na makanisa kuyafanyika kuwa kama kitu chenye tabia ya binadamu kwa jumla, yakiwa badala ya mchungaji ama malaika.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujisomea wa fasiri, ambao una maana kuwa, unawajibika kwa tafsiri yako binafsi ya Biblia. Kila moja wetu sharti atembee katika nuru tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni kipaumbele katika tafasiri. Usiachie kazi hii kwa mfasiri.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa kukusaidia mambo muhimu ya kipengele cha kitabu hiki. Yamekusudiwa kukuchokonoa mawazo na sio kutoa maana.

1. Sura ya 1 inatoa kweli au mawazo yoyote yawezayo kuasaidia kujua jinsi ya kutafsiri kitabu cha ufunuo?,
2. Je kitabu cha ufunuo kimekusudiwa kwa siku zake ama kwa siku za mwisho? Kwanini?
3. Kwanini Yohana anafanya vidokezo vingi kwenye Agano la Kale lakini hafanyi nukuu ya moja kwa moja kutoka kwake?
4. Kwa nini kuna vyeo vingi sana vilivyotumika kwa Mungu katika sura hii?
5. Kwa nini maelezo ya Ufu. 1:12-20 yalitumika kutambulisha kila moja ya makanisa saba kwenye sura ya 2 na 3?
6. Kwanini Yesu aliyetukuzwa anaelezwa kufanana na malaika wa Dan. 10?

# UFUNUO 2 – 3

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Ujumbe kwa Waefeso | Kanisa Lililopungukiwa upendo | Waraka wa Kwanza | Ujumbe kwa Waefeso | Efeso |
| 2:1a | 2:1-7 | 2:1 | 2:1a | 2:1-7 |
| 2:1b-7 | | 2:2-7 | 2:1b-7a | |
| | | | 2:7b | |
| Ujumbe kwa Smirna | Kanisa Lililoteswa | Waraka wa Pili | Ujumbe kwa Smirna | Smirna |
| 2:8a | 2:8-11 | 2:8 | 2:8**a** | 2:8-11 |
| 28b-11 | | 2:9-11 | 2:8b-10 | |
| | | | 2:11a | |
| | | | 2:11b | |
| Ujumbe kwa Pergamo | Kanisa Lenye Kuchukuliana | Waraka wa Tatu | Ujumbe kwa Pergamo | Pergamo |
| 2:12a | 2:12-17 | 2:12 | 2:12a | 2:12-13 |
| 2:12b-17 | | 2:13-17 | 2:12b-16 | 2:14-17 |
| | | | 2:17a | |
| | | | 2:17b | |
| Ujumbe kwa Thiatira | Kanisa Fisadi | Waraka wa Nne | Ujumbe kwa Thiatira | Thiatira |
| 2:18a | 2:18-29 | 2:18 | 2:18a | 2:18-29 |
| 2:18b-29 | | 2:19-29 | 2:18b-23 | |
| | | | 2:24-28 | |
| | | | 2:29 | |
| Ujumbe kwa Sardi | Kanisa Lililokufa | Waraka wa Tano | Ujumbe kwa Sardi | Sardi |
| 3:1a | 3:1-6 | 3:1a | 3:1a | 3:1-6 |
| 3:1b-6 | | 3:1b-6 | 3:1b-5 | |
| | | | 3:6 | |
| Ujumbe kwa Filadelfia | Kanisa Aminifu | Ujumbe wa Sita | Ujumbe kwa Filadelfia | Filadelfia |
| 3:7a | 3:7-13 | 3:7 | 3:7a | 3:7-13 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3:7b-13 | | 3:8-13 | 3:7b-12 | |
| | | | 3:13 | |
| Ujumbe kwa Laodikia | Kanisa la Uvuguvugu | Waraka wa Saba | Ujumbe kwa Laodikia | Laodikia |
| 3:14 | 3:14-22 | 3:14 | 3:14a | 3:14-22 |
| 3:14b-22 | | 3:15-22 | 3:14b-21 | |
| | | | 3:22 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI "kutoka [Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia"(A Guide to Good Bible Reading)]

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA.*

Huu ni mwongozo wa usomaji wa fasiri ambayo inamaanisha kwamba unao wajibu wa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembeee katika nuru tuliyo nayo. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika kukalimani. Hupaswi kumuachia mfasiri vitu hivi.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua mada. Linganisha mgawanyiko wa mada zako kwa ulinganifu wa tafsiri tano za hapo juu. Kugawa ki-aya hakujavuviwa, lakini ni ufunguo wa kufuatilia kusudio la awali la mwandishi, ambachoo ndicho kiini cha kukalimani. Kila aya inayo mada moja na ni moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu,
4. Nk.

## USULI WA JUMLA

A. Sehemu hii ya fasihi (sura ya 2-3) imeunganishwa na vyeo vya Agano la Kale vya YHWH vilivyotumiwa na Masihi (kama vile Ufunuo 1:12-20). Hii ni njia moja ambayo kwayo mwandishi wa Agano Jipya aliuthibitisha Uungu wa Yesu. Ufunuo wa Yohana unahamisha vyeo ya Agano la Kale na matendo ya YHWH kwa Yesu, aliyepaa, Masihi anayetukuzwa.
B. Kusudi lake ni kuyaonyesha mahitaji ya kiroho ya makanisa haya saba ya karne ya kwanza, na kwa mtiririko, makanisa yote (yaani, hesabu saba). Huduma ya Yohana katika zama zake ilikuwa katika Asia Ndogo, hasa huko Efeso. Yohana ki uwazi sana ana ufahamu juu ya makanisa haya na miji. Nyaraka hizi zinaonyesha upande wa maadili ya Ukristo. Wao ni wito wa uaminifu na utauwa. Kanisa pia litahukumiwa (kama vile 2 Wakorintho 5:10).
C. Kulikuwa na makanisa mengi katika jimbo la Kirumi la Asia Ndogo katika siku za Yohana. Kwa nini mwandishi aliandika kwa hayo saba tu?
   1. Ni tarakimu ya kibiblia inayoonyesha ukamilifu (kama vile Mwanzo 1). Kuna aina nyingi za fasihi za namba saba katika unabii wa Yohana.
   2. Makanisa haya yalitengeneza njia ya kusafiri, kuanzia Efeso na kuishia Laodikia. Inawezekana lilikuwa pito la safari asisi.
   3. Kwa namna fulani kuna kiasi cha uwakilishi wa aina ya makanisa yanayopatikana katika kila kizazi na tamaduni.
D. Ni nini umuhimu wa kipengele hiki cha fasihi kwetu leo?
   1. Baadhi wanayatafsiri makanisa haya kama maelezo ya unabii wa historia ya Magharibi tangu Pentekoste mpaka Kuja kwa Mara ya Pili.
      a. Efeso = Kipindi cha Mitume, 33-100 B.K. (Pentekoste hadi kwa Yohana)
      b. Smirna = Kipindi cha mateso, 100-313 B.K. (Yohana hadi kwa Constantine)
      c. Pergamo = Kipindi cha Constantine, 313-590 B.K. (Constantine hadi kwa Gregory)

d. Thiatira = Roma ya Upapa, 590-1517 B.K. (Gregory hadi kwa Luther)
e. Sardia = Matengenezo, 1517-1792 B.K. (Luther - Carey)
f. Filadelfia = Vuguvugu la Kisasa la Umisionari, 1792-1914 B.K. (Carey hadi unyakuo)
g. Laodikia = Kipindi cha Uasi, 1914 B.K. - Parousia (WWI - Parousia)

Hivi ni vipimo vya kutafakari ya hivi karibuni ambayo imejitokeza na "fafanuzi ya miaka elfu iliyopita" (ambayo mara nyingi huiona Mathayo 13 katika mfanano wa yale makanisa 7). Hata hivyo, hakuna kitu katika uandishi wenyewe wa kuuthamini mtazamo huu. Ingawa baadhi ya mambo ya historia ya magharibi yanakifaa kiini hiki, wasio kuwa nacho wengine. Ni sawa na kiburi kuthibitisha kuwa Biblia ilikuwa imeandikwa ki-pekee ili kuushughulikia utamaduni wa magharibi tu. Mpango huo usingekuwa na maana kwa wasikilizaji wa karne ya kwanza.

2. Wengine hutafsiri makanisa haya kama sampuli-wakilishi ya aina ya makanisa ambayo hupatikana katika zama zote na tamaduni.

E. Mojawapo ya vitabu ambavyo vimenisaidia kutafsiri unabii/mambo ya siku za mwisho ni D. Brent Sandy, *Plowshares na Pruning Hooks: Rethinking the Language of Biblical Prophecy and Apocalyptic.* Anatoa jambo zuri sana la kitheolojia juu ya ahadi zote zilizofanywa kwa waumini waaminifu katika sura 2-3 (kurasa 28-32). Inaziorodhesha ahadi kama
1. mti wa uzima
2. taji ya uzima
3. jiwe jeupe
4. mamlaka juu ya mataifa
5. Nyota ya Asubuhi
6. waliovishwa mavazi meupe
7. nguzo katika hekalu la Mungu
8. Jina la Mungu
9. Jina la Yerusalemu
10. kukalia kiti cha enzi cha Mungu

Anasema haya hayana maana ya kutafsiriwa kwa kifasihi au kwa kibinafsi, lakini kama kutimilizwa kwa umoja, kama inavyoonekana katika Ufunuo 21: 3. Nadhani hii ni mbinu ya kanuni za kiufasiri wake kwa aina hii.

## UMOJA WA KIMUUNDO WA NYARAKA SABA

A. Wafasiri wengi wanaona muundo wa u-saba uliopo katika nyaraka nyingi, ingawa sio zote saba zilizomo katika kila kanisa.
1. Maelezo yanayofanana na yanayojirudia ya Yesu "kwa malaika wa kanisa andika..." (kama vile Ufunuo 2: 1,8,12,18; 3: 1,7,14).
2. Maelezo ya Yesu yaliyo chukuliwa kutoka katika Ufunuo 1: 12-20, ambayo ni vyeo na matendo ya YHWH ya Agano la Kale, yanautambulisha kila ujumbe.
3. Maarifa ya Yesu juu ya makanisa, yote ni chanya na hasi, "najua ..." (kama vile Ufunuo 2: 2, 9,13,19; 3: 1,8,15).
4. Yesu anazungumzia makanisa binafsi na fursa zao za kitamaduni, kijiografia na kiroho.
5. Yesu anasema juu ya ughafla wake, ujao karibuni, ama kwa hukumu ya wakati usio rasmi au Kuja kwa Mara ya Pili, (kama vile Ufunuo 1: 1,3, 2: 5,16,25; 3: 3,11).
6. Yesu anaonya kuhusu usikivu na uelewa wa kiroho, (kama vile Ufunuo 2: 7,11,17,29; 3: 6,13,22). Yesu alitumia "Yeye aliye na sikio, asikie" katika Injili (kama vile Mathayo 11:15, 13: 9, 43, Marko 4:24.)
7. Yesu anatoa zawadi kwa wafuasi waaminifu, (kama vile Ufunuo 2: 7,11,17,25-26; 3: 4-5,11-12,21).

Hatua hizi saba si thabiti katika kila waraka. Utaratibu unabadilika na mambo mengine yameachwa nje ya makanisa fulani, lakini kwa ujumla muundo huu mzima unaonyesha mojawapo ya miundo kadhaa ya fasihi ya u-saba-funganifu.

## MIJI AMBAYO NYARAKA ZILIELEKEZWA KWAYO

A. Efeso

1. Ulikuwa ndiyo mji mkubwa zaidi katika jimbo la Kirumi la Asia Ndogo. Haukuwa mji mkuu, ingawa gavana wa Kirumi aliishi huko. Kilikuwa kituo cha kibiashara kwa sababu ya bandari yake ya asili iliyokuwa bora.
2. Ulikuwa mji huru, ambao uliruhusu kuwa na serikali za mitaa na uhuru mkubwa, ikiwa ni pamoja na kutokuwepo ngome ya kijeshi ya askari wa Kirumi.
3. Ni jiji pekee ambalo liliruhusiwa kushikilia michezo ya kawaida kila mwaka ya Asia.
4. Lilikuwa ni eneo la Hekalu kwa Artemi (Diana katika Latini), ambayo ilikuwa ni moja ya maajabu saba ya ulimwengu ya siku yake. Lilikuwa 425 'x 220' na nguzo 127 ambazo zilikuwa 60 'urefu; 86 kati ya hizo walikuwa wamezijaladia kwa dhahabu (angalia Pliny's *Hist. Nat.* 36:95 na kuendelea). Sanamu ya Artemi ilidhaniwa kuwa elekezi ambayo ilifananishwa kwa wingi na mwanamke aliyetiwa chuchu. Hili liliashiria kwamba kulikuwa na makahaba wengi wa kitamaduni wanaoishi katika mji huu (angalia Matendo 19). Lilikuwa ni jiji lenye uhalifu sana, na wa tamaduni-mchanganyo.
5. Paulo alikaa katika mji huu zaidi ya miaka mitatu (angalia Matendo 18:18 na kuendelea; 20:13).
6. Simulizi zinasema kwamba palikuwa maskani ya Yohana baada ya kifo cha Maria huko Palestina.

B. Smirna
1. Ulidhaniwa kuwa uliasisiwa na Amazon (kiongozi mwanamke mwenye nguvu) aitwaye Smirna. Katika siku ya Yohana ulikuwa mji wa takriban watu 200,000.
2. Ulikuwa umekitwa kwenye bahari ya Aegean. Ulikuwa na bandari nzuri ya asili na kwa hiyo, kulikuwa kituo cha kibiashara kilitarajiwa kutumika na Efeso tu katika Asia Ndogo. Iilikuwa jiji lenye utajiri mwingi sana.
3. Liliharibiwa na Walidia yapata 600 K.K., lakini lilijengwa tena na Lysimicus kufuatia mipango ya Alexander Mkuu ambako njia ya hewa ya baharini ilipunga kila mitaa yake.
4. Pia lilikuwa jiji la uhuru kwa sababu limewasaidia askari wa Kirumi waliokimbia baada ya kushindwa na Mithradates.
5. Kilikuwa ni kituo cha ibada ya mungu-mke wa Rumi (195 K.K.) na pia ibada ya Mfalme. Lilikuwa na hekalu la kwanza kwa Mfalme Tiberia (A. 26).
6. Kilikuwa ni kituo cha kidini cha ibada ya Cybele na mwangalizi wa Homer. Kulifanyika hata utamaduni kwamba Homer alizaliwa hapa. Mahekalu yake mengi yalikuwa kwenye vijilima viitwayo Pagos na njia ya dhahabu kati ya Hekalu la Zeus na Cybele.
7. Lilikuwa na idadi kubwa ya wakazi wa kupambana na Wakristo wa Kiyahudi.
8. Ulikuwa ni mji ambapo Polycarp (mwanafunzi wa Yohana Mtume) aliuawa katika 155 B.K.

C. Pergamo
1. Iilikuwa jiji kubwa la utajiri na mji mkuu wa Asia Ndogo (tangu 282 K.K.), ingawa haukujengwa kwenye barabara kuu ya biashara.
2. Iilijivunia maktaba kubwa zaidi katika ulimwengu wa Kirumi nje ya Alexandria, Misri. Iilikuwa na vijitabu vya ngozi zaidi ya 200,000!
3. Karatasi iliyotengenezwa kwa ngozi ilivumbuliwa hapa. Palichakatwa ngozi za wanyama ambazo zilitumika kwa kuandikIa. Zana hizi za kuandikwa zilifanywa kwa sababu Alexandria, Misri, walikataa kuwauzia tete za mafunjo. Hii ilikuwa ni kwa sababu mfalme wao, Eumenes II (197-159 K.K) alijaribu kuajiri Mkutubi wa Alexandria, Aristophanes. Wakati mfalme wa Makedonia, Epiphanes (205-182 K.K.) wa Alexandria alipogundua, alikamatwa msimamizi wa maktaba na kuzuia tete kutoka Pergamo. Kulikuwa na uhasama dhahiri kati ya vituo viwili hivi vya mafunzo. Anthony baadaye alimtuma mkutubi wa maktaba ya Pergamo kwa Alexandria kama zawadi kwa Cleopatra.
4. Palikuwa maskani ya Galen tabibu na kitovu cha sanaa za uponyaji za Asclepios. Pia inasemekana kwamba Asclepios alikuwa "mungu wa Pergamo." Ishara ya mungu huyu ilikuwa ni nyoka.
5. Pia ulikuwa na hekalu ya Rumi na Mfalme Augustus (29 B.K.) na kilikuwa kituo cha utawala (*neokopros*) wa tamaduni za ki-falme. Uaminifu wake kwa Rumi ulijulikana sana.

6. Ulijulikana kwa ibada yake na ulinzi wa miungu ya dini ya Kigiriki. Kulikuwa na Hekalu kubwa kwa mungu wa Kiyunani juu ya vilima iliyouatamia mji mzima. Ulikuwa na umbo kama kiti cha enzi (yaani, enzi ya Shetani).

D. Thiatira
1. Ulikuwa mji mdogo wa kibiashara. Kuna rekodi nyingi za vyama vyake vya ki-biashara vingi na vyema, kila kimoja kikiwa na usimamizi wake pekee. Ulikuwa kwenye barabara kubwa kati ya Pergamo na Sardi ambayo ilielekea Filadefia na Laodikia. Ulikuwa maarufu kwa bidhaa zake za nyuzi-pamba. Lidia (angalia Matendo 16:14), muuzaji wa kitambaa cha rangi ya zambarau, alitoka katika mji huu.
2. Ulipanuliwa na Seleucus Nicateo, ambaye aliwaweka askari wake wa Makedonia hapa.
3. Ulikuwa na mahekalu kadhaa kwa ajili ya uungu wa mitaa.
   a. Tyrimnos (Apollo) - mungu jua
   b. Artemi (Diana) - mungu wa upendo
   c. Sibyl Sambathe – mwanamke wa nyumbani msoma bahati

E. Sardi
1. Ulikuwa ni mji mkuu wa kale, wenye utajiri. Kwa miaka ilikuwa mji mkuu wa Ufalme wa Lidia kwa sababu ya msimamo wake mkubwa wa jeshi, 1500 'kwa umahiri wa mlima. Umetajwa katika kumbukumbu za Kiajemi kwa sababu Koreshi Mkuu aliuteka mji huo. Pia umetajwa katika Obadia 1:20. Ulikuwa umeanguka kiumaarufukwa kiwango kikubwa katika siku ya Yohana.
2. Ulijulikana kwa bidhaa zake za nyuzi-pamba za rangi. Mchakato huo ulianzishwa huko, kwa hiyo walikuwa na uhalali wa umiliki.
3. Kilikuwa ni kituo cha ibada ya Cybele, mungu-mama. Masazo ya hekalu bado yanaonekana kwenye vilima vilivyoinuka juu. Umaarufu wa ibada hii ulijulikana na ulipingwa katika dola yote ya Kirumi.

F. Filadelfia
1. Ulikuwa uko kwenye Kilima juu na ulilindwa kwa maji. Hili liliufanya kuwa na nafasi nzuri ya kutamanika kijeshi. Iilikuwa jiji jipya katika miji saba. Uliasisiwa na Attalus II (159 - 138 K.K.).
2. Ulikuwa uko kwenye njia kuu ya biashara iendayo Sardi na ulikuwa imestawi.
3. Ulikuwa katika eneo la kilimo bora, haswa kwa zabibu. Yeye mungu Bacchus, au Dionysus, alikuwa mmoja wa miungu yake mikuu. Pia ulikuwa ni eneo la tetemeko kali la ardhi na uliharibiwa wakati wa tetemeko kubwa la 17 B.K, ambalo pia liliharibu miji mikubwa mingine kumi ya eneo hilo. Hata hivyo, hofu ya baada ya mshtuko huo uliendelea katika eneo hili na idadi ya watu ilihamia pembezoni mwa mji.
4. Pia kilikuwa kituo cha tamaduni za Mfalme (kama vile Smirna na Pergamo) ambacho kiliweza kuwa chanzo cha mateso mengi ya Makanisa katika mikoa.
5. Kilikuwa ni kituo kikuu cha utamaduni wa Kiyunani kati ya hadhi ya juu na wa kisasa na uhamiaji wake wa ushawishi wa nguvu. Unaonekana kuwa Ulianzishwa kwa lengo hili hasa kwenye mpaka wa Misia, Lidia na Frigia.

G. Laodikia kwenye Mto Luko
1. Ulikuwa mojawapo ya miji mitatu katika bonde la Mto Luko (miji mingine ilikuwa Kolosai na Hierapolis). Makanisa yalianzishwa katika kila moja ya miji mitatu hii, yawezekana na wanafunzi wa Paulo, Epafra (angalia Wakolosai 1:17; 4: 12-13).
2. Ulianzishwa na mtawala wa Seleucid, Antiochus II, ambaye aliiita baadaye kwa heshima ya jina la mkewe, Laodice, katika 250 K.K. Ulikuwa kwenye eneo la kijeshi lililojitetea kama Filadefia.
3. Ulikuwa kwenye njia kuu ya biashara ya mashariki mwa magharibi. Ulijulikana kama kituo cha benki.
4. Ulikuwa uko katika eneo la kilimo lenye rutuba na la uchungaji, hasa lililofaa kwa ajili ya kuwakuza kondoo maalum weusi ambao walikuwa maarufu duniani kote. Wingi wake ulizalisha vazi la nje jeusi linaloitwa "trimeta."
5. Ulikuwa na idadi kubwa ya watu wa Kiyahudi.

6. Kama Pergamo, ulikuwa ni kituo cha ibada ya mungu mponyaji Asclepios. Jiji hilo lilikuwa kitovu na shule ya utabibu ambayo ilikuwa ikijulikana kwa faraja ya kupunguza maumivu ya maskio na macho.

## USOMAJI WA NENO NA FUNGU LA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 2:1**
**[1]Kwa malaika wa kanisa lililoko Efeso andika; Haya ndiyo anenayo yeye azishikaye hizo nyota saba katika mkono wake wa kuume, yeye aendaye katikati ya vile vinara saba vya dhahabu.**

**2:1 "malaika"** Neno la Kiebrania na Kiyunani kwa malaika linaweza kumaanisha mjumbe. Linaweza kumaanisha pia

1. mchungaji (angalia Mal. 2: 7)
2. malaika wa kanisa (angalia Danieli 10)
3. roho ya kipekee au tabia ya makusanyiko moja moja.

Kifungu hiki hiki kinautambulisha kila waraka (angalia Ufunuo 2: 1, 8, 12, 18; 3: 1, 14).

▣ **"Kanisa"** Neno hili la Kigiriki *ekklesia* ni mchanganyiko wa maneno mawili ya Kiyunani, "nje ya" na "kuita." Iilitumika katika maandiko ya kale ya Kiyunani ili kufasiri neno la Kiebrania, *qahal*, au "mkusanyiko wa Israeli." Wakristo wa kwanza walilitumia kujitambulisha kwa sababu

1. walijiona kama watu wa Mungu, kama Israeli
2. walijiona kama kiungu wakiitwa na Mungu kwa namna ya wokovu na huduma

Angalia Mada Maalum katika Ufunuo 1: 4.

▣ **"Yeye azishikaye hizo nyota saba"** Haya ni maelezo ya Yesu yaliyochukuliwa toka katika Ufunuo 1:16. Nyota hizi saba zilizotajwa ni makanisa (angalia 1:20). Neno "shikilia" (KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO) linamaanisha imara, kwapua kwa hakika (kama vile Yohana 10:28). Hakuna na hayupo mtu aliyeweza kuwatenganisha makanisa haya kutoka kwa Yesu (kama vile Warumi 8: 31-39) isipokuwa kukataa kwao wenyewe kutubu na kumfuata Yeye! Kutokuamini tu ndiko kunaweza kuwatenganisha.

▣ **"katika mkono Wake wa kuume"** Hii ni namna ya kumwelezea Mungu kwa lugha ya kibinadamu (imzungumziayo Mungu kwa maneno ya kimwili) mfano wa nguvu na mamlaka (kama vile Ufunuo 1: 16,17, 20; 2: 1; 5: 1,7).
▣ **"aendaye katikati ya"** Mfano huu wa kumwelezea Mungu kwa lugha ya kibinadamu hutumiwa katika Mwanzo 3: 8 kama ishara ya kuwepo kwa Mungu na wanadamu (kama vile Walawi 26:12).

### MADA MAALUMU: MUNGU ANAELEZEWA KWA LUGHA YA KIBINADAMU (SPECIAL TOPIC:GOD DESCRIBED AS A HUMAN (ANTHROPOMORPHIC LANGUAGE)

▣ **"vinara vya taa vya dhahabu"** Hii haina maana ya vinara vya taa vya Hemani, lakini ni ishara nyingine kwa makanisa saba (kama vile Ufunuo 1: 12-13).

▣ **"husema"** Maneno ya mwisho ya Yesu kwa kanisa lake sio Mat. 28: 18-20 au Matendo 1: 7-11, lakini ni Ufunuo 2-3.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 2:2-7**
**[2]Nayajua matendo yako, na taabu yako, na subira yako, na ya kuwa huwezi kuchukuliana na watu wabaya, tena umewajaribu wale wajiitao mitume, nao sio, ukawaona kuwa waongo; [3] tena ulikuwa na subira na kuvumilia kwa ajili ya jina langu, wala hukuchoka. [4]Lakini nina neno juu yako, ya kwamba umeuacha upendo wako wa kwanza. [5]Basi, kumbuka ni wapi ulikoanguka; ukatubu, ukayafanye matendo ya kwanza. Lakini, usipofanya hivyo, naja kwako, nami nitakiondoa kinara chako katika mahali pake, usipotubu. [6] Lakini unalo**

**neno hili, kwamba wayachukia matendo ya Wanikolai, ambayo na mimi nayachukia.** 7**Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa. Yeye ashindaye, nitampa kula matunda ya mti wa uzima, ulio katika bustani ya Mungu.**

**2:2 "Nayajua"** Muundo huu ni KAULI TIMILIFU TENDAJI ELEKEZI ya *oida*, lakini ilitafsiriwa kama ILIYOPO. Yesu anayaona, anayaelewa, na kuyajali makanisa Yake. Kujali kwake kunahusisha yote, uthibitisho na nidhamu (ambayo ni muundo wa upendo wa wazazi). Kifungu hiki hiki kinarudiwa katika nyaraka zote saba (kama vile Ufunuo 2: 2,4,13,19; 3: 1,8,15).
Msingi wa Agano la Kale wa neno hili unamaanisha uhusiano wa karibu, wa kibinafsi (kama vile Mwanzo 4: 1; Yer 1: 5).

**MADA MAALUMU: FAHAMU (TUMIA ZAIDI KUMBUKUMBU LA TORATI KAMA KIELELEZO) (SPECIAL TOPIC: KNOW (USING MOSTLY DEUTERONOMY AS A PARADIGM)**

▣ **"matendo yako na taabu yako"** Hili lilikuwa kanisa lililo changamfu, lakini wamesahau kipaumbele cha ushirika na Kristo (kama vile Ufunuo 2: 4). Mambo mengi mema yaliwapokonya yale yaliyo bora (kama vile Gal 3: 1).

▣ **"subira"** Neno hili lina maana ya uhiyari wa kujishughulisha, usiotetereka, na kwa mshikamano. Hiki ndicho kiini kikuu cha kitabu hiki (kama vile Ufunuo 1: 9, 2: 2,3,19; 3:10; 13:10; 14:12).
Ustahimivu lazima uwe kwa ulinganifu na usalama (kama vile Ufunuo 2: 7,11,17,26; 3: 5,11-12,21). Ukweli zaidi wa kibiblia hutolewa kwa lugha ya kimapenzi, inayoonekana kama ya kuchanganya, jozi. Vyote ni kweli zilizo sawa, lakini pia si kweli pekee. Wokovu ni toba ya awali na imani ikifuatiwa na mfumo wa maisha na toba, imani, utii, huduma, na ushikamanifu! Angalia Mada Maalum hapa chini.

**MADA MAALUMU: USTAHIMILIVU (SPECIAL TOPIC: PERSEVERANCE)**

**NASB "watu waovu"**
**NKJV "wale walio waovu"**
**NRSV "watenda maovu"**
**TEV "watu waovu"**
**NJB "watu wabaya"**

Kwa uhalisia hii ni *kakous (kakos),* ambayo mara nyingi hutumiwa kwa "watu waovu." Jina sawa linaweza *ponēros* linaweza kutumika kwa uovu (JINSIA YA KIUME) au watu waovu na kilele cha Yule muovu (MASCULINE, kama vile Mathayo 5:37, 13:38; Yohana 17:15). Muktadha na matumizi yanathibitisha kwamba maandiko haya lazima yatawarejea "watu waovu" (kama vile Warumi 2: 9; 13: 4) katika kanisa (walimu wa uongo) au labda katika jamii.

*Kakos* limetumiwa mara mbili tu katika Ufunuo, hapa na kaika Ufunuo 16: 2, ambapo hutumiwa kuelezea matokeo ya "vitasa vya ghadhabu ya Mungu" (yaani, maumivu).

▣ **"umewajaribu"** Neno hili la kiyunani *(peirazō*) lilimaanisha kupima kwa mazuri au mbaya makusudi (mengi) (kama vile Ufunuo 2: 2,10; 3:10). Neno linalohusiana *(peirasmos*) lilikuwa na upimaji kwa mtazamo wa uharibifu. Uwiano unapatikana katika 1 Yohana 4: 1 ambako waumini wanapaswa kupima (*dokimazō*) kwa lengo la kuidhinishwa wale wanaodai kuzungumza kwa niaba ya Mungu. Wito kwa waumini kuwachunguza wale wanaotaka kuzungumza kwa niaba ya Mungu wakipatikana katika Agano Jipya (kama vile Kumbu 13: 1-5, 18:22, Mathayo 7: 15-23; 1 Yohana 4: 1-6).

Kuna mvutano katika Agano Jipya unayohusiana na waumini kwa uzingativu wa kila mmoja (kama vile Mathayo 7: 1-5). Hata hivyo, Wakristo wanaitwa ili kumtathmini kila mmoja kwa majukumu ya uongozi (kama vile Mathayo 7: 5,6,15, 1 Wakorintho 5: 1-12, 1 Timotheo 3, 1 Yohana 4: 1-6). Tabia na lengo ndiyo funguo za tathmini sahihi (angalia Gal 6:1, Rum 2: 1-11, 14: 1-23; Yakobo 4: 11-12).

**MADA MAALUMU: NENO LA KIYUNANI LINALOSIMAMA BADALA YA "JARIBU" NA VIDOKEZO VYAKE (SPECIAL TOPIC: GREEK TERMS FOR "TESTING" AND THEIR CONNOTATIONS)**

▣ **"wale wajiitao mitume"** Matumizi haya ya neno "mitume" hayawarejelei Wale Kumi na Wawili, bali kwa matumizi mapana ya neno (kama vile Matendo 14:14, Warumi 16: 7, 1 Wakorintho 15: 7, Wagalatia 1:19; Waefeso 4:11, 1 Wathesalonike 2: 6). Agano Jipya mara nyingi linazungumzia somo la mitume au walimu wa uongo (kama vile Mathayo 7: 15-16; 24:24, Matendo 20:29, 2 Wakorintho 11: 13-15, 1 Yohana 4: 1 na katika nyaraka zote za kichungaji). Kanisa hili liliwaeleza kwa usahihi kuwabaini mitume hawa wa uongo na kuwakataa.

**2:3** Kanisa hili lilikuwa aminifu katikati ya hali ngumu, hata katika mateso. Hawakuwa wamemkataa Kristo au kuchoka katika kutenda mema (kama vile Wagalatia 6: 9, Ebr 12: 3; Yakobo 5:7-8). Angalia angalizo katika Ufunuo 2:7.

**2:4**
**NASB, NKJV "umeuacha upendo wako wa kwanza"**
**NRSV "umeutelekeza upendo uliokuwa nao mara ya kwanza"**
**TEV "hunipendi sasa kama ulivyonipenda hapo mwanzo"**
**NJB "una upendo haba sasa kulinganisha na ule wa zamani"**

Kumekuwa na nadharia kadhaa kuhusu nini hiki kinachomaanishwa.
1. Fasiri za TEV na Charles Williams zililichukulia kwa maana ya upendo kwa Kristo.
2. James Moffatt anadhani linamaanisha kupendana.
3. Hershell Hobbs katika fasiri yake andhani lina maana ya upendo kwa waliopotea.
4. J. B. Phillips katika fasiri yake anayaunganisha yote yaliyo hapo juu.
5. Wengine wanafikiri linahusiana na tatizo la waamini wa kizazi cha pili (kama vile Waamuzi 2: 7-10).
6. Wengine wanaliona kama kanisa lisilopunguza upendo kwa jamii ya kiimani halisi baridi (kama vile 1 Wakorintho 13).

**2:5 "Kumbuka"** Hili ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO yenye maana "daima kuweka akilini." Waumini mara nyingi wanashauriwa kukumbuka hali yao ya awali katika dhambi na nafasi yao mpya katika neema na huruma za Mungu kupitia Kristo.
▣ **"wapi ulikoanguka"** Hii ni KAULI TIMILIFU TENDAJI YENYE KUARIFU. Kuuacha "upendo wao wa kwanza" kumekuwa hali ya kudumu ya kutelekezwa!
▣ **"ukatubu, ukayafanye matendo ya kwanza"** Hizi ndizo KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU mbili. Litazame kanisa kwa ujumla linaitwa kufanya maamuzi ya toba (kama vile 2 Wakorintho 7:14) na kuwa hai katika upendo kwa Kristo, kwa ajili ya kila mmoja, na kwa waliopotea.

Toba ni muhimu kwa uhusiano wa imani na Mungu (kama vile Mathayo 3: 2, 4:17, Marko 1:15, 6:12, Luka 13: 3,5, Matendo 2:38; 3:19; ). Neno la Kiebrania lilimaanisha mabadiliko ya vitendo, wakati kwa Kiyunani lilikuwa na maana ya mabadiliko ya fikra. Toba ni ukubalifu wa kubadili kutoka katika matamanio ya ki-binafsi hadi katika maisha yaliyo habarishwa na kuelekezwa kwa Mungu. Ni wito wa kugeuka kutoka katika kipaumbele na kifungo cha nafsi. Kimsingi ni mtazamo mpya, mtazamo mpya wa ulimwengu, mpango mpya. Toba ni mapenzi ya Mungu kwa kila mwana wa Adamu aliyeanguka, Adamu aliyefanywa kwa sura yake (kama vile Ezek 18: 21,23,32 na 2 Pet 3: 9).

Kifungu cha habari cha Agano Jipya ambacho kwa uzuri sana kinaaksi misamiati tofauti ya Kiyunani kwa maana ya toba ni 2 Kor. 7: 8-12.
1. *lupē*, "sononeko" au "huzuni" Ufunuo 2: 8 (mara mbili), Ufunuo 2: 9 (mara tatu), Ufunuo 2:10 (mara mbili), Ufunuo 2:11.
2. *metamelomai*, ""baada ya kujali," Ufunuo 2: 8 (mara mbili), Ufunuo 2: 9
3. *metanoeō*, "tubu," "baada ya akili," Ufunuo 2: 9, 10

Tofauti iko kati ya toba ya uongo (*metamelomai*, kama vile Yuda, Mathayo 27: 3 na Esau, Ebr. 12: 16-17) na toba ya kweli (*metanoe*, kama vile Petro, Yohana 21: 15-23; 26:75; Marko 14:72; Luka 22:62).
Toba ya kweli imeunganishwa na elimu ya ki-dini

1. Kuhubiri kwa Yesu juu ya masharti ya Agano Jipya (kama vile Mathayo 4:17, Marko 1:15, Luka 13: 3,5)
2. Hotuba za kitume katika Matendo ya Mitume (*kerygma*, kama vile Matendo 3: 16,19; 20:21)
3. Karama ya Mungu mwenye uweza (kama vile Matendo 5:31, 11:18 na 2 Tim 2:25)
4. Kuangamia (kama vile 2 Pet 3: 9)

Toba siyo hiari!

▣ **"au sivyo naja kwako"** Hiki ni kiini cha kawaida katika kitabu hiki; Kristo anakuja hivi karibuni (kama vile Ufunuo 1: 2,3; 2: 5,16; 25; 3: 3,11). Katika Agano la Kale kuja kwa Mungu kunaweza kuleta baraka au hukumu. Katika muktadha huu Kristo alikuja kulitiisha kanisa lake (kama vile 1 Pet 4:17)! Kwa hiyo, ina muda tu, pamoja na msimamo wa elimu ya mambo yajayo.

▣ **"na nitakiondoa kinara chako katika mahali pake"** Kinara cha taa kina taswira ya kanisa lote. Huenda hii ilihusisha kuondolewa kwa uwepo wa Kristo na baraka zake. Kutaniko lote halikuasi, lakini walipotelewa kwa huduma yao yenye ufanisi. Hili pia linatumika kwa makanisa ya Pergamo (kama vile Ufunuo 2:16); Thiatira (kama vile Ufunuo 2: 22-23); Sardi (kama vile Ufunuo 3:3); na Laodikia (kama vile Ufunuo 3:19). Inawezekana kwamba kila moja ya makanisa haya yaliathiriwa na aina ya Wanikolai ya mafundisho ya uongo ambayo yamekuza maelewano na utamaduni wa kipagani.

**2:6 " kwamba wayachukia matendo ya Wanikolai"** Kumekuwa na uzushi mkubwa juu ya Wanikolai hawa kuwa walikuwa nani na waliamini nini. Chanzo pekee cha kibiblia tulicho nacho ni Ufunuo 2: 6, 14-15. Uzushi ulianza mapema katika Kanisa karibu 180 B.K. wakati Irenaeus na Hippolitus walipodhani kwamba hawa walikuwa ni mojawapo ya wafuasi "saba" wa wale waliochaguliwa katika Matendo ya Mitume 6:5 aitwaye Nikolas. Hili kwa ujumla halikunufaisha kabisa. Irenaeus, katika kitabu chake, *Contra-heresies*, 3:11:7, walidhani kwamba walikuwa wafuasi wa mafunuo ya Cyrene na mafundisho ya Gnostic wa karne ya pili. Eusebio, katika kitabu chake *Ecclesiastical History*,3:29:1, alisema kuwa dhehebu hili halikudumu muda mrefu.

Katika Ufunuo 2:14-15, mafundisho ya Balaamu na mafundisho ya Wanikolai ni sawa. Kuna uhusiano unaowezekana wa asili ya neno kati ya majina yao kwa Kiyunani; yakimaanisha "mtawala" na "watu" (sawa na maana ya jina la Nikodemo). Kilicho cha wazi ni kwamba wote wawili walikuwa wakiwatia moyo waumini kushiriki katika ibada za kipagani ambazo zilihusisha shughuli za ngono za ki-ibada. Kwa maana hii, Wanikolai na Balaamu (kama vile Hesabu 25: 1-9; 31: 16-18) wako sambamba na mafundisho ya Yezebeli (kama vile 2:20).

**2:7"Yeye aliye na sikio, na asikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa"** Ushauri huu unarudiwa katika nyaraka zote kwa makanisa saba (kama vile Ufunuo 2:7,11,17,29; 3:6,13,22). Lilikuwa ni neno ambalo lilitoka katika matamko ya Yesu (kama vile Mathayo 11:15; 13: 9,43). Ukweli wa kiroho lazima ujibiwe kwa akili na mkono. Hili ni sawa na neno la kiebrania Shema, "sikia ili ufanye" (kama vile Kumbu 5: 1; 6: 4, 9: 1, 20: 3; 27: 9-10).

▣ **"makanisa"** Angalia Mada Maalumu katika Ufunuo. 1:4.

▣ **"Yeye ashindaye"** Kuna msisitizo unaoendelea wa kitheolojia juu ya kug'ag'ania kwa waamini (kama vile Ufunuo 2:7,11,17,25-26; 3:4-5,11-12,21). Ni ushahidi wa uzoefu wa uongofu wa kweli (kama vile Mathayo 24:13, Wagalatia 6:9)! Jonathan Edwards akasema, "Uhakika wa ushahidi wa uchaguzi ni kwamba mtu aushikilie hadi mwisho." W. T. Conner alisema, "Wokovu wa mwanadamu aliyechaguliwa kwa wokovu unatoka katika umilele ndani ya akili na kusudi la Mungu, lakini ni hali ya juu ya imani, na imani inayohimili na kushinda." Angalia Mada Maalum katika Ufunuo 2: 2.

▣ **"Nitampa kula ya mti wa uzima ambao uko katika Paradiso ya Mungu"** Huu ni mwelekeo wa mti katika bustani ya Edeni (kama vile Mwanzo 2:9). Kama wanadamu walianza kushirikiana na Mungu na wanyama katika bustani, hivyo Biblia inaishia kwa namna hiyo (kama vile Isaya 11: 6-9, Ufunuo 22: 2,14,19).

Neno "paradiso" lilikuwa neno la Kiajemi kwa wasimamizi wa bustani iliyozingirwa, ambayo ilitumiwa katika maandiko ya kale ya kiyunani kutafsiri bustani ya Edeni (kama vile Ezek 28:13; 31:8). Ni mojawapo ya marejeo mengi ya zama za Kimasihi ambazo hupatikana katika nyaraka zote wa makanisa saba.

Neno "paradiso" linatumiwa kwa mitazamo miwili: (1) katika Luka 23: 4 inaweza kurejea sehemu ya haki ya Sheol / Peponi (angalia Mada maalum ya Ufunuo 1:8). Yesu anamwambia mwizi anayegeuka kuwa atakuwa pamoja Naye huko siku hiyo (Yesu hakurudi mbinguni kwa siku 40, kama vile Yohana 20:17) na (2) katika 2 Kor. 12: 3 inahusu uwepo wa Mungu, chumba cha kiti cha enzi cha Mungu cha mbinguni ("mbingu ya tatu").

Kusudi la Mungu kwa wanadamu, lililofanyika kwa mfano wake na kwa mfanano wake (Mwanzo 1:26-27), daima limekuwa maisha ya milele. Kuanguka kwa Mwanzo 3 na hati zote za Biblia ni ahadi ya Mungu kwa ukombozi wa wanadamu na ushirika wa milele pamoja naye. Dunia hii iliyoanguka, pengo hili katika ushirika kamili, haikuwa shauku ya Mungu, bali aibu ya wanadamu. Mungu ataurejesha uumbaji kwa makusudio Yake.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) UFUNUO 2:8-11**
**[8]Na kwa malaika wa kanisa lililoko Smirna andika; Haya ndiyo anenayo yeye aliye wa kwanza na wa mwisho, aliyekuwa amekufa, kisha akawa hai. [9]Naijua dhiki yako na umaskini wako, (lakini u tajiri) najua na matukano ya hao wasemao ya kuwa ni Wayahudi, nao sio, bali ni sinagogi la Shetani. [10]Usiogope mambo yatakayokupata; tazama, huyo Ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani ili mjaribiwe, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi. Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima. [11] Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa. Yeye ashindaye hatapatikana na madhara ya mauti ya pili.**

**2:8 "Wa kwanza na wa mwisho"** Hii ni mojawapo ya majina ya mara kwa mara ya Yesu yaliyopatikana katika Ufunuo 1:17 na 22:13. Mwanzoni ilitajwa kuwa YHWH (kama vile Isaya 41: 4; 44: 6; 48:12). Ni sawa na maneno "Mimi ni Alfa na Omega" (kama vile Ufunuo 1: 8; 21: 6; 27:13) na "mwanzo na mwisho" (kama vile Ufunuo 21: 6; 22: 13). Angalia angalizo kamili katika Ufunuo 1: 8.

◙ **"aliyekuwa amekufa, kisha akawa hai"** Huenda hiki pia kilikuwa kwenye ibada ya asili ya Cybele, mungu-mwanamke. Dini nyingi za kale za rutuba zinajumuisha maoni yao juu ya mzunguko wa kibinadamu wa asili, kifo cha majira ya baridi, na kuzaliwa kwa mara ya pili wakati wa joto. Katika muktadha hili linahusiana ki-theolojia na 1:18; 5: 6, ambapo Yesu ni kondoo aliyeuawa lakini sasa yu hai. Inamsisitiza kwa jumuisho la mkazo (huo mara kwa mara) kifo cha mbadala na ufufuo (kama vile Waebrania 7:27; 9: 12,28; 10:10).

**2:9 "Naijua dhiki yako na umaskini wako"** Haya ni maneno mawili ya Kigiriki yenye nguvu sana. Ni muhimu kwa sababu mji wa Smirna ulifanikiwa sana. Ukweli kwamba kanisa lilikuwa maskini unaonekana kaika kuwa na mateso ya kiuchumi. Ni muhimu kithiolojia kwamba katika kitabu cha Ufunuo waumini wanaonyesha kuteseka "dhiki" kutoka kwa wasioamini na yule mwovu, lakini wasioamini wanakabiliwa na "ghadhabu ya Mungu." Angalia angalizo kamili katika Ufunuo 7:14. Waumini hulindwa daima (hutiwa muhuri, angalia Mada maalum katika Ufunuo 7: 2) kutokana na hukumu ya Mungu.

## MADA MAALUMU: DHIKI (SPECIAL TOPIC: TRIBULATION)

◙ **"(bali u tajiri)"** Waumini hawawezi kuusemea msimamo wao katika Kristo kwa viwango vya kidunia (kama vile Mathayo 6:33).

**NASB, NKJV "makufuru"**
**NRSV, NJB "udanganyifu"**
**TEV "maovu dhidi yako"**

Kimsingi, hili ni neno "kufuru," ambalo lilikuwa na utambulisho wa Agano la Kale wa "kutukana" na mara nyingi hutumiwa kuhusiana na mashambulizi ya maneno juu ya YHWH (kama vile Mambo ya Walawi 24: 13-23). Mara mbili katika Agano la Kale la neno "heri" (*barak*) linatumika kwa maana ya kukufuru (angalia 1 Wafalme 21: 10,13).

Katika muktadha wa wanadini hii wa Kiyahudi wanadai kumjua Mungu ("mbariki Mungu"), lakini hawafanyi hivyo (kama vile Mathayo 7: 21-23).

▣ **"wanasemao ya kuwa ni Wayahudi, nao sio"** Neno sawa linatumiwa katika Ufunuo 3:9; hapo li dhahiri kuwa ni Wayahudi wenye msimamo mkali wanaodai kuwa watu wa Mungu lakini kwa kweli sio (kama vile Yohana 8:44, Warumi 2:28-29, Wagalatia 3:29, 6:16). Kutoka kwa Matendo ya Mitume na Wagalatia tunajua kwamba Wayahudi walisababisha upinzani mkubwa wa kuihubiri injili (kama vile Matendo 13:50, 14: 2, 5, 19; 17: 5).

Ufunuo 2:13 inapendekeza kwamba hili linarejelea ibada za kawaida za mfalme aitwaye Concilia ambaye alidai kwamba Wakristo humwita Kaisaria "Bwana" na kumfukizia uvumba mara moja kwa mwaka.

▣ **"sinagogi la Shetani"** Yohana aliona dunia kwa utofauti kabisa, Mungu dhidi ya Shetani. Shetani (angalia MADA MAALUMU: SHETANI (SPECIAL TOPIC: SATAN) katika Ufunuo 12: 3) hutajwa mara nyingi katika kitabu (kama vile 2: 9,13; 3: 9, 12: 9,10; 20: 2,7). Anawadhulumu waumini na kuwatia nguvu watesaji wao. Mgogoro huu wa pande mbili katika ulimwengu wa kiroho unaonyesha fasihi za mambo ya siku za mwisho. Kuna mtafaruku wa udhibiti wa nyoyo na akili za wana wa Adamu.

**2:10 "Usiogope"** Hili ni KAULI YA KATI au TENDWA (yenye ushahidi) SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ikiwa na KIAMBATA HASI ambayo mara nyingi ilikuwa na maana ya kuacha kitendo kilicho tayari katika mchakato. Makanisa haya yaliogopa. Mateso yalikuwa ndiyo ishara ya wokovu wao na baraka za Mungu (kama vile Mathayo 5: 10-12).

▣ **"shetani yu karibu kuwatupa baadhi yenu gerezani "** Nyuma ya viongozi waovu kumejificha uweza binafsi usioonekana wa uovu (kama vile Waefeso 6: 10-19).

Neno Shetani ni jina la Agano Jipya na maelezo. Kazi yake ya kupewa na Mungu ilikuwa kuendesha namna ya uasi, mbadala kwa ubinadamu wa mvuto wa kujijali na hivyo kuwashtaki wakati walipoingia katika majaribu (kama vile Mwanzo 3, Ayubu 1-2, Zakaria 3). Kuna maendeleo ya uovu katika Agano la Kale. Shetani aliumbwa kama mtumishi na aliendelezwa kuwa adui (angalia Theolojia ya Agano la Kale na A. B. Davidson kurasa 300-306).

Kwa hakika ni wazo la kudhaniwa kwamba taswira ya lugha ya kiwango cha juu ya Isaya 14, ambayo inamrejea moja kwa moja Mfalme wa Babiloni mwenye kiburi, na Ezekieli 28, ambayo inamrejea moja kwa moja Mfalme wa Tiro mwenye majivuno, hatimaye hutambua kiburi cha kiroho na kuanguka kwa Shetani. Lugha ya Ezekieli 28 inachukuliwa kutoka katika maelezo ya bustani ya Edeni. Ni vigumu kukubali maelezo ya mwanadamu, kihistoria, mfalme wa kipagani katika maneno ya ki-malaika kuchukuliwa toka Edeni (kama vile Mwanzo 3). Hata hivyo, Ezekieli anafanya jambo lile lile na Mfalme wa Misri katika sura ya 31. Alielezea kama mti mkubwa katika bustani ya Edeni.

Waumini wote wanatamani taarifa zaidi, hasa juu ya asili ya Mungu, malaika, uovu, nk. Lazima tuwe waangalifu wa kuzigeuza taswira, maelezo ya kinabii katika mbinu ya theolojia. Theolojia ya kisasa inatoka kwenye utenganifu, taswira ya kimaandiko yaliyochanganywa na dhana za kisasa, vyote ki-theolojia na ki-maandishi (Dante na Milton).

Katika Agano Jipya anaitwa shetani (kama vile Ufunuo 12: 9,12; 20: 2,10), ambayo lina muundo wa neno la Kigiriki lenye maana ya "kuneneana vibaya," "kuzushiana," au "kuleta mashtaka dhidi ya. " Hii tena inaonyesha kazi yake ya kumshtaki na kumjaribu. Maneno haya yanafanana katika Ufunuo (kama vile Ufunuo 12: 9; 20: 2). Angalia MADA MAALUMU: UOVU BINAFSI (SPECIAL TOPIC: PERSONAL EVIL) katika Ufunuo 12:9.

▣ **"ili mpate kujaribiwa"** Neno hili linatumiwa katika mitazamo miwili: (1) waumini wanajaribiwa ili kuonyesha imani yao ya kweli na makuzi thabiti (kama vile Ufunuo 2:10, Matendo 14:27, Rum 5: 3-4; 8: 17- 19, Ebr 5: 8, Yakobo 1: 2-4, 1 Pet 4: 12-19) na (2) wasioamini wanaojaribiwa ili kuonyesha uasi wao na hukumu stahiki (kama vile Ufunuo 3:10). Katika Ufunuo majaribio ya Kikristo huitwa "dhiki" (kama vile Mada maalum ya Ufunuo 2: 9), wakati wasioamini wanakabiliwa na "ghadhabu ya Mungu."

Yapo maneno mawili ya Kigiriki yaliyotafsiriwa "tahini," "jaribu," au "pima." Mojawapo likiwa na kionjo cha "kupima kwa mwelekeo wa uharibifu" (*peirasmos, peirasmo*). Maaneno mengine (*dokimos, dokimazo*) yalitumiwa kama kionjo cha "kupima kwa mtazamo wa mwelekeo wa idhinisho." Shetani hujaribu kuharibu; Mungu anajaribu

kuimarisha (kama vile 1 Wathesalonike 2: 4, 1 Pet 1: 7, Mwa 2: 4; 2:22; 2 Mambo ya Walawi 32:31). Angalia Mada Maalum katika Ufunuo 2: 2.

◘ **"siku kumi"** Kumekuwa na uvumi mwingi juu ya maneno "siku kumi":

1. Wengine wanasema kwamba ilikuwa inahusu siku halisi ya kipindi cha mateso katika mji wa Smirna nyakati za Yohana.
2. Wengine wanasema kuwa kwa sababu kumi ni tarakimu ya ukamilifu, kwa kawaida ilikuwa na maana tu ya tarakimu kamilifu ya siku za mateso
3. Wengine wanasema kwamba ilirejelea kipindi kisichoainishwa cha mateso

Habari njema ni kwamba ina kikomo. Mateso yatakoma! Hata hivyo, katika kitabu chenye mambo ya siku za mwisho hakuna aliye na uhakika kama tarakimu zilitumiwa kwa mfano au kikawaida. Ikiwa tarakimu mara nyingi ilitumiwa katika Agano la Kale na kipindi kati ya agao la kale na agano jipya juu ya udukuzi wa matukioa ya siku za mwisho kwa maana ya taswira basi, yawezekana ni mfano. Tarakimu za kawaida zinazotumiwa mara nyingi ni 3, 4, 6, 7, 10, 12 na mazidisho yao (angalia Mada maalum ya Ufunuo 1: 4).

◘ **"uwe mwaminifu hadi kufa"** Hii ni KAULI YA KATI au TENDWA (shahidi) SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ambayo inasisitiza haja ya muumini kuendelea na imani hata kama inamaanisha kifo cha kimwili (kama vile Mathayo 2:13, 12:11, 10:22, 24:13, Luka 12: 4; Gal. 6: 9). Waumini wengine waliuwawa na kuendelea kuuawa. Hii ni fumbo juu ya utawala wa Mungu na uzoefu wetu katika ulimwengu ulioanguka.

◘ **"nami nitakupa taji ya uzima"** Hii ilikuwa taji ya mshindi aitwaye "stefano" (kama vile 1 Wakorintho 9:25). Ilikuwa ni malipo kwa mateso ya waamini wa Kikristo. Tunajifunza kutoka kwa Eusebio 'Historia ya kitabu cha Muhubiri, 4:15, kwamba kulikuwa na wahanga wengi, ikiwa ni pamoja na Askofu Polycarp wa Smirna. Pia kuna taji zingine (zawadi) zilizotajwa katika Agano Jipya (kama vile 2 Tim 4: 8, Yakobo 1:12, 1 Pet 5: 4, Ufunuo 3:11).

Katika maisha yake, Yohana analitumia neno, *zoē*, kuurejea uzima wa milele, maisha ya ufufuo (kama vile Yohana 1: 4, 3: 15,36; 4: 14,36; 5: 24,26,29,39,40; 6:27,33,35,40,47,48,51,53,54,63,68 8:12 10: 10,28 11:25 12: 25,50 14: 6 17: 2 , 3: 20:31, Ufunuo 2: 7,10, 3: 5, 13: 8, 17: 8, 20: 12,15; 21: 6,27; 22: 1,2,14,17,19 ). Uzima wa kweli ni zaidi ya uwepo wa kimwili!

## MADA MAALUMU: VIWANGO VYA THAWABU NA ADHABU (SPECIAL TOPIC: DEGREES OF REWARDS AND PUNISHMENT)

**2:11 "Yeye ashindaye"** Hili pia ni agizo la kawaida la uaminifu (kama vile Ufunuo 2: 7,17,26; 3: 5,12,21; 21: 7). Kwa hakika ni msisitizo juu ya uvumilivu (angalia Mada maalum katika Ufunuo 2: 2).

◘ **"kutokuathiriwa na mauti ya pili"** Huu ni UUNDAJI HASI MARA MBILI ukiwa na KAULI TENDWA TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU ambayo inaonyesha kujali kwa Mungu kwa karibu kwa wale waliouawa (taz. Ufunuo 12:11). "Mauti ya pili" inachorejelewa kuwa Jehanamu (angalia Mada maalum katika Ufunuo 1:18) au kutenganishwa milele na ushirika na Mungu (kama vile Ufunuo 20: 6,14; 21: 8).

◘ **"Yeye aliye na sikio, na asikie"** Hii ni wazo a mara kwa mara kwa tahadhari ya kiroho na utambuzi (kama vile Ufunuo 2:7,11,17,29; 3: 6,13,22; 13: 9).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) UFUNUO: 2:12-17**
**[12]Na kwa malaika wa kanisa lililoko Pergamo andika; Haya ndiyo anenayo yeye aliye na huo upanga mkali, wenye makali kuwili. [13]Napajua ukaapo, ndipo penye kiti cha enzi cha Shetani; nawe walishika sana jina langu, wala hukuikana imani yangu, hata katika siku za Antipa shahidi wangu, mwaminifu wangu, aliyeuawa kati yenu, hapo akaapo Shetani. [14]Lakini ninayo maneno machache juu yako, kwa kuwa unao huko watu washikao mafundisho ya Balaamu, yeye aliyemfundisha Balaki atie ukwazo mbele ya Waisraeli, kwamba wavile vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu, na kuzini. [15]Vivyo hivyo wewe nawe unao watu wayashikao**

**mafundisho ya Wanikolai vile vile. [16] Basi tubu; na usipotubu, naja kwako upesi, nami nitafanya vita juu yao kwa huo upanga wa kinywa changu. [17] Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa. Yeye ashindaye nitampa baadhi ya ile mana iliyofichwa, nami nitampa jiwe jeupe, na juu ya jiwe hilo limeandikwa jina jipya asilolijua mtu ila yeye anayelipokea.**

**2:12"Yeye aliye na upanga mkali,"** Hii ni rejea ile ile kwa Yesu aliyetukuzwa ipatikanayo katika Ufunuo 1:16. Ulikuwa ni mfano wa Agano la Kale kwa YHWH (kama vile Isa 11: 4; 49: 2). Inatumiwa katika Agano Jipya kwa nguvu ya mpenyo wa neno la Mungu (kama vile Ufunuo 2:16, 2 Wathesalonike 2: 8, Waebrania 4:12).

**2:13 "Napajua ukaapo"** Neno "Kaa" katika Agano la Kale linamaanisha" kuishi kwa kudumu sana. "Waumini hawa walikabiliwa na nguvu za serikali za mitaa zenye shinikizo za kipepo.Yesu aliwatambua kwa hali zao ovu.

▣ **"penye kiti cha enzi cha Shetani"** Kumekuwa na tafsiri nyingi iwezekanavyo za maneno haya:

1. Inaweza kuwa rejea ya kiti kikubwa cha enzi cha mungu wa kiyunani kilichokuwa Pergamo.
2. Inaweza kuwa rejea ya mungu wa uponyaji, Asclepios, ambaye alama yake ilikuwa nyoka.
3. Inaonekana kuwa jiji zima lilionekana kama kiti cha enzi kikubwa kwa sababu ya vilima viliyosimama kwa mamia ya futi juu ya jiji lenyewe.
4. Inaweza kuwa rejeo la Concilia, ushirika wa mahala ili kukuza ibada ya mfalme, iliyokuwa yenye nguvu sana katika Pergamo. Kwa sababu ya muktadha wa kihistoria, ama # 1 au # 4 inaonekana kuwa bora.

▣ **"walishika sana jina langu"** Hii ni KAULI TENDAJI YENYE KUARIFU YA WAKATI ULIOPO. Inaonyesha umuhimu wa jina kama wakilishisho la tabia ya mtu. Waumini huamini kwa kuliita jina lake (kama vile Yohana 1:12, 3:18, Warumi 10: 9-13) na kuabudu kwa kuliita jina lake (kama vile Mwanzo 4:26, 12:8;) na kuvumilia kwa kuliiita jina lake (kama vile Yohana 17: 11-12).

**MADA MAALUMU: JINA LA BWANA (SPECIAL TOPIC: THE NAME OF THE LORD)**

▣ **"wa hukuikana imani Yangu"** Hili ni KAULI YA KATI (shahidi) YENYE KUARIFU YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Wakati wa karne hizi za kwanza za Ukristo, na hata leo katika jamii fulani, kulikuwa na jaribu halisi la kuokoa mafanikio ya mtu au maisha kwa kuikana imani katika Kristo wakati wa majaribi ya kimwili au ya ki-mahakama. Kanisa daima limejitahidi kwa jinsi ya kuwashughulikia waasi hawa.

**MADA MAALUMU: IMANI (*PISTIS* [JINA], *PISTEUŌ,* [TENDO], *PISTOS* [KIVUMISHI) (SPECIAL TOPIC: FAITH (*PISTIS* [NOUN], *PISTEUŌ,* [VERB], *PISTOS* [ADJECTIVE]**

▣ **"Antipa, shaidi Wangu"** Hatujui chochote kumhusu mtu huyu. Jina alilopewa ni sawa na lile lililotumika kwa Kristo katika Ufunuo 5: 1. Neno "shahidi" linaweza kumaanisha "mhanga wa mateso" (kama vile 11: 3; 17: 6). Tertullian alisema kwamba Antipa alikaangwa ndani ya bwawa la shaba, lakini hii ilikuwa ni jadi tu wakati uliopita.

**2:14 "lakini ninayo maneno machache juu yako"** Yesu alikuwa na taarifa hasi kwa makanisa sita kati ya saba. Kuishi kwa haki katika maeneo mengine hakusamehi dhambi kwa wengine!

▣ **" kwa unao huko watu washikao mafundisho ya Balaamu"** Balaamu alikuwa nabii wa Mungu (kama vile Hesabu 24: 2) ambaye alikuwa amekumbwa katika kusaidia kuwapinga watu wa Israeli (kama vile Hesabu 22-25 na 31:16). Analaumika katika Agano la Kale na Agano Jipya (kama vile Hesabu 31:16, 2 Pet 2:15; Yuda 11).

Inawezekana kwamba jina Balaamu kwa Kiebrania linamaanisha "mkombozi wa watu" na jina la Nikolau labda lingemaanisha kitu katika Kigiriki (Nikodemo wa Yohana 3 pia ina maana sawa). Hii ingeyatambua makundi haya mawili kama ya mazoea yao ya uasherati (kama vile Yezebeli, 2:20).

▣ **"yeye aliyemfundisha Balaki atoe ukwazo mbele ya Waisraeli"** Ushauri wa Balaamu kwa Balaki, Mfalme wa Moabu, ulikuwa ni kuwahusisha wana wa Israeli katika ibada ya uzinzi ya Baali (kama vile Hesabu 25: 1-3). Kulikuwa na mwendelezo wa jaribu la kitamaduni kwa namna ya ibada za ngono za wapagani wa karne ya kwanza.

**MADA MAALUMU: ISRAELI (JINA) (SPECIAL TOPIC: ISRAEL (THE NAME))**

▣ **"wavile vitu vilivyotolewa kwa sanamu na kufanya *vitendo vya* uasherati"** Dhambi hizi mbili zilijumuisha ibada za kipagani (taz. Hesabu 25: 1-3 na 31:16). sio tu kulikuwa na vyakula vya kipagani ambako chakula kilikuwa kikitolewa sadaka kwa sanamu (kama vile 1 Wakorintho 8: 1-13), lakini mara nyingi uasherati kuwa mtindo wa maisha na tendo la ibada tarajiwa katika makusanyiko haya ya kipagani. Shughuli ya ngono ya kibinadamu ilikuwa ni njia inayotakiwa kuhakikisha afya na uzazi wa mifugo, mazao, na jamii.

**2:15 "wewe nawe unao watu ambao kwa namna hiyo hushikilia mafundisho ya Wanikolai"** Kwa sababu ya kufanana kwa mafundisho ya Balaamu, Wanikolai (taz. 2: 6), na Yezebeli (taz. 2:20), yote matatu haya yanataja mazoea ya kipagani, ibada za sanamu. Waumini hawapaswi kurudia, au kuchukuliana na tamaduni za kipagani.

**2:16 "Hivyo basi, tubu" Angalia angalizo katika Ufunuo. 2:5.**

▣ **"la sivyo naja kwenu upesi, nami nitafanya vita nao kwa upanga wa kinywa Changu"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Kuna msisitizo unaoendelea juu ya toba (kama vile Ufunuo 2: 5,16,22; 3:3,19). Ujio unaweza kurejea hukumu ya muda dhidi ya kanisa au Kuja Mara ya Pili kwa Kristo kuhuikumu dunia. Ni muhimu kwamba kanisa kwa ujumla limeitwa kutubu (kama vile Ufunuo 3:20, 2 Wakorintho 7:14) kwa sababu ya dhambi za wengine; kama hawakuwa wao, basi, matokeo yalikuwa ya nidhamu ya ki-ushirika! Tazama Mada Maalum: Ujio wa mapema katika Ufunuo 1:2.

**2:17 "kwake yeye nitampa baadhi ya ile mana iliyofichwa"** Mana ilikuwa ni utoaji wa Mungu wa kipekee kwa wana wa Israeli wakati wa kutangatanga jangwani (kama vile Kut. 16: 14-15,31, Zaburi 78: 17-33, hasa Ufunuo 2:24). Kumekuwa na nadharia kadhaa zilizopendekezwa kutafsiri maneno haya magumu yenye maana zilizojificha:

1. Inaweza kurejelea Sanduku la Agano lililotolewa katika kufichwa na Yeremia kutoka Mlima Nebo (kama vile II Maccabees 2: 4-8) kwa sababu lilikuwa na chombo cha mana (kama vile Kut. 16: 32-34, Waebrania 9: 4).
2. Inaweza kurejelea chakula cha zama mpya za haki (kama vile II Baruch 29: 8).

Rejea halisi haijulikani lakini ilikuwa dhahiri kuwa na maana ya wakati mpya wa Roho ulioanzishwa na Kristo. Wengine walisisitiza kuwa kwa sababu ya Yohana 6:31-35, mana iliyofichwa inajulikana kwa Kristo mwenyewe. Huu ni mfano mzuri wa ugumu katika kutafsiri maelezo maalum ya kitabu hiki ambacho msikilizaji wa kisasa alielewa, lakini kumbukumbu halisi zimepotezwa.

▣ **"nami nitampa jiwe jeupe"** Jiwe hili, pia liliitwa *Tessera*, lilikuwa na matumizi mengi katika Near East ya kale.

1. Ingelitumika kama tiketi ya karamu maalum
2. Ingelitumika kupiga kura kwa kuhukumiwa kimahakama
3. Ingelitumika kama ishara ya ushindi kwa mwanariadha
4. Ingelitumika kuonyesha uhuru wa mtumwa.

Katika muktadha huu, # 1 unaonekana kuwa bora zaidi, ukirejelea karamu ya Kimasihi (mada inayojitokeza sana katika fasihi ya Kiyahudi ya matukio ya siku ya mwisho).

▣ **"na jina jipya lililoandikwa juu ya jiwe ambalo hakuna mtu alijuaye bali yeye anayelipokea"** Jina hili jipya linaonekana kuwa ishara ya zama mpya au jina la Masihi (kama vile Isaya 56: 5, 62: 2, 65:15; kama vile MADA MAALUMU: MASIHI (SPECIAL TOPIC: MESSIAH) katika Ufunuo 1: 1). Jina hili jipya linalotajwa mara nyingi katika kitabu cha Ufunuo (kama vile Ufunuo 3:12, 14: 1, 19: 12,13,16; 22: 4).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) UFUNUO: 2:18-29**
**[18]Na kwa malaika wa kanisa lililoko Thiatira andika; Haya ndiyo anenayo Mwana wa Mungu, yeye aliye na macho yake kama mwali wa moto, na miguu yake mfano wa shaba iliyosuguliwa sana. [19] Nayajua matendo yako na upendo na imani na huduma na subira yako; tena kwamba matendo yako ya mwisho yamezidi yale ya kwanza. [20] Lakini nina neno juu yako, ya kwamba wamridhia yule mwanamke Yezebeli, yeye ajiitaye nabii na kuwafundisha watumishi wangu na kuwapoteza, ili wazini na kula vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu. [21]Nami nimempa muda ili atubu, wala hataki kuutubia uzinzi wake. [22] Tazama, nitamtupa juu ya kitanda, na hao wazinio pamoja naye, wapate dhiki kubwa wasipotubia matendo yake; [23]nami nitawaua watoto wake kwa mauti. Na makanisa yote watajua ya kuwa mimi ndiye achunguzaye viuno na mioyo. Nami nitampa kila mmoja wenu kwa kadiri ya matendo yake. [24]Lakini nawaambia ninyi wengine mlioko Thiatira, wo wote wasio na mafundisho hayo, wasiozijua fumbo za Shetani, kama vile wasemavyo, Sitaweka juu yenu mzigo mwingine. [25]Ila mlicho nacho kishikeni sana, hata nitakapokuja. [26] Na yeye ashindaye, na kuyatunza matendo yangu hata mwisho, nitampa mamlaka juu ya mataifa, [27]naye atawachunga kwa fimbo ya chuma, kama vyombo vya mfinyanzi vipondwavyo, kama mimi nami nilivyopokea kwa Baba yangu. [28]Nami nitampa ile nyota ya asubuhi. [29] Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa.**

**2:18 "Mwana wa Mungu"** Ilikuwa ni kawaida sana kumtaja Yesu kama "Mwana." Jina la mara kwa mara linalotumia kielelezo hiki ni "Mwana wa Adamu," ambayo ilikuwa jina la pekee la Yesu aliyechaguliwa. Neno jingine ni "Mwana wa Mungu" ambalo lilikuwa jina la mara kwa mara la Yesu katika maandiko ya Yohana (kama vile Yohana 1: 34,49; 5:25, 9:35, 10:36, 11: 4,27; 19: 7 , 20:31, 1 Yohana 3: 8; 4:15; 5: 5,10,12,13,20). Matumizi ya tatu ya "mwana" yanapatikana katika kitabu cha Waebrania (kama vile Ebr 1: 2, 3: 6; 5: 8; 7:28) ambako Yesu anafananishwa na mtumishi (yaani Musa, manabii) . Yeye ni mwana familia kamili pamoja na Baba.

Hii siyo mojawapo ya misemo elekevu kutoka sura ya 1. Neno hili, kama

"mzaliwa- bikira," lilitumiwa kidogo na waandishi wa Agano la Kale yawezekana kwa sababu ya kutokuelewa kwa wasikilizaji wa kipagani, ambao mara, wataelezea maneno haya kwa matumizi yao katika miungu ya kipagani ya dini za Kigiriki. Miungu ya kale ya Kiyunani na miungu wa kike mara nyingi walikuwa wachangamfu wa kufanya ngono na wanadamu, wakizalisha uzao maalum.

## MADA MAALUMU: MWANA WA MUNGU (SPECIAL TOPIC: THE SON OF GOD)

▣ **"yeye aliye na macho kama moto uwakao, na miguu Yake ni kama shaba iliyochomwa"** Hili lilikuwa jina jingine la Yesu lililochukuliwa kutoka katika Ufunuo 1:14,15. Ni kielelezo cha Dan. 10:6 inayoonyesha asili ya Yesu ya mbinguni. Inawezekana kwamba ilitumiwa kimahusiano na Thiatira kwa sababu mji huu ulijulikana kwa shabaha yake.

**2:19** Aya hii ni ya Yesu kuitambua huduma ya waumini huko Thiatira. Walikuwa wakichangamkia kuifanya kazi katika ufalme na kupata zaidi sana kazi kutenda. Hili linathibitisha, hata hivyo, hakuwapo udhuru wa uzushi wa Ufunuo 2:20.

**2:20 "Lakini nina jambo hili dhidi yako, kwamba unachukuliana na mwanamke Yezebeli, mwenyewe kujiita nabii"** Hiki ni kidokezo juu ya Yezebeli wa 1 Wafalme 16: 31-33; 2 Wafalme 9: 21-22. Kwenye machapisho ya Biblia ya Kiyunani la Alexandrinus (MSS A) anaongeza neno"yako" kabla ya Yezebeli, ambayo ina maana kwamba yawezekana alikuwa mke wa mchungaji wa kanisa hili au kiongozi wa kanisa mwenye nguvu. Lakini huu ni uvumi. Mafundisho yake (kama vile Ufunuo 2:20c) yalikuwa sawa na Wabalaamu katika Ufunuo 2:14b na Wanikolai katika Ufunuo 2:15.

Yezebeli hakukataliwa kwa sababu alikuwa nabii mwanamke. Kuna mifano mingi ya ki-Biblia ya viongozi wanawake wacha Mungu.

1. Miriamu, Kut. 15:20
2. Debora, Waamuzi 4: 4
3. Hulda, 2 Wafalme 22:14

4. Anna, Luka 2:36
5. Binti za Filipo, Matendo ya Mitume 21: 9
6. Phibi, Warumi 16: 1

## MADA MAALUMU: WANAWAKE KATIKA BIBLIA (SPECIAL TOPIC: WOMEN IN THE BIBLE)

**2:21** Rehema ya Mungu na subira yake pamoja na haki yake ni dhahiri katika Ufunuo 2: 21-23 (kama vile Warumi 2: 5).
**2:22 "nitamtupa juu ya kitanda cha ugonjwa"** Hii ni kejeli kuhusiana na kitanda chake cha uzinzi (mafundisho kuhusu uasherati).

▣ **"dhiki kuu"**angalia MADA MAALUMU:DHIKI (SPECIAL TOPIC:TRIBULATION) katika Ufunuo. 2:9 na wakati mmoja mkuu wa mwisho katika Ufunuo. 7:14.
▣ **"isipokuwa wakitubia matendo yake"** Hii ni KAULI SHURUTISHI DARAJA LA TATU, ambayo inaelezea hatua tendaji ya baadaye lakini kwa kipengele cha tahadhali.

**2:23 "nitawauwa watoto wake"** Hili haimaanishi watoto wa kweli, bali kwa wafuasi wake (kama vile Ufunuo 2:22; 2 Yohana 1: 1).
▣ **"nayo makanisa yote yatajuwa"** Hii inaonyesha kwamba nyaraka saba zilipaswa kusomwa na ukweli kutumiwa na makanisa yote, wakati huo na sasa. Kwa "kanisa" tazama Mada maalum katika Ufunuo 1: 4.

▣ **"mimi ndiye achunguzaye viuno na mioyo"** Biblia inasema kwamba Mungu anajua nia na mawazo ya wanadamu wote (kama vile Zab 7: 9, 26: 2, 39: 1, Mithali 24:12, Yer 11:20, 17:10, Luka 16:15 Matendo 1:24, Heb 4: 12-13; 8:27).

## MADA MAALUMU: MOYO (SPECIAL TOPIC: THE HEART)

▣ **"nami nitampa kila mmoja wenu kwa kadri ya matendo yeke"** Ukweli huu wa kiroho unawasilishwa kwa wazi katika Wagalatia 6: 7. Tunavuna kile tunachopanda. Kanuni hii haina maana ya wokovu kwa jitihada za kibinadamu (kama vile Waefeso 2:8-9), bali kwamba wale ambao wamekutana na Mungu katika Kristo wataishi maisha ya kiungu, ya upendo, na kuhudumia maisha ya watu (kama vile 3:12, Mathayo 25: 1-46; Waefeso 2:10).

Hii ni kanuni ya kiroho. Mungu ni mwenye maadili-adilifu na kadhalika uumbaji Wake. Wanadamu wanavunjika kinyume cha viwango vya Mungu. Tunavuna kile tulichopanda. Hiyo ni kweli kwa waumini (lakini haiathiri wokovu) na wasioamini (kama vile Ayubu 34:11; Zab 28: 4, 62:12, Mith 24:12, Matendo ya Mitume 12:14, Yer 17:10; 32:19, Mathayo 16:27, 25: 31-46, Rum 2: 6, 14:12, 1 Wakorintho 3: 8, 2 Wakorintho 5:10, Gal 6: 7-10; 4:14, 1 Pet 1:17, Ufunuo 2:23, 20:12, 22:12).

**2:24 "mambo ya kina ya Shetani"** Kuna nadharia kadhaa zinazohusiana na neno hili
1. kwa maneno-yenye mshiko ya Yezebeli na wafuasi wake
2. Mkazo wa walimu wa mafunuo ya uwongo juu ya maarifa
3. kwa ibada za kuanzishwa kwa dini za siri za Dola ya Kirumi
4. kwa namna ya kupinga, "vitu vya kina vya Mungu" (kama vile Warumi 11:33, 1 Wakorintho 2:10, Waefeso 3:18)
5.

▣ **"Sitaweka juu yenu mzigo mwingine"** Huu ni uthibitisho wa waumini wa kweli katika mji wa Thiatira. Walikuwa na imani yenye nguvu, yenye ukali (kama vile Ufunuo 2:19).

**2:25 "ila mlicho nacho kishikeni sana, hata nitakapokuja"** Wafuasi wa Kristo lazima waendelee (kama vile Ufunuo 2:20) wakati wa mateso, ukatili na kutojali. Hii ni amri (KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA

USIOTIMILIFU). Yesu yu njiani Kwake; Anakuja hivi karibuni (kama vile Ufunuo 2:16; 22: 7,20). Hili ni tumaini na faraja ya kila kizazi cha Wakristo.

**2:26-27** Hii ni dokezo la Zaburi 2: 8-9, yawezekana na Isa. 30:14 na Yer 19:11 iliyoongezwa ndani yake. Yesu ni mfalme wa Kimasihi. Ufalme wake unakuja katika kwa nguvu na utimilifu duniani kote. Itapaswa kutukia huku wafuasi Wake kumwona!

**2:26 "mataifa"** Matumizi ya neno hili kutoka katika Agano Jipya inaonyesha kwamba inawawakilisha wale walio nje ya agano la YHWH (isipokuwa 7: 9). Inakuwa njia ya kurejelewa watu wasio na hatia, watu waovu (taz. Ufunuo 2:26, 5: 9, 10:11, 11: 2,9,18; 12: 5; 13: 7, 14: 6,8; 16:19, 17:15, 18: 3,23; 19:15; 20: 8).

**2:27 "pia nimepokea mamlaka kutoka kwa Baba yangu"** Yesu tayari amepewa mamlaka yote (kama vile Zaburi ya 2, Mathayo 28:18, Wafilipi 2: 9-11). Ufalme wa Yesu ulikuwapo, bali haujatimilizwa.
Nukuu ya Agano la Kale katika mstari wa 27 inatoka katika Zab. 2: 8 ambayo mwanzoni ilikuwa inajulikana kwake Masihi (kama vile Ufunuo 12: 5; 19:15), lakini hapa hutumiwa kwa waumini ambao wameweka tumaini lao katika Yesu Kristo. Wanatawala pamoja Naye. Angalia Mada Maalum katika Ufunuo 5:

**2:28 "nami nitampa ile nyota ya asubuhi"** Kumekuwa na tafsiri nyingi iwezekanavyo za maneno haya:
1. Ilielezea mfano wa Kristo (kama vile Ufunuo 22:16)
2. Ilielezea maarifa ya karibu na ushirika pamoja na Kristo (kama vile 2 Pet 1:19)
3. Ilielezea ufufuo (kama vile Dan 12: 3)
4. Ilimwelezea Masihi wa kijeshi aliyetajwa katika Hesabu. 24:17
5. Ilielezea furaha ya watu wa Mungu (kama vile Ayubu 38: 7)
6. Ilielezea maneno yaliyotumiwa na Shetani katika Isa. 14:12, bali sasa kwa Kristo

**2:29** Angalia angalizo katika Ufunuo. 2:7.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 3:1-6**
**[1]Na kwa malaika wa kanisa lililoko Sardi andika; Haya ndiyo anenayo yeye aliye na hizo Roho saba za Mungu, na zile nyota saba. Nayajua matendo yako, ya kuwa una jina la kuwa hai, nawe umekufa. [2]Uwe mwenye kukesha, ukayaimarishe mambo yaliyosalia, yanayotaka kufa. Maana sikuona matendo yako kuwa yametimilika mbele za Mungu wangu. [3]Basi kumbuka jinsi ulivyopokea, na jinsi ulivyosikia; yashike hayo na kutubu. Walakini usipokesha, nitakuja kama mwivi, wala hutaijua saa nitakayokuja kwako. [4]Lakini unayo majina machache katika Sardi, watu wasioyatia mavazi yao uchafu. Nao watakwenda pamoja nami hali wamevaa mavazi meupe, kwa kuwa wamestahili. [5]Yeye ashindaye atavikwa hivyo mavazi meupe, wala sitalifuta kamwe jina lake katika kitabu cha uzima, nami nitalikiri jina lake mbele za Baba yangu, na mbele ya malaika zake. [6]Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa.**

**3:1 "kanisa"** Angalia Mada Maalumu katika Ufunuo 1:4.

▣ **" Yeye aliye na hizo roho saba za Mungu na zile nyota saba"** Maneno haya ni kidokezo kingine kwake Kristo aliyetukuzwa (kama vile Ufunuo 1: 4,16,20). Zile nyota saba huyarejea yale makanisa na viongozi wake katika Ufunuo 1:20; zile roho saba zinaweza kuwa mfano unaohusiana kwa sababu katika Ufunuo 4: 5 zinahusiana na vile vinara vya taa saba, ambavyo pia vinasemewa katika Ufunuo 1:20 kama vile kuyarejea makanisa. Hizi roho saba za Mungu zinasemwa pia katika Ufunuo 5: 6 kama sehemu ya maelezo ya mwana-kondoo. Tazama Mada Maalum: Roho Saba katika Ufunuo 1: 4.

▣ **"Nayajua matendo yako"** Yesu alikuwa akijua nguvu na udhaifu wa makanisa yake (kama vile Ufunuo 2: 2,19; 3: 1,8,15).

**NASB, NKJV "kwamba unalo jina kwamba u hai"**
**NRSV "kwamba una jina la kuwa hai"**

**TEV "kwamba una sifa ya kuwa hai"**
**NJB "jinsi unavyosemekana kuwa hai"**

Huu ulikuwa ni ufunuo wenye uharibifu. Wao walidhani walikuwa sawa na Mungu, wenye kumpendeza kiroho (kama vile Isaya 29:13, Warumi 2: 19-20, Wakolosai 2: 16-23, 2 Tim 3: 5), lakini hawakuwa!

**3:2**
**NASB, NRSV,**
**TEV, NJB"Amka"**
**NKJV"Uwe macho"**

Hii ni NJEO YA KATI YA WAKATI ULIOPO (shahidi) SHURUTISHI( ikiwa na KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO), kwa kweli "daima uwe mwangalifu." Ni ya kwanza kati ya KAULI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO zile tano zilizopatikana kwenye mstari wa 2 na 3. Yesu analiamuru kanisa lake kuendelea kuwa macho!

**NASB, NKJV "yaimarishe mambo yaliyobaki"**
**NRSV "imarisha kile kinachobakia"**
**TEV "imarisha kile ulicho nacho"**
**NJB "weka ufumbuzi fulani katika nguvu ndogo iliyosalia"**

Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu. Walipaswa kuchukuwa hatua sasa na kuendelea kutenda ili kuhifadhi kile kilichobaki cha imani yao inayokufa.

▣ **" kwa maana siyaoni matendo yako kuwa kamili mbele ya Mungu Wangu"** KITENZI cha kwanza ni KAULI TMILIFU TENDAJI YENYE KUARIFU. Yawezekana kuwa waliyaangalia kiroho (kama vile Isaya 29:13), lakini zaidi walikuwa kama watu wa kidini waliotajwa katika Mathayo. 7: 21-23 na Wakolosai 2: 16-23.

Neno "kukamilika" ni KAULI TIMILIFU TENDWA YENYE HALI YA KUENDELEA yenye maana "kukomaa, kamilifu, kilichoandaliwa kwa ajili ya kazi iliyopangwa." Hawakuruhusu Mungu kukamilisha kile imani ilichokianza (kama vile Wafilipi 1: 6).

**3:3 "kikumbuke kile ulichokipokea na kusikia"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ikifuatiwa na KAULI TIMILIFU TENDAJI YENYE KUARIFU na KAULI TENDAJI YENYE KUARIFU YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Hii inahusiana na injili waliyoisikia na kuendelea kuipokea. Ukristo sio uamuzi tu, bali uhusiano wa mtindo wa maisha. Inahusisha kuuamini ujumbe na mtu kuupokea. Inaleta matokeo ya mabadiliko ya maisha na kugeukia maisha ya toba (KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU, Ufunuo 3:3b) na utii (KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO, Ufunuo 3:3b).

▣ **"kaa *nayo*"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ambayo ni agizo endelevu.

▣ **"tubu" Hii** ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU yenye kumaanisha toba timilifu. Tazama andiko katika Ufunuo 2:5.

▣ **"Kwa hiyo usipo amka**" Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU ilivyo 2:22. Uwezo ni hatua, uwiano wa jibu lao kwa agizo la Yesu, lakini bila kuthibitishwa.

▣ **"nitakuja kama mwivi"** Hii mara nyingi hutumiwa kwa kuja kwa pili (kama vile Mathayo 24: 43-44; Luka 12: 39-40, 1 Thes 5: 2,4, 2 Pet 3:10, Ufunuo 16:15). Hata hivyo, katika muktadha huu inaonekana kutajwa hukumu ya wakati wa kanisa hili.

**3:4 "watu wachache huko Sardia ambao hawajayatia uchafu (udongo) mavazi yao "** Kuvaa na kuyavua mavazi kulitumika kama mfano wa maisha ya Kikristo (kama vile Waefeso 4: 22,24,25,31; Kol 3: 8,10,12,14 Waebrania 12: 1; Yakobo 1:21, 1 Pet 2: 1). Waumini wengine hawakuwa wamekubaliana na utamaduni wa kipagani.

▣ **"watakwenda pamoja Nami hali wamevaa mavazi meupe"** Nguo nyeupe hutumiwa kama ishara ya usafi au ushindi katika Ufunuo 3: 4,5,18; 6:11; 7: 9, 13-14; 19:14. Neno "kutembea" mara nyingi hutumiwa kama mfano wa maisha ya Kikristo (kama vile Ufunuo 3: 5, 21:24, 1 Yohana 1: 6,7; 2: 6,11; 3 Yohana 3-4).

**3:5 "Yeye ashindaye"** Mambo manne atapewa yeye anayeshinda.

1. Watakwenda pamoja na Masihi, Ufunuo 3: 4
2. Watakuwa wamevishwa weupe
3. Majina yao kamwe hayataondolewa katika kitabu cha uzima
4. Masihi atawatambua kama wa kwake mwenyewe mbele ya Baba na malaika

Angalia Mada Maalumu juu ya ustahimilivu katika ufunuo 2:2.

▣ **"Sitalifuta kamwe jina lake katika kitabu cha uzima"** Hii ni KAULI HASI MARA MBILI yenye nguvu. Raia walipokufa, majina yao yangepaswa kufutwa kutoka kwenye kumbukumbu ya jiji lao lakini Mungu hatawaondoa waumini kutoka kwenye kumbukumbu zake. Ki-sitiari Kifungu hiki "kitabu cha uzima" kinapatikana pia katika Ufunuo 20: 12-15, ambapo vitabu viwili vinatajwa:

Maneno haya ya kitaswira 'kitabu cha uzima' pia hupatikana katika Ufunuo 20: 12-15, ambapo vitabu viwili vinasemwa:

1. kitabu cha uzima kimetengenezwa kwa majina ya watu wa Mungu (kama vile Kut. 32: 32-33, Zaburi 69:28, Isa 4: 3, Dani 12: 1, Luka 10:20; Wafilipi 4: 3, Waebrania 12:23, Ufunuo 13: 8; 17: 8; 20: 12,15; 21:27)
2. Kitabu cha matendo au kumbukumbu ambazo zinatunza matendo ya waovu na waadilifu (kama vile Zaburi 56: 8, 139: 16, Isaya 65: 6; Mal 3:16)

Kwa ajili ya "kitabu" Angalia angalizo katika Ufunuo 5:1.

▣ **" name nitalikiri jina lake mbele ya Baba Yangu na mbele ya malaika Zake"** Kama waumini wanavyomkiri Kristo ('kuliitia jina lake,' Rum 10: 9-13), pia anawakiri mbele ya Baba (kama vile Mathayo 10:32; Luka 12: 8).

"kiri" ni neno la Kiyunani *exomulogeō*. Lililokuwa limetumika katika mitazamo mitatu:

1. Kukiri dhambi kwa Mungu adharani na katika uwepo wa wengine ( Mathayo 3: 6, Marko 1: 5, Matendo 19:18; Yakobo 5: 16)
2. Kukiri imani hadharani katika Kristo (kama vile Filipi 2: 1 na labda Rum 14:11)
3. Kumtukuza Mungu hadharani katika umma (kama vile Mathayo 11:25; Luka 10:21, Rum 14:11 {Isa 45:23}, 15: 9 [Zab 18:49])

Neno la Kiyunani linalohusiana na *homologeō* lilikuwa linatumika kwa namna sawa:

1. Kukiri dhambi (kama vile 1 Yohana 1: 9)
2. Kukiri imani katika Kristo (kama vile Mathayo 10:32, Luka 10:32; Yohana 9:22 [vibaya, Yohana 1:20; 12:42])

## MADA MAALUMU: UKIRI (SPECIAL TOPIC: CONFESSION)

**3:6** Angalia angalizo katika Ufunuo. 2:7.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 3:7-13**
**7 Na kwa malaika wa kanisa lililoko Filadelfia andika; Haya ndiyo anenayo yeye aliye mtakatifu, aliye wa kweli, aliye na ufunguo wa Daudi, yeye mwenye kufungua wala hapana afungaye, naye afunga wala hapana afunguaye. 8 Nayajua matendo yako. Tazama, nimekupa mlango uliofunguliwa mbele yako, ambao hapana awezaye kuufunga, kwa kuwa unazo nguvu kidogo, nawe umelitunza neno langu, wala hukulikana jina langu. 9 Tazama, nakupa walio wa sinagogi la Shetani, wasemao kwamba ni Wayahudi, nao sio, bali wasema uongo. Tazama, nitawafanya waje kusujudu mbele ya miguu yako, na kujua ya kuwa nimekupenda. 10 Kwa**

**kuwa umelishika neno la subira yangu, mimi nami nitakulinda, utoke katika saa ya kuharibiwa iliyo tayari kuujilia ulimwengu wote, kuwajaribu wakaao juu ya nchi. 11Naja upesi. Shika sana ulicho nacho, asije mtu akaitwaa taji yako. [12] Yeye ashindaye, nitamfanya kuwa nguzo katika hekalu la Mungu wangu, wala hatatoka humo tena kabisa, nami nitaandika juu yake jina la Mungu wangu, na jina la mji wa Mungu wangu, huo Yerusalemu mpya, ushukao kutoka mbinguni kwa Mungu wangu, na jina langu mwenyewe, lile jipya. [13] Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa.**

**3:7 "Yeye aliye mtakatifu, aliye wa kweli"** Mstari wa 7 ni mfululizo wa vifungu vinne vinavyomwelezea Yesu kwa majina ya YHWH. 'Mtakatifu' lilitumika mara 30 katika Isaya kumwelezea YHWH. Yohana mara nyingi alilifanyia mbadala hili neno 'haki' (kama vile Ufunuo 15: 3, 16: 7, 19: 2). 'Kweli' mara nyingi lilitumika kama YHWH (kama vile Isaya 65:16; Yer 10:10, 1 Yohana 5:20, Ufunuo 15: 3, 16: 7, 19: 2). Mawili ya mwanzo, 'takatifu' na 'kweli,' yanatumiwa tena na Mungu katika Ufunuo 6:10. Neno 'kweli' katika Kigiriki lilimaanisha 'kweli kama juu ya uongo,' lakini kwa Kiebrania lilimaanisha 'mwaminifu au mwenye kutumainika.' Kwa kweli kwa namna zote Yesu ndivyo alivyo (kama vile Ufunuo 3:14, 19:11, 21: 5; 22: 6).

▣ **"aliye na ufunguo wa Daudi"** Hili lina maana ya Masihi wa kifalme wa ki-Daudi wa 2 Samweli 7, na hasa ya Isa. 22:22, ambapo picha hii halisi yake inaanzia.

▣ **"Naye afunga wala hakuna afunguaye"** Hili lina rejelea mahubiri ya injili (kama vile maelezo katika Ufunuo 3: 8).

## MADA MAALUMU: MATUMIZI YA "MLANGO" KATIKA AGANO LA KALE (SPECIAL TOPIC: USE OF "DOOR" IN THE NT)

**3:8 "Nimeuweka mbele yako mlango uliofunguliwa mbele yako, ambao hapana awezaye kuufunga"** Hii ni KAULI TIMILIFU TENDAJI YENYE KUARIFU na KAULI TIMILIFU TENDWA YENYE HALI YA KUENDELEA. Hii inamaanisha ama

1. Fursa za kuhubiri (funguo, kama vile Mathayo 16:19)
2. Kuingilia kwenye karamu ya Kimasihi (kuvishwa katika weupe, kama vile Ufunuo 3: 4)
3. Fursa ya ki-Mungu kwa ajili ya huduma (kama vile Matendo 14:27, 1 Wakorintho 16: 9, 2 Wakorintho 2:12, Kol. 4: 3)

▣ **"Kwa kuwa unazo nguvu kudogo"** Hii ndiyo sababu ya kwanza kati ya sababu tatu, kwa nini Yesu aliufungua mlango mpana wa fursa kiasi hiki. Hili ndilo pekee kati ya makanisa saba ambayo kwayo Yesu hakuwa na kitu cha kusema.

▣ **"nawe umelitunza neno langu"** NJEO YA KITENZI (KAULI TENDAJI YENYE KUARIFU YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU) inamaanisha wakati maalumu wa mateso au tendo la udanganyifu la utii. Walikuwa na 'imani kidogo,' lakini waliitumia vizuri!

▣ **"wala hukulikana jina Langu"** Hii linaweza kuwa rejea ya mateso yaliyosababishwa na madai ya Concilia, wafuasi wa mlengo wa kawaida wa ibada ya ki-falme (kama vile Ufunuo 2:13).

**3:9 " Nitawasababisha *wale* wa sinagogi ya Shetani,"** Hii inaweza kurejea upinzani wa Ki-yahudi dhidi ya Injili. Kanisa, sio Wayahudi wasioamini, ni watu wa kweli wa Mungu.

▣ **"nitawafanya waje kusujudu mbele ya miguu yako"** Huu ni msisitizo wa Isa. 45:14; 49:23; 60:14, ambayo hapo awali ulizungumza ujio wa watu wa mataifa mengine katika taifa la Kiyahudi, lakini kwa sababu hawa wanaoitwa Wayahudi walimkataa Masihi wangelikuja kuwainamia waumini wa Ki-yahudi kwa kuwaonyesha upendo wa Mungu kwao (kama vile Isaya 43:4,9). Huu ni mfano mzuri wa jinsi Agano Jipya kwa ujumla, na Yohana kwa umaalumu, imeuboresha unabii wa Agano la Kale kuhusu Israeli. Yohana anayatumia maandishi ambayo hapo awali yaliwashuhudia watu wa mataifa mengine wakija Yerusalemu kuirejesha ibada ya YHWH, lakini katika wakati mpya wa uadilifu hii taswira ya kisiasa inaenea kwa mjumuisho wa ulimwengu uaminio (Wayahudi na Mtaifa) wakiwa na Wayahudi wasio amini waje na kuinama! Ulimwengu huu wa Israeli na Yerusalemu unaonyesha

kwamba Ufunuo, mbali na kuthibitisha utimilifu wa kweli wa unabii wa Agano la Kale kwa taifa la Wayahudi, umewabadilisha (angalia Waefeso 2:11-3: 13). Hii ni 'siri ya Injili iliyofichwa tangu zama'!

**3:10**
**NASB 'Kwa sababu umeliweka neno la ustahimilivu Wangu'**
**NKJV, NJB' Kwa sababu umeituza amri Yangu ya kustahimili '**
**NRSV' Kwa sababu umelituza neno langu la ustahimilivu wa uvumilivu '**
**TEV' Kwa sababu umeitunza amri yangu ya kuvumilia '**

Hili linaweza kuwa rejeo la Yohana 8:51 au 17:6. Yesu haahidi kulitenga kanisa lake kutoka kwenye mateso kwa sababu katika waraka wa mateso kwa makanisa saba ya mateso, hata mauti, ilijitokeza.

Mstari wa 10 unahusu hukumu ya Mungu duniani kote kwa wasioamini. Ni muhimu kutofautisha kati ya 'dhiki' waumini huvumilia kwa imani na 'ghadhabu ya Mungu' inayouangukia ulimwengu usioamini.

Wafasiri daima wanatofautiana juu ya jinsi kanisa litalindwa katikati ya hukumu hii ya kiama

1. Wengine wanaliona kanisa kana kwamba linahifadhiwa na Mungu (kama vile Yohana 17:15)
2. Wengine walinaona hili kama kuuelekea unyakuo wa siri wa waumini kabla ya kipindi hiki

Napendelea # 1. Watu wa Mungu hawakuyaepuka mateso na kifo wakati wa karne chache za kwanza katika utamaduni wa Wagiriki-Warumi au mateso endelevu na kifo huku injili ikienea, au watahifadhiwa wakati wa uzao wa mwisho Zama Mpya. Daima, mateso yamelitakasa na kuliimarisha kanisa!

Kipengele cha fasihi cha sura ya 2-3, ambapo kwacho Kanisa linakabiliwa na mateso, kinatimizwa na kipengele cha maandishi cha mbingu, ambapo Kanisa la wahanga wa mauaji limeomba kulipiza kisasi. 'Hasira ya Mungu' inatolewa kwa hatua za ukali (mihuri1/4, baragumu 1/3, uharibifu wa jumla wa vitasa), kila hatua ikitolewa kwa lengo la kuwaita waliopotea waurudie wokovu. Hasira ya mwisho ya Mungu, kifo cha pili, ziwa la moto (kama vile. Ufunuo 20), si tena kwa ajili ya ukombozi, bali kiujumla linaadhibika kabisa. Kanisa lililoteswa linakuwa kanisa la ushinda na watesi wasionamini wanapitia mateso! Mungu akiwa katika udhibiti! Tazama Mada Maalum: Uvumilivu katika Ufunuo 2:2.

▣ **"kuwajaribu wakaao juu ya nchi"** Kifungu hiki kinatumiwa mara kwa mara katika kuirejea hali tulivu ya uasi wa waaminio (kama vile Ufunuo 6:10, 18:13, 1:10, 12:12, 13: 8, 12, 14, 17: 8). Mungu anataka watubu na kuamini (taz. 1 Tim 2:4, 2 Pet 3:9), lakini hawataweza, hata katika wakati wa kupanuka kwa hukumu za mihuri, tarumbeta, na vitasa. Tazama Mada Maalum:Maneno ya Kiyunani ya kujaribiwa katika Ufunuo 2:2.

**3:11 "Naja upesi"** Huu ni msisitizo endelevu juu ya uharaka wa ujio wa Bwana (kama vile Ufunuo 1:1, 3, 2:16; 22: 7,12,20). Kanisa la kwanza lilitarajia kurudi kwa uharaka wa Bwana. Hili ni tumaini la kila kizazi cha Wakristo. Tazama Mada Maalum: Ujio wa Mapema katika Ufunuo 1: 3.

▣ **"shika sana ulicho nacho"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO, yenye maana ya 'kuendelea kushikilia sana' kama KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU ya Ufunuo 2:25 ilitazamia tendo la udanganyifu la kushikilia sana (angalia Mada maalum ya Ufunuo 2:2). Kama waumini wamshikiliavyo Mungu, atawashikilia nao (kama vile Wagalatia 6:9). Huu ndio uhusiano wa ki-maagano wa utawala wa Mungu na wajibu wa wanadamu!

Wokovu ni uamuzi wa awali wa toba na imani (kama vile Marko 1:15, Matendo 3:16,19; 20:21) ikifuatiwa na toba ya mtindo wa maisha na imani, utii, huduma, na uvumilivu. Vitu vyote hivi ni muhimu katika ukomavu wa Ukristo.

▣ **"taji"** Hili ni rejeo jingine kwa taji ya Stefano iliyotajwa katika Ufunuo 2:10. Lililokuwa zawadi kwa uaminifu.

**3:12 "Yeye ashindaye"** Angalia katika angalizo 2.2.

▣ **"Nitamfanya kuwa nguzo katika hekalu la Mungu Wangu"** Filadelfia ilikuwa katika eneo la tetemeko la ardhi; mfano wa nguzo ulioonyesha dhana ya utulivu. Majina ya raia maarufu yaliandikwa kwenye nguzo za hekalu huko Filadelfia. Neno 'hekalu' hapa ni neno (*naos*) kutoka katika KITENZI cha neno 'kukaa' na lilitumiwa mahali ambapo

uwepo wa mungu ulipofanya maskani. Waumini walioshinda kamwe hawatatoka mbele ya Mungu (kama vile Zaburi 23:6; 27:4-6). Huu unaweza kuwa mfano kwa sababu inaonekana hapata kuwa na hekalu katika zama mpya (kama vile 21:22).

◙ **"Nami nitaandika juu yake jina la Mungu Wangu"** Angalia marudio matano-funganifu ya neno 'Yangu' katika Ufunuo 3:12. Huku ni kukubalika kwa urahisi wa urafiki na Mungu. Jina liliashiria umiliki (kama vile 7: 3; 14: 1; 22: 4).

◙ **"Yerusalemu mpya. . .jina jipya"** Ufunuo huzichukua nabii za Isaya.

1. Vitu vipya, Isa. 42:9; 43:19; 48:6 (Ufunuo 21:5)
2. Wimbo mpya, Isa. 42:10 (Ufunuo 5:9; 14:3)
3. Jina jipya, Isa. 62:2; 65:15 (Ufunuo 2:17)
4. Mbingu mpya na nchi mpya, Isa. 65:17; 66:22 (Ufunuo 3:12; 21:1).

Mji mpya wa mbinguni, Yerusalemu, pia umetabiriwa katika Isaya 40: 2,9; 41:27; 44: 20,28; 52: 1,2,9; 62: 1,6,7; 65: 18,19; 66: 10,13,20 (Ufunuo 21: 2,10). Ni mfano wa uwepo wa Mungu kati ya watu Wake. Unabii wa Agano la Kale umewekwa ki-ulimwenguni. Yerusalemu mpya sio mji katika Palestina, bali ni ahadi ya zama mpya za haki.

**3:13** Angalia angalizo katika Ufunuo. 2:6.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 3:14-22**
**14 Na kwa malaika wa kanisa lililoko Laodikia andika; Haya ndiyo anenayo yeye aliye Amina, Shahidi aliye mwaminifu na wa kweli, mwanzo wa kuumba kwa Mungu. 15 Nayajua matendo yako, ya kuwa hu baridi wala hu moto; ingekuwa heri kama ungekuwa baridi au moto. 16 Basi, kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi wala moto, nitakutapika utoke katika kinywa changu. 17 Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi. 18 Nakupa shauri, ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri, na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane, na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona. 19 Wote niwapendao mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu. 20 Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami. 21 Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi, kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi. 22 Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa.**

**3:14 "Aliye Amina"** Huu ni msisitizo wa jina la YHWH, 'Mungu wa Amina,' katika Isa. 65:16. Neno 'Amina' ni aina ya neno la Agano la Kale kwa maana ya 'kuamini' au 'imani' (kama vile Mwa. 15:16; Hab 2: 4). Mara kwa mara lilisisitiza uaminifu au chenye kutumainika (kama vile 1: 6; 2 Wakorintho 1:20). Angalia Mada Maalum katika Ufunuo 1: 6.

◙ **"shahidi aliye mwamini na kweli"** Hili inaweza kuwa maneno mengine kutoka sura ya 1 (kama vile Ufunuo 1: 5). Katika maandiko ya kale ya Kiyunani zote mbili hizi zinazotumiwa kumtaja YHWH. Inawezekana kwamba *emeth*, ambalo ni neno la Kiebrania kwa maana ya 'imani,' 'amini' au 'tumaini,' lilitafsiriwa kama *pistos* (aminifu) na *alētheia* (kweli). Maneno haya mawili ya kiyunani hutumiwa mara kwa mara katika Ufunuo kwa ajili ya Yesu (kama vile Ufunuo 3:14, 19:11, 21: 5, 22: 6).

**NASB, NKJV'mwanzo wa uumbaji wa Mungu '**
**NRSV 'asili ya uumbaji wa Mungu'**
**TEV 'asili ya yote ambayo Mungu ameumba'**
**NJB 'kanuni ya uumbaji wa Mungu'**

Huu ni mwelekezo wa Mwanzo 1:1 na Yohana 1:1. Neno 'mwanzo' (Kiebrania, *bereshith*) na 'asili' (Kigiriki, *archē*) lina mahusiano mawili: (1) kuanza au (2) asili, chanzo. Maneno haya yalitumiwa katika malumbano ya Arian

/ Athanasius (mtu wa Utatu) wa karne ya nne na inaelezea Mith. 8:22-31. Hekima ilikuwa ni kiumbe cha kwanza cha YHWH na kwa njia ya hekima vyote viliumbwa. Hii labda ndiyo asili ya matumizi ya Yohana ya '*logos*' katika Injili yake (kama vile Yohana 1:1). Hii ni mojawapo ya vifungu vingi zaidi juu ya kuwepo kwa mapema kwa Kristo (kama vile Yohana 1: 1, 8: 57-58, 2 Wakorintho 8: 4, Filipi 2: 6-7; Wakolosai 1:17), na pia kuwa Kristo kuwa wakala-Baba katika uumbaji (kama vile Yohana 1:3, 1 Wakorintho 8:16; Kol.1: 15,18; Waebrania 1: 2).

**MADA MAALUMU: *ARCHĒ* (SPECIAL TOPIC: *ARCHĒ*)**

**3:15"hu baridi wala hu moto"** Hii inaweza kuwa na maana ya maji ya uvuguvugu ambayo watu wa jiji huu wangepaswa kunywa kwa sababu ya chemchem za moto za mahala hapo. Tukio kama hilo linafanyika dhidi ya kanisa la Sardi (kama vile 3: 1).

**3:16"Nitakutapika kutoka katika kinywa Changu"** Maonyo ya Ufunuo 2:5; 3:3,16,17 yanastaajabisha inapogundulika kuwa yanashughulikiwa kwenye makanisa yinayoonekana ya karne ya kwanza. Huku siko kupotezwa kwa wokovu, bali kupotezwa kwa huduma thabiti (kama vile Ufunuo 3:19, Ebr 12: 5-13).

**3:17 "Kwa kuwa wasema, mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja na kitu"** Mstari wa 17 na 18 ni dokezo la kihistoria la Laodikia kama kituo cha benki, kituo cha pamba safi iliyotiwa nakshi, na kituo cha jicho la utumwa. Hatari ya mafanikio yao ni kwamba walidhani walikuwa na vingi wakati walikuwa na kidogo (kama vile 3: 1).

**MADA MAALUMU: UTAJIRI (SPECIAL TOPIC: WEALTH)**

**3:18 "ununue Kwangu"** Hii inaweza kuwa na maana ya Isa. 55:1-3, ambapo sadaka ya Mungu ya wokovu ilikuwa huru, bali emeelezewa kama yenye gharama.

▣ **"mavazi meupe"** Angalia angalizo katika Ufunuo 3:4.

▣ **"aibu ya uchi wako isionekane"** Katika Agano la Kale uchi ulikuwa ni ishara ya kushindwa, hukumu, na umaskini.

**3:19"Nawakemea"** Neno hili la Kiyunani *elegchō* linatumiwa kwa maana ya 'kufungua na kwa namna hiyo kuponya au kusahihisha' (kama vile Yohana 3:20, Waefeso 5: 11-14).

▣ **"na kuwarudi"** Kuadhibiwa na Mungu ni ishara kwamba tu washirika wa familia yake (kama vile Ayubu 5:17, Mith. 3:12; Zab 94:12, Ebr 12: 6).

▣ **"uwe na bidii"** Hili ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Inatoka katika mzizi ule ule sawa na neno 'joto' au 'kuchemsha' (*zestos*) litumikalo katika Ufunuo 3:15-16. Kumjua na kumtumikia Mungu lazima kuwe kwa shauku kali na mtindo wa maisha.

▣ **"utubu"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Kuna msisitizo wa mara kwa mara katika nyaraka hizi saba ambazo Wakristo, si tu waamini, wanapaswa kutubu na kurudi kwa Kristo kwa maana ya ukomavu, uimarifu, na furaha (kama vile Ufunuo 2:5, 16, 22, 3:3, 19). Toba ni muundo wa maisha, si tu hatua ya awali!

**3:20"Tazama, nasimama mlangoni, nabisha"** 'na kuendelea kubisha.' Ingawa kanisa hili halikupokea neno la sifa, lilipokea mwaliko mzuri. Huu sio mwaliko wa kuwa Mkristo, lakini zaidi sana, mwaliko kwa washirika wa kanisa kurudi kwenye ushirika muhimu pamoja na Kristo. Aya hii mara nyingi hutumiwa pasipo muktadha kuurejelea uinjilisti. Taswira ya 'mlango' ilitumiwa katika Injili (kama vile Marko 13: 28-29; Luka 12:36) kama njia ya kurejelea ukaribu wa kuja kwa Kristo. Angalia Mada maalum: Mlango katika Ufunuo 3: 7.

▣ **"mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU inayoashiria kitendo muhimu lakini kisichojulikana. Katika maeneo mengi ya ulimwengu kubisha hodi hufuatana

na matamshi ya salamu. Angalia kipengele hiki; mtu/kanisa lazima aitikie na kufungua mlango. Hiki ni kipengele cha ki-maagano cha uhusiano wote wa Mungu na wanadamu. Anachukua hatua, anaweka ajenda, lakini wanadamu wanapaswa kujibu. Pia, angalia kwamba majibu sio ya awali tu bali endelevu. Wokovu sio bidhaa, bali ni uwiano wa mfumo wa maisha. Unazo changamoto zake, lakini kuna hakikisho la kudumishwa kwa ibada.

▣ **"nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nani"** Huu ni mwelekezo wa sadaka ya amani (kama vile Mambo ya Walawi 3, na 7), wakati wa ushirika ambapo Mungu katika mfano alikula pamoja na mtoaji. Wengine wanaona hii kama rejea ya karamu ya kimasihi ya siku ya kiama

Neno lililotumiwa hapa kwa ajili ya mlo ni lile lile lililotumika kwa ajili ya mlo wakati wa mwisho wa siku, ambayo ilikuwa ni wakati mkuu wa ushirika wa familia na mshikamano. Katika Mashariki kula daima imekuwa ishara ya agano, urafiki, na ushirika.

**3:21"nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi,"** Hii ni picha yenye nguvu ya ushirika wa karibu na yenye kujumuishwa. Kuna vodokezo vingi katika Agano Jipya kwa waumini 'wanaotawala na Kristo (kama vile Ufunuo 2:26, 27, Luka 22:30, Mathayo 19:28, 1 Kor 6: 2 ; 2 Tim 2:12; 20: 4). Ufunuo 22:5 ina maana ya utawala wa milele pamoja na Wakristo. Angalia Mada Maalum juu ya Utawala ndani ya Ufalme wa Mungu katika Ufunuo 5:10.

▣ **"kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na baba yangu katika kiti chake cha enzi"** Ni jambo la ajabu kujua kwamba Yesu tayari ameushinda ulimwengu (kama vile Yohana 16:33, Waefeso 1:21-22) na kwamba tayari ameketi mkono wa kuume wa Baba (kama vile Waefeso 1:20; 2:1 na Ufunuo 22:1) na kwamba anataka tuungane naye katika ushindi wake!

**MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa masomo ya fasiri wenye kumaanisha kwamba wewe unao wajibu wa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu lazima aenende katika nuru tuliyonayo. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kuyaacha mambo haya kwa Mfasiri.

Maswali haya ya majadiliano yanatolewa ili kukusaidia kufikiri kufikiria juu ya maswala makuu ya sehemu hii ya kitabu. Yamekusudiwa kukuchokonoa fikra, lakini siyo kutoa maana.

1. Kwa nini unabii wa Yohana wa nyakati za mwisho huanza na nyaraka kwa makanisa saba (na kwa nini saba tu) katika Asia Ndogo?
2. Kwa nini kila waraka huanza na maelezo ya Kristo kuanzia sura ya 1?
3. Nyaraka hizi zinahusianaje na Kanisa leo?
4. Je, unatafsirije maonyo haya yenye nguvu yaliyoelekezwa kwa makanisa haya?
5. Ni namna gani mafundisho ya 'mara ukishaokolewa, daima umeokolewa' yanavyohusiana na onyo na wito wa ustahimilivu katika nyaraka hizi?
6. Kwa nini 3:20 siyo ahadi ya wokovu?
7. Ni kwa namna gani sehemu nyingine ya fasihi inahusiana na nyaraka kwa makanisa saba? Je! Mungu atawaokoa waumini wa wakati wa mwisho kutokana na mateso, bali siyo waumini wa karne ya kwanza?

# UFUNUO 4 & 5

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Ibada ya mbinguni | Chumba cha Kiti Cha enzi cha Mbinguni | Maono ya Utukufu wa Mungu na Mwana Kondoo | Kuabudu Mbinguni | Mungu hukabidhi Hatima ya ulimwengu kwa Mwana Kondoo |
| 4:1-6a | 4:1-11 | 4:1-6a | 4:1-6a | 4:1-11 |
| 4:6b-11 | | 4:6b-11 | 4:6b-8 | |
| Gombo na Mwana Kondoo | Mwana Kondoo atwaa gombo | | Gombo na Mwana Kondoo | |
| 5:1-14 | 5:1-7 | 5:1-5 | 5:1-5 | 5:1-5 |
| | Mwana Kondoo Anastahili | 5:6-10 | 5:6-10 | 5:6-10 |
| | 5:8-14 | | | |
| | | 5:11-14 | 5:11-14 | 5:11-14 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia (A Guide to Good Bible Reading)")

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa kusoma wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi zako kwa tafsiri zako za Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika nuru tuliyonayo. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja na somo ni moja tu.

5. Aya ya kwanza
6. Aya ya pili
7. Aya tatu
8. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Sura hizi mbili zinaunda umoja wa fasihi :sura ya 4 inamwonyesha Mungu kama muumbaji (kidokezo cha *Elohim*, Mungu muumbaji, mtoaji na muendelezaji wa uhai wote, kama vile Zaburi 104) na sura 5 inaonyesha Mwana –Kondoo (Yesu) kama mkombozi (kidokezo juu ya YHWH, Mungu kama mwokozi, Mkombozi, na Mungu wa kufanya agano, k.v Zaburi 103). Mazingira makubwa ya fasihi yanaendelea mpaka kwenye ufunguzi wa muhuri saba. Hata hivyo, muhuri yenyewe inaanza katika sura ya 6 na kuendelea mpaka sura ya 8:1.
B. Sura ya 4 huunda dhamira (utukufu salama na utawala wa YHWH) ya kitabu cha Ufunuo. Mandhari ya kiti cha enzi yafanana na hema takatifu la mbinguni la Waebrania 8 na 9. Wazo hili linalorudiwa rudiwa (utukufu wa Mungu wa mbinguni) huunda kiini cha lengo la imani ya Kiyahudi ya kumfikia Mungu kwa fikra.

C. Kitabu cha ufunuo kimsingi sio jinsi gani na lini ya Kuja kwa mara ya Pili; Kimsingi ni mamlaka ama enzi ya Mungu katika historia ya mwanadamu. Sura hizi mbili ni za lazima kwenye kuelewa sehemu ya kitabu iliyobaki pamoja na kusudi lake!

D. Ni dhahiri kutokana na sura mbili hili ambazo Yohana anatumia lugha ya matukio ya siku za mwisho kuelezea ukweli wa Kiroho. Kuelezea ukweli wa kiroho, Yohana alitumia michoro kutoka mafungu ya maneno ya maangamizi ya siku za mwisho wa ulimwengu ya Agano la Kale hasa kitabu cha Ezekiel, sura ya 1 na ya 10; pia 2:9,10; Daniel 4; 7:13-14 na pia rejea nyingi za maandishi ya Kiyahudi ya matukio ya siku za mwisho ya kipindi cha agano la kale na agano jipya kama vile I Enock. Kama hili ni kweli basi sio vizuri kabisa kuulazimisha ufunuo katika uhalisia, kuwa kwenye mstari wa ufasiri kihistoria, hasa pale tunalazimisha matukio ya siku zetu za leo, tamaduni zetu, muundo wa kijografia kuwa kwenye maelezo ya kitabu cha kale cha matukio ya siku za mwisho. Hii sio kumaanisha kwamba kwa namna yeyote ile ufunuo sio wa kweli. Hii haikumaanisha kufasiri kama simulizi za kihistoria; mfano mzuri wa kanuni za ufasiri yaweza kuwa ile mifano ya Yesu (tazama Fee and Stuart, *How To Read* The *Bible For All Its Worth*, uk. 256)!

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 4:1-11**

[1] **Baada ya hayo naliona, na tazama, mlango ukafunguka mbinguni, na sauti ile ya kwanza niliyoisikia kama sauti ya baragumu ikinena nami, ikisema, Panda hata huku, nami nitakuonyesha mambo ambayo hayana budi kuwako baada ya hayo. [2] Na mara nalikuwa katika Roho; na tazama, kiti cha enzi kimewekwa mbinguni na mmoja ameketi juu ya kile kiti; [3] na yeye aliyeketi alionekana mithili ya jiwe la yaspi na akiki, na upinde wa mvua ulikizunguka kile kiti cha enzi, ukionekana mithili ya zumaridi. [4] Na viti ishirini na vinne vilikizunguka kile kiti cha enzi, na juu ya vile viti naliona wazee ishirini na wanne, wameketi, wamevikwa mavazi meupe; na juu ya vichwa vyao walikuwa na taji za dhahabu. [5] Na katika kile kiti cha enzi kunatoka umeme na sauti na ngurumo. Na taa saba za moto zilikiwaka mbele ya kile kiti cha enzi, ndizo Roho saba za Mungu. [6] Na mbele ya kile kiti cha enzi kulikuwa na mfano wa bahari ya kioo, kama bilauri; na katikati ya kile kiti cha enzi, na pande zote za kile kiti, walikuwako wenye uhai wanne, wamejaa macho mbele na nyuma. [7] Na huyo mwenye uhai wa kwanza alikuwa mfano wa simba; na mwenye uhai wa pili alikuwa mfano wa ndama; na mwenye uhai wa tatu alikuwa na uso kama uso wa mwanadamu; na mwenye uhai wa nne alikuwa mfano wa tai arukaye. [8] Na hawa wenye uhai wanne, kila mmoja alikuwa na mabawa sita; na pande zote na ndani wamejaa macho, wala hawapumziki mchana wala usiku, wakisema, Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi, aliyekuwako na aliyeko na atakayekuja. [9] Na hao wenye uhai wanapompa yeye aketiye juu ya kiti cha enzi utukufu, na heshima, na shukrani, yeye aliye hai hata milele na milele, [10] ndipo hao wazee ishirini na wanne huanguka mbele zake yeye aketiye juu ya kile kiti cha enzi, nao humsujudia yeye aliye hai hata milele na milele, nao huzitupa taji zao mbele ya kile kiti cha enzi, wakisema, [11] Umestahili wewe, Bwana wetu na Mungu wetu, kuupokea utukufu na heshima na uweza; kwa kuwa wewe ndiwe uliyeviumba vitu vyote, na kwa sababu ya mapenzi yako vilikuwako, navyo vikaumbwa.**

**4:1**
**NASB, NKJV "baada ya hayo naliona"**
**NRSV "baada ya hili naliona"**
**TEV "katika hatua hii nalipata maono mengine na niliona"**
**NJB "tena, katika maono yangu, niliona"**

Kanuni hii ya kisarufi, ikiwa na tofauti ndogo, pia yapatikana katika Ufu. 7:1,9; 15:5; 18:1 na ikiwezekana Ufu. 19:1. Kuna mfululizo wa maono. Mengi kati ya maono ya kinabii yalikuwa yamewekwa katika hali iliyotakiwa ki-maagano, ikisisitiza neno "ikiwa. . .basi" la Agano la Mungu na Israel. Imani ya Israeli wakati huo iliamua hatima yake. Hili pia ni kweli kwenye maono ya Yohana katika kitabu cha ufunuo

1. Maneno ya Yesu kwa makanisa saba yana mashariti. Mwitikio wake kwa maonyo yake uliamua hatma yake.
2. Hukumu za muhuri na baragumu pia zina mashariti. Mungu anapenda wasioamini watubu na kurudi kwake

Kama katika Agano la Kale, Mpango wa Mungu wa ukombozi wa ulimwengu. (kama vile Mwa. 3:15; 15:12-2; 17:1-8, pia angalia Matendo 2:23; 3:18; 4:28; 13:29) ni usio na mashariti (kama vile Mwa. 12:1; Ufunuo 2-3) juu ya mwitikio wa kimaagano wa binadamu. Huu mpango wa ukombozi wa wote unafunuliwa katika matukio ya kimbingu ya sura ya 4 na 5.

**MADA MAALUM : MPANGO WA UKOMBOZI WA MILELE WA YHWH (SPECIAL TOPIC: YHWH's ETERNAL REDEMPTIVE PLAN)**

◙ **"mlango ukafunguka mbinguni"** Hii ni KAULI TIMILIFU TENDWA ENDELEVU, ikimaanisha kwamba mlango ulifunguliwa na Uungu (IRABU TENDWA) na kubaki wazi (NJEO TIMILIFU). Hii ni njia nyingine ya kuelezea mafunuo ya Mungu mwenyewe kwa mwanadamu. Hii inafanana katika Ufu.19:11; Ezek. 1:1; Mt. 3:16; Yohana 1:51 na Matendo 7:55-56. Angalia Mada Maalum katika Ufu.3:7.

Neno "mbingu" limetumika zaidi ya mara 50 katika maandiko ya Yohana na mara zote liko katika UMOJA isipokuwa kwa mara moja Katika Ufu. 12:12. Maana hasa ya badiliko hili, kutoka kwenye UMOJA kwenda kwenye WINGI, kitheolojia haijulikani. Walimu wa dini ya Kiyahudi walijadiliana kama kulikuwepo mbingu tatu ama saba (kama vile 2 Kor. 12:2). Yohana anaangazia juu ya uwepo wa mbingu moja, mahali pale Mungu huishi. Ingawa pana misukosuko duniani, lakini mbinguni hapatakuwa hivyo.

**MADA MAALUM: MBINGU NA MBINGU YA TATU (SPECIAL TOPIC: THE HEAVENS AND THE THIRD HEAVEN)**

◙ **"na sauti ile ya kwanza niliyoisikia kama sauti ya baragumu"** Sauti kama ya baragumu ilitamkwa katika Ufu. 1:10 (angalia nukuu). Mara ya kwanza inamaanisha Yesu anazungumza, lakini kwa sababu sura ya 4 & 5 ni sehemu ya fasihi na Yesu hatambulishwi hadi 5:5,9-10,12,13, pengine hapa inamaanisha malaika anayefunua (tabia ya fasihi ya matukio ya siku za mwisho). Sauti ya malaika na mvumo wa wa baragumu vinahusiana na maelezo ya Paulo kuhusu Kuja mara ya Pili (kama vile 1 The. 4:16).

◙ **"Panda hata huku"** Wenye kujua mpango wa Mungu wamechukulia kwamba hii ni siri ya fuyraha nyingi kupita kiasi ya kanisa kwa sababu ya uelewa wao wa kimatarajio wa kitabu cha ufunuo (unabii wote wa Agano la Kale kiuhalisia lazima utimilizwe; kanisa na Israeli vimetengana kabisa; kanisa litanyakuliwa kwa siri kwenda mbinguni ili kwamba unabii wa Agano la Kale upate kutimilizwa kwa Israeli ya kidunia). Mara nyingi ufasiri huu unajengewa na hoja ya chini kwa chini, pale neno"kanisa" halionekani katika Ufunuo baada ya sura ya 3 (isipokuwa katika Ufu. 22:10). Hata hivyo, hakuna chochote kwenye maandiko kuonyesha mtu yeyote aliyeitwa mbinguni ila Yohana.

Kwasababu ya "umeme" na "ngurumo" ya Ufu. 4:5, hili laweza kuwa dokezo kwamba Musa aliitwa (kama vile Kut. 19:20,24) kwenye mlima wa Sinai kupokea ufunuo wa Mungu (kama vile Kutoka 19-20, hasa. 19:16,19). Pia tambua sauti ya Mungu iliyotajwa kama sauti ya baragumu katika kitabu cha Kut. 19:19(angalia Mada Maalum: Pembe zilizotumika Israel katika Ufu. 1:10)

◙ " **mambo ambayo hayana budi kuwako baada ya hayo"** Kifungu hiki chaweza kuwa kidokezo cha Dan. 2:29,45, kama ndivyo basi inahusu matukio ya kihistoria katika mlolongo, na sio matukio ya baadaye. Ufunuo sio mambo ya karne ya kwanza na vitu katika karne nyingi za baadaye, bali matukio ambayo:

1. Hujirudia katika kila kizazi (kama vile Mt. 24:4-14)
2. Huakisi kipindi chote katikati ya Kuja kwa Kristo kwa mara ya kwanza na Kuja kwake mara ya pili (sehemu saba ya fasihi ya kitabu)

Kirai hiki ni sawa na 1:1. Neno la Mungu na mapenzi yake lazima (*dei*) vitimie. Hapa kipengere cha Muda (yaani, muda mfupi) kimeachwa, lakini suala la muda kujulikana limebaki. Mungu atatimiza mpango wake wa ukombozi!

**4:2"Na mara nalikuwa katika Roho"** Yohana anaelezewa kama aliye katika Roho Ufu. 1:10; 17:3 na 21:10. Hii yaweza kufanana na kile kilichotokea kwa Ezekieli katika Ezek. 8:1-4; 11:1, Yesu katika Mt. 4:8; kwa Filipo Katika 8:39-40, na Paulo katika 2 Kor. 12:1-2. Haijulikani kama ulikuwa ni usingizi wa kiroho au kuhamishwa kimwili.

◙**"kiti cha enzi kimewekwa mbinguni na mmoja ameketi juu ya kile kiti"** Neno hili" kiti cha enzi" (*thronos*) limetumika mara 47 ndani ya kitabu hiki. Utawala wa Mungu ndilo wazo kuu linalorudiwa rudiwa katika ufunuo (sura 4 & 5). Kiti cha enzi ni ishara ya mafumbo, ni njia ya matukio ya siku za mwisho kuonyesha kuwa YHWH yupo katika udhibiti wa historia yote. Mungu ni roho binafsi, ya milele; Hakai kwenye kiti cha Enzi (angalia Mada Maalum Katika Ufu. 2:1)!
Kusudi moja la uwasilishaji wa unabii na matukio ya siku za mwisho ni maarifa ya Mungu na udhibiti wake wa matukio yajayo. Historia yote inajulikana na ni yenye makusudi (*telos*,kama vile. Mt. 24:14; 1 Kor. 15:24-28).
Kiti cha enzi kimeelezewa kama "kimewekwa." Hii NJEO YA WAKATI USIOTIMILIFU yawezakuwa na maana mbili: (1) kwa muda wote kilikuwa kimewekwa au (2) ulikuwa ni muundo tu. Hili laweza kuwa dokezo kwa Dan. 7:9, "viti vya enzi vilikuwa ni muundo tu."

**4:3"na yeye aliyeketi alionekana mithili"** Yohana hawezi kuelezea umbo la Mungu kwa sababu katika fikra za Kiyahudi, hili halikustahili kabisa (k.v. Kut. 33:17-23; Isa. 6:5). Lakini ataelezea utukufu wa Mungu katika rangi tatu ya vito vya thamani. Vito vya thamani pia vimetumika katika Ezek.28:13 kuelezea lugha ya picha (Bustani ya Mungu) ya kimbingu.

**NASB, NKJV,**
**NRSV, TEV "Yaspi"**
**NJB "almasi"**
Rangi halisi na vito vya thamani havijulikani katika fasihi ya kale. Majina ya vito vya thamani na rangi vilibadilishwa toka nchi hadi nchi na kipindi hadi kipindi. Yaspi lilikuwa jiwe la kwanza kupatikana kwenye dirii ya kuhani mkuu ambalo limetajwa katika Kut.28:17-21. Jiwe hili laonekana kuwa jiwe safi. Litahusianishwa na "bahari ya kioo" (kama vile Ufu. 4:6; 15:2; 21:11,18,21). Laweza kufananishwa na almasi.

**NASB, NKJV "Sardoniki"**
**NRSV, TEV "Akiki"**
**NJB "Rubi"**
Akiki lilikuwa jiwe lenye rangi nyekundu kama damu. Lilikuwa jiwe la mwisho kwenye dirii ya kuhani mkuu. Hili laweza kuwa kidokezo kwa Mungu akiwa wa kwanza na wa mwisho pamoja na msisitizo kwa kabila la kimasihi la Yuda (upinde wa zumaridi). Mawe haya mawili yaliyo orozeshwa katika maandishi ya kale kama muhtasari wa madini yote.

◙ **"na upinde wa mvua ulikizunguka kile kiti cha enzi, ukionekana mithili ya zumaridi"** Zumaridi Ndilo jiwe la Yuda kwenye dirii ya kuhani mkuu. Msisitizo juu ya upinde wa mvua kwa kiasi kikubwa ni wakukisiwa sana lakini kuna nadharia mbili.

1. Baadhi wanaliona kama kidokezo cha Mwa. 9:16, ambapo upinde wa mvua ni ishara ya kinga ya Mungu ya kimaagano na ishara kwamba gharika imekwisha; katikati ya hukumu palikuwepo na ahadi na rehema.
2. Wengine wanahusisha na Ezek. 1:28, isharaya utukufu wa YHWH.

Ikiwa upinde wa mvua ni ishara ya hukumu au maagano haijulikani, lakini kiuhakika ulikuwa ni upinde usio wa kawaida kwa sababu ulikuwa ni wa kijani kwa rangi yake na na haukaksi mwanga wake wa kawaida.

**4:4 "naliona wazee ishirini na wanne, wameketi"** Sababu ya viti vya enzi ishirini na vine imekuwa ikileta mgogoro.

1. Baadhi waliona hili kama kufananishwa na taratibu za ukuhani wa aina ya Haruni iliyopangwa na Daudi katika 1 Nya. 24:7-19

2. Wengine waliona hili kama kidokezo kwa baraza la mbinguni lilitajwa katika 1 Fal. 22:19; Isa. 24:23; Dan. 7:9-10,26
3. Bado kuna wengine waliona kama muunganisho wa mitume wa kabila kumi na mbili za Israeli na mitume kumi na wawili, wanaowakilishwa watu kamili wa Mungu (kama vile Ufu. 21:12,14)

Inashangaza kuona kwamba hesabu hii haionekani kwenye maandiko ya Kiyahudi yenye matukio ya siku ya mwisho kati ya kipindi cha agano la kale na agano jipya.

◙ **"Wazee ishirini na wanne wameketi"** Kumekuwapo na mjadala mkubwa kuhusu utambulisho wa wazee hawa. Zipo nadharia kuu mbili

1. Wanawakilisha waaminio:
   a. Wakionekana kama waliovishwa mavazi meupe (kama vile 1 Kor. 9:25; 1 The. 2:19; 2 Tim. 4:8; Yakobo 1:12; 1 Pet. 5:4)
   b. Malaika kamwe hawajasemekana kuvaa taji na kukaa kwenye viti vya enzi kama vile Ufu. 4:4,10)
   c. Wako katika orodha ambayo kwa udhihirisho inajumuisha malaika (kama vile Ufu. 5:11)
   d. Ufu. 5:9-10 katika toleo la biblia za Kilatini na ki-Shamu, na baadaye katika upokeaji wa maandiko ulijumuisha wazee watatu kwenye wimbo wa ukombozi
2. Wanawakilisha malaika:
   a. Malaika huvaa mavazi meupe (kama vile Mt. 28:3; Yohana 20:12; Marko 16:5; Matendo 1:10; Ufu. 15:6 na Dan. 10:5,6)
   b. Wazee hawa wakati wote wanatambulishwa na viumbe hai kama katika Ufu. 5:11,14, ambao waonekana kuorodheshwa makundi matatu tofauti ya malaika
   c. Mmoja wa wazee anatenda kama malaika (kama vile 5:5)
   d. Katika Isa. 24:23 malaika wa baraza la mbinguni la Mungu wanaitwa "wazee"
   e. Ushahidi wa kimaandiko wa Ufu. 5:10 waonyesha kwamba mzee hajijumuishi katika wimbo wa watu waliokombolewa

MADA MAALUM: MZEE (SPECIAL TOPIC: ELDER)

◙**"taji za dhahabu"** Hakuna mahala popote kwenye maandiko panapoonyesha malaika kuvishwa taji (hata yule malaika mwenye nguvu katika Daniel 10). Kundi kubwa la malaika waovu toka kuzimu wameelezewa kuvaa kitu Fulani kinachofanana na taji la dhahabukatika Ufu. 9:7

**4:5"Na katika kile kiti cha enzi kunatoka umeme na sauti na ngurumo"** Hii inafanana na Kut. 19:16-19, inaelezea tukio halisi la ajabu lililozunguka uwepo wa Mungu juu ya Mlima Sinai. Virai hivi vinaonyesha uwepo wa Mungu (kama vile Ufu. 11:19) ama hukumu yake (kama vile Ufu 8:5; 16:18).

◙ **"taa saba za moto"** Hizi zaonekana kuwa taa saba tofauti (mienge), Sio bakuri moja pamoja lenye tambi saba (kama vile Kut. 25:37; Zek. 4:2). Zinafanya kazi kwa njia ifananayo na zile nyingine "saba," ikirejea juu ya uwepo wa Mungu.

◙ **"ndizo Roho saba za Mungu"** Kifungu hiki cha maneno kinatumika katika Ufu.1:4; 3:1 na 5:6. Mara nyingi inatafsiriwa kama rejeo la Roho Mtakatifu kwa msingi wa 1:4, lakini hakuna rejeo lingine lolote miongoni mwa mengine linalothibitisha tafsiri hiyo. Kifungu hiki cha maneno kinaonekana kuchukuliwa kuwa sawa na makanisa (nyota saba, Ufu. 3:1; taa saba, Ufu. 4:5) ama pamoja na kuwa na uwezo wote wa kujua mambo yote kwa Mwana-Kondoo (Ufu. 5:6). Angalia Mada Maalum: Roho Saba katika Ufu. 1:4.

**4:6 "bahari ya kioo, kama bilauri"** Kumekuwepo nadharia nyingi kuhusu kifungu hiki cha maneno:

1. Kinahusu beseni kubwa la hekaluni (kama vile 1 Fal. 7:23; 2 Nya. 4:2-6)
2. Inahusiana na dhana ya sakafu ya Yakuti Samawi inayopatikana katika Kut. 24:9-10
3. Ni sehemu ya gari lililokuwa linabeba Kiti cha Enzi cha Mungu katika Ezek. 1:22,26; 10:1

4. Ni alama ya kutenganishwa kutoka kwenye utakatifu wa Mungu (kama vile Ufu.15:2).

Bahari inaondolewa katika Ufu.21:1, kuonyesha laana (kama vile Mwanzo 3) ya dhambi ya binadamu na matengano yameondolewa. Angalia Ufu 21:1.

◙ **"wenye uhai wanne"** Viumbe hawa waliohai wanaelezwa katika Ufu. 4:6-8. Wao ni mchanganyiko wa Makerubi *cherubim* wa Ezek. 1:5-10 na 10:1-17 na maserafi *seraphim* wa Isa. 6:2,3. Hesabu za mabawa na nyuso vinatofautiana, lakini ni taswira ya viumbe mbalimbali vilivyo tofauti tofauti kama vile wanadamu /wanyama/malaika wanaozunguka kiti cha enzi cha Mungu (kama vile Ufu 4:6,8,9; 5:6,8,11,14; 6:1,3,5,7; 7:11; 14:3; 15:7; 19:4).

MADA MAALUM: *CHERUBIM* (SPECIAL TOPIC: *CHERUBIM*)

◙ **"wamejaa macho mbele na nyuma"** Hii inaweza kurejea moja ya zile nyuso nne za wale makerubi au yaweza kuwa sitiari ya kibiblia ya uwezo wa Mungu wa kujua mambo yote kama vile (kama vile Ufu. 4:8; Ezek. 1:18; 10:12).

**4:7 "simba. . .ndama. . .mwanadamu. . . tai"** Hiki ni kidokezo dhahiri cha Ezek. 1:6,10. Katika fasihi za walimu wa dini ya Kiyahudi vimeorodheshwa kama viumbe venye nguvu kwenye taratibu za uumbaji wa Mungu. Irenaeus (120-202 B.K) alitumia sura hizi nne zilizotofautiana kuelezea waandishi wanne wa injili (mapokeo ya kanisa mwishowe wakalowea kwa Yohana, tai; Luka, mwanadamu; Marko, maksai; Mathayo, simba) lakini hili ni la kimtazamo sana na kiistiari. Hivi viumbe venye tabia tofauti, ni vya mfano tu, na sio halisia. Kuujua msisistizo wa Agano la kale juu ya kuendeleza utaratibu wa uumbaji wa Mungu, mwanadamu mwenye tabia zaidi ya moja na kiumbe mnyama ki-Lawi watakuwa si safi. Hizi sio simulizi za kihistoria za vitu na matukio halisi, lakini ni mfano wa juu sana wa namna ya uwasilishaji ukitafuta kuelezea ukweli wa ndani, wa kiroho; kwa maana hiyo anabaki kuwa Mungu ambaye hajawahi kuwepo, (kur. 8,9), Mtakatifu pekee(uk. 8), na muumbaji wa vitu vyote (uk.11).

**4:8 "Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu"** Hawa viumbe walio hai wanarudia wimbo wa maserafi *seraphim* katika. 6:2,3. Hii ndiyo tenzi ya kwanza ya rohoni kati ya nyingi zipatikanazo katika kitabu cha Ufunuo (kama vile. 4:8,11; 5:9-10,12,13; 7:12; 11:17-18; 12:10-12; 15:3-4; 16:5-7; 18:2-8; 19:1-3, 6-7). Mara nyingi tenzi za rohoni ni njia za kutafsiri maono alama nyingine, kama bahari ya kioo itendayo kazi kwa ubora kabisa wa Kiebrania wa kikomo cha utakatifu wa Mungu.

◙ **"Bwana Mungu Mwenyezi, aliyekuwako na aliyeko na atakayekuja"** Hizi zilikuwa nyadhifa tatu za Agano la kale kwa minajili ya Mungu (Ufu. 1:8)

1. BWANA= YHWH (kama vile Kut.3:14; Zab.103)
2. Mungu = *Elohim* (kama vile Zaburi 104)
3. Mkuu= *El Shaddai*, jina la ubaba kwa Mungu (kama vile Kut. 6:3)

Angalia **MADA MAALUM: MAJINA YA MIUNGU (SPECIAL TOPIC: NAMES FOR DEITY)** katika Ufu. 1:8.

◙**"ALIYEKUWAKO NA ALIYEKO NA ATAKAYEKUJA"** Kifungu hiki ni kile chenye wadhifa wenye kujirudi (kama vile Ufu. 1:4; 4:8; angalia nukuu katika Ufu. 1:4). Hii ni kulichezea jina la Mungu wa Agano, YHWH, linalotokana na KITENZI "aliyekuwako." Somo hili limerudiwa katika Ufu.4:9 na 10 kwenye kifungu "kwake Yeye aishiye Milele na Milele" (kama vile Ufu. 10:6; 15:7).

**4:9-11** Hii ni sentensi ya Kiyunani, inayoonyesha kwamba ibada ya ndani ina Yeye aketiye katika Kiti cha enzi na aishiye milele (kama vile Zaburi 47; Dan. 4:34; 12:7). Hili lawezakuwa ni dokezo kwa malaika wahudumiao wanaoitwa baraza la mbinguni (kama vile 1 Fal. 22:19; Ayubu 1:6; Dan. 7:10) ama "malaika wa uwepo" (yaani, Tobit 12:15).

**4:9"wenye uhai"** Hawa viumbe wa kimalaika mara nyingi wametajwa kitabuni (kama vile Ufu. 5:6,8,14; 6:1; 7:11; 14:3; 15:7; 19:4).

**4:10"nao huzitupa taji zao mbele ya kile kiti cha enzi"** Hii ni ishara ya kukiri kwao kwamba Mungu anastahiri sifa zote na heshima! Walitambua kwamba uweza ulitoka kwa Mungu!

**4:11"wewe ndiwe uliyeviumba vitu vyote"** Wazee na wenye uhai humsifu Mungu kama muumbaji, Mwezeshaji na mpaji wa vitu vyote. Huu ndio msisitizo wa kithiolojia wa jina la *Elohim* (kama vile Mwanzo 1; Ayu 38-41; Zaburi 104). Sura hii hutumia maana ya kithiolojia ya majina mawili yatumikayo sana kumhusu Mungu kuelezea matendo yake. Mwendelezo wa ufunuo wa Agano Jipya unaweka wazi kwamba Yesu alikuwa wakala wa Baba katika uumbaji. (kama vile Yohana 1:3; 1 Kor. 8:6; Kol. 1:16 na Ebr. 1:2).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 5:1-5**
**[1] Kisha nikaona katika mkono wa kuume wake yeye aliyeketi juu ya kile kiti cha enzi kitabu kilichoandikwa ndani na nyuma, kimetiwa muhuri saba. [2] Nikaona malaika mwenye nguvu akihubiri kwa sauti kuu, N'nani astahiliye kukifungua kitabu, na kuzivunja muhuri zake? [3] Wala hapakuwa na mtu mbinguni, wala juu ya nchi, wala chini ya nchi, aliyeweza kukifungua hicho kitabu, wala kukitazama. [4] Nami nikalia sana kwa kuwa hapakuonekana mtu astahiliye kukifungua hicho kitabu, wala kukitazama. [5] Na mmojawapo wa wale wazee akaniambia, Usilie; tazama, Simba aliye wa kabila ya Yuda, Shina la Daudi, yeye ameshinda apate kukifungua kile kitabu, na zile muhuri zake saba.**

**5:1"**Kisha nikaona katika mkono wa kuume wake yeye aliyeketi juu ya kile Kiti cha enzi**"** Tafsiri iliyo bora ya kifungu hiki cha maneno ingekuwa (toleo la Biblia ya ki-Shamu (Peshitta) iliyotafsiriwa kwa kiingereza na Lamsa na Amplified Bible). Sio wazo la Mungu kushikilia kwa nguvu kitabu bali Mungu hukishikilia kwa ajili ya mtu Fulani ili akichukue na kukifungua.
Kifungu "mkono wake wa kuume" ni tabia za mwanadamu ki-Biblia kuelezea nguvu na mamlaka ya Mungu (angalia Mada Maalum kwenye Ufu. 2:1) Mungu hana mwili wa asili; Yeye ni Roho (kama vile Yohana 4:24), ambaye hakuumbwa na wa milele.

◙ **"kitabu"** Neno la Kiyunani ni "*biblion*" ambalo baadaye lilitumika kuhusu kitabu cha mswada wa kale. Watoa maoni wengi wanakubali kwamba vitabu havikuonekana hadi karne ya pili (NKJV, NRSV, TEV and NJB). Kuna nadharia kadhaa kuhusu maana ya kitabu hiki.

1. Kitabu cha mateso kipatikanacho katika Ezek. 2:8-10; na Ufu. 10:8-11
2. Kitabu ambacho hawako tayari kukisoma kwa sababu Mungu anawapofusha kiroho (kama Isa. 29:11; Rum. 11:8-10,25)
3. Matukio ya siku za mwisho (kama vile Dan. 8:26)
4. Wosia wa kirumi wa mwisho ama Agano ambalo lilitiwa muhuri kidesturi na muhuri saba
5. Kitabu cha uzima (kama vile Dan. 7:10; 12:1), ambacho kimetajwa mara nyingi katika kitabu cha ufunuo (kama vile 3:5; 17:8; 20:12,15)
6. Agano la Kale (kama vile Kol. 2:14; Efe. 2:15)
7. Vibao vya kuandikia vya mbinguni vya 81:1,2.

Kwa maoni yangu mwonekano wa #1, #2, au #3 yawezekana kuwa bora kuliko yote; gombo ni kitabu cha hatima ya mwanadamu na upeo wa historia.

◙**"kilichoandikwa ndani na nyuma"** Hii haikuwa kawaida katika ulimwengu wa kale kwa sababu ya ugumu wa kuandika upande wa pili wa mafunjo, ingawa imetajwa katika Ezek. 2:8-10 na Zecharia 5:3. Inamaanisha Mungu anatawala na kudhibiti juu ya historia yote na hatma ya mwanadamu.
Mambo yote yako kwenye NJEO ENDELEVU (yaliyoandikwa na kupigwa muhuri) yale yanayoelezea kuwa magombo yapo kwenye KAULI TENDWA YA WAKATI TIMILIFU. La kwanza lipo kwenye muundo maalumu wa

kisarufi lililotumika kuelezea maandiko kwa namna yalivyovuviwa (yaani, Yohana 6:45; 8:17; 10:34, n.k). La pili ni njia ya kuelezea kuwa gombo lililindwa, kutunzwa na kuwekwa akiba na Mungu.

◙ **"kimetiwa muhuri saba"** Muhuri saba ina vyanzo viwili vinavyoonekana.

1. Saba ilikuwa ni Hesabu ya ukamilifu tangu Mwanzo 1, kwahiyo, kilitiwa muhuri kikamilifu.
2. Wosia za kirumi zilipigwa muhuri saba.

Muhuri ilikuwa matone madogo yana yaliyokuwa na alama ya mmiliki yaliyowekwa mahali ambapo kitabu ama gombo lingefunguliwa (Angalia Mada Maalum katika Ufu. 7:2). Katika Ufu. 6:1-8:1 kuvunjwa kwa muhuri hii huleta majonzi katika uso wa dunia, lakini kilichomo ndani ya gombo hakifunuliwi katika maandiko. Kwa hakika katika Muundo wa kitabu, muhuri wa saba huanzisha baragumu saba ambazo ndiyo muhuri saba.

**5:2"Nikaona malaika mwenye nguvu"** Baadhi kiasili wanaona uhusiano wa jina Gabriel, ambalo linamaanisha " mtu wa Mungu mwenye nguvu." Malaika mwingine mwenye nguvu anatamkwa katika Ufu.10:1 na 18:21. Upatanisho wa kimalaika ni wa kawaida katika fasihi ya matukio ya siku ya mwisho ya Wayahudi ya kipindi kati ya agano la kale na agano jipya.

◙ **"akihubiri kwa sauti kuu"** Alikuwa anautambulisha uumbaji wote.

◙ **"Ni nani astahiliye kukifungua kitabu, na kuzivunja muhuri zake"** Neno "stahiliye" ni neno la kibiashara linalohusu matumizi ya seti ya mizani. Ilikuja kumaanisha "lile lenye kutangamana na." Kitu Fulani kinawekwa upande mmoja wa mzani wa kile kiwekwacho upande ule mwingine ni sawa. Kingaliweza kutumika katika maana ya chanya au hasi. Hapa, ni thamani isiyokadilika ya mwokozi asiye na dhambi. Ni Yesu pekee aliyelingana na jukumu la kukamilisha. Ni Yesu pekee anayestahilli. (kama vile Ufu. 5:7, 9-10,12).

**5:3"Wala hapakuwa na mtu mbinguni, wala juu ya nchi, wala chini ya nchi, aliyeweza kukifungua hicho kitabu, wala kukitazama"** Hii inaonyesha kutoweza kabisa kwa malaika ama wanadamu kuyatekeleza mapenzi ya Mungu! Uasi umewaathiri wote! Uumbaji hauwezi kujisaidia wenyewe! Hapana yeyote anayestahili!

**5:4"nikalia sana"** Hii ni NJEO YA KITENZI CHA WAKATI USIOTIMILIFU, ambacho inaonyesha mwanzo wa kitendo ama kitendo kilichorudiwa wakati uliopita. Hii ilimanisha "kilio cha sauti kubwa," kwa hiyo ikawa ni sifa watu wa mashariki ya kale.

**5:5 "Na mmojawapo wa wale wazee akaniambia"** Hapa tunamkuta mmoja wa wazee akitenda katika shughuli ya mtafsiri wa kimalaika, kama katika kitabu cha Daniel. Angalia MADA MAALUM: MZEE (SPECIAL TOPIC: ELDER)katika Ufu. 4:4.

◙ **"Usilie"** Hii ni KAULI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ikiwa na KIAMBATA HASI ambayo mara nyingi humaanisha kuzuia kitendo kilichoko kwenye mchakato.

◙ **"Simba aliye wa kabila ya Yuda"** Hiki ni kidokezo cha Mwa. 49:9-10 (kama vile II Esdras 12:31,32). Masihi ndiye ashindaye vita (Mfalme) kutoka katika kabila la Yuda.

◙ **"Shina la Daudi"** Hiki ni kidokezo kwa 2 Samueli 7 na hasa Isa. 11:1-10. Wazo hili hili la Masihi wa ufalme wa Daudi waweza kupatikana katika Yer. 23:5; 33:5 na Ufu. 22:16.

◙ **"yeye ameshinda"** Hii ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU, ambayo inamaanisha ulikuwa ni ukweli uliotimilizwa (yaani, Kalvary na kaburi tupu). Tambua kuwa Simba haendi kushinda kwa nguvu zake, lakini ni kwa kujitoa kwake (kama vile ufu 5:6).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 5:6-10**

**[6] Nikaona katikati ya kile kiti cha enzi na wale wenye uhai wanne, na katikati ya wale wazee, Mwana-Kondoo amesimama, alikuwa kana kwamba amechinjwa, mwenye pembe saba na macho saba, ambazo ni Roho saba za Mungu zilizotumwa katika dunia yote. [7] Akaja, akakitwaa kile kitabu katika mkono wa kuume wake yeye aliyeketi juu ya kile kiti cha enzi. [8] Hata alipokitwaa kile kitabu, hao wenye uhai wanne na wale wazee ishirini na wanne wakaanguka mbele za Mwana-Kondoo, kila mmoja wao ana kinubi, na vitasa vya dhahabu vilivyojaa manukato, ambayo ni maombi ya watakatifu. [9] Nao waimba wimbo mpya wakisema, Wastahili wewe kukitwaa hicho kitabu na kuzifungua muhuri zake; kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa, [10] ukawafanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu; nao wanamiliki juu ya nchi.**

**5:6 "Mwana-Kondoo amesimama"** Dhana hii ya Mwana –Kondoo (yaani kondoo mtoto, *arnion*) yaonyesha mfano wa kulipa fidia ki-kweli kweli na ufufuo wa Yesu. Mwana –Kondoo ametamkwa katika kitabu chote cha Ufunuo (Kama vile Ufu. 5:6,8,12,13; 6:1,16; 7:9,10,14,17; 12:11; 13:8; 14:1,4(mara mbili),10; 15:3; 17:14; 19:7,9; 21:9,14,22,23,27; 22:1,3). Sitiari ya sadaka inatoka kwa

1. Mwana –Kondoo wa pasaka (Kutoka 12)
2. Mmojawapo wa wanakondoo aliyetolewa pasaka kila siku asubuhi na jioni (yenye kuendelea, kama vile Kut. 29:38-46; Hes. 28:3,6,10,23,31; 29:11,16,19,22,25,28,31,34,38)
3. Mwana-Kondoo aliyechinjwa Katika Isa 53:7 au Yohana 1:7,29

Sitiari hii inatumika kumhusu Yesu kwa maana tofauti mbili: (a) kama mhanga wa sadaka asiye na hatia na (b) kama mshindi ajaye (pia inapatikana katika mafundisho ya Kiyahudi yenye matukio ya siku ya kiyama, k.v. I Enock 90:9; Testament of Joseph 19:8-9). Katika Agano Jipya Yohana Mbatizaji pekee katika Yohana 1:29,36 na Yohana katika Ufunuo 5:6,8,12,13; 61:1, anamrejea Yesu kama “Mwana - Kondoo”(Paulo anadai hili, lakini bila kuwa na neno katika 1 Kor. 5:7).

◙ **"kana kwamba amechinjwa"**Alikuwa amekufa lakini sasa yu hai. Kufufuka kwa Masihi (kama vile Ufu. 13:3).

◙ **"mwenye pembe saba na macho saba"** Neno la kwanza linahusu nguvu au mwenye nguvu (kama vile Kut. 27:2; 29:12; Kumb. 33:17; 2 Nya. 18:10; Zab. 112:9; 132:17; Yer. 48:25; Ezek. 29:21; Zak. 1:18-21). Neno la pili linahusu uwezo wa Mungu (kama vile Ufu. 4:6,8; Ezek. 1:18; 10:12; Zek. 3:9 na 4:10).
Maana ya ishara hii inafanana na ya kwenye Dan. 7:13-14.

◙ **"ambazo ni Roho saba za Mungu"** Angalia Mada Maalum katika Ufu. 1:4 na maelezo katika Ufu. 4:5.

**5:8"alipokitwaa kile kitabu, hao wenye uhai wanne na wale wazee ishirini na wanne wakaanguka mbele za Mwana-Kondoo"** Hii inaonyesha kuabudiwa kwa Mwana Kondoo kama aabudiwavyo Mungu (kama vile Ufu. 5:13), ambalo ndo wazo kuu katika Ufunuo.

◙ **"na vitasa vya dhahabu vilivyojaa manukato, ambayo ni maombi ya watakatifu"**Malaika ndio walikuwa wabeba maombi kuyapeleka mbele za Mungu katika maandiko ya Kiyunani kwenye kipindi kati ya agano la kale na agano jipya (kama vile Tobit 12:15; III Baruch 11). Wazo la manukato kuwakilisha maombi limetumika mara kadhaa kwenye maandiko (kama vile Ufu. 8:3-4; Zab. 141:2; Luka 1:10).

◙ **"watakatifu"** Ingawa neno "kanisa" halionekani baada ya sura ya 3, dhana ya "watakatifu" inaendelea kitabu chote na lazima ihusu watu wa Mungu. Dhana ya waaminio kama “watakatifu” ni ya kawaida katika ufunuo (kama vile Ufu. 8:3-4; 11:18; 13:7,10; 14:12; 16:6; 17:6; 18:20,24; 19:8 na 20:9).

**MADA MAALUM: WATAKATIFU (SPECIAL TOPIC: SAINTS)**

**5:9-10** Kuna utofauti muhimu wa maandiko ya Kiyunani yahusianayo na KIWAKILISHI NOMINO "sisi." Biblia ya NKJV ina KIWAKILISHI NOMINO "sisi" katika Ufu. 5:9, "tumekombolewa kumwelekea Mungu" na katika ufunuo 5:10," "ametufanya kuwa wafalme na makuhani kwa Mungu wetu." Tafsiri nyingi za kisasa (NASB, NRSV, TEV, NJB) zinaruka neno "sisi" kwenye aya zote mbili. Ikiwa sisi ipo kwenye aya zote mbili hivyo sadaka ya kifo cha Yesu inajumuisha wale wazee ishirini na nne wanaoonekana kuwa viumbe wa kimalaika. Pia kuwepo kwa hao, (*autous*) katika ufu. 5:10 Kisarufi kunaondoa uwezekano wa "sisi" kuwa asilia.

**5:9 "Nao waimba wimbo mpya wakisema"** Katika Agano la Kale kuna vidokezo kwenye wimbo mpya (kama vile Zab. 33:3; 40:3; 98:1; 144:9; 149:1 na Isa. 42:10). Katika kila tukio kubwa kwenye Agano la Kale, watu wa Mungu walitiwa moyo kuimba wimbo mpya wakisifu utendaji wa Mungu. Huu ndio wimbo wa kikomo kuhusu kujifunua Mungu mwenyewe kwa njia ya Masihi na kazi ya Masihi ya ukombozi kwa niaba ya waaminio (kama vile Ufu. 5:9,12,13; 14:3).
Msisitizo juu ya Mambo mapya ni sifa ya kizazi kipya katika Isaya 42-66.

1. " mambo mapya," Isa. 42:9
2. " wimbo mpya," Isa. 42:10
3. "fanya jambo jipya," Isa. 43:19
4. "mambo mapya," Isa. 48:6
5. " jina jipya," Isa. 62:6
6. "mbingu mpya na dunia mpya," Isa. 65:17; 66:22.

Katika Ufunuo kuna "mambo mapya mengi."

1. "Yerusalemu mpya," Ufu. 3:12; 21:2
2. "jina jipya," Ufu. 2:17; 3:12
3. "wimbo mpya," Ufu. 5:9,10,12,13; 14:3
4. "mbingu mpya na dunia mpya," Ufu. 21:1

◙ **"Wastahili wewe kukitwaa hicho kitabu na kuzifungua muhuri zake"** Wimbo huu mpya (Ufu. 5:9-10) ni aina tano za ufafanuzi wa kustahili kwa Mwana Kondoo.

1. kifo cha mbadala (kama vile Ufu. 5:6,9,12; 13:8; 1 Pet. 1:18-19)
2. gharama ya ukombozi imelipwa (kama vile Ufu. 5:9; 14:3-4; Marko 10:45; 1 Kor. 6:19-20; 7:23; 1 Tim. 2:6)
3. watu walionunuliwa kutoka kila taifa (kama vile Ufu. 5:9; 7:9; 14:6)
4. kufanya waaminio kuwa ufalme wa makuhani (kama vile Ufu. 1:6; 5:10)
5. watatawala pamoja naye (kama vile Ufu. 3:21; 5:10; 20:4)

◙ **"watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa"** Hii ni sitiari ya kujirudia kwa wote (kama vile Ufu. 7:9; 11:9; 13:7; 14:6). Yaweza kuwa ni dokezo kwenye Dan. 3:4,7.

◙**"ukamnunulia Mungu kwa damu yako"** Hakika hii ni nukuu ya upatanisho wa kushangaza wa Mwana Kondoo wa Mungu. Dhana hii ya Yesu kujitoa sadaka kwa ajili ya dhambi ni ya kati katika ufunuo (kama vile Ufu. 1:5; 5:9,12; 7:14; 12:11; 13:8; 14:4; 15:3; 19:7; 21:9,23; 22:3) na pia katika agano jipya lote (kama vile Mt. 20:28; 26:28; Marko 10:45; Rum. 3:24-25; 1 Kor. 6:20; 7:23; 2 Kor. 5:21; Gal. 3:13; 4:5; Efe. 1:7; Flp. 2:8; 1 Tim. 2:6; Tito 2:14; Ebr. 9:28; na 1 Pet. 1:18-10).

**MADA MAALUM: KULIPA FIDIA/KOMBOA (SPECIAL TOPIC: RANSOM/REDEEM)**

**5:10 "ukawafanya kuwa ufalme na makuhani"** Hiki ni kidokezo cha Kut. 19:6 na Isa. 61:6. Istirahi hii sasa inatumika kwa kanisa, watu wa agizo kuu la Mungu Angalia maelezo katika 1:6.

◙ **"nao wanamiliki juu ya nchi"** Baadhi ya watafsiri wanaliona hili katika dhana ya wakati ujao na wengine huliona kama uhalisia wa wakati huu. Kuna utofauti wa maandiko ya Kiyunani kati ya NJEO ZA WAKATI UJAO katika MSS א, P na NJEO YA WAKATI ULIOPO katika MS A (Alexandria). Kama yapo kwenye maana ya WAKATI ULIOPO basi yanafanana na ya Rum.5:17 na Efe.2:6. Kama ni WAKATI UJAO inawezekana kuhusika na kutawala kwa watu wa

Mungu wakiwa na Kristo (kama vile Mt. 19:28; Luka 22:30; 1 Kor. 4:8; 2 Tim. 2:12; Ufu. 3:21; 5:10). Hata utawala wa wakati ujao unaonekana katika njia mbili.

1. Katika Ufu. 20:4, 6 yaonekana kurejea utawala wa miaka 1000
2. Katika Ufu Ufu. 22:5 yaonekana kurejea utawala wa milele (kama vile Zab. 145:13; Isa. 9:7; Dan. 2:44; 7:14,18,27)
3. Yumkini miaka 1000 ni ishara ya milele

Toleo la UBS[4] linaipa njeo ya wakati ujao daraja "A"

**MADA MAALUM: KUTAWALA KATIKA UFALME WA MUNGU (SPECIAL TOPIC: REIGNING IN THE KINGDOM OF GOD)**

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 5:11-14**
**11 Nikaona nikasikia sauti ya malaika wengi pande zote za kile kiti cha enzi, na za wale wenye uhai, na za wale wazee, na hesabu yao ilikuwa elfu kumi mara elfu kumi na elfu mara elfu, 12 wakisema kwa sauti kuu, Astahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa, kuupokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na baraka. 13 Na kila kiumbe kilichoko mbinguni na juu ya nchi na chini ya nchi ya juu ya bahari, na vitu vyote vilivyomo ndani yake, nalivisikia, vikisema, Baraka na heshima na utukufu na uweza una yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na yeye Mwana-Kondoo, hata milele na milele. 14 Na wale wenye uhai wanne wakasema, Amina. Na wale wazee wakaanguka, wakasujudu.**

**5:11"malaika wengi"** Mstari huu unaorodhesha makundi matatu ya malaika (1) makundi ya malaika maelfu kwa maelfu (2) viumbe wenye uhai wanne; (3) Wazee ishirini na wanne

◙ **"na hesabu yao ilikuwa elfu kumi mara elfu kumi na elfu mara elfu"** Hii yaonekana kuwa kidokezo cha baraza la mbinguni la Dan.7:10 (angalia nukuu katika Ufu. 5:1).

**5:12"Astahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa kuupokea uweza"** Hii ni uthibitisho wa mwana kutoka kwenye viumbe vya kimalaika. "aliyechinjwa" ni KAULI TIMILIFU TENDWA ENDELEVU (kama vile Ufu. 5:6; 13:8), inayomaanisha "alichinjwa kipindi cha nyuma" akiwa na mabaki ya alama na athari za kuchinjwa. Tutakapomwona Yesu atakuwa bado ana alama za misumari kipindi cha kusulibiwa kwake. Amebaki kuwa alama ya heshima kwao! Dhana ya msalaba imebaki kuwa dokezo na kitovu katika ufunuo. Angalia nukuu katika Ufu.5:9.
Katika aya hii sifa saba zinatolewa juu ya Mwana Kondoo kwa utaratibu wa kimalaika:

1. Nguvu
2. Utajiri
3. Hekima
4. Ukuu
5. Heshima
6. Utukufu
7. Baraka

Sifa zaweza kuwa zimetoka 1 Nya.29:10-12, ambazo zaweza pia kuwa chanzo cha hitimisho la kiluturujia kwenye sala ya Bwana katika Mt. 6:13 katika tamaduni za maandiko ya Kiyunani.
Toleo la Biblia ya NASB (uk. 1855) inaongeza nukuu kwamba sifa za Mungu zilianza na tatu katika Ufu. 4:11, kisha nne katika Ufu. 5:13, na hatimaye saba katika Ufu. 5:12 na 7:12. Kumbuka mafundisho ya matukio ya siku ya kiyama ni muundo wa aina ya uwasilishaji wa hali ya juu ambao mara nyingi hutumia tarakimu za alama.

**5:13** ufahamu wote juu ya uumbaji wa mwanadamu (yawezekana kwaya kubwa ya mwanadamu), wanadamu (wote walio hai na walio kufa) katika Ufu. 5:13 wanawabariki Baba na Mwana zikiwemo na Baraka nne (kama vile Ufu. 5:14; Zab. 103:19-20; Flp. 2:8-11) na maagizo ya kimalaika (viumbe wanne wenye uhai na wazee ishirini na wanne) wakikizunguka kiti cha enzi wanatangaza Baraka (kama vile Ufu. 5:14).

**5:14 "Amina"** Hili ni tangazo kutoka kwa malaika wanne wa kwenye kiti cha enzi (viumbe wanne wenye uhai). Angalia Mada Maalum katika Ufu.1:6**.**

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa masomo wa fasiri ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika nuru tuliyonayo. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa kukusaidia mambo muhimu ya kipengele ya kitabu hiki. Yamekusudiwa kukuchokonoa mawazo na sio kutoa maana.

1. Je! Sura ya 4 na 5 zinatoshelezaje kusudi kuu la kitabu hiki?
2. Ni nini aina ya uwasilishaji wa fasihi ya Sura ya 4 na 5?
3. Je! Kutoka chanzo kipi Yohana hupata maono yake?
4. Je! Wazee ni akina nani?
5. Je! Viumbe vilivyo fafanuliwa katika Ufu. 4:7-10 ni makerubi ama maselafi?
6. Orodhesha vyeo vya Masihi katika Agano la Kale vinavyopatikana katika sura ya 5.
7. Orodhesha sifa tano za agano la kale juu ya Masihi zinazopatikana katika Ufu. 5:9 na 10.

# UFUNUO 6:1-7:17

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Muhuri | Muhuri wa kwanza: Mshindi | Ufunguzi wa mihuri sita ya kwanza | Muhuri | Mwana-Kondo kufungua muhuri saba |
| 6:1-2 | 6:1-2 | 6:1-2 | 6:1-2 | 6:1-2 |
| | Muhuri ya pili: MIgogoro Duniani | | | |
| 6:3-4 | 6:3-4 | 6:3-4 | 6:3-4 | 6:3-4 |
| | Muhuri ya tatu: Mapungufu Duniani | | | |
| 6:5-6 | 6:5-6 | 6:5-6 | 6:5-6 | 6:5-6 |
| | Muhuri ya nne: Kuenea kwa Vifo Duniani | | | |
| 6:7-8 | 6:7-8 | 6:7-8 | 6:7-8 | 6:7-8 |
| | Muhuri ya tano: Kilio cha wafiadini | | | |
| 6:9-11 | 6:9-11 | 6:9-11 | 6:9-11 | 6:9-11 |
| | Muhuri ya Sita: Machafuko Ulimwengu Mzima | | | |
| 6:12-17 | 6:12-17 | 6:12-17 | 6:12-17 | 6:12-17 |
| 144,000 ya Waisraeli Waliotiwa Muhuri | Waliotiwa Muhiri katika Kila Kabila la Waisraeli | Kipindi cha mapumziko | Watu 144,000 wa Israeli | Watumwa wa Mungu watalindwa |
| 7:1-8 | 7:1-8 | 7:1-8 | 7:1-8 | 7:1-8 |
| Makutano kutoka Kila Taifa | Makutano kutoka katika Dhiki ile iliyo Kuu | Makutano Makubwa | | Kuwapa thawabu watakatifu |
| 7:9-12 | 7:9-17 | 7:9-12 | 7:9-12 | 7:9-12 |
| 7:13-17 | | 7:13-17 | 7:13 | 7:13-17 |
| | | | 7:14a | |
| | | | 7:14b-17 | |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (**Kutoka** "**Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia"("A Guide to Good Bible Reading")**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika nuru tuliyonayo. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa,lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

9. Aya ya kwanza
10. Aya ya pili
11. Aya tatu

12. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Sehemu hii inahusishwa kimazingira na sura ya 4 na 5.Sura ya 4 a 5 inaelezea matukio ya mbinguni. Wakati Ufu. 6:1-8 huelezea kuonyeshwa kwa hukumu ya Mungu juu ya dunia. Kama suala la kweli,Ufu. 4:1-16:21 huunda kitengo cha fasihi moja.
B. Utambulisho wa mpanda farasi wa kwanza (kama vile Ufu. 6:2) ni mgumu, lakini kuisadiki ni ishara ya uovu, wapanda farasi wanne ni ishara ya mateso wanayokumbana nayo waaminio katika ulimwengu wa uadui, ulioanguka (kama vile Mt. 24:6-7). Neno "dhiki" (*thlipsis*) linatumika mara kwa mara na kwa pekee kwa mateso ya Wakristo na wasioamini.
   Muhuri ya sita ilianza katika Ufu.6:12 kuelezea ghadhabu ya Mungu juu ya wasioamini. Waaminio wanasamehewa kutoka katika ghadhabu (*orgē*, kama vile Ufu. 6:16) ya Mungu, lakini walikumbana na mateso na ghadhabu ya ulimwengu usioamini.
C. Kuna matatizo matatu yenye fasiri katika sehemu hii.
   1. Je! Mihuri, baragumu, na bakuli vinahusiana kwa jinsi gani katika historia
   2. Ni watu gani hao 144,000 wa Ufu.7:4 na ni jinsi gani wanavyohusiana na kundi la pili lililotajwa katika Ufu. 7:9
   3. Kwa wakati gani wa dhiki na aina gani ya dhiki ambayo kundi katika Ufu. 7:14 linarejelewa

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): UFUNUO 6:1-2**
**[1]Kisha nikaona napo Mwana-Kondoo alipofungua moja ya zile muhuri saba, nikasikia mmoja wa wale wenye uhai wanne akisema, kama kwa sauti ya ngurumo, Njoo! [2]Nikaona, na tazama, farasi mweupe, na yeye aliyempanda ana uta, akapewa taji, naye akatoka, ali akishinda tena apate kushinda.**

**6:1 "napo Mwana-Kondoo alipofungua moja ya zile muhuri saba"** Aya hii huonyesha muunganisho kati ya sura ya 5 na 6. Muhuri huu ulifunguliwa kabla ya kitabu hakijasomwa, kwa hiyo wafasiri walisadiki kwamba walikuwa wawakilishi wa matatizo ambayo yalitokea katika kila zama (kama vile Mt. 24:6-12). Hata hivyo, kwa sababu ya kukua kwa kiwango cha hukumu, baadhi waliona kama njia ya kujiandaa haraka kwa zama za mwisho. Hapa ni mvutano wa ufasiri kati ya ufalme kama WAKATI ULIOPO na ule UJAO. Kuna sintofahamu katika agano jipya kati ya "ulimwengu ulio tayari" na "ule ambao haujatimilizwa." Kitabu cha Ufunuo chenyewe kinaelezea kwa mifano mvutano huu. Iliandikwa kwa ajili ya waamini walioteswa wa karne ya kwanza (na kila karne) na bado kuhutubia kinabii kizazi cha mwisho cha waaminio. Dhiki ni kawaida kwa kila enzi!

Muhuri wa saba ni baragumu saba na baragumu ya saba ni bakuli saba. Kama ilivyo bainishwa, kila mmoja ni wa nguvu zaidi kuliko mmoja uliyopita. Mbili za kwanza ni za ukombozi kwa kusudi fulani. Wao kimsingi walithibitisha kwamba hukumu ya Mungu ni kwa sababu tu wasioamini hawatatubu, kwa hiyo mfuatano wa mwisho (yaani, bakuli) hauna nafasi kwa toba, bali ni hukumu pekee! Lakini inaonekana kwangu kwamba muhuri ya sita na baragumu saba inaelezea mwisho wa enzi. Kwa hiyo, huu ni upatanisho katika asili na sio utaratibu wa kufuatana kwa wakati na mahara.

Ujio wa mara ya pili umejadiliwa mara tatu, mwishoni mwa ile mihuri (kama vile Ufu. 6:12-17) na baragumu (kama vile Ufu. 11:15-18), na sio tu mwisho wa bakuli katika Ufu.16:17-21 na tena katika Ufu. 19:11-21. Huu ni mpangilio wa muundo wa kitabu. Ni tamthiliya ya matukio ya kiyama katika matendo kadhaa! Tazama utangulizi wa Ufunuo wa Yohana.

◙**"mmoja wa wale wenye uhai wanne akisema, kama kwa sauti ya ngurumo "** Wale wenye uhai wanne, kama wazee, ni ngazi ya uumbaji wa kimalaika. Sauti hii, kama ngurumo, pia ilitajwa katika Ufu. 14:2 na19:6.

◙"'Njoo'" Neno hili lina maanisha ama "njoo" au "nenda." Maandiko ya kale ya kiyunani ya mswada ya herufi kubwa ya biblia yaliyopatikana katika mlima Sinai (א) huongeza neno"na tazama" (kama vile KJV, NKJV, ambayo yanaweza kurejelea kwa Yohana), lakini Alexandrinus (A) ina neno"njoo" pekee (ambalo linaweza kurejelea kwa farasi wanne). UBS4 inatoa kwa muundo huu mfupi daraja "B" (karibu na hakika). Katika muktadha amri hii (KAULI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO) hairejelei kwa Yohana au kanisa, lakini kwa wapanda farasi wanne (kama vile Ufu 6:3,5,7).

**6:2"Nikaona, na tazama, farasi mweupe"** Muktadha huu ni dokezo kwa Zek. 1:8 (farasi wane) na Zek. 6:1-8 (vibandawazi vinne). Kumekuwa na mijadala mingi kuhusu utambulisho wa huyu mpanda farasi. Tafsiri imeenea katika njia zote kutoka kwa Yesu (Irenaeus) kwa mpinga Kristo.Kwa aina hiyo ya mchafuko, kung'ang'ania hakufai. Wengine wanaamini kwamba inarejelea kwa Kristo kwa sababu ya maelezo sawa yanayopatikana katika Ufu.19:11-21, lakini mfanano pekee unaonekana kuwa rangi ya farasi. Wengine wanaona hii kama rejeo kwa kuenea kwa injili. Hii ni kwa sababu wao wanaona sura hii kama ufanano wa mahubiri ya mizeituni ya Mt. 24; Mk 13, na Lk. 21. Kwa hiyo, hii ilisadikiwa kuwa rejeo kwa Mathayo 24:14 na Marko 13:10.
Imewahi kupendekezwa, ikisimamia juu ya Ezekieli 39, kwamba hii inarejelea kwa Gogu akiongoza askari wake dhidi ya watu wa Mungu. Hii inaweza kuashiria wakati wa mwisho wa mpinga Kristo (kama vile 2 Wathesalonike 2). Kwa hali isiyo ya kawaida inaonekana kwamba malaika wangeweza kumuamuru Yesu kuja. Ingawa Yesu huvaa taji katika sura ya 6 na 19, maneno ya Kiyunani kwenye kuelezea mataji haya ni tofauti.Huko, Yesu anaitwa "muaminifu na mkweli," lakini sio hapa. Ushindi wa mpanda farasi haujaelezewa kabisa. Mpanda farasi alielezewa kama alikuwa na uta katika sura ya 6, lakini katika 19, Kristo ana upanga mkali ukatao kuwili katika kinywa chake kwa hiyo, mfanano kwa mbali ulishinda kwa sababu ya tofauti zilizokuwepo.Hii inaweza kuwa moja tu ya mifano ya Agano la kale. Mifano hii, ambayo ni dokezo kwa Walawi 26 na Eze.14:21, ilitamkwa katika Ufu. 6:8. Nyeupe ilikuwa sio tu ishara ya rangi kwa haki, lakini pia ishara ya Warumi ya ushindi wa kijeshi. Wakuu wa Kirumi ambao walikuwa wakishinda katika vita walipanda magari ya farasi kupitia miji ya Roma wakivutwa na farasi weupe wanne.

◙ **"na yeye aliyempanda ana uta"** upinde ulikuwa siraha ya kiuchaguzi ya warusha mishale wa milimani wa kundi kubwa la ufalme wa Parthia (ambao waliopanda juu ya farasi weupe). Upinde ulituumika mara nyingi katika Agano la kale kumuelezea YHWH kama shujaa (kama vile Zab. 45:4-5; Isa. 41:2; 49:2-3; Hab. 3:9; Zek. 9:13 na labda Mwa. 9:13). Kuna mifano pia ya YHWH kuhukumu mataifa mengine katika sitiari kwa namna ya kuvunja pinde zao (kama vile Zab. 46:9; Yer. 51:56 na Hosea 1:5).

◙ **"akapewa taji"** Hili ni taji "*stephanos*", kumaanisha taji la ushindi, wakati ile moja iliyotajwa katika Ufu.19:11 kwa Kristo ni "*diadema*," taji la kifalme.

◙ **"ali akishinda tena apate kushinda"** Ishara katika Ufu.6:1 ni juu ya vita na ushindi. Kwa sababu wapanda farasi wa kwanza na wa pili wameelezewa kwa madhumuni sawa, wengine waliona hii moja kama vita vya ushindi na ya pili kama vita vya wenyewe kwa wenyewe. Huu ni uvumi tu, lakini farasi wawili wanafanana kwa namna Fulani.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 6:3-4**
**[3] Na alipoifungua muhuri ya pili, nikamsikia yule mwenye uhai wa pili akisema, Njoo! [4] Akatoka farasi mwingine, mwekundu sana, na yeye aliyempanda alipewa kuiondoa amani katika nchi, ili watu wauane, naye akapewa upanga mkubwa.**

**6:4 "Akatoka farasi mwingine, mwekundu sana"** Hili ni dokezo kwa baadhi ya aina ya mauaji ya kijeshi.

◙**"naye akapewa upanga mkubwa"** Huu ulikuwa upanga mdogo wa Kirumi ulioitwa "*machaira*." Ulikuwa unavaliwa juu ya ukanda wa askari wa Kirumi na ulikuwa unatumika kwa adhabu kuu ya raia wa Kirumi (kama vile. Rum. 13:4). Kifungu "watu wauane" kinavutia kwa sababu katika Agano la kale hii ni moja ya njia YHWH alitumia kuwashinda maadui wa watu wake (kama vile Amu. 7:22; 1 Sam. 14:20; 2 Nya. 20:22).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 6:5-6**
[5] **Na alipoifungua muhuri ya tatu, nikamsikia yule wa tatu mwenye uhai akisema, Njoo! Nikaona, na tazama, farasi mweusi, na yeye aliyempanda ana mizani mkononi mwake.** [6] **Nikasikia kama sauti katikati ya hao wenye uhai wanne, ikisema, Kibaba cha ngano kwa nusu rupia, na vibaba vitatu vya shayiri kwa nusu rupia, wala usiyadhuru mafuta wala divai.**

**6:5"na tazama, farasi mweusi"** Hii ni ishara ya njaa (kama vile Mt. 24:7) ambayo ilifuatiwa na vita.

**6:6 "Kibaba cha ngano kwa nusu rupia"** Rupia moja ilikuwa ni ujira wa siku kwa askari au mfanyakazi (kama vile Mt. 20:2). Tunajifunza kutoka kwa Herodotus kwamba hii ingeweza kununua kiasi cha kawaida cha chakula kilichohitajika kwa mtu mmoja kwa siku moja. Hii huonyesha ukali wa njaa: kwamba mtu anaweza kufanya kazi siku nzima na kupata tu chakula cha kutosha kwa ajili yake mwenyewe.

**MADA MAALUM: SARAFU ZILIZOTUMIKA KATIKA PALESTINA KATIKA SIKU ZILE ZA YESU (SPECIAL TOPIC: COINS IN USE IN PALESTINE IN JESUS' DAY)**

◙ **"na vibaba vitatu vya shayiri kwa nusu rupia"** Shairi ilikuwa chakula kikuuu kwa masikini. Hili neno la Kiyunani "vibaba" ni "*choinix*" na iliyokuwa na thamani sawa na painti 1.92.

◙ **"wala usiyadhuru mafuta wala divai"** Inastajabisha ni kwa namna gani fasiri nyingi zina maelezo haya. Wengi wanajaribu kurudi nyuma kwenyemagombo ya hekaluni yaliyopatikana kwenyebahari ya chumvi kwa ajili ya kutafuta vidokezo kwenye dhabihu ya Wayahudi. Mafuta na divai kilikuwa chakula kikuu cha watu wa Mediteraniane. Ukweli kwamba hii ilikuwa haiumizi kuonyesha njaa ilyokuwa na kikomo. Ukomo huu unaweza pia kuonekana katika Ufu.6:8. Mungu hupunguza hukumu yake ili wasioamini wapate muda wa kutubu (kama vile Ufu. 16:9). Pia inawezekana kwamba yote ya haya yalikuwa yanatumika kwa madhumuni ya matibabu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 6:7-8**
[7]**Na alipoifungua muhuri ya nne, nikasikia sauti ya yule mwenye uhai wa nne akisema, Njoo!** [8] **Nikaona, na tazama, farasi wa rangi ya kijivujivu, na yeye aliyempanda jina lake ni Mauti, na Kuzimu akafuatana naye. Nao wakapewa mamlaka juu ya robo ya nchi, waue kwa upanga na kwa njaa na kwa tauni na kwa hayawani wa nchi.**

**6:8**
**NASB"farasi wa rangi ya kijivujivu"**
**NKJV"farasi wa rangi ya kijivujivu"**
**NRSV"farasi wa rangi ya kijani kijivu"**
**TEV"farasi alietiwa rangi ya kijivujivu"**
**NJB"farasi wa kifo"**

Neno "rangi ya kijivujivu" lilirejelea juu ya ile kijani ya njanonjano au ya rangi nyeupe. Katika kiingereza tunapata neno "Klorine" kutoka kwenye neno hili la Kiyunani. Bila shaka hii ilikuwa rangi ya maiti. Kwa sababu ya orodha ya njia za kifo katika Ufu. 6:8, hii inaweza kurejelea kwa wale waliouwawa au kuliwa na wanyama mwitu, ambayo ilikuwa ni moja ya laana za Agano la kale (kama vile Law. 26:22; Yer. 15:3; Eze. 5:17; 14:21).

◙ **"na yeye aliyempanda jina lake ni Mauti"** Hili ni dokezo la Agano la kale kwa Zab. 5:5 au Hosea 13:14. Ni mfano halisi wa sifa ya maneno kwa mwisho wa maisha ya kiroho. Maneno haya mawili yametumika mara tatu pamoja katika Ufunuo wa Yohana (kama vile Ufu. 1:18; 20:13-14). Neno "*kuzimu*" ni lenye maana sawa kwa neno la Agano la kale "*Sheol*," ambalo lina maanisha "mahali pa ufufuo wa wafu." Angalia MADA MAALUM: Wafu Wako Wapi? (SPECIAL TOPIC: Where Are the Dead?) katika Ufu.1:18.

◙ **"Nao wakapewa mamlaka juu ya robo ya nchi"** Angalia KIWAKILISHI NOMINO cha neno "nao" kikirejelea kwa farasi wote wanne na wapanda farasi wao. Kuna mkazo wa hukumu katika baragumu (yaani, moja ya tatu, kama vile Ufu. 8:7,8,10,12); kuna uharibifu kamili katika bakuli (kama vile Ufu. 16:1-21). Sehemu hizi ni mbinu za fasihi kuonyesha kwamba hukumu za Mungu zilikuwa na kusudi la ukombozi (kama vile Ufu. 9:20-21; 14:7; 16:9,11), lakini wanadamu walioanguka, waasi, wenye mioyo migumu wasingaliweza kuitikia katika hili (ingawa wachache wangeweza, kama vile Ufu. 11:13).

◙ **"waue kwa upanga"** Wapanda fasiri hawa wane wanawakilisha hukumu za agano katika Agano la kale (kama vile Law. 26:21-26; Yer. 15:2-3; 24:10; 27:8; 29:17-18; 32:24,36; 34:17; Eze. 5:12,17; 14:21; Amo 4:6-10). Neno kwa "upanga" ni tofauti kutoka katika Ufu. 6:4. Hii inarejelea upanga mkubwa wa vita, *hromphaia*. Hukumu zote nne za Agano la kale za vita, njaa, mapigo, na wanyama mwitu ziliorodheshwa katika Law. 26:21-26 na Eze. 14:21. Hukumu hizi za agano zilijadiliwa wazi katika Kumb. 27-29. Kumbuka, kiasili kusudi lao lilikuwa kuwasababisha Waisraeli kutubu na kurudi kwa YHWH. Wanafanya kazi hapa kwa maana ile ile ya ukombozi (kama vile Ufu. 9:20-21; 11:13; 14:7; 16:9,11).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 6:9-11**
**9 Na alipoifungua muhuri ya tano, nikaona chini ya madhabahu roho zao waliochinjwa kwa ajili ya neno la Mungu, na kwa ajili ya ushuhuda waliokuwa nao. 10 Wakalia kwa sauti kuu, wakisema, Ee Mola, Mtakatifu, Mwenye kweli, hata lini kutokuhukumu, wala kuipatia haki damu yetu kwa hao wakaao juu ya nchi? 11 Nao wakapewa kila mmoja nguo ndefu, nyeupe, wakaambiwa wastarehe bado muda mchache, hata itakapotimia hesabu ya wajoli wao na ndugu zao, watakaouawa vile vile kama wao.**

**6:9"nikaona chini ya madhabahu"** Kumekuwepo na majadiliano mengi juu ya madhabau yapi yalikuwa yanarejelewa. Neno "madhabahu" hutumiwa mara nyingi sana katika Ufunuo (kama vile Ufu. 8:3,5; 9:13; 11:1; 14:18; 16:7). Wengine wanaamini kwamba hii inarejelea kwa dhabihu ya madhabau iliyotajwa katika Law. 4:7 na iliyotajwa na Paulo katika Flp. 2:17, wakati wengine wanaamini kwamba ni madhabau ya uvumba katika Mahali patakatifu pa hema (kama vile Ufu. 8:3-5) au hekalu kwa Ufu. 11:1. Labda ni madhabau ya dhabihu kwa sababu

1. walimu wa sheria za Kiyahudi waliona hii kama sehemu ya heshima kubwa
2. inarejelea kwenye kifo (yaani, damu) cha wafiadini

Mmoja anaweza kuuliza "kwa nini wafuasi wamekusanyika chini ya madhabau?" Kumbuka kwamba katika Agano la kale "damu" ilikuwa ishara ya uhai (kam avile Mwa. 9:4; Law. 17:11,14). Katika mfumo wa dhabihu ya Waisraeli damu haikuwekwa juu ya pembe za dhabihu ya madhabahu, lakini walimimina katika msingi (yaani, Kut. 29:12; Law. 4:7,18,25; 8:15; 9:9). Kwa hiyo, uhai (yaani roho) wa wafiadini waliochinjwa katika msingi wa madhabau.

◙ **"roho zao waliochinjwa"** Roho hizi ni za waaminio waliofiadini (kati ya kifo na ufufuo) wasio na mwili (kama vile Ufu. 13:15; 18:24; 20:4). Hii ni ya kushagaza kwa sababu ni wazo la Kiyunani zaidi kuliko dhana ya Kiebrania. Wakristo wote wanaitwa kuwa wafiadini kama hali inaruhusu (kama vile Ufu. 2:10,13; Mt. 10:38-39; 16:24).
Kunaonekana kuwa hakuna uhusiano kati ya wale waliouawa na wapanda farasi wanne wa Ufu. 6:1-8 na hawa wafiadini!

**NASB"na kwa ajili ya ushuhuda waliokuwa nao "**
**NKJV"kwa neno la Mungu na kwa ajili ya ushuhuda waliokuwa nao "**
**NRSV"kwa neno la Mungu na kwa ushuhuda waliotoa"**
**TEV"na kwa ajili ya ushuhuda walikuwa nao "**
**NJB"kwa sababu ya neno la Mungu, kwa kushuhudia kwa hilo "**

Kifungu hiki ni dhamira ya mara kwa mara katika Ufunuo (kama vile Ufu. 1:9; 12:11,17; 19:10; 20:4). Inafanana sana katika maana kwa kifungu "kwa yeye ambaye hushinda" (kama vile Ufu. 2:6,11,17,26; 3:5,12,21). Hawa waliuawa kwa sababu walikuwa Wakristo watendaji.

**6:10"Wakalia kwa sauti kuu, wakisema. . . hata lini kutokuhukumu, wala kuipatia haki damu yetu"** Watoa maoni wengi wanaangalia hili kama walikuwa wakristo wa chini. Huenda hii ikawa sababu ya watoa maoni hawa

kutowahi kuwa na mateso makubwa kutoka kwa wasioamini wenyewe. Watu hawa hawakuhitaji kisasi, lakini walihitaji haki! Hii inaweza kuwa dokezo kwa Kumb. 32:43 (kama vile Ufu. 19:2). Ombi hili linafuata ushauri wa Paulo katika Rum. 12:19.

◙**"Ee Mola"** Neno hili "Mola" (*despotēs*) huelezea mamlaka kamili.Tunapata neno la Kiingereza "mdhalimu" kutoka katika neno hili la Kiyunani. Linatumika kwa YHWH katika Luka 2:29 na Mdo. 4:24 na kwa Yesu katika 2 Pet. 2:1 na Yuda 1:4.

◙**"kwa hao wakaao juu ya nchi"** Hiki ni kifungu cha kawaida sana katika Ufunuo; daima kinarejelea kwa wasioamini (kama vile Ufu. 3:10; 8:13; 11:10; 13:8,12,14; 17:2,8).

**6:11"Nao wakapewa kila mmoja nguo ndefu, nyeupe"** Hii ni sitiari kwa "raha," "hali ya kubarikiwa" au "ushindi." Kwa baadhi ya tatizo la kitheolojia lililohusishwa hapa ni njisi gani roho isio na mwili ingeweza kuvaa vipande vya nguo. Kuwa mwangalifu na uhalisia wa kupita kiasi, hasa wakati unafasiri matukio ya kiyama ukweli kwamba hata watoa maoni wanajadili hili kuonyesha kiasi gani hawakuelewa namna ya uwasilishaji wa kitabu! Usifanye ili mradi liende katika Ufunuo!

◙ **"hata itakapotimia hesabu ya wajoli wao na ndugu zao, watakaouawa vile vile kama wao"** Moja ya ukweli muhimu wa kitabu hiki ni kwamba Mungu ni mwenye mamlaka ya kila kitu (kama vile Ufu. 6:8), hata kicho cha wakristo wafiadini! Historia zote ziko katika mikono yake. Mungu hashangazwi na matukio yoyote, matendo, au matokeo. Angali kuna maumivu bado, mateso na kutokuwa na haki katika ulimwengu huu ilioanguka. Kwa mjadala mzuri wa matatizo ya uovu angalia John W. Wenham's *The Goodness of God*.

Dhana hii ya hesabu iliyotimizwa ya wafiadini (kama vile I Enoch 47:4) ni njia ya kuashiria ya kurejelea kwa marifa ya Mungu na mpango kwa mwanadamu. Hii ni sawa sawa na dhna ya Paulo ya "ukamilifu wa mataifa" (kama vile Rum. 11:12,25) ambao unarejelea kwa maarifa ya Mungu ya mataifa yote ambayo watakobolewa.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 6:12-17**

**12 Nami nikaona, alipoifungua muhuri ya sita, palikuwa na tetemeko kuu la nchi; jua likawa jeusi kama gunia la singa, mwezi wote ukawa kama damu, 13 na nyota zikaanguka juu ya nchi kama vile mtini upukutishavyo mapooza yake, utikiswapo na upepo mwingi. 14 Mbingu zikaondolewa kama ukurasa ulivyokunjwa, na kila mlima na kisiwa kikahamishwa kutoka mahali pake. 15 Na wafalme wa dunia, na wakuu, na majemadari, na matajiri, na wenye nguvu, na kila mtumwa, na mwungwana, wakajificha katika pango na chini ya miamba ya milima, 16 wakiiambia milima na miamba, Tuangukieni, tusitirini, mbele za uso wake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na hasira ya Mwana-Kondoo. 17 Kwa maana siku iliyo kuu, ya hasira yao, imekuja; naye ni nani awezaye kusimama?**

**6:12"alipoifungua muhuri ya sita"** Aya hii ni lugha ya Wayahudi inayohusu matukio ya kiyama ya mwisho wa enzi (kama vile Yoeli 2:30-31; 3:15-16; Isa. 13:9,10; 34:4; Yer. 4:23-28; Hag. 2:6; Mt. 24:29; and *The Assumption of Moses*, 10:5). Angalia vifungu saba katika Ufu. 6:12-14. Lugha hii inatumika katika Agano la kale kwa siku ya Bwana. Inatumika hapa katika muhuri ya sita na baadaye katika baragumu ya sita ni sababu moja, naamini, kwamba kila moja ya mfululizo huu wa miisho saba na mwisho wa enzi, kuja kwa mara ya pili kwa Kristo (kama vile Ufu. 6:12-17; 11:15-18; 14:14-20; 16:17-21; 19:11-21; 22:6-16). Ufunuo sio utaratibu wa kufuatana kwa wakati na mahari. Ni matukio ya matendo saba.

◙**"palikuwa na tetemeko kuu la nchi"** Kuna matetemeko mengi yametajwa katka kitabu hiki (kama vile Ufu. 8:5; 11:13,19; 16:18). Inafuarahisha kutambua kwamba kuna vipengere saba kwenye mwisho huu, matukio ya siku ile ya mwisho. Pia kuna aina saba tofauti zimeorodheshwa katika Ufu. 6:15 (angalia Mada Maalumu: Hesabu ya ishara kwa maandiko katika Ufu. 1:4). Huu ni mfano mwingine wa mfumo ulioundwa, ufafanuzi wa kifasihi juu ya matukio ya siku ile ya mwisho (kama vile Ufu. 5:12).

◙ **"jua likawa jeusi. . . mwezi wote ukawa kama damu"** Hili ni dokezo la Agano la kale kwenye siku ya hukumu (kama vile Isa. 13:10; 24:23; 50:3; Eze. 32:7; Joel 2:2,10,31; 3:15; Mt. 24:29; Mk. 13:24-25; Lk. 21:25).

**6:13 "na nyota zikaanguka"** Sitiari hii inaweza kuwa na asili mbili:

1. Uthabiti wa utaratibu ulioundwa na Mungu (kama vile Ayubu. 38:31-33; Zab. 89:36-37; Isa. 13:10; Yer. 31:35-36; 37:20-26; Enoch 2:1) hulainisha hukumu za Mungu (kama vile Mt. 24:29)
2. Kuanguka kwa nyota ni sitiari ya kawaida ya Kiyama kwa kipindi kati ya agano la kale na agano jipya (ambayo kawaida inarejelea kwa malaika, yaani Ufu. 12:4; Dan. 8:10)

Katika muktadha huu # 1 inafaa zaidi.

**6:14 "Mbingu zikaondolewa"** Watu wa kale walitizama anga kama uwanja mgumu wa ngozi ilionyooshwa (kama vile Ayubu 22:14; Zab. 104:2; Mit. 8:27; Isa. 40:22). Hii ni sitiari ya kufungua Uungu katika utaratibu wa asili (kama vile Isa. 34:4).

◙**"na kila mlima na kisiwa kikahamishwa kutoka mahali pake"** Katika Agano la kale, wakati wowote Mungu alipotembelea uumbaji wake, ama kwa kubariki au kuhukumu, ilitetemeka. Maelezo mara nyingi yalijengwa kwa maneno ya kiyama. Ufu.15-17 inaelezea ghadhabu ya Mungu juu ya watesaji wasioamini (kama vile Ufu. 16:20). Maelezo haya sawa yanatumika katika Agano la kale kufanya upenyo wa kimwili kuufikia uwepo wa Mungu kirahisi, kama vile kuishusha milima, kuikausha mito, n.k. (kama vile Isa. 40:4).

**6:15 "wakajificha katika pango na chini ya miamba ya milima "** Kama Mungu alivyowateswa watu walipaswa kujificha kutoka kwenye mateso ya wasioamini (kama vile Ebr. 11:38), Hivyo sasa tajiri na wenye nguvu (yamkini ni dokezo kwa Zab. 2:2) wanatafuta kimbilio kutoka kwa ghadhabu ya Mungu (kama vile Isa. 2:10,19,21). Aya hii huelezea anguko la mwanadamu, asiyeamini katika njia saba. Matumizi haya ya namba saba ni mpangilio wa msingi katika kitabu cha Yohana (angalia Mada Maalumu katika Ufu. 1:4).

**6:16"Tuangukieni, tusitirini, mbele za uso wake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi "** Hili ni dokezo kwa Hosea 10:8 (kama vile Isa. 2:19,21 na Luka 23:30). Angalia kwamba ghadhabu ya Baba na Mwana ilihusishwa na masikitiko ya yale yanayotokea kwenye familia yao ya watu wa imani. Wanatenda katika historia kuthibitisha uaminifu na kuadhibu waasi (kama vile Gal. 6:7).

◙ **"na hasira ya Mwana-Kondoo"** Hii ni sitiari yenye mchanganyiko wenye nguvu. Picha hii ya Mwana-kondoo wa ushindi inatoka kwenye maandiko ya Kiyahudi kipindi kati ya agano la kale na agano jipya. Kwa neno“hasira”(*orgē*) tazama maelezo katika Ufu. 7:14.

**6:17** Aya ya 17 inaonekana kuwa na dokezo ama kwa Yoeli 2:11 au Mal. 3:2. Watoa maoni wengi wanaamini kwamba Ufu. 6:17 huweka hatua kwa kipindi cha mapumziko kinachopatikana katika sura ya 7, ambayo hujaribu kujibu swali, “Vipi kuhusu waaaminio ambao wapo duniani wakati wa matukio haya ya kiyama na mfululizo wa hukumu?” daima kuna majadiliano miongoni mwa watoa maoni kama muhuri katika Sura ya 6 ni ya ukombozi au ya haki (kama vile Ufu. 9:20-21; 14:7-8; 16:9,11). Sura ya 6 inarejerea kwa hukumu ya Mungu juu ya wasioamini ambao walikataa kuamini. Hukumu hizi zinaanza kuathiri 1/4 ya ulimwengu, kisha 1/3 na mwisho katika bakuli la ulimwengu mzima wa wasioamini (kama vile Sef. 1:14-18).

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA SURA YA 7:1-17

A. Aya ya 7 huunda kipindi cha ukimya kati ya muhuri ya sita na kufungua ile muhuri ya saba (kama vile Ufu. 8:1, kama iliyo Ufu. 10:1-11:13 kati ya baragumu ya sita na saba). Hii inajishughulisha na swali la kile kinatokea kwa waaminio wakati wa mzunguko huu wa hukumu ya Mungu juu ya wasioamini. Muhuri ya saba inakuwa baragumu saba.
B. Hiki kipindi cha ukimya kinajishughulisha na makundi mawili ya wale waaminio

1. Watu 144,000 kutoka katika makabila kumi na mbili duniani (kama vile Ufu. 7:1-8, hasa. Ufu. 7:4)
2. Wenyeji wasiohesabika kutoka katika makabila ya dunia nzima ambao sasa wapo mbinguni (kama vile Ufu. 7:9-17, hasa. Ufu. 7:9)

C. Mungu anatenda katika nguvu, kwa kukinga, kuthibtisha njia kwa niaba ya watu wake. Hakuna tofauti katika Ufunuo kati ya Wayahudi wanaoamini na mataifa (kama vile Rum. 2:28-29; 3:22; 1 Kor. 12:13; Gal. 3:28; Kol. 3:11). Tofauti za kimbali za Agano la kale zimewekwa ulimwenguni kwa waaminio na wasioamini.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 7:1-3**
**1 Baada ya hayo nikaona malaika wanne wamesimama katika pembe nne za nchi, wakizizuia pepo nne za nchi, upepo usivume juu ya nchi, wala juu ya bahari, wala juu ya mti wo wote. 2 Nikaona malaika mwingine, akipanda kutoka maawio ya jua, mwenye muhuri ya Mungu aliye hai; akawapigia kelele kwa sauti kuu wale malaika wanne waliopewa kuidhuru nchi na bahari, 3 akisema, Msiidhuru nchi, wala bahari, wala miti, hata tutakapokwisha kuwatia muhuri watumwa wa Mungu wetu juu ya vipaji vya nyuso zao.**

**7:1"nikaona malaika wanne. . . wamesimama katika pembe nne za nchi, wakizizuia pepo nne za nchi "** Katika Agano la kale uashiriaji wa namba nne unarejelea kwa dunia nzima (kama vile Isa. 11:12; Yer. 49:36; Dan. 7:2; Zek. 1:8; 6:1,5; Mt. 24:31, angalia Mada Maalumu katika Ufu. 1:4).

Kumekuwa na fasiri kadhaa za pepo hizi nne.
1. walimu wa sheria za Kiyahudi walitazama pepo za misimu kwa namna ya uovu (kama vile Mdo. 27:14)
2. Wengine huirejelea kama pepo za uovu au labda hukumu ya Mungu ya Yer. 49:36 na Dan. 7:2
3. Wengine huitazama kama dokezo kwa hesabu nne katika Zek. 1:8 na 6:5, ambapo wapanda farasi wane na wapanda farasi wanne ni watumwa wa Mungu ulimwenguni kote (kama vile Mt. 24:31)

◙ **"upepo usivume juu ya nchi, wala juu ya bahari, wala juu ya mti wo wote"** Hii, kama Ufu. 6:6 na 8, huonyesha hukumu zenye mipaka (kama vile Ufu. 7:3; 9:4).

**7:2 "Nikaona malaika mwingine, akipanda kutoka maawio ya jua"** Mashariki (jua) ilikuwa ishara ya uhai, afya, au siku mpya.

◙ **"mwenye muhuri ya Mungu aliye hai"** Muhuri ya Mungu unarejelea tena katika Ufu.9:4 na 14:1 na labda 22:4. Muhuri ya Shetani umetajwa katika Ufu.13:16; 14:9; na 20:4. Madhumuni ya mihuri hii ni kutambulisha watu wa Mungu ili kwamba ghadhabu ya Mungu haitawaathiri. Muhuri wa Shetani hutambulisha watu wake, ambao hupinga ghadhabu ya Mungu.
Katika Ufunuo neno "dhiki" (yaani, *thlipsis*) daima linamaanisha wasioamini kuwatesa waaminio, wakati ghadhabu (yaani, *orgē* or *thumos*) daima humaanisha hukumu ya Mungu juu ya wasioamini ili kwamba waweze kutubu na kurudi kwenye imani katika Kristo.Madhumuni haya mazuri ya hukumu yanaweza kuonekana katika laana za Agano/Baraka za Kum 27-28. Kifungu cha neno "Mungu aliye hai" ni dhihaka juu ya sifa ya YHWH (kama vile Kut. 3:14; Zab. 42:4; 84:2; Mt. 16:16, angalia Mada Maalumu katika Ufu. 1:8). Dhihaka ile ile mara nyingi inapatikana katika viapo vya kibiblia, "kama Bwana aishivyo."

### MADA MAALUM: MUHURI (SPECIAL TOPIC: SEAL)

◙ **"wale malaika wanne waliopewa kuidhuru nchi na bahari"** Hii ni KAULI TENDWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO USIOTIMILIFU. Mungu yu katika mamlaka ya hukumu juu ya dunia na wasioamini. Mipaka yake juu ya hukumu ina madhumuni mawili:
1. kwamba waaminio hawata umizwa na wao

2. kwa waasioamini wanapaswa kutubu, kumwita kwa jina lake, na kumpa utukufu (kama vile Ufu. 9:20-21; 14:6-7; 16:9,11; 21:7; 22:17)

**7:3 "hata tutakapokwisha kuwatia muhuri watumwa wa Mungu wetu juu ya vipaji vya nyuso za"** Hili ni dokezo kwa Eze. 9:4,6 (kama vile Ufu. 9:4; 14:1). Kinyume cha muhuri huu ni kutiwa muhuri na Shetani, alama ya mnyama (kama vile Ufu. 13:16,17; 14:9,11; 16:2; 19:20; 20:4).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 7:4**
4 **Nikasikia hesabu yao waliotiwa muhuri katika kila kabila ya Waisraeli, watu mia na arobaini na nne elfu**

**7:4 "mia na arobaini na nne elfu"** Kundi kama hili la ajabu limetajwa katika Ufu.14:1,3. Kumekuwepo na mijadala mingi kuhusu hii hesabu na nani inamwakilisha. Hesabu hii ni ishara, sio halisi, kwa sababu zifuatazo.

1. Tarakimu yenyewe ni hesabu ya jumla na makabila yote yana hesabu sawa (ambayo hawakuifanya katika Agano la kale)
2. Hesabu yenyewe ni kigawe cha kumi na mbili ambayo ni hesabu ya kibiblia ya ushirika (ama yawezekana hawa ni watu wa Mungu) na kumi, ambayo ni hesabu ya kibiblia ya utimilifu (angalia Mada Maalumu katika Ufu. 1:4)
3. Sura ya 7 iko kwenye lugha ya matukio ya siku za mwisho
4. Orodha ya makabila ya Waisraeli yalibadilishwa kidogo (Dani anaondolewa, na Efraimu inabadilishwa na Yusufu ).Wayahudi wangejua kwamba ilikuwa haimaanishi kuchukuliwa kihalisia.

Baadhi ya fasiri zilizowezekana za kundi hili zimekuwa:

1. Kwamba huenda wakawa Waisrael watakao amini siku ya mwisho (kama vile Zek. 12:10)
2. Kwamba wale waaminio wapya walioongoka watakaokuwepo baada ya unyakuo wa siri wa Kanisa
3. Kwamba ni yale mabaki ya waamini wa Kiyahudi (kama vile Warumi 11)
4. Kwamba ni wadhifa wa Kanisa la Agano Jipya (kama vile Ufu Rev. 1:6)

Utiwaji mhuri ulio katika Ufunuo haukuwekewa mipaka kwa kundi moja, isipokuwa hunawakilisha umiliki na ulizi wa Mungu wa watu Wake (kama vile 2:20; 11:18; 19:2,5; 22:36). Shetani huwatia muhuri wafuasi wake wote (kama vile 13:16,17; 14:9,11; 16:2; 19:20; 20:4), kumuiga Mungu (kama vile 3:12; 7:3; 14:1; 22:4).

Agano Jipya mara nyingi hulielezea Kanisa katika maneno ambayo yalitumika kwa Israeli (kama vile Rum. 2:28-29; 4:11; 9:6,8; Gal. 3:29; 6:16; Flp. 3:3) na hasa katika kitabu cha Ufunuo ambapo katika Ufu. 1:6 Kanisa linaelezewa na sifa iliyotumika kwa Israeli katika Kut. 19:4-6 (kama vile 1 Pet. 2:5,9). Katika kitabu cha Yakobo (kama vile 1:1) na 1 Petro (kama vile 1:1) Kanisa pia limeelezewa kama "kutawanyika kwa Wayahudi miongoni mwa watu wa mataifa" ni jina kwa wale Wayahudi waliotengana sana ambao walikuwa hawaishi katika Palestine.Inaonekana ni bora kwangu wakati huu katika utafiti wangu wa kitabu hiki kutambua watu 144,000 katika Ufu.7:4 na "kusanyiko kubwa sana" kwenye Ufu. 7:9 kama watu wa AJ wa Mungu—wale ambao wanamuamini Kristo, lakini walitazamwa katika maana mbili tofauti (Wayahudi wanaoamini na wa Mataifa wanaoamini).

## MADA MAALUM: THENASHARA/HESABU YA KUMI NA WAWILI (SPECIAL TOPIC: THE NUMBER TWELVE

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 7:5-8**
**5 Wa kabila ya Yuda kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri. Wa kabila ya Reubeni kumi na mbili elfu. Wa kabila ya Gadi kumi na mbili elfu. 6 Wa kabila ya Asheri kumi na mbili elfu. Wa kabila ya Naftali kumi na mbili elfu. Wa kabila ya Manase kumi na mbili elfu. 7 Wa kabila ya Simeoni kumi na mbili elfu. Wa kabila ya Lawi kumi na mbili elfu. Wa kabila ya Isakari kumi na mbili elfu. 8 Wa kabila ya Zabuloni kumi na mbili elfu. Wa kabila ya Yusufu kumi na mbili elfu. Wa kabila ya Benyamini kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri.**

**7:5"Wa kabila ya Yuda"** ille orodha ya makabila katika Ufu. 7:5 haikubaliani na orodha yo yote yenye zile nyongeza ishirini zilizopatikana katika Agano la Kale. Hasa hii haikubaliani na Eze. 48:2-7, ambayo iliorodhesha watu wa Mungu kwenye matukio ya ile siku ya mwisho. Kabila Dani anaondolewa, Yuda anaorodheshwa kwanza, Efraimu ameachwa, lakini Yusufu anaorodheshwa katika nafasi yake na Lawi anawekwa pamoja na makabila mengine. Myahudi ye yote angeweza kutambua kwamba orodha hii ni ile isiofuata kanuni na inamaanisha kuchukuliwa kiishara.

F. F. Bruce, *Answers to Questions*, uk. 139, anataja kwamba sababu ya Dani kuondolewa kutoka kwenye orodha desturi ya Kanisa hurejealea ile fasiri ya Irenaeus ya Yer. 8:16 katika yale Maandiko ya Agano la Kale ya Kiyunani yanasomeka:

> "Tunapaswa kusikia mlio wa farasi wake mwepesi nje ya Dani: ardhi yote ilitetemeka katika sauti ya mlio wa farasi wake: na anapaswa kuja, na kuteketeza ardhi na ukamilifu wake; mji, na wale wote waishio ndani yake."

Irenaeus aliuona ule ujio wa mpinga Kristo kama ujio wa kabila la Dani. Hili ni dhahanio tu, sio fasili ya maandiko!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 7:9-12**

**[9]Baada ya hayo nikaona, na tazama, mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha, wamesimama mbele ya kile kiti cha enzi, na mbele za Mwana-Kondoo, wamevikwa mavazi meupe, wana matawi ya mitende mikononi mwao; [10] wakilia kwa sauti kuu wakisema, Wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi, na Mwana-Kondoo. [11] Na malaika wote walikuwa wakisimama pande zote za kile kiti cha enzi, na za hao wazee, na za wale wenye uhai wanne, nao wakaanguka kifulifuli mbele ya kile kiti cha enzi, wakamsujudu Mungu, [12] wakisema, Amina; Baraka na utukufu na hekima na shukrani na heshima na uweza na nguvu zina Mungu wetu hata milele na milele. Amina.**

**7:9** Mkutano mkubwa sana ulitajwa katika aya hii ni tafauti ya wazi kutoka katika mia na arobaini na nne elfu ambayo metajwa katika Ufu. 7:4. Kama kundi la kwanza limekuja kutoka katika makabila tofauti ya duniani.Inaonekana kwamba haya makundi mawili yanawakilisha kundi lile lile la watu katika maana tofauti. Kama Ufu. 7:1-8 inarejelea kwa Wayahudi wanaoamini, basi Ufu. 7:9 inarejelea kwa watu wa Mungu wa watu wa makundi yote (kama vile Ufu. 5:9; 11:9; 13:7; 14:6; 17:15).
Hata hivyo, ukweli kwamba wao wanasema (1) wametoka katika dhiki ile iliyo kuu (kama vile Ufu. 7:14); (2) walisimama mbele ya kiti cha enzi (kama vile Ufu. 7:9); na (3) wamevikwa mavazi meupe (kama vile 6:11) wangeweza kuwatambua kama hesabu kamili ya wafiadini (kama vile Ufu. 6:11; 17:6; 18:24; 19:2; 20:4).

◙ **"ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu"** Hii inaweza kuwa dokezo kwa ahadi kwa Ibrahimu ya uzao mwingi.

1. mavumbi ya nchi – Mwa.13:16; 28:14; Hes. 23:10
2. nyota za mbinguni – Mwa. 15:5; 22:17; 26:4; Kumb. 1:10
3. mchanga ulioko pwani – Mwa. 22:17; 32:12
4. maelezo ya jumla – Mwa. 16:10

◙ **"wana matawi ya mitende mikononi mwao"** Baadhi walijaribu kutambua hili na Law. 23:40 au Neh. 8:15 kama ishara ya furaha na ushindi. Wengine walifananisha na taratibu za sikukuu ya Pasaka kama katika Yohana 12:13 na bado wengine, kwa sababu kifungu hiki kinaunganishwa na kipindi cha safari ndefu jangwani (kama vile Ufu. 7:15-16), na sikukuu ya mahema.Matawi ya mtende yanaweza tu kuwa ishara ya ushindi.

**7:10"Wokovu una Mungu wetu"** Hili ni neno la kawaida la Kiyunani kwa "wokovu" (*sōteria* from *sōzō*), lakini linaweza kutumika katika maana ya "ushindi" (NEB) au "kushinda kabisa." Kwa hiyo, inaweza kurejelea kwa (1) Ukombozi kutoka katika matatizo ya maisha duniani au (2) Kiroho, wokovu wa milele. Neno la Agano la kale

(*yasha*) lina maanisha ukombozi wa kimwili (kama vile Yakobo 5:15). Neno hili ni lile lile lililotumika katika mfululizo wa Baraka kwa Mungu mara tatu katika Ufunuo (kama vile Ufu. 7:10; 12:10; 19:1).

◙ **"na Mwana-Kondoo"** Angalia kwamba Masihi anabarikiwa kwa njia ile ile kama YHWH.Hii husisitiza asili ya Mungu ya Mwana.

**7:11** Tambua kwamba makundi kadhaa yemetofautishwa.

1. malaika
2. wazee
3. wale wenye uhai wanne

Makundi haya yote yamehusianishwa na kle kiti cha Enzi cha ufalme cha Mungu huko mbinguni. Haya yako tofauti na wale watu 144,000 na mkutano mkubwa.
Kwa neno "wazee" angalia MADA MAALUM: WAZEE (SPECIAL TOPIC: ELDER) katika Ufu. 4:4.

**7:12 "wakisema"** Angalia Baraka saba za Mungu zilizowekwa pamoja (na Masihi, kama vile Ufu. 7:10), ambazo ni sawa na Baraka saba ya Mwana Kondoo aliyechinjwa wa Ufu. 5:12.

◙ **"Amina"** Angalia jinsi inavyoanza na kuhitimisha juu ya baraka. Tazama Mada Maalumu katika Ufu.1:6.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 7:13-17**
**[13] Akajibu mmoja wa wale wazee akiniambia, Je! Watu hawa waliovikwa mavazi meupe ni akina nani? Na**
**wametoka wapi? [14] Nikamwambia, Bwana wangu, wajua wewe. Akaniambia, Hao ndio wanatoka katika dhiki**
**ile iliyo kuu, nao wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo.[15] Kwa hiyo**
**wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, nao wanamtumikia mchana na usiku katika hekalu lake, na yeye**
**aketiye katika kiti cha enzi atatanda hema yake juu yao. [16] Hawataona njaa tena, wala hawataona kiu tena,**
**wala jua halitawapiga, wala hari iliyo yote.[17] Kwa maana huyo Mwana-Kondoo, aliye katikati ya kiti cha enzi,**
**atawachunga, naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhai, na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao.**

**7:14"Nikamwambia, Bwana wangu, wajua wewe"** Huu ni mwitikio wa kawaida la binadamu kwa wajumbe kimalaika (kama vile Zek. 4:5,13; Dan. 10:16), ambao huimarisha utambulisho wa wazee na kundi la malaika wenye uhai.
Fasihi ya matukio ya siku za mwisho inabainishwa na upatanisho wa kimalaika na fasiri. Fasiri hizi zinakuwa za muhimu (kama nyimbo za kwaya) katika kufafanua na kuelewa lugha ya ishara.

◙**"Hao ndio wanatoka katika dhiki ile iliyo kuu"** Hii ni KAULI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO na ni dokezo kwa makanisa yaliyoteswa katika siku ya Yohana (kama vile Ufu. 1:9; 2:9,10,22). Hata hivyo, ni dhahiri kwamba dokezo la kihistoria katika Ufunuo linaeleza yale mateso ya watakatifu katika kila enzi na pia kuonyesha mkazo wa wakati wa mwisho wa mateso (kama vile Dan. 12:1). Hii inahusiana na

1. yale mateso ya watoto wa Mungu (kama vile Mt. 24:21-22; Mk. 13:19; 2 The. 2:3 na kuendelea; Ufu. 2:10; Dan. 12:1)
2. ujio wa ghadhabu ya Mungu juu ya wasioamini (kama vile 2 The. 1:6-9; Ufu. 3:10; 6:17; 8:2 na kuendelea; 16:1 na kuendelea)

Matatizo haya, kwa kiasi fulani, yamehusishwa na kila enzi. Wakristo wamekuwa wakiteseka mara nyingi kwa jina la Yesu (kama vile Yohana16:33; Mdo. 14:22; Rum. 5:3; 1 Pet. 4:12-16). Matukio haya yote mara nyingi yaliiitwa uchungu wa kuzaa wa enzi mpya ya haki (kama vile Marko 13:8 na kitabu cha kubuniwa cha II Baruch, sura ya 25-30).
Neno la Kiyunani *thlipsis* (dhiki) katika Ufunuo daima hutumiwa na waaminio wanaoteseka kwa mkono wa wasioamini (kama vile Ufu. 1:9; 2:9,10,22; 7:14). Maneno ya Kiyunani *thumos* (kama vile Ufu. 12:12; 14:8,10,19;

15:1,7; 16:1; 18:3; 19:15) na *orgē* (kama vile Ufu. 6:16,17; 11:18; 14:10; 16:19; 19:15) daima hutumiwa kwa Baba au ghadhabu ya Mwana juu ya uasi, wale wakaidi wasioamini.

Kwa namna nyingine ya kitheolojia, ikiwa kitabu kiliandikwa kuwatia moyo waaminio waliopitia kwenye dhiki, Je! Kwa nini baadhi ya wafasiri wanasisitiza juu ya siri ya kuwa na shauku kwa kusamehe baadhi ya kizazi cha baadaye kwa mateso ya waaminio? Mateso yalikuwa mengi kwa viongozi wa kwanza wa Kanisa, na kila kizazi cha waaminio. Je! Kwa nini basi kundi moja la baadaye linapaswa kusamehewa?

◙ **"nao wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo"** Hii inavyoonekana inarejelea kwa wafiadini ambao walikufa kwa imani yao katika Kristo wakati wa dhiki ile iliyo kuu. Ni sitiari ya kuvutia ya ukombozi (kama vile Ufu. 22:14)! Wazo hili la kutakasa kwa njia ya dhabihu ya kifo cha Kristo linaweza kuonekana katika Rum. 3:25; 5:9; 2 Kor. 5:21; Efe. 1:7; Kol. 1:20; Ebr. 9:14; 1 Pet. 1:19; na 1 Yohana 1:7. Ukweli wa msalaba mara nyingi umetajwa katika Ufunuo (kama vile Ufu. 1:5; 5:12; 7:14; 12:11; 13:8; 14:4; 15:3; 19:7; 21:9,23; 22:3). Tazama mpangilio wa utoaji wa Kristo na uhitaji wa mwanadamu kuitikia kwenye wito wa Mungu. Kipengele cha kimaagano cha maagano yote huonyesha uanzilishaji na utoaji wa Mungu, lakini Mungu mwenye nguvu amechagua pia kwamba binadamu walioanguka wanapaswa kuitikia (kama vile Yohana 1:12; Mk. 1:15; Mdo. 3:16,19; 20:21; Rum. 10:9-13).

**7:15-16** Wakati wa baadaye wa furaha kamili na amani ya mbinguni umeelezewa katika maneno ya Agano la kale, hili ni dokezo kwa kipindi cha safari ndefu ya jangwani na mahali pa hema la kukutanikia (kama vile Kut. 40:34-38; Hes. 9:15-23). Ni dokezo la ziada kwa wingu la *Shekinah* la utukufu, ambalo linaashiria uwepo wa Mungu na watu (kama vile Isa. 49:10; Mt. 5:6; Yohana 4:14; 6:35; 7:37). Kipindi hiki cha historia ya Waisraeli kweli kilikuwa kipindi cha hukumu. Hata hivyo, YHWH hakuwa karibu na angalifu zaidi kuliko kipindi hiki cha hukumu. Mara nyingi inarejelewa na walimu wa sheria za Kiyahudi kama YHWH na fungate la Waisraeli

**7:15"nao wanamtumikia mchana na usiku"** Katika Agano la kale hii inarejelea kwa makuhani wa kilawi (kama vile Zab. 134:1; 1 Nya. 9:33). Njia ya kufikia kwa Mungu na huduma ya Mungu imepanuliwa kwa (1) waaminio walioteswa na (2) waaminio wote. Hakuna tena ukuhani wa wasomi wa Kiyahudi (kama vile 1 Pet. 2:5,9; Ufu. 1:6). Kifungu cha neno "mchana na usiku" ni sitiari ya mwendelezo. Hupatikana mara kadhaa katika Ufunuo (kama vile Ufu. 4:8; 7:15; 12:10; 14:11; 20:10).

◙ **"katika hekalu lake"** Ni vigumu kwa kiasi Fulani kuhusisha kifungu hiki (na Ezekieli 40-48) na Ufu. 21:22 ambacho husema hakutakuwepo na hekalu mbinguni. Wengine wamejaribu kufanya utofauti kati ya miaka elfu ya utawala wa Kristo wa dunia hii na utawala wa milele. Dhahiri, sitiari na kiunzi cha wakati katika kitabu hiki kinaleta sintofahamu. Hii inaweza kurejelea juu ya hema la kiroho mbinguni (kama vile Ebr. 9:23).

◙ **"atatanda hema yake juu yao"** Hii ni sitiari ya maneno ya Mungu yaishio ndani ya watu wake. Hema la Mungu huwakilisha uwepo wake wa kudumu na watu wake wapya kutoka kila ukoo na kabila.Madhumuni ya mwanzo ya bustani ya edeni yamerejeshwa.Ubinadamu umekobolewa (kama vile Mwa. 3:15). Ushirika wa ndani na Mungu unawezekana tena (yaani, Mwa. 3:8).

**7:16-17** Hizi ni baraka (kutoka katika Agano la kale) kwa waaminio wote, sio tu wafiadini.

**7:16"Hawataona njaa tena, wala hawataona kiu tena"** Aya ya 16 ni dokezo kwa Isa. 49:10-13. Utoaji wa Mungu juu ya mambo ya kimwili unatumika kama ishara ya utoaji wa Mungu juu ya mambo ya kiroho (kama vile Mt. 5:6; Yohana4:14; 6:35; 7:37).

◙ **"wala jua halitawapiga, wala hari iliyo yote"** Hili ni dokezo kwenye kivuli kilichotolewa na wingu la *Shekinah* la utukufu wakati wa miaka 38 ya safari ndefu ya kutangatanga jangwani (kama vile Zab. 121:5-7).

**7:17"Kwa maana huyo Mwana-Kondoo, aliye katikati ya kiti cha enzi, atawachunga "** Hili ni dokezo la Agano la kale kwa Eze. 34:23. Tazama kwamba aliyeuawa lakini akafufuliwa kama mwokozi akawa ndiye kiini cha shughuli ya ukombozi wa Mungu. Mchungaji mzuri katika Yohana 10:11 sasa ni mchungaji wa kondoo wote (kama vile Yohana 10:16).

◙ **"naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhai"** maji ya watu wa jangwani siku zote yamekuwa kama ishara ya utosherevu na uzima. Hili ni dokezo kwa Isa. 49:10 (kama vile Zab. 23:2), ambalo limerudiwa mwisho wa kitabu katika Ufu. 21:6; 22:1.

◙ **"na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao"** Hili ni dokezo kwa dhifa ya kimasihi na mji mpya wa Mungu katika Isa. 25:6-9 (kama vile Ufu. 21:4). Ni faraja namna gani ingalipaswa kuwa kwa wale waaminio walioteswa siku ya Yohana na kila enzi!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa masomo ya fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri za Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika nuru tuliyonayo. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa ili kukusaidia kufikiri mambo muhimu yaliyoko katika kipengele cha kitabu hiki. Yamekusudiwa kukuchokonoa kiakili na si kutoa maana ya kuhitimisha.

1. Je! Watu 144,000 ni watu gani? Elezea jibu lako kutoka katika maandiko ya Ufunuo.
2. Je! Ni kwa jinsi gani watu 144,000 wanahusiana na kundi kubwa katika Ufu. 7:9?
3. Je! Kwa nini ishara hizi ni ngumu sana kwetu sisi kuzifasiri?
4. Je! Ni pigo gani kuu la sura ya 6 na 7?
5. Je! Ina maana gani wakati inasemwa kwamba sura ya 7 ni kipindi cha mapumziko?Je!Kipindi kingine cha mapumziko kinapatikaa wapi katika kitabu?

# UFUNUO 8:1-9:21

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Mihuri saba na chetezo ya dhahabu | Muhuri wa saba: umezitangulia zile baragumu saba | Muhuri wa saba | Muhuri wa saba | Muhuri wa saba |
| 8:1-2 | 8:1-6 | 8:1-2 | 8:1-2 | 8:1<br>Maombi ya watakatifu yanaleta kuja kwa ile siku kuu karibu sana<br>8:2-5 |
| 8:3-5<br>Baragumu | | 8:3-5<br>Baragumu ya sita | 8:3-5<br>Baragumu | Baragumu nne za kwanza |
| 8:6 | Baragumu sita za kwanza | 8:6 | 8:6 | 8:6-12 |
| 8:7 | 8:7<br>Baragumu ya pili: Muhuri umepigwa | 8:7 | 8:7 | |
| 8:8-9 | 8:8-9<br>Baragumu ya tatu: Maji yamepigwa | 8:8-9 | 8:8-9 | |
| 8:10-11 | 8:10-11<br>Baragumu ya nne: Mbingu zimepigwa | 8:10-11 | 8:10-11 | |
| 8:12 | 8:12 | 8:12 | 8:12 | |
| 8:13-9:6 | 8:13<br>Baragumu ya tano: nzige kutoka shimo lisilo na mwisho | 8:13<br>Pigo la nzige wa Kimapepo | 8:13 | 8:13<br>Baragumu ya tano |
| | 9:1-12 | 9:1-6 | 9:1-6 | 9:1-6 |
| 9:7-11 | | 9:7-11 | 9:7-11 | 9:7-11 |
| 9:12 | Baragumu ya sita: Malaika kutoka Frati | 9:12 | 9:12 | 9:12 |
| 9:13-19 | 9:13-19 | 9:13-19 | 9:13-19 | 9:13-19 |
| 9:20-21 | | 9:20-21 | 9:20-21 | |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** **"Kutoka. Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia"("A Guide to Good Bible Reading")**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA.*

Huu ni mwongozo wa usomaji wa fasiri, ambayo inamaanisha kwamba unao wajibika kwa ukalimani wako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu lazima aenende katika nuru tuliyo nayo. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika ukalimanii. Hutakiwi kumuachia vitu hivi mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Yatambue masomo. Linganisha mgawanyiko wa mada zako kwa ulinganifu wa tafsiri tano za hapo juu. Aya haijavuviwa, lakini ni ufunguo wa kufuata kusudi la msingi wa mwandishi, ambao ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya inayo moja na katika hilo ni somo moja tu.

5. Aya ya kwanza
6. Aya ya pili
7. Aya ya tatu,

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA 8:1-9:21

A. Kama baragumu saba zinavyoendelea kutoka kwenye Mihuri saba, swali ni, "Ni uhusiano upi uliopo kati ya baragumu, muhuri na bakuli?" Kuna sehemu, kama sio yote inayojirudia kwa muhtasari. Vinatimiza muda ule ule wa kipindi chote. Vimejengwa kwa mpangilio huo huo na vinafuatana kimoja baada ya kingine. Sehemu ya nadharia inayojirudia kwa muhtasari inaonekana kuwa imeendelezwa kwenye karne ya tatu na Victorinus wa Pettau (tazama *The Ante-Nicene Fathers*, vol. 7, kr. 344-360). Anataja tu uhusiano sambamba kati ya baragumu na bakuli. Mtu anapolinganisha hivyo vitatu, vyaonekana kuwa ni matukio ya siku ya mwisho, sitiari zenye mwendelezo wa maangamizo ya kipindi kile kile cha matukio ya siku za mwisho. Yawezekana kabisa kwamba jinsi muhuri wa sita (kama vile Ufu. 6:12-17) unavyotufikisha kwenye mwisho, baragumu ya saba (kama vile Ufu. 11:15-19) pamoja na bakuli saba (kama vile Ufu.16:L17-21) vinafafanua matukio ya mwisho.
B. Ni kutoka wapi Yohana anapata picha zake za maono yahusuyo matukio ya siku ya mwisho? Kuna nadharia kadhaa:
   1. Kuna vidokezo kwenye vifungu kadhaa katika Agano la Kale, hasa katika sura ya 3 na 9, kwa mapigo ya Misri na kwa uvaamizi wa nzige katika Yoeli 2. Kama ilivyo kila wakati katika Ufunuo, matumizi ya lugha ya picha kwa Danieli, Ezekieli na Zakaria huunda msingi wa historia
   2. Maandishi ya Kiyahudi juu ya matukio ya kiyama kipindi kati ya agano la kale na agano jipya, kama 1 Enoki. I Enoki kilijulikana sana kwenye karne ya kwanza ya Kiyahudi, vile vile pia katika kanisa na ilidokezwa na waandishi wa Agano jipya ( kama vile 2 Petro 2 na Yuda).
   3. Mapangilio wa kihistoria wa karne ya kwanza, hasa kuabudiwa kwa Mfalme mkuu wa Warumi na mateso ya mahali.

   Chaguo tunalochagua, kama chanzo kikuu cha mifano ya kufikirika itaamua jinsi tunavyofasiri sura hizi mbili. Ikiwa tutaliona hili dhidi ya historia ya ufalme wa Rumi, tutafaa katika historia ya Warumi (wale wenye kuamini kuwa matukio ya siku ya mwisho yameisha timia[preterist). Ikiwa tutaliona hili dhidi ya lugha ya Kiyahudi kuhusu matukio ya siku ya mwisho, itakuwa na uwezekano zaidi kwa kuifasiri kama ishara (wale wenye kulindwa na nadhalia kuliko uhalisia[idealist). Ikiwa tutaliona hili dhidi ya manabii wa Agano la kale, tutakisanifu katika mpangilio wa Kiyunani wa siku za mwisho (wale wenye kuongozwa na matukio ya siku za baadaye).
C. Sura hizi mbili huelezea hukumu inayozidi kuongezeka kwa waaminio. Hata hivyo, lazima isisitizwe kwamba Mungu huleta hukumu juu yao kwa kusudi la ukombozi wao (kam vile Ufu. 9:20-21; 14:7; 16:9,11). Kwa hiyo, zinafanya kazi kama laana za kimaagano katika Kumbukumbu 27-29.
D. Kama ilivyo katika sura zilizotangulia, uashiriaji unakuwa usio wa wazi kiasi kwamba watoa maoni baadhi hudhani ni Kristo, wengine hudhani ni Shetani. Kwa aina hiyo ya siontofahamu ya uasilishaji, kulazimisha imani haifai kabisa. Wafasiri wanapaswa kutoa muhtasari wa maono kamili kwenye kweli moja. Kweli kuu lazima iongoze tafsiri ya maelezo na kubaki kuwa suala kuu la kusisitizwa kitheolojia!

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): UFUNUO 8:1-2**
**[1] Hata alipoifungua muhuri ya saba, kukawa kimya mbinguni kama muda wa nusu saa. [2] Nami nikawaona wale malaika saba wasimamao mbele za Mungu, nao wakapewa baragumu saba.**

**8:1"Hata alipoifungua muhuri ya saba"** Yesu ndiye atakaye fungua muhuri wa saba, lakini kutokana na hili la malaika wao nao watahusika katika kutangaza baragumu saba na baadaye bakuli saba.

◙ **"kukawa kimya mbinguni kama muda wa nusu saa"** Kumekuwa na nadharia kadhaa kuhusu ukimya huu. Walimu wa sheria za Kiyahudi wanahusisha hili na kipindi cha ukimya kuruhusu maombi ya watakatifu kusikilizwa

1. Baadhi wanahusisha na kitabu cha II Esdras 7:29-31, ambapo ukimya ni mwanzo wa enzi mpya
2. Wengine wanahusisha na vifungu kadhaa vya Agano la kale wakati wanadamu watakuwa kimya katika uwepo unaokuja wa Mungu (kama vile Hab. 2:20; Sef. 1:7; Zek. 2:13)
3. Wengine wanahusisha na athari ya matukio ya kuvutia ya kuja kwa hukumu kali sana juu ya wasioamini
4. Victorinus alihusisha na mwanzo wa milele

**8:2"Nami nikawaona wale malaika saba wasimamao mbele za Mungu"** Inavutia kwamba KIBAINISHI CHENYE UKOMO kimeonekana, "malaika saba." Katika sheria za kiyahudi uwepo wa malaika saba umetajwa katika Tobit 12:15; Jubilii 1:27,29; 2:1-2,18; na I Enoki 20:1-7. Wao ni Urieli, Rafaeli, Ragueli, Mikaeli, Sarakaeli au Sarieli, Gabrieli, and Remieli. Wengine wanaona kifungu hiki kuhusishwa na Masihi (sambamba na "Malaika wa uwepo wake ") katika Isa. 63:9 au kwa hukumu juu ya wale walioasi na kumhuzunisha Roho Mtakatifu (kama vile Isa. 63:10). Uhusiano wa safari kutoka Misri unaweza kuonekana kwa malaika katika Kut. 23:20-23; 33:12-16.

◙ **"nao wakapewa baragumu saba"** Kuna malaika Saba wanaoendana na baragumu saba (kama vile Ufu. 8:6). Katika baragumu za Agano la kale mara nyingi yalitumika kwa kuwasiliana na watu wa Mungu, ama kidini au kijeshi (kama vile Kut. 19:16; Hes. 10:1-10; Isa. 27:13; Yer. 4:5-9; YoelI 2:1; Sef. 1:16; Zek. 9:14; II Esdras 6:23, tazama Mada Maalumu katika Ufu. 1:10). Katika Agano jipya baragumu litatangaza kuja kwa mara pili kwa Yesu (kama vile. Mt.24:31; 1 Kor. 15:52-53; 1 The. 4:16).

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): UFUNUO 8:3-5**
**3 Na malaika mwingine akaja akasimama mbele ya madhabahu, mwenye chetezo cha dhahabu, akapewa uvumba mwingi, ili autie pamoja na maombi ya watakatifu wote juu ya madhabahu ya dhahabu, iliyo mbele ya kiti cha enzi. 4 Na moshi wa ule uvumba ukapanda mbele za Mungu pamoja na maombi ya watakatifu, kutoka mkononi mwa malaika. 5 Na huyo malaika akakitwaa kile chetezo, akakijaza moto wa madhabahu, akautupa juu ya nchi, kukawa radi na sauti na umeme na tetemeko la nchi.**

**8:3"Na malaika mwingine akaja akasimama mbele ya madhabahu, mwenye chetezo cha dhahabu "** Maandishi haya na 5:8 yametumika kuendeleza dhana ya kitheolojia ya walimu wa sheria za Kiyahudi kwamba malaika ndio wabebao maombi kuyapeleka kwa Mungu.Biblia imekaa kimya juu ya jinsi gani ya kufasiri aina hii ya maelezo.Vifungu hivi vya kiishara havipaswi kutumika kufafanua maelezo ya kuthibitisha kitheolojia. Haya ni maono na hayamaanishi kuelezea shughuli za malaika fulani.Inathibitisha kwamba maombi ya watakatifu humgusa Mungu.

Madhabahu yametambulishwa kama madhabahu ya uvumba mbele ya pazia katika mahali patakatifu (kama vile Kut. 30:1-10) au madhabahu ya dhabihu (kama vile Ufu. 8:5; 9:13). Hata hivyo, maono haya sio hema la kidunia au hekalu katika Yerusalemu, lakini chumba cha kiti cha enzi cha Mungu mbinguni (kama ville Ebr. 8:2; 9:11,24). Uvumba wa madhabau unafaa muktadha huu zaidi.

◙**"maombi ya watakatifu wote "** hakuna hakika ni kundi lipi la watakatifu kundi hili huwawakilisha kwalo, lakini hii inaonyesha kwamba Mungu anajua na anajibu mahitaji ya watu wake (kam avile Kut. 3:7). Uvumba ulikuwa ni ishara ya maombi (kama vile Zab. 141:2; Ufu. 5:8) kwa sababu moshi ulipaa juu na kutoweka kwenye ulimwengu unaoonekana kwenda kwenye ulimwengu usioonekana.

Kwa "**watakatifu**" tazama MADA MAALUMU: WATAKATIFU (SPECIAL TOPIC: SAINTS) katika Ufu.5:8.

**8:4** katika kitabu chote cha Walawi uvumba ulipaa hadi kwenye uwepo wa Mungu, kwa hiyo, uvumba ulikuja kuwakilisha maombi ya watu wa Mungu.

**8:5"Na huyo malaika akakitwaa kile chetezo, akakijaza moto wa madhabahu, akautupa juu ya nchi "** Hili ni dokezo kwa Ezek. 10:2. Mkaa kwa ajili ya madhabahu ya uvumba mbele ya pazia mwanzoni yangalichukuliwa toka kwenye madhabahu ya kutolea dhabihu mbele ya hema ya kukutanikia (kama vile Ufu. 9:13; Law. 16:11-13). Hizi ni ishara za hema ambazo maana yake haifahamiki. Wazo kuu la Kitheolojia ni kwamba hili linatendeka mbele ya Mungu wa Mbinguni.

◙ **"kukawa radi"** Aina hizi za matukio ya ajabu mara nyingi yalihiusishwa na uwepo wa YHWH (kama vile Ufu. 4:5; 11:19; 16:18; Kut. 19:16-19; Zab. 18:10-13).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 8:6**
**6 Na wale malaika saba wenye baragumu saba wakajifanya tayari ili wazipige.**

**8:1-6** Aya hizi zinawakilisha matendo wakati wa kipindi cha ukimya.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 8:7**
**7 Malaika wa kwanza akapiga baragumu, kukawa mvua ya mawe na moto vilivyotangamana na damu, vikatupwa juu ya nchi; theluthi ya nchi ikateketea, na theluthi ya miti ikateketea, na majani mabichi yote yakateketea.**

**8:7"kukawa mvua ya mawe na moto vilivyotangamana na damu"** Kiasi kikubwa cha matumizi ya lugha picha kimetolewa kutoka katika mapigo ya Misri. Hiki kifungu ni dokezo kwa Kut. 9:24. Pia inawezekana kwamba hii imetolewa kutoka katika Ezek. 38:22, kupinduliwa kwa majeshi ya Gogu yaliyoshambulia.

◙**"theluthi ya nchi ikateketea"** Hii asilimia ndogo, lakini yenye ukweli imetajwa mara nyingi sana katika sura chache zifuatazo (kama vile Ufu. 8:7-8,9,10,11,12; 9:15,18; 12:4). Mfululizo wa pili wa hukumu ni wenye nguvu zaidi kuliko wa kwanza (kama vile 6:8, ambapo robo imetamkwa). YHWH bado anajaribu kuwafikia wanadamu wenye dhambi kwa njia ya mapigo ya kimwili (kama vile Kutoka 7-11; Kumbukumbu 28-29), lakini hawakuweza kuitikia kwenye toba na imani!

◙ **"na majani mabichi yote yakateketea"** Hii inapaswa kurejelea kwenye maagamizi ya majani mabichi yote ndani ya theluthi moja ya eneo, kwa sababu majani mabichi yanalindwa katika Ufu. 9:4.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBOREHWA): UFUNUO 8:8-9**
**8 Malaika wa pili akapiga baragumu, na kitu, mfano wa mlima mkubwa uwakao moto, kikatupwa katika bahari; theluthi ya bahari ikawa damu. 9 Wakafa theluthi ya viumbe vilivyomo baharini, vyenye uhai; theluthi ya merikebu zikaharibiwa.**

**8:8"mfano wa mlima mkubwa uwakao moto, kikatupwa katika bahari"** Kwa mara nyingine tena suala hili ni chanzo cha taswira ya Yohana— Warumi, kipindi cha Wayahudi kati ya agano la kale na agano jipya, au Agano jipya.

1. Ikiwa ni Agano la kale, kisha Zab.46:2 au Kut. 7:20-21 ni rejeo.
2. Ikiwa kiyama ya Wayahudi, basi rejeo ni I Enoki 18:13-16 au yumkini katika kitabu cha Sibylline Oracle 5:158.
3. Ikiwa ni Warumi basi yawezekana ni dokezo la kihistoria ya kulipuka kwa Mlima Vesuvius, ambao Wayahudi walifasiri kama hukumu ya Mungu juu ya Rumi kwa kuangamiza Yerusalemu.

Chanzo halisi cha sitiari ya Yohana hakina uhakika, bali wanasema juu ya ghadhabu ya Mungu kwenye uumbaji wenye uasi na kusudi la ukombozi katika fikra.

◙ **"theluthi ya bahari ikawa damu"** Hili ni dokezo lingine la mapigo kwa Wamisri (kama vile Kut. 7:20-21).

**8:9 "theluthi ya viumbe. . . Wakafa "** Hili ni dokezo lingine kwa mapigo kwa Wamisri (kama vile Kut. 7:21).

◙ **"theluthi ya merikebu zikaharibiwa"** Hii haina ufanano katika Agano la kale, katika maandiko juu ya matukio ya siku ya mwisho, au katika maandiko ya Kirumi ya karne ya kwanza. Ni dhahiri tunaona biashara ikiathiriwa, na bidhaa na chakula vingekuwa adimu.Huthibitisha hukumu ya Mungu endelevu isiyo na kikomo. Hukumu yake huzidishwa (1/4 kwenye muhuri, 1/3 kwenye baragumu) hadi kwenye bakuli mpaka muda wa toba utimie ndipo ile hukumu itokee.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 8:10-11**
**[10] Malaika wa tatu akapiga baragumu, nyota kubwa ikaanguka kutoka mbinguni, iliyokuwa ikiwaka kama taa, ikaanguka juu ya theluthi ya mito, na juu ya chemchemi za maji. [11] Na jina lake ile nyota yaitwa Pakanga; theluthi ya maji ikawa pakanga, na wanadamu wengi wakafa kwa maji hayo, kwa kuwa yalitiwa uchungu.**

**8:10"nyota kubwa ikaanguka kutoka mbinguni"** Hii inaeleza juu ya dokezo kwenye Isa. 14:12. Wengi walijaribu kuhusisha hili na Ufu. 6:13 au 9:1, lakini hii inaweza kujaribu kufunga lugha ya picha ya Yohana yenye kubana sana, jihadhari na kujaribu kufasiri yote na kila maelezo. Hii ni picha ya uandishi wa mawazo ya kufukirika wenye kuchangamsha na kuvutia. Hii ki-tamthilia ni lugha ya picha.Kawaida katika fasihi ya Wayahudi ya matukio ya siku ya mwisho kuanguka kwa nyota kunarejelea kwa malaika (yaani 9:1).

**8:11 "Na jina lake ile nyota yaitwa Pakanga"** Katika Agano la kale pakanga inahusishwa na ibada ya sanamu (kama vile Kumb. 29:17-18). Inaonekana pia kama imechanganywa na sumu na ndivyo, kwa hiyo, inauwa (kama vile Yer. 9:15; 23:15; Amosi 6:12). Pakanga, kwa yenyewe (kama vile TEV), ilikuwa chungu lakini sio yenye kusababisha mauti. Hapa ni sitiari kwa hukumu ya Mungu.

Mfano mzuri usiofaa kwa watu wa leo ni kulazimisha habari za ufunuo wa nyakati zao kuonyesha kwamba mtambo wa kinyuklia wa Chernobyl wa Warusi uliopata tatizo la kuvujisha sumu ulitimiliza unabii kwa sababu jina hilo lilimaanisha pakanga katika lugha ya Kirusi. Kitendo hiki cha kufasiri biblia kilichohusianishwa na gazeti la asubuhi kimekuwa cha kawaida katika miaka yote elfu mbili na inapaswa kutuonya kuwa waangalifu kwa utaratibu wa namna hiyo!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHBWA): UFUNUO 8:12**
**[12] Malaika wa nne akapiga baragumu, theluthi ya jua ikapigwa, na theluthi ya mwezi, na theluthi ya nyota, ili kwamba ile theluthi itiwe giza, mchana usiangaze theluthi yake, wala usiku vivyo hivyo.**

**8:12** Giza daima limekuwa ishara ya hukumu ya Mungu (kama vile Kut. 10:21; Isa. 13:10; 34:4; 50:3; Ezek. 32:7-8; Yoeli 2:2,10,31; 3:15; Amosi 5:18; Marko 13:24). Miili ya mbingu mara nyingi iliabudiwa kama nguvu za kiroho. Mungu aliwaumba (kama vile Mwa. 1:14-19; Isa. 40:26); na kuwapa majina (kama vile Zab. 147:4; Isa. 40:26); anawatawala (kama vile Isa. 48:13); na wanamtukuza Yeye (kama vile Zab. 148:3).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 8:13**
**[13] Kisha nikaona, nikasikia tai mmoja akiruka katikati ya mbingu, akisema kwa sauti kuu, Ole, ole, ole wao wakaao juu ya nchi! Kwa sababu ya sauti zisaliazo za baragumu za malaika watatu, walio tayari kupiga.**

**8:13 " Kisha nikaona, nikasikia tai mmoja akiruka katikati ya mbingu, akisema "**Toleo la KJV ina neno "malaika" badala ya "tai" lakini hili linakuja kutoka kwenye maandishi ya Kiyunani ya mwishoni mwa karne ya tisa. Machapisho yote mawili yaliotolewa katika vitabu vya Sinai (א) na Alexandrinus (A) yana neno "tai." Hii inaweza

kurejelea kwa: tai, ambayo mara nyingi ilikuwa ishara ya kuchinja (kama vile Ezek. 17:3; Hab. 1:8; Mt. 24:28; Lk17:37)

1. Dokezo kwenye mandhari ya hukumu katika Ezek. 39:17-20; Hos. 8:1
2. Dokezo kwenye kitabu chenye matukio ya kiyama kipindi kati ya agano la kale na agano jipya cha II Baruch 77:21-22, ambayo tai hutuma ujumbe kwa watu wa Mungu wanaoteseka
3. Viwango vya jeshi la Warumi ambavyo vimewekewa tai upande juu

Neno "kuruka katikati ya mbingu" labda ni dokezo lingine kwa ndege wanaowinda wakipaa angani juu ya nchi (kam avile Ufu. 14:6; 19:17).

◙**"Ole, ole, ole"** yumkini hii inafanana na baragumu tatu za mwisho ambazo zinakuja (kama vile Ufu. 9:12; 11:14; 12:12); inaweza pia kuwa ishara ya nguvu nyingi (kama, mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu" kwa Ufu. 4:8). Katika Kiebrania kurudia rudia kitu mara tatu ni SIFA YA JUU KABISA (kama vile Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu kwa Isa. 6:3). Katika Agano la kale neno "ole" linaweka alama ya ombolezo mahsusi la kishairi likihusishwa na kifo pamoja na hukumu.

◙ **"wao wakaao juu ya nchi"** kifungu hiki kinarejelea kwa wasiokombolewa (kama vile Ufu. 3:10; 6:10; 11:10; 13:8; 17:2).

# UFUNUO 9

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 9:1-6**

**[1] Malaika wa tano akapiga baragumu, nikaona nyota iliyotoka mbinguni, imeanguka juu ya nchi; naye akapewa ufunguo wa shimo la kuzimu. [2] Akalifungua shimo la kuzimu; moshi ukapanda kutoka mle shimoni kama moshi wa tanuru kubwa; jua na anga vikatiwa giza kwa sababu ya ule moshi wa shimoni. [3] Nzige wakatoka katika ule moshi, wakaenda juu ya nchi, wakapewa nguvu kama nguvu waliyo nayo nge wa nchi. [4] Wakaambiwa wasiyadhuru majani ya nchi, wala kitu cho chote kilicho kibichi, wala mti wo wote, ila wale watu wasio na muhuri ya Mungu katika vipaji vya nyuso zao. [5] Wakapewa amri kwamba wasiwaue, bali wateswe miezi mitano. Na maumivu yao yalikuwa kama kuumwa na nge, aumapo mwanadamu. [6] Na siku zile wanadamu watatafuta mauti, wala hawataiona kamwe. Nao watatamani kufa, nayo mauti itawakimbia.**

**9:1"nikaona nyota iliyotoka mbinguni, imeanguka juu ya nchi"** Kumekuwapo na nadharia kadhaa kama kwenye utambulisho wa nyota mfano wa mtu ambayo huitwa malaika.

1. Kwa sababu KITENZI ni NJEO YA WAKATI TIMILIFU, ingeweza kurejelea kwa Shetani baada ya kuanguka katika siku za nyuma na anaendelea kuanguka kutoka mbinguni (kam vile Isa. 14:12; Ezek. 28:16; Luka 10:18; Ufu. 12:9)
2. Kwa sababu ya mazingira inaweza kuwa tu ni malaika mtumishi mwingine aliyehusika katika hukumu ya Mungu (kama vile Ufu. 20:1)

Malaika kama nyota ziangukazo mara nyingi hupatikana katika maandiko ya Kiyahudi juu ya matukio ya kiyama kwenye kipindi kati ya agano la kale na agano jipya.

◙ **"naye akapewa ufunguo wa shimo la kuzimu"** Neno "ufunguo" limetamkwa katika Ufu.1:18 na 20:1.Huashiria mamlaka.Mungu ataonyesha mamlaka juu ya hukumu kubwa ya mapepo.

Kuzimu ni neno la Kiyunani linalomaanisha "kina" lililokanushwa na KIAMBISHI AWALI.

1. Inatumika katika andiko la agano la kale (tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale) katika Mwa. 1:2; 7:11; Zab. 42:7; 107:26 kwa vina vya maji kwenye uumbaji.
2. Katika Zab. 71:20 inarejelea mahali pa wafu.
3. Hii pia ni kweli ya I Enoki 18:12-16; 21:7-10; 108:3-6, ambapo ni kifungo cha muda na cha milele kwa malaika walioanguka.

4. Inaonekana kuwa sawa na neno "*tartarus*" (kama vile 2 Pet. 2:4 na I Enoki 21:7), sehemu ambapo malaika waovu wamewekwa kifungoni (kama vile Luka 8:31; Yuda 6; Ufu. 11:7; 17:8; 20:1-3; na I Enoki 10:4; 86:1; 88:1; Jubilii 5:6-11).
5. Paulo alitumia neno hili (kuzimu) katika Rum.10:7 kwa maana ya mahali pa wafu (kama vile Isa. 24:21-22).
6. Baadaye walimu wa sheria za Kiyahudi walisema lilikuwa ni jina la sehemu isio kuwa ya haki ya *Sheol*/*kuzimu* (tazama Mada Maalumu katika Ufu. 1:18).

◙ **"akapewa"** Kuna mfululizo wa VITENZI VYA IRABU TENDEWA katika sura zote ya 8 na 9, ambavyo husistiza mamlaka ya Mungu ya mambo yote ya historia na yenye pepo wabaya (kama vile Ufu. 8:3,7,8,11,12; 9:1,3,4,5). Mara nyingi wandishi wa Kiyahudi wanatumia IRABU TENDWA kama MANENO YA KUZUNGUSHA kwa matendo ya Ki-Ungu.

**9:2"moshi ukapanda kutoka mle shimoni kama moshi wa tanuru kubwa"** Istilahi hii imetumika kwa maana kadhaa katika Agano la kale:
1. ilifuatana na hukumu juu ya sodoma na gomora (kama vile Mwa. 19:2
2. ilifuatana na hukumu ya Mungu juu ya mataifa (kama vile Isa. 34:10)
3. ilifuatana na uwepo wa Mungu juu ya Mlima Sinai (kama vile Kut. 19:18)

**9:3"Nzige"** Mara nyingi hizi hutumika kama ishara za ghadhabu ya Mungu (kama vile Ufu. 10:12-15; Yoeli1:4; 2:1na kuendelea) kwa sababu ziliashiria jeshi la uvamizi (kama vile Ufu. 9:7; Yoeli. 2:4-5, 7-9).

**9:4"Wakaambiwa wasiyadhuru majani ya nchi, wala kitu cho chote kilicho kibichi, wala mti wo wote"** Haya majeshi yenye pepo wabaya yamewekewa mipaka katika adhabu zao. Hawapaswi kuharibu uhai wa mimea yoyote na wanaweza kutesa tu, lakini sio kuua, wasioamini (kam avile Ufu. 9:5; 7:4); waaminio wanalindwa na Mungu (kama vile walivyokuwa kwenye mapigo ya Misri).

◙ **"muhuri ya Mungu katika vipaji vya nyuso zao"** Angalia maelezo kamili katika Ufu.7:2. Ni dokezo kutoka katika Ezek. 9:4.

**9:5"miezi mitano"** Wengine wanafasiri kipindi hiki kipana kama muda wa kuishi kwa nzige. Hata hivyo, yawezekana ni nusu ya namba kumi, ambazo zingekuwa sitiari nyingine kwa mipaka ya hukumu (kama vile Ufu. 6:6,8; 8:7-12).

◙ **"kuumwa na nge"** Mwiba wa nge ni sitiari nyingine ya Agano la kale (kama vile 2 Nya. 10:11,14).

**9:6** Huu ni ufanano wa moja kwa moja kwa 6:15-16, ambao ingekuwa ushahidi wa ziada kwa nadharia za ufupisho miongoni mwa muhuri, baragumu, na bakuli. Hii inaweza kuwa dokezo kwa hawa Wayahudi waabudu sanamu wasio na imani ya Yerusalemu katika Yer. 8:2-3

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 9:7-11**
**[7] Na maumbo ya hao nzige yalikuwa kama farasi waliowekwa tayari kwa vita, na juu ya vichwa vyao kama taji, mfano wa dhahabu, na nyuso zao zilikuwa kama nyuso za wanadamu.[8] Nao walikuwa na nywele kama nywele za wanawake. Na meno yao yalikuwa kama meno ya simba. [9] Nao walikuwa na dirii kifuani kama dirii za chuma. Na sauti ya mabawa yao ilikuwa kama sauti ya magari, ya farasi wengi waendao kasi vitani. [10] Nao wana mikia kama ya nge, na miiba; na nguvu yao ya kuwadhuru wanadamu miezi mitano ilikuwa katika mikia yao. [11] Na juu yao wanaye mfalme, naye ni malaika wa kuzimu, jina lake kwa Kiebrania ni Abadoni, na kwa Kiyunani analo jina lake Apolioni.**

**9:7-9"Na maumbo ya hao nzige"** Maelezo ya asili ya nzige ni sawa na Yoeli 2:4-9 na pia mithali moja ya Waarabu mashuhuri ambayo inasema, " nzige wana kichwa kama cha farasi, kifua kama simba, miguu kama ngamia, mwili kama nyoka, na papasi kama nywele za mwana mwali."

Kawaida hili ni dokezo kwa kitabu cha Yoeli katika maelezo yake:

1. Meno ya simba (kama vile Ufu. 9:8; Yoieli 1:6)
2. Hesabu kubwa sana ya vibanda wazi na farasi wakikimbilia vitani (kama vile Ufu. 9:9 na Yoeli 2:5)

**9:8** Baadhi waliona hili kama rejeo kwa kundi kubwa la Waparthi, paleKalvari wakiwa na nywele ndefu. Hawa walijulikana kwa ustadi wao kama watupa mishale walioko milimani.Warumi waliwaogopa wavamizi hawa wakatili.

**9:11"Na juu yao wanaye mfalme"** Mithali 30:27 inaseama kwamba nzige hawana Mfalme, lakini hili ni dokezo kwa kundi kubwa la wenye pepo wabaya, sio nzige wa asili.

◙ **"naye malaika wa kuzimu"** Neno "kuzimu" linarejelea kwenye utawala wa wafu (kama vile Ufu. 9:1,2,11; 11:7; 17:8; 20:1,3; na Rum. 10:7).Angalia maelezo kamili katika Ufu.9:1.

◙**"naye ni malaika wa kuzimu, jina lake kwa Kiebrania ni Abadoni, na kwa Kiyunani analo jina lake Apolioni"** Neno la kiebrania (kiaramu) lina maanisha "uharibifu" na neno la Kiyunani lina maanisha "mharibifu." Neno la Kiebrania lilitambuliwa kama *Sheol*, utawala wa wafu (kama vile Ayu 26:6; 29:22; 31:12; Zab. 88:11 Mit. 15:11; 27:20).

Robert B. Girdlestone anayo maoni ya kuvutia juu ya neno hili katika kitabu chake kiitwacho *Synonyms of the Old Testament:* "Neno hili linaonyesha "kuangamia" yapata kama sura mia moja.Linapotumika kwa mtu kwa kawaida linaashiria kifo, linapotumika kwenye ardhi humaanisha iliotelekezwa" (uk. 273).

Katika Ayubu 28:22 limepewa nafsi pamoja na kifo. Hali hii ya kupewa nafsi pia kwa ajili ya magombo ya bahari ya chumvi na fasiri ya Kiyahudi ya matukio ya siku ya mwisho kwenye kipindi kati ya agano la kale na agano jipya. Jambo hili kwa kiasi fulani sio la kawaida kwa sababu malaika wa mauti katika Agano la kale ni mtumishi wa YHWH (kama vile Kut. 12:23; Ayu 15:21) au hata YHWH kufanyika mfano wa mwanadamu (kama vile Kut. 12:13,29). Lakini hapa malaika anaonekana kuwa mtawala wa wale waliofungwa, umati wenye pepo wabaya.Hii inaweza kuwa njia nyingine kuonyesha mamlaka ya Mungu juu ya vitu vyote.

Wengine walionyesha kwamba utawala wa Nero na Domitian walidai kuwa wao walikuwa ni mfano halisi wa Apollo, kwamba jina hili la Kiyunani ni muundo uliyoharibiwa na dokezo kwa malaika wa maaangamizi. Kuna vipande viwili vya ushahidi wa kulitetea hili,

1. Nzige zilikuwa ishara kwa Apollo
2. Neno Apollo na Apollyon yote yanatoka katika mzizi huo huo wa Kiyunani

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 9:12**
**12 Ole wa kwanza umekwisha pita. Tazama, bado ziko ole mbili, zinakuja baadaye.**

**9:12** Aya hii huungana na Ufu. 11:14 na 12:2.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 9:13-19**
**13 Malaika wa sita akapiga baragumu, nikasikia sauti moja iliyotoka katika zile pembe za madhabahu ya dhahabu iliyo mbele za Mungu, 14 ikimwambia yule malaika wa sita aliyekuwa na baragumu, Wafungue nao malaika wanne waliofungwa kwenye mto mkubwa Frati. 15 Wale malaika wanne wakafunguliwa, waliokuwa wamewekwa tayari kwa ile saa na siku na mwezi na mwaka, ili kwamba waue theluthi ya wanadamu. 16 Na hesabu ya majeshi ya wapanda farasi ilikuwa elfu ishirini mara elfu kumi; nilisikia hesabu yao. 17 Hiyo ndivyo nilivyowaona hao farasi katika maono yangu, nao waliokaa juu yao, wana dirii kifuani, kama za moto, na za**

**samawi, na za kiberiti; na vichwa vya farasi hao ni kama vichwa vya simba, na katika vinywa vyao hutoka moto na moshi na kiberiti. [18] Theluthi ya wanadamu wakauawa kwa mapigo matatu hayo, kwa moto huo na moshi huo na kiberiti hicho, yaliyotoka katika vinywa vyao. [19] Kwa maana nguvu za hao farasi ni katika vinywa vyao, na katika mikia yao; maana mikia yao ni mfano wa nyoka, ina vichwa, nao wanadhuru kwa hivyo.**

**9:13"nikasikia sauti moja iliyotoka katika zile pembe za madhabahu ya dhahabu "** Hili ni dokezo kwa madhabau ya uvumba katika hema la kukutanikia (kama vile Kut. 30:2,310) kuna madhabau mbili zimetajwa kwenye sehemu hii: madhabau ya dhabihu ambapo roho za wafiadini zilipatikana (kama vile Ufu. 6:9-11), na madhabau ya uvumba ambapo juu yake huwekwa maombi ya watu wa Mungu (kama vile Ufu. 8:3-5).Pembe zilikuwa ishara ya nguvu kwenye Agano la kale. Madhabau yote ya uvumba na madhabau ya dhabihu yalikuwa na pembe. Angalia maelezo katika Ufu.8:3.

**9:14"Wafungue nao malaika wanne waliofungwa kwenye mto mkubwa Frati"** wale ambao wanatafuta vidokezo vya kihistoria vya karne ya kwanza wanaliona hili kama kundi tu la Waparthi mbele ya mto Frati (yaani, mipaka ya utawala wa Warumi, kama vile I Enoki 56:5-8). Wengine, hata hivyo, wanaona hili kama dokezo kwa Agano la kale ambapo, wale farasi wanne kwenye siku ya mwisho wanapatikana katika Zek. 1:8 na 6:1-8, hawa malaika wanne wanaonekana kuwa sitiari kwa watumishi waliochaguliwa na Mungu kuleta hukumu juu ya kuanguka, na uasi wa ulimwengu (kama vile Ufu. 7:1). Hata hivyo, kwa sababu malaika hawa wamefungwa, inaweza kuwa rejeo kwa malaika waovu (kama vile Yuda 1:6). Hawa malaika wanaleta mauti kwa theluthi moja ya wanadamu (kama vile Ufu. 9:18).Sehemu ya kaskazini ya vijito vya mto Frati ilikuwa mpaka wa kaskazini mashariki mwa nchi ya ahadi (kama vile Mwa. 15:18; Kum. 1:7; 11:24; Yos. 1:4).

**9:15"Wale malaika wanne wakafunguliwa, waliokuwa wamewekwa tayari kwa ile saa na siku na mwezi na mwaka"** Kuna KIBAINISHI CHENYE UKOMO pamoja na neno "muda" ambalo lina maanisha usahihi wa kifungu hiki kilicho kamili. Hili ni rejeo kwa mamlaka na utawala wa Mungu wa historia (kama vile I Enoki 92:2). Huu ni msaada mkubwa kwa wale wanaopitia mateso.

**9:16"Na hesabu ya majeshi ya wapanda farasi ilikuwa elfu ishirini mara elfu kumi"** Hii ni hesabu ya kiishara ya umati wa wenye pepo wabaya ambao humeza wanadamu ambao hawajakombolewa. Hesabu hii inalinganishwa na idadi kubwa sana ya malaika wanao mtumikia Mungu **(**kama vile Ufu. 5:11; Kumb. 33:2; Zab. 68:17; Dan. 7:10; Ebr. 12:22; Yuda 1:14).

Tena, kujaribu kuhusisha hili kwenye taifa la kisasa la china ni mfano mwingine wa kulazimisha fasihi ya kitamathali katika historia ya wakati huu. Shauku ya Wakristo kutafuta kujua mambo ya wakati ujao na kushawishiana na maarifa ya siri ni tatizo la wakati uliopo.

**9:17-19"hao farasi katika maono yangu, nao waliokaa juu yao"** Maelezo yanayofuata yanaona farasi na wapanda farasi kama kitu kimoja. Mawakala wa ukweli wa mauti na mateso ni farasi wenyewe (kama vile Ufu. 9:19). Rangi za farasi—nyekundu (moto), rangi ya samawati (hyacinth) na manjano (salfa)—zinatambulisha umati huu hasa wenye pepo wabaya wanaohusishwa na mapigo matatu ya moto, moshi wa ragi ya samawati, na salfa zimetajwa katika Ufu. 9:18.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 9:20-21**
**[20] Na wanadamu waliosalia, wasiouawa kwa mapigo hayo, hawakuzitubia zile kazi za mikono yao, hata wasiwasujudie mashetani, na sanamu za dhahabu na za fedha na za shaba na za mawe na za miti, zisizoweza kuona wala kusikia wala kuenenda. [21] Wala hawakuutubia uuaji wao, wala uchawi wao, wala uasherati wao, wala wivi wao.**

**9:20"Na wanadamu waliosalia, wasiouawa kwa mapigo hayo, hawakuzitubia zile kazi za mikono yao"** Haya ni maelezo ya wazi, yasiyo na kauli tata yenye madhumuni ya ukombozi wa haya mapigo (kama vile Ufu. 9:21; 14:6-7; 16:9,11; 21:7; 22:17).

Kama Mungu alitumia mapigo juu ya Misri kama kichocheo kwa (1) Wamisri kuamini na kumtumikia Yeye na (2) Israeli kukaa katika uaminifu na kumtumikia Yeye (kama vile Kumbukumbu 27-28), hivyo mapigo haya sawa yalimanisha kuwabadilisha wanadamu wasioamini warudi kwa Muumba wao, lakini walikataa. Kutokuamini kwa kiburi chao ilikuwa hali ya uasi waliyoiafiki (kama vile Rum. 1:24,26).

◙**"zile kazi za mikono yao "** Hili ni dokezo kwa ibada ya sanamu (yaani, kuabudu mapepo, kama vile Kum. 32:17; Zab. 106:37; 1 Kor. 10:20) imetajwa mara nyingi sana katika Agano la kale (kama vile Kum. 4:28; 28:36,64; 29:17; 32:17; Zab. 115:4-8; 135:15-18; Isa. 2:8; 37:19; 40:19-20; 44:17; Yer. 1:16; 10:3-5; Dan. 5:23; Mik. 5:13). Angalia katika Agano jipya kwamba ibada ya sanamu imehusianishwa na pepo wabaya (kama vile Ufu. 16:14; 1 Kor. 10:20; 1 Tim. 4:1).

**9:21** Mambo haya manne (ibada ya sanamu, uuaji wao, uchawi wao, uasherati wao) yalihukumiwa katika Agano la kale (kama vile Kum.18:10-11,14,20; Kut. 22:18; Law. 20:6) na yaliainisha maisha yasio ya kiadilifu ya wale wasioamini (kama vile Warumi 1-2; 1 Tim. 4:1; Ufu.18:23). Kundi hili lililojumuishwa sawa na wasioamini na kutubu limetanjwa katika Ufu.13:15-17; 14:9; 16:2,9,11.

**NASB, NKJV,**
**NRSV"uchawi wao"**
**TEV"nguvu za giza"**
**NJB"uchawi"**

Tunapata neno la Kiingereza "famasia" kutoka katika neno hili la Kiyunani uchawi (*pharmakeia*, kama vile Gal. 5:20). Hii inaweza kuwa rejeo kwa sehemu furani ya nguvu za giza au kutia sumu, kama pakanga iliyotajwa hapo awali (kam vile Ufu. 8:11). Katika ulimwengu wa kale madawa yalitumika kusababisha uzoefu wa "kidini".

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa usomaji wa fasiri, ambayo inamaanisha kwamba unao wajibu wa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu lazima aenende katika nuru tuliyo nayo. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumuachia vitu hivi mfasiri.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa ili kukusaidia kufikiri mambo muhimu yaliyoko katika kipengele cha kitabu hiki. Yamekusudiwa kukuchokonoa akili, na sio kutoa maana ya mwisho.

1. Tupate wapi chanzo cha taswira ya hizi sura: (1) Agano la kale; (2) maandiko ya Kiyahudi ya matukio ya kiyama; au (3) matukio ya kihistoria ya Ufalme wa Warumi?
2. Je! Matukio haya yanarejelea kwa (1) karne ya kwanza, (2) kila karne, au (3) siku zijazo?
3. Je! Sura hizi zinamanisha kuchukuliwa kikawaida au kwenye matukio ya siku ya kiyama?
4. Je! upi ni msukumo mkubwa wa sura ya 8-9?
5. Je! Ni kwa jinsi gani muhuri wa saba na baragumu ya saba zinahusishwa katika sura ya 8 na 9?
6. Kwa nini kutakuwepo na kuongezeka kwa shughuli za kimalaika na kipepo kabla ya Kuja kwa mara ya pili kwa Yesu?

# UFUNUO 10:1-11:19

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Malaika na Kitabu Kidogo | Malaika Mkuu na Kitabu | Pumziko kati ya matukio | Malaika na Kitabu Kidogo | Ukaribu wa adhabu ya mwisho |
| 10:1-7 | 10:1-7 | 10:1-7 | 10:1-4 | 10:1-7 |
| | Yohana anakila Kitabu Kidogo | | 10:5-7 | Muonaji Anakila Kitabu Kidogo |
| 10:8-11 | 10:8-11 | 10:8-10 | 10:8 | 10:8-11 |
| | | | 10:9 | |
| | | | 10:10-11 | |
| | | 10:11 | | |
| Mashahidi wawili | Mashahidi wawili | Kulipima Hekalu na wale Mashahidi wawili | Mashahidi wawili | Mashahidi wawili |
| 11:1-13 | 11:1-6 | 11:1-3 | 11:1-3 | 11:1-10 |
| | Mashahidi wanauwawa | 11:4-6 | 11:4-6 | |
| | 11:7-10 | 11:7-10 | 11:7-13 | |
| | Mashahidi Wahuishwa | | | |
| | 11:11-14 | 11:11-13 | | 11:11-13 |
| | | Baragumu ya Saba | | |
| 11:14 | | 11:14 | 11:14 | 11:14 |
| Baragumu ya Saba | Baragumu ya Saba:Ufalme unatangazwa | | Baragumu ya Saba | Baragumu ya Saba |
| 11:15-19 | 11:15-19 | 11:15-19 | 11:15-18 | 11:15-18 |
| | | | 11:19 | 11:19 |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** **("Kutoka** **Mwongozo  Mzuri wa Usomaji wa Biblia"( A Guide to Good Bible Reading)**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA.*

Huu ni mwongozo wa usomaji wa hitifaki, ambayo inamaanisha kwamba unao wajibu wa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu lazima aenende katika nuru tuliyo nayo. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Unalazimika kutokuondoa hili toka kwa msemaji.

Soma sura katika mkao mmoja. Yatambue masomo. Linganisha mgawanyiko wa mada zako kwa ulinganifu wa tafsiri tano za hapo juu. Aya haijavuviwa, lakini ni ufunguo wa kufuata kusudi la msingi wa mwandishi, ambao ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya inayo moja na katika hilo ni somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu,
4. Nk.
5.

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Pumziko la matukio la kwanza (sura ya 7) lilikuja kati ya mihuri ya sita na saba. Uhusiano huu wa pili (Ufu. 10: 1-11: 14) huja kati ya tarumbeta ya sita na ya saba. Hakuna uhusiano kati ya kitasa cha sita na cha saba (Ufu. 16), lakini kuna mwingiliano mwingine kabla yao (Ufu. 12-14).

B. Uingiliano huu, kama wa Ufunuo 7, hutumia maneno ya Agano la Kale (hema, madhabahu, Yerusalemu). Hata hivyo, kama vile vikwazo vya Wayahudi katika Ufunuo 7 vinawarejea watu wa Mungu wa Kanisa katika Agano la Kale, Kanisa, hivyo kadhalika, katika sura hii. Vidokezo vinavyotokana na Danieli 9 lakini vimeelekezwa kwa mazingira ya Wagiriki-Warumi, karne ya kwanza.

   Hapa kuna nukuu fupi kutoka katika hitifaki ya Alan Johnson *Commentary on Revelation*, "Maoni ya Kiyahudi yanakabiliwa na uwezo wake duni wa kuhusisha sura hii kwa muktadha wa sura ya 10, kwa kufanana na mlingano wa muhuri (Ufu. 7), kwa huduma na umuhimu wa mashahidi wawili, na kwa sura zaidi katika Ufunuo (hasa Ufu.12-13) Kwa hivyo, ni vizuri kuuelewa Ufunuo 11 kama unavyorejelea jamii yote ya Kikristo "(uk. 104)

C. Kama vile Alan Johnson anavyouona Ufunuo 11 katika uhusiano wake na Ufunuo 7, 10 na 12-13, George Ladd anaona kama kitengo cha kujitegemea kinachohusiana na uhifadhi wa Wayahudi na wokovu wao wa mwisho (kama vile Mat. 23:39, Luka 21:24, Rom 11:26). Angalia *Commentary on the Revelation of John*,kr. 150-151.

   Ni vigumu kuamua kati ya maoni haya mawili. Kwa hakika ninahisi kuwa kwa sababu ya ahadi za Mungu kwa Israeli, kutakuwa na uamsho wa wakati wa mwisho kati ya Israeli ya asili au wabadili dini ambao kwao wengi wataigeukia imani katika Kristo (kama vile Zakaria 12:10); hii ni sehemu ya hoja ya Paulo katika Warumi 11 (hakika inawezekana kwamba uamsho uliotajwa katika Zakaria 12:10 ulifanyika katika kanisa la Palestina la karne ya kwanza). Hata hivyo, muktadha wa Ufunuo 7,10, na 12-13 inamaanisha wigo wa ulimwengu wote wa ulinzi kwa watu wote wa Mungu na hukumu dhidi ya wasioamini wote. Katika mstari huu msisitizo wa Kiyahudi wa kuamini au hata msisitizo wa Wayahudi-dhidi ya Mataifa haukuwepo.

D. Je, patakuwapo na mashahidi wawili wa wakati wa mwisho, au huu ni mfano wa shahidi wa mwisho? Ni vigumu sana kuwa na ujasiri katika kutafsiri alama za kitabu hiki. Ikiwa Yohana alitaka kuwa halisi, angeweza kuchagua aina tofauti ili kuwafunulia hii kwa waamini wa nyakati zote.

   Je! rejeo hili kwa "mashahidi wawili" lina maana maalum kwa waumini wa karne ya kwanza waliokuwa na mateso (huenda ni ibada zakienyeji za kiffalme)? Hii haiwezi kujibiwa kwa hitimisho. Uchaguzi wa Yohana wa taswira unatokana na vyanzo kadhaa: Agano la Kale, fasihi za matukio ya siku za mwisho, utamaduni wa Wagiriki-Warumi na wakati mwingine simulizi za Mashariki (sura ya 12). Je! Wasikilizaji wa kwanza kabisa na kiujumla walielewa kikamilifu vyanzo vyake na mfano? Yawezekana sivyo, siyo kwa njia maalumu, bali waliielewa aina! Wasingeweza kulazimisha utimilifu halisi wa kihistoria kwa maelezo yote.

   Hofu yangu pekee katika kuifanya kauli hii ni jinsi unabii wa Agano la Kale ulivyobashiriwa na kufasiriwa na waandishi wa Agano Jipya walioongozwa! Mara nyingi waliona utimilifu halisi wa maelezo ya Agano la Kale katika maisha ya Kristo. Baadhi ya utekelezaji huu yalikuwa maneno ya walimu wenye aina ustadi wa maneno / aina hasi. Chini ya mwongozo wa Roho (au mafundisho ya Yesu, kama vile Luka 24: 13-35) mazingira ya sasa ya Mitume yalionekana kupitia maandiko ya unabii ya Agano la Kale. Kitu hicho kinaweza kutokea kwa kizazi cha mwisho cha waumini walioteswa. Hata hivyo, wakalimani wanaoingilia

kati hawana uwezo wa kubashiri yapi maelezo kati ya haya kwa njia ya thiolojia au kanuni za ufasiri! Wafasiri wa kisasa hawapaswi (1) kuzipachika historia zao katika maandiko haya ya matukio ya siku za mwisho wala (2) kutafuta utimilifu halisi juu ya kila undani wa aina hii ya mfano. Muda utajisemea!

E. Mifumo ya fasihi na picha za mihuri na tarumbeta zinakaribiana kwa usawa. Vyote huleta historia ya kibinadamu mpaka mwisho (kama vile Ufu 6: 12-17 na 11: 15-19).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (ILIYOBORESHWA): UFUNUO 10:1-7**
**[1] Kisha nikaona malaika mwingine mwenye nguvu akishuka kutoka mbinguni, amevikwa wingu; na upinde wa mvua juu ya kichwa chake; na uso wake ulikuwa kama jua, na miguu yake kama nguzo za moto. [2] Na katika mkono wake alikuwa na kitabu kidogo kimefunguliwa. Akaweka mguu wake wa kuume juu ya bahari, nao wa kushoto juu ya nchi. [3] Naye akalia kwa sauti kuu, kama simba angurumavyo. Na alipolia, zile ngurumo saba zikatoa sauti zao. [4] Hata ngurumo saba zilipotoa sauti zao, nalikuwa tayari kuandika. Nami nalisikia sauti kutoka mbinguni ikisema, Yatie muhuri maneno hayo yaliyonenwa na hizo ngurumo saba, usiyaandike. [5] Na yule malaika niliyemwona, akisimama juu ya bahari na juu ya nchi, akainua mkono wake wa kuume kuelekea mbinguni, [6] akaapa kwa yeye aliye hai hata milele na milele, yeye aliyeziumba mbingu na vitu vilivyomo, na nchi na vitu vilivyomo, na bahari na vitu vilivyomo, ya kwamba hapatakuwa na wakati baada ya haya; [7] isipokuwa katika siku za sauti ya malaika wa saba atakapokuwa tayari kupiga baragumu; hapo ndipo siri ya Mungu itakapotimizwa, kama alivyowahubiri watumishi wake hao manabii**

.

**10:1"Nikaona malaika mwingine mwenye nguvunakishuka kutoka mbinguni"** Tambua kwamba Yohana amerejea duniani baada ya maono ya Ufu 4-5 (ikiwa wito wa Yohana kwenda mbinguni katika Ufu. 4 ulikuwa ni unyakuo wa kanisa, je! huku ni kuanguka kwa kanisa?). Malaika huyu anaelezewa kwa maneno ambayo yanatumika kwa YHWH katika Agano la Kale na kwa Kristo katika Ufu. 1: 12-20. Kwa sababu hili, wengi wamesema kwamba huyu ni Kristo Mwenyewe. Hata hivyo, hili linatia mashaka kwa sababu zifuatazo:

1. Kristo haitwi kamwe malaika katika Ufunuo
2. Kuna malaika wengine wenye nguvu walioorodheswa katika Ufunuo (kama vile Ufu. 5: 2; 18:21)
3. Malaika huyu ataapa kwa Mungu katika Ufu. 10: 6, ambako hakufai kwa ajili ya Kristo
4. Yupo malaika katika Danieli 10 ambaye pia anaelezewa kwa maneno yafananayo.

Maelezo haya kina yanaweza kumtofautisha malaika huyo wa mwanga na malaika wa shimo katika Ufunuo 9. Kama malaika katika Ufunuo 9 alivyoelekezwa, malaika huyu anajiongoza. Hii inaweza kuwa na maana ya malaika mwenye nguvu wa Dan. 10: 5-6 au Michael, malaika mkuu wa Israeli katika Dan. 10:13 na 12:1.

◙ **"amevikwa wingu"** Katika Agano la Kale mawingu yalikuwa ni usafiri pekee ya mambo ya Uungu (kama vile Zab 97: 2, 104: 3; Dan 7:13; Matendo 1: 9).

◙ **"na upinde wa mvua juu ya kichwa chake"** Wengi wanaliona hili kama rejea ya Ufu.4: 3 na hivyo jina jingine la nguvu na mamlaka linakumbushia uungu. Nukuu inaweza kurudi kwa Ezek. 1:28, ambapo upinde wa mvua ni kiti kinacho hamishika cha enzi / gari moto la YHWH.

◙ **"na uso wake ulikuwa kama jua"**Hili hufuata maelezo ya Kristo yapatikanayo katika Ufu. 1:16 (kama vile Mathayo 17: 2).

◙**"na miguu yake kama nguzo za moto"** Maelezo haya pia ni sawa na Kristo katika Ufu. 1:15.

**10:2 "Na katika mkono wake alikuwa na kitabu kidogo kimefunguliwa"** Pamekuwapo na majadiliano mengi kuhusu kitabu hiki kidogo. Wengine wanakiona kama kitabu kidogo cha Ufu. 5: 1, kikiwa kimefunguliwa, lakini maneno mawili ya Kigiriki hutumiwa (Ufu.5: 1, *biblion*, Ufu.10: 2, *biblaridion*). Wengine wanayaona kama yalivyohusiana na Ezekieli 2: 8-3: 14. Kwa kuwa huyu ni malaika na sio Kristo, Ezekieli ni pendekezo bora.

◙ **"Akaweka mguu wake wa kuume juu ya bahari, nao wa kushoto juu ya nchi."** Ukubwa wa malaika huzungumzia ujumbe wa ulimwengu wote. Waalimu (katika buku la sheria na maadili ya Kiyahudi) walimzungumzia malaika mmoja aitwaye Sandelfon, ambaye urefu wake ulikuwa sawa na umbali wa maili 500 zaidi kuliko malaika wengine (kama vile Hagigah 13b).

**10:3 "Naye akalia kwa sauti kuu, kama simba angurumavyo"** Neno hili "unguruma" (*mukaomai*) hutumiwa kwa sauti ya ng'ombe (chini ya kilindi). Hata hivyo, inaonekana kufaa kwa kuwa hii ni nukuu kwenye vifungu vya Agano la Kale ambako Mungu aliongea kama simba (kama vile Yer 25:30, Hos 11:10; Yoeli 3:16; Amosi 3: 8).

◙ **"zile ngurumo saba zikatoa sauti zao"** Utambulisho wa mbingu hizi saba una mgongano. Hii inaweza kuwa:

1. Kutaja kwa "sauti" saba za Mungu katika Zab. 29: 3-9
2. Sambamba na muhuri saba na tarumbeta saba, ambazo zilikuwa mduara wa hukumu ya Mungu juu ya wasioamini (kama vile Ufu. 8: 5, 11:19; 16:18) kwa lengo la ukombozi
3. Sauti inayotoka katika kiti cha enzi cha Mungu (kama vile Ufu. 4: 5)
4. Inaweza pia kuhusiana na zile roho saba za Mungu (kama vile Ufu. 1: 4, 4: 5; 5: 6 kutoka Isa. 11:22)

**10:4 "Yatie muhuri"** Kuna maeneo kadhaa katika Biblia ambapo mtu amepokea ufunuo kutoka kwa Mungu lakini hakuweza kuupambanua. Mawili kati ya haya ni (1) Danieli (kama vile Dan 8:26; 12: 4,9) na (2) Paulo (kama vile 2 Kor 12: 4). Hata hivyo, hili ni tamko la kushangaza sana. Yohana anaambiwa kuandika kile akionacho (kama vile 1: 11,19, 14:13, 19: 9; 21: 5). Yohana anaambiwa katika Ufu.22:10 kwamba maneno ya unabii huu yasifungwe. Lazima erejewe ujumbe huu pekee!

**10:5 "akainua mkono wake wa kuume kuelekea mbinguni"** Hii ni ishara ya kuingia katika kiapo (kama vile Mwa. 14:22, Ex 6: 8, Hes 14:30, Kumb.32:40, Ezekieli 20:15, 28, Dan 12: 7). Aina ya kiapo hiki inavutia sana katika majina yake kwa Mungu.

**10:6 "Yeye aliye hai hata milele na milele"** Sifa hii ya Mungu inakumbushia majina yake mawili ya kawaida ya Agano la Kale:

1. YHWH kutoka katika KITENZI cha Kiebrania "kuwa" (kama vile Kut 3:14). "Mimi niko" jina la agano la uungu; lilisisitiza Mungu kama Mwokozi na Mkombozi (kama vile Mwa. 14:19, Kut.20:11, Neh 9: 6; Zab 146: 6).
2. Elohimu, ambalo lilitumiwa na Mungu katika Mwanzo 1 kama Muumbaji, Mwezeshaji, na Mtoaji wa kila kitu duniani (kama vile Mwa.14:19, Kut. 20:11, Neh 9: 6; Zab 146: 6) .

Kiapo hiki ni njia ya kuthibitisha kutumainiwa kwa ujumbe wa malaika.

◙**"hapatakuwa na wakati baada ya haya"** Hii inaweza kuwa ni jibu kwa swali la wafiadini katika Ufu. 6:10. Ni kweli neno "wakati huo (*chronos*) haitakuwapo tena." Dhana ya muda haijulikani sana katika kitabu hiki kwa sababu kadhaa.

1. Kuna maneno tofauti mawili ya Kiyunani ambayo yanaelezea muda.
   a. *chronos*, muda upitao (kama vile Ufu. 10: 6)
   b. *kairos*, wakati maalum, msimu, au tukio (kama vile Ufu. 1: 3, 11:18, 12: 12,14).
2. Kuna vidokezo kadhaa vinavyotumika:
   a. "mambo ambayo lazima yatokee hivi karibuni" (kama vile Ufu. 1: 1; 22: 6)
   b. "wakati u karibu" (kama vile Ufu. 1: 3; 3:11; 22:10)
   c. "Naja upesi" (kama vile Ufu. 2: 5,16; 22: 7,12,20)
   d. "Nitakuja kama mwivi" (kama vile Ufu. 3: 3; 16:15)

Yote haya yanasemea uharaka (angalia Mada maalum katika Ufu.1: 3). Hata hivyo, vifungu vingine vinazungumzia ucheleweshaji (kama vile Ufu. 6:11; 10: 6; 14:13). Lahaja nyingine ni zinaashilia kwamba siku ya hukumu na tuzo imefika, "imekuwa" (kama vile Ufu.16:17; 21: 6) au "wakati umetimia" (kama vile Ufu. 11:18; ).

Sintofahamu hii imetumiwa na mifumo tofauti ya kutafsiri ili kusisitiza kipengele fulani cha wakati (karne ya kwanza, kila enzi, au kizazi cha mwisho). Kiapo cha malaika ni kwamba matukio ya muda wa mwisho lazima sasa

yaanze. Sala za wahanga wa ki-Kiristo zimejibiwa! Ufunuo lazima ufasiriwe kwa mujibu wa wasomaji wake wa kwanza (angalia John Bray, *Matthew 24 Fulfilled*).

**10:7**
**NASB" siri ya Mungu itakapotimizwa"**
**NKJV"siri ya Mungu ingetimizwa"**
**NRSV"siri ya Mungu ingetimilika"**
**TEV"Mungu atautimiliza mpango wake wa siri"**
**NJB"siri ya Mungu itakamilishwa"**

Neno lina vidokezo kadhaa.

1. Paulo hulitumia mara kwa mara kutaja mpango wa ukombozi wa milele wa Wayahudi na Mataifa kupitia imani katika Kristo (kama vile Efe. 2: 11-3: 13, angalia MADA MAALUMU: MPANGO WA UKOMBOZI WA MILELE WA YHWH ( SPECIAL TOPIC: ETERNAL REDENPTENTION PLANN) katika Ufunuo 4: 1
2. Ufunuo mara nyingi unahusu siri juu ya sehemu ya maono (kama vile Ufu. 1:20; 17: 5,7).
3. Katika Ufu.10: 7 unamaanisha mpango wa ukombozi wa milele wa Mungu, kama Paulo alivyofanya katika Rum. 16: 25-26 na Efe. 2: 11-3: 13.Inawezekana kwamba Yohana alilichukua neno hili kutoka kwa Danieli, hasa sura ya 2 (kama vile Dan 2: 18,19,27,28,29,30,47). Ikiwa ndivyo, basi linarejelea kwa uwezo wa Mungu wa kufunua matendo Yake. Mungu ni mwenye ujuzi wa yote na udhibiti wa historia yote.

**MADA MAALUMU: SIRI KATIKA INJILI ( SPECIAL TOPIC: MYSTERY IN THE GOSPELS)**

◙ **"hao manabii"**

**MADA MAALUMU: UNABII WA AGANO LA KALE (SPECIAL TOPIC: OLD TESTAMENT PROPHECY)**

**ANDIKO LA NASB (ILIYOBORESHWA): UFUNUO 10:8-11**
**8Na sauti ile niliyoisikia kutoka mbinguni ilinena nami tena, ikisema, Enenda, ukakitwae kile kitabu kilichofunguliwa katika mkono wa yule malaika, aliyesimama juu ya bahari na juu ya nchi. 9Nikamwendea malaika yule nikamwambia kwamba anipe kile kitabu kidogo. Akaniambia, Kitwae, ukile, nacho kitakutia uchungu tumboni mwako, bali katika kinywa chako kitakuwa kitamu kama asali. 10 Nikakitwaa kile kitabu kidogo katika mkono wa malaika yule, nikakila; nacho kikawa kitamu kama asali kinywani mwangu, na nilipokwisha kukila tumbo langu likatiwa uchungu. 11Wakaniambia, Imekupasa kutoa unabii tena juu ya watu na taifa na lugha na wafalme wengi.**

**10:8 "Na sauti ile niliyoisikia kutoka mbinguni** ilinena **nami tena"** Kumekuwa na uvumi mkubwa juu ya utambulisho wa msemaji. Wengine walisisitiza kwamba ni Mungu, au Kristo, au Roho Mtakatifu, au mmoja wa malaika wenye nguvu.

Katika Ufu. 10:11 sauti ni WINGI, yawezekana ikimaanisha Utatu wa Mungu. Huo WINGI uliotumiwa na Uungu katika Agano la Kale (jina Elohim na "sisi" ile ya Mwa. 1:26, 3:22; 7:11; Isa 6: 8) daima imepata kuelezewa kwa namna kadhaa.

1. muundo wa kisarufi uitwao "WINGI wa utukufu" ambapo WINGI unauongezea dhana au neno
2. YHWH anazungumza kwa ujumla juu ya baraza la kimalaika (kama vile 1 Fal 22:19, Ayubu 1: 6; 2: 1; Yer 23:18; Dan 7:10)
3. Muundo wa kwanza wa Mungu wa Utatu au Utatu (kama vile Zab.110: 1, Zek 2: 8; 17:10)

Angalia MADA MAALUMU: MAJINA YA UUNGU (SPECIAL TOPIC: NAMES FOR DEITY) katika Ufu. 1:8.

**10:9 "' Kitwae, ukile'"** Hili ni dokezo kwa Ezek. 2: 8-3: 14 au Yer. 15: 16-17. Hii inaashiria kutumwa ili kuusema ujumbe wa Mungu. Kitabu kidogo kinaashiria ujumbe wa Mungu unaobeba vyote, uhakika kwa waumini (asali,

kama vile Zab 19: 10-11, 119: 103) na hukumu kwa wasioamini (uchungu). Gombo hili si sawa na lile Yesu alilofungua katika sura ya 6. Hili linaurejelea ujumbe kutoka kwa malaika mwenye nguvu (kama vile Ufu. 10: 7-11).

**10:11 "Wakaniambia"** Malaika mwenye nguvu au Mungu wa Utatu anamthibitisha Yohana kama mwandishi wa kinabii na msemaji.

◙**" watu na taifa na lugha na wafalme wengi"** Istihali hii inatumiwa kwa wasioamini wote (kama vile Ufu. 11: 9, 13: 7-8, 14: 6; 17:15) na waaminio (yaani, kabla ya Siku ya Hukumu kama vile Ufu. 7: 9, 15: 4 na baada ya Siku ya Hukumu k.v. Ufu. 21: 24,26; 22: 2). Mstari huu unaweza kumaanisha kuhubiri injili (kama vile Ufu. 10:11; 14: 6) kwa mataifa yote (kama vile Mt 24:14, Mk 13:10) au utabiri wa hukumu zaidi ya wakati wa ghadhabu ya Mungu.

# UFUNUO 11

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 11:1-6**
**[1] Nikapewa mwanzi kama fimbo; na mmoja akaniambia, Inuka, ukalipime hekalu la Mungu, na madhabahu, na hao wasujuduo humo. [2] Na behewa iliyo nje ya hekalu uiache nje wala usiipime, kwa maana Mataifa wamepewa hiyo, nao wataukanyaga mji mtakatifu miezi arobaini na miwili. [3] Nami *nitawaruhusu* mashahidi wangu wawili, nao watatoa unabii siku elfu na mia mbili na sitini, hali wamevikwa magunia. [4] Hao ndio ile mizeituni miwili na vile vinara viwili visimamavyo mbele za Bwana wa nchi. [5] Na mtu akitaka kuwadhuru, moto hutoka katika vinywa vyao na kuwala adui zao. Na mtu akitaka kuwadhuru, hivyo ndivyo impasavyo kuuawa. [6]Hao wana amri ya kuzifunga mbingu, ili mvua isinyeshe katika siku za unabii wao. Nao wana amri juu ya maji kuyageuza kuwa damu, na kuipiga nchi kwa kila pigo, kila watakapo.**

**11:1 "mwanzi kama fimbo"** Katika sehemu zilizopita Yohana anaangaliwa kama malaika afanyae kazi, bali katika tarumbeta ya saba Yohana atashiriki katika tendo hilo.

Neno "fimbo ya kupimia" (*kalamos,* linatumiwa kwa maana hii pekee hapa) labda linaonyesha matumizi ya Agano la Kale ya tete za mto ambazo zilitumiwa kama vyombo vya kupima usawa (angalia MADA MAALUMU: HAKI (SPECIAL TOPIC: RIGHTEOUSNESS) katika Ufu. 19:11). Walikuwa kati ya hatua za miguu minane hadi kumi na mbili kwa urefu (kama vile Ezek. 40:5-42:20).

◙ **"Inuka, ukalipime"** Kupima ilikuwa ni ishara ya (1) kuwa na ulinzi ulioahidiwa (kama vile Yer 31: 38-40; Ufu.21:15). Hii inaweza kuwa dokezo kwa Hekalu la wakati wa mwisho la Ezekieli (kama vile 40-48) au Yerusalemu mpya ya Zekaria (kama vile Zekaria 1:16; 2: 1-13); au (2) hukumu (kama vile 2 Sam 8: 2; 2 Fal 21:13, Isa 28:17, Omb 2: 8). Hapa, kama muhuri wa sura ya 7, ni ishara ya ulinzi wa Mungu wa waumini. Ikiwa hii ni sawa na sura ya 7 basi hekalu hili ni watu wote wa Mungu (Wayahudi waaminio na Mataifa waaminio). Hii pia ingekuwa kadhalika sambamba na Ufu. 12.

◙ **"hekalu la Mungu, na madhabahu, na hao wasujuduo humo"** Utambulisho wa hekalu hili unategemeana na dhanio ya tafsiri ya mtu.

1. Ikiwa tunadhani kwamba taswira ya Yohana inatokana na Ezekieli 40-48, basi hili kiuhalisia ni juu ya hekalu la wakati wa mwisho huko Yerusalemu (kama vile 2 The 2: 4).
2. Ikiwa, hata hivyo, tukichukulia kuwa nukuu ni za Zakaria 2 basi taswira ni ile ya mji wa Mungu, Yerusalemu mpya.
3. Tukilichukulia hekalu la mbinguni (kama vile Ufu.7:15, 11:19, 15:58, Ebr.9:23) basi makutano ya Ufunuo 7: 9 (Kanisa, na mwanamke wa Ufu. 12) yawezekana kuwa ndilo lengo (kama vile Ufu. 21: 15-16).

Ni jambo la kuvutia kukumbuka kwamba Yohana anaambiwa kupima watu wanaoabudu huko. Hii ni istilahi isiyo ya kawaida. Picha hii inahusisha zaidi ya jengo tu. Hii ni taswira ambayo inawazuia watu wa imani kutoka kwa wasioamini waelekeao kuipata ghadhabu ya Mungu. Kwa hiyo, ni sawa na alama ya Mungu juu ya vipaji vya wauminio (kama vile Ufu.7: 3-4).

**11:2 " Na behewa iliyo nje ya hekalu"** Dhana hii ya uwanda wa nje kihistoria inarejelea kihistoria kwa mahakama ya Mataifa katika Hekalu la Herode. Kuna vidokezo kadhaa vya Agano la Kale katika wazo la Yerusalemu na Hekalu lililokanyagwa na Wayahudi (kama vile Zab. 79: 1-7, Isa. 63:18, Dan. 8:13, Zak 12: 3 katika maandiko ya kale ya Kiyunani) . Yesu anaonekana akielezea moja kwa moja kwa Dan. 8:13 katika Luka 21:24.

◙ **"mataifa"** Angalia maelezo katika Ufu.2:26 na 10:11.

◙ **"miezi arobaini na miwili"** Angalia Mada Maalumu hapo chini.

## MADA MAALUMU: MIEZI AROBAINI NA MBILI (SPECIAL TOPIC: FORTY-TWO MONTHS)

◙**"mji mtakatifu"** Hili linaweza kuimaanisha Yerusalemu (kama vile Isaya 52: 1, Mathayo 27:53). Hata hivyo, kufuatia ufafanuzi wa hekalu katika Ufu. 3:12 kama kuwaelezea waumini wa Agano la Kale, kanuni hiyo hiyo lazima ifuatiwe na maneno haya. Katika sura za baadaye za Ufunuo inahusu watu wa Mungu wa Agano Jipya (kama vile 20: 9; 21: 2,10; 22:19).

Yohana anaivuta mifano kutoka katika Agano la Kale lakini anawahusisha watu wa Mungu wa Agano Jipya. Kanisa linaundwa na Wayahudi waaminio na Mataifa. Hakuna msisitizo wa kitabaka juu ya Wayahudi dhidi ya watu wa Mataifa katika Ufunuo. Hakuna tena Myahudi wala Myunani (kama vile 1 Wakorintho 12:13, Wagalatia 3:28, Wakolosai 3:11).

**11:3 "Nami *nitawaruhusu* mashahidi wangu wawili"** Hili linaonekana lina maana ya Mungu Baba akizungumza kwa sababu Yesu anarejewa katika Ufu. 11: 8 (ingawa kuna shida ya kiuandishi wa Kiyunani na KIWAKILISHI NOMINO, ambacho kimeondolewa katika P47 na א).

◙ **"mashahidi wawili"** Kumekuwa na nadharia nyingi kuhusu utambulisho wa wahubiri hao wawili mahiri:

1. Dodoso (kama vile Ufu.11: 4) limetokana na Zak. 4: 3,11,14. Hili kimsingi lilikuwa linahusu uzao wa Daudi uliorudi, Zerubabeli, na kurejea kwa uzao wa Kuhani Mkuu, Yoshua, ambao walikuwa viongozi wawili waongozwao na roho (mizeituni miwili) ambao walisababisha urejesho kutoka utumwa wa Babeli (yaani watu wa Mungu wa waliorejeshwa).
2. Vinara vya taa viwili (kama vile 1:20) vinaweza kuashiria makanisa mawili maaminifu, Smirna, 2: 8-11 na Fladelfia, 3: 7-13.
3. Mashahidi wawili wanaweza kuthibitisha ushuhuda mahakamani (kama vile Hes.35:30, Kumb.17: 6, 19:15).
4. Maelezo ya mashahidi hawa wawili yanamaanisha Eliya (alizifunga mbingu kutokana na Ufu. 11: 6, kama vile 1 Fal 17: 1, 18: 1, Luka 4:25; Yakobo 5:17 na kuushusha moto, kama vila 1 Fal 18: 24,38; 2 Fal. 1: 10,12) na Musa (kuyafanya maji kuwa damu katika Ufu. 11: 6, kama vile Kut. 7: 17-19). Yote haya mawili yalionekana kwa Yesu pale Mlimani alipobadilika sura (kama vile Mathayo 17: 4).
5. Kitabu cha matukio ya mwisho kati ya kipindi cha agano la kale na agano jipya cha 1 Enock 90:315 na makasisis wawili ya awali, Tertullian and Hippolitus, wanadhihirisha kuwa wao ndio watu wawili kutoka katika Agano la Kale ambao hawakufa kifo cha asili, Enoko (kama vile Mwa. 5:21-24) na Elija (kama vile 2 Wafalme. 2:11).
6. Nakala ya awali ya NJB inalisemea kwa kumhusisha Petro na Paulo, wote waliuawa huko Roma katika utawala wa Nero (ukurasa wa 435).

Mimi binafsi ninawaona kama mfano wa ushahidi wa watu wote wa Mungu kwa sababu ya muundo fanani wa mihuri saba na pumziko kati ya matukio na baragumu saba na pumziko kati ya matukio. Kwa hiyo, wote 144,000 (Wayahudi wanaoamini) na kundi lisilo na hesabu (yaani mataifa yaaminio), pamoja na mashahidi wawili, wanalisemea kanisa.

◙**"wamevikwa magunia"** Hii inaweza kuwa ama (1) ishara ya kuomboleza na toba (kama vile Mwanzo 37:34, 2 Sam 3:31) au (2) kwa kikawaida, mavazi ya kawaida ya nabii (kama vile 2 Fal1: 8; Isa 20: 2; Zek 13: 4).

◙**"nao watatoa unabii siku elfu na mia mbili na sitini,"** Miezi arobaini na miwili ya siku thelathini kila mmoja ni sawa na siku elfu moja mia mbili sitini. Injili itatangazwa wakati huu wa mateso na mataifa yasiyoamini (kama vile Mathayo 24: 8-14, 21-22). Tarakimu hii ya mfano hutoka Dan. 7:25; 12: 7 na hutumiwa mara nyingi katika Ufunuo (kama vile 12: 6, 13: 5).

**11:4 "ile mizeituni miwili"** Hili ni dokezo kwa Zerubabeli, uzao wa Daudi ya watumwa waliorudi na Yoshua, uzao wa Haruni wa watumwa waliorudi (kama vile. Zekaria 4: 3,11,14). Hii inaweza kumaanisha kuwa ushahidi wa Injili wa siku ya mwisho utawakilisha mkazo juu ya utawala wa Kimasihi na ukuhani wa Kimasihi (Yesu kama Mfalme na Kuhani, kama vile Zaburi ya 110, Waebrania 1: 3). Wahubiri hao wawili waliovuviwa juu ya toba wanaileta nuru ya Mungu (taz. Zakaria 4) kwa ulimwengu wa uasi (Israeli ya uasi sasa inakuwa mwanadamu aliyeasi, taz. Isa 6: 9-11, 43: 8-13; -29; Ezek 12: 2).

**11:5 "Na mtu akitaka kuwadhuru. . . Na mtu akitaka kuwadhuru"** Zote hizi mbili ni SENTENSI ZENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA ambazo zinachukulia kwamba wapo wale wanaotaka kuwajeruhi, lakini watalindwa ki-Ungu mpaka kusudi lao lipate kukamilishwa.

◙**"moto hutoka katika vinywa vyao na kuwala adui zao"** Tambua kwamba nguvu iko katika kinywa chao ambayo inamaanisha uwezo wa ujumbe ambao wanautangaza. Katika Ufunuo kinywa ni silaha, ulimi kama upanga (kma vile 9:17, 19:15, Waebrania 4:12).

**11:6** Hivi vitendo vya Agano la Kale vinakumbuka moja ya yale ya Eliya (kama vile 1 Fal 17: 1) na Musa (kama vile Kut 7: 17-19).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 11:7-10**
**7 Hata watakapoumaliza ushuhuda wao, yule mnyama atokaye katika kuzimu atafanya vita nao, naye atawashinda na kuwaua. 8 Na mizoga yao *itakuwa* katika njia ya mji ule mkuu, uitwao kwa jinsi ya roho Sodoma, na Misri, tena ni hapo Bwana wao aliposulibiwa. 9Na watu wa hao jamaa na kabila na lugha na taifa *waitazama* mizoga yao siku tatu u nusu, wala hawaiachi mizoga yao kuwekwa kaburini. 10 Nao wakaao juu ya nchi *wa*furahi juu yao na kushangilia. Nao watapelekeana zawadi wao kwa wao, kwa kuwa manabii hao wawili waliwatesa wao wakaao juu ya nchi.**

**11:7 "yule mnyama atokaye katika kuzimu"**Ikiwa mstari huu ni dokezo kwa Danieli 7, basi mnyama ni kielelezo cha pamoja cha wanyama wote wanne waliotajwa katika Danieli 7, ambacho kinamwakilisha Mpinga-Kristo wa wakati wa mwisho (kama vile 2 Wathesalonike 2: 3).

Neno "Kuzimu" ni maskani ya pepo (kama vile Ufunuo 9: 1; 20: 1). Dhana hii ya mnyama imeandikwa katika Ufunuo 13 na 17.
◙**"atafanya vita nao, naye atawashinda na kuwaua"** Mstari huu ni dokezo kwa Dan. 7:21 ambao utafafanuliwa kikamilifu katika Ufunuo 13. Hapa, maneno hayo yanaweza kuashiria kwamba mashahidi wawili ni mfano wa idadi kubwa ya watu (kama vile Ufu. 13: 7 yaani, watu wa Mungu). Kumbuka kwamba hawayajui mateso na mauti.

**11:8 "Na mizoga yao itakuwa katika njia ya mji"** Fedheha hii ya kuiacha wazi miili ya watu waliokufa ilikuwa ni njia ya kuonyesha dharau (kam vile Ufu.11: 9, Kumb. 28:26; Zab 79: 2, Yer 7:33; 8: 2; 16: 4; ; 34:20). Hata hivyo, Mungu alitumia miili yao kuonyesha nguvu yake ya ufufuo na uthibitisho wa jumbe zao

◙**"ule mji mkuu"** Hii inaonekana kuwa ni maelezo juu ya Yerusalemu; hata hivyo, lugha ya mfano inaashiria mapambano ya kiroho kati ya ufalme wa kidunia na ufalme wa mbinguni. Hizi ndizo sababu zangu.

1. Maneno haya "mji mkuu" hutumiwa kwa ajili ya Babeli au Rumi (kama vile Ufunuo 16:19, 17:18, 18: 10,16,18,19,21).

2. Ingawa Yerusalemu inaitwa Sodoma katika Ezek. 16: 46-49 na Isa. 1: 9-10, hauitwi kamwe Misri; Sodoma na Misri vinaonekana kuwa mfano wa dhambi na utumwa.
3. "Ambapo Bwana alisulubiwa" inaonekana kurejelea kwa Yerusalemu, lakini inaweza kuwa njia nyingine ya kuzungumza juu ya falme zilizo kinyume na Mungu za ulimwengu huu.
4. "Watu na kabila na lugha na mataifa" katika Ufunuo 11: 9 vyamaanisha.
   a. mji ambapo dunia nzima itakuwa pale, ambapo unaifaa Rumi kuliko Yerusalemu
   b. "mji" uliotumiwa kama mfano wa wanadamu waasi (kama vile Mwanzo 4:17; 10: 8-10)
5. "Wale wanaoishi duniani watafurahi juu yao na kushangilia" katika Ufunuo 11:10 ina maana kwamba ujumbe wa mashahidi hawa wawili si tu kwa Wayahudi, bali kwa ulimwengu mzima wa wasioamini.

Hii inaelezea vita vinavyoendelea kati ya falme za dunia hii na ufalme wa Kimasihi (kama vile Ufunuo 11:15), hasa kama ilivyo katika Danieli 2 na Zaburi 2.

**11:9 "Na watu wa hao jamaa na kabila na lugha na taifa"** Angalia maelezo katika Ufunuo 10:11.

◙ **"kwa siku tatu u nusu"** Wakati wa Ufunuo 11: 9 pamoja na Ufunuo 11:11 ni sawa na tarakimu saba, ambazo hutumiwa mara nyingi katika Ufunuo. Tukio hili lilikuwa wakati timilifu wa Mungu.

**11:10 " kushangilia; nao watapelekeana zawadi wao kwa wao, "** Wengine wanaliona hili kama sikukuu ya kupeana zawadi (Purimu) iliyopotoshwa (kama vile Esta 9: 19,22). Inaonekana kuwa zaidi kutajwa na Yohana 16:20 ("ulimwengu utafurahi"). Kuunganishwa huku kwa ulimwengu usioamini kunaufunua uwezo wa ujumbe wa mashahidi wawili, bali wasioamini hawakutubu (kama vile Ufunuo 9: 20-21; 16: 9,11).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 11:11-13**
**[11]Na baada ya siku hizo tatu u nusu, roho ya uhai itokayo kwa Mungu ikawaingia, wakasimama juu ya miguu yao; na hofu kuu ikawaangukia watu waliowatazama.[12] Wakasikia sauti kuu kutoka mbinguni ikiwaambia, Pandeni hata huku. Wakapanda mbinguni katika wingu, adui zao wakiwatazama. [13]Na katika saa ile palikuwa na tetemeko kuu la nchi, na sehemu ya kumi ya mji ikaanguka; wanadamu elfu saba wakauawa katika tetemeko lile. Na waliosalia wakaingiwa na hofu, wakamtukuza Mungu wa mbingu.**

**11:11 "siku hizo tatu u nusu"** Hili ni dokezo kutoka kwa Danieli na ni kipindi cha mfano cha mateso. Angalia maelezo kamili katika Ufunuo 11: 9.

◙**"roho ya uhai itokayo kwa Mungu ikawaingia"** Mstari huu ni dokezo kwa Ezekieli 37, bonde la mifupa mikavu. Huu ni mzaha kwenye neno la Kiebrania "*ruach*" ambalo lina maana pumua, upepo, na roho (kama vile lilivyo neno la Kigiriki *pneuma*).

**MADA MAALUMU: ROHO KATIKA BIBLIA ( SPECIAL TOPIC: SPIRIT IN THE BIBLE)**

**11:12 "Wakasikia sauti kuu kutoka mbinguni ikiwaambia, Pandeni hata huku"** Wengine wanauona unyakuo wa siri wa Kanisa katika Ufunuo 4: 1 ambao katika huo Yohana aliitwa mbinguni, wengine wanuaona hapa siri za dhiki ya kati za Kanisa kama mashahidi hawa wawili wanaitwa mbinguni katika aya hii. Hapa tena dhahanio yetu na thiolojia zinaongoza kuelezea fasiri za kitaswira, maandiko yaliyopinda!

◙ **"Wakapanda mbinguni katika wingu"** Huu ni usafiri wa kiungu. Masihi alipanda katika mawingu ya mbinguni katika Dan.7:13. Yesu alipanda mbinguni katika mawingu (kama vile Mdo. 1: 9). Yesu atarudi akiwa katika mawingu ya mbinguni (kama vile Mathayo 24:30, 26:64, Marko 13:26, 1 Wathesalonike 4:17, Ufunuo 1: 7; 14:14).

**11:13 " Na katika saa ile palikuwa na tetemeko kuu la nchi, na sehemu ya kumi ya mji ikaanguka"** Kuna marejeo saba katika Ufunuo katika tetemeko la ardhi (kama vile Ufunuo 6:12; 8: 5; 11: 13,19; 16:18). Hili linaonyesha

hukumu zilizopo, zinazoendelea, hukumu ndogo ya Mungu kwa wasioamini. Hii inaweza kuwa dokezo kwa Ezek. 38: 17-23.

◙ **"Na waliosalia wakaingiwa na hofu, wakamtukuza Mungu wa mbingu"** Kumekuwa na majadiliano mengi juu ya utambulisho wa neno "wengine." Inaweza kurejelea kwa

1. wenyeji halisi wa Yerusalemu (kama vile Zekaria 12:10) au Rumi
2. wale ambao wanaokolewa wakati wa dhiki, yaani, wale wanaotubu kweli
3. Wayahudi waaminio, kutoka katika Warumi 11
4. Watu, kama Nebukadreza na Koreshi, ambao walishangazwa na matendo vya Mungu, lakini hawakuwa waongofu kweli.

Kwa sababu ya Ufunuo 9: 20-21; 14: 7-8 na 16:10, # 4 ndilo chaguo bora zaidi.
Hata hivyo, katika Ufunuo 16: 9, kutoa utukufu kunahusiana na toba. Kwa hakika inawezekana kwamba hawa (Wayahudi au wapagani) waliamini! Hili ndilo dhumuni la Mungu lililoelezea la hukumu (kama vile. Ufunuo 9: 20-21; 16: 9,11)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 11:14**
**14 Ole wa pili umekwisha pita, tazama ole wa tatu unakuja upesi.**

**11:14** Huu ni mpango wa mpito (kama vile Ufu. 9:12; 12:12).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 11:14-16**
**15 Malaika wa saba akapiga baragumu, pakawa na sauti kuu katika mbingu, zikisema, Ufalme wa dunia umekwisha *kuwa ufalme* wa Bwana wetu na wa Kristo Wake, naye atamiliki hata milele na milele. 16 Na wale wazee ishirini na wanne waketio mbele za Mungu katika viti vya enzi vyao wakaanguka kifulifuli, wakamsujudia Mungu**

**11:15 "Ufalme wa dunia"** KJV na NKJV zina "falme za dunia hii." WINGI haupo katika machapisho yoyote ya kale ya Kiyunani.

◙ **"umekwisha *kuwa*"** Hii ni KAULI YA KATI (shahidi wa maandishi) YENYE KUARIFU YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Haya ni maelezo ya mwisho ya utawala wa serikali za binadamu zilizoanguka na mwanzo wa utawala wa Mungu wetu (kama vile 12:10). Wakati mpya wa Roho umewadia kikamilifu. Hiyo inathibitisha theolojia ya nadharia kuwa ujio wa haraka wa mara ya pili kutatokea mwishoni mwa kila mzunguko wa tatu wa hukumu: mihuri (kama vile Ufunuo 6: 12-17), baragumu (kama vile Ufunuo 11: 15-18), na bakuli (kama vile Ufunuo 19). Ufunuo hauko katika utaratibu wa kihistoria, uwiano, bali uwasilishaji mkubwa katika mizunguko saba, kila mmoja akikizamia kipindi hicho, lakini muhuri, tarumbeta, na bakuli katika kiwango cha juu kuimarishwa hukumu (1/4, 1/3, kamili) .

◙ **" Bwana wetu na wa Kristo Wake "** Angalia jinsi Baba na Mwana wanavyounganishwa kwa ukaribu (kama vile Zaburi 2). Angalia, pia, kwamba msisitizo wa 1 Kor. 15: 24-28 na Efe.5: 5 sasa umetimizwa. Wengine wanaona msukumo kwa Zak. 14: 9 ambao unawezekana kwa sababu vyanzo pendelewa vya Yohana vyenye picha za matukio ya siku ya mwisho katika Danieli, Ezekieli na Zakaria.

◙**" naye atamiliki hata milele na milele"** Hii inarejelea kwenye utawala wa milele wa Mungu wetu (kama vile Kut. 15:18, Zaburi 10:16; 29:10, Isaya 9: 6-7, Dan 2:44; 4:34; 7:14, Lk 14: 9, Luka 1:33, 1 Wathesalonike 4:17, 2 Pet 1:11), si utawala wa milenia (kama vile Ufunuo 20) wa Kristo. Huu ni utimizaji wa sala ya Yesu katika Mt. 6:10 ili mapenzi ya Mungu yatendeke duniani kama ilivyo mbinguni.

Ufalme wa Mungu ni jambo kuu katika Injili na katika Ufunuo. Kuna sintofahamu na mvutano kati ya hali halisi ya sasa kuwa (Yesu atarudi tena baada ya utawala wa miaka 1000 na Yesu atatawala hapa duniani miaka 1000 ) na matumizi yake ya baadaye ( historia ya utawala wa kanisa kabla ya miaka 1000 na utawala wa mwanzo wa kanisa kabla ya miaka 1000). Ufafanuzi huo huo pia umekitwa kati ya kipengele chake cha kidunia (miaka elfu ya utawala wa Kristo) na kipengele chake cha umilele. Wachapishaji, wanazuoni, na madhehebu hukaa kwenye kipengele kimoja cha maelezo, lakini hawajui au huwapuuza wengine ili kufanana na dhanio zao na mifumo ya kitheolojia. Ni vigumu kwa watu wa magharibi kuelewa usafi, mfano, na mvutano wa maandiko ya mashariki, hasa aina yake ya matukio ya siku ya mwisho. Mungu wetu na Kristo wake wamewatawala, unawatawala na utawatawala; maelezo haya ya kina ni muhimu! Kunaweza kuwa na utawala wa Kimasihi duniani kwa kipindi fulani (kama vile 1 Wakorintho 15: 23-28); Israeli wa kitaifa unaweza kuwa na sehemu fulani (kama vile Warumi 11). Hata hivyo, tarakimu na alama za Ufunuo huzungumzia Kanisa zima, si Israeli (kama vile Dan 2: 34-35,44). Mimi binafsi nikafungua uwezekano wa Israeli kuwa na sehemu katika matukio ya wakati wa mwisho kwa sababu ya ahadi ya Agano la Kale kwa uzao wa Ibrahimu (kama vile Isaya 9: 6-7, Zakaria 12:10) kulingana na tabia ya Mungu (kama vile Ezek. 36: 22-38).

**11:16 "Na wale wazee ishirini na wanne"** Angalia Mada Maalumu katika Ufunuo. 4:4.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 11:17-18**
**"[17]wakisema, Tunakushukuru wewe, Bwana Mungu Mwenyezi, uliyeko na uliyekuwako, kwa sababu umeutwaa uweza wako ulio mkuu, na kumiliki. [18] Na mataifa walikasirika, hasira yako nayo ikaja, na wakati *ukaja* wa kuhukumiwa waliokufa, *na wa* kuwapa thawabu yao watumwa wako manabii na watakatifu, na hao walichao jina lako, wadogo kwa wakubwa, na wa kuwaharibu hao waiharibuo nchi."**

**11:17-18** Sala hii ya sifa imeandikwa katika muundo wa mashairi katika NKJV, NRSV, na TEV na katika mfumo wa lugha ya mjazo katika NASB na NJB. Maonyesho haya ya sala na sifa mara nyingi ndiyo fasiri bora ya maono yaliyotangulia (pamoja na nyimbo na fasiri za kimalaika).

**11:17 " Bwana Mungu Mwenyezi"** Hili linarejelea sifa tatu kuu za Agano la Kale kwa Mungu.
1. YHWH, Mungu wa agano kama Mwokozi (kama vile Kut. 3:14, Zaburi 103)
2. Elohim, Mungu Muumba kama mtoa huduma na mstahili (kama vile Mwanzo 1: 1; Zaburi 104)
3. El Shaddai (kama vile 1: 8), Mungu mwenye nguvu au mwenye huruma ambalo lilikuwa jina la mzee kiongozi mkuu wa familia kwa uungu (kama vile Kut. 6: 3)

Angalia MADA MAALUMU: MAJINA YA UUNGU ( SPECIA TOPIC: NAMES FOR DEITY) katika Ufu. 1:8.

**NASB"aliyepo na aliyekuwapo"**
**NKJV"Yeye aliyepo na aliyekuwapo na ajaye"**
**NRSV"aliye na aliyekuwapo"**
**TEV"Yeye aliyepo na aliyekuwako"**
**NJB" Aliyeko na Aliyekuwako"**

Tambua kwamba kipengele cha baadaye cha maelezo haya ya kawaida ya Mungu (isipokuwa kwa karne ya kumi na sita ya mwongozo wa maandishi ya Kiyunani ya herufi ndogo) yamesalia nje kwa sababu Mungu ameanza kutawala. Mwisho wa mambo haya matatu ya mfululizo hautatajwa tena katika kitabu cha Ufunuo. Ufalme umekuja (kama vile 11: 15-16)! Hii inatoa ushahidi kwamba nadharia ya kuelezea tena kwa ufupi juu ya uhusiano kati ya mihuri, tarumbeta, na vinara ni kweli!

**NASB" kwa sababu Umeuchukuwa uweza Wako ulio mkuu, na kuanza kumiliki"**
**NKJV" kwa sababu umeutwaa uweza wako ulio mkuu, na kumiliki"**
**NRSV"maana umeutwaa uweza wako mkuu na kuanza kumiliki"**

**TEV"kwa sababu umeutwaa uweza wako mkuu na umeanza kumiliki"**
**NJB"Kwa kuchukuliana na uweza wako mkuu na kuuanza utawala wako"**

Hii ni KAULI TIMILIFU TENDAJI YENYE KUARIFU ikifuatiwa na KAULI TENDAJI YENYE KUARIFU YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Uweza daima umekuwa ni Wake, bali utawala Wake umeanza sasa (MWINGILIO WA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU)

**11:18 "Na mataifa walikasirika"** Hili ni dokezo kwa Zab. 2; 46: 6; na Ezekieli 38-39 (na uwezekano wa utangulizi wa matukio ya siku ya mwisho kwa Esta katika maandiko ya agano la kale). Hasira hii ya mataifa inaweza kutazamwa kwa njia mbili.

1. mfumo wa ulimwengu ulioanguka unamchukia Mungu na mipango Yake na utawala Wake na watu wake
2. Kutakuwa na uasi wa wakati wa mwisho dhidi ya Mungu unaohusika na vita (Har-Magedoni, kama vile Ufunuo 20)

◙ **"hasira yako nayo ikaja"** Hii inaweza kuwa dokezo kwa Zab. 2 au 110: 5-6. Hili ni neno la Kiyunani *orgē*. Angalia maelezo kamili katika Ufunuo 7:14.

◙**" na wakati *ukaja*"** Siku ya Bwana ni siku ya hukumu kwa baadhi na tuzo kwa wengine. Mambo haya mawili yanaweza kuonekana katika Mt. 25: 31-46 na Ufu. 20: 11-15. Watu wote (wadogo kwa wakuu) siku moja watasimama mbele za Mungu na kutoa hesabu ya maisha yao (kama vile Gal 6: 7, 2 Wakorintho 5:10).

**MADA MAALUMU: SIKU HIYO (SPECIALTOPIC: THAT DAY)**

◙ **"na wakati *ukaja* wa kuhukumiwa waliokufa"** Hukumu ya wakati wa mwisho wa Mungu inajadiliwa katika Mathayo 25 na Ufunuo 20. Kifungu hiki kinathibitisha tafsiri ya Ufunuo katika matendo saba (matukio) ambapo mwisho wa wakati hutokea baada ya kila kitengo (hasa wazi katika muhuri, baragumu na bakuli).

◙**"watumwa wako manabii"** Maneno haya halisi yanaonekana katika Ufunuo 10: 7. Yohana anajitambulisha kama nabii na kitabu chake cha unabii, kwa hiyo, neno hili hutumiwa mara nyingi katika kitabu cha Ufunuo. Inaweza karibu kusemekana kwamba neno hili linachukua nafasi ya sifa "mtume" (kama vile 10: 7, 11: 10,18; 16: 6, 18: 20,24; 22: 6,9). Angalia Mada Maalum: Unabii wa Agano Jipya katika Ufunuo 16: 6.

◙ **"watakatifu"** Neno "watakatifu" linamaanisha nafasi ya waumini katika Kristo, sio kutokuwa na dhambi. Inapaswa pia kuelezea mfanano wao endelevu na ukristo. Daima neno lilikuwa WINGI isipokuwa kwa Flp. 4:21. Hata hivyo, hata katika hali hii ilikuwa katika shirika. Kuwa Mkristo ni kuwa sehemu ya jamii, familia, mwili. Angalia MADA MAALUMU: WATAKATIFU (SPECIALTOPIC: SAINTS) katika Ufunuo 5:8. Jina hili hakika linawakilisha watu wa Mungu wa Agano Jipya, yaani kanisa.

◙**"wadogo kwa wakubwa"** Inaonekana kuwapo makundi mawili tu yaliyotajwa katika aya hii, manabii na watakatifu. Neno hili "wadogo kwa wakubwa" hupatikana katika Ufunuo 19: 5. Ilikuwa ni maonyesho ya kupendeza katika Injili ya Yohana (taz. Ufunuo 13:16; 19: 5,18; 20:12; 19: 5 inaelezea Zaburi 115: 13, ambao ilikuwa ni pamoja na kundi lolote).

◙ **"kuwaharibu hao waiharibuo nchi"** Tabia hii ya ubinadamu ulioanguka inaaksi Mwanzo 3 na Rum. 8: 18-22. Waovu huruhusu tamaa na kujitegemea kimatumizi, manyanyaso, na kuvitumia viumbe viumbe vya Mungu vibaya.

Hii inaweza kutafsiriwa kama watu waovu ambao wanamlazimisha Mungu kuleta hukumu duniani (mafuriko, Mwanzo 6-9, mateso ya Misri, Kutoka 7-12, laana ya agano, Kumbukumbu la Torati 27-28, au ardhi iliyoharibiwa na moto, 2 Pet 3:10). Katika Ufunuo, muhuri huharibu 1/4, baragumu 1/3, na bakuli jumla ya uharibifu wa kiasili wa dunia.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 11:19**
**19 Kisha Hekalu la Mungu lililoko mbinguni likafunguliwa, na sanduku la agano Lake likaonekana ndani ya**

**hekalu Lake. Kukawa na umeme, na sauti, na radi, na tetemeko la nchi, na mvua ya mawe nyingi sana.**

**11:19 "Hekalu la Mungu lililoko mbinguni likafunguliwa"** Kumbuka kwamba maono haya yalianza na mlango kufunguliwa mbinguni (kama vile Ufunuo 4: 1; 15: 5). Sasa, mahali patakatifu pa ndani sana pa Hekalu la mbinguni la Mungu panaweza kuonekana (kama vile Waebrania 8: 5; 9: 23-28).Yesu alipokufa, pazia la Hekalu lilipasuka kutoka juu mpaka chini, kuonyesha kwamba kumfikia Mungu kulikuwa wazi kwa wote kupitia Kristo (kama vile Mathayo 27:51, Marko 15:38, Luka 23:45; 9: 8; 10:20). Ishara hiyo hiyo inarudiwa hapa. Mungu hupatikana kwa wote. Mahali patakatifu pa ndani pa mbinguni pako sasa wazi na panayoonekana.

◙ **"sanduku la agano Lake"** Sanduku la agano lilipotea wakati fulani wakati wa Uhamisho wa Babeli (au kwa Farao Shishak wa Misri, kama vile 1 Fal 14:25). Ilikuwa mfano wa uwepo wa Mungu baada ya kuvuka Israeli Mto Yordani kwenda Nchi ya Ahadi. Pia ilikuwa mfano wa ahadi za agano la Mungu, ambazo zinaweza kumaanisha siri (kama vile Ufunuo 10: 7), mpango wa Mungu wa ukombozi kwa wanadamu wote (kama vile Warumi 16: 25-26). Katika Agano la Kale tu Kuhani Mkuu anaweza kukabiliana na makala hii ya samani takatifu, mara moja kwa mwaka katika Siku ya Upatanisho (kama vile Law. 16). Sasa, watu wote wa Mungu wanaweza kuja mbele ya Mungu.

◙ **" umeme, na sauti, na radi, na tetemeko la nchi, na mvua ya mawe nyingi sana"** Hii ni sawa na Ufunuo 8: 5 na 16: 18-21, ambayo inaaksi Kut. 9:24 na 19: 16-19.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa usomaji wa hitifaki, ambayo inamaanisha kwamba unao wajibu wa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu lazima aenende katika nuru tuliyo nayo. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Unalazimika kutokuondoa hili toka kwa msemaji.

Maswali haya ya majadiliano yanatolewa ili kukusaidia kufikiri kupitia maswala makuu ya sehemu hii ya kitabu. Yamekusudiwa kuwa chanzo cha uchochezi wa mada, lakini siyo hakika.

1. Nini kusudi la kuliingilia kati hili?
2. Kwa nini watafsiri wengi wanajaribu kumtambua malaika katika sura ya 10 na Kristo?
3. Ni siri gani ya Mungu iliyotajwa katika Ufunuo 10: 7?
4. Lipi Jina la kitabu kidogo ambacho Yohana aliamuliwa kukila?
5. Mashahidi wawili ni akina nani? Ujumbe wao ulikuwa ni nini?
6. Je, Ufunuo 11: 9 unaelezea mji wa Yerusalemu au falme za ulimwengu zenye kumpinga Mungu? Kwa nini?
7. Andika orodha ya miingiliano yote ya Agano la Kale katika hali hii.

# UFUNUO 12

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **USB[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Mwanamke na lili Joka kuu | Mwanamke, mtoto na lile joka | Ule mtazamo wa mwanamke, mtoto Na lile joka kuu | Mwanamke na lile joka kuu | Ule mtazamo wa mwanamke na lile joka kuu |
| 12:1-6 | 12:1-16 | 12:1-6 | 12:1-2 | 12:1-6 |
| | Shetani alifukuzwa kutoka Mbinguni | | 12:1-6 | |
| 12:7-12 | 12:7-12 | 12:7-9 | 12:7-9 | 12:7-12 |
| | Mwanamke Ateswae | 12:10-12 | 12:10-12 | |
| 12:13-17 | 12:13-17 | 12:13-17 | 12:13-18 | 12:13-17 |
| Wale wanyama Wawili | Mnyama aliyetoka Baharini | Wale wanyama wawili | Wale wanyama wawili | Joka kuu jekundi ampaye mnyama Uweza |
| 12:18 | 12:18 | | 12:18 | 12:18 |
| 13:1-4 | 12:1-10 | 13:1-4 | 13:1-4 | |
| 13:5-8 | | 13:5-8 | 13:5-8 | |
| 13:9-10 | Mnyama asimamae Juu ya mchanga wa Bahari | 13:9-10 | 13:9-10 | Manabii wa uwongo kama watumwa wa yule mnyama |
| 13:11-18 | 13:11-18 | 13:11-18 | 13:11-17<br>13:11-18 | 13:11-17<br>13:11-18 |
| Wimbo wa wale 144,000 | Mwana kondoo na wale 144,000 | Vile vipindi vya mapumziko | Mwana kondoo na watu wake | Huruma ya Mwana kondoo |
| 14:1-5 | 14:1-5 | 14:1-5 | 14:1-5 | 14:1-5 |
| Habari ya wale Malaika watatu | Mfuatano wa malaika watatu | | Malaika watatu | Malaika watangaza siku ya hukumu |
| 14:6-7 | 14:6-13 | 14:6-7 | 14:6-7 | 14:6-7 |
| 14:8 | | 14:8 | 14:8 | 14:8 |
| 14:9-12 | | 14:9-11 | 14:9-11 | 14:9-12 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 14:12 | 14:12 | |
| 14:13 | | 14:13 | 14:13 | |
| | | | 14:13b | |
| Mavuno ya nchi | kukomaa kwa mavuno Ya nchi | | mavuno ya nchi | Mavuno na kile kipindi cha mataifa |
| 14:14-16 | 14:14-16 | 14:14-16 | 14:14-16 | 14:14-16 |
| | | | 14:17-20 | |
| | Kuvuna matunda Ya ghadhabu | | | |
| 14:17-20 | 14:17-20 | 14:17-20 | 14:17 | 14:17-20 |
| | | | 14:17-20 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Angalia **Semina ya Ukarimani wa Biblia (Bible Interpretation Seminar)**

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa usomaji wa hitifaki, ambayo inamaanisha kwamba unao wajibu wa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu lazima aenende katika nuru tuliyo nayo. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Unalazimika kutokuondoa hili toka kwa msemaji.

Soma sura katika mkao mmoja. Yatambue masomo. Linganisha mgawanyiko wa mada zako kwa ulinganifu wa tafsiri tano za hapo juu. Aya haijavuviwa, lakini ni ufunguo wa kufuata kusudi la msingi wa mwandishi, ambao ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya inayo moja na katika hilo ni somo moja tu.

13. Aya ya kwanza
14. Aya ya pili
15. Aya ya tatu,
16. Nk.

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA UFUNUO 12:1-17

A. Uwazi mwingine unaanza katika Ufu. 12:1 na kundelea hadi Ufu. 14:20. Huu mtiririko mwingine wa namba saba. Kitengo hiki cha fasihi huelezea mgoogoro wa kiroho katika uwili wa maneno kati ya
   1. Falme mbili
   2. miji miwili
   3. mashahidi wawili wa mauaji na wale wauaji
B. Mistari ya 1-6 inaeleza juu ya yale (ya kiulimwengu) mapambano ya milele baina ya mema na mabaya katika maneno ya kimafumbo yaliyochukuliwa kutokana na tamaduni za Mashariki ya Karibu ya Kale (kama vile Grant Osborne, *The Hermeneutical Spiral* uk. 229).
   1. Maelezo ya usanifu wa Babeli—Tiamat (machafuko), myama mkubwa mwenye vichwa saba aliyeangusha theluthi ya nyota za mbinguni, dhidi ya Marduk, mkuu wa mungu wa mji wa Babeli, muuaji na aliyekuwa mkuu wa hekalu la miungu yote.
   2. Simulizi za kale za Kimisri—Set (Kimbunga), joka kubwa mwekundu dhidi ya Isis (Hathor), aliyemzalia Horus. Huyu baadaye alimuua Set.
   3. Hekaya za Baal mwenye makazi huko Ugarit—Yam (maji) dhidi ya Ba'al. Ba'al aliyeuawa kwa Yam.

4. Similizi za kale zi Kiajemi—Azhi Dabaka (joka la uovu) dhidi ya mwana wa Ahura Mazda (mungu mzuri na mkuu).
5. Simulizi za kubuni za Kiyunani—Chatu (joka/mnyama wa baharini) dhidi ya Leto yule mjazamzito (mama wa Apolo, ambaye alimuua yule Chatu).

C. Ni vigumu kutambua namna ya kuifasiri sura hii. Wengine wanajaribu kuifasiri sura hii katika maneno ya kihistoria, lakini hii kwangu inaonekana kuwa mapambano ya kiishara baina ya zile falme za zama hizi zilizo kinyume na Mungu na zile zama za ufalme mpya wa Kristo wetu (kama vile Ufu. 11:18; Zaburi 2). Hivyo, hii iko pande zote yaani dokezo la kihistoria kuhusiana na kuzaliwa kwa Kristo na ule msistizo kuhusiana na ule ujio wa ufalme wa ki-Masihi. Huu ni uwili wa mtu na (Masihi) kundi (watu wa Mungu) dhidi ya yule mtu (Ibilisi) na lile kundi (kupagawa kwa wale wasio amini). Uwili huu unaofanana unaonekana katika Nyimbo za Mtumishi Isaya. Huyu mtumishi ni taifa la Israeli (kama vile Isa. 41-50), pia bado ni Masihi (kama vile Isa. 52:13-53:12).

D. Paulo aunajadili utawala wa kiulimwengu wa Kristo katika Wakorintho 1-2 (pia nukuu Ebr. 1:2-3).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 12:1-6**

[1] **Na ishara kuu ilionekana mbinguni; mwanamke aliyevikwa jua, na mwezi ulikuwa chini ya miguu yake, na juu ya kichwa chake taji ya nyota kumi na mbili.** [2] **Naye alikuwa ana mimba, akilia, hali ana utungu na kuumwa katika kuzaa.** [3] **Ikaonekana ishara nyingine mbinguni; na tazama, joka kubwa jekundu, alikuwa na vichwa saba na pembe kumi, na juu ya vichwa vyake vilemba saba.** [4] **Na mkia wake wakokota theluthi ya nyota za mbinguni, na kuziangusha katika nchi. Na yule joka akasimama mbele ya yule mwanamke aliye tayari kuzaa, ili azaapo, amle mtoto wake.** [5] **Naye akazaa mtoto mwanamume, yeye atakayewachunga mataifa yote kwa fimbo ya chuma. Na mtoto wake akanyakuliwa hata kwa Mungu, na kwa kiti chake cha enzi.** [6] **Yule mwanamke akakimbilia nyikani, ambapo ana mahali palipotengenezwa na Mungu, ili wamlishe huko muda wa siku elfu na mia mbili na sitini.**

**12:1 "Na ishara kuu ilionekana mbinguni"** Huu ndiyo mwanzo wa zile "ishara saba" za Ufunuo. Hili neno maalumu la kitheolojia (*sēmeion*) linalotumika mara nyingi katika Injili ya Yohana (kama vile Yohana 2:11,23; 3:2; 4:54; 6:2,14,30; 7:31; 9:16; 10:41; 11:47; 12:18,37; 20:30). Na sasa limeonekana mara saba kati ya Ufu. 12:1 na 9:20—ishara mara tatu huko mbingini (kama vile Ufu. 12:1,3; 15:1) na ishara mara nne duniani (kama vile Ufu. 13:13,14; 16:14; 19:20).

◙ **"mbinguni"** Bila shaka hii inamaanisha "juu mawinguni" na si mbingini kwenyewe. Hili neno mbingu katika Agano la Kale linaweza kurejelea mazingira ya juu ya uso wa dunia (kama vile Mwa. 1:1,8-9,17,20; Zab. 104:2-3) au mahali ambapo Mungu anaishi (kama vile Zab. 11:4; 103:19; Isa. 66:1; 2 Korintho 12). Huu utata ni ule unaosababishwa na walimu wa sheria za Kiyunani kukisia idadi ya mbingu—tatu au saba.

MADA MAALUM: MBINGU NA MBINGU YA SABA (SPECIAL TOPIC: THE HEAVENS AND THE THIRD HEAVEN)

◙ **"mwanamke aliyevikwa"** Mwanamke huyu ni yule anayeelezwa kuwa mzuri sana, kinyume na yule kahaba mkuu wa Ufu. 17:4 mwenye kuashiria tawala za ulimwengu za wale wampingao Mungu kama vile Babeli, Roma, na ule mfumo wa ulimwengu wa wapinga Kristo. Kumekuwa na nadharia mbili kuhusiana na kile chanzo cha Yohana kutumia tamathali za semi katika semi zake:

1. Mwanzo 3, ambapo kuna mwanamke, joka kubwa na kijana wa kiume
2. dokezo zingine za neno "kuzaliwa" katika Agano la Kale (kama vile Isa. 26:17-18 katika Maandiko ya Agano la Kale na Isa. 66:7-13)

Israeli inaelezwa kama mwanamke azaaye (kama vile Mik. 4:10), hivyo, huyu mwanamke anawakilisha watu wa Mungu walio wa kweli (kama vile Ufu. 12:1-6), lakini katika Ufu. 12:13-17 huyu atakuwa wale watu wa Mungu wa

Agano Jipya walioikimbia ile hasira kali ya lile joka kubwa. Kwa nadharia nyingine angalia Alan Johnson's *Revelation*, kr. 117-119.

Katika kitabu cha *Answers to Questions* F. F. Bruce anasema, "Mwanamke ambaye naweza kufikiria kumhusu kama yule wa jumuiya kimasihi au ile 'Israeli ya Mungu' hasa yule aliyedhihirishwa katika eneo la kanisa la Palestina, kanisa mama kwa uzuri; . . . Yale 'mabaki ya uzao wake' yatakuwa wale Wakristo katika sehemu zingine za dunia, mwenye shabaha ya mashambulizi katika Ufu. 13:7" (uk. 140).

Katika *New Bible Commentary* George R. Beasley-Murray anasema, "Watu wa dini wa ulimwengu wa kale wangeweza kuonekana katika utungu wa mwanamke Mungu wa kike aliyevikwa taji la nyota kumi na mbili za ule mhimili; Myahudi ye yote angeweza kumwelewa kama Mama wa Sayuni (tazama Isa. 26:16; 27:1; 49:14-25; 54:1-8; 66:7-9), lakini kwa Yohana huyu anawakiisha yule 'Mama' wa jamii ya Kimasihi, watu wa Mungu wanaoamini wa yale maagano ya kale na yale mapya" (uk. 1441).

◙**"nyota kumi na mbili"** Hapa tena makisio yetu yanaikazia fasiri yetu.

1. ikiwa ni Agano la Kale hii pia linarejelea kwa yale makabila kumi na mawili ya Kiyahudi
2. ikiwa ni kipindi cha utumiaji wa fasihi katika kuyafunua maandiko ya Agano la Kale na Agano Jipya, aya hii inarejea juu ya zile ishara za nyota
3. ikiwa ni katika Agano Jipya hii aya inarejelea juu ya wale Mitume kumi na wawili

Kumi na mbili ni ishara ya kawaida ya kibiblia ya namba ya ushirika

Hata hivyo, ile maana ya sura ya 12 haikuwekewa masharti ya ule utambuzi sahihi wa zile ishara zilizotumiwa na Yohana, bali kile kiini cha ule muktadha wa ile kweli. Hii kanuni yapaswa kutunzwa. Hutupaswi

1. kuhojihoji undani wake
2. kuchagua mambo mengine kifasihi na kishara
3. kuzilazimisha fasiri zetu katika mazingira yetu ya kihistoria

Mada Maalum: Hesabu Kumi na Mbili (Special Topic: The Number Twelve)

**12:2** Utungu wa kuzaa ulitumika kama ishara ya

1. matukio yaliyotarajiwa, lakini maitikio ya ghafla
2. yale maumivu au matatizo yanayohusiana na tukio
3. mwanzo wa kitu kipya chenye umuhimu mkuu

Wayahudi waliamini kwamba ule ujio wa zile "zama mpya" ungehusisha ule usumbufu na matatizo (kama vile Isa. 13:8; 21:3; 26:17; 66:7-13; Mt. 24:8; Marko 13:8; 1 The. 5:3). Yohana anaitumia dhana hii kubainsha mgogoro kati ya Ibilisi na wafuasi wake na Mungu na wafuasi wake (kama vile Isa. 66:7-24).

Matukio ya kiulimwengu yanazidi kuwa mabaya na mabaya zaidi, lakini Mungu yuko juu ya historia (huu ni mtazamo wa kabla ya ile miaka elfu ya utawala na baraka za Kristo na kile kipindi cha kufanya kila jambo katika upendo, ambapo Mafundisho yanayohusu Ujio wa pili wa Kristo kama kilele cha unabii wa ile miaka elfu ya utawala wake, ambayo katika baraka ni ya kimatumaini zaidi kuhusiana na historia ya ulimwengu). Wafuasi wake wamezingirwa dhidi ya yale masumbufu na ushindi dhidi ya ule ushindi wa muda mfupi, hata kifo cha mwili (kama vile Yohana 16:20-21). Swali ni kwamba, "Ni kwa jinsi gani Mungu atawalinda wafuasi wake?" Muhuri wake juu paji za nyuso zao huwalinda dhidi ya uharibifu "ile ghadhabu kali ya Mungu," lakini si katika yale masumbufu ya wale wasioamini (mateso). Mungu yu kwa ajili yao, yuko nao, na anawapenda, lakini wengi wataangamia!

Mada Maalumu: Utungu wa Kuzaa wa Zama Mpya (Special Topic: Birth Pains of the New Age)

**12:3 "joka kubwa jekundu, alikuwa na vichwa saba na pembe kumi, na juu ya vichwa vyake vilemba saba"** Huu ni ufafanuzi wa uovu na ile nguvu kubwa (kama vile 13:1 na 17:3). Zile pembe na vile vichwa huashiria nguvu kamili (kama vile Danieli7) na vilemba huwakilisha jitihada za yule mwovu za kuutwaa ufalme wa Kristo.

Hili neno "joka kubwa" linaweza kurejelea juu ya Agano la Kale

1. yule nyoka wa Mwanzo 3
2. majitu mawili ya kutisha ya machafuko
    a. Rahabu (kama vile Zab. 89:10; Isa. 51:9-10)
    b. Lewithani (kama vile Zab. 74:13-14; 104:26; Ayubu 3:8; 7:12; 41:1; Isa. 27:1; Amosi 9:3)
3. Kuna majina mbalimbali ya yule mwovu anayepatika katika Agano Jipya
    a. "Ibilisi," limetuka mara 33
    b. "Shetani," limetumika mara 32
    c. "Mjaribu," (kama vile Mt. 4:3; 1 The. 3:5)
    d. "yule mwovu," (kama vile Mt. 6:13; 13:19; 1 Yohana 5:18)
    e. "Adui," (kama vile Mt. 13:39)
    f. "Mkuu wa Mapepo," (kama vile Mt. 9:34; 12:24)
    g. "Mkuu wa Ulimwengu huu," (kama vile Yohana 12:31; 14:30; 16:11)
    h. "Mfalme wa uwezo wa anga," (kama vile Efe. 2:2)
    i. "Mungu wa dunia hii," (kaamvile 2 Kor. 4:4)
    j. "Beliari," (kama vile 2 Kor. 6:15)
    k. "Beelzebuli," (kama vile Marko 3:22; Luka 11:15,18-19)
    l. "Joka kubwa," (kama vile Ufu. 12:3,4,7,9; 20:2)
    m. "Joka," (kama vile Ufu. 12:9,15; 20:2)
    n. "Mshtaki," (kama vile Ufu. 12:10,15)
    o. "Mshtaki," (kama vile 1 Pet. 5:8)
    p. "simba angurumaye," (kama vile 1 Pet. 5:8)

MADA MAALUM: SHETANI (SPECIAL TOPIC: SATAN)

**12:4 "Na mkia wake wakokota theluthi ya nyota za mbinguni, na kuziangusha katika nchi"** Kwa sababu ya hili neno "nyota za mbinguni" mara nyingi linatumika kwa uficho katika Agano la Kale kurejelea juu ya watakatifu wa Mungu (kama vile Mwa. 15:5; Yer. 33:22; Dan. 12:3), wengine wamedhani kuwa hili neno linarejelea juu ya watakatifu, lakini muktadha wake unaweza kuwarejelea malaika (kama vile Dan. 8:10; 2 Pet. 2:4; Yuda 1:6). Malaika walioanguka (yaani, nyota zilizoanguka) ni kipengele muhimu katika fasihi ya Kitabu cha Ufunuo (kama vile I Enock).

Shetani anawakilishwa na wale malaika wa mbinguni mbele ya Mungu katika Ayubu 1-2 na Zekaria 3. Bila shaka huyu alikuwa "kerubi afunikaye" (kama vile Eze. 28:12-18). Ubainifu huu, unaotumia stiari inayotokana na ile Bustani ya Edeni, si sawa na ile ya Mfalme wa Tiro, bali yale majivuno na kiburi kilichoigwa na Shetani (Nimekuwa nikiumizwa sana na mtazamo huu kwa sababu katika Ezekieli 31 yule mfalme wa Misri anaelezwa kama mti wa ujuzi wa mema na mabaya.Kwa kawaida Ezekieli anatumia maneno Edeni kueleza juu ya wafalme). Katika Agano la Kale Shetani ni adui wa Mungu, lakini wa mwanadamu pia (kama vile 12:10). Ibilisi hakuumbwa kama mwovu bali amejengwa katika sura ya ule mti wa uadui wa mambo yote yaliyo mema na matakatifu (kama vile A. B. Davidson's *An Old Testament Theology,* kr. 300-306). Mara kadhaa huyu ametajwa kufukuzwa mbinguni (kama vile Isa. 14:12; Eze. 28:16; Luka 10:18; Yohana 12:31; na Ufu. 12:9,12). Tatizo ni lini. Hiki ni:

1. kile kipindi cha Agano la Kale
    a. kabla ya uumbaji wa mwanadamu
    b. wakati mwingine baada ya Ayubu lakini kabla ya Ezekieli 28
    c. kipindi baada ya kutoka utumwani, lakini baada ya Zakaria

2. kile kipindi cha Agano Jipya
    a. Baada ya majaribu ya Yesu (kama vile Mathayo 4)
    b. kipindi cha safari ya umisheni wa wale sabini (kama vile Luka 10:18)
    c. katika zile nyakati za mwisho zenye uasi unaokaribia (kama vile Ufu. 12:9).

Mtu anaweza kushangaa ikiwa theruthi ya nyota hurejea juu ya wale malaika waliomwasi Mungu na kuchagua kumfuata Shetani. Ikiwa ni hivyo, huu unaweza kuwa msingi pekee wa maandiko ya Agano Jipya yanayoeleza juu ya wale pepo wabaya na namna yanavyohusiana na wale malaika walionguka (kama vile Ufu. 12:9,12). Ile idadi, theruthi, inaweza kuhusishwa na ule mpaka wa uharibifu wakati wa kupiga baragumu za hukumu (kama vile Ufu. 8:7-12; 9:15,18) na si idadi maalumu. Au, inaweza kuwakilisha yale maangamizi ya Shetani ya kuikokota sehemu ya malaika katika mapambano.Pia inawezekana kuwa hili linaaksi zile simulizi za kale zinazoihusu Babeli. Angalia Tambuzi za Kimuktadha, kipengele B.
Kwa maelezo haya hili linaweza kusaidia katika kukumbuka kuwa ingawa jambo hili linatia shauku, bila shaka halikuwa kusudi la mwandishi katika muktadha huu kujadili juu ya (1) ile asili ya pepo wabaya; (2) kuanguka kwa Shetani; au (3) uasi wa kimalaika huko mbinguni. Katika Kipindi kile kati ya Agano la Kale na Agano Jipya kilichohusu udukuzi wa Matukio ya siku za mwisho hili wazo kuu lenye kubeba maono ni muhimu, lakini uhalisia wa uwasilishaji, ule undani na taswira ni wa kuvutia, ni wa kiishara, ni wa kubuni. Ni tunu na heshima kwetu kwa kuwa Biblia hutuhamasisha kwa undani, kimantiki, mafundisho yenye kuelekeza kwa usahihi. Uwe mwangalifu kutozingatia haya maelekezo; mara nyingi hiki kipindi kati ya Agano la Kale na Agano Jipya ni theolojia halisi inawasilishwa katika mfumo wa kubuni. Ni kweli, lakini iliwasilishwa kiishara!

Mada Maalum: Vita Mbinguni (Special Topic: War In Heaven)

◙ **"amle mtoto wake"** Mtoto Huyu ainamrejelea yule Masihi aliyehaidiwa (kama vile Ufu. 12:5). Ibilisi hutaka kuizuia mipango ya Mungu kwa kila namna, mipango yote ya kiulimwengu iliyo kwa ajili ya ukombozi (maagano yasiyo na masharti) na mpango binafsi wa ukombozi (maagano yenye masharti, kama vile Mt. 13:19; 2 Kor. 4:4).

**12:5 "Naye akazaa mtoto mwanamume"** Hili linaweza kuwa dokezo la Isa. 66:7-8. Tazama jinsi Yohana alivyoanza kuanzia lile umbo mwili la Yesu hadi ile hatma ya utawala wake wa zile siku za mwisho. Mambo yote ya kati yanajikita katika Injili ya Yohana, lakini si katika Ufunuo.

◙ **"yeye atakayewachunga mataifa yote kwa fimbo ya chuma"** Hili ni dokezo la Zab. 2:9 au 110:5-6 na ndilo, hivyo, ni la ki-Masihi (yaani, tazama Isa. 9:4). Katika Ufu.19:15, kifungu hiki kinatumika kumzungumzia Masihi, ambapo katika Ufu. 2:26-27 kinatumika kuwazungumzia watakatifu. Hapa kuna bubujiko baina ya Masihi (binafsi) na ile jamii ya waaminio (ushirika), kama zilivyo nyimbo za mtumishi Isaya (yaani, taifa la Israeli, kama vile Isa. 42:1-9,19; 49:1-7; 50:4-11; 52:13-53:12). Kama mwovu ayatawalavyo mataifa, ndivyo mtawala ajavyo na siku moja ataukamilisha utawala wake.

◙ **"Na mtoto wake akanyakuliwa hata kwa Mungu, na kwa kiti chake cha enzi"** Wengine wanaliona hili kama kupaa kwa Kristo, lakini tunaikosa hoja ya sehemu ya fasihi ikiwa tunayafanya kuwa dokezo lenye nguvu kuhusu historia ya maisha ya Kristo.Yohana, katika kitabu cha Ufunuo, hazungumzii maisha ya Yesu ya kidunia au kifo. Yeye anaendelea kitheolojia kuanzia umbo-mwili hadi kule kupaa kwake. Tazamio la kitabu cha Ufunuo limetukuzwa, Kristo aliyeinuliwa (kama vile Ufu. 1:4-20). Uwasilishaji wa Yohana kuihusu injili katika Ufunuo unatazamia ile toba na kule kumpa Mungu utukufu. Hili halimaanishi kuishusha hadhi kazi ya Yesu iliyo kuu (kama vile Ufu. 5:9,12; 7:14; 12:11), bali kuitazamia kazi iletayo ufalme wa milele (kama vile 1 Kor. 15:25-28); ule ufalme wa wote yaani Baba na Mwana!

**12:6 "Yule mwanamke akakimbilia nyikani"** Hapa wengi huliona lile dokezo la Kutoka na kile kipindi cha Kutanga tanga Jangwani, ambacho kinapatikana katika muktadha hii yote. Kile kipindi cha Kutanga tanga Jangwani kwa Walimu wa sheria za Kiyunani kilionekana kama kipindi cha ndoa kati ya YHWH na Israeli. Katika kipindi hiki, yeye aliwapa mahitaji yao yote na kuhusiana nao kwa ukaribu sana.

◙ **"mahali palipotengenezwa na Mungu"** Ingawa muktadha wa jumla unaaksi kile kipindi cha kutangatanga jangwani, kifungu hiki kinabeba maana nyingine za kihistoria.

1. Eliya kwenye mto Kerithi (kama vile 1 Fal. 17:1-7)
2. Safari ya Eliya kwenda rasi ya Sinai (kama vile 1 Fal. 19:1-14)

3. wale elfu saba waaminifu (kama  vile 1 Fal. 19:18)
4. wale walioukimbia uharibifu wa huko Yerusalemu mnamo miaka 70  B. K (kama vile Mt. 24:15-20; Marko 13:12-18)

◙ **"muda wa siku elfu na mia mbili na sitini"** Tena, mstari huu inaonekana kutoazimiwa, lakini ina mipaka, kipindi cha mateso. Kipindi hiki hiki cha muda kinarejelewa katika njia kadhaaa na tofauti tofauti ambazo ni sawa na miaka mitatu na nusu.

1. "nyakati mbili na nusu wakati" (kama vile Dan. 7:25; 12:7; Ufu. 12:14)
2. "nyakati za asubuhi na jioni 2,300" (kama vile Dan. 8:14)
3. "miezi arobaini na miwili" (kama vile Ufu. 11:2; 13:5); "siku1,260 " (kama vileUfu. 11:3; 12:6); "siku1,290" (kama vile Dan. 12:11); na "siku1,335" (kama vile Dan. 12:12).

Namba Saba ni namba timilifu katika taaluma ya Kiebrabia inayohusiana na tarakimu (kama vile Mwa. 1:1-2:3). Ile iliyo chini ya saba huzungumzia kule kutokamilika kwa mwanadamu na 666 (kama vile Ufu. 13:17-18) ni kule kutokamilika kwa mwanadamu milele, yule Mpinga Kristo (kama vile. 2 Thesalonike 2). Katika mwelekeo huo, miaka mitatu na nusu ni ishara ya ule mpaka, lakini usio dhahiri, kipindi cha mateso.

MADA MAALUM: MIEZI AROBAINI NA MIWILI (SPECIAL TOPIC: FORTY-TWO MONTHS)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 12:7-10a**

**7 Kulikuwa na vita mbinguni; Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka, yule joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake; 8 nao hawakushinda, wala mahali pao hapakuonekana tena mbinguni. 9 Yule joka akatupwa, yule mkubwa, nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani, audanganyaye ulimwengu wote;akatupwa hata nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye. 10 Nikasikia sauti kuu mbinguni, ikisema**

12:7 "Kulikuwa na vita mbinguni"

MADA MAALU: VITA MBINGUNI (SPECIAL TOPIC: WAR IN HEAVEN)

◙ **"Mikaeli"** Katika Biblia kuna majina ya malaika wawili (yaani,Mikaeli, Gabrieli). Huyu malaika emepewa jina kama malaika wa taifa la Israel katika Dan. 10:13,21 na 12:1. Huyu anaitwa malaika mkuu katika Yuda 1:9. Jina lake linamaanisha "aliye sawa na Mungu." Wengine huliona hili kama jina lingine la Kristo, lakini hili linaonekana kwenda mbali zaidi. Mungu haathiriwi na ule uasi wa yule aliye mwovu. Biblia haiendi katika uwili, kama ilivyo ile dini ya kale ya Uajemi iliyoamini juu ya uwepo wa Mungu mmoja. Mungu alimwondoa yule mwovu kwa kumtumia malaika (ingawa katika ukweli hii ilikuwa kazi ya Kristo kwa ajili ya ukombozi).

Katika sitiari ya kisheria, Mikaeli mwanasheria mkuu mlinzi, ambapo Shetani anatenda kazi kama mwendesha mashtaka na YHWH Mwamuzi! Mikaeli huishinda kesi kupitia

1. dhabihu ya kifo, ufufuo, na kupaa kwa Kristo (kama vile Ufu. 12:16)
2. mashahidi waaminifu wa kanisa (kama vile Ufu. 12:11b)
3. ustahimilivu wa kanisa (kama vile Ufu. 12:11c)

◙ **"yule joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake"** Ni vigumu kueleza kibiblia hawa malaika wa Ibilisi ni akinanani hasa . Wengine huwaona kama pepo wabaya (kama vile Mt. 25:41; Efe. 6:10 na kuendelea). Lakini kuna swali la mara kwa mara linaloleta usumbufu kuhusiana na wale malaika katika shimo (kama vile 2 Pet. 2:4), na wale malaika waliotajwa katika Ufu. 9:14, ambao kwa udhihirisho wanatawaliwa na Mungu lakini kwa uwazi ni malaika wa uovu.  Mgogoro zaidi katika ulimwengu wa kimalaika kimsingi haukuelezwa (kama vile Danieli 10).

Pia kuna mjadala unaoendelea kuhusiana na ule uhusiano baina ya wale malaika wa Agano la Kale walioanguka na wale pepo wa Agano Jipya. Kuhusiana na jambo hili Biblia imenyamaza. Maandiko ya matukio ya siku za mwisho kati ya Kipindi cha Agano la Kale na Agano Jipya (hasa I Enoch) yanadai kuwa wana wa Mungu, wana wa

wanadamu wa Mwa. 6:1-4 ndiyo wale pepo wachafu wa Agano Jipya waliokuwa wakitafuta kuishi ndani ya miili ya wanadamu. Haya bado ni makisio, lakini yamefanya mambo kadhaa ambayo baadhi ya Wayahudi wa karne ya kwanza waliyafikiria kulihusu somo hili.

KITENZIJINA cha WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU haionekani kuendana na muktadha huu. Bila shaka katika zile lugha za kale kama Kiebrania, Kiaramu na Kiarabu zingeweza kutafsiriwa kama "ilimbidi kupigana" (kama vile *The Expositor's Bible commentary,* juzuu. 12, "Ufunuo" na Alan Johnson, uk. 519, maelezo ya ziada kuhusiana jambo linalozungumziwa #7. Huyu ni mmoja wa watoa maoni niliopendezwa nao kuhusiana na kitabu cha Ufunuo).

**12:8** Hili ni la kwanza katika ule mtiririko wa maneno yeye msistizo kwa Kanisa lililo katika mateso. Ufu. 12:8, 11, 14 inatoa faraja kuu kwa watu wa Mungu waliokuwa wakiteswa katika karne ya kwanza na katika kila karne. Shetani alishindwa mara dufu: aliapokuwa katika juhudi za kumuua Mtoto (kama vile Ufu. 12:4) na sasa yuko katika juhudi za kukivamia kiti cha enzi cha Mungu (kama vile Ufu. 12:7-9); pia ataondoshwa katika juhudi zake za kuwangamiza watu wa Mungu walioko duniani.

◙ **"wala mahali pao hapakuonekana tena mbinguni"** Mstari huu unadokeza kwamba wakati mwingine Shetani amekuwa, mbinguni (kama vile Ayubu 1-2; Zakaria 3; na 1 Fal. 22:21). Tazama KIWAKILISHI cha WINGI, ambacho kinadokeza malaika wengine walikuwa na ushiriki na Shetani.

**12:9 "Yule joka akatupwa, yule mkubwa, nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani"** Hapa na Ufu. 20:2 (kama vile Hekima ya Suleimani 2:24), ni sehemu pekee ambapo Shetani ameelezwa kwa uwazi na yule nyoka wa Ufunuo 3 na kwa uwazi katika 2 Kor. 11:3. Neno "ibilisi" ni neno la Kiyunani lenye maana ya "mwongo," ambapo neno "Shetani" ni neno la Kiebrania lenye maana ya "adui" (kama vile 2 Sam. 19:22; 1 Fal. 11:14). Haya yote yanazungumzia juu ya kazi ya yule mwovu kama mshtaki wa ndugu zetu (kama vile Ufu. 12:10). Neno "Shetani" katika Agano la Kale si NOMINO sahihi, bali liko katika vipengele maalum vitatu: (1) Ayubu 1-2; (2) Zek. 3:1-3; na (3) 1 Nyak. 21:1. Kwa neno "alitupwa chini" angalia maelezo kamili katika Ufu. 12:4 na 7.

MADA MAALUM: UOVU BINAFSI (SPECIAL TOPIC: PERSONAL EVIL)

◙**"audanganyaye ulimwengu"** Mstari huu unaeleza kuhusu kazi ya yule mwovu. Injili ni ya kiulimwengu (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:47; Matendo 1:8), hivyo kuna wapinga injili wengi sana! Kitabu kizuri sana nilichokisoma kuhusu maendeleo ya Shetani katika Biblia, kutoka utumishi hadi uadui, ni A. B. Davidson's *A Theology of the Old Testament*, kr. 300-306. Kazi ya Shetani inaelezwa katika 2 Kor. 4:4; 1 Pet. 5:8; Ufu.13:14; 19:20; 20:3,8,10; 2 Yohana 7. Ni vigumu kumdhania Shetani kama mtumishi wa Mungu lakini linganisha 2 Sam. 24:1 na 1 Ko. 21:1.

◙ **"akatupwa hata nchi"** Neno "kutupwa chini" limetumika mara kadhaa katika muktadha huu: mara mbili katika Ufu. 12:9; katika Ufu. 12:10, na Ufu. 12:13. Pia limetumika katika Ufu. 19:20; 20:3,10,14,15 na bila shaka ni dokezo la Isa. 14:12 au Luka 10:18; na bila shaka Yohana 12:31.

Dunia imekuwa ufalme wa shughuli za Shetani. Angalia maelezo kamili kuhusiana na anguko la Shetani katika Ufu. 12:4 na 7.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 12:10b-12**
**10 Sasa kumekuwa wokovu, na nguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake; kwa maana ametupwa chini mshitaki wa ndugu zetu, yeye awashitakiye mbele za Mungu wetu, mchana na usiku. *11* Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa. *12* Kwa hiyo shangilieni, enyi mbingu, nanyi mkaao humo. Ole wa nchi na bahari! Kwa maana yule Ibilisi ameshuka kwenu mwenye ghadhabu nyingi, akijua ya kuwa ana wakati mchache tu.**

**12:10b-12** Huu ni ujumbe wa yule mwenye sauti kuu kutoka mbinguni.

**12:10 "kumekuwa wokovu, na nguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake"** Huu ni usawa wa kimaandishi kwa Ufu. 11:15-18. Mwisho umekwisha fika na Mungu ni mshindi! Hili lilisaidia sana kwa lile kundi la waamimio waliokuwa wakipitia na mateso makali, hata kifo.

◙ **"mshitaki wa ndugu zetu"** Mstari huu unaonyesha kwamba ile sauti ya Ufu. 12:10 haikiwa ya malaika, bali wale waamini kamili, bila shaka ni wale mashahidi wa Ufu. 6:9-11. Neno la Kiebrania *Satan* linamaanisha "mshtaki." Tunamuona shetani katika nafasi hii katika Ayubu 1:9-11 na Zek. 3:1.

Mada Maalum: Shetani (Special Topic: Satan)

◙ **"awashitakiye mbele za Mungu wetu, mchana na usiku"** Shetani aliyefukuzwa mbinguni bado anawashitaki wale waaminifu mbele za Mungu. Hili jambo ni aina ya sintofahamu. Utawala wake umeangushawa, lakini bado yuko makini (hata hivyo, amewekewa mipaka na Mungu. Ayubu 1-2).

**12:11 "Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao"** Ushindi umekuwako baada ya ule upatanisho wa Masihi wa Mungu (kama vile Ufu. 1:5; 7:14; 1 Pet. 1:18-19; 1 Yohana 1:7). Upatanisho huu ni pamoja na

1. neema ya Mungu kupitia dhabihu ya kifo cha Kristo (kama vile Marko 10:45; 2 Kor. 5:21)
2. mwitikio wa Imani unaohitajika kwa waamini (kama vile Ufu. 6:9; Marko 1:15; Yohana 1:12; 3:16; Matendo 3:16,19; 20:21) na ushiriki wao wa imani (yaani, maisha na matendo)

Kifungu hiki kinafanana sana na Ufu. 14:12. Kuna ufanano mkubwa kati ya Ufu. 12:11 na 17. Ufunuo 11 unaonekana kuelezea juu ya wokovu, ambapo Ufu.12:17 inaonekana kueleza juu ya ukomavu wa Mkristo na ustahimilivu. Tazama ushindi wa Kristo uliotokea huko Kalvari, na si ile miaka elfu.

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"ambao hawakupenda maisha yao hata kufa"** |
| **NKJV** | **"ha hawakupenda maisha yao kwa ajili ya kifo"** |
| **NRSV** | **"kwa maana hawakuyashikiria maisha yao hata katika sura ya kifo"** |
| **TEV** | **"maana hawakuyathamini maisha yao kuwa kitu sana, wakawa tayari kufa"** |
| **NJB** | **"kwa kuwa hata katika sura ya kifo hawakung'ania kuishi"** |

Waamini wa karne ya kwanza na familia zao walikumbana na vifo vya kutisha (kama ilivyo katika kila zama). Hawa watatiwa muhuri na kulindwa na Mungu, lakini bado hawa ni wahanga wa mateso yatokayo kwa wale wasioamini. Imani katka Kristo ilikuwa ya nguvu kuliko ule woga wao wa kifo (kama vile Ufu. 2:10; Marko 8:35; 13:13; Luka 14:26; Yohana 12:25).

**12:12 "shangilieni, enyi mbingu, nanyi mkaao humo"** Hii ni KAULI YA KATI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO (kama vile Ufu. 18:20).Hili linaweza kuwa dokezo la Zab. 96:11 au Isa. 49:13. Mbingu zinashangilia kwa kuwa Shetani ameondolewa, lakini huzuni iko katika dunia! WINGI wa neno "mbingu" unatumika katika Agano la Kale kumaanisha (1) lile eneo lililo juu ya dunia (kama vile. Mwa. 1) na (2) mahali Mungu anakokaa. Katika muktadha huu hili neno ni #2.

Hili neno "kukaa" (NASB, NKJV, NRSV) au "kuishi hapo" (TEV, NJB) linatokana na NOMINO "hema." Hili linamaanisha makao ya kudumu na Mungu (kama vile Ufu. 7:15; 12:12; 13:6; 21:3 na Yohana 1:14 ihamhusu Kristo pamoja nasi).

◙ **"ghadhabu"** Angalia maelezo kamili katika Ufu. 7:14.

Mada Maalum: Dhiki kuu (Special Topic: Tribulation)

◙ **"akijua ya kuwa ana wakati mchache tu"** Mstari huu unaonekana kurejelea juu ya kile kipindi cha wakati kati ya Kupaa kwa Kristo (kama vile Matendo 1:9-11) na ule ujio wa Mara ya pili ambao Yohana na wale Wakristo wa karne ya kwanza walifikiri kuwa ujio huo ungekuwa katika kipindi kifupi cha wakati. Sasa yapata miaka 2,000; kila kizazi kina matumaini juu kule kukariba kwa kurudi kwa Bwana. Waamini wametahadharishwa juu ya huku kukawia katika 2 Wathesalonike na Mt. 24:45-51. Chukua tahadhari kwamba kule kukawia hakupunguzi imani (kama vile 2 Pet. 3:3-4).

MADA MAALUM: WAKATI WO WOTE WA KURUDI KWA YESU DHIDI YA KUKAWIA (FUMBO LA AGANO JPYA) (SPECIAL TOPIC: THE ANY-MOMENT RETURN OF JESUS VERSUS THE NOT YET (NT PARADOX)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 12:13-17**
**[13] Na joka yule alipoona ya kuwa ametupwa katika nchi, alimwudhi mwanamke yule aliyemzaa mtoto mwanamume. [14] Mwanamke yule akapewa mabawa mawili ya tai yule mkubwa, ili aruke, aende zake nyikani hata mahali pake, hapo alishwapo kwa wakati na nyakati na nusu ya wakati, mbali na nyoka huyo. [15] Nyoka akatoa katika kinywa chake, nyuma ya huyo mwanamke, maji kama mto, amfanye kuchukuliwa na mto ule. [16] Nchi ikamsaidia mwanamke; nchi ikafunua kinywa chake, ikaumeza mto ule alioutoa yule joka katika kinywa chake. [17] Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu; naye akasimama juu ya mchanga wa bahari.**

**12:13 "mwanamke"** Bila shaka kiuhalisia "huyu mwanamke" anairejelea ile jamii ya waaminio ya Agano la Kale; sasa inarejelea juu ya watu wa Mungu wa Agano Jipya (kama vile Ufu. 12:17; 13:7). Katika kitabu cha *Word Pictures in the New Testament,* Juzuu 6, A. T. Robertson anamuita mwanamke huyu "Israeli ya kweli katika nchi" (uk. 395).

**12:14 "Mwanamke yule akapewa mabawa mawili ya tai yule mkubwa"** Haya mabawa ya tai ishara ya ulinzi wa Mungu na gawio (kama vile Kut. 19:4; Kumb. 32:11; Zab. 36:7; 57:1; 63:7;90:1,4; na Isa. 40:31). Huu unaweza kuwa mtajo mwingine wa uhamisho mpya.

◙ **"ili aruke, aende zake nyikani hata mahali pake"** Nyikani panaonekana kuwa ile sehemu ya ulinzi mtakatifu, unaotaja ile historia ya Israeli ya kile Kipindi cha Kutanga tanga Nyikani (kama vile Ufu. 12:6). Huu unaweza kuwa utiwaji moyo kwa kanisa lililoumia.

◙ **"wakati na nyakati na nusu ya wakati"** Hili ni dokezo la Dan. 7:25; 12:7. Kwa maelezo kamili juu ya kifungu hiki angalia Ufu.11:2 na 12:6

Mada Maalum: Miezi Arobaini na Miwili (Specia Topic: Forty-Two Months)

**12:15 "Nyoka akatoa katika kinywa chake, nyuma ya huyo mwanamke, maji kama mto"** Hakuna ufanano halisi wa Agano la Kale na hili. Hii inaweza kuwa stiari yenye uhusiano wa moja kwa moja na ile ghadhabu ya Mungu inayoonekana katika Hosea 5:10 au stiari za zile nyakati za gharika na maumivu kama Zab. 18:4; 124:4-5. Lakini kwa sababu sura ya 12 imekazia sana juu ya taswira yake kutokana na ule uumbaji wa simulizi za kale za Mashariki ya Kale, bila shaka hii inarejea juu ya maji yenye kughalikisha, mapambano ya asili juu ya mema dhidi ya mabaya, utaratibu dhidi ya machafuko.

Asili iliyowapigania Baraka na Debora dhidi ya mji wa Kanaani wa Hazori na amiri jeshi wake, Sisera: (1) mvua ikayeyuka (kama vile Amu. 5:4) na (2) hata zile nyota (inafikiriwa kuwa nguvu za kimalaika) zikapigana dhidi ya Sisera (kama vile Amu. 5:20).

**12:17 ". . . akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia "** Yule mwovu alijaribu kuiharibu ile jamii ya Kimasihi kwa

1. kumharibu yule Masihi

2. kuliharibu lile kanisa mama
3. kwa kuwaaribu wafuasi wote wa Kimasihi

Hiki kifungu "kufanya vita" kistiari ni cha kiroho, kisiasa, na cha upinzani wa kiuchumi. Hili ni dokezo la Dan. 7:21 (kama vile 11:7; 13:7). Taabu hii ni uthibitisho wa ushindi wa kanisa kupitia Kristo (kama vile Flp. 1:28).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa usomaji wa hitifaki, ambayo inamaanisha kwamba unao wajibu wa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu lazima aenende katika nuru tuliyo nayo. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Unalazimika kutokuondoa hili toka kwa msemaji.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa kukusaidia mambo muhimu ya kipengele cha kitabu hiki. Yamekusudiwa kukuchokonoa mawazo, yasio ya hakika.

1. Bainisha maudhui ya baragumu ya saba.
2. Je, Kwa nini maono ya Sanduku la Agano linasistiza juu ya hawa Wakristo wa karne ya kwanza?
3. Mwanamke huyu wa kitabu cha Ufunuo 12 ni nani?
4. Je, mapigano haya ya mbinguni yalitokea lini?
5. Ni kwa jinsi gani malaika hawa wa shetani wanahusiana na wale pepo wabaya?
6. Je, hiki kifungu cha "wakati, nyakati na nusu wakati" kinamaanisha nini katika kitabu cha Danieli na Ufunuo?
7. Ni kwa namna gani kifungu hiki kiliweza kuwatia moyo Wakristo wa karne ya kwanza, waliokuwa wakikumbana na mateso?

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA UFUNUO 13:1-18

A. Sura ya 13 ni mwendelezo zaidi wa matumizi ya tamathali za semi za Ufu. 12:13-17.
B. Ule usuli wa Agano la Kale kuhusiana na sura hii na kitabu cha Danieli 7. Zile falme nne za Mashariki ya Karibu zinazozungumziwa katika kitabu cha Danieli zilizounganishwa katika umilele wa namna moja, ulimwengu, wampingao Mungu, ufalme wa wakati wa mwisho.
C. ibada ya kumwabudu mfalme wa karne ya kwanza (hasa katika Asia Ndogo) ni moja ya utimilifu wa kihistoria wa kumwabudu mnyama, kama itakavyokuwa katika nyakati za mwisho kwa mwanadamu mwenye dhambi (kama vile 2 Wathesalonike 2), na ile pembe ndogo ya Dan. 7 (kama vile Ufu. 13:8,11,20,25), ambayo iko nje ya ufalme wa nne, Rumi.
D. Huyu mnyama amebainishwa katika njia mbili
   1. Kama mwendelezo, mafundisho/walimu wa uongo/ (kama vile 1 Yohana 2:18,22; 4:3; 2 Yohana 7). Huyu yuko katika hali zote yaani WINGI na UMOJA, yuko katika hali zote yaani wakati uliopo na wakati ujao.
   2. Kama mtu halisi, bila shaka alitabiliwa katika uovu wa mwanadamu katika historia nzima (Antioko, Wafalme wa Kirumi, Hitler, n.k. lakini hatimaye kafanyika mwili katika umbo la siku ya mwisho, cf. 2 Thess. 2:1-10).

A. Angalia MADA MAALUM: SERIKALI YA MWANADAMU (SPECIAL TOPIC: HUMAN GOVERNMENT)

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 12:17b-13:6**
**12:17b naye akasimama juu ya mchanga wa bahari 1 Kisha nikaona mnyama akitoka katika bahari, mwenye pembe kumi, na vichwa saba, na juu ya pembe zake ana vilemba kumi, na juu ya vichwa vyake majina ya makufuru. 2 Na yule mnyama niliyemwona alikuwa mfano wa chui, na miguu yake ilikuwa kama miguu ya dubu, na kinywa chake kama kinywa cha simba, yule joka akampa nguvu zake na kiti chake cha enzi na uwezo mwingi. 3 Nikaona kimoja cha vichwa vyake kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti, na pigo lake la mauti likapona. Dunia yote ikamstaajabia mnyama yule. 4 Wakamsujudu yule joka kwa sababu alimpa huyo**

**mnyama uwezo wake; nao wakamsujudu yule mnyama, wakisema, Ni nani afananaye na mnyama huyu? Tena ni nani awezaye kufanya vita naye? [5] Naye akapewa kinywa cha kunena maneno makuu, ya makufuru. Akapewa uwezo wa kufanya kazi yake miezi arobaini na miwili. [6] Akafunua kinywa chake amtukane Mungu, na kulitukana jina lake, na maskani yake, nao wakaao mbinguni**.

**13:1 "naye akasimama juu ya mchanga wa bahari"** Tafsiri za NASB, NKJV na NJB zinakianza kitabu cha Ufu. 13 pamoja na kifungu hiki cha maneno (yaani, Ufu. 12:17b), ambapo TEV inakihitimisha kitabu cha Ufunuo 12 kwa kifungu.

Kuna tofauti ya maandishi inayohusiana na KITENZI katika Ufu. 12:18 na 13:1, "kusimama"

1. "akasimama," linalomlejelea yule mnyama/joka ambaye anahusiana na Ufunuo 12 – MSS $P^{47}$, א, A, C, (NASB, NRSV, TEV, REB, NET, NIV)
2. "Nikasimama," kifungu kinachorejelea kwa Yohana na ambacho kinachohusiana na ule mwendelezo wa Ufu. 13 – MSS P, 046, 051 (NKJV, NJB)

   UBS[4] inatoa uchaguzi wa #1 daraja "B" (wenye kuwa na uyakini).

Ile "bahari" inaweza dokezo la kitabu cha Dan. 7:2-3. Hii ilikuwa ishara ya

1. Ule utu kamili (kama vile Isa. 17:12-13; 57:20; Ufu. 17:15)
2. Ile nguvu ya gharika (kama vile Mwa. 1; Isa. 51:9-10)

◙ **"Kisha nikaona mnyama akitoka katika bahari"** Yule mnyama wa nyikani (kama vile. Ufu. 13:14,15; 15:2; 16:13; 15:8) kwanza anatajwa pasipo mshindo katika Ufu. 11:7 kama alivyotoka katika shimo la uharibifu (kama vile Ufu. 17:8). Hii inaoneka na kurejelea juu ya "Mpinga Kristo" wa 1 Yohana 2:18a,22; 4:3; 2 Yohana 1:7, pia anafahamika "mtu wa kuasi" katika 2 The. 2:3. Ubainifu ule ule wa huyu mnyama unapatikana katika Ufu. 12:3 na17:3,8.

Kifungu cha maneno "kutoka katika bahari" kimetafsiriwa katika maana kadhaa.

1. Kimaandishi, ni kama katika kipindi kile cha Agano la Kale na Agano Jipya kutumia fasihi katika matukio ya siku ya mwisho kama Mamba na katika Ufu. 12:11 kama Kiboko
2. hili dokezo la kitabu cha Danieli 7, ambapo yule mnyama alitoka katika bahari katika Ufu. 13:3 na duniani katika Ufu. 13:17, ambaye katika kitabu cha Danieli 7 ana ufananano, lakini Yohana amewatenganisha wale wanyama wa mwisho katika ufanano wa nyakati mbili za mwisho zilizo za uovu na zilizo jitenga: myama wa baharini, Ufu. 13:1 na na yule mnyma atokaye katika nchi, Ufu. 13:11
3. ile ishara ya mwanadamu aliyeanguka (kama vile hasa Ufu. 17:15, lakini pia kitabu cha Dan. 7:2-3; Isa. 17:12-13; 57:20)

Sababu iliyofanya wale wanyama wawili wa sura ya 13 kutajwa kama viumbe waliotoka katika bahari na katika nchi ni

1. kwa sababu sura hii inaangukia katika kitabu cha Danieli 7 kwa ukaribu sana
2. kwa sababu hawa wanaungana ajili ya kuiwakilisha dunia nzima
3. Pia inawezekana kuwa wale wanyama wawili pamoja na Shetani wanaunda ule mwigo wenyekuubeza Utatu.

Mada Maalum: Mpinga Kristo (Specia Topic: The Antichrist)

◙ **"pembe kumi, na vichwa saba, na juu ya pembe zake ana vilemba kumi"** Huu si uhalisia wa joka (kama vile Ufu. 12:3) bali ni ufanano wa karibu sana (kama vile Ufu. 17:3,7-12). Zile pembe kumi zinazungumzia juu ya nguvu kamili; vile vichwa saba vinawakilisha ule udhihirisho kamili wa uovu, na vile vilemba kumi ni maelezo ya nafasi ya ukuu. Mara nyingi uovu ni mambo ya kughushi yanayofanana na ukweli. Huu ni uigaji wa kwanza kati ya miigo kadhaa kwa Kristo.

◙ **"majina ya makufuru"** Machapisho ya Kiyunani yamegawanyika kwa usawa kati ya WINGI (MS A) "majina" (NRSV, NJB) na UMOJA (MSS $P^{47}$, א, C, P) "majina" (NKJV, TEV). $UBS^4$ haiwezi kuamua ni kifungu kipi kilicho halisi. Cho chote kilicho cha kweli, kwa udhihirisho hili ni dokezo la Dan. 7:8,11,20,25 au 11:36. Haya majina ya makufuru yanahusiana na (1) maelezo ya Uungu au (2) majina ya uovu (kama vile Ufu. 17:3).

**13:2 "yule mnyama niliyemwona alikuwa mfano wa chui. . . dubu. . . simba"** Huu muungano wa wanyama kadhaa ni dokezo lingine la Dan. 7:4,5,6, aidha mstari huu uinarejelea juu ya mtiririko wa wafalme, lakini hapa uwasilishaji umkebadilika na kuwa katika muungano wa mifumo yote ya wapinga Mungu na uliofananishwa na kiongozi mmoja (kama vile Dan. 7:24).

◙ **"yule joka akampa nguvu zake na kiti chake cha enzi na uwezo mwingi"** Huu ni ufanano wa 2 The. 2:9, ambayo inazungumza juu ya ule msukumo wa uwezo wa Kishetani. Yule mnyama si Shetani, bali ile nguvu yenye kumwezesha mwanadamu kujithihirisha au lile umbo lake la mwili (kama vile Ufu. 13:4,12). Huu ni uigaji mwingine wa kumwiga Kristo (kama vile Ufu. 5:6).

**13:3 "Nikaona kimoja cha vichwa vyake kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti"** Hii ni KAULI TIMILIFU TENDEWA YA HALI YA KUENDELEA, ambayo kisarufi ina ufanano na yule Mwana-Kondoo wa Ufu. 5:6. Huu ni muigo mwingine wa kifo cha Yesu na ufufuo.

◙ **"na pigo lake la mauti likapona"** Je, Shetani anao uwezo wa kuwafufua watu wake, au hii ni hila, udanganyifu, na uigaji (kama vile Ufu. 13:15)? Shetani huiga ile nguvu ya Mungu iliyomfufua Kristo. Kihistori hili linawezakuwa dokezo la ile simulizi ya "kurudi tena kwa Nero", ambayo inadai kwamba Nero angerudi kuishi tena, na kurudi na jeshi kubwa la mashariki (WaParthi), na kuishambulia Rumi (kama vile *Sibylline Oracles*, vitabu vya III-V).

◙**"Dunia yote ikamstaajabia mnyama yule"** Shetani anatumia miujiza kuushawishi ule ulimwengu usiamini umfuate yeye (kama vile Mt. 24:24; Marko 13:22; 2 The. 2:9; Ufu. 13:5; 17:8), ambao ni uigaji mwingine wa kumwiga Kristo. Ulimwebgu ulishinda kwa nguvu za mashahidi wawili katika Ufu.11:13; sasa kigeugeu chao kinaonekana katika kumwabudu mnyama.

**13:4 "Wakamsujudu yule joka. . . nao wakamsujudu yule mnyama"** Uovu si shauku ya nguvu ya kisiasa, bali ibada ya kidini (kama vile Ufu. 13:8). Shetani hutaka kusujudiwa (kama vile Ufu. 13:12; 14:9,11; 16:2; 19:20; Mt. 4:8-9). Yeye anataka kuwa kama Mungu (kama vile. Bila shaka Isa. 14:12-15). Kwa maana nyingine, hili linarejelea juu ya ule uongo wa Nyoka katika Mwa. 3:5 na katika Mt. 4:9; Luka 4:5-7.

◙ **"Ni nani afananaye na mnyama huyu"** Kumekuwa na asili zilizopendekezwa kwa ajili ya kifungu hiki. Wengine wanakiona kifungu hiki kama

1. uigaji wa jina la YHWH linalopatikana katika kitabu cha Kut. 15:11; Zab. 35:10; 113:4
2. uigaji wa YHWH katika Isa. 40:18-22;43:11; 44:6,8,9-20 45:6
3. marejeleo ya yule mnyama mkubwa na mnyama katika ile fasihi ya Kiyahudi uhusuyo matukio ya siku za mwisho (mfano mmoja katika Agano la Kale ni Ayubu 41, hasa Ufu. 13:33-34)

**13:5** Katika Ufu. 13:5-7 na Ufu. 13:14-15 kuna VITENZI TENDWA vingi ambavyo vinamaanisha kuwa kibali kilitolewa na Shetani na hatimaye Mungu (kama vile Ayubu). Mungu anamtumia shetani kwa makusudi yake mwenyewe! Uovu huifunua shauku yake kwa maneno na matendo.

◙ "**kinywa cha kunena maneno makuu, ya makufuru"** Hili dokezo la:

1. "yule mnyama" katika Dan. 7:8,11,20,25; 11:36
2. Antiokio IV Epiphane katika Dan. 8; I Wam. 1:24
3. "yule mpingamizi" katika 2 The. 2:4

4. lile chukizo la uharibifu la Mt. 24:15, ambalo hurejelea juu ya yale mashambulizi na ule uharibifu wa Yerusalemu chini ya utawala wa Kirumi wa moja kwa moja, na baadaye Mfalme, Tito, mnamo mwaka 70 B.K.

Huu ni mfano mzuri wa namna mtazamo wa kihstoria wa ishara hizi unavyobadilika. Katika kitabu cha Danieli 8 mfano huu unarejelea juu ya Antioko IV Epiphane wa kipindi kile kati ya Agano la Kale na Agano Jipya; katika Mathayo 24 inarejea juu ya ule uharibifu wa Yerusalemu mnamo mwaka 70 B.K na katika Danieli 7 (na bila shaka Dan. 11:36-39) kuna urejeleo wa ile kazi ya Wapinga Kristo wa nyakati za mwisho.

◙ **"miezi arobaini na miwili"** Hili ni dokezo la moja kwa moja kwa Dan. 7:25. Kwa mara ya kwanza aya hii imetajwa katika Ufu. 11:2-3. Hii ni stiari ambayo inamaanisha kile kipindi cha mateso.

Mada Maalum: Miezi Arobaini na Miwili (Special Topic: Forty-Two Months)

**13:6 "Akafunua kinywa chake amtukane"** Aidha kuna makufuru mawili au matatu dhidi ya jina la Mungu yaliyofungamana katika mstari, hema la Mungu, na watu wa Mungu. Hii inategemea namna mtu anavyokitafsiri kifungu hiki cha Kiyunani.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 13:7-10**
**[7]Tena akapewa kufanya vita na watakatifu na kuwashinda, akapewa uwezo juu ya kila kabila na jamaa na lugha na taifa. [8] Na watu wote wakaao juu ya nchi watamsujudu, kila ambaye jina lake halikuandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia. [9]Mtu akiwa na sikio na asikie. [10]Mtu akichukua mateka, atachukuliwa mateka. Mtu akiua kwa upanga, atauawa kwa upanga. Hapa ndipo penye subira na imani ya watakatifu**.

**13:7 "akapewa kufanya vita na watakatifu na kuwashinda"** Hii ni KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU na KAULI TENDAJI YA KITENZIJINA YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Kile kidokezi cha IRABU TENDEWA ni kuwa Mungu aliliruhusu hili litokee. Hatuyaelewi yote yaliyo nyuma yake bali ni kutokana na kitabu cha Ufunuo kuwa Mungu yu juu ya historia yote. Vita hii iliyo juu ya watakatifu wake inatajwa katika Dan. 7:21,25. Hili linarejelea juu ya kile kifo cha mwili cha watakatifu wa Mungu. Kuna wakati ambao adui huonekana kuwa mshindi (kama Kalvari), lakini kitabu cha Ufunuo na Danieli kinafundisha kuwa huu ni ushindi wa muda mfupi! Kumbuka kuwa watu wa Mungu wanalindwa dhidi ya ghadhabu ya Mungu, lakini si ile ghadhabu ya yule mnyama na wafuasi wake. Kwa uwazi Mungu huuruhusu ushindi wenye uovu ili kuzifunua dhamira halisi na asili yake.

◙**"watakatifu"** Angalia Mada Maalum: Watakatifu (Special Topic: Saints)

◙ "**akapewa uwezo juu ya kila kabila na jamaa na lugha na taifa."** Kifungu hiki kinaashiria

1. kwamba kitabu cha Ufunuo kinahitaji kutafsiriwa katika maana pana kuliko ile Dora ya Kirumi pekee, kwa sababu ya huu ulimwengu, kifungu hiki kikiwemo
2. kwamba kifungu hiki kinarejelea juu ya tukio pana la Dora.

**13:8 "wakaao juu ya nchi"** Hiki ni kifungu cha mara kwa mara chenye kurejelea kwa wale wasioamini katika Ufunuo (kama vile Ufu. 3:10; 6:10; 8:13; 11:10; 13:8,12,14; 17:8).

◙ **"ambaye jina lake halikuandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo, aliyechinjwa"** Haijulikani ikiwa kifungu "tangu kuwekwa misingi ya dunia" hii ni ya kuchukuliwa kama

1. "majina yetu yaliyoandikwa" (kama vile RSV, NRSV, TEV, NJB na 17:8; Efe. 1:4)
2. "Mwana-Kondoo aliyechinjwa" (kama KJV, NKJV na 1 Pet. 1:19-20)
3. mpangilio wa wa andiko hili na Ufu. 17:8 linadokeza kuwa bila shaka hiki kifungu kinaeleza juu ya majina ya waaminio yaliyoandikwa katika kitabu cha uzima hata kabla ya uumbaji!

Kifungu cha maneno "misingi ya dunia" kinatumika mara kadhaa katika Agano Jipya (kama vile Mt. 25:34; Yohana 17:24; Efe. 1:4; 1 Pet. 1:19-20). Pia kuna kifungu chenye ufananao sana katika Mat. 13:35; Luka 11:50; EbR. 4:3; 9:26 na Ufu. 17:8. Muungano wa vifungu hivi unaonyesha kazi ya Mungu ya ukombozi kabla ya uumbaji wa dunia. Waamini wako salama katika Kristo (kama vile Ufu. 7:4; 11:1; 13:8). Uovu umewekewa mipaka na Mungu (idadi ya VITENZI TENDEWA katika sura hii na wakati wa uliowekewa mipaka). Hiki knaonekana katika utupu, lakini litazame katika picha iliyo kuu!

Mada Maalumu: Misingi ya Dunia (Specia Topic: The Foundation of the Earth)

◙ **"kitabu cha uzima"** Kutokana kiatabu cha Dan. 7:10 na Ufu. 20:11-15 tunaelewa kuwa kuna vitabu viwili vya kistiari vilivyotajwa katika ule uhusiano wa hatima ya mwanadamu:

1. kile Kitabu cha Uzima, ambacho kina majina ya wale ambao kibinafsi wanajulikana kwa Mungu (Agano la Kale) na wamempokea Kristo (Agano Jipya) [kama vile Kutoka. 32:32-33; Zab. 69:28; Dan. 12:1; Isa. 4:3; 34:16; Luka 10:20; Flp. 4:3; Ebr. 12:23; Ufu. 13:8; 17:8; 20:15; 21:27]
2. kile kitabu cha Matendo ya Mwanadamu, ambacho kimenakili matendo ya mwanadamu, yote mema na mabaya (kama vile Zab. 56:8; 139:16; Isa. 65:6; Mal. 3:16)

Hizi ni stiari dhahiri, lakini kwa ufasaha zinabainisha ule uwezo wa Mungu wa kuwajua wale walio wake na kuwashikiria wale waliyoyakataa majukumu yake (kama vile. Gal. 6:7).

Mada Maalum: Vitabu Viwili vya Mungu (Special Topic: The Two Books Of God)

◙ **"aliyechinjwa"** Angalia maelezo katika Ufu.5:12.

**13:9 "Mtu akiwa na sikio na asikie"** Hili ni wazo liliorudiwa rudiwa katika zile barua za yale makanisa saba (kama vile Ufu. 2:7,17; 3:6,13,22). Hili, kama vilivyo vifungu vingine katika Ufu. 13:9-10, ni SENTENSI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA, ambayo inadhahaniwa kuwa kweli kutokana na lile kusudi la mwandishi wa maandishi. Hili ni wazo kuwa vifungu hivi vinavyohusiana na makanisa vinaonekana kumaanisha kuwa kifungu kinachofuatia (mst. 10) kimeelekezwa kwa watu wa Mungu.

**13:10** Huu mstari unaweza kuwa dokezo la Yer.15:2 au 43:11, inayozungumzia juu ya ile hukumu ya Mungu. Kuna tofauti kadhaa za machapisho ya Kiyunani yanayohusiana na na hiki KITENZI "kuua." Hili limesababisha tofauti za Kiingereza kuuhusu mstari huu.

1. Tafsiri ya toleo la KJV na NKJV zinahisiana na vifungu vyote vinavyohusu mateso ya watu wa Mungu.
2. Tafsiri ya toleo la RSV na NRSV zinakifanya kile kishazi cha kwanza kihusiane na wale Wakristo wanaoteswa na kishazi cha pili ni kwa ajili ya mateso ya wale waliokinyume na Mungu.
3. Tafsiri ya tatu isiyo na shaka (TEV na NJB) ni kwamba vishazi vyote vinarejelea juu ya wale Wakristo wateswao.

Ukweli wenye kuonyesha kuwa kuna tofauti sana katika tafsiri unaonyesha uyumkini. Ni dhahiri kuhusiana na ile kweli ya kiroho kwamba Mungu yu juu ya historia yote. Swali pekee ni kwa nani kifungu hiki kilielekezwa kwake.

1. kuwasistiza wakristo kueendelea kukaa katika imani (kama vile Mt. 26:52; Flp. 1:28)
2. Kuwahakikishia wale wateswao kuwa siku moja watawajibika mbele ya Mungu kwa chaguzi na matendo yao?

**NASB " Hapa ndipo penye subira na imani ya watakatifu"**

**NKJV "Hapa ndipo palipo na uvumilivu na imani ya watakatifu"**

**NRSV "Hapa kuna wito wa ustaimilivu na imani ya watakatifu"**

**TEV "Huu ni wito wa ustahimilivu na imani kwa upande wa watu wa Mungu"**

**NJB "Ndiyo maana watakatifu yawapasa kuwa na uvumilivu na imani"**

Kitabu cha Ufu. 13:9 na mwishoni mwa Ufu. 13:10 kinaonyesha kwamba kifungu hiki lazima kirejelee juu ya watu wa Mungu (kama vile Mt. 26:52). Kifungu hiki pia kinabainisha yule mwamini wa kweli (kama vile Ufu. 14:12;

12:11,17). Hawa wanasistizwa kushikiria hadi mwisho (kama vile Ufu. 2:3,7,11,17,26; 3:5,12,21; 21:7). Ustahimilivu ni ushahidi wa ule wokovu wa kweli (kama vile 1 Yohana 2:19). Angalia maelezo katika Ufu. 2:2.

Mada Maalum: Ustahimilivu (Specia Topic: Perseverance)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 13:11-18**

***11*** **Kisha nikaona mnyama mwingine, akipanda juu kutoka katika nchi; naye alikuwa na pembe mbili mfano wa Mwana-Kondoo, akanena kama joka.** ***12*** **Naye atumia uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza mbele yake. Naye aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudie mnyama wa kwanza, ambaye jeraha lake la mauti lilipona.** ***13*** **Naye afanya ishara kubwa, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu.** ***14*** **Naye awakosesha wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kuzifanya mbele ya huyo mnyama, akiwaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama, aliyekuwa na jeraha la upanga naye akaishi.** ***15*** **Akapewa kutia pumzi katika ile sanamu ya mnyama, hata ile sanamu ya mnyama inene, na kuwafanya hao wote wasioisujudu sanamu ya mnyama wauawe.** ***16*** **Naye awafanya wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao;** ***17*** **tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani, jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake.** ***18*** **Hapa ndipo penye hekima. Yeye aliye na akili, na aihesabu hesabu ya mnyama huyo; maana ni hesabu ya kibinadamu. Na hesabu yake ni mia sita, sitini na sita.**

**13:11 "Kisha nikaona mnyama mwingine, akipanda juu kutoka katika nchi"** Hili ni dokezo la Dan. 7:17.

1. inaweza kudhaniwa kwamba hawa wanyama wawili ni ule uigaji wa wale mashahidi wa Mungu katika Ufu. 11:13-14
2. wengine wamedhani kwamba yule joka na wale wanyama wawili ni ule uigaji wa Utatu.

Kama yule mnyama alivyo dokezo la mamba (kama vile Ayubu 41:1-34), bingwa wa fujo, hivyo yule mnyama aliyetoka na kusimama juu ya mchanga ni dokezo la Kiboko (kma vile Ayubu 40:15-24), ule ufanano wa yule mnyama mkubwa wa alisimama juu ya mchanga wa bahari (hii ni njia moja ya kurejerea juu ya wale dinosaria, lakini ni kwa elimu ya viasili vya kale vya mashariki).

Hawa wanyama ni ishara za uovu (machafuko) na uhasi katika ule mpangilio ulioumbwa na Mungu (kama vile Zab. 74:12-14; Ayubu. 3:8; Isa. 51:9-11; Amosi 9:3). Wakati mwingine Mamba anaitwa *Rahab* ("yule aliyetumbuliwa," yaani, yule nyoka, kama vile Isa. 51:9). Katika sehemu nyingine *Rahab* ni jina la Misri (Nile, yaani, mto uliopinda, kama vile. Zab. 87:4; Isa. 30:7 na bila shaka Ezekieli 32, hasa Ufu. 13:2-3).

◙ **"naye alikuwa na pembe mbili mfano wa Mwana-Kondoo, akanena kama joka"** Haya marejereo ya Mwana-Kondoo ni uigaji halisi kwa Kristo (kama vile Ufu. 5:6). Ile sauti yake na/au habari hufunua tabia yake ya kweli. Baadaye katika kitabu cha Ufunuo mnyama wa pili mara kwa mara anarejelewa kama yule nabii wa uongo (kama vile Ufu. 16:13; 19:20; 20:10). Huyu hatafuti utukufu kwa ajili yake mwenyewe, bali kuifanya dunia imsujudie mnyama (kama vile Ufu. 13:12). Huu ni uigaji wa ile kazi ya Roho Mtakatifu (kama vile Yohana 14-16) katika kumsaidia Kristo. Hivyo tunao utatu usio mtakatifu:

1. Shetani kama mwigaji wa Mungu Baba
2. myama wa baharini kama mwigaji wa Mungu Mwana
3. mnyama aliyesimama juu ya mchanga wa bahari kama mwigaji wa Mungu Roho Mtakatifu

**13:13 "Naye afanya ishara kubwa"** Hii ni KAULI YA KITENZI CHA WAKATI ULIOPO ambacho kinamaanisha kuwa huyu anaendelea kufanya maajabu. Ilingojewa kwamba hawa walimu wa uongo wa wakati wa mwisho wataweza kufanya miujiza na hata kuwapotosha wale wateule, kama ingewezekana (kama vile Mt. 24:24; Marko 13:22; 2 The. 2:9-11; Didache 16:3,4). Miujiza si ishara za Mungu zenye kujiendesha zenyewe (kama vile Kut. 7:8-13). Huu ni uigaji mwingine wa huduma ya Kristo.

Mada Maalum: Ishara (Agano la Kale) (Specia Topic: Sign (OT))

◙ **"hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu"** Hii ni sawa na Eliya katika 1 Flp. 18:38, ambapo hiki kinaweza kuwa chanzo cha ubainifu wa wale mashahidi wawili wanaopatikana katika Ufu. 11:5. Mstari huu unawaza kuurejelea ule moto ambao ulianguka kama hukumu ya Mungu katika Eze. 38:22 au 39:6. Huu unaweza kuwa uigaji mwingine

1. wa wale mashahidi wawili
2. wa matendo ya Mungu katika Agano la Kale
3. wa Pentekoste katika Matendo 2

Mada Maalum: Moto (Specia Topic: Fire)

**13:14 "aliyekuwa na jeraha la upanga naye akaishi"** Hili neno "jeraha" (*plēge*, kama vile Ufu. 13:3,12,14) mara nyingi linatafsriwa kama "mapigo" katika Ufunuo (kama vile 9:18,20; 11:6; 15:1,6,8; 16:9,21; 18:4,8; 21:9; 22:18). Yale maelezo ya ziada ya tafsiri ya NRSV yana

1. Ufu. 13:3 "pigo lake la mauti"
2. Ufu. 13:12 "ambaye kwa jeraha lake la mauti"
3. Ufu. 13:14 " aliyekuwa na jeraha la upanga"

Kusudio la kitheolojia la tafsiri hizi ni kuonyesha kuwa yule mpinga Kristo si mtu, bali ule mfumo wa ulimwengu. Hili neno linaweza kutumika kistiari kama "mvumo wa bahati" au maangamizi (kama vile BAGD, uk. 674), lakini maana yake ya msingi ni kiharusi, au jeraha.

Kifungu cha maneno kinachofuatia "naye akaishi" kinaonyesha kuwa neno "pigo" si tafsiri bora katika mistari hii inayohusiana na mnyama. Hili wazo la wale Mpinga kristo apingaye uwepo wa Mungu mmoja anayeyaongoza mataifa katika uasi anatabiriwa katika Agano la Kale katika Ezekieli 38-39; Zekaria 14; Danieli 7:21-27; 9:24-27; 11:36-39 na katka ile fasihi ya kipindi cha Agano la Kale na Agano Jipya kuhusu matukio ya siku za mwisho, Sibylline Oracles, book III; IV Esdras 5.4,6 na Apocalypse of Baruch XL, na katka Agano Jipya, 2 The. 2:3,8-9.

**13:15 "Akapewa kutia pumzi katika ile sanamu ya mnyama"**Mahali pengine huyu mnyama aliyekuwa amesimama katika mchanga wa bahari anaitwa nabii wa uongo (kama vile Ufu. 16:13; 19:20; 20:10). Huenda hii ni stiari ya kurejesha uzima (yaani, Kiebrania *ruah* = pumzi) katika (kama vile Ezekieli 37).

**13:16 "watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao"** Kama watakatifu walivyotiwa mhuri katika Mungu katika Ufu. 7:3 (kama vile Ufu. 13:16; 14:9), hapa yule mwovu huyaiga matendo ya Mungu kwa kuwatia chapa wale walio wake. Lile neno la Kiyunani linamaanisha alama ya mnyama au nyaraka za kiserikali. Kwa sababu ya ile ishara, wengine wamefikiri kuwa hii ilikiwa

1. ule uigaji wa ule mkoba wa Kiyahudi (kama vile Kumb. 6:8)
2. iliyohusiana na ule utamaduni wa Kirumi wa karne ya kwanza, ambapo watumwa walikuwa wakipigwa chapa ya wamiliki wao
3. askari walijichora kwa heshima ya ukuu wao

**13:17** Ile chapa ya mnyama inahusiana na manunuzi ya chakula, na bila shaka ajira. Watu wa Mungu hawalindwi kutokanana huu ubinafsishaji wa kiuchumi.

**13:17-18 "hesabu yake"** Lugha za kale zilitumia herufi za alfabeti zake kusimamia hesabu pia. Kama konsonanti za Kiebrania za jina la Yesu zinavyoongezeka hadi 888 (kama vile *Sibylline Oracles*, 1.324), hivyo jina la yule mnyama, umbo la mwili la Shetani la wakati wa mwisho, linaongezeka hadi 666. Hesabu sita ni ndogo kuliko ile namba 7 iliyokamili (kama vile Mwa. 1:1-2:3, siku saba za uumbaji); hii imerudiwa mara tatu na inaunda SIFA YA JUU KABISA ya Kiebrania (kama vile Isa. 6:3; Yer. 7:4).

Pia inawezekana kuwa kwa kuwa namba sita ni namba ya mwanadamu, inaweza kurejelea juu ya ule mfano halisi wa sifa ya kila mwanadamu wa ule utatu usio mtakatifu—lile joka kuu (Shetani), yule mnyama wa baharini (Mpinga Kristo) na yule mnyama aliyesimama katika mchanga wa bahari (nabii wa uongo). Kwangu hili

linaonekana kuwa yule mnyama wa kwanza ni ule ufanano wa ule mfumo wa kisiasa ulio kinyume na Mungu mmoja na pia kwangu hili linaonekana kwamba yule mnyama wa pili ni ufanano wa ule mfumo wa kidini ulio kinyume na Mungu. Tunasonga mbele hadi kwa yule kahaba mkuu wa sura ya 17, asili ya ule mfumo wa kidunia ulio kinyume na Mungu mmoja kutokana na Danieli 7. Aidha ni Babeli ya Kale, Rumi ya karne ya kwanza, au ule mchanganyiko wa ufalme wa ulimwengu wa wakati wa mwisho, hii inaonyesha kuwa historia ya mwanadamu inaendelea hadi katika mgogoro wa milele kati ya "yule mungu wa dunia hii" (kama vile 2 Kor. 4:4) na wafuasi wake dhidi ya Mungu wa uumbaji na na Masihi wake (kama vile Zaburi 2).

**13:18 "hesabu yake ni mia sita, sitini na sita"** Hakuna muafaka kuhusiana na ni nani hesabu hii inarejelea kwake. Hakuna kisio lisilihesabika, lakini hakuna aliyehitimisha. Hapa kuna nadharia tatu za mnyama katika wazo langu.

1. Kwa kuwa kuna tofauti za machapisho kati ya 666 na 616, inawezekana kulitumia jina la Mfalme Nero. Zile herufi za Kiyunani zilizotafsiriwa katika Kiebrania ni sawa na 666 na zile herufi za Kiyunani zilizotafsiriwa katika Kilatini ni sawa na 616.
2. Kwa kuwa marudio fungamano huhesabu kwa LUGHA YENYE KUONGEZA SIFA ya Kiebrania, 666 haya yanaweza kumaanisha mtu aliye mwovu kabisa.
3. Kwa kuwa muktadha unadokeza juu ya uigaji wa Utatu, hizi nafsi tatu za Uungu zinaakisiwa katika 777, ambapo zile nafsi tatu zilizo za kughushi ni 666.

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA UFUNUO 14:1-20

A. Inawezekana kuwa Ufu. 14 ni mwitikio wa mwonekano wa kuushinda uovu wa Ufu. 12 na 13. Nina uhakika ya kuwa viongozi wanayashangaa yale ambayo yangetokea kwa watakatifu katika wakati wa mwisho wenye mateso ya kuogopesha.
B. Wengine wameuona muundo mwingine wa kifasihi wa neno "saba" katika Ufu. 14:6-20. Kuna mpangilio wa malaika saba, lakini muundo huu hauonekani kuwa wa muhumi kitheolojia.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 14:1-5**

**[1]Kisha nikaona, na tazama, huyo Mwana-Kondoo amesimama juu ya mlima Sayuni, na watu mia na arobaini na nne elfu pamoja naye, wenye jina lake na jina la Baba yake limeandikwa katika vipaji vya nyuso zao. [2]Nami nikasikia sauti kutoka mbinguni, kama sauti ya maji mengi, na kama sauti ya radi kuu. Na hiyo sauti niliyoisikia ilikuwa kama sauti ya wapiga vinubi, wakivipiga vinubi vyao; [3]na kuimba wimbo mpya mbele ya kile kiti cha enzi, na mbele ya wale wenye uhai wanne, na wale wazee; wala hapana mtu aliyeweza kujifunza wimbo ule, ila wale mia na arobaini na nne elfu, walionunuliwa katika nchi. 4 Hawa ndio wasiotiwa unajisi pamoja na wanawake, kwa maana ni bikira. Hawa ndio wamfuatao Mwana-Kondoo kila aendako. Hawa wamenunuliwa katika wanadamu, malimbuko kwa Mungu na kwa Mwana-Kondoo. [5] Na katika vinywa vyao haukuonekana uongo. Maana hawana mawaa.**

**14:1 "huyo Mwana-Kondoo"** Mstari huu unamrejelea kwa Masihi (kama vile Ufu. 5:6,8,12-13; 13:8; Isa. 53:7; Yohana 1:29,36; 1 Pet. 1:18-19).

1. "amesimama juu ya Mlima Sayuni" Kumekuwa na nadharia nyingi zenye kukibainisha kifungu hiki.
2. kwamba kinamaanisha ule Mlima Moria na eneo la Hekalu katika Yerusalemu (kama vile. Isa. 24:23; Yoeli 2:32)
3. kwamba inamaanisha ile Yerusalemu ya mbinguni (kama vile Ebr. 11:10,16; 12:22-23; 13:14; Gal. 4:26)
4. kwamba ni ishara ya mafunuo ya matukio ya siku za mwisho yanayopatikana katika kile kitabu cha II Esdras 2:42-47; 13:35,39-40 kisicho cha sheria za kanisa
5. kwamaba kinarejelea vile vifungu vya Agano la Kale ambavyo vinazungumzia juu ya kusanyiko la watu wa Mungu katika wakati wa mwisho (kama vile Zaburi 48; Isa. 24:23; Yoeli 2:32; Mika 4:1,7; Oba. mist. 17,21)
6. kwamba usuli, kama vilivyo vifungu vingine katika kipengele hiki, ni Zaburi 2, hasa Ufu. 14:6.

Kumbuka kwamba watoa maoni wanahusianisha kila moja ya maoni haya aidha kwa

1. vile vifungu vya Agano la Kale au maeneo ya Kipalestina
2. fasihi ya mafunuo ya Matukio ya Siku za Mwisho katika Kipindi cha Agano la Kale na Agano Jipya
3. historia ya Wagiriki-Waroma wa karne ya kwanza

Kwangu mimi mitazamo hii ya mambo ya Agano la Kale inayoanza na sura ya 6, inahusiana na watu wa Mungu wa Agano Jipya (Mataifa na Wayahudi wanaoamini), wale watakatifu, kanisa. Katika jambo hili muhimu, hili ni dokezo la hekalu la mbinguni (kama vile Ebr. 8:2; 9:11,24).

◙ "**watu mia na arobaini na nne elfu pamoja naye**" Hili ni kundi linalofanana

1. la wale waliookolewa kama katika Ufu. 5:9
2. la wale waliotiwa mhuri katika Ufu. 7:4-8 (tazama maelezo kamili katika Ufu 7:4)
3. la wale waliooshwa katika damu ya Mwana-Kondoo katika Ufu. 7:14-17

Kwa hiyo, katika maoni yangu, aya hii inamaanisha watu wa Mungu wa Agano Jipya, wale watakatifu, kanisa. Kwa maelezo kamili kuhusiana na huu upekee wa 144,000, tazama Ufu. 7:4. Katika marejeleo ya kale hawa walikuwa wakitiwa muhuri na waliendelea kuteseka, lakini walikuwa washindi!

◙ **"wenye jina lake na jina la Baba yake limeandikwa katika vipaji vya nyuso zao"** Je, mstari huu unarejelea jina moja au majina mawili? Hii inaweza kuwa inayalejelea yale majina ya Isa. 9:6, ambayo yanawahusu wote Baba na Mwana. Hawa ndiyo wale waliokwisha kutiwa muhuri na kuwa washirika wa Mungu (kama vile Ufunuo 7). Angalia maelezo katika Ufu.7:2.

**14:2 "nikasikia sauti kutoka mbinguni kama"** Hivi vifungu bainifu vilitumika kwa sauti ya Mungu katika Eze. 43:2, kwa sauti ya Yesu katika Ufu. 1:15, na kwa sauti ya makutano ya mbinguni katika Ufu. 19:6. Mara nyingi mstari huu unatumika kuashiria kwamba huyu mnenaji yuko mbinguni (kama vile Ufu. 4:5; 11:19; 16:8).

**14:3 "na kuimba wimbo mpya mbele ya kile kiti cha enzi"** Hili ni dokezo la Ufu. 5:9. Ile "wa" inaweza kurejelea juu ya

1. Viumbe wa kimalaika waliokuwa wakiimba wimbo katika Ufu. 5:9
2. Ule wimbo wa mia na arobaini na nne elfu katika ile sehemu ya hitimisho la Ufu. 14:3 na 15:2
3. Hili ni dokezo la Isa. 42:10 na bila shaka Zab. 33:3; 40:3; 96:1; 98:1; 144:9; 149:1
   Zile zama mpya za Roho zilizoahidiwa zimekuja!

◙**"wazee"** Angalia maelezo katika Ufu. 4:4.

◙**"walionunuliwa katika nchi"** Hii ni dhana ya Agano la Kale ya yenye uhusiano wa karibu na kuachiwa huru kwa mmoja wa wanafamilia (*go'el*, yaani, Ruthu na Boazi). Hii inatumika kwa wale ambao Kristo aliwafia (kama vile Ufu. 5:9; 7:14).
Mada Maalum: Fidia/Ukombozi (Specia Topic: Ransom/Redeem)

**14:4 "Hawa ndio wasiotiwa unajisi pamoja na wanawake"** Kumekuwa na mjadala mkubwa kuhusiana na mstari huu kwa sababu unaonekana kumaanisha kwamba huu ni uteuzi, kundi la wanaume waseja wapatao 144,000 wa sura ya saba 7. Hata hivyo, Nafikiri kwamba vifungu hivi vinaweza kuelezwa katika ishara, au angalau, katika maneno ya Agano la Kale, na kamwe hayakumaanisha kuchukuliwa kifasihi. Kifungu cha maneno "wasiotiwa unajisi pamoja na wanawake" kinaweza kueleweka katika njia kadhaa.

1. kifasihi hiki kinamaanisha useja
2. hiki kinarejelea ile zinaa ya kiroho na yule mnyama au yule kahaba mkuu (kama vile Ufu. 14:8; 17:2; 18:9)
3. hiki kinarejelea yale maneno maalum yaliyondikwa kwa makanisa saba (kama vile Ufu. 2:14,20,22; 3:4)
4. hiki kinarejelea zile taratibu za Agano la Kale za kujiutakasa kwa ajili ya ibada au mapigano (kama vile Kut. 19:14-15; Kumb. 23:9-10; 1 Sam. 21:4-5; 2 Sam. 11:6-13
5. ki msingi hiki ni kidokezo cha majina ya watu wa Mungu katika Agano la Kale, "wale mabinti Sayuni walio Bikra" (kama vile 2 Fal. 19:21; Yer. 18:13; Omb. 2:13; Amosi 5:2; 2 Kor. 11:2; Efe. 5:27).

Yatupasa kuzingatia kwamba tendo kujamiina miongoni mwa wanandoa ni kazi ya kiroho. Kujaamiina (ndoa) ni mpango wa Mungu, ni njia yake ya kuijaza nchi, ni amri yake (kama vile Mwa. 1:28; 9:1). Useja kwa hakika ni karama ya kiroho kwa ajili ya huduma (kama vile 1 Wakorintho 7), lakini si hali ya utakatifu. Utawa wa Kiyunani si wa kibiblia (aidha ni kabla ya tendo la kuoa kuolewa)!

Mada maalum: Useja na Ndoa (Special Topic: Celibacy and Marriage)

◙ **"Hawa ndio wamfuatao Mwana-Kondoo kila aendako"** Hili linazungumza kuhusu uanafunzi na huduma (kama vile Yohana 7:17; 10:4).

◙ **"Hawa wamenunuliwa katika wanadamu malimbuko kwa Mungu"** Neno hili lilitumika katika Agano la Kale kuonyesha umiliki wa malimbuko yote ya Mungu (kama vile Kut. 23:19; 34:76). Katika Agano la Kale hili linalirejelea kanisa (kama vile Ebr. 12:23; Yakobo1:18), watu wa Yesu, ambao ni matunda ya kwanza ya ufufuo (kama vile 1 Kor. 15:20,23; Ufu. 1:5).

**14:5 "katika vinywa vyao haukuonekana uongo"** Kuna asili za stiari hii:

1. hii inahusiana na kile kifungu sawa na katka Ufu. 21:27 na 22:15
2. hii inahusiana na ile ibada ya kumwabudu mfalme ambapo Wakristo hawawezi kuikubali amri ya mfalme atesaye kwa kusema, "Mfalme ni Bwana"
3. hii ni ishara ya ule unajisi wa Agano la Kale (kama vile Zab. 32:2; Sef. 3:13)
4. hili lnaweza kuwa rejeleo la ile imani ya uongo kama ilivyo katika Rum. 1:25; 1 Yohana 2:22

◙ **"Maana hawana mawaa"** Hili ni la kifasihi "pasipo hatia" (kama vile Flp. 3:6). Kiuhalisia aya hii inarejea juu ya wanyama wa dhabihu, lakini hapa imetumia kistiari kumaanisha wanadamu (kama vile Nuhu, Mwa. 6:9,17 na Ayubu, Ayubu 1:1). Tena linatumiaka kwa Yesu katika Ebr. 9:14 na 1 Pet. 1:19. Hii ni njia nyingine ya kuyarejelea yale maisha yenye ufanano na Kristo. Kufanana na Kristo ni mapenzi ya Mungu kwa watu wake (kama vile Law. 19:2; Kumb. 18:13; Mt. 5:48; 1 Pet. 1:16).

MADA MAALUM: PASIPO MWAA, PASIPO KOSA, PASIPO HATIA, BILA LAWAMA (SPECIAL TOPIC: BLAMELESS, INNOCENT, GILTLESS, WIOTHOUT REPROACH)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 14:6-7**
**[6] Kisha nikaona malaika mwingine, akiruka katikati ya mbingu, mwenye Injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa, [7] akasema kwa sauti kuu, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji.**

**14:6 "nikaona malaika mwingine, akiruka katikati ya mbingu"** Katika Ufu.8:13 kuna tai anayeruka katikati ya mbingu, ambaye anamaanisha kile kitu kinachoonekana vema na chenye uwezo wa kutangaza dunia mzima.

◙**"Injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi"** Kifungu cha maneno, "injili ya milele" kinapatikana hapa pekee. Ni muhimu kwamba ile "injili" ni kwa wale wanaoishi (kaa) juu ya nchi na hii imetumika mara kwa mara katika Ufunuo wa wale wasioamini. Wengine wanaliona hili kama utimilifu wa Mt. 28:18-20 au zaidi hasa, Mt. 24:14 na Marko 13:10. Yale yaliyomo ndani ya injili hii yanafanana sana na ule ujumbe wa Yohana Mbatizaji (kama vile Luka 3:3-14) au ule usemi wa Yesu kwa yule mwovu katika Mt. 4:10. Ule ujumbe wa hukumu ni jambo la muhumu katika injili hii. Mistari ya 6-7 ni muhimu, au ile yenye kutuonyesha hukumu zote za Mungu zilizotumwa kwa mwanadamu aliyepotea zenye makusudi ya ukombazi (kama vile Ufu. 9:20-21; 16:9,11).

Katika Ufu. 14:12 waamini wa kweli wanabainishwa kama wale (1) kuzishika (yaani, WAKATI ULIOPO ENDELEVU) amri za Mungu na (2) kuishika (yaani, kitenzi kile kile cha WAKATI ULIOPO ENDELEVU) katika Yesu.

Mada Maalum: Injili (Specia Topic: The Gospel)

◙**"na kila taifa na kabila na lugha na jamaa"** Angalia maelezo katika Ufu. 10:11.

**14:7 "na kila taifa na kabila na lugha na jamaa"** Hii ni KAULI YA KITENZI TENDEWA (yenye ushahidi) SHURUTISHI na KAULI YA KITENZI TENDAJI SHURUTISHI. Kuna KAULI YA KITENZI SHURUTISHI katika Ufu.14:7. Mwanadamu anaamriwa kuwa na mwitikio kwa Mungu katika matendo muhimu ya imani (kama vile Yohana 1:12; Rum. 10:9-13). Katika Ufu. 11:13 mwanadamu aliyeanguka anaonekana kumpa Mungu utukufu, lakini ni mwepesi wa kukimbilia miujiza ya yule myama wa 13 (theolojia inayofanana na ule Mfano wa Udongo katika Mathayo 13; Marko 4; Luka 8).

Mada Maalum: Utukufu (*kabod*, Agano la Kale) (Specia Topic: Glory *(*kabod, OT)

Mada Maalum: Utukufu (*doxa*, Agano Jipya) (Specia Topic: Glory (doxa, NT)

◙ **"kwa maana saa ya hukumu yake imekuja"** Hili neno "saa" ni muhimu katika Injili ya Yohana (kama vile Yohana 2:4; 4:21,23; 5:25,28; 7:30; 8:20; 12:23,27; 13:1; 16:21,32; 17:1). Hili linazungumzia juu ya ule wakati wa tukio lililopo la Uungu (ile siku ya Bwana, kama vile Ufu. 14:15 na 9:15).

MADA MAALUM: SAA (SPECIAL TOPIC: THE HOUR)

Mada Maalum: Hukumu katika Agano Jipya (Specia Topic: Judgment in the NT)

◙ **"Msujudieni yeye"** Hii ni kauli nyingine YA KITENZI TENDAJI SHURUTISHI chenye kumaanisha kitendo muhimu.

Mada Maalum: Kusujudu (Specia Topic: Worship)

◙ **"aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji"** Hii ni sawa na ule ukubalifu uanaopatikana katika Matendo 14:15, ambayo inanukuu Mwa.14:19; Kut.20:11 au Zab. 146:6. Mungu anaelezwa kama muumbaji kama katika Ayubu 38-41. Kifungu pekee kisicho cha kawaida ni "chemchemi za maji," ambacho wengine wanakiona kama

1. chenye kuhusiana na yale mapigo ya kale ya malaika (kama vile Ufu. 8:10)
2. katika utofauti wa maji ya bahari yasiyonyweka

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 14:8**
**[8] Kisha mwingine, malaika wa pili, akafuata, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa, maana ndio uliowanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake.**

**14:8 "Umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa"** Hiki KITENZI hakikirudiwa tu, bali kimetokea katka sentensi ya kwanza ya Kiyunani, kusistiza KAULI HIZI ZA VITENZI TENDAJI ELEKEZI. Ni vigumu kukifasiri kitabu cha Ufunuo kwa sababu dhana zimepanuka katika maeneo mbalimbali (huyu mnyama ameelezewa kwa ufupi katika Ufu. 11:7 lakini hakujadiliwa hadi sura ya 13). Mjadala kamili wa kuanguka kwa Babeli unapatikana katika Ufu. 16:19 na 17:1-18:24. Hili linamaanisha Rumi (kama vile 1 Pet. 5:13; II Baruch 11:1; 67:7; Sibylline Oracles 5:143, 159, 424), hatimaye hili linamaanisha ile jamii ya wanadamu wote waliojikusanya na kutenda kinyume na Mungu. Huku kujitegemea kwa mwanadamu ni matokeo ya moja kwa moja ya anguko (kama vile Mwanzo 3) na kwa mara ya kwanza hili linaelezwa katika ule Mnara wa Babeli (kama vile Mwanzo 10-11). Zile dora za kiulimwengu zimekuwa kinyume na Mungu, ambapo zitahusika na hatima ya ule ufalme wa ulimwengu wa yule Mpinga Kristo katika wakati wa mwisho (kama vile Dan. 2:7-8). Hili linaweza kuwa dokezo la Isa. 21:9; Yer. 51:8.

[Mada Maalum: Serikali ya Mwanadamu (Special Topic: Human Government)]

◙ **"ndio uliowanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake"** Hili dokezo ni la Yer. 51:7-8 (kama vile Ufu. 17:2,4; 18:3). Hili neno "ghadhabu" ni neno la Kiyunani "*thumos,*" ambalo linahusianisha ule mlipuko wa hisia (tazama maelezo kamili katika Ufu. 7:14, kama vile 17:2,3; 18:3). Wale wainywao mvinyo ya Babeli watainywa mvinyo ya YHWH (kama vile Ufu. 14:9)!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 14:9-12**
[9] **Na mwingine, malaika wa tatu, akawafuata, akisema kwa sauti kuu, Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake,** [10] **yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo.** [11] **Na moshi wa maumivu yao hupanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana wala usiku, hao wamsujuduo huyo mnyama na sanamu yake, na kila aipokeaye chapa ya jina lake.** [12] **Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu**

**14:9 "aki. . ."** Hii SENTENSI SHURUTISHIDARAJA LA KWANZA yenye VITENZI viwili, "kusujudu"na "kupokea." Wanadamu wengine, wanadamu walio wengi, watayatenda matendo yenye kuambatana na ibada ya sanamu. Hiki ni kinyume halisi cha kumpokea Masihi wa Mungu katika Ufu. 14:7 na 12. Ndiyo wale watakaokumbana na ghadhabu ya Mungu (kama vile Ufu. 14:10).

**14:10 "yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu"** Wanadamu wanao uchaguzi wa kiroho katika namna mbili, Mungu au uovu. Neno la Kiyunani ghadhabu *orgē* linarejelea juu ya "lile suluisho la upinzani." Angalia maelezo kamili katika Ufu.7:14. Ni dokezo la Isa. 51:17 au Yer. 25:15-16 (kama vile Ufu. 16:19; 19:15). Waamini lazima wakumbane na ile ghadhabu ya Babeli (kama vile Ufu. 14:8), lakini wale wasioamini watakumbana na ile ghadhabu ya Mungu (kama vile Ufu. 14:10).

Muungano huu wa ajabu wa haya maneno (kifasihi "mchanganyiko na usiomchanganyiko") unamaanisha kwamba ghadhabu ya mvinyo ya Mungu imechanganyika na mambo mengine ili kuifanya ilevye zaidi, lakini ile isiyo changanywa imetiwa maji ndani yake. Hili neno "kikombe" mara nyingi lilitumika katika Agano la Kale kwa ajili ya hukumu (kama vile Isa. 51:17,22; Jer. 25:15-17,27-29; Zab. 75:8). Yesu alikinywea kikombe cha ghadhabu ya Mungu kwa ajili ya wanadamu wote (kama vile Marko 14:36). Ule ulimwengu usioamini hautawajibika kwake kwa imani, na hivyo, walikumbana na kile kikombe wao wenyewe!

[MADA MAALUM: MTAZAMO WA KIBIBLIA KUHUSU KILEO NA ULEVI (SPECIAL TOPIC: BIBLICAL ATTITUDEA TOWARDS ALCOHOL AND ALCOHOLISM)]

◙ **"naye atateswa kwa moto na kiberiti"** Hili ni dokezo la hukumu ya Mungu juu ya Sodoma na Gomora (kama vile Mwa. 19:24,28; Luka 17:29; au hukumu kwa ujumla, kama vile Zab. 11:6; Isa. 34:8-11; Eze. 38:22). Mateso makali ndiyo hatima ya milele ya huyu mnyama (kama vile 19:20), yule mwovu (kama vile 20:10), na yule mwanadamu asiyetubu (kama vile 20:15; 21:8).

Moto ilikuwa sitiari ya Agano la Kale iliyozungumzia juu ya ule utakatifu wa Mungu (kama vile Hes. 9:15-16, n.k.) Huu ulitumika kwa maana ya kusafisha (kama vile Law. 8:17,32; 9:11,24; 13:32,55,57, n.k.) na hukumu (kama vile Law. 10:1-2; Hes 11:1-3, n.k.). Uhusiano huu unaoihusu hukumu ulipanuliwa ili kuelezea ile sehemu yenyewe ya hukumu. Yesu alitumia neno la ziwa la moto huko Yerusalemu ya kusini katika bonde la wana wa Hinnom (*Gehenna*) kama ishara ya ile adhabu ya milele (kama vile Ufu. 20:10, 14-15).

[Mada Maalum: Moto (Specia Topic: Fire)]

**14:11 "Na moshi wa maumivu yao hupanda juu hata milele na milele"** Nafikiri kwamba yanipasa kuamini katika ile mitazao ya kiulimwengu hata katika nafasi ile ya pili kwa ajili ya ile fursa ya mwitikio wa injili, lakini kulingana na Maandiko yawapasa wanadamu kuiitikia ile neema ya Mungu ya bure katika imani (kama vile Marko 1:15; Matendo 3:16,19; 20:21) ambapo huishi (kama vile Heb. 9:27); ikiwa watakaidi kuitikia, matokeo ni ile adhabu ya milele na milele (kama vile Marko 9:47-48; Mt. 25:46; Yohana 5:29; Matendo 24:15; 2 The. 1:6-9). Ile adhabu ya milele kwa wale walio wadhalimu inalinganishwa na yale mateso ya muda mfupi kwa watakatifu. Hili linaungwa mkono katika kifungu "hawa hawatapumzika mchana na usiku," ambapo katika Ufu. 14:13 watakatifu yawapasa kupumzika.

Hili si somo rahisi kulijadili. Upendo wa Mungu na moyo wake kwa ajili ya ukombozi uko katika kutofautisha ile hukumu ya adhabu ya milele. Hukumu za Mungu zilizo nyingi katika kitabu cha Ufunuo ni ukombozi, kama yale mapigo juu ya Misri na zile laana za agano za kile kitabu cha Kumbukumbu la Torati 27-29. Bado, hatimaye mwitikio hasi wa Mungu ni wa kudumu. Hii si ya kinidhamu, ni ya kuadhibu! Hili ni vigumu sana kulielewa, kulishikilia kihisia. Hili linakazia ule uhitaji wa uinjilisti!

Kabla sijalimaliza somo hili hebu nishirikiane nawe lile wazo nililo nalo katika eneo hili. Kama jehanamu ilivyo mbaya kwa wanadamu, pia ni mbaya kwa Mungu. Mungu aliwaumba wanadamu kwa mfano wake kwa ajili ya ushirika. Uumbaji wote ni hatua ya Mungu kukutana na mwanadamu. Mungu aliwapenda wana wote Adamu wa kike na wa kiume (kama vile Eze. 18:32; 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9). Yeye aliwapenda sana hata akakubali kumtuma Mwanae wa pekee kufa badala yao (kama vile Yohana 3:16; 2 Kor. 5:21). Lakini yeye amechagua kuwa wale watenda dhambi yawapasa kuwa na mwitikio kwake katika tumaini, imani, toba, utii, huduma, ibada, na ustahimilivu. Mungu hampeleki mtu ye yote Jehanamu, bali wale wasioamini hujipeleka wao wenyewe (kama vile Yohana 3:17-21). Jehanamu I wazi, kuna damu ya maumivu ndani ya moyo wa Mungu ambayo haitatibika kamwe! Sina uhakika kama ana "siku njema." hasa, yale maumivu ya makusudi katika ile sura ya pendo la dhabihu!

**14:12** Ustahimilivu ndiyo mada kuu katika kitabu kizima (kama vile Ufu. 1:9; 2:7,11,17,19,26; 3:5,10,12,21; 13:10; 21:7). Watu wa Mungu wameonyeshwa kuwa waaminifu hata katikati ya mateso. Angalia maelezo kamili katika Ufu. 2:2.

Mada Maalum: Ustahimilivu (Specia Topic: Perseverence)

◙ **"watakatifu"** Angalia Mada Maalum: Watakatifu (Specia Topic: Saints)

◙ **"hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu "** Maelezo yaliyo sawa kuhusiana na waamini yanapatikana katika Ufu. 12:17. Kumbuka kuwa msistizo uko juu ya ule uhusiano wa imani binafsi na Yesu, ukifuatiwa na yale maisha ya utii (kama vile Ufu. 12:17; Luka 6:46).

Mkristo aliyekomaa ni pamoja na vitu vifuatavyo
1. mtu akaribishaye (awe na uhusiano binafsi na Yesu)
2. kweli kumhusu huyo mtu wa kumwamini (kweli ya mafundisho ya Agano Jipya)
3. maisha ya kuishi kama yule mkristo (ufanano wa Kristo wa kila siku)

Haya yote yanahitajika kwa ajili ya ukomavu, afya, imani iliyokuwa.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 14:13**
**[13]Nikasikia sauti kutoka mbinguni ikisema, Andika, Heri wafu wafao katika Bwana tangu sasa. Naam, asema Roho, wapate kupumzika baada ya taabu zao; kwa kuwa matendo yao yafuatana nao.**

**14:13 "Heri"** Hii ni ya pili kati ya zile heri saba zinazopatikana katika kitabu cha Ufunuo (kama vile Ufu. 1:3; 14:13; 16:15; 19:9; 20:6; 22:7,14).

Mada Maalum: Heri (Agano la Kale) (Special Topic: Blessings (OT)

◙ **"Heri wafu wafao katika Bwana"** Hii linawarejelea wale mashahidi (kama walivyofanya wale 144,000), lakini wakati maalum wa kifo hiki haujulikani. Baadhi ya watoa maoni wanalihusianisha hili na zile siku za Yohana na wengine wanalihusianisha na ule wakati wa mwisho. Ingawa wakati maalumu haufahamiki, ni muhimu kufahamau kwamba kile kifo cha watakatifu wa Mungu ni cha thamani machoni pa Mungu (kama vile Zab. 116:15).

Ingawa kundi hili limeundwa na wale wafia-dini wa Kristo, ni vizuri kulitafsiri hili kama "mashahidi" katika maana ya jumla zaidi ya waamini. Si waamini wote waliouawa katika karne ya kwanza, si wote watakaouawa katika zile taabu za ule wakati wa mwisho, bali waamini wote yawapasa kubaki waaminifu kwa Kristo. Sitiari hii ni hitimishi, si tengefu.

◙**"kwa kuwa matendo yao yafuatana nao"** Hili ni fumbo la Ukristo kuwa waamini wamekirimiwa na Roho katika wokovu kwa ajili ya huduma bora na kwa ajili ya mwili wa Kristo (kamavile 1 Kor. 12:7,11). Mungu huita, hutenga, na kuzalisha matunda ya milele kupitia kwa wale waamini walio wakamilifu. Hii ni neema yake, Yule Roho wake atiaye nguvu, lakini watakatifu huipokea thawabu kwa ajili ya uaminifu wao, upatikanaji, na ustahimilivu (tazama Mada Maalum katika Ufu. 2:10). Waamini hawaokolewi kwa kazi zao (juhudi zao wenyewe), bali wanaokolewa katika kazi iliyonjema (kama vile Efe. 2:8-9,10). Mapenzi ya Mungu kwa kila mwamini ni huduma yenye kufanana na Yesu (kama vile Rum. 8:29; Gal. 4:19; Efe. 1:4)!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 14:14-16**
***14*Kisha nikaona, na tazama, wingu jeupe, na juu ya wingu hilo ameketi mmoja, mfano wa Mwanadamu, mwenye taji ya dhahabu juu ya kichwa chake, na katika mkono wake mundu mkali. *15*Na malaika mwingine akatoka katika hekalu, akimlilia kwa sauti kuu yeye aliyekuwa ameketi juu ya lile wingu, Tia mundu wako, ukavune; kwa kuwa saa ya kuvuna imekuja; kwa kuwa mavuno ya nchi yamekomaa. *16* Na yeye aliyeketi juu ya wingu akautupa mundu wake juu ya nchi, nchi ikavunwa.**

**14:14-16** Kuna mavuno ya aina mbili tofauti tofauti (kama vile IV Ezra 13:10-11) yanayoelezwa katika Ufu. 14:14-16 na 17-19. Ya kwanza ni yale mavuno ya nafaka na ya pili ni yale mavuno ya zabibu. Ikiwa tofauti hizi zinaweza kushikiliwa (katka Yoeli 3:13 haya mazao ya aina mbili yanatazamiwa kama hukumu ya aina moja), zao la aina ya kwanza hurejelea juu ya yale mavuno ya mwenye haki (kama vile Mt. 9:37-38; 13:30,38; Marko 4:26-29; Luka 10:2; Yohana 4:35-38), ambapo mavuno ya pili ya nafaka yaliyotajwa katika Isa. 63:2-6; Jer. 51:33; Omb. 1:15; Yoeli 3:13 na Ufu.19:15 huwarejelea wale wadhalimu.

**14:14 "wingu jeupe, na juu ya wingu hilo ameketi mmoja, mfano wa Mwanadamu, mwenye taji ya dhahabu juu ya kichwa chake,"** Tatizo lenye upekee ule ule katka sura ya 6 na 10 limetumka katika mistari hii. Je, huu ndiyo ubainifu wa yule Masihi wa Uungu (kama vile. Dan. 7:13) au ni malaika mwingine aliyeokoa badala yake? Nafikiri huyu ni malaika mwingine mwenye nguvu, kwa sababu

1. yeye yu katika mtiririrko wa malaika wake (kama vile Ufu. 14:15,17,18)
2. Mt. 13:39, 41-42, 49-50 inasema huyo malaika atawakusanya na kuwatenga watu katika wakati wa mwisho (wengine kwa ajili ya heri na wengine kwa ajili ya hukumu)
3. yule malaika alimsurutisha (kama vile Ufu. 14:15)

**14:15** Hili ni dokezo la Yoeli 3:13.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 14:17-20**
***17* Kisha malaika mwingine akatoka katika lile hekalu lililoko mbinguni, yeye naye ana mundu mkali.**
***18* Na malaika mwingine akatoka katika ile madhabahu, yule mwenye mamlaka juu ya moto; naye akamlilia kwa sauti kuu yule mwenye mundu ule mkali, akisema, Tia mundu wako mkali, ukachume vichala vya mzabibu wa nchi, maana zabibu zake zimeiva sana. *19* Malaika yule akautupa mundu wake hata nchi, akauchuma mzabibu wa nchi, akazitupa zabibu katika shinikizo hilo kubwa la ghadhabu ya Mungu.**

**[20] Shinikizo lile likakanyagwa nje ya mji, damu ikatoka katika shinikizo mpaka kwenye hatamu za farasi, kama mwendo wa maili mia mbili.**

**14:17 "malaika mwingine akatoka katika lile hekalu lililoko mbinguni"** Mstari huu unarejelea juu ya hekalu la kiroho la huko mbinguni (kama vile Ebr. 8:2; 9:11,23-24).

**14:18 "yule mwenye mamlaka juu ya moto"** Malaika wanayo mamlaka ya kulitawala wingu (kama vile Ufu. 7:1), juu ya moto (kama vile Ufu. 14:18), na juu ya maji (kama vile Ufu. 16:5). Mstari huu unarejelea juu ya ile dhana ya Walimu ya Sheria za Dini za Kiyahudi ilikuwa ikizungumzia juu ya uhusishwaji wa kimalaika katika ulimwengu wa asili. Ingawa kitabu cha Agano la Kale hakilisistizi hili, hili halimaanishi kwamba halina usahihi (kama vile Ebr. 1:7,14).

**14:20 "nje ya mji"** Wengine wanaliona hili kama dokezo limdokezalo Kristo aliyesulibiwa nje ya mji (kama vile Ebr. 13:12). Wengine huliona hili kama sheria za utakaso wa kitabu cha Agano la Kale ambapo wale waliokuwa najisi walitolewa nje ya kambi (kama vile Ufu. Law. 8:17; 9:11). Hata hivyo, hili linaweza kudokeza juu ya kile kitendo cha kuwakusanya maadui wa Mungu waliouzunguka mji wa Yerusalemu katika ule wakati wa mwisho (kama vile Zab. 2:2,6; Dan. 11:45; Yoeli 3:12-14; Zek. 14:1-4; na kile kitabu cha I Enoch 53:1 cha kipindi cha Agano la Kale na Agano Jipya chenye kueleza juu ya yale mafunuo ya matukio ya siku za mwisho). Tena hapa, lile tatizo la kipi kilicho cha kimaandishi na kipi kilicho cha kitamathali linakuwa jambo kuu la kufasiri!

◙ **"damu ikatoka katika shinikizo mpaka kwenye hatamu za farasi, kama mwendo wa maili mia mbili"** Haya yatakuwa matokeo ya yale mapambano makubwa ambayo yanaelezwa katika zile sura zinazofuatia, au ile sitiari ya pekee iliyotokana na ile rangi ya juisi ya nafaka. Swali halisi ni aidha ni ya kimaadishi au ya kiishara. Je, Hili linaeleza juu ya yale mapambano katika wakati/nafasi au yale mapambano ya kiishara ya kiulimwengu kuyahusu mema na mabaya? Kukifunza kunakoelekea katika hatima, lakini maneno ya Mathayo 24; Marko 13; na Luka 21 yanafundisha hata yale yaliyopita.

Muda halisi haufahamiki. Wengine husema (1) maili 65; (2) maili184; au (3) maili 200 Maneno yaliyo sahihi ni mita 6,600. Hii si idadi ya ishara ya kawaida. Wengine husema hili linarejelea juu ya ule umbali kutoka Dani hadi Bersheba, ambapo hili linamaanisha ile hukumu ya kiishara iliyoizunguka Nchi Takatifu.

Neno "shinikizo" ni sitiari ya hukumu (kam vile Isa. 63:3; Omb. 1:15). Bila shaka hii ni kwa sababu ya ule ufanano kati ya ule wekundu wa juisi ya barungi na damu. Hili pia limetajwa katka Ufu.19:15.

◙ **"ile ghadhabu ya Mungu"** Angalia maelezo kamili katika Ufu.7:14.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa usomaji wa hitifaki, ambayo inamaanisha kwamba unao wajibu wa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu lazima aenende katika nuru tuliyo nayo. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Unalazimika kutokuondoa hili toka kwa msemaji

Maswali haya ya kujadili yanatolewa kukusaidia mambo muhimu ya kipengele cha kitabu hiki. Yamekusudiwa kukuchokonoa mawazo, yasiyo ya hakika.

1. Nini uhusiano kati ya 144,000 inayopatikana katika sura za 7 na 14?
2. Je, Mlima Sayuni unalejelea nini?
3. Je, vile vigezo vinavyopatikana katika Ufu. 14:4 ndivyo vielelezo vya wale watu wa Mungu waliochaguliwa kwa ajili ya kumfurahia?
4. Je, ni nini umuhimu wa Ufu. 14:6 na 7?
5. Je, Babeli ni nani?
6. Je, Jehanamu ni ya milele?
7. Je, ni mtu gani akaaye mawinguni katika Ufu. 14:14-16 na kwa nini?

# UFUNUO 15-16

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Malaika mwenye mapigo ya mwisho | Kutangulizwa bakuri lenye hukumu | Bakuli ya saba ya ghadhabu ya Mungu | Malaika mwenye mapigo ya mwisho | Wimbo wa Musa na Mwana-kondoo |
| 15:1 | 15:1-16:1 | 15:1 | 15:1 | 15:1-4 |
| 15:2-4 | | 15:2-4 | 15:2-4 | Bakuli ya saba Ya mapigo |
| 15:5-8 | | 15:5-16:1 | 15:5-8 | 15:5-8 |
| Bakuli la ghadhabu ya Mungu | | | Bakuli lenye hasira ya Mungu | |
| 16:1 | Bakuli la kwanza: pakawa na jipu baya,bovu | | 16:1 | 16:1 |
| 16:2 | 16:2 Bakuli la pili: bahari ikawa damu | 16:2 | 16:2 | 16:2 |
| 16:3 | 16:3 Bakuli la tatu: maji yakageuka damu | 16:3 | 16:3 | 16:3 |
| 16:4-7 | 16:4-7 Bakuli la nne: Watu wakaungua | 16:4-7 | 16:4-7 | 16:4-7 |
| 16:8-9 | 16:8-9 Bakuli la tano: Giza na maumivu | 16:8-9 | 16:8-9 | 16:8-9 |
| 16:10-11 | 16:10-11 Bakuli la sita: Mto Frate unakauka | 16:10-11 | 16:10-11 | 16:10-11 |
| 16:12-16 | 16:12-16 Bakuli la saba: miji ya mataifa ikatetemeka | 16:12-16 | 16:12-14 | 16:12-16 |
| | | | 16:16 | |
| 16:17-21 | 16:17-21 | 16:17-21 | 16:17-21 | 16:17-21 |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka" **Mwongozo wa Usoma Mzuri wa Biblia"(A Guide to Good Bible Reading")**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

17. Aya ya kwanza
18. Aya ya pili
19. Aya tatu

20. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA UFUNUO 15:1-16:21

A. Bakuli saba ambazo zimetambulishwa katika Ufu. 15 na kuelezewa katika Ufu. 16 ni la tatu katika mpango wa mizunguko mitatu ya mapigo yaliyotumwa na Mungu kwa kusudi la ukombozi (kama vile Ufu. 9:20-21; 14:6-7; 16:9,11). Kila mzunguko unapata mapigo uendelevu makali zaidi: 1/4, 1/3, na uharibifu mzima (hukumu na kutengwa kwa uovu). Hii yawezekana ililenga juu ya "kulaani na kubariki" sehemu ya Kumbukumbu 27-28.

B. Kuna uhusiano wa maandishi kati ya mizunguko hii. Muhuri wa saba ni baragumu saba. Baragumu nne za kwanza pia ni ufanano wa moja kwa moja kwa bakuli nne za kwanza.

C. Bakuli la saba ni kuanguka kwa Babeli, ambayo ni sihara ya kuanguka kwa jamii ya mwanadamu aliyeongozwa na kufanya kazi kinyume na Mungu. Katika siku za Yohana ilikuwa Roma. Katika Danieli 2 kila Ufalme wa ulimwengu uliofanikiwa ukawa zaidi na zaidi wa kumpinga Mungu mpaka miisho ya dunia, ufalme unaompinga Mungu ambamo Masihi alizaliwa ambayo ni Roma (tazama utangulizi kwa Danieli 8, www.freebiblecommentary.org.

D. Sura ya 15 na 16 inaleta picha yao kutoka kwenye uzoefu wa mateso ya Waisraeli walipokuwa wanatoka utumwani ( kam ailivyofanya Ufu .12-14). Ukombozi huu wa wakati wa siku za mwisho kutoka kwenye uovu unaonekana kama mwisho wa safari ya kutoka Misri hadi nchi ya ahadi (yaani, ukombozi).

E. Mnyama na makahaba wa Babeli (jamii ya wanadamu waasi) wanashindwa pale Har-Magedoni (Ufu.16:12-16),wakati Shetani anashindwa pamoja na Gogu na Magogu (wanadamu waasi) mwisho sana (kama vile Ufu.20:7-10). Kuja kwa mara ya pili kwa Kristo katika Ufu. 19 ni kuongezeka na utimilifu wa muhuri wa saba na baragumu ya saba na hukumu ya bakuli saba. Hili ni jibu la Mungu kwa swali la wafiadini katika Ufu.6:9-11.

F. Mtatizo katika kufasiri vita hizi za nyakati za mwisho ni:

   1. Aina ya fasihi iliyotumika kuelezea, matukio ya siku ya mwisho/na kinabii.
   2. Wanajishughulisha na hatua zenye mafanikio, mizunguko, au vitendo vya kitamthilia.
   3. Kuna sintofahamu kati ya makundi na ishara.
   4. Kuna ugumu wa kuutenganisha utimilifu wa karne ya kwanza kutoka kwenye utimilifu wa nyakati za mwisho.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 15:1-3a**
[1] **Kisha nikaona ishara nyingine katika mbingu, iliyo kubwa, na ya ajabu; malaika saba wenye mapigo saba ya mwisho; maana katika hayo ghadhabu ya Mungu imetimia.** [2] **Tena nikaona kitu kama mfano wa bahari ya kioo iliyochangamana na moto, na wale wenye kushinda, watokao kwa yule mnyama, na sanamu yake, na kwa hesabu ya jina lake, walikuwa wamesimama kando-kando ya hiyo bahari ya kioo, wenye vinubi vya Mungu.** [3] **Nao wauimba wimbo wa Musa, mtumwa wa Mungu, na wimbo wa Mwana-Kondoo, wakisema,**

**15:1 "katika mbingu"** Hii ni ya tatu katika mfululizo wa ishara alizoziona Yohana huko mbinguni.
Mada Maalumu: Mbingu (Special Topic: Heaven)

Mada Maalumu: Mbingu na Mbingu ya tatu (Special Topic: The Heaven and Third Heaven)

◙**" iliyo kubwa, na ya ajabu "**Kifungu hiki hutokea hapa tu na kuelekeza kwenye dokezo la Agano la kale katika Ufu. 15:3, ambalo linaweza kuja kutoka kwenye moja ya sehemu kadhaa (yaani Kum.32:3-4; Zab. 111:2; 139:14;

au Hos. 14:9). Aya ya 3-4 inafanya dokezo moja refu lenye mitindo mingi ya Agano la kale kutoka sehemu kadhaa zinazowezekana.

◙ **"ghadhabu ya Mungu"** Angalia Maelezo kamili katika Ufu.7:14.

Mada Maalumu: Dhiki Kuu (Special Topic: Tribulation)

◙ **"imetimia"** Hii ni KAULI TENDEWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO USIOTIMILIFU ya *teleō* yenye maana ya kumaliza au kutimiza. Bakuli ni na hukumu ya mwisho juu ya kutokuamini kwa kupinga mamlaka. Hakuna tumaini zaidi ya kutubu na imani, hukumu tu na kutengwa! Inawezekana kitheolojia kwamba mfuatano wa muhuri, baragumu, na bakuli ilikuwa njia ya tumaini la Mungu la toba ya mwanadamu, lakini mwishoni, ni uondoaji jumla wa hukumu yake, na kutengwa kwa uovu kulikothibitishwa! Moto wa milele ndilo chaguo pekee lililobaki.

Mada Maalumu: Mwisho au Ukamilifu (Special Topic: End or Full)

**15:2 "nikaona kitu kama mfano wa bahari ya kioo"** Hili kwa mara ya kwanza limetajwa katika Ufu. 4:6. Kwa sababu ya matumizi yake katika Ufu. 21:1, Inaonekana kuwa sitiari ya Utakatifu wa Mungu, iliyomzuia binadamu mdhambi kumakaribia yeye (yaani, yumkini sitiari kwa maji ya mbinguni). Siku moja kizuizi hiki kitaondolewa. Dokezo kwa Agano la kale ama ni Kut. 24:10 au Ezek. 1:22; 10:1. Tazama Maelezo kamili katika Ufu.4:6.

◙ **"iliyochangamana na moto"** Hiki ni kipengele kipya kisichopatikana katika Ufu.4:6. Kumekuwepo na nadharia kadhaa.

1. Ni muundo wa jua ulioaksi juu ya historia ya mwanadamu
2. Huwakilisha moto ambao husimama kwa hukumu ya Mungu
3. Ni damu ya wafiadini
4. Imehusianishwa na ushindi katika Bahari ya shamu na wimbo wa Musa tangu historia ya Agano la kale pale sura ya 15 na 16 ni mapigo ya kutoka kwenye kipindi cha mateso ya Wamisri (kama vile Kut 7-12; 15)

**NASB "na wale wenye kushinda"**
**NKJV "na wale ambao wana ushindi"**
**NRSV "na wale ambao walishinda"**
**TEV "na wale ambao walishinda ushindi"**
**NJB "na wale waliokuwa wamepigana dhidi yao"**

Mwanzoni hii inaonekana kurejelea kwa wafiadini, lakini Ufu.12:11 huonyesha kwamba inapaswa kuwekwa kwa wale ambao wamepata vifo vya asili lakini wasiomwabudu huyo mnyama (kama vile Ufu 20:4).

**NASB "watokao kwa yule mnyama, na sanamu yake, na kwa hesabu ya jina lake"**
**NKJV " juu ya mnyama, juu ya sanamu yake na juu ya alama yake"**
**NRSV "mnyama na sanamu yake na hesabu ya jina lake"**
**TEV " juu ya mnyama na sanamu yake na juu ya wale ambao majina yao yaliwakilishwa na hesabu"**
**NJB "mnyama na watu, na dhidi ya sanamu yake na hesabu ambayo ni jina lake"**

Mnyama mara ya kwanza ametajwa katika Ufu.11:7. Kutoka katika sura ya 13 ni dhahiri kwamba kuna wanyama mwitu wawili: mmoja ni yule aliyepewa mwili wa Shetani (yaani, kumwiga Kristo ) na mwingine ni unabii wake wa uongo (yaani, kumwiga Roho). Kutoka Ufu. 13:18 tunajua kwamba hesabu yake ni 666, ambayo tunajua sio hesabu ya mtu kama ilivyo kwenye anguko na uhaba wa jamii ya binadamu (yaani, serikali) mbali na Mungu.

◙**"walikuwa wamesimama kando-kando ya hiyo bahari ya kioo "** Baaadhi ya tafsiri zina neno "juu ya" (NASB, NKJV), na nyigine zina neno"kando ya" (NRSV) au neno"karibu na" (TEV, NJB). Maana ya msingi wa KIHUSISHI cha Kiyunani ni neno"juu ya." Sitiari hii huzungumzia kwa wale washindi kuwa karibu na Mungu. Neno "bahari" katika ufunuo husimama kwa utengano kati ya Mungu Mtakatifu na uumbaji wenye dhambi. Bahari hii imeondolewa

kabisa katika Ufu.21:1 wakata ushirika kamili ulirejeshwa (yaani, ushirika wa bustani ya Edeni ulirejeshwa). Kwa chaguzi za ufasiri juu ya maana ya "bahari ya kioo" angalia maelezo katika Ufu.4:6.

◙ **"wenye vinubi vya Mungu"** Malaika wameelezewa kama wana vinubi katika Ufu. 5:8 na 14:2. Katika mazingira haya inarejelea kwa waaminio ambao wanafanana na watu 144,000 wa sura ya 14. Kama vile malaika walivyoabudu wakiwa na muziki mbele za Mungu huko mbinguni, sasa pia, waaminio washindi!

**15:3 "Nao wauimba wimbo wa Musa. . . na wimbo wa Mwana-Kondoo"** Hii huonyesha umoja wa agano la kale na agano jipya katika wimbo huu wa ukombozi. Wimbo wa Musa ni dokezo kwa Kut. 15:1-19, ambapo Musa anamshukuru Mungu kwa kumshinda Farao katika Bhari ya shamu. Hata hivyo, inawezekana kwamba Yohana alikuwa na Kumbukumbu 32 kwenye fikra kwa sababu kifungu cha kwanza kinaweza kuwadokezo kwa Kum. 32:3-4. Wimbo wa Mwana-kondoo hapo awali umetambuliwa katika Ufu. 5:9 na 14:3. Tazama kwamba ni wimbo wa ushirika, sio binafsi, wa ukombozi (kama vile Mwa. 3:15).

◙ **"mtumwa wa Mungu"** Hii ni sifa ya heshima kwa wahusika wa Agano la kale kama Musa, Yoshua, na Daudi. Inaweza kuwa asili ya Paulo "mtumwa wa Kristo." Mada Maalum: Mtumishi Wangu(Special Topic: My Servant)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 15:3b-4**
**[3B]NI MAKUU, NA YA AJABU, MATENDO YAKO, EE BWANA MUNGU MWENYEZI; NI ZA HAKI, NA ZA KWELI, NJIA ZAKO, EE MFALME WA MATAIFA. [4] NI NANI ASIYEKUCHA, EE BWANA, NA KULITUKUZA JINA LAKO? KWA KUWA WEWE PEKE YAKO U MTAKATIFU; KWA MAANA MATAIFA YOTE WATAKUJA NA KUSUJUDU MBELE ZAKO; kwa kuwa matendo yako ya haki yamekwisha kufunuliwa.**

◙ **"NI MAKUU, NA YA AJABU,MATENDO YAKO"** Hili ni dokezo lenye sehemu mbali mbali kwa Zab.40:5; 92:5; 111:2; 139:14 na Hos 14:9.

◙ **"EE BWANA MUNGU MWENYEZI"** Hili ni dokezo kwa sifa tatu zaidi zilizotumika katika Agano la kale kwa Mungu (kama vile Ufu. 1:8; 4:8; 11:7; 16:7).

1. Neno "Bwana" linarejelea kwa YHWH,mwokozi, mkombozi,agano la Mungu.
2. Neno "Mungu" linarejelea kwa *Elohim*, muumbaji, mtoaji na muendelezaji wa maisha yote duniani.
3. Neno " mwenyezi" linarejelea kwa *El Shaddai*, jina la mkuu wa kaya kwa Mungu wa ibrahimu, Isaka, na Yakobo (kama vile Kut. 6:3).

Angalia MADA MAALUM: MAJINA YA UUNGU (SPECIAL TOPIC: NAMES FOR DEITY), C. na D.

Mada Maalum: *Shaddai* (Special Topic: *Shaddai)*

◙ **"NI ZA HAKI, NA ZA KWELI, NJIA ZAKO"** katikati ya mateso ya watakatifu, msisitizo huu ni wa muhimu sana (kama vile. 16:7). Hili linawezakuwa dokezo kwa Hosea 14:9.
Mada Maalumu: haki (Special Topic: Righteousness)

Mada Maalumu: Kweli (neno) katika maandiko ya Yohana (Special Topic: Truth (the term) In John's Writtings)

**NASB, NRSV, TEV, NJB "ee mfalme wa mataifa"**
**NKJV "ee mfalme wa watakatifu"**

Kuna tafsiri tatu tofauti za aya hii zinazopatikana katika kiingereza cha leo.

1. Mfalme wa milele" (ASV, NIV, REB) ambayo inapatikana katika Kiyunani cha kale MSS $P^{47}$, א [*,2], na C (kama vile 1 Tim. 1:17; I Enoki 9:4)
2. "Mfalme wa mataifa" (NRSV, TEV, NJB) ambayo inapatikana katika MSS א[a], A, P, na herufi ndogo sana (kama vile Ufu. 15:4; Yer. 10:7)

3. “Mfalme wa watakatifu” (NKJV) MSS 296, 2049 (Metzger, *Textual Commentary*, uk. 753) litokanalo na kutokuelewana kwa maandiko ya kilatini ya kale.

Chaguo #2 labda ndilo lililo la asili. Toleo la UBS[4] huipatia daraja "B" (karibu hakika).

Mada Maalum: Uhakiki wa Tofauti Za Kiuandishi ( Special Topic: Textual Criticism)

**15:4 "NI NANI ASIYEKUCHA, EE BWANA, NA KULITUKUZA JINA LAKO"** Huyu ndiye Mtakatifu wa uumbaji aliepita uwezo wa Binadamu (kama vile Ufu. 14:7; Yer. 10:7-10). Bado yeye hutoa wokovu kwa yeyote na atakaye mhofu Yeye na kulitukuza jinalake.
Mada Maalum: " Jina" la YHWH (AGANO LA KALE (Special Topic: “The Name” of YHWH (OT)

◙ **"KWA MAANA MATAIFA YOTE WATAKUJA NA KUSUJUDU MBELE ZAKO"** Katika unabii wa Agano la kale mataifa yote siku moja wataingia Yerusalemu (kama vile Zab. 22:27; 66:4; 86:9; Isa. 2:2-4; 19:19-24; 27:13; 56:7; 66:19-24; Mal. 1:11). Yohana anatumia unabii wa Agano la kale na matumizi ya tamathali za semi kuelezea juu ya wokovu wa ulimwengu. Yerusalemu ya Agano la kale imekuwa Yerusalemu ya mbinguni kwa Wayahudi wanaoamini pamoja na mataifa. Kitabu hiki hakilengi kwa Wayahudi dhidi ya mataifa kama Agano la kale lilivyofanya, bali juu ya waaminio dhidi ya wasioamini (linganisha Isa. 45:23 pamoja na Flp. 2:9-11). Tazama Utangujlizi Muhimu katika mwanzo wa fasiri.Mada Maalum: Kusujudu (Special Topic: Worship)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 15:5-8**
**5 Na baada ya hayo nikaona, na hekalu la hema ya ushuhuda mbinguni lilifunguliwa; 6 na wale malaika saba, wenye mapigo saba, wakatoka katika hekalu, wamevikwa mavazi ya kitani safi, ya kung'aa, wamefungwa vifuani mwao mishipi ya dhahabu. 7 Na mmoja wa wale wenye uhai wanne akawapa wale malaika saba vitasa saba vya dhahabu, vimejaa ghadhabu ya Mungu, aliye hai hata milele na milele. 8 Hekalu likajazwa moshi uliotoka kwenye utukufu wa Mungu na uweza wake. Wala hapakuwa na mtu aliyeweza kuingia ndani ya hekalu, hata yatimizwe mapigo saba ya wale malaika saba.**

**15:5 "na hekalu la hema ya ushuhuda mbinguni lilifunguliwa "** Katika Ufu. 4:1 mlango wa mbinguni ulifuguliwa kwa ajili ya Yohana; katika Ufu. 11:19 sanduku la agano lilionekana ndani ya hekalu ili waaminio walione. Sasa hema lote la kimbingu linaonekana (kama vile Kut. 25:9,40; 38:21; Hes. 10:11; 17:7; Mdo 7:44). Dokezo hili la Agano la kale limeendelezwa katika Ebr.8:5 na 9:23. Kitengo hiki cha fasihi kinatumia kipindi cha kutoka katika mateso ya Waisraeli na kipindi cha safari ndefu jangwani kama pazia la nyuma la Agano la kale. Hii huashiria kipindi cha pili na mwisho cha mateso ya Waisrael kutoka katika utumwa (utumwa wa dhambi).

**15:6 "wamevikwa mavazi ya kitani safi, ya kung'aa"** hawa viumbe saba wa kimalaika wanakuja kutoa kwenye sehemu ya katikati kabisa pa hekalu la mbinguni, ambayo huonyesha mamlaka kwa sababu wanatoka katika uwepo wa karibu na Mungu. Katika walimu dini ya kiyahudi kuna malaika saba wenye uweza wamezunguka kiti cha enzi cha Mungu, waitwao “malaika wa uwepo.”

Mavazi yao yameelezewa kama (1) "kitani" (*linon* or *linoun* [P[47]]) ambayo yalikuwa yanavaliwa na makuhani katika Kut. 28:4 (UBS[4],daraja "B") au (2) ASV hutafsiri hili kama “jiwe lenye thamani” (*lithon*) ambayo hufuata miswada ya Kiyunani ya Herufu kubwa A na C, na inaweza kuwa dokezo kwa Ezek. 28:13 kama vazi la kimalaika la bustani ya Eden.

Ikiwa misingi miwili ya dhanio la uhakiki wa maandishi (tazama kiambatisho): (1) yale yaliyo magumu kusoma yumkini ndiyo chimbuko na (2) usomaji wake mzuri unaoelezea utofauti pengine ndio asili, kisha “jiwe” yamkini ndilo chaguzi.

◙ **"wamefungwa vifuani mwao mishipi ya dhahabu"** Hii inafanana sana na malaika anayepatikana katika Dan. 10:5 au Kristo mwenyewe katika Ufu. 1:18. Dhahiri hawa ni malaika wenye nguvu sana wanamwakilisha Mungu au Kristo.

**15:7 "vitasa saba vya dhahabu, vimejaa ghadhabu ya Mungu"** Bakuli hizi ya dhahabu yenye kina kifupi zimetajwa katika Ufu.5:8, ambapo pana maombi ndani yake ya watakatifu. Kuna muunganiko katika kitabu chote cha Ufunuo kwa maombi ya watoto wake walioteswa na ghadhabu ya Mungu juu ya wasioamini (tazama maelezo katika Ufu.7:14).

◙ **"aliye hai hata milele na milele"** Hiki ni kiapo kinachotegemezwa juu ya mzizi wa maana ya neno YHWH (kama vile Kut. 3:14). YHWH ndiye pekee aishiye: wengine wote wanapata uzima kutoka kwake. Mada Maalum: Majina ya Uungu (Special Topic: Names for Deity) D.

MADA MAALUMU: MILELE (lahaja ya Kiyunani) [SPECIAL TOPIC: FOREVER (Greek Idiom)

MADA MAALUMU: MILELE (*'olam*) [SPECIAL TOPIC: FOREVER *('olam*)

**15:8 "Hekalu likajazwa moshi uliotoka kwenye utukufu wa Mungu"** Haya yalikuwa maelezo ya kawaida katika Agano la kale ya uwepo wa Mungu (kama vile Kut. 19:18; 40:34; 1 Fal. 8:10-11; 2 Nya. 5:13-14; Isa. 6:4). Hili ni dokezo kwa wingu la *Shekinah* la utukufu ambalo liliwakilisha uwepo wa Mungu kwa Israeli wakati wa kipindi cha Waisrael kutoka katika mateso. Lakini kwa sababu ya uhusiano wa kimktadha na bakuli, inaweza kurejelea kwa wingi wa uvumba ukiwakilisha maombi ya watoto wa Mungu wa haki.
MADA MAALUMU: UTUKUFU (*kabod*, AK) [SPECIAL TOPIC: GLORY (*kabod*, OT)

◙ **"Wala hapakuwa na mtu aliyeweza kuingia ndani ya hekalu, hata yatimizwe mapigo saba ya wale malaika saba"** Hii yawezekana ina maanisha kwamba hapakuwapo na kuzuia ghadhabu ya Mungu pale inapokuwa imekwisha kuanza. Ghadhabu hii ni ngumu kuilinganisha kitheolojia na Ufu. 16:9 na 11, ambayo ina maanisha kwamba ukombozi bado ndilo lengo, hata katika bakuli bado ndilo tumaini na nia kwamba mwanadamu aliyeanguka, aliyefanywa kwa mfano wa Mungu, atatubu na kumrudia Mungu!

# UFUNUO 16

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 16:1**
[1] **Nikasikia sauti kuu kutoka hekaluni, ikiwaambia wale malaika saba, Enendeni, mkavimimine vile vitasa saba vya ghadhabu ya Mungu juu ya nchi.**

**16:1 "Nikasikia sauti kuu kutoka hekaluni, ikiwaambia wale malaika saba"** Ufunuo 15:8 yaonyesha kwamba hii lazima itakuwa sauti ya Mungu mwenyewe.Kundi hili la mwisho la malaika lilikuwa na mamlaka ya mwisho kuangamiza dunia ya Mungu. Katika Agano la Kale malaika wa kifo na malaika wa maangamizi ni watumishi wa Mungu, sio shetani.

◙ **"Enendeni, mkavimimine vile vitasa saba vya ghadhabu ya Mungu juu ya nchi"** Hii ni ishara ya Agano la Kale ya hukumu ya Mungu juu ya mataifa yasiyo amini (kama vile Zab 79:6; Yer. 10:25; Ezek. 22:31; Zef. 3:8). Neno hili latumika katika muktadha huu kwa ghadhabu ya wasioamini (tazama nukuu katika Ufu. 7:14, kama vile Ufu. 16:1,2,3, 4,8,10,12,17) kwa sababu ya

1. Kufuru yao (kama vile Ufu. 16:9)
2. Kutesa kwao wasio amini (kama vile Ufu. 16:6)
3. Kiburi chao cha kukataa kutubu (kama vile Ufu. 9:20-21; 16:9-12)

Kwa "ghadhabu ya Mungu" tazama maelezo kamili katika Ufu.7:14.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 16:2**
[2] **Akaenda huyo wa kwanza, akakimimina kitasa chake juu ya nchi; pakawa na jipu baya, bovu, juu ya wale watu wenye chapa ya huyo mnyama, na wale wenye kuisujudia sanamu yake.**

**16:2** Bakuli hili la kwanza linafanana sana na mojawapo ya Mapigo ya Wamisri (kama vile Kut. 9:10-11). Baadhi wanaliona hili kama limehusishwa na Kumb. 28:35, ambalo liko katika sehemu ya laana na baraka ya kufanya upya agano la Musa. Inapaswa kuelezewa kwamba,kama mapigo ya Wamisri, mapigo haya yaliwaathiri wasioamini.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 16: 3**
[3] **Na huyo wa pili akakimimina kitasa chake juu ya bahari, ikawa damu kama damu ya mfu, na vitu vyote vyenye roho ya uhai katika bahari vikafa.**

**16:3-4** Bakuli la pili na la tatu yanawiana na baragumu la pili na la tatu (kama Ufu. 8:8-11) na pia yanaaksi mapigo ya kipindi cha Waisrael kutoka kwenye mateso katika Kut. 7:17-21; Zab.78:44.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 16:4-7**
[4] **Na huyo wa tatu akakimimina kitasa chake juu ya mito na chemchemi za maji; zikawa damu.** [5] **Nami nikamsikia malaika wa maji akisema, Wewe u mwenye haki, uliyeko na uliyekuwako, Mtakatifu, kwa kuwa umehukumu hivi;** [6] **kwa kuwa walimwaga damu ya watakatifu na ya manabii, nawe umewapa damu wainywe; nao wamestahili.** [7] **Nikaisikia hiyo madhabahu ikisema, Naam, Bwana Mungu Mwenyezi, ni za kweli, na za haki, hukumu zako.**

**16:5 "malaika wa maji"** Hii inaweza kuaksi istilahi ya kipindi kati ya agano jipya na agano la kale cha kiyama ya Wayahudi I Enok 66:2. Katika Ufunuo kulikuwepo na malaika mwenye mamlaka na upepo (Ufu. 7:1) na malaika mwenye mamlaka na moto (Ufu. 14:8), Hivyo si kawaida kumwona malaika mwenye mamlaka na maji. Tena, upatanisho na shughuli za kimalaika ni kawaida katika maandiko ya matukio ya siku ya kiyama kwenye kipindi kati ya agano la kale na agano jipya. Lazima tufasiri Ufunuo katika nuru ya aina yake yenyewe, siku yake yenyewe, na sio mfumo wetu wa theolojia ya magharibi ya leo ya matukio ya siku za mwisho.

◙ **"Wewe u mwenye haki"** Hili ni dokezo kwa wimbo wa Musa katika Kumb.32 (hasa Ufu. 16:5) au yawezekana Zab.119:137.

◙ **"uliyeko na uliyekuwako"** Tambua kwamba hakuna dalili za baadaye kama katika Ufu. 1:4,8; 4:8, kwa sababu hakuna wakati ujao (tazama maelezo kamili katika Ufu. 11:17). Huu ndio mwisho! Hii ni makusudi; Tazama makusudia ya mara tatu ya Ufu. 1:4. Muda haupo tena! Mwisho (yaani, *Parousia*) umefunuliwa mara kadhaa katika Ufunuo, na sio Ufunuo 19 tu. Kila mojawapo ya muhuri, baragumu, na bakuli huishia na kuja mara ya pili kwa Yesu na mwisho wa historia. Hii ndiyo sababu nadhani nadharia ya ufupisho kwa fasiri ya Ufunuo ni bora zaidi!
**16:6 "watakatifu"** Tazama MADA MAALUM: WATAKATIFU(SPECIAL TOPIC: SAINTS)

◙ **"manabii"** Kuhusu unabii Tazama wa Agano la Kale:
MADA MAALUM: UNABII WA (AGANO LA KALE) [SPECIAL TOPIC: PROPHECY (OT)

MADA MAALUM: UNABII WA (AGANO JIPYA) [SPECIAL TOPIC: PROPHECY (NT)

**16:7 "nikaisikia hiyo madhabahu ikisema"** Pembe za madhabahu zilikuwa tayari zimezungumzwa katika Ufu.9:13. hii yaonekana kurejelea kwa (1) nafsi zilizokuwa chini ya madhabahu (kama vile ufu. 6:9; 14:18) au (2) maombi ya watoto wa mungu (kama vile ufu. 8:3-5). Pia yaweza kuwa ni msisitizo dhahili kwa mfano halisi wa kibinadamu.

◙ **"Bwana Mungu Mwenyezi"** Angalia maelezo katika Ufu. 1:8 na 15:3b

◙ **"ni za kweli, na za haki, hukumu zako"** Hili linaweza kuwa dokezo kwa Zab. 19:9; 119:137. Huu ni ukumbusho wenye msaada katikati ya mateso makali kwa Wakristo (kama vile Ufu. 15:4 na 19:2). Mungu ataweka vitu vyote sawa siku moja!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 16:8-9**
**[8] Na huyo wa nne akakimimina kitasa chake juu ya jua, nalo likapewa kuwaunguza wanadamu kwa moto. [9] Wanadamu wakaunguzwa maunguzo makubwa, nao wakalitukana jina la Mungu aliye na mamlaka juu ya mapigo hayo; wala hawakutubu wala kumpa utukufu.**

**16:8** Bakuli la nne ni sawa na muhuri ya sita ya Ufu. 6:12 na inafanana sana na baragumu ya sita ya Ufu. 8:12.

◙ **"nalo likapewa kuwaunguza wanadamu kwa moto"** Jua walilipa nafsi kama ilivyo katika Zab. 19:1-6. Mungu hutawala miili ya mbinguni (kama vile Mwa. 1:14-19).Wao sio Miungu. Wanafanya kazi kama wajumbe (ufunuo wa asili) na ishara kwa ajili ya majira (kwa kuabudu).
MADA MAALUM: MOTO (SPECIAL TOPIC: FIRE)

**16:9 "wala hawakutubu wala kumpa utukufu"** Madhumuni ya ghadhabu ya Mungu ni ukombozi katika Muhuri na Baragumu (kama vile Ufu. 9:20-21; 14:6-7; 16:9,11), Hata hivyo mwanadamu ni mwenye kiburi, wanadamu waasi walikataa kutubu. Katika bakuli tumaini la kutubu limeisha pita: kilichobaki ni hukumu tu!
Mada Maalum: Toba (AGANO JIPYA) [Special Topic: Repentance (NT)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 16:10-11**
**[10] Na huyo wa tano akakimimina kitasa chake juu ya kiti cha enzi cha yule mnyama; ufalme wake ukatiwa giza; wakatafuna ndimi zao kwa sababu ya maumivu, [11] wakamtukana Mungu wa mbingu kwa sababu ya maumivu yao, na kwa sababu ya majipu yao; wala hawakuyatubia matendo yao.**

**16:10 "Na huyo wa tano akakimimina kitasa chake juu ya kiti cha enzi cha yule mnyama"** Kiti cha enzi cha shetani kilipewa mnyama katika Ufu. 11:7. Nguvu yake inaelezewa katika Ufu. 13:2 na kuendelea. Hii inaonekana kurejelea kwa mji mkuu wa siku yake ya mwisho, serikali moja ya ulimwengu.

◙ **"ufalme wake"** Shetani anamwigiza Mungu. Kama Mungu alivyo mfalme, ndivyo na Shetani alivyo na ufalme. Katika sura zilizobaki huduma ya Mungu katika Kristo ni mwigizo wa kubezwa na utatu wa uovu. Ufalme wa shetani, kupitia mnyama, ni wa kimataifa (kama vile Ufu. 13:14-17).

◙ **"ukatiwa giza"** Hili ni dokezo lingine kwa mapigo ya Wamisri (kama vile Kut. 10:21-23). Mungu hutawala nuru (kama vile Ufu.8:12; 9:2; Mwa. 1:5,14-18).

**16:11 "wakamtukana Mungu wa mbingu"** Wasioamini hawa walitambua chanzo na sababu ya maumivu yao, lakini wasingetubu na kurudi kwa Kristo! Mapigo juu ya Misri yalitumwa kuifunua miungu ya uongo ya Misri na kusababisha Wamisri kumwamini Mungu wa Israeli. "Laana" za Kumbukumbu 27-28 zilitumwa kurejesha Wayahudi wasioamini kwenye imani na utii. Hukumu ina lengo la ukombozi (isipokuwa lile la mwisho)!

Sifa ya "Mungu wa mbinguni" ilitumika hapo awali katika Ufu.11:13 na huakisi sifa ya Uungu wa Babeli na Waajemi iliyotumiwa mara nyingi na Danieli (kama vile Dan.2:18, tazama fasiri yangu kwa Daniel katika www.freebiblecommentary.org.

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): UFUNUO 16:12-16**
[12] **Na huyo wa sita akakimimina kitasa chake juu ya mto ule mkubwa Frati; maji yake yakakauka, ili njia itengenezwe kwa wafalme watokao katika maawio ya jua.** [13] **Nikaona roho tatu za uchafu zilizofanana na vyura, zikitoka katika kinywa cha yule joka, na katika kinywa cha yule mnyama, na katika kinywa cha yule nabii wa uongo.** [14] **Hizo ndizo roho za mashetani, zifanyazo ishara, zitokazo na kuwaendea wafalme wa ulimwengu wote kuwakusanya kwa vita ya siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi.** [15] **(Tazama, naja kama mwivi. Heri akeshaye, na kuyatunza mavazi yake, asiende uchi hata watu wakaione aibu yake.)** [16] **Wakawakusanya hata mahali paitwapo kwa Kiebrania, Har-Magedoni.**

**16:12 "Na huyo wa sita akakimimina kitasa chake juu ya mto ule mkubwa Frati"** Mto huu ulitajwa katika Ufu. 9:13-19 wakati majeshi ya kimapepo yalipovuka mipaka yake kuwatesa wanadamu. Maji ya vijito vinavyoingia mto Frati vilikuwa mipaka ya kaskazini ya nchi ya ahadi na nje ya mipaka ya Ufalme wa Warumi. Msingi wa kihistoria kwa sitiari hii ya majeshi ya ki-pepo ilikuwa Kalvari ya Waparthi. Hawa wavamizi wa kutisha wapinga Warumi walikuwa tishio kwa vikosi vya Kirumi.

◙ **"maji yake yakakauka"** Mara nyingi katika Agano la Kale kukauka kwa maji kulionekana kama kitendo cha Mungu kama inavyoonekana katika

1. Bahari ya shamu (kama vile Kut. 14:21)
2. Mto Yordani (Yos. 3:17)
3. Vidokezo kadhaa katika fasihi ya kinabii (kama vile Isa. 11:15-16; 44:27; Yer. 51:36; Zech. 10:11)

Kitendo hiki cha asili kinaashiria kwamba Mungu anaruhusu mgogoro wa siku za mwisho kufikia kilele. Kithiolojia iko sambamba na 2 The. 2:6-7, "nini/nani anazuia."

Mada Maalum:Maji (Special Topic: Waters)

◙ **"ili njia itengenezwe kwa wafalme watokao katika maawio"** Kumekuwepo na mijadala mingi kwa jinsi gani "wafalme wa mashariki" katika Ufu. 16:12 wanavyohusishwa na "wafalme wa ulimwengu wote" katika Ufu. 16:14:

1. wao ni sawa
2. wao ni wapinzani (hadithi za kubuniwa za Nero na Jeshi la Waparthi)
3. wafalme wa mashariki wanarejelea kwa jeshi la Mungu

Kama ndivyo, ni dokezo kwa Mungu kuwaita watu wake kutoka Babeli (kama vile Isa. 41:2,25; 45:1-3; 46:11). Yawezekana kutokana na muktadha kwamba wafalme wa mashariki ni vyombo vya Mungu kwa ajili ya kushambulia majeshi ya mnyama (yaani, dokezo la kihistoria kwa Waparithi kushambulia Roma). Hata hivyo, Ufu.16:14 na sura ya 19 na 20 zinaonyesha kwamba kuna jeshi moja tu la kibinadamu lililoungana kinyume na Mungu (kama vile Zaburi 2; Yer. 25:15-26).

**16:13 "joka, na katika kinywa cha yule mnyama, na katika kinywa cha yule nabii wa uongo"** Hii ndiyo mara ya kwanza ambapo mnyama wa pili (kama vile Ufu. 13:11) anaitwa "nabii wa uongo," lakini kuanzia sasa atakuwa anarejelewa kwa jina hili kila wakati (kama vile Ufu. 16:13; 19:20; 21:10). Zote tatu zinarejelea kwa utatu wa shetani ambao utashindwa katika hatua mbili: wanyama wawili kwenye bonde la Megiddo (kama vile Ufu. 16:12-16) na shetani wakati wa mwisho wa utawala wa Kristo duniani (kama vile Ufu. 20:7-10).

◙ **"roho tatu za uchafu zilizofanana na vyura"** Neno "roho wachafu" litatumika kwenye injili za Agano Jipya kurejelea kwa mapepo. Kwa nini wamepewa sifa kama vyura umekuwa mjadala mkubwa:

1. Hii ni rejeo lingine kwa mapigo ya Misri (kama vile Kut. 8:6)
2. Katika wale wanaoamini uwepo wa Mungu mmoja vyura ni ishara ya uovu wa mwisho
3. Wanarejelea kwa wanyama wachafu (kama vile Ufu. 11:10,31)

MADA MAALUM: MAPEPO (ROHO MCHAFU) [SPECIAL TOPIC: DEMONIC (UNCLEAN SPIRIT)

**16:14 "Hizo ndizo roho za mashetani, zifanyazo ishara"** Inavutia sana kueleza kwamba ishara hizi na maajabu yatawaongoza wasioamini wote mbali na kweli, lakini sio haba kwa wana wa Mungu (kama vile Ufu.13:13; Mt.

24:24; Mk 13:22; 2 The. 2:9-11). Kigezo hiki cha mwisho cha fasihi (bakuli) ni mlinganisho kati ya kile kitakacho watokea watoto wa Mungu na kile kitakachotokea kwa wakazi wa duniani. Kristo huzungumza maneno ya kweli, haki na rehema kuleta amani duniani, lakini roho za vyura wa kipepo husema uwongo na hukusanya watu kwa ajili ya vita.

◙ **"zitokazo na kuwaendea wafalme wa ulimwengu wote"** Hili linaweza kuwa dokezo kwa Zab.2:2, ambalo huunda tamathali za semi katika sura hizi za mwisho za Ufunuo.

◙ **"kuwakusanya kwa vita ya siku ile kuu ya Mungu"** Maelezo ya vita ya nyakati za mwisho yanaonekana katika Ufu. 6:2-8; 11:7-10; 12:17; 16:14; 17:14; 19:19 na 20:8. Yawezekana yote haya yanawakilisha vita moja kutoka katika mitazamo tofauti (yaani,Ufananisho).

**16:15** Kifungu hiki kina maneno ya Kristo ambayo yalihisiwa kutia moya na kuonya watu wa Mungu. Hii ni Baraka ya tatu kati ya baraka saba kwa waaminio (kama vile Ufu. 1:3; 14:13; 16:15; 19:9; 20:6; 22:7,14).

◙ **"naja kama mwivi"** Maneno haya ya Yesu (kama vile Mt. 24:43-44; Lk 12:39-40) yalitumika awali katika Ufu. 3:3 na yalitajwa katika 1 The. 5:2 na 2 Pet. 3:10. Inaonekana kurejelea kwa wakati wowote, kuja kwa gafla kwa Kristo kwa ajili ya hukumu katika *Parousia* (Kuja kwa mara ya pili kwa Kristo).

MADA MAALUMU: KUJA MARA YA PILI (SPECIAL TOPIC: THE SECOND COMING)

◙ **"Heri akeshaye, na kuyatunza mavazi yake"** Hii ni Baraka ya tatu kati ya Baraka saba walizopewa waaminio waaminifu (kama vile Ufu. 1:3; 14:13; 16:15; 19:9; 20:6; 22:7,14). Hili linaonekana kuwa onyo la kipindi cha matukio ya siku za mwisho yanayopatikana katika Marko 13:33-37; Luka 12:37. Aya hii lazima itakuwa haina maana endapo ile nadharia ya siri ya kuwa na shauku ya kanisa kabla ya wakati huu wa mateso ukithibitishwa. Je! Yesu anazungunza na nani? Tazama Mt. 24:37-42 mtandaoni katika **www.freebiblecommentary.org**.

◙ **"asiende uchi hata watu wakaione aibu yake"** Hili linaweza kuwa dokezo kwa Ufu. 3:18. Katika Agano la kale, uchi ulikuwa ishara ya hukumu (kama vile Ezek. 23:29; Hos. 2:3; Amos 2:16; Mik. 1:8). Hata hivyo, inarejelea sio kupotea kwa wokovu, lakini kwa wakristo watakao fedheheshwa kwa shughuli zao na kupungukiwa na maisha ya imani katika kuja kwa mara ya pili kwa Yesu. Yesu anakuja kama muhukumu na mshindi, ambavyo haswa ni jinsi Wayahudi walivyotarajia Masihi kurudi, imeelezewa katika Ufu. 19:11-16.
Mada Maalumu: Fedheha (Special Topic: Shame)

**16:16 "Wakawakusanya hata mahali"** Hii ilirudiwa katika Ufu.20:8.

**NASB "kwa ki-Ebrania Har-Magedoni"**
**NKJV, NJB "kwa ki-Ebrania Har-Magedoni"**
**NRSV "kwa ki-Ebrania Har-Magedoni"**
**TEV "kwa ki-Ebrania Har-Magedoni**"

Neno hili limeandikwa tofauti katika miswada kadhaa ya Kiyunani.Kumekuwepo na nadharia kadhaa kwa kuelezea jina hili (ambalo halionaekani mahali popote katika Kiebrani aua fasihi ya Kiyunani).

1. Inarejeleakwa "mlima wa Megiddo," mji wa kaskazini katika ugawaji wa kabila la Manase, uliojengwa juu ya mlima.
2. Inarejelea kwa "mji wa Megiddo,"lakini tatizo ni kwamba hizi sio tarajio hasa za mji huo
3. Ni tafsiri ya kifungu "mlima wa kukutania" unaopatikana katika Isa. 14:13, ambao unarejelea kwa mlima wa ndani wa Uungu ambao Shetani hushambulia
4. Inarejelea kwa nchi yote ya ahadi (kama vile "milima ya Israeli" imetanjwa katika Ezek. 38:8,20,21; 39:2,4,17)

5. Inarejelea kwa “mlima wenye matunda” ambao ungeashiria Yerusalemu, mahali pa wakati wa mwisho penye vita hivi vya mwisho katika ya mema na mabaya (kama vile, unabii wa Yoeli)
6. Maana ya msingi ya “megiddo” inaweza kuwa “kukata au kushambulia” kufanya rejeo hili kwa “mlima wa maangamizo” wa Yer. 51:25, ishara ya uharibifu wa Rumi.

Yohana alichagua mji ambao ulijulikana sana na amebadili kidogo maneno yake (tazama Metzger, *Textual Commentary*, uk. 755). Hii inafanana na orodha yake isiyosahii ya makabila kumi na mawili katika Ufu. 7:5-8 ili kuonyesha ishara zake za asili . Fasiri hii ya kiishara imeendelea kuonekana katika matumizi ya kifungu “kwa Kiebrania” ambayo huonyesha uashiriaji, kama katika Ufu. 9:11. Ni kweli kwaba Bonde la Yezreeli au uwanda wa Esdraelon palikuwa mahali pa vita nyingi za Agano la kale (kama vile Amu. 5:19-21; 2 Fal. 9:27; 23:29-30; 2 Nya. 35:22; Zek. 12:11). Njia hii ya uvamizi ya kasikazini ya Mesopotamia nguvu zilikuwa ishara ya utamaduni kwa uovu (kama vile Isa. 14:31; Yer. 1:13-14; 4:6; 10:22; 46:20-24; 47:2-7; 50:3,9,41; 51:48; Ezek. 38:6,15; 39:2).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 16:17-21**
**[17] Na huyo wa saba akakimimina kitasa chake juu ya anga. Sauti kuu ikatoka katika hekalu, katika kile kiti cha enzi, ikisema, Imekwisha kuwa. [18] Pakawa na umeme na sauti na radi; na palikuwa na tetemeko la nchi kubwa, ambalo tangu wanadamu kuwako juu ya nchi hapakuwa namna ile, jinsi lilivyokuwa kubwa tetemeko hilo. [19] Na mji ule mkuu ukagawanyikana mafungu matatu, na miji ya mataifa ikaanguka; na Babeli ule mkuu ukakumbukwa mbele za Mungu, kupewa kikombe cha mvinyo ya ghadhabu ya hasira yake. [20] Kila kisiwa kikakimbia, wala milima haikuonekana tena. [21] Na mvua ya mawe kubwa sana, ya mawe mazito kama talanta, ikashuka kutoka mbinguni juu ya wanadamu. Wanadamu wakamtukana Mungu kwa sababu ya lile pigo la mvua ya mawe; kwa maana pigo lake ni kubwa mno.**

**16:17 "Na huyo wa saba akakimimina kitasa chake juu ya anga"** Hili linaweza kuwa rejeo kwa Ufalme wa Shetani kama unavyopatikana katika Efe. 2:2. Anga juu ya nchi ilichukuliwa kama mamlaka ya uovu ya karne ya kwanza ya ulimwengu. Vita ya kupigana na uovu imekwisha (kama vile Ufu. 16:17c-21).

**16:18** Matumizi haya ya tamathali za semi yametumika mara kadhaa katika Ufunuo (kama vile Ufu. 4:5; 8:5; 11:19; 16:18).

**16:19 "Na mji ule mkuu"** Wengine huona hili kama rejeo kwa Yerusalemu kwa sababu ya Ufu. 11:8. Hata hivyo, Nadhani hata Ufu. 11:8 ni ishara ya Roma (kama vile Ufu.11:8; 16:19; 17:18; 18:10,18-19,21). Roma imeelezewa kama kahaba mkuu wa babeli (kama vile Ufu.14:8) ambayo ilikuwa kiti cha kale cha jamii isiyomjua Mungu.Katika siku za Yohana Roma palikuwa kituo cha madhehebu ya Ufalme ambayo yalitesa Kanisa. Katika Kipindi cha nyakati za mwisho za Mpinga Kristo unaweza kuwa mji mwingine wa ulimwengu. Yohana anaendelea kuelezea uharibifu wa kiti cha mwanadamu aliyeanguka, serikali inayompinga Mungu katika.17-18.

◙ **"ukagawanyikana mafungu matatu"** Yawezekana hili ni dokezo kwa maono ya Ezekieli 5, ambayo huelezea kushindwa kikamilifu.

◙ **"na miji ya mataifa ikaanguka "** Hii huonyesha ushirikiano usioleta ufanisi wa serikali za mwanadamu aliyeanguka dhidi ya Mungu wetu na Kristo wake (kama vile Zaburi 2). Tazama maelezo katika Ufu.10:11.

◙ **"na Babeli ule mkuu ukakumbukwa mbele za Mungu "**Kifungu “kisha Mungu akakumbuka” mara nyingi ni ishara ya hukumu ya Mungu (kama vile Ufu.18:5; 19:15). Kikombe hiki mahususi cha hukumu kilijadiliwa hapo awali katika Ufu.14:10.

◙**"kikombe cha mvinyo ya ghadhabu ya hasira yake "** Ulevi ilikuwa sitiari ya AK kwa hukumu ya Mungu (kama vile Zab. 60:3; 75:8; Isa. 51:17,22; Yer. 25:15-16, 27-28).

"Ghadhabu" ni neno *orgē*. Tazama maelezo kamili katika Ufu.7:14.
Mada Maalumu: Mvinyo na Vileo vikali (Special Topic: Wine and Strong Drinks)

Mada Maalumu: Dhiki (Special Topic: Tribulation)

**16:20 "Kila kisiwa kikakimbia"** Hii ni sawa na muhuri ya sita (kama vile Ufu. 6:14).

◙ **"wala milima haikuonekana tena"** Hivi vilikuwa vifungu vya Agano la kale vya kiishara kwa gharika za matukio ya mwisho ya maafa makubwa ya nyakati za mwisho (kama vile Zab.97:5; Mik. 1:4; Nah. 1:5).

**16:21 "mvua ya mawe kubwa sana"** Mvua ya mawe daima imekuwa ishara ya hukumu ya Mungu (kama vile Yos. 10:11; Isa. 28:2). Yamkini hili ni dokezo lingine kwa mapigo ya Wamisri (kama vile Kut. 9:23-24). Katika Ezek. 38:22 mvua ya mawe inatumika juu ya maadui wa Mungu wa nyakati za mwisho. Uzito wa mvua ya mawe umetofautiana.

◙ **"ya mawe mazito kama talanta"** Hii kiuhalisia ni "uzito wa talanta."Katika mashariki ya kale imetofautiana kutoka talanta 45 hadi 138.Uzitoo kamili haujulikani, lakini uzito huu dhahiri umetiwa chumvi kuonyesha uharibifu na vifo ambavyo vilisababishwa. Mada Maalumu: ANE Uzito na Ujazo (Special Topic: ANE Weights and Volume)

**MASWALI YA MJADALA**

Huu ni mwongozo wa maoni ya usomaji, ukiwa na maana kuwa, unawajibika kwa fasiri binafsi ya Biblia. Kila mmoja wetu yampasa atembee katika nuru tulionayo, na Roho Mtakatifu ndiye kipaumbele katika fasiri yetu.Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa ili kukusaidia kufikiri mambo muhimu yaliyoko katika kipengele cha kitabu hiki. Yanamaanisha kuwa maswali ya kichokonozi, yasio na hakika.

1. Je! "bahari ya kioo" inaashiria nini?
2. Je! Kwa nini Mungu anaonyesha maoni ya Yohana ya hema la mbinguni?
3. Orodesha mfanano kati ya muhuri, baragumu, na mapigo ya Misri?
4. Je! Ni jinsi gani Wafalme wa mashariki katika Ufu. 16 :12 wanahusishwa na Wafalme wa dunia yote katika Ufu. 16:14?
5. Je! Har-Magedoni ni nini na iko wapi? (Ufu. 16:16)
6. Je! "mji mkuu" unarejelea kitu gani? (Ufu. 16:19)

# UFUNUO 17-18

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Kahaba Mkuu na kuvikwa nguo za rangi Mnyama | Mwnamke Mwenye Nyekundu na mnyama Mwekundu | Kuanguka kwa Babeli | Kahaba Maarufu | Kahaba Mkuu |
| 17:1-6a | 17:1-6 | 17:1-6a | 17:1-2 | 17:1-7 |
| | Maana ya mwanamke Na mnyama | | 17:3-6a | |
| 17:6b-14 | | 17:6b-8 | 17:6b-8 | |
| 17:7-18 | | | | Viwakilishi vya Mnyama na kahaba |
| | | | | 17:8 |
| | | 17:9-14 | 17:9-11 | 17:9-11 |
| | | | 17:12-14 | 17:12-14 |
| 17:15-18 | | 17:15-18 | 17:15-17 | 17:15-18 |
| | | | 17:18 | |
| Kuanguka kwa Babeli | Kuanguka kwa Babeli Kuu | Maombolezo juu ya Mji Ulioanguka | Kuanguka kwa Babeli | Malaika Anatangaza juu ya kuanguka kwa Babeli |
| 18:1-3 | 18:1-8 | 18:1-3 | 18:1-3 | 18:1-3 |
| | | | | Watu wa Mungu Wanaitwa ili Waachiliwe |
| 18:4-8 | Ulimwengu unaomboleza Kuanguka kwa Babeli | 18:4-8 | 18:4-8 | 18:4-8 |
| 18:9-10 | 18:9-20 | 18:9-10 | 18:9-10 | 18:9-13 |
| 18:11-20 | | 18:11-20 | 18:11-17a | |
| | | | | 18:14 |
| | | | | 18:15-17a |
| | Hitimisho la kuanguka Kwa Babeli | | 18:20 | |
| 18:21-19:4 | 18:21-24 | 18:21-24 | 18:21-23 | 18:21-24 |
| | | | 18:24-19:4 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "**Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia"(A Guide to Good Bible Reading")**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa,lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

21. Aya ya kwanza
22. Aya ya pili
23. Aya tatu
24. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA UFUNUO 17:1-18:24

A. Sura hizi mbili zinafunua kwa maelezo ya undani kule kuharibiwa kwa Babeli ambaye kuanguka kwake kulitajwa awali katika Ufu. 14:8 na 16:19, pia 18:2,21. Kila moja miongoni mwa haya inatokea katika sehemu yake kiuandishi (12-14), (15-16), na (17-19). Huu unaweza kuwa mfano mwingine wa ufanano na muhutasari.

B. Usuli wa hizi sura mbili kwa uande wa kitabu cha Agano la Kale unanapatikana katika maombolezo ya msiba zilizoandikwa kwa ajili ya kutoa pongezi ya kuanguka kwa miji ya kale ya miungu;

   1. Babeli (kama vile Isaya 13,14,21 na Yer. 50-51)
   2. Tiro ( kama vile Isaya 23 na Ezekieli 26-28)
   3. Ninawi ( kama vile Nahumu)
   4. Yerusalemu yenye uovu (Isa. 1:1-26; Eze. 16:51-52)

C. Hii dhana ya mfumo wa ulimwengu ulioanguka ambao unapingana na Mungu inawasilishwa katika Zaburi 2, Danieli 2; 7; 9:24-27; Mathayo 24: Marko 13; Luka 21; na 1 Yohana 2:15-20.

D. Kitabu cha Ufunuo kinatumia maombolezo ya msiba ya Agano la Kale kueleza kuhsiana na kuanguka kwa Rumi, ulimwengu wa ngome ya mpiga Mungu enzi za Yohana. Hata hivyo, mfumo huu huu wa ulimwengu wenye kijitegemea, wenye majivuno, wa mali, unaompinga Mungu upo mpaka leo katika kila kizazi (kama vile 1 Yohana 2:18). Hatimaye huu pia utajifunua wenyewe kama mtawala wa nyakati za mwisho na ufalme wa ulimwengu (kama vile 2 Wathesalonike 2). Maelezo ya ndani yatakayosaidia kizazi cha mwisho cha wasomaji wa Yohana kutambua nyakati za Mpinga Kristo yanaweza kutokea tena katika siku za mwisho. Tatizo limekuwa ni kwamba kila Kizazi cha waaminio kimejaribu kulazimisha kitabu cha Ufunuo katika nyakati zake!

> Kitabu hiki kina umuhimu na karne ya kwanza, umuhimu na kila karne, na umuhimu na karne ya mwisho. Ni vizuri tusilazimishe maelezo. Hawa walikuwa na maana (wasikiaji wa kwanza); waatakuwa na maana tena (kwa kizazi cha mwisho). Lakini kwa vizazi vingi vya waaminio walio wengi ni vya siri. Ni bora zaidi kuwa na tamaa ya kweli kuu katika sehemu hizi saba za fasihi. Hizi zitakuwa na umuhimu wa milele! Kama maelezo yatakuwa ya uhalisia kabisa katika vizazi vya mwisho vya waaminio wanaopitia dhiki, hawatahitaji mtoa maoni awaambie!

E. William Hendriksen, *More Than Conquerors*, anautetea ufanano wa vipengele vyote saba vya kitabu cha Ufunuo (angalia maelezo C. uk. wa 10). Katika kufanya hivyo anaulezea ufanano wa anguko la maadui wa Waaminio (Shetani; wanyama wawili: na Babeli, mpinga Mungu, mfumo wa ulimwengu wa mpinga Kristo). Ingawa uharibifu wao unashughulikiwa kiutofauti (Shetani, Ufu. 20:7-10: wanyama wawili, Ufu. 19:17-21: na Babeli, Ufu. 18:1-19:4), wapo kwa wakati huohuo, kama vile mihuri, baragumu na vitasa. Kwa njia nyingi huu ni muundo wa tafsiri unaovutia unaopanua usambamba wa dhahiri wa mihuri (Ufu. 4-7), baragumu (Ufu. 8-11) na vitasa (Ufu. 15-16) kwenda Ufu. 17-19 na Ufu. 20-22.

## USOMAJI WA NENO NA VIFUNGU VYA MANENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 17:1-7**

[1]**Akaja mmoja wa wale malaika saba, wenye vile vitasa saba, akanena nami, akisema, Njoo huku,**

**nitakuonyesha hukumu ya yule kahaba mkuu aketiye juu ya maji mengi; [2] ambaye wafalme wa nchi wamezini naye, nao wakaao katika nchi wamelevywa kwa mvinyo ya uasherati wake. [3] Akanichukua katika Roho hata jangwani, nikaona mwanamke, ameketi juu ya mnyama mwekundu sana, mwenye kujaa majina ya makufuru, mwenye vichwa saba na pembe kumi. [4] Na mwanamke yule alikuwa amevikwa nguo ya rangi ya zambarau, na nyekundu, amepambwa kwa dhahabu, na kito cha thamani, na lulu, naye alikuwa na kikombe cha dhahabu mkononi mwake, kilichojawa na machukizo, na machafu ya uasherati wake. [5]Na katika kipaji cha uso wake alikuwa na jina limeandikwa, la siri, BABELI MKUU, MAMA WA MAKAHABA NA MACHUKIZO YA NCHI. [6]Nikamwona yule mwanamke amelewa kwa damu ya watakatifu, na kwa damu ya mashahidi wa Yesu. Nami nilipomwona nikastaajabu ajabu kuu. [7]Na yule malaika akaniambia, Kwani kustaajabu? Nitakuambia siri ya mwanamke huyu, na ya mnyama huyu amchukuaye, mwenye vile vichwa saba na zile pembe kumi.**

**17:1"Mmoja wa wale Malaika saba"** Malaika mwingine anafunuliwa kwa njia ile ile ya ya Ufunuo 21:9. Ule uhusiano wa kimtiririko kati ya Ufunuo 17 na 18 na kumwagwa kwa vitasa saba katika Ufunuo 16

1. Inaweza kuwa kabla ya kumwagwa kwa vitasa
2. Inaweza ikawa maelezo ya ziada ya matokeo ya vitasa
3.

◙"**nitakuonesha hukumu ya Kahaba mkuu"** hali hii ya kiroho inafunuliwa katika Ufunuo 17:5 kama "Babeli kuu, mama wa makahaba," na Ufunuo 18:10 kama "Mji mkuu, Babeli" kulingana na sura zilizotangulia majina haya humaanisha tabia za mfumo wa ulimwengu ulioanguka ndani ya:

1. Babeli ya Danieli
2. Nyakati za kati ya Biblia za kati za Antiochus IV
3. Wakati wa Yohana wa Mfalme wa Rumi alipojidai kuwa mungu
   Katika Sura ya 17 nguvu ya kikahaba na tamaa zinalinganishwa na na nguvu ya kuuza na kununua ya Sura ya 18. Katika Agano la Kale miji mitatu inaitwa kahaba
   1. Tiro (Phoenicia) katika Isaya 23:15-16
   2. Ninawi (Ashuru) katika Nahumu 3:4
   3. Yerusalemu (Yuda isiyokuwa na matunda) katika Isaya 1:21; Ezekieli 16:31, 35:23.

◙**"yeye akaaye juu ya maji mengi"** Maelezo ya Agano la Kale katika Yeremia 51:11-14, inayomaanisha jiji la kale la Babeli, lililokuwa lipo katika Euphrates (kama Ninawi ilipokuwa katika mto Tigris) na ilikuwa na mfumo mpana wa umwagililiaji uliotengenezwa na wanadamu na mifereji ya usafirishaji. Hatahivyo, katika ufahamu wa Ufunuo 17;15, tungo hii inatafsiriwa kama ufalme wa Kimataifa (kama vile Danieli 7:2,3).

**17:2**
**NASB" ambaye wafalme wa nchi walifanya nae vitendo vya uchafu"**
**NKJV, NRSV" ambaye wafalme wa nchi walifanya naye uasherati"**
**TEV" ambaye wafalme wa nchi walifanya naye uchafu wa uasherati"**
**NJB"ambaye wafalme wa nchi walifanya nae ukahaba wenyewe"**

Ukahaba huu una sehemu mbili za msingi;

1. Ushirikiano wa kibiashara (kama vile Tiro, Isaya 23:13-18; na Ninawi, Nahumu 3:4)
2. Ushirikiano wa Kisiasa unaojumuisha kuabudu miungu ya mataifa kimkataba katika sherehe za kutafuta kukubaliwa au kuthibitishwa (kama vile,Yerusalemu pia unaitwa kahaba katika Isaya 1:21 na Yeremia 3)
3. Kumuabudu mfalme wa Rumi kama mungu

◙"**wale waliokaa juu ya nchi walileweshwa kwa mvinyo wa unajisi wake"** Haya ni maelezo ya Yeremia 51:7. Pia inatambulishwa katika Ufunuo 14:8. Maneno "wale wakaao juu ya nchi" ni mada inayojitokesa katika Ufunuo ikimaanisha isiyoweza kurejeshwa, uanadamu ulioanguka mbali na Mungu (kama vile Ufu. 3:10; 6:10; 8:13; 11:10; 13:8, 14; 17:8).

Neno "Kunywa" ni stiari ya Agano la Kale inayomaanisha hukumu (Zab. 75:6-8).

**17:3"Nae akanichukua katika roho"** Maneno haya yanatumika kutambulisha maono ya Yohana (Ufu. 1:10; 4:2; 17:3; 21:10). Msingi wa uelewa wa Watoa maoni wengi wanaweka katika muundo wa Ufunuo wa maono haya. Kumbuka, maandiko ya siku za mwisho yana aina ya uandishi wa muundo uliosukwa sana. Muundo unakuwa msingi wa tafsiri.

◙"**kwenda nyikani"** Hii inaweza kumaanisha

1. stiari ya sehemu salama (Ufu. 12:6,14, ambapo ni dokezi la kile kipindi cha kutangatanga nyikani kwa Israeli)
2. mahali ambapo uovu na mapepo huishi (yaani, Law. 16:8; 17:7)
3. dokezo la jiji la kale la Babeli inayopatikana katika Isa. 21:1-10, ambapo ni stiari ya hukumu

Taswira za Yohana ni simtofahamu. Katika Ufu. 17;1 mwanamke anakaa juu ya maji (Mto Eufrate) na katika Ufu. 17:3 anakaa katika kitambaa cha mnyama nyikani.

◙"**Naliona mwanamke ameketi juu ya kitambaa chekundu cha mnyama**" neno "kitambaa" linaweza kumaanisha

1. muuaji, kama vile Ufu. 17:6-7
2. anasa, kama vile Ufu. 18:12-16
3. shetani kama Joka jekundu, kama vile Ufu. 12:3

Mnyama anafunuliwa kwa maelezo ya kina zaidi katika Ufu.13:1-10. Inamaanisha mpinga Kristo wa siku za mwisho (kama vile Danieli 7:9-14; 9:24-27; 11:36-45; 2 Wathesalonike 2; 1 Yohana 2:18).

◙**"amejaa majina mengi ya kukufuru"** hii ni sawa na Ufu. 13:1, 5-6. Majina haya yanafanana kihistoria na Mfalme wa Rumi kujipa Uungu. Wanajipa majina wao wenyewe ya Uungu kama vile "uungu," "mkombozi," "bwana." Kilele ya lengo la mnyama si nguvu za kisiasa za ulimwengu, ila kuabudiwa kidini (kama vile Dan. 7:8,20; 8:11,25; 9:36,37) kama mwakilishi au udhihirisho wa shetani (yawezekana imewakilishwa katika Isa. 14:13-14 na Ezekieli 28:16-17).

◙ **"akiwa na vichwa kumi na pembe kumi"** kufunuliwa huku ni sawa na kufanana kwa joka jekundu (Ufunuo 12:3) na mnyama wa majini (kama vile Ufu. 13:1). Ufanano huu umekusudiwa kuonesha umoja wa nafsi hizi zimpingazo Mungu. Katika hesabu za viwakilishi(1) Vichwa saba vinafanana na maarifa "kamili" au kilele cha kiongozi wa dunia wa siku za mwisho, wakati (2) pembe kumi zinafanana na nguvu kamili au mamlaka ya kiulimwengu (kama vile 17:7,9,12,16).

**17:4"Mwanamke aliyejifunika katika kitambaa cha zambarau na kitambaa chekundu"** rangi hizi zinaweza kumaanisha ufalme (zambarau) na uchafu (nyekundu) au kwa lugha nyepesi ni ulinganifu wa starehe, mali, na utajiri (kama vile Ufu. 18:12,16).

◙"**aliyepambwa na dhahabu na mawe ya thamani na lulu"** Huu ni uwakilishi wa kidunia na nguvu na nafasi ya kiroho (inatumika na Ezekieli kama ulinganifu wa ki-Edeni kwa kiburi cha mfalme wa Tiro, kama vile Eze. 28:13).

◙**"kikombe cha dhahabu"** Haya ni maelezo ya jiji la Babeli (kama vile Yeremia 51:7)

**17:5 "katika paji la uso wake jina liliandikwa"** Seneca's *Controversies* 1:2 and Juvenal's *Satires* 6:122-123, inarekodi kuwa makahaba wa Kirumi walivaa bangili lenye majina yao au jina la mmiliki wao katika paji zao za uso. Hii inaweza kuwa dhana ya kihistoria nyakati za Yohana au katika mazingira ya Ufunuo: inawezekana ikawa ni rejea ya alama katika paji la uso la wasioamini(kama vile Ufu. 13:16-17; 14:9,11; 15:2; 16:2; 19:20; 20:4) ambayo inaigiliza alama ya Mungu ya wasioamini (Ufu.7:2; 9:4).

**NASB"siri, 'Babeli kuu'"**
**NKJV"siri, Babeli kuu"**
**NRSV"siri: 'Babeli kuu"**

**TEV"maana ya siri: 'Babeli kuu"**
**NJB"jina, jina lililofumbwa: 'Babeli kuu"**

Kuna hali ya kutofautiana kama neno "siri" linatakiwa liwe sehemu ya jina au njia ya kumaanisha asili ya kiwakilishi cha jina (kama vile Ufu. 17:7). Babeli ina asili yake katika ustaarabu wa kwanza, ulioanzishwa na Nimrod (Babeli),iliyomwasi Mungu na kufukuzwa katika Mwanzo 11. Kwa matumizi haya na kutokana na ukweli kuwa Babeli iliwachukua watu wa Mungu (Yuda) kwenda uhamishoni,ilikuwa mbadala wa uovu,nguvu ya kiutawala ya ulimwengu. Katika nyakati za Yohana, nguvu hii ilikuwa ni Rumi (kama vile 1 Pet. 5:13).

**17:6** Mstari huu unazungumzia dhiki kuu na ushujaa wa waaminio (kama vile Ufu. 11:7; 13:7; Dan. 7:21).

◙ **"nilishangaa sana"** Toleo la Biblia la KJV linatafsiri hii kama "kwa mvuto mkuu" lakini toleo ka NKJV linasema "nikashangaa kwa mshangao mkuu." Yohana hakuwa anavutiwa naye, lakini alishangazwa kwa kutisha na matendo yake. Aliruhusiwa kusababisha dhiki na kuua watu wa Mungu (Ufu. 13:5,7,15; 11:7).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 17:8-14**
**[8] Yule mnyama uliyemwona alikuwako, naye hayuko, naye yu tayari kupanda kutoka kuzimu na kwenda kwenye uharibifu. Na hao wakaao juu ya nchi, wasioandikwa majina yao katika kitabu cha uzima tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, watastaajabu wamwonapo yule mnyama, ya kwamba alikuwako, naye hayuko, naye atakuwako. [9] Hapo ndipo penye akili zenye hekima. Vile vichwa saba ni milima saba anayokalia mwanamke huyo. [10] Navyo ni wafalme saba. Watano wamekwisha kuanguka, na mmoja yupo, na mwingine hajaja bado. Naye atakapokuja imempasa kukaa muda mchache. [11] Na yule mnyama aliyekuwako naye hayuko, yeye ndiye wa nane, naye ni mmoja wa wale saba, naye aenenda kwenye uharibifu. [12]Na zile pembe kumi ulizoziona ni wafalme kumi, ambao hawajapokea ufalme bado, lakini wapokea mamlaka kama wafalme muda wa saa moja pamoja na yule mnyama. [13] Hawa wana shauri moja, nao wampa yule mnyama nguvu zao na mamlaka yao. [14]Hawa watafanya vita na Mwana-Kondoo, na Mwana Kondoo atawashinda, kwa maana Yeye ni Bwana wa Mabwana, na Mfalme wa Wafalme, na hao walio pamoja naye ndio walioitwa, na wateule, na waaminifu.**

**17:8"Yule mnyama uliyemuona alikuwako,naye hayuko,naye anakaribia kutoka"** mfuatano huu wa mafunuo umesababisha malumbano makubwa sana baina ya watoa maoni.

1. Wengine wanaiangalia kwa namna ya kihistoria ambayo inamaanisha hasa kule kurudi kwa masimulizi ya kishujaa ya Nero.
2. Wengine kama mwendelezo wa ufalme wa ulimwengu unaofanana na Danieli 2, kupelekea katika mfumo wa ulimwengu wa nyakati za mwisho wa mpinga Mungu.
3. Wengine wanaangalia kuwa inafanana na shughuli za matendo ya mwisho ya mnyama yanayofunuliwa katika Ufunuo 13:3, 12, 14, inayofanana na kuigilizwa kwake au kebehi ya huduma ya Kristo.
4. Inaweza kuwa na uhusiano na dhana ya Waraka wa 1 wa Yohana juu ya roho ya mpinga Kristo katika kila kizazi, ambayo inapelekea mpinga Kristo wa siku za mwisho (kama vile 1 Yohana 2:18,22; 4:3; 2 Yohana 7)

   Pia ni kebehi nyingine kwa jina la YHWH (kama vile Ufu. 1:4, 8)

◙"**kuzimu"** Hili ni neno la Kigiriki linalomaanisha "kina" likiwa na kiambishi awali hasi. Linatajwa kwa mara ya kwanza katika Ufu. 9:1 na 11:7. Ni neno linalowasilisha uovu na ushetani. Angalia maelezo katika Ufu. 9:1

◙"**kitabu cha uzima"** angalia maelezo katika Ufu. 5:1 na 13:8

◙**"tangu kuwekwa kwa misingi ya ulimwengu"** angalia maelezo katika Ufu. 3:5 na 13:8

**17:9**

**NASB, NKJV" Huu ndio ufahamu wenye hekima"**
**NRSV" Hii inaitaji ufahamu wenye hekima"**
**TEV"Hii inaitaji hekima na uelewa"**
**NJB"Hii inaitaji maamuzi na uwezo mzuri wa kuamua"**

Neno hili linafanana na lile la 13;18, linalojishughulisha na idadi ya majina ya mnyama. Fumbo hili na maandiko limefanya kila mmoja kuainisha dhana yake! Hata hivyo, ukweli ni kwamba kuwapo kwa tafsiri nyingi sana kunaonesha kuwa wengi wetu hatuna hekima! (kama vile 1 Kor. 1:26-31). Kwangu mimi, ni namna nyingine ya Yohana kueleza siri, viwakilishi na aina ya uandishi wake wenye asili ya mafumbo (kama vile Frank Stagg, *New Testament Theology*, uk. 317).

◙**"Vile vichwa saba ni milima saba anayokalia mwanamke huyo."** Hii ni dhana ya Rumi. Rumi kama ilivyo Yerusalemu, ilijengwa juu ya vilima saba. Neno hili linatokea katika maandishi mengi ya kale yakifunua jiji la Rumi. Kwa hiyo, kwasasa watafsiri angalau wanatakiwa waliangalie hili katika ufahamu wa Ufalme wa Rumi, ingawa kwa ukweli dhana hii yote ya sura ya 17 na 18 iko na mfumo wa kiulimwengu unaompinga Mungu ambao unachukua nafasi yake katika siku za mwisho na ukweli wake upo katika kila kizazi.

**17:10-11** watoa maoni wengine wanaona hili kama mwendelezo wa Wafalme wa Rumi: : Augustus, Tiberius, Caligula, Claudius, na Nero kama "watano walioanguka." Vespasian ni yule "ambaye yupo kwa sasa" na Titus ni yule "ambaye atakuja kwa muda mchache" (kama vile F. F. Bruce, *Answers to Questions*, uk. 141). Tafsiri hii ni kama haina mashiko;Wafalme wengineo wadogo (Galba, Otho, na Vitellius) waliogombea kiti miaka ya 68-69 B.K. wameondolewa. Hata hivyo, licha ya matatizo yake, hiii inaonekana kuwa shabaha ya Ufunuo 17:10 na 11, ikitilia mkazo kurejea kwa hadithi ya Nero na kurudi kwa wapanda farasi wa Parthia kuvamia Rumi (hii inaweza kuelezea Ufu. 17:16, kama vile The Sibyllian Oracles, 5:361-368).

Wengine wanauangalia unabii huu kama unatimilizwa katika dhiki za Wadomitia. Kuna vikwazo vikuu katika tafsiri hii:

1. Ingehitajika Ufunuo uwe umeandikwa wakati wa utawala wa Vespasian, ambayo iko katika mgogoro na desturi za kale za kanisa ambazo Yohana aliandika wakati wa utawala wa Wadomitia.
2. Utumiaji wa viwakilishi vya namba kuanzia mwanzo wa kitabu mpaka mwisho
   Kwanini kufanya halisi kihistoria? Tena, inawezekana ni jambo ambalo Yohana alilifanya kwa makusudi ili kuonesha asili ya viwakilishi vya maono yake, ambayo hayakumaanishwa kufungwa kabisa kabisa katika kipindi chochote cha kihistoria.

Uwezekano mwingine wa tafsiri ni kuwa hii inaweza kumaanisha mfululizo wa falme za Agano la Kale zilizokuwa maadui za watu wa Mungu: Misri, Ashuru, Babeli, Iran, Ugiriki ("tano zimeanguka"), Rumi ("iliyopo"), falme impingayo Mungu nyakati za mwisho ("nyingine haijaja bado"). Utafsiri huu unashabihiana na utaratibu wa jumla wa mfululizo wa falme zinazompinga Mungu kutoka Danieli 2:1-8 (rejea George Ladd, *Revelation*,ukurasa wa 227-231).Bado tafsiri ya kale ni asili ya uwakilishi wa namba zote na maelezo ya Ufunuo ambayo yangegeuza sura hii kuwa mfano mwingine wa kilele cha mgongano kati ya Mungu na muovu (Alan Johnson's *Revelation*, uk. 152-153, 157-161).

Huu ni mfano mzuri wa mgogoro wa ndani kama mtafsiri. Zipo tafsiri nyingi sana za wanataaluma wanaomjua Mungu ninaowaamini. Dhana ya kwanza ni ya mwandishi ninayempendelea zaidi, F. F. Bruce. Wanaofuatia wawili ni watoa maoni wa Ufunuo ninaowapendelea zaidi , George Ladd na Alan Johnson. Wote wanapingana! Suala muhimu hapa ni kama maandiko yanaleta dhana ya karneya kwanza (F. F. Bruce), Agano la Kale (George Ladd), au taswira za siku za mwisho (Alan Johnson). Mpaka hatua hii na kwa kusoma kwangu, mimi nafikiri muono wa Johnson ndio bora zaidi kuliko zote.

**17:12 "Na zile pembe kumi ulizoziona ni wafalme kumi"** Hii ni dhana ya Dan. 7:7,23-24. Daniel 7 maelezo yanayofunua Mpinga Kristo wa nyakati za mwisho. Wengine wanaona kama jambo hili linafanana kihistoria na watawala kumi wa ardhi wa Rumi, wakati wengine wanaona kama wapanda farasi wa kipepo wa Ufunuo 9. Kwa wengi,asili ya uwakilishi ya namba katika kitabu cha Ufunuo inafanya tu Ufu. 17:12 imaanishe viongozi wa ulimwengu wa siku za mwisho, lakini bila kuweka bayana.

Wengi wanaelezea, tafsiri halizi za kitabu cha Ufunuo zimejikita kwenye ubayana wa maelezo ya Ufu. 17:10-12. Nabii hizi ziko bayana sana, ambapo inaweza kumaanisha kutimilizwa kiuhalisia kwa nyakati za mwisho. Hata hivyo, asili ya aina ya uandishi inatuelekeza katika utafsiri wa viwakilishi wa namba hizi na maelezo (angalau kwa sisi ambao sio wa kizazi cha mwisho cha waaminio wanaopitia dhiki)

**17:13** Mstari huu unatuonesha umoja wa uovu, wakati Ufunuo 17:15-16 unatuonesha kutengana kwa uovu, uovu utageuzwa wenyewe kwa wenyewe kama katika Ufu. 16:12

**17:14"Hawa watafanya vita na Mwana-Kondoo"** Mwana kondoo anatambuliwa na watu wake (kama vile Mt. 25:35-40; Matendo 9:4).

◙**"na Mwana Kondoo atawashinda... na hao walio pamoja naye"** angalia kutambuliwa kwa karibu katika ya ushindi wa Kristo na ushindi wa watu wake.

◙**"kwa maana Yeye ni Bwana wa Mabwana, na Mfalme wa Wafalme"** Jina hilihili linatajwa katika Ufunuo 19:16 kama tabia za kurudi kwa Masiha. Asili yake inapatikana katika (1) maelezo yanayomfunua YHWH kutoka Kumbukumbu la Torati 10:17; Zaburi 136:2-3 au (2) jina la Babeli linalotumika kwa Nebukadneza katika Danieli 2:37, 47. Thamani ya namba ya neno hili ni sawa na 777 katika lugha ya Kiaramaiki, ingawa haikutajwa katika andiko.

◙**"ndio walioitwa, na wateule, na waaminifu"** angalia dhana ya mwisho inapatikana katika maneno "wateule" na "walioitwa," lakini angalia wanapewa wito wa kuvumilia kwao kunakounganishwa na "uaminifu." Sisi ni wake kwa wito na imani (vyote kwa mwanzo na kuendelea). Angalia Mada Maalum kuhusu Ustahimiliv katika Ufunuo 2:2

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 17:15-18**

**[15]Kisha akaniambia, Yale maji uliyoyaona, hapo aketipo yule kahaba, ni jamaa na makutano na mataifa na lugha. [16] Na zile pembe kumi ulizoziona, na huyo mnyama, hao watamchukia yule kahaba, nao watamfanya kuwa mkiwa na uchi, watamla nyama yake, watamteketeza kabisa kwa moto. [17]Maana Mungu ametia mioyoni mwao kufanya shauri lake, na kufanya shauri moja, na kumpa yule mnyama ufalme wao hata maneno ya Mungu yatimizwe. [18]Na yule mwanamke uliyemwona, ni mji ule mkubwa, wenye ufalme juu ya wafalme wa nchi.**

**17:15** Mstari huu unaonesha utawala wa kiujumla wa siku za mwisho wa kiongozi ampingae Mungu na ufalme wake. Angalia angalizo katika Ufunuo 10:11

**17:16** Hii ni dhana kwa Ezekieli 16:39-40; 23:25-27; 28:18. Inaonekana ikimaanisha magomvi ya ndani kati ya nguvu za uovu kama katika Ufunuo 16:12. Magomvi haya yalikuwa ni mbinu ya Mungu (kama vile Ufu. 17:17)

**17:17 "mioyo"** angalia Mada Maalumu katika Ufunuo 2:23

**17:18** Jiji hili kubwa linatajwa katika Ufunuo 11:8 na 16:19 ikiwa na dhana aidha ya Yerusalemu (wanaoamini kuwa nyakati hizi zimewekwa na Mungu ili kuongoza matukio ya ulimwengu) au Rumi (wanaoamini kuwa baadhi au unabii wote umekwisha tukia). Mazingira ya kisehemu hiki cha uandishi yanapendekeza kuwa muundo wa nguvu ya mpinga Mungu inawakilishwa kama jiji. Ambapo jiji si jambo kubwa: suala kubwa ni kuwepo kwa mfumo wa kiserikali ambao uko tofauti kabisa na Mungu, wanadamu wanaojaribu kupata mahitaji yao (ubinadamu usioamini katika Mungu).

# UFUNUO 18

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 18:1-3**

**[1]Baada ya hayo naliona malaika mwingine, akishuka kutoka mbinguni, mwenye mamlaka kuu; na nchi ikaangazwa kwa utukufu wake. [2]Akalia kwa sauti kuu, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli ule mkuu; umekuwa maskani ya mashetani, na ngome ya kila roho mchafu, na ngome ya kila ndege mchafu mwenye kuchukiza; [3] kwa kuwa mataifa yote wamekunywa mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake, na wafalme wa nchi wamezini naye, na wafanya biashara wa nchi wamepata mali kwa nguvu za kiburi chake.**

**18:1"naliona malaika mwingine, akishuka kutoka mbinguni, mwenye mamlaka kuu; na nchi ikaangazwa kwa utukufu wake"** Huyu alikuwa malaika wa ajabu mwenye nguvu. Jina "mamlaka" yaani "authority" *(exousia)* haitumiki kwa malaika mwingine katika kitabu. Katika Yohana 5:27, inatumika kama mamlaka ya Mungu yaliyokabidhiwa kwa Yesu. Katika Ufu. 22:16 Yesu anasema alituma malaika kuzungumza na yeye kama muwakilishi wake.

**18:2"Umeanguka, umeanguka Babeli ule mkuu"** Huu ni mfano mmojawapo wa ugumu wa kutafsiri kitabu cha Ufunuo. Sehemu ya taarifa inaletwa ndani katika sehemu ya maono, kwa sehemu imekuzwa nusu, na ikiwa imekuzwa tena katika maono mengine (mf. Kama vile Ufu. 11:8; 14:8; na 16:19-20 au hii inaweza ikawa mfano mwingine wa kurudiarudia kati ya sehemu saba za uandishi) hii ni dhana ya Isaya 21:9 na/au Yeremia 51:8

◙**"umekuwa maskani ya mashetani, na ngome ya kila roho mchafu, na ngome ya kila ndege mchafu mwenye kuchukiza;"** Hii ni dhana ya mabaki ya jiji la kale:

1. Babeli (kama vile Isa. 13:21-22; 14:23; Yer. 50:39; 51:37)
2. Edomu (kama vile Isa. 34:10-15)
3. Nineveh (kama vile Sef. 2:14)

   Katika Agano la Kale wanyama mara nyingi wanasemekana kutembelea katika mabaki ya miji iliyoharibiwa. Hii ni ishara ya vyote uharibifu na uwepo wa roho waovu (rejea NEB). Wengi wa ndege hawa huwakilisha mapepo.

   Maandiko ya Yohana ni yenye kubadilika sana. Mstari huu unafunua jiji ambalo limeachwa na linalokaliwa na mapepo, wakati Ufu. 19:3 inalifunua kama lililochomwa na linalowaka moto.

**18:3 "mataifa yote wamekunywa mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake"** Maneno haya ni dhana ya unabii wa Agano la Kale juu ya uharibifu wa Babeli (kama vile Yer. 51:7). Yeremia kuweka bayana anatumia ulevi (ambayo "kikombe cha dhahabu") kama kiwakilishi cha tamaa na mali.

◙**"ghadhabu"** Hii kiuhalisia ni "hasira" yaani (*thumos*). Angalia maelezo kamili katika Ufu. 7:14

◙**"na wafanya biashara wa nchi wamepata mali kwa nguvu za kiburi chake"** Hii ni dhana ya tatizo kubwa ya kuanguka kwa mwanadamu kunafungamanishwa na ubinafsi na kupenda mali kwa siku za mwisho, mfumo wa ulimwengu umpingao Mungu. Kuna makundi matatu ya binadamu ambao wanaomboleza kuanguka kwa kahaba mkuu:

1. wafanya biashara (kama vile Ufu. 18:3, 11-16)
2. wafalme wa nchi (kama vile Ufu. 18:3,9-10)
3. wafanyabiashara mabaharia ( kama vile Ufu. 18:3,17-19)

   hawa watatu wanawakilisha mifumo ya kiuchumi ya kibinadamu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA: UFUNUO 18:4-8**

**[4]Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, Tokeni kwake, enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake. 5 Kwa maana dhambi zake zimefika hata mbinguni, na Mungu**

**amekumbuka maovu yake. [6]Mlipeni kama yeye alivyolipa, mkamlipe mara mbili kwa kadiri ya matendo yake. Katika kikombe kile alichokichanganyisha, mchanganyishieni maradufu. [7]Kwa kadiri alivyojitukuza na kufanya anasa, mpeni maumivu na huzuni kadiri iyo hiyo. Kwa kuwa husema moyoni mwake, Nimeketi malkia, wala si mjane, wala sitaona huzuni kamwe. [8]Kwa sababu hiyo mapigo yake yatakuja katika siku moja, mauti, na huzuni, na njaa, naye atateketezwa kabisa kwa moto. Kwa maana Bwana Mungu aliyemhukumu ni mwenye nguvu.**

**18:4"Tokeni kwake, enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake"** Hii ni dhana ya Agano la Kale kwa Isaya Isaya 48:20; 52:11; Yeremia 50:8,28; 51:6,9,45 au Zekaria 2:6-7. Kauli hii iko katika KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Inayozungumzia uharaka wa watu wa Mungu kutokamatwa katika mfumo huu wa dunia ulioanguka.

**18:5 "Kwa maana dhambi zake zimefika hata mbinguni"** Hii ni dhana ya Mwanzo 18:20-21 au Yer. 51:9. Uvumilivu wa Mungu ulitumika kama sababu ya kufanya dhambi zaidi badala ya kutubu (kama vile Ufu. 2:21; Rum. 2:4).

◙**"Mungu amekumbuka"** Mara nyingi katika Biblia Mungu hukumbuka matendo ya uovo yanayopelekea katika hukumu ( kama vile Ufu. 16:19; Zab. 79:8; Isaya 64:9; Yer. 14:10; 17:1-4; 44:21-23; Hos. 7:2; 8:13; 9:9; Amo. 8:7).
**18:6 "Mlipeni kama yeye alivyolipa**" Haya ni maelezo ya ukweli kwamba tunavuna tulichopanda (kama vile Gal. 6:7 kwa ajili ya kupata idadi yote angalia www.freebiblecommentary.org). Hii kweli inawasilishwa katika namna nyingi katika Biblia (kama vile Zab. 137:8; Yer. 50:15,29; Mt. 7:2; Ufu. 13:10).

◙**"mkamlipe mara mbili kwa kadiri ya matendo yake"** Hii ni dhana kwa Yeremia 16:18 na 17:18, lakini ukweli unawasilishwa katika mazingira mengi (kama vile Kut. 22:4-9; Zab. 75:7-8; Isa. 40:2). Nahau inazungumzia hukumu kamili na iliyojaa, kama kifungu cha maneno yanayofuata yanavyosema. Mstari huu ungekuwa wa kutia moyo sana kwa Wakristo wanaopitia dhiki.

◙**"Katika kikombe kile alichokichanganyisha, mchanganyishieni maradufu"** kikombe ni ulinganifu wa Agano la Kale wa hukumu ya Mungu (kama vile Zab. 11:6; 60:3; 75:6-8; Isa. 51:17,22; Yer. 25:15-16,27-28).

**18:7"Kwa kuwa husema moyoni mwake, NIMEKETI MALKIA, WALA SI MJANE, wala sitaona huzuni kamwe".** Hii kiubayana inafanana na Sef. 2:15 na Isa. 47:7-8. Ni dhana ya ubinafsi na kiburi, ambavyo vinaweza kuwa vilikuwa vyanzo vya kuanguka kwa shetani (inawezekana inaelezewa katika Isaya 14 na Ezekieli 28), kuanguka kwa mwanadamu (kama vile Mwanzo 3), na mfumo huu wa ulimwengu wa siku za mwisho. Tatizo ni kiburi cha ubinafsi!

Kwa "moyo" angalia Mada Maalum katika Ufu. 2:23

**18:8"Kwa sababu hiyo mapigo yake yatakuja katika siku moja"** Haya ni maelezo ya moja kwa moja kwa Isaya 47:9, dhana ya huzuni kumtawala ndani ya siku moja inarudiwa rudiwa katika Ufunuo 18:17-19, ambapo neno la Ki-Yohana "saa" linatumika. Hii ilikuwa ni kutiwa moyo sana kwa Wakristo wanaopitia dhiki.

◙"**naye atateketezwa kabisa kwa moto"** haya yanaweza kuwa maelezo ya Mambo ya Walawi 21:9. Angalia MADA MAALUMU: MOTO (SPECIAL TOPIC: FIRE ) katika Ufu. 16:8

◙**"Kwa maana Bwana Mungu aliyemhukumu ni mwenye nguvu."** Haya ni maelezo ya Yer. 50:34

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 18:9-10**
**[9]Na hao wafalme wa nchi, waliozini naye na kufanya anasa pamoja naye, watalia na kumwombolezea; wauonapo moshi wa kuungua kwake; [10]wakisimama mbali kwa hofu ya maumivu yake, wakisema, Ole, ole, mji ule ulio mkuu, Babeli, mji ule ulio na nguvu! Kwa kuwa katika saa moja hukumu yako imekuja.**

**18:9-10 "Na hao wafalme wa nchi"** Hawa lazima ni wafalme tofauti na waliotajwa katika Ufu. 17:12, 16 walioshiriki katika uharibifu na kuanguka kwa kahaba mkuu. Wafalme hawa kwa wakati huu walikuwa ni mataifa wafanyabiashara waliojipatia faida kutoka katika biashara na mfumo wa ulimwengu umpingao Mungu. Haya ni maelezo ya mji wenye nguvu kibiashara unaoitwa Tiro na mfalme wao mwenye kiburi katika Eze. 26-28. Sura inayobaki ya 18 inahusu kuharibika kwa nguvu ya kibiashara inayohusishwa na kuanguka kwa mfumo wa ulimwengu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 18: 11-20**

**11 Nao wafanya biashara wa nchi walia na kumwombolezea, kwa sababu hapana mtu anunuaye bidhaa yao**
**tena; 12 bidhaa ya dhahabu, na fedha, na kito chenye thamani, na lulu, na kitani nzuri, na nguo ya rangi ya zambarau, na hariri, na nguo nyekundu; na kila mti wa uudi, na kila chombo cha pembe, na kila chombo cha mti**
**wa thamani nyingi, na cha shaba, na cha chuma, na cha marimari; 13 na mdalasini, na iliki, na uvumba, na marhamu, na ubani, na mvinyo, na mafuta ya mzeituni, na unga mzuri, na ngano, na ng'ombe, na kondoo, na**
**farasi, na magari, na miili na roho za wanadamu. 14 Na matunda yaliyotamaniwa na roho yako yamekuondokea;**
**na vitu vyote vilivyo laini na vitu vya fahari vimekupotea; wala watu hawataviona tena kamwe. 15 Na wafanya**
**biashara ya vitu hivyo, waliopata mali kwake, watasimama mbali, kwa hofu ya maumivu yake; wakilia na**
**kuomboleza, 16 wakisema, Ole, ole, mji ule mkuu! Uliovikwa kitani nzuri, na nguo ya rangi ya zambarau, na nguo**
**nyekundu, na kupambwa kwa dhahabu, na kito cha thamani, na lulu; 17 kwa kuwa katika saa moja utajiri mwingi namna hii umekuwa ukiwa. Na kila nahodha na kila aendaye mahali popote kwa matanga, na**
**mabaharia, nao wote watendao kazi baharini, wakasimama mbali; 18 wakalia sana, walipouona moshi wa**
**kuungua kwake, wakisema, Ni mji upi ulio mfano wa mji huu mkubwa! 19 Wakatupa mavumbi juu ya vichwa vyao, wakalia, wakitokwa na machozi na kuomboleza, wakisema, Ole, ole, mji ule ulio mkuu! Ambao ndani yake wote wenye merikebu baharini walipata mali kwa utajiri wake; kwa kuwa katika saa moja umekuwa**
**ukiwa. 20 Furahini juu yake, enyi mbingu, nanyi watakatifu na mitume na manabii; kwa maana Mungu amehukumu hukumu yenu juu yake.**

**18:11-19"Nao wafanya biashara wa nchi walia na kumwombolezea"** Hii ni sawa na Ezekieli 27:

1. Ufu. 18:11 – Eze. 27:31,36
2. Ufu. 18:12-13 – Eze. 27:12,13,22
3. Ufu. 18:15 – Eze. 27:31,36
4. Ufu. 18:17 – Eze. 27:26-30
5. Ufu. 18:18 – Eze. 27:32
6. Ufu. 18:19 – Eze. 27:30-34

   Hii inafunua biashara ya kimataifa

1. dhahabu kutoka Hispania
2. kitani kutoka Misri
3. hariri kutoka China
4. mbao za citron kutoka Afrika Magharibi
5. pembe za ndovu kutoka Afrika
6. chuma kutoka Hispania au Bahari Nyeusi
7. mdalasini kutoka India
8. zoezi la kiulimwengu la biashara ya watumwa

**18:13**
**NASB, NKJV,**
**NRSV, NJB"magari ya farasi"**
**TEV"usafiri"**
Hii ilimaanisha gari binafsi, lenye matairi manne, la starehe na si magari ya vita

**18:14 "vilivyo laini na vitu vya fahari"** Huu ni kama mchezo wa maneno kwa Wagiriki neno *lipara* (luxury) yaani fahari na *lampra* (splendid) chenye mvuto au ubora wa hali ya juu.

**18:17** Haya ni maelezo kwa Ezekieli 26-28 (jiji la Tiro), ambapo wale walioajiliwa katika starehe hizi waliomboleza kwasababu maisha yao yalikuwa yameathiriwa.

**18:19 "Wakatupa mavumbi juu ya vichwa vyao"** angalia MADA MAALUMU: IBADA ZA HUZUNI (SPECIAL TOPIC: GRIEVING RITES )katika Ufu. 1:7
**18:20 "Furahini juu yake"** Haya ni maelezo kwa Yeremia 51:48, ingawa wengine wanaona kama inamaanisha Kumb. 32:43 (Andiko la Kiyunani la Agano la Kale) yaani maandiko ya kale ya Kigiriki yaliyotafsiri maandiko ya Kiyahudi kama washirika wa kiuchumi wa huzuni juu ya kuanguka kwa Babeli, kwahiyo waamini furahini!

◙**"Mungu amehukumu hukumu yenu juu yake"** Katika kitabu chote, Hukumu za Mungu zimeunganishwa na maombi ya watoto wake (Ufu. 6:10).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 18:21-24**

**[21] Na malaika mmoja mwenye nguvu akainua jiwe, kama jiwe kubwa la kusagia, akalitupa katika bahari, akisema, Kama hivi, kwa nguvu nyingi, utatupwa Babeli, mji ule mkuu, wala hautaonekana tena kabisa. [22] Wala sauti ya wapiga vinanda, na ya wapiga zomari, na ya wapiga filimbi, na ya wapiga baragumu, haitasikiwa ndani yako tena kabisa; wala fundi awaye yote wa kazi yo yote hataonekana ndani yako tena kabisa; wala sauti ya jiwe la kusagia haitasikiwa ndani yako tena kabisa; [23] wala nuru ya taa haitamulika ndani yako tena kabisa; wala sauti ya bwana-arusi na bibi-arusi haitasikiwa ndani yako tena kabisa; maana hao wafanya biashara wako walikuwa wakuu wa nchi, kwa kuwa mataifa yote walidanganywa kwa uchawi wako. [24]Na ndani yake ilionekana damu ya manabii, na ya watakatifu, na ya wale wote waliouawa juu ya nchi.**

**18:21 "Na malaika mmoja mwenye nguvu akainua jiwe, kama jiwe kubwa la kusagia, akalitupa katika bahari"** Haya ni maelezo kwa Yer. 51:63-64. Ni habari yenye nguvu inayoonyesha Babeli kuwa haiwezi kuinuka kamwe tena. Na ukweli ni kwamba, katika Ufu. 18:21-33, kuna UKANUSHI MARA MBILI, "hakika haitakuwa hivyo," "sivyo namna yoyote ile," na "kamwe, hapana, kamwe"

◙**"wala hautaonekana tena kabisa"** Hii inaonesha uharibifu wa kudumu na wa kiujumla (rejea Ezekieli 26:21).
**18:22-23** Hizi zilikuwa ni kelele za maisha ya kila siku katika Mashariki ya Karibu ya Kale. Hukumu ya Mungu inaleta mwisho wa jamii isyomjua Mungu (kama vile Isa. 24:8; Yer. 7:34; 25:10; Eze. 26:13).

**18:23"mataifa yote walidanganywa kwa uchawi wako"** Haya ni maelezo kwa Nahumu 3:4. Angalia kwamba katika Ufu. 18:23-24 zinatajwa sababu tatu za kuanguka kwa mji mkuu.

1. kiburi na mali (kama vile Isa. 23:8)
2. kuabudu miungu mingine na ushirikina (kama vile Law. 19:26,33; Kumb. 18:9-12)
3. kunyanyasa watu wa Mungu (kaama vile Ufu. 16:6, 17:6).

**18:24** Hil ni dokezo la Yer. 51:49

## MASWALI YA MJADALA

Haya ni maoni ya <u>mwongozo</u> kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je! Ufu. 17 na 18 ni kifasihi ni kitu kimoja? Kama ni ndivyo, kwanini?

2. Kwa nini ni vigumu sana kufasiri lini Babeli ilianguka?
3. Je! Babeli, kahaba mkuu, ni nani ukirejea katika siku za Yohana? katika siku zetu? Jekatika siku za mwisho?
4. Je! uovu na mvinyo vinamaanisha nini katika Ufu. 14:8; 17:2; 18:3 katika uwiano na mfumo wa ulimwengu huu?
5. Tafadhali elezea fasiri yako mwenyewe ya Ufu. 17:10-11
6. Ni kutoka katika kitabu kipi cha Agano la Kale ambamo maelezo mengi ya Yohana huchukuliwa?

# UFUNUO 19

| MGAWANYO WA AYA WA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKSV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| (18:21 -19:4) | Mbingu hufurahi juu ya Babeli | Nyimbo za sifa Mbinguni | (18:24-19:4) | Nyimbo za ushindi mbinguni |
| Karamu ya arusi ya Mwana – Kondoo | 19:1-10 | 19:1-4 | Sikukuu ya arusi ya Mwana-Kondoo | 19:1-4 |
| 19:5-8 | | 19:5-8 | 19:5-8 | 19:5-10 |
| 19:9-10 | | 19:9-10 | 19:9<br>19:10a-b<br>19:6c | |
| Mpandaji Farasi Mweupe | Kristo juu ya Farasi Mweupe | Ushindi wa Kristo na majeshi yake ya Mbinguni | Mpandaji farasi Mweupe | Vita ya kwanza ya matukio ya siku za Mwisho |
| 19:11-16 | 19:11-16<br>Mnyama na Majeshi Yake wameshindwa | 19:11-16 | 19:11-16 | 19:11-16 |
| 19:17-21 | 19:17-21 | 19:17-21 | 19:17-18<br>19:19-21 | 19:17-18<br>19:19-21 |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Angalia**"** **Semina ya Ukarimani wa Biblia" (Bible Interpretation Seminar)**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

25. Aya ya kwanza
26. Aya ya pili
27. Aya tatu
28. N.k

**TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA UFUNUO 19:1-21**

A. Mgawanyo wa sura katika sehemu hii ya Ufunuo ulifanywa kwenye sehemu isiyofaa (migawanyo ya sura, Migawanyo ya aya, migawanyo ya mstari, uwekaji wa herufi kubwa, na kuweka vituo vya uandishi sio sehemu ya maandiko ya asili ya Kiyunani yaliyovuviwa). Ufunuo 19:1-10 dhahiri ni maneno ya kuhitimisha kuhusu uharibifu wa kahaba mkuu aliyeelezewa katika Ufu. 17:1-18:24. Kama vile watu walivyofurahia juu ya kuanguka kwa Ashuru na Babeli katika Agano la Kale, sasa malaika watakatifu (kama vile Ufu. 19:4) wanafurahia juu ya kuanguka kwa Babeli, kahaba (yaani, serikali ya kibinadamu mbali na Mungu), kama walivyofanya waaminio katika Ufu. 18:20.
B. Mfululizo wa kusifu wa Ufu. 19:1-10 ni mwitikio kwa 18:20. Sura ya 17-19 zinaunda kitengo cha fasihi kama, sura inavyounda sura ya 20-22.

C. Huu ni uelewa wa jumla kama ilivyokuwa sura ambayo huelezea kuja kwa Kristo mara ya pili (kama vile Ufu. 19:11-16). Lakini inapaswa kuonekana kwamba sura hii hukaribia mzunguko mwingine wa hukumu. Kurudi kwa kristo kulielezewa katika sura hii kwa neno hasa la Kiyahudi, ambalo linaonekana kuwa tofauti kabisa na maelezo ya Paulina wa 1 The. 4:14-18. Wayahudi walitarajia kurudi kwa masihi kwa mtindo ulioelezewa katika Ufu. 19:11-16. Agano jipya huelezea kuja kwa mara ya pili katika njia kadhaa tofauti lakini zinazohusiana. Wakristo walio wengi wanaona wakati wa mwisho katika maneno ya mahubiri ya Yesu kwenye mlima wa Mizeituni (kama vile Mathayo 24; Marko 13; Luka 21) na mjadala wa Paulo katika
   1. Furaha nyingi kupita kiasi, 1 The. 4:13-18
   2. Neno "mtu wa dhambi" (kama vile 2 Wathesalonike 2)

D. Kwa wale wanaopata mateso, Yesu kama shujaa, mtetezi, na mwamuzi alikuwa mfariji wa kutumainiwa.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 19:1-5a**

[1] **Baada ya hayo nikasikia sauti kama sauti ya makutano mengi, sauti kubwa mbinguni, ikisema, Haleluya; wokovu na utukufu na nguvu zina BWANA MUNGU wetu.** [2] **kwa kuwa hukumu zake ni za kweli na za haki; maana amemhukumu yule kahaba mkuu aliyeiharibu nchi kwa uasherati wake, na kuipatiliza damu ya watumwa wake mkononi mwake.** [3] **Wakasema mara ya pili, Haleluya. Na moshi wake hupaa juu hata milele na milele.** [4] **Na wale wazee ishirini na wanne, na wale wenye uhai wanne, wakasujudu na kumwabudu Mungu, aketiye katika kile kiti cha enzi, wakisema, Amina, Haleluya.** [5] **Sauti ikatoka katika kile kiti cha enzi ikisema,**

**19:1 "Baada ya hayo nikasikia sauti kama sauti ya makutano mengi, sauti kubwa mbinguni"** Mstari huu ni dokezo kwa Yer. 51:48. Sura ya 17-18 inavuta umakini kutoka Yeremia 50-51 (Uharibifu wa Babeli) kwa sanamu zao. Kifungu hiki cha maneno au dhana ile ile pia inapatikana katika Ufu.11:15 (Kuja kwa Mara ya Pili kwa Yesu baada ya baragumu ya saba) na 19:6. Kumekuwepo na mjadiliano mengi kuhusu umati huu unaweza kuwa wa kina nani, lakini ni kisio tu kama ni jeshi la malaika waaminifu, mwanadamu aliyekombolewa, au yote mawili.

◙ **"Haleluya"** Neno hili la Kiebrania humaanisha "msifuni YHWH" (BDB 237 II na 219). Hili ni tukio tu la neno hili katika Agano jipya. Linatokea katika mazingira haya mara nne: Ufu. 19:1,3,4, na 6. Historia ya Agano la kale kwa neno hili linapatikana kwenye Zaburi za Kusifu zilizotumika katika kawaida ya ushirika Mtakatifu wa vyote pasaka na sikukuuu ya vibanda (kama vile Zab. 104:35; 105:45; 106:48; 111:1; 112:1; 113:1; 116:19; 117:2; 125:1,21; 146:1,10; 147:1;148:1,14; 149:1,9; 150:1,6).Kifungu cha maneno chenye ufanano kinapatikana katika Ufu. 19:5b.

◙**"wokovu"** Mstari huu unaonyesha shauku la Mungu kwa wanadamu wote (kama vile Ufu. 9:20-21; 14:6-7; 16:9,11; 21:7; 22:17; Ezek. 18:23,30-32; Yohana 3:16; 4:42; 1 Tim. 2:4; 4:10; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 4:14). Inaweza kurejelea kwa dhana ya Agano jipya ya ukombozi wa kimwili, lakini labda inahusu wokovu wa jumla, milele, wa kuhusu ulimwengu mzima kwa watu wanaoamini na uumbaji wote wa kimwili, (kama vile Matendo 3:21; Rum. 8:18-25; Kol. 1:19).

Mada Maalum: Wokovu (neno katika Agano la Kale) (Special Topic: Salavation (OT term))

Mada Maalum: Mpango wa ukombozi wa milelel wa YHWH (Special Topic: YHWH's Eternal Redemptive Plana)

◙ **"utukufu na nguvu"** Kupitia kitabu chote kizima kwaya za mbinguni hulipuka kwa nyimbo za kumsifu Mungu. Mara nyingi nyimbo hizi za kusifu ni muhimu kwa kutafsiri muktadha kwa mara moja.

Mada Maalum: Utukufu (*doxa*, Agano Jipya) (Special Topic: Glory (doxa, NT))

**19:2 "KWA KUWA HUKUMU ZAKE NI ZA KWELI NA ZA HAKI"** Mstari huu unaweza kuwa dokezo kwa Zab. 19:9; 119:138 na 142. Hukumu za Mungu ni halali na haki (inaonekana katika mzunguko wa tatu wa hukumu). Hili lingeweza kuwa lenye kutia moyo sana kwenye kundi la wakristo wanaopitia mateso (kama vile. Ufu. 19:11; 15:3,4; 16:7).

Mada Maalum: Kweli (neno) katika maandiko ya Yohana (Special Topic: True (the term) in John's Writings)

Mada Maalum: Haki (Special Topic: Righteousness)

◙ **"kahaba mkuu"** Kuanguka huku, kwa mfumo wa ulimwengu unaompinga Mungu unatambulika kwa majina kadhaa:

1. Mji mkuu
2. Babeli
3. Kahaba (kama vile Ufu. 14:8; 16:19-21; 17:1-18:24)

Mstari wa 1-4 unaendeleza muktadha kutoka Ufu.17 na 18.

◙ **"aliyeiharibu nchi kwa uasherati wake"** Mstari huu unarejea juu ya kupenda vitu na anasa, ibada ya sanamu, au ibada ya uasherati wa uzazi wa Kipagani, au kuabudu wafalme (kama vile Ufu. 2:14,20,21; 9:21; 14:8; 17:2,4; 18:3).

MADA MAALUM: HARIBU, UHARIBIFU, POTOSHA *(PHTHEIRŌ) (*SPECIAL TOPIC: DESTROY, RUIN, CORRUPT*(PHTHEIRŌ)*

◙ **"KUIPATILIZA DAMU YA WATUMWA WAKE MKONONI MWAKE"** Mstari huu unaweza kuwa dokezo kwa Kumb.32:43 au 2 Fal. 9:7 (kama vile Rum. 12:19). Mungu hutenda kwa niaba ya maombi ya watakatifu wake (kama vile Ufu. 6:9-11; Mt. 7:7-8; 21:22; Yohana 21:22; 14:13-14; 15:7,16; 16:23-24, 26; Yakobo 4:2; 1 Yohana 3:22; 5:14-16). Mfumo wa ulimwengu unaompinga Mungu daima umehisishwa katika mateso na uuwaji wa watu wa Mungu. Mungu huruhusu uovu kufunua malengo yake ya ukweli (kama vile Ufu. 13:5,7,15).

**19:3 "NA MOSHI WAKE HUPAA JUU HATA MILELE NA MILELE"** Mstari huu ni dokezo kwa Isa. 34:10 ambalo huelezea hukumu ya ulimwengu. Tunapaswa kukumbuka kwamba aina hii ya fasihi (matukio ya siku za mwisho) hutumia ishara kuwasilisha ukweli. Ukweli hapa huonekana kuwa mmoja kati ya hatua kuu mbli zinazowezekana:

1. Adhabu ya milele (kama vile Ufu 6:10; Mt. 3:12; 25:41; Luka 3:17; Marko 9:43,48)
2. Uharibifu kamili (kama vile Isa. 34:8-10). Ukweli huu huu unapatikana katika Ufu.14:11

**19:4 "wazee ishirini na wanne"** Angalia maelezo katika Ufu 4:4.

◙ **"Amina"** Neno hili linatumika katika Ufu.1:6,7; 3:14; 5:14 na 7:12; 19:4; 22:20; na 22:21. Ni umbo la neno la Kiebrania la Agano la Kale "imani" (*emeth,* kama vile Hab. 2:4). Asili ya mwanzo wa neno ulikuwa "kuwa imara" au "kuwa na hakika." Lilikuja kutumika katika Agano la Kale kwenye kuaminika kwa Mungu. Hata hivyo, katika Agano Jipya, matumizi yake ni kawaida ya ushirika mtakatifu wa mwanzoni katika maana ya "kukubali" au "kuthibitisha." Angalia MADA MAALUM: AMINA (SPECIAL TOPIC: AMEN)

MADA MAALUM: Kuamini, Amini, Imani, na Imani katika Agano la Kale (SPECIAL TOPIC: Believe, Trust, and Faithfulness in the Old Testament)

**19:5 "Sauti ikatoka katika kile kiti cha enzi ikisema"** Kwa sababu ya kifungu hiki "Mungu wetu" (Ufu. 19:5b), huyu lazima awe malaika, sio Uungu.Yesu kamwe hamwiti Mungu "Mungu wetu" (Michael MaGill, NT Transline, uk. 1011).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO19: 5b-6a**

**[5b]Msifuni Mungu wetu, enyi watumwa wake wote, ninyi mnaomcha, wadogo kwa wakuu. [6a] Nikasikia sauti kama sauti ya makutano mengi,**

◙ **"Msifuni Mungu wetu"** Mstari huu ni dokezo kwa Zab. 115:13; 134:1; 135:1. Neno ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO, lakini ni neno tofauti kuliko "Halleluya,"ambalo linapatikana katika Ufu. 19:1,3,4 na 6. Ni kawaida kitheolojia kwamba malaika angetumia maneno, "Mungu wetu," lakini Ufu.19:10 huonyesha kwamba malaika wanajitambulisha sio pekee pamoja na watakatifu katika huduma, bali pia na watakatifu katika ushuhuda wao kumuhusu Yesu.

◙ **"enyi watumwa wake wote, ninyi mnaomcha, wadogo kwa wakuu"** Mstari huu ni dokezo kwa Zab.115:13 (kutumika hapo awali katika Ufu. 11:18).

**19:6** Hivi vifungu vya kutoa wasifu vilitumika

1. Kwa Mungu katika Ezek. 43:2
2. Kwa Nguvu ya malaika katika Dan. 10:6
3. Kwa Kristo katika Ufu.1:15
4. Kwa jumuiya iliyokobolewa katika Ufu.14:2
5. Kwa muktadha huu hii yaonekana kama kwaya ya kimalaika

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO19:6b-8**

**[6b]na kama sauti ya maji mengi, na kama sauti ya radi yenye nguvu, ikisema, Haleluya; kwa kuwa Bwana Mungu wetu, Mwenyezi, amemiliki. [7] Na tufurahi, tukashangilie, tukampe utukufu wake; kwa kuwa arusi ya Mwana-Kondoo imekuja, na mkewe amejiweka tayari. [8] Naye amepewa kuvikwa kitani nzuri, ing'arayo, safi; kwa maana kitani nzuri hiyo ni matendo ya haki ya watakatifu.**

◙**" kwa kuwa Bwana Mungu wetu, Mwenyezi"** Sifa hii ya mara tatu kwa Mungu kutoka Agano la Kale (YHWH, Elohim, na El Shaddai huonekana katika sura ya tofauti tofauti katika Ufu. 1:8; 4:8; 11:7; 15:3; 16:7,14; 19:15; na 21:22.

KIWAKILISHI NOMINO cha neno "wetu" si cha kawaida sana kwa sababu kimetamkwa na malaika. Hakipatikani kwenye tukio lolote lingine pamoja na sifa hii kwa mara tatu. Hata hivyo ushahidi wa maandishi kwa kushirikishwa ni kwenye nguvu.

1. "Bwana Mugu wetu" katika sahihisho la awali la MS א [2] (UBS4 huweka hili katika maaandiko lakini huipatia daraja "C")
2. "Mungu, Bwana wetu"katika asili ya MS ya א*
3. katika maandiko mengine madogo sana ya baadaye ya Kiyunani, "Mungu wetu" (MSS 051, 209)
4. "Bwana Mungu" (MS A)
5. "Bwana" (toleo la biblia la Ki-Shamu na toleo la biblia la Coptic)

Mada Maalum: Majina ya Miungu, C. na D.(Special Topic: Names for Deity), C. and D

MADA MAALUM: Shaddai (SPECIAL TOPIC: Shaddai)

◙ **"amemiliki"** Kumekuwepo mjadala mkubwa juu ya NJEO HII YA KITENZI CHA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU (kama vile Ufu. 11:17). Baadhi wanaliona kama utawala wa mwanzo wa Mungu (KAULI ANZILISHI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU, kama vile Zab. 93:1; 97:1, NJB). Hata hivyo, Mungu daima alitawala, (KAULI ISIYOBADILIKA AU TATA YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU, kama vile Zab. 99:1). Wengine wanaiona kama kutawala kwa Mungu juu ya dunia sasa kama alivyotawala mbinguni (KAULI YENYE UKOMO AU STAHILI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU, kama vile Mt. 6:10). Mwisho wa nyakati na ukamilisho wa Ufalme wa Mungu

hutokea mara kadhaa katika Ufunuo katika mwisho wa mzunguko tofauti wa Hukumu (muhuri, baragumu, bakuli). Hii hinaonekana kuwa na ufanano na Ufu. 11:15. Linaweza kuwa dokezo kwa Isa. 24:23; 52:7 au Mika 4:7. Angalia [MADA MAALUMU: Kutawala katika ufalme wa Mungu (SPECIAL TOPIC: Reigning in the Kingdom of God)]

**19:7** VITENZI viwili vya kwanza katika Ufu.19:7 ni TEGEMEZI.

1. Na tufurahi – NJEO TENDAJI YA WAKATI ULIOPO
2. Tushangilie – NJEO TENDAJI YA WAKATI ULIOPO

KITENZI cha tatu kina tofauti kadhaa.

1. *dōsōmen* (KAULI TENDAJI TEGEMEZI ISIYOTABIRIKA YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU) – MS P
2. *dōsomen* (WAKATI UJAO), "tutatoa utukufu" – MSS אi[2], A
3. *dōmen* (KAULI TENDAJI TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU) – MS א[*]

Namba 1 na 3 zingetafsiriwa kama VITENZI viwili, "tukampe utukufu." Hesabu 2 ingetafsiriwa "tutampa utukufu"(RSV). UBS[4] huipatia #1 daraja "C"; UBS[3] huipatia daraja "D". Kamati haikuweza kuamua ni ipi ilikuwa ya asili.

[Mada Maalum: Uhakiki wa Tofauti za Kiuandishi (Special Topic: Textual Criticism)]

◙ **"tukampe utukufu wake"** Mstari huu ungeweza kuwa Kifungu cha Kistiari kwa neno kutumaini, kuamini, au kuweka imani katika Kristo. Katika Ufu. 11:13 Ingeweza kumaanisha kwamba baadhi walitubu na kuwa waaminio kama matokeo ya matendo ya Mungu ya hukumu. Kifungu hiki kinatumika kwa watu wa Mungu katika Ufu. 14:7 na kwa wasioamini walioteswa kwa kukataa kwao kumsujudu Mungu katika Ufu.16:9.

[Mada Maalum: Utukufu (*kabod*, Agano la Kale) (Special Topic: Glory (kabod,OT)]

[Mada Maalum: Utukufu (*doxa*, Agano Jipya) (Special Topic: Glory (doxa, NT)]

◙ **"kwa kuwa arusi ya Mwana-Kondoo"** Neno "Mwana – Kondoo" lina kidokezo cha dhabihu ya Agano la Kale (kama vile Law. 1-7). Kifungu hiki cha maneno kinaunganisha kipengele cha dhabihu na ushirika wa meza ya bwana (sadaka ya amani). Kuna dokezo kwa Sikukuu ya arusi hii katika Mt. 8:11; 26:29; Luka 14:15; 22:16. Kinaelekeza kwenye desturi ya ndoa ya Kiyahudi ya kipindi cha kusubiri au kungojea, na sikukuu ya siku saba ya arusi. Inapendeza kunukuu kwamba miongoni mwa Vifungu kadhaa na sitiari hubadilika kwa watu wa Mungu, sio bibi harusi, lakini kama wageni wa harusi (kama vile Ufu. 19:9 na Mt. 22:1-14). Sitiari itabadilika tena katika Ufu. 21:2,9 kwa watu wa Mungu kama "Yerusalemu mpya." Dhana ya uhusiano wa kindoa kati ya Mungu na kanisa lake unapatikana katika Agano la kale kwa Isa. 54:4-8; 62:5; Yer. 31:32; Ezekieli 16; na Hosea 2:14-19. Sitiari inaonekana katika Agano jipya kwa 2 Kor. 11:2; Efe. 5:21-31; Ufu. 19:9; 21:2,9; 22:17. Vile vile, Yesu anafafanuliwa kama bwana harusi (kama vile Mt. 9:15; Marko 2:19-20; Luka 5:34-35; Yohana 3:29). Mifano kadhaa katika Mathayo inaendeleza dhamiara hii (kama vile Mt. 22:1-14; 25:1-13). Ndoa inaweza kuwa mfano bora zaidi wa dhana ya agano la kibiblia.

◙ **"mkewe amejiweka tayari"** Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO USIOTIMILIFU. Baadhi walifasiri hili kama kazi ya binadamu yenye kustahili. NJEO TENDEWA YA WAKATI ULIOPO USIOTIMILIFU ya Ufu.19:8 Huonyesha fasiri hii haiwezi kuwa kweli. Muktadha huu unathibitisha uhusiano wenye kweli kinzani kati ya shughuli ya kwanza ya Mungu (kama vile Yohana 6:44,65) inaonekana kwenye mwaliko wa Ufu. 19:9, ambao ni KAULI TENDEWA ENDELEVU YA WAKATI TIMILIFU, na imani muhimu ya mwanadamu kujibu (kama vile Marko 1:15; Matendo 3:16,19; 20:21). Uhusiano huu wenye kweli kinzani unaweza kuonekana katika Flp. 2:12-13. Unatiwa nguvu na ukweli kwamba katika Ufu. 19:8 Mungu hutoa ruhusa kuvaa, lakini vazi linarejerea kwa matendo mema (matendo ya haki) ya watu wa Mungu (kama vile Ufu 14:13; Efe. 2:10; 1 Tim. 5:25).

Katika *Word Pictures in the New Testament* A. T. Robertson ana maoni mazuri juu ya Ufu. 19:7. " Sitiari tatu za kuonekana kwa wanawake katika ufunuo (Mama katika sura ya 12, na kahaba katika sura ya 13 na 19, na Bibi harusi wa Kristo hapa mwishoni).Wa kwanza na wa tatu wanawakilisha kanisa chini ya vipengele viwili tofauti vya uhai wake, wakati ya pili hujibu kwa mpinzani wake mkuu na adui (Swete)'" (uk. 449).

**19:8"matendo ya haki ya watakatifu"** Neno "matendo ya haki" (*dikaiōma*) lina matumizi kadhaa katika Agano jipya.

1. Inarejelea kwenye matendo ya Mungu ya haki (kama vile Ufu. 15:4)
2. Inarejelea kwenye kitendo cha Yesu kufa kwa niaba ya wanadamu (kama vile Rum. 5:16,18)
3. Inarejelea maisha ya waaminio ya haki (kama vile Ufu. 19:8)
4. Inarejelea amri, sheria, au amri iliyowekwa na mamlaka, kwa kawaida sheria ya Musa (kama vile Luka 1:6; Rum. 1:32; 2:26; 8:4; Ebr. 9:1,10).

Suala kuu la kitheolojia linahusiana na maneno ya kifamilia ya Kiyunani (*dikaioō*, *dikaiōsis*, *dikaios*, *dikaiosune*) ni jinsi gani wanadamu walioanguka wanavyoweza kudai kuwa sahihi, wenye haki, walio halali, waliohesabiwa kuwa wenye haki. Lazima litamkwe kwa kusisitizwa sana kwamba hali hii ya Kiroho haikukamilishwa kwa juhudi ya binadamu (kama vile Rum. 3:21-30; Efe. 2:8-9), bali kwa uchaguzi wa Kiungu (Baba), Kupitia tendo la Kiungu (Mwana), na kuvutwa Kiungu kwa Roho (kama vile Yohana 6:44,65). Mwanadamu anaweza tu kupokea matokeo yaliyokwisha malizika (kama vile Rum. 5; 2 Kor. 5:21).

Lengo la kusimama kwa usahihi ni maisha sahihi, kuishi kama Kristo, (kama vile Rum. 9:29; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 2:10). Kuishi katika haki ni ushahidi wa uhusiano na Mungu (kama vile Ufu. 14:13), sio misingi ya uhusiano huo (kama vile Gal. 3:1-3)!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO19: 9-10**
**9 Naye akaniambia, Andika, Heri walioalikwa karamu ya arusi ya Mwana-Kondoo. Akaniambia, Maneno haya ni maneno ya kweli ya Mungu. 10 Nami nikaanguka mbele ya miguu yake, ili nimsujudie; akaniambia, Angalia, usifanye hivi; mimi ni mjoli wako na wa ndugu zako walio na ushuhuda wa Yesu. Msujudie Mungu. Kwa maana ushuhuda wa Yesu ndio roho ya unabii.**

**19:9 "Heri"** Hii ni Heri ya nne miongoni mwa Heri saba kwa kukombolewa katika Ufunuo (kama vile Ufu. 1:3; 14:13; 16:15; 19:9; 20:6; 22:7,14).

◙ **"walioalikwa karamu"** Hii ni KAULI TENDEWA ENDELEVU YA WAKATI TIMILIFU, ambayo husisitiza wito wa Mungu kwa wokovu (kama vile Ufu. 17:14; Yohana 6:44,65).

◙ **"Maneno haya ni maneno ya kweli ya Mungu"** Kifungu hikicha maneno husisitiza uaminifu wa ujumbe wa malaika (kama vile Ufu. 21:5; 22:6).

Mada Maalum: Kweli (neno) katika maandiko ya Yohana (Special Topic: True (the term) in John's Writings)

**19:10 "Nami nikaanguka mbele ya miguu yake, ili nimsujudie"** Kumekuwepo na mijadala mingi kuhusu jaribio la Yohana kumsujudu malaika (kama vile Ufu. 22:8). Yawezekana Yohana alilihusisha kwa makusudi kama neno la kupinga kusujudu malaika (kama vile Ufu. 22:9; Kol. 2:18). Yohana alikuwa ameshangazwa na kutishwa sana mtu huyu wa kimalaika mwenye nguvu na alidhani kuwa alikuwa ama

1. Mwenye mfano wa Ki-Ungu aliyefanyika kuwa binadamu (kama vile Mwa. 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16; Kut. 32,4; 13:21; 14:19; Amu. 2:1; 6:22-23; 13:3-22; Zek. 3:1-2; Luka 24:5)
2. Au dhihirisho la kimwili kwa Roho (kama vile Ufu. 22:8-9).

Mada Maalum: Kusujudu (Special Topic: Worship)

◙ **"mimi ni mjoli wako na wa ndugu zako walio na ushuhuda wa Yesu"** Yohana alijiita na neno hili hili katika Ufu. 1:1. Malaika hujitambulisha sio tu kama mtumwa wa Mungu (kama vile Kumb. 33:2; Zab. 103:21; Dan. 17:10) laikini pia wanadamu waliokombolewa (kama vile Ebr. 1:14) Malaika huyu pia hujitambulisha pamoja na ushuhuda wa Yesu, ambao kawaida ulisemwa kwa watakatifu badala ya malaika (kama vile Ufu. 12:17).

◙ **"Kwa maana ushuhuda wa Yesu ndio roho ya unabii"** Hiki ni kifungu cha maneno cha juu kisicho cha kawaida na kimefasiriwa kwa upana sana. Kinaweza kurejeleaama kwa

1. Yesu kama lengo la unabii
2. Ukweli kwamba unabii umerudi kama ishara kwamba Yesu ameleta enzi mpya ya roho (kama vile Ufu. 1:2; 6:9; 12:17 na 14:12 kwa matumizi yanayo fanana na kifungu hiki)
3. Yesu ndiye pumzi yenyewe ya unabii (sawa na " lenye pumzi ya Mungu" ya 2 Tim. 3:16)

Muktadha huonyesha kwamba wale waliomwamini Kristo wameongozwa na Roho. Hakuna awezaye kuja kwa Kristo mbaka

1. roho huugua kwa ajili yake (kama vile Yohana 6:44,65)
2. humsaidia kuelewa ujumbe wa injili
3. Humtia moyo kumtumaini Kristo
4. Humbatiza katika Kristo
5. Humuunda Kristo ndani yake (kama vile Yohana 16:8-11)

Huduma ya roho ni kumtukuza Kristo!

Mada Maalum: Yesu Na Roho (Special Topic: Jesus and the Spirit)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO19: 11-16**

**[11] Kisha nikaziona mbingu zimefunuka, na tazama, farasi mweupe, na yeye aliyempanda, aitwaye Mwaminifu na Wa-kweli, naye kwa haki ahukumu na kufanya vita. [12] Na macho yake yalikuwa kama mwali wa moto, na juu ya kichwa chake vilemba vingi; naye ana jina lililoandikwa, asilolijua mtu ila yeye mwenyew[13] Naye amevikwa vazi lililochovywa katika damu, na jina lake aitwa, Neno la Mungu. [14] Na majeshi yaliyo mbinguni wakamfuata, wamepanda farasi weupe na kuvikwa kitani nzuri, nyeupe, safi. [15] Na upanga mkali hutoka kinywani mwake ili awapige mataifa kwa huo. Naye atawachunga kwa fimbo ya chuma, naye anakanyaga shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya hasira ya Mungu Mwenyezi. [16] Naye ana jina limeandikwa katika vazi lake na paja lake, MFALME WA WAFALME, NA Bwana WA MABwana.**

**19:11 "Kisha nikaziona mbingu zimefunuka"** Hii ni KAULI TIMILIFU TENDWA YA MANENO na linaweza kuhusiana na Ezek. 1:1. Mara kadhaa katika Ufunuo, mbingu zimefunguliwa (katika njia za kiasi) kufunua ukweli kwa Yohana katika hatua zinazoendelea (kama vile Ufu. 4:1;11:19; 15:5). Tazama nukuu katika Ufu. 3:7.

◙ **"farasi mweupe"** Bwana harusi katika aya zilizopita anafunuliwa zaidi kama shujaa wa wote walioshinda. Hii huelezea kuja kwa Yesu kama Wayahudi walivyomtarajia mara ya kwanza, Jemedari wa majeshi yenye nguvu. Hii kwa namna Fulani ni tofauti na ufafanuzi wa Paulo wa kuja kwa mara ya pili (the *Parousia*) Kunakopatikana katika 1 The. 4:13-18. Kwa kundi la Wakristo wanaoteswa hii ni sitiari inayotia moyo sana. Watafsiri wanapaswa kukumbuka

1. kwamba huu sio mjadala kamili na mkamilifu wa kuja kwa mara ya pili kwa Kristo
2. Kwamba umevikwa kwa ishara, lugha ya kiyama
3. Kwamba ni kweli ; Mungu wetu, katika Kristo, anakuja tena katika mwili kuwapokea walio wake (kama vile Yohana 14:2-3) na kuhukumu wanadamu wote sawasawa na matendo yao (kama vile Gal. 6:7)

◙ **"na yeye aliyempanda"** Ingawa kuna farasi mweupe katika Ufu.6:2, hii dhahiri ni tofauti.

◙ **"aitwaye Mwaminifu na Wa-kweli"** Neno "Mwaminifu na Wa -kweli" kwa Kiebrania huomyesha uaminifu (kama vile Ufu. 3:14 kama ilivyo Ufu. 1:5; 3:7).

MADA MAALUM: "Ukweli" (dhana) katika maandiko ya Yohana (SPECIAL TOPIC: "Truth" (the concept) in John's Writings

MADA MAALUM: "Kweli" (neno) katika maandiko ya Yohana ( SPECIAL TOPIC: "True" (the term) in John's Writings

◙ **"naye kwa haki ahukumu na kufanya vita"** Mstari huu ni dokezo kwa Isa. 11:3-5 (kama vile Isa. 9:7; 16:5; 32:1; Zab. 96:13), ambacho huelezea enzi mpya ya haki, enzi mpya ya roho.

MADA MAALUM: Haki (SPECIAL TOPIC: Righteousness)

**19:12 "Na macho yake yalikuwa kama mwali wa moto"** Haya ni maelezo ya Yesu kutoka Ufu. 1:14 na 2:18. Una historia ya kimalaika katika Agano jipya kutoka Dan.10:6.

◙ **"na juu ya kichwa chake vilemba vingi"** Hii hurejelea kwa taji la kifalme. Yesu ana taji nyingi kuliko

1. Farasi mweupe na Yeye aliyempanda katika Ufu. 6:2 (inayoashiria vita yenye nguvu)
2. Shetani (joka jekundu la Ufu. 12:3)
3. Mnyama wa Ufu. 13:1

◙ **"naye ana jina lililoandikwa, asilolijua mtu ila yeye mwenyewe"** Mstari huu unaweza kuwa dokezo kwa Ufu. 2:17, lakini kama ndivyo, maana yake bado haijulikani. Baadhi wanaona kama dokezo kwa watu wa kale waliamini kwamba kujua jina la miungu ilikuwa kuwa na nguvu juu yao.Wengine wanaamini kwamba huwasilisha ukweli kwamba hakuna awezaye kujua kikamilifu sifa ya Kristo. Kwakuwa sifa haijulikani, hairejelei kwa sifa ya aina yoyote ya Yesu:

1. "Mwaminifu na Wa-kweli" ya Ufu.19:11
2. "Neno la Mungu" ya Ufu.19:13)
3. "Mfalme wa Wafalme na Bwana wa MaBwana " ya Ufu. 19:16

**19:13 "Naye amevikwa vazi lililochovywa katika damu"** Mstari huu ni dokezo kwa shairi la Hukumu ya YHWH kutoka Isa. 63:3, ambalo pia limedokezwa katika Ufu. 19:15. Neno "lililochovya" (MS A, UBS[4] huipatia daraja B) au"lililonyunyiziwa" (MSS א[*], P kutoka Isa. 63:3) ni katika NJEO YA WAKATI TIMILIFU; watoa maoni hawakubali kama inaweza kurejelea kwa damu ya maadui wake, ambayo inaonekana kuwa lengo la aya na imeakisiwa katika Targum kwenye Mwa. 49:10-11 (hata hivyo, katika Muktadha, vita haijatokea) ukombozi wake mwenyewe,kwa damu ya dhabihu ambayo watakatifu wamefua mavazi yao na kuyafanya meupe (kama vile Ufu. 7:14) yawezekana kuwa ni damu ya mashahidi wake,ambao ni wenye thamani kwake

Katika muktadha chaguo #1 laonekana kuwa bora.

◙ **"na jina lake aitwa, Neno la Mungu"** Hili ni neno *logos*, ambalo launganisha kitabu cha Ufunuo na Mtume Yohana, Kwakuwa yeye ndiye mwandishi pekee wa kibiblia ambaye hutumia hili kama sifa ya Yesu (kama vile Yohana 1:1,14; 1 Yohana 1:1).Injili ni vyote viwili mtu (neno lililohai la Mungu, Yesu) na Ujumbe (Neno la Mungu lililoandikwa, Biblia). Hiki ni kipengele kile kile chenye sura mbili na kinaaksiwa katika matumizi ya Biblia ya neno "imani," ambayo ni vyote viwili tendo binafsi la kumkaribisha Yesu na tendo la kuwa na utambuzi wa kuamini kweli za kimafundisho ("imani," kama vile Yuda 1:3,20).

MADA MAALUM: Historia ya Kieberania na Kiyunani ya *Logos* (SPECIAL TOPIC: Hebrew and Greek Background of *Logos*)

**19:14 "Na majeshi yaliyo** mbinguni**"** Mstari huu ulifasiriwa kwa njia mbili.

1. Kwa sababu ya Ufu.17:14 na maelezo ya watakatifu katika Ufu. 19:8 katika muktadha huu wa karibu sana, Wengi wamechukulia kwamba hii inarejelea kwa watakatifu.
2. Kwa sababu ya historia ya Agano la Kale ya Kumb.33:2; Zab. 68:17; na Zek. 14:5 pamoja na vifungu vya Agabo la Kale vya Mt. 13:41; 16:27; Marko 8:38; 13:27; Luka 9:26; 1 The.3:13; 2 The.1:7, wengi wanaamini kwamba lazima kurejelea kwa malaika.

Utata huo huo upo katika vifungu vingi.

**19:15 "hutoka kinywani mwake"** Mstari huu ni dokezo kwa Isa. 11:4 na Ufu. 1:16 na 2:16. Sitiari ile ile ya kuhukumu imepatikana katika fasihi ya matukio ya siku za mwisho ya Kiyahudi (kama vile IV Esdras 12:6; Zaburi za Suleimani 17:10,45,49; na kitabu cha I Enoki 62:6).

◙ **"Na upanga mkali"** Hii ni sitiari juu ya uweza wa injili au neno lililonenwa na Mungu (kama vile Mwa. 1; Isa. 55:11; Yohana 1:1; 2 The. 7:8), sio maelezo halisi. Mwisho wa maangamizi ya uasi wa majeshi ya binadamu umefafanuliwa katika Ezek. 38-39. Mangamizi haya yanakamilishwa na (1) upanga (kama vile Ezek. 38:21 na Ufu. 19:15,21) au (2) moto kutoka mbinguni, kama vile Ezek. 38:22; 39:6; na Ufu. 20:9. Mlinganisho huu kati ya Ufunuo 19 na Ufunuo 20 (yaani, njia tofauti za kuangamiza maadui wa mataifa), yote ambayo yanaaksi Ezekieli 38-39, huonyesha muhtasari. Kuja kwa Mara ya Pili kwa Kristo katika 19 kumerudiwa katika lugha tofauti kwenye Ufu. 20:1-10. Muhtasari tayari umeonekana kati ya muhuri,baragumu, na bakuli.

◙**"mataifa"** Asili ya Agano la kale la majeshi haya ni mataifa yasiyo mcha Mungu yaliyo orodheshwa katika Ezekieli 38 kutoka mashariki ya karibu ya kale (kama vile. 19:2,5,6,13). Yohana anatumia vita ya wakati wa mwisho katika Ezekieli 38-39 (au yawezekana Zaburi 2) kama chanzo cha matumizi ya tamathali za semi kuhusu vita ya matukio ya siku za mwishoni kati ya wema na mabaya! Yesu anao upanga ulio mkubwa kuliko zote! Angalia maelezo katika Ufu.2:26 and 10:11.

◙ **"Naye atawachunga kwa fimbo ya chuma"** Huu ni ufafanuzi wa pili kati ya fafanuzi tatu kuhusu farasi mweupe na ampandaye. Ufafanuzi huu wa hukumu unaotoka katika Zab. 2:9 na 110:5-6 (kama vile Ufu. 2:27; 12:5).

◙ **" naye anakanyaga shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya hasira ya Mungu Mwenyezi"** ufafanuzi huu wa tatu wa hukumu ni dokezo kwa Isa. 63:2-3; Yer. 51:33; Omb. 1:15; Yoeli 3:13 (kama vile Ufu. 14:19-20). Rangi za zabibu zilizosagwa hukumbusha zamadamu za kale, kifo, na vita!

Kwa "ghadhabu ya Mungu" Angalia maelezo katika Ufu.7:14.

19:16 " Naye ana jina limeandikwa katika vazi lake na paja lake " Kumekuwako na mijadala mingi ya neno "paja lake":

1. Dokezo la Agano la kale kwa Zab. 45:3
2. Hapa ndipo mahali ambapo upanga wake ulikuwa umening'inia
3. Hapa ndipo mahali ambapo vazi lake lilionekana kwa uwazi kwenye mgongo wa farasi
4. Ndio ulikuwa msuli wake wenye nguvu zaidi katika mwili wake na ilikuwa ishara ya nguvu yake

◙ **"MFALME WA WAFALME, NA Bwana WA MABwana"** Je hii inarejelea kwa jina moja au mawili? Ufunuo 17:14 huonyesha kwamba inarejelea kwa jina moja (kama vile 1 Tim. 6:15). Ina uwezekano wa historia mbili za Agano jipya:

1. Ufafanuzi wa YHWH (kama vile Kumb. 10:17 na Enock 9:4)
2. Wababeli na siofa ya Ashuru ya uungu ulioamishwa kwa YHWH (kama vile Dan. 2:37)

Inapendeza kutambua kwamba kifungu hiki kwa Kiaramu hujumuisha 777, kikipingana kwa hesabu ya mnyama, ambayo ni 666. Utimilifu halisi dhidi ya utimilifu usio halisi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO19: 17-18**

**[17] Kisha nikaona malaika mmoja amesimama katika jua; akalia kwa sauti kuu, akiwaambia ndege wote warukao katikati ya mbingu, Njoni mkutane kwa karamu ya Mungu iliyo kuu; [18] mpate kula nyama ya wafalme, na nyama ya majemadari, na nyama ya watu hodari, na nyama ya farasi na ya watu wawapandao, na nyama ya watu wote, waungwana kwa watumwa, wadogo kwa wakubwa.**

**19:17 "ndege wote"** Aya hii yenye kujaza mshutuko ni dokezo kwa vifungu viwili vya Agano la kale ambavyo vinajishughulisha na zinazoshugulika na mandhari ya vita. Manzingira haya ni vita ile ile iliyojadiliwa katika Ufu. 16:12-16, iitwayo Her-Magedoni. Ndege wanaonyanganya wanaelezewa kama waliopelekwa vitani kama katika 1 Sam. 17:46 (kama vile Mt. 24:28; Luka 17:37) na Ezek. 39:17-20, ambayo ni wakati wa mwishowa vita ya Gogu na Magogu.Yohana mara nyingi hutumia tamathali za semi katika njia mpya. Katika sura ya 20 vita ya Gogu na Magogu hujishughulisha pamoja na shetani baada ya miaka elfu moja ya utawala wa Kristo, wakati vita katika sura ya 19 hutokea kabla ya utawala wa Kristo miaka 1000 na hujishughulisha pamoja na mnyama mwitu na nabii wake wa uongo.

◙ **"Njoni mkutane kwa karamu ya Mungu iliyo kuu"** Neno lililotafsiriwa "njoni" ni KIELEZI kilichotumika kama KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA UWINGI YA WAKATI ULIPO USIOTIMILIFU ambalo hufanana na neno la pili "mkutano," ambaloni ni KAULI TENDEWA SHURUTISHI YA UWINGI YA WAKATI ULIOPO USIOTIMILIFU.Hii ni tofauti na arusi ya Mwana –kondoo iliyotajwa katika Ufu. 19:7 na 9. Mwana-Kondoo anawaalika watu waliopotea kuja na kukombolewa na kujiunga na sikukuu ya arusi yake. Lakini malaika anawaalika ndege wa mawindo kuja kwenye sikukuu ya miili iliyokufa (na nafsi zilizokufa) katika vita ile kuu ya wakati wa mwisho (kama vile Yer. 12:9; Ezek. 39:17). Ghadhabu ya Mungu ni kweli na huashiria kama sikukuu, kwenye miili ya maadui wake (kama vile Isa. 34:6; Yer. 12:12; 46:10; Zef. 1:7).

**19:18** Hii inarejea nyuma hadi Ufu.6:15, ambayo pia ni mpangilio wa matukio ya siku za mwisho ambapo aina hiyo hiyo ya jumla kwa mwanadamu pia ilitajwa. Hofu ya kutokuzikwa ulikua mshituko hasa kwa watu wa kale karibu na Mashariki. Kurudi kwa Yesu kwa ushindi hutokea katika mwisho wa mzunguko wa kila hukumu: muhuri, Ufu. 6:12-17; baragumu, Ufu. 11:15-18; na bakuli, Ufu. 19:1-21.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO19: 19-21**

**[19] Kisha nikamwona huyo mnyama, na wafalme wa nchi, na majeshi yao, wamekutana kufanya vita na yeye aketiye juu ya farasi yule, tena na majeshi yake. [20] Yule mnyama akakamatwa, na yule nabii wa uongo pamoja naye, yeye aliyezifanya hizo ishara mbele yake, ambazo kwa hizo aliwadanganya watu wale walioipokea ile chapa ya huyo mnyama, nao walioisujudia sanamu yake; hao wawili wakatupwa wangali hai katika lile ziwa la moto liwakalo kwa kiberiti; [21] na wale waliosalia waliuawa kwa upanga wake yeye aliyeketi juu ya yule farasi, upanga utokao katika kinywa chake. Na ndege wote wakashiba kwa nyama zao.**

**19:19** Vita halisi huanza. Hili ni dokezo kwa Zaburi 2. Je hii inarejea kwenye vita maalumu, halisi ya wakati wa mwisho, au ni ishara ya mapambano kati ya mema na uovu? Namana ya ufunuo humaaniasha ishara: ufanano wa vifungu katika Mathayo 24; Marko 13; Luka 21; na 2 Wathesalonike 2 huwa na maana halisi. Utata huu ndio chanzo cha kutokuafikiana kwa kiwango kikubwa katika fasiri ya Ufunuo kwa watu wa Mungu. Kulazimisha imani hakika ni hali isiyofaa!

**19:20 "nabii wa uongo pamoja naye, yeye aliyezifanya hizo ishara"** Yeye ni mnyama wa pili (kama vile Ufu. 13:11-18; 16:13). Hii inarejea kwa Ufu.13:12-13, ambapo uhusiano wa nabii wa uongo kwa mnyama wa baharini ni kuiga kwa kubeza kwa uhusiano wa Roho Mtakatifu na Kristo.

◙ **" walioipokea ile chapa ya huyo mnyama"** (kama vile Ufu. 13:16-17).

◙ **"hao wawili wakatupwa wangali hai katika lile ziwa la moto"** Kifungu cha maneno "ziwa la moto" ni cha pekee katika kitabu cha Ufunuo, lakini ni kisawe kwa neno *Gehenna* (angalia Mada Maalum: Wafu wako wapi?), (Special Topic: Where are the Dead?), ambalo Yesu mara nyingi alitumia kuonyesha Jehanamu. Dokezo maalumu katika Agano la kale linaweza kuwa kwa Isa. 30:23-33 na Dan. 7:11. Kuna vifungu vingi vy7a maneno vya kinabii vinavyo husianisha hukumu na moto au kuungua. Dhamira ya moto wa Milele imeendelezwa katika matukio ya siku za mwisho ya Kiyahudi (Kama vile Enock 27:1na kuendelea; 54:11 na kuendelea; 56:3 na kuendelea; 90:26; IV Ezra 7:36; Apoc. of Baruch 59:10; 85:13 [orodha imechukuliwa kutoka kwa George E. Ladd, *Revelation*, uk. 258]). Kifungu hiki cha maneno kimetumika kwa Ufunuo katika Ufu. 20:10,14; 21:8. Ni pahali palipoandaliwa kwa ajili ya shetani na malaika wake, lakini wanadamu wanaoasi dhidi ya Mungu pia watajikuta mahali hapa panakuwa sehemu yao ya kukaa ya siku za mwisho.Ni sehemu ya mwisho ya kukaa ya Shetani. Ni matokeo ya asili ya uasi dhidi ya Mungu na ni mfumo wa kudumu wa kuzimu (kama vile Mt. 25:46; Ufu. 9:11; 11:7; 17:8; 20:1,3).

**19:21** Wale waliopokea ile chapa ya mnyama (kama vile Ufu. 13:16; 14:9,11), wale wale waliowatesa waaminio, sasa wanauawa na neno la Kristo (kama mnyama wa baharini atakavyokuwa, kama vile 2 The. 2:8).

## MASWALI YA MJADALA

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa ili kukusaidia kufikiri mambo muhimu yaliyoko katika kipengele cha kitabu hiki. Yanamaanisha kuwa maswali ya kichokonozi, yasio ya hakika.

1. Orodhesha makundi mbali mbali yhaliyomsujudia Mungu katika Ufu. 19:1-8 na sababu ya kusifu kwao.
2. Je Ni wapi dhana ya arusi ya mwana –kondoo inatokea na maana yake ni nini?
3. Je Ufu. 19:10 unadokeza nini kuhusu malaika?
4. Elezea umuhimu wa Ufu. 19:11-16 kama unavyouhusisha na Kristo.
5. Je Ni vita gani innaelezewa katika Ufu. 19:17-21? Kuna vita ngapi zilizo katika siku za mwisho?

# UFUNUO 20

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Miaka Elfu | Shetani akafungwa miaka Elfu | Kufungwa kwa Shetani na utawala wa wafiadini | Miaka Elfu | Utawala wa Miaka Elfu |
| 20:1-3 | 20:1-3 | 20:1-3 | 20:1-3 | 20:1-3 |
| | Watakatifu kutawala pamoja na Yesu Miaka Elfu | | | |
| 20:4-6 | 20:4-6 | 20:4-6 | 20:4-6 | 20:4-6 |
| Kushindwa kwa Shetani | Uasi wa kishetani ulivunjwa | Kuwekwa huru kwa Shetani na vita ya mwisho | Kushindwa kwa Shetani | |
| 20:7-10 | 20:7-10 | 20:7-10 | 20:7-10 | 20:7-10 |
| Hukumu kwenye kiti kile cha enzi, | Hukumu kwenye kiti kile cha enzi | Hukumu ya mwisho | Hukumu ya mwisho | Hukumu ya mwisho |
| 20:11-15 | 20:11-15 | 20:11-15 | 20:11-15 | 20:11-15<br>20:13-15 |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI** (Kutoka” **Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia”(“A Guide to Good Bible Reading”)**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa usomaji wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako binafsi ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika nuru tuliyonayo. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumwachia kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo. Linganisha mgawanyo wa masomo yako na tafsiri tano hapo juu. Kugawanya katika aya hakuna uvuvio, isipokuwa ni ufunguo wa kufuatilia kusudio la asili la mwandishi ambalo ndilo kiini cha ukalimani. Kila aya ina somo moja na ni moja tu.

29. Aya ya kwanza
30. Aya ya pili
31. Aya tatu
32. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA UFUNUO 20:1-15

A. Sura ya 20 lazima ihusiane kitheolojia na Ufu. 19 (kuja kwa mara ya pili kwa Kristo) na Ufu. 21-22 (ufalme wa milele). Swali la kifasiri ni kama kuja kwa mara ya pili kwa Kristo hutanguliwa na miaka elfu ya utwawala wa Kristo, ikiwa hivyo basi baadhi ya sura ya utawala wa Kristo miaka elfu kabla hauepukiki ( hii inapaswa kufasiriwa kama masimulizi ya kihistoria). Lakini Je! Kama Ufu. 20-22 ni kitu kipya cha marudio

ya Ufu .17-19 (kama vile W. Hendriksen, *More Than Conquerors*)? Mabadiliko haya yangeweza kuwa sawa kwa muhtasari kati ya muhuri, baragumu, na bakuli, kisha baadhi ya sura za udhanifu au wanafalsafa wanaokataa kuwepo kwa miaka elfu ya utawala wa Kristo hufaa zaidi.

B. Ufu. 20 hutambulisha dhana kadhaa za kitheolojia ambazo hazikufunuliwa katika sehemu nyingize ya Biblia:
   1. Hatua mbili za ufufuo
   2. Utawala wa Wafiadini wa dunia hii ulio na kikomo
   3. Utawala wa dunia ya kimasihi kwa miaka 1000
   4. Utawala usioweza wa Masihi (mwandamu kuasi tena katika kuchochea maasi ya Shetani baada ya miaka 1,000 ya utawala wa Kristo)
   5. Vita nyingine na wasioamini baada ya hukumu ya kiti cha enzi cheupe

C. Ugumu katika kufasiri umekuwepo kwa sababu ya
   1. Utofautishaji wa kitheolijia wa Ufu.20
   2. Utata uliopo katika maeneo muhimu kadhaa
      a. Kufungwa kwa Shetani, Ufu. 20:2
      b. Idadi  ya makundi katika Ufu. 20:4
      c. Nani anahusishwa katika ufufuo wa kwanza, Ufu. 20:5
      d. Ni nani, na wapi, na jinsi gani, ya utawala huu pamoja na Kristo, Ufu. 20:6e.ni wapi "mataifa" katika Ufu. 20:8 yanatoka
      e. Maana na sehemu ya "mji huo uliopendwa," Ufu. 20:9
      f. Nani anahusishwa katika hukumu ya kiti cha enzi cheupe katika Ufu. 20:11-15 na jinsi gani inahusiana na Mt. 25:31na kuendelea
   3. Kuna ukosefu mkubwa  wa ukubalifu miongoni mwa watoa maoni wa ki-Mungu, wanaoamini, hata wale wa nadharia sawa ya miaka elfu ya utawala wa Kristo. Nadharia moja ya miaka elfu ya utawala wa Kristo haipaswi kuathiri ukweli wa kimwili, kuja kwa Kristo kwa mara ya pili kiuhalisia kama unavyorejelewa mara nyingi katika AJ.
   4. Baadhi ya nukuu za watu ninazo amini
      a. Katika fasiri yake ya, *Revelation*, George E. Ladd anasema "Wainjilisti wa Kiamerika waliweka msisitizo bila sababu juu ya mafundisho haya ya miaka elfu ya utawala wa Kristo. Kitu kimoja kilicho wazi; Yeye (Yesu) hakujishughulisha kufundisha ufalme wa muda wa  kidunia kabla ya amri ya milele katika enzi ijayo."
      b. Katika *Word Pictures in the New Testament*, A. T. Robertson anasema, "Kitabu hiki kizuri sana kiliandikwa kuwafariji watakatifu katika wakati wa jaribu kubwa, sio kutengeneza mgongano miongoni mwao " (kr. 457-458).
      c. Katika  *Worthy is the Lamb*, Ray Summers anasema, "Sura hii huhitaji kukaribiwa na unyenyekevu mkubwa wa roho, utambuzi wa ugumu wake, kuepuka kauli zilizo tolewa bila kuthibitishwa, na heshima kwa fasiri za uaminifu za wengine. Sura hii imekuwa sehemu ya majadilano ya uchungu kwa wakristo kwa karne nyingi "(uk. 202).
      d. Katika fasiri yake juu ya *The Book of Revelation*, *New International Commentary Series*, Robert H. Mounce, anasema, "Kuhukumu kutoka katika kiasi cha  uangalifu uliotolewa na waandishi wengi kwa aya kumi za mwanzo za sura ya 20, mmoja angeweza kuihukumu kuwa sehemu moja iliyo muhimu sana ya kitabu cha ufunuo. Mwelekeo wa wafasiri wengi katika hatua hii ni kuwa watetezi kwa mtazamo fulani wa miaka elfu ya utawala wa Kristo. Pasipo kukataa maaana ya kifungu hiki muhimu, haipaswi  kuinuliwa juu zaidi ya dhamira hiyo ya msingi kama kurudi kwa Kristo, hukumu ya mwisho na kuondolewa kwa madhaifu yote, na utukufu wa hali ya milele.Kusoma kwa makini kifungu cha miaka elfu ya utawala wa Kristo (Ufu. 20:1-10) kutaonyeha kwamba huenda ni kwa ufufuo wa wafiadini tu, na kwamba haionyeshi kiashiria chochote maalumu kuwa  utawala wao pamoja na Kristo utafanyika duniani au kwamba hauepukiki ule ujio wa mara ya pili " (uk. 351).

D. Utawala wa miaka elfu ya Kristo sio ule ule kama
   1. Enzi ya kimasihi, au

    2. Ufalme wa Mungu (zote #1 na #2 ni milele, kama vile. Dan. 7:14,27; Isa. 9:7; Lk1:33; 2 Pet. 1:11; Ufu. 11:15; 22:5)

E. Dhana ya miaka 1,000 ya furaha kamili na Kristo inaweza kuja kutoka kwenye wazo la miaka 6,000 ya historia na kisha pumziko la siku ya sabato ya baraka kutoka Mwanzo 1. Inaonekana hii (kabla ya mika elfu ya utawala wa Kristo) ilikuwa ni baadhi ya sehemu ya maandiko ya awali ya Wakristo (kama vile Waraka wa Barnaba 15 na II Enoki 33).

F. Sura hii inatia msukumo dhahiri kwa ufunuo na ina madhumuni ya Mungu. Hata hivyo, Je! Ni madhumuni gani: (1) kueleza kwa muhtasari matukio ya wakati wa mwisho au (2) kutoa utambuzi wa kiroho katika mapambano ya kiroho ya kila enzi?
Wafasiri wanapaswa kuwa makini kwa kusukuma ajenda zao wenyewe na sio za Yohana. Udadisi, hali ya kuwa zaidi ya mwingine, au uaminifu kwa nafasi ya kitheolojia au mwalimu kusababisha kundi la wafasiri na mitazamo mibaya. Ajenda/ madhumuni ya Yohana inachukuliwa kwa namna ya chaguo lake la uwasilishaji na chaguo lake la Agano la kale, na sio Agano jipya, tamathali za semi! Kuchukulia kikawaida maandiko yenye matukio ya siku ya kiyama kiuhalisa sio ishara ya kupenda mabadiliko, lakini shauku iliyopotoka! Kwa nini wafasiri wa kiasasa wamejaribu kufanya baadhi ya ishara zingine halisi na zingine za kitamathali (hii haina maana kwamba si kweli)! Uwasilishaji wa Yohana wa wakati wa mwisho ni mfumo wa awali wa Agano la kale. Yeye anaonekana kwa makusudi kupuuza mafundisho ya matukio ya siku za mwisho ya Yesu na Paulo. Waandishi wa kibiblia, wote wa Agano la kale na Agano jipya, hawakufunua matukio ya siku za mwisho kwa utaratibu. Hakika waliwakilisha ukweli, lakini si kwa mantiki,kwa wendo, au kwa njia ya utaratibu! Hebu tuhakikishe ukweli wa msingi wa maono na si kuwa wenye kulazimisha kauli kuhusu maelezo.

G. Sura hii imefanywa kwa kubeba uzito wa uwiano wa kitheolojia kwa nafasi yake katika mfumo wote na ujumbe wa kitabu! Huu sio msistizo mkubwa wa mwandishi! Miaka elfu ya utawala wa Kristo ni ujumbe kwa utawala wa milele wa Mungu. Ufunuo pekee ndio umechagua kutaja utawala huu wa maisha ya kimasihi. Umeonekana Katika aina ambayo huwasilisha kweli na njia ya lunga ya kiishara. Binafsi, sio miaka elfu ya utawala wa Kristo ambao umenishangaza (katika nuru ya maandiko ya AK), lakini
    1. hukumu yenye hatua mbili
    2. kuchangamana kwa watakatifu waliofufuliwa na wanadamu wa kawaida pamoja katika mazingira ya kidunia
    3. uwepo wa uasi baada ya utawala wa kimasihi wa muda mrefu mno

    Je! Utawala binafsi wa Kristo utakuwa usioweza kumleta mwanadamu katika haki hata pamoja na kutokuwepo kwa Shetani? Au Je! Hii ni njia ya kiishara kwa kuonyesha wazi urefu na kipindi cha ufisadi wa mwanadamu?

H. Mungu anatusaidia sisi sote katika nuru ya Ufu. 22:18-19! Sote tunaathiriwa na asili yetu ya dhambi, umri wetu, uzoefu wetu, na walimu wetu!

## WAANDISHI WENYE KUWEZA KUKUSAIDI

A. Alan Johnson, "Revelation," *The Expositors Bible Commentary*, juzuu. 12
B. George Ladd, *Revelation of John*
C. Leon Morris, "The Revelation of St. John," *Tyndale New Testament Commentaries*, juzuu. 20
D. Robert Mounce, "The Book of Revelation," *The New International Commentary*
E. Ray Summers, *Worthy Is the Lamb*
F. Craig Blaising na Darrell Bock, *Progressive Dispensationalism*
G. D. Brent Sandy, *Plowshares and Pruning Hooks*

## NENO NA FUNGU LA KUSOMA

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUFUO 20:1-3**

**[1] Kisha nikaona malaika akishuka kutoka mbinguni, mwenye ufunguo wa kuzimu, na mnyororo mkubwa mkononi mwake. [2] Akamshika yule joka, yule nyoka wa zamani, ambaye ni Ibilisi na Shetani, akamfunga**

**miaka elfu; [3] akamtupa katika kuzimu, akamfunga, akatia muhuri juu yake, asipate kuwadanganya mataifa tena, hata ile miaka elfu itimie; na baada ya hayo yapasa afunguliwe muda mchache.**

**20:1 "Kisha nikaona malaika akishuka kutoka mbinguni, mwenye ufunguo wa kuzimu"** Hii inafanana na malaika amabao walikuwa na funguo ya kuzimu katika Ufu. 9:1-2,11. Inavutia kwamba Shetani alifungwa na malaika asiyejulikana.

◙ **"ufunguo wa kuzimu"** Tunapaswa kuona "funguo" mbili katika Ufunuo. Yesu anafunguo za Kifo na kuzimu katika Ufu. 1:18 na malaika asiyejulikana anafunguo ya kuzimu katika Ufu. 9:1. Neno "funguo" ni neno la kistiari kwa "mamlaka juu ya." Neno "kuzimu" ni neno la Kiyunani lenye maana ya "kina" likiwa na viumbe wa ajabu (shimo la kuzimu) na limejadiliwa katika Ufu. 9:1. Inaonekana kuwa kifungo cha roho za pepo wabaya. Hata hivyo, haiwezi kuwa fasiri kamili kwa sababu ya matumizi ya Paulo katika Rum. 10:7 inaweza kuwa yenye maana sawa na "shimoni" kama mahali pa kifungo kwa roho zote za uovu (kama vile Luka 8:31; Yuda 1:6; 2 Pet. 2:4). Katika walimu ya sheria za kiyahudi wa Uyahudi wa karne ya 2nd na 3rd ilikuwa imeeleweka kuwa sehemu siyo ya haki ya kuzimu.

**20:2 "yule joka, yule nyoka wa zamani, ambaye ni Ibilisi na Shetani"** Hizi sifa mara nne za yule muovu, ambazo zilijadiliwa katika Ufu. 12:9, zilisisitizwa kwa kueleza kwa usahihi nani aliyefungwa na nani baadaye atatupwa katika ziwa la moto (kama vile Ufu. 20-10). Hii inaunganisha mwanzo (kama vile Mwanzo.3) na mwisho (Ufunuo 20-22).

Neno "joka" (angalia Mada Maalam: Joka kubwa jekundu (Special Topic: A Great Red Dragon) linaweza kuwa

1. na ufanano na neno "nyoka." Katika Agano la kale neno la Kiebrania *tannin* (angalia Mada Maalum: Nyoka(Special Topic: Serpent) linaweza kurejelea kwa
   a. nyoka wa nchi kavu (kama vile Kut. 7:9,10,12; Kumb. 32:33; na labda Zab. 91:13)
   b. nyoka wa majini(kama vile Mwa. 1:21; Zab. 148:7)
2. mfano wa mnyama mkubwa wa baharini, kiboko (kama vile Ayu 7:12; Zab. 74:13-14; Isa. 27:1), ambao hutumiwa kuelezea moja ya viumbe wa Mungu (kama vile Ayu 41; Zab. 104:24-26), au kama ishara ya uovu (kama Rahabu, kama vile Isa. 51:9)
3. hutumika kwa mfano wa viongozi maadui wa Israeli
   a. Misri (kama vile Zab. 87:4; Rahabu; Ezek. 29:3)
   b. Babeli (kama vile Yer. 51:34)
4. hutumika katika simulizi za Mesopotania kama mnyama mkubwa wa vita (kama vile Utangulizi wa Ufunuo 12 #B na hasa katika Ufu. 12:3)

Toleo la King James hutafsiri maneno yote *tannin* na *tannim* (Mbwa-mwitu au Mbweha, kama vile Ayu 30:29; Zab. 44:19; Isa. 13:22; 34:13; 35:7; 43:20; Yer. 9:11; 10:22; 49:33; 51:37; Ezek. 29:3 na Mik. 1:8) kama "joka," lakini sio maneno yanayohusiana. Mbweha ni wingi wa *tan*.

◙ **"akamfunga miaka elfu"** Watu daima wanahisi kwamba matokeo ya laana ya pamoja kutoka katika chaguo la Adamu na Eva si haki. Inaweza kuwa kwamba hili ondoleo la uovu na majaribu hutoa mazingira sawa ya kitheolojia kama ya Bustani ya Edeni. Sio tu watu wataokolewa na majaribu kutoka kwa Shetani, watafurahia uwepo wa Masihi aliyetukuzwa kwa muda mrefu. Sikitiko ni kwamba mwanadamu tena ataasi dhidi ya utawala wa Mungu katika Kristo (kam avile Ufu. 20:7-9)!

Dhana ya Agano la kale la enzi mbili za Wayahudi zilikuwa njia ya kufafanua migogoro kati ya mema na mabaya (pande mbili zisizoisha). Wayahudi walionyesha mgogoro huu wa ulimwengu mzima kama umeisha tatuliwa katika vita ya wakati wa mwisho (kama vile Zaburi 2). Yohana anatumia tamathali hizi za semi kusaidia wakristo walioteswa kwa siku zake na kila siku. Katika kitabu cha namna ya uashiriaji huo na ufunuo uliotengwa kihivyo na usiorudiwa kama miaka 1000 ya utawala wa Kristo, Je! Kwa nini mtu yeyote angetaka kutafsiri hili kwa uhalisia? Swali liko katika madhanio ya Wafasiri, sio katika fasili ya maandiko.Sio jambo la kuamini Biblia; ni jambo

la ufasiri sahihi, endelevu la maandiko yenye matukio ya siku ya mwisho. Waaminio wanashauku ya habari zaidi kuhusu siku ya mwisho iliyowatia hamasa (1) kurejesha kitabu hiki katika utaratibu wa uwasilishaji wa kuja kwa Kristo kwa mara ya pili na (2) kulazimisha maelezo ili yaweze kuifaa historia yao wenyewe, tamaduni, na ufasiri. Kama hii itachukuliwa kiuhalisia, wakristo pekee ambao waliishi na kufa wakati wa kipindi hiki watatawala pamoja na Kristo (kama vile Ufu. 20:4-5)!

**20:3 "akamtupa katika kuzimu, akamfunga, akatia muhuri juu yake"** Kuna VITENZI vitano vilivyohusishwa juu ya kufungwa kwa Shetani na malaika asiyejulikana:

1. "akamshika"
2. "akamfunga"
3. "akamtupa"
4. "akamfunga"
5. "akatia muhiri"

Zote hizi ni KAULI TENDAJI ELEKEZI ZA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Hii huonyesha kuondolewa kimamilifu kwa ushawishi wa Shetani. Hili linaweza kuwa dokezo kwa Isa. 24:22.

◙ **"kuwadanganya mataifa tena"**Udanganyifu daima umekuwa dhumuni la yule muovu na mawakala wake (kama vile Ufu. 12:9 13:11-14; 16:14; 19:19; 20:8). Kwa sababu alijua kwamba muda wake ni mfupi (kama vile Ufu. 12:12), alijaribu kuwaongoza wengi kadri iwezekanavyo waume na wake nje ya uumbaji pendwa wa Mungu, na kutuingiza katika uasi na kutoamini. Yeye pia hutamani kusujudiwa, kama ilivyoonekana kwenye majaribu ya Yesu katika Mt. 4:9 na 13:4.

Swali la kufaa sana ni, kwa nani neno “mataifa” linarejelewa? Mataifa ya wasioamini hapo awali yaliharibiwa katika Ufu.17:2; 18:3 na 19:18-21.Baadhi walisema kwamba inarejelea kwa mataifa yale yale, lakini ni masazo yao, sio jeshi lao lililoshindwa. Wengine walisema kwamba ni mataifa tofauti ambayo hayakuhusishwa katika kumpinga Mungu, na njama ya kumpinga Kristo. Uashiriaji wa “mataifa” ni mgumu sana (tazama maelezo katika Ufu. 2:26 na10:11) kwa sababu walionekana tena katika Ufu. 22:2, hata baada ya kuharibiwa kwa Shetani na wasioamini wote.

Inawezekana kwamba Ufu.19:11-21 (yaani, Ufu. 17-19) umerudiwa kwa muhtasari katika Ufu.20:1-10 (yaani, Ufu. 20-22). Hii inaweza kutatua swali la uwepo wa “mataifa” baada ya hukumu kamili na ya mwisho ya suta 19. Neno “mataifa” kawaida hurejelea kwa walio waovu na, watu wasiomcha Mungu (tazama maelezo katika Ufu. 2:26 na 10:11 na makala iliyoandikwa na Dave Mathewson, "*A Re-examination of the Millennium* katika Ufu. 20:1-6: *Consummation and Recapitulation*,"JETS, juzuu. 44 #2, June 2001, kr. 237-251). Kutafutwa na Shetani katika Ufu. 20:1-10 inaweza kuwa ya kufanana na Luka 10:17-20 (Shetani akatupwa kutoka mbinguni); Mt. 12:26-29 (Ufalme wa Shetani ulishindwa na Yesu kwa kuyatoa mapepo); Kol. 2:10,15 (kuwavunja nguvu watawala na wenye mamlaka). Ufunuo 20:1-10 ungeweza kurejelewa kwa ushindi wa Kristo katika kuja kwake kwa mara ya kwanza na matokeo kungojea mpaka kabla ya kuja kwake kwa mara ya pili (mtazamo wa wanafalsafa wanaokataa kuwepo kwa miaka elfu ya utawala wa Kristo).

Kama muhtasari huu ni kweli basi unaonyesha jinsi gani Yohana alishawishiwa na vita moja ya wakati wa mwisho kwa kipengele kinachorudiwa katika Ezekieli 38-39 (na pia Zaburi 2). Yohana alichukulia mkabiliano huu wa Agano la kale pamoja na mataifa yasiomcha Mungu katika Asia ndogo na kuyafanya kiulimwengu katika vita ya matukio ya siku za mwisho kati ya watu wa Mungu na watu wanaoshawishiwa na Shetani wasioamini.

◙ **"hata ile miaka elfu itimie; na baada ya hayo yapasa afunguliwe muda mchache"** Kumekuwepo na majadiliano mengi kuhusu kwa nini Shetani “yampasa” (*dei*) afunguliwe muda mchache. Baadhi wanaona kama Mungu anaonyesha haki ya laana yake kwa binadamu waasi; wengine wanaona kama inawezekana ni moja ya nafasi zaidi ya ukombozi kama katika Ufu. 9:20-21; 14:6-7; 16:9,11.

Pia inawezekana kuona kufungwa kwa Shetani kama ishara ya uovu kushindwa akitumia taswira ya Kiyahudi ya matukio ya siku ya mwisho kutoka katika I Enoki 10:4-6,11-13, ambapo Azazeli (pepo wa jangwani katika Law.

16:8,10,26) alifungwa na malaika ili kwamba asiweze kuwaongoza watu kwa kupotoka. Kifungo kilikuwa ni njia ya kumfunga malaika muovu mpaka siku ya hukumu katika Isa. 24:21-22; 2 Pet. 2:4; na Yuda 1:6.

Pia inawezekana kuwa kufunguliwa kwake kunachokonoa mambo ya siku za mwisho, kutokuwepo na malidhiano ya moja kwa moja kati ya Mungu, Masihi, Roho, na wafuasi wao dhidi ua Shetani, mnyama wa baharini, mnyama wa ardhini, na wafuasi wao. Uumbaji utautakasa kwa ajili ya uovu. Historia imekuwa uwanja wa vita, historia itakuwa sehemu ya matukio ya mwisho wa kukabiliana. Kipengele kinachurudiwa katika Agano la kale ni kutoka katika Zaburi 2 na Ezekieli 38-39. Hukumu hii ile ile inaonekana katika Ufu, 19:19-21. Kama hii ni kweli basi Ufu. 17-19 na 20 hufanana na kufunika kipindi kile kile kutoka ujio wa mara ya kwanza wa Kristo kwenye ujio wake wa mara ya pili.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 20:6**

**4 Kisha nikaona viti vya enzi, wakaketi juu yake, nao wakapewa hukumu; nami nikaona roho zao waliokatwa vichwa kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu, na kwa ajili ya neno la Mungu, na hao wasiomsujudia yule mnyama, wala sanamu yake, wala hawakuipokea ile chapa katika vipaji vya nyuso zao, wala katika mikono yao; nao wakawa hai, wakatawala pamoja na Kristo miaka elfu.
5 Hao wafu waliosalia hawakuwa hai, hata itimie ile miaka elfu.
6 Huo ndio ufufuo wa kwanza. Heri, na mtakatifu, ni yeye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza; juu ya hao mauti ya pili haina nguvu; bali watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo, nao watatawala pamoja naye hiyo miaka elfu.**

**20:4 "Kisha nikaona viti vya enzi"** Hili ni dokezo kwa Dan. 7:9. Uwingi wa viti vya enzi umetajwa katika Ufunuo:

1. Kiti cha enzi cha Mungu (kama vile Ufu. 5:1,1,17; 6:16; 7:10,15; 19:4; 21:5)
2. Kiti cha enzi cha Shetani (kama vile Ufu. 2:13)
3. Kiti cha enzi cha mnyama (kama vile Ufu. 13:2; 16:10)

Ni sitiari ya mamlaka na nguvu.

◙ **"wakaketi juu yake"** Hili ni dokezo kwa Dan. 7:22. Swali ni, kwa nani neno "wao" linarejelea? Katika Danieli inaweza kuwa malaika wenyeji au watakatifu.Kumekuwepo na majadiliano mengi miongoni mwa watoa maoni kuhusu jinsi gani makundi mengi yametajwa katika aya hii.

1. wengine wanaona makundi matatu (walioko katika kiti cha enzi, wakristo waliofiadini, na wakristo wengine wasiomsujudia mnyama)
2. wengine wanona makundi mawili.
3. wengine wanaona kundi moja.

Kama ni kundi moja, linarejelea kwa wakristo wafiadini, hata hivyo, hakuna ufanano mwingine wa kiamaandiko juu ya utawala usiokoma wa wafiadini. Biblia imeahidi utawala kwa watakatifu wote (kama vile Ufu. 3:21; 5:10; 22:5; Mt. 19:28; Lk 22:29-30; 2 Tim. 2:12). Angalia Mada Maalum: Kutawala katika ufalme wa Mungu (Special Topic: Reigning in the Kingdom of God) .

Wengine wanayatoa maoni yao ya makundi haya mawili juu ya kifungu kidogo katika sehemu ya waraka ya Ufu.20:4, "waliokataa kumsujudia mnyama mwitu." Wanaona hili kama kundi la pili la Wakristo, waaminio wote waliokufa kifo cha asili lakini waliokataa kumsujudia mnyama. Katika nuru ya kuja kwa Yesu kwa mara ya pili katika Ufu. 19 na hukumu ya kiti cha enzi cheupe katika Ufu. 20:11, hii inaweza kuwa fasiri bora. Kama fasiri hii ni kweli, basi hukumu ya kiti cha enzi cheupe katika mst. 11 na kuendelea inarejelea tu kwa waliopotea na sio ufanano wa moja kwa moja kwa Mt. 25:31 na kuendelea.

**NASB "nao wakpewa hukumu"**
**NKJV "na hukumu imetolewa kwao"**
**NRSV "hao wlipewa mamlaka ya kuhukumu"**
**TEV "walipewa uweza wa kuhukumu"**
**NJB "walipewa mamlaka ya kutoa hukumu"**

Kifungu hiki cha Kiyunani kinaweza kurejelea ama kwa

1. Utawala wao pamoja na Kristo (kama vile Ufu. 2:26-27; 1 Kor. 6:2)
2. Kuipata haki yao (kama vile Ufu. 6:9-11; Dan. 7:22).

◙ **"roho zao waliokatwa vichwa"** Wengine wanafasiri hili kama Roho zisizokuwa na mwili (kama vile Ufu. 6:9). Neno "kukata kichwa" linarejelea kwenye shoka lenye makali pande zote ambalo lilikuwa linatumika kwa adhabu kuu katika Jamuhuri ya Kirumi (kama vile Rum. 13:4 na Josephus, *Antiquities of the Jews*, 14:9:4). Hii inarejelea kwa wakristo wafiadini.

◙ **"na hao wasiomsujudia yule mnyama"** Kifungu hiki kinaweza kurejelea
1. Kama kifungu cha hapo juu kinavyorejelea kwa wafiadini, basi kifungu hiki kinarejelea kwa wengine waliokufa wakati wa kipindi hiki cha muda huu (kama vile Ufu. 13:15).
2. Kama hii ni sura ya kipindi kati ya kuja mara mbili kwa Kristo, basi inarejelea kwa waaminio wote.
3. Kama hiki ni kipindi cha wakati wa mwisho tu, basi ni uzao huo pekee.

◙ **"wala hawakuipokea ile chapa"** Angalia maelezo katika Ufu.13:16-17. Chapa ni ufanano kwa "wasiomsujudia mnyama na sanamu yake."

◙ **"nao wakawa hai"** Neno hili (*zōē*) mara nyingi linarejelea kwenye ufufuo wa kimwili (kama vile Mt. 9:18; Yohana 4:25; Mdo1:3, 9-11; Rum.14:9; Ufu. 1:18; 2:8; 13:14). Wafasiri hawawezi kufasiri tumizi moja la neno katika Ufu.20:4 kama ufufuo wa kiroho na matumizi ya pili katika Ufu. 20:5 kama ufufuo wa kimwili. Je! Wafiadini waliootawala pamoja na Kristo wanamiili ya ufufuo au miili ya asili ambayo inaoza? Kama wanamiili ya ufufuo, Je! vipi kuhusu "mataifa"?

◙ **"wakatawala pamoja na Kristo miaka elfu"** Dhana ya kutawala kwa Yesu imetajwa katika Ufu. 12:5; 19:5 na inaoonekana kutajwa pia katika Zab. 2:8-9; utawala wa watakatifu pamoja na Kristo umetajwa katika Mt. 19:28; Lk 22:28-30; 2 Tim. 2:12; Ufu. 3:21; 5:10; 20:4,6 na 22:5. Je! Utawala ni wa miaka elfu au milele (kama vile Dan. 7:14,18,27 na Ufu. 22:5)? Je! Ni utawala wa kidunia (kama vile Ufu. 5:10) katika mazingira ya Wapalestina au mazingira ya ulimwengu? Tazama jedwali la maoni tofauti ya miaka elfu ya utawala wa Kristo katika mwisho wa fasiri hii.

Kama miaka 1,000 ni ishara ya enzi ya kanisa (kuwa na mwili kwenye ujio wa mara ya pili), basi hii, miaka 1,000 (10x10x10 – mtindo wa sifa ya juu kabisa kwa Waebrania ya hesabu kwa ukamilifu) inarejelea kwa milele. Hata hivyo, mpangilio huu wa matukio ya baadaye hauendani vizuri zaidi katika Ufu. 20:5-6. Huu ni mfano mzuri wa jinsi gani mtazamo wa ufasiri wa mtu hujibu baadhi ya maandiko vizuri, lakini sio yote. Mpango huu wa ufasiri tofati ulianzishwa kwa namna tofauti ya wafasiri walivyosisitiza juu ya maandiko na kupelekea Agano jipya kusomwa lote kupitia maandiko Fulani "muhimu" yaliyochaguliwa. Hapa kuna sintofahamu, utata, na siri. Hebu tusichanganye tatizo na kutochanganyikana na wengine na ung'ang'aniaji wa kauli/imani !
Mada Maalumu: Kutawala katika ufalme wa Mungu (Special Topic: Reigning in the Kingdom of God)

**20:5** Tafsiri za NRSV na TEV zinafanya Ufu.20:5 kuwa kwenye mabano. Yule ambaye amehusishwa katika ufufuo huu wa kwamza atambainisha yule ambaye amehusishwa katika hukumu ya wote katika Ufu. 20:11na kuendelea. Hapa ni chaguo kwa "hao wafu waliosalia."
1. Waliopotea (kama vile Ufu. 20:6; Dan. 12:2)
2. Wakristo kutoka vipindi vya kwanza (kama vile Ufu. 20:6; 2 Tim. 2:12)
3. Wakristo kutoka kipindi hiki, lakini waliokufa vifo vya asili (kama vile Ufu. 20:4c)

◙ **"ufufuo wa kwanza"** Katika Agano jipya lote kumekuwa na msisitizo juu ya ufufuo wa wafu (kama vile Yohana 5:28-29; Luka 14:14; Mdo 24:15; 1 Kor. 15:52; Flp. 3:3; 1 The 4:16; 2 The. 1:7-10). Hata hivyo, hakuna ufanano katika Biblia kwa fufuo mbili tofauti za waamini, isipokuwa pawepo na dokezo juu ya ufufuo mara mbili wa Dan. 12:2 (waliopotea na waliokombolewa), ingawa George Ladd huona Yohana 5:29 na 1 Kor. 15:24-25 kama zenye kufanana. Mfumo wote wa kithealojia, hata wale ambao wanaamini katika uhalisia wa miaka elfu ya utawala wa

Kristo, zina matatizo makuu ya ufasiri pamoja na ufufuo huu uliogawanyika. Ni wakristo waliokuwa na shauku (kama vile 1 The. 4:13-18; Ufu. 4:11 au 11:12) kuhusishwa katika utawala wa miaka elfu wa Kristo; Je! Waaminio wa Agano jipya wanahusishwa katika utawala wa miaka elfu wa Kristo? Je! Hii ni pamoja na wafiadini wa Agano la kale, au ni wale pekee waliofiadini wakati wa dhiki ya wakati wa mwisho?

◙ **"watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo"** Hili ni dokezo kwa Kut. 19:5-6. Istilahi hii, inarejelewa kwa Israeli kama mtumishi wa Mungu wa ufufuo wa mataifa na ukombozi, kama Agano jipya lilivyopanuliwa kuyajumuisha makanisa yote (kama vile 1 Pet. 2:5,9 na Ufu. 1:6; 5:10). Katika waraka kwa kanisa la Philadelphia, dokezo limefanywa kwa watakatifu kuhusianisha na hekalu (kama vile Ufu. 3:12). Sitiari imebadilishwa kutoka watumwa wa Mungu kwa niaba ya ulimwengu huu ili kuonyesha ushirika na Mungu.

**20:6** Aya hii imeongezwa kwa sababu ya tatizo la ufasiri. Je! Kwa nini muamini yoyote atakabiliwa na kifo cha pili, ambayo ni sitiari kwa Jehanamu (kama vile Ufu. 20:6)? Je! Ni makuhani wafiadini pekee kwa Mungu au ni watakatifu wote (kama vile Ufu. 1:6; 5:10; 2 Pet. 2,5,9)? Je! Wafiadini pekee wa karne ya kwanza ndio watatawala au wafiadini wa Agano la kale nao watahusishwa, Je! Wafiadini katika kila enzi watahusishwa au wakristo wote walioobaki katika uaminifu watahusishwa?

Hasa! Mimi, maswali ni mengi sana!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 20:7-10**
**7 Na hiyo miaka elfu itakapokwisha, Shetani atafunguliwa, atoke kifungoni mwake; 8 naye atatoka kuwadanganya mataifa walio katika pembe nne za nchi, Gogu na Magogu, kuwakusanya kwa vita, ambao hesabu yao ni kama mchanga wa bahari. 9 Wakapanda juu ya upana wa nchi, wakaizingira kambi ya watakatifu, na mji huo uliopendwa. Moto ukashuka kutoka mbinguni, ukawala. 10 Na yule Ibilisi, mwenye kuwadanganya, akatupwa katika ziwa la moto na kiberiti, alimo yule mnyama na yule nabii wa uongo. Nao watateswa mchana na usiku hata milele na milele.**

**20:7 "Shetani atafunguliwa, atoke kifungoni mwake"** Ezekieli 36-39 ni historia kwa muktadha huu. Katika Ezekieli watu wa Mungu watapumzika salama katika mazingira ya matukio ya siku za mwisho (Yuda au Yerusalemu au mji wa ahadi), lakini bado wanashambuliwa na mataifa maovu (Gogu na Magogu). Katika sheria za Kiyahudi hawa maadui wawili wamekuja tumika kuelezea maadui wote wa Masihi na watu wa Mungu. Kiasilia, Gogu walikuwa watu kutoka mji wa Magogu, lakini katika sura hii, maneno yamepewa nafsi katika maadui sawa. Yohana daima hufanya kazi yake upya ya vidokezo vya Agano la kale kufaa kwa wasomaji wake wa karne ya kwanza.

Mada Maalum: Shetani (Special Topic: Satan)

**20:8 "naye atatoka kuwadanganya"** Inastajabisha kwamba wanadamu wanaweza kuongozwa katika uasi baada ya miaka 1,000 ya utawala wa Kristo! Je! Mataifa haya yalikuwa ya “wasioamini” au “waaminio wa awali?" Je! Ni uwepo na utawala wa Kristo haukuwa wenye uwezo wa kuathiri mabadiliko ya kudumu katika jamii ya mwanadamu?

◙ **"Gogu na Magogu"** Hili ni dokezo juu ya uasi endelevu kwa mataifa yasioamini. Baada ya Israeli Kurejeshwa kwenye nchi ya ahadi (kma vile Ezekiel 37), ikihusishwa juu ya matendo ya Mungu (kama vile Ezekieli 36), bado itakuwa na matatizo na mataifa ambayo yatamvamia tena ("Gogu katika mji wa Magogu, mwana Mfalme wa Roshi, Mesheki na Tubali," Ezek. 38:2). Hii linahusu majina ya viongozi au majina ya mahali pa majeshi vamizi; Ezek. 38:5-6,13 inalifanya kuwa jeshi la kimataifa. Sura ya 38-39 za Ezekiel zina mazingira ya wakati wa mwisho (kama vile Ezek. 38:8,10,14,16,18; 39:11). Sura hizi zimekuwa chanzo cha mengi kwa vidokezo vya wakati wa mwisho vya Yohana katika Agano la kale. Mambo yatakuwa mabaya zaidi (maumivu ya uzazi wa enzi mpya) kabla hawajawa vizuri zaidi (Yersalemu mpya).

Tazama jinsi Yohana alivyochukua maandiko ya Agano la kale lakini aliyafanya upya katika nuru ya utamaduni wa Wigiriki-Wirumi wa karne ya kwanza. Gogu, Magogu, na Babeli sio maadui kutoka Mesopotania au uturuki, lakini ni kutoka Roma.

◙ **"mataifa walio katika pembe nne za nchi"** Hii dhahiri ni udanganyifu na uasi wa ulimwengu (kama vile Ufu. 7:1). Hesabu "nne" ilikuwa ni yenye maana ya kuwakilisha ulimwengu mzima.

◙ **"kama mchanga wa bahari"** Kifungu hiki kiasilia kilitumika kama mbegu ya Ibrahimu (kama vile Mwa. 15:5; 22:17; 32:12 na Ebr. 11:12). Hii inaweza kuwa mfano mwingine kwa uovu kuiga maneno ambayo yanawaelezea watu wa Mungu. Hata hivyo, kwa sababu ya kifungu cha kwanza cha Ufu. 20:9, Huu unaonekana kuwa ufafanuzi mwingine tu kwa kuonyesha jeshi kubwa sana.

**20:9** Je! Aya hii inarejelea kwenye vita halisi juu ya mawanda ya Megiddo kama wakati wa mwisho jeshi linasonga kuelekea mji wa Yerusalemu ya Palestina? Kumekuwa na vidokezo vingi kwa mpangilio huu wa matukio ya baadaye katika AK (kama vile Zaburi 2; Ezekieli 38-39; Dan. 9:24-27; Zek. 13-14). Hata hivyo, Yerusalemu ni maili nyingi kutoka Megiddo.

Katika Ufunuo "mji" ni kawaida kwa

1. Jamii ya mwanadamu iliyoandiliwa na kufanya kazi kinyume na Mungu. Iliyopewa nafsi kama Babeli
2. Kihistoria inarejelea kwa Roma katika siku ya Yohana (kama vile Ufu. 14:8; 16:19; 17:18; 18:2,10,16,18,19,21)
3. Hata hivyo, mji wa Yerusalemu labda unarejelewa katika Ufu. 11:8 na hapa.

Waandishi wa Aagano jipya kwa ujumla, na hasa Yohana, amechukua tamathali za semi za Aagano la kale na alizifanya kilimwengu kwa kuhusisha na wanadamu wote. Tatizo katika Ufunuo sio Wayahudi dhidi ya Mataifa, lakini ni waaminio dhidi ya wasioamini. Hii basi ni vita ile ile yawakati wa mwisho kama Ufu.6:15-16; 11:18; 16:12,14,16; 19:19 (usambamba).

◙ **"Moto ukashuka kutoka mbinguni, ukawala"** Hili ni dokezo kwa Ezek. 38:22 na 39:6. Mshindi ni Mungu!

Mada Maalumu: Moto (Special Topic: Fire)

**20:10 "Na yule Ibilisi, mwenye kuwadanganya, akatupwa katika ziwa la moto na kiberiti"** Hapa ndipo ambapo mnyama na nabii wa uongo walitupwa katika Ufu. 19:20. Hapa ndipo ambapo kifo na kuzimu vitatupwa katika Ufu. 20:14 na ambapo wote ambao hawakumuamini Kristo watatupwa katika Ufu. 20:15. Ni lenye maana sawa na *Gehenna* (jehanamu) na huwakilisha utengano wa milele kutoka katika ushirika pamoja na Mungu na Kristo wake (kama vile Marko 9:43,48). Mada Maalumu: Ibilisi (Special Topic: Devil)

◙ **"Nao watateswa mchana na usiku hata milele na milele"** Hii inafanana sana kwenye Ufu. 14:10-11 na 19:5. Dhana ya utengano wa kudumu umedokezwa katika Mt. 25:46 ambapo neno lile lile (*aiōnios*), limetumika kumaanisha mbingu, na limetumika kumaanisha jehanamu.

Hukumu nyingi za Yohana zina kusudi la ukombozi: hiyo ni kweli ya Agano la kale na Agano jipya. Jehanamu haina kusudi la ukombozi linalojulikana.Hukamilisha ahadi ya Mungu kwa kurejesha haki na uadilifu. Jehanamu ni kutengwa kwa uovu kutoka kwa uumbaji mzuri wa Mungu. Pa kutisha kama Jehanamu ni kwa ajili ya mwanadamu, hapamstahili Mungu. Kwa kuruhusu uumbaji wake wa juu, mwandamu akawa na uchaguzi (kipengele kimoja cha mfano wa Mungu ndani ya mwanadamu), Mungu alijua kwamba asilimia kubwa ingechagua nafsi na dhambi. Jehanamu iko wazi, kuvuja damu ya uchungu katika moyo wa Mungu ambao kamwe hautaweza kuponywa. Jehanamu ni siri ya majonzi ya kweli kinzani ya upendo wa milele na haki kwa Mungu!
Mada Maalum: Milele (lahaja ya Kiyunani) [Special Topic: Forever (Greek Idiom)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 20:11-15**

**[11] Kisha nikaona kiti cha enzi, kikubwa, cheupe, na yeye aketiye juu yake; ambaye nchi na mbingu zikakimbia uso wake, na mahali pao hapakuonekana. [12] Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi; na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao. [13] Bahari ikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake; na Mauti na Kuzimu zikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake. Wakahukumiwa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake. [14] Mauti na Kuzimu zikatupwa katika lile ziwa la moto. Hii ndiyo mauti ya pili, yaani, hilo ziwa la moto. [15] Na iwapo mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto.**

**20:11 "Kisha nikaona kiti cha enzi, kikubwa, cheupe"** Hili ni dokezo kwa Dan. 7:9. Kiti cha enzi cheupe kinaonekana kuwa na ufanano na katika Mt. 25:31-46, lakini ikiwa hii ni hukumu tu kwa waliopotea, haiwezi kuwa na ufanano na Mathayo 25 Kwa sababu kuna kondoo (waliookolewa) na mbuzi (waliopotea) wanahutubiwa pamoja. Mada Maalum: Hukumu katika Agano Jipya (Special Topic: Judgement in the NT)

◙**"na yeye aketiye juu yake"** Hili ni dokezo kwa Dan. 7:9. Katika Agano Jipya Mungu alimfanya Kristo ili ahukumu (kama vile Yohana 5:22,27; 9:39; Mdo 10:42; 17:31; 2 Kor. 5:10; 2 Tim. 4:1 na 1 Pet. 4:5).Hata hivyo, katika baadhi ya vifungu, Kristo alisema kwamba Yeye hakuja ili kuhukumu (kama vile Yohana 3:17-21; 12:47-48). Kristo hakuja ili kuhukumu, lakini alikuja ili kuokoa, hata hivyo, ukweli kwamba wanadamu kumkataa Yeye ni kuleta hukumu juu yao wenyewe. Hivyo, Je! ni nani aketiye juu ya kiti hiki cha enzi? Hii inawezekana kwa sababu ya Mt. 25:31-46 na hasa Yohana 5:22 na 2 Kor. 5:10, hata hivyo, mara nyingi katika Agano Jipya na hasa katika kitabu cha Ufunuo, Mungu Baba ndiye aliyeketi juu ya kiti cha enzi (kama vile Rum. 14:10; Ufu. 5:1,7,13; 6:16; 7:10,15; 19:4 na21:5).

◙ **"ambaye nchi na mbingu zikakimbia uso wake"** Baadhi wanaona hili kama kuondolewa kwa laana ambayo iliwekwa juu ya uumbaji wa kimwili wakati Adamu na Eva walipoasi na Kuanguka (kama vile Mwa. 3:17-19 na Rum. 8:19-22). Wengine wanaona hili kama sitiari kwa uharibifu kamili wa utaratibu wa sasa wa kimwili kama ilivyoelezewa katika 2 Pet. 3:10,12 (kama vile Mdo 3:21; Rum. 8:21).

Hii ni lugha ya Agano la kale huonyesha:

1. Kuja kwa Mungu kwa ajili ya uumbaji wake, kama vile Zab. 114:3-6; Isa. 13:10; 24:19-20,23; Joel 2:10,30-31; 3:15; Zek. 14:6)
2. Mungu haitaji tena mashahidi wake wawili wa milele, kama vile Hes.35:30; Kum.17:6; 19:15. Yeye hutawala!

Mbingu katika muktadha huu hairejelei juu ya kiti cha enzi cha Mungu, lakini kwa anga juu ya dunia kama katika Mwa. 1:1.

**20:12 "Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi"** Mpangilio halisi wa kundi hili kubwa haujulikani na kawaida umetegemea juu ya dhanio la mtu mmoja, kama ilivyo fasiri nzuri zaidi za maelezo ya maono katika kitabu cha Ufunuo. Kifungu "wakubwa na wadogo" kinaweza kurejelea kwa (1) waaminio (kama vile Zab.115:13;Ufu.11:18;19:5) au (2) wasioamini (kama vile Ufu. 13:16; 19:18). Katika muktadha huu ni ufanano na "kondoo na mbuzi" katika Mt. 25:31-46 au "Wale walio mbinguni, na juu ya dunia, na chini ya dunia " katika Flp. 2:10-11.

◙ **"na vitabu vikafunguliwa"** Hili ni dokezo kwa Dan. 7:10. Kuna vitabu viwili vimetajwa: kitabu cha matendo au kumbukumbu na kitabu cha uzima (kama vile Ufu. 3:5; na 13:8). Kitabu cha uzima kimeelezewa katika Kut.32:32-33; Zab. 69:28; Isa. 4:3; Dan. 12:1; Lk 10:20; Flp. 4:3; Ebr. 12:23; Ufu.3:5; 13:8; 17:8; 20:15; 21:27. Kitabu cha matendo au kumbukumbu kimeelezewa katika Zab.56:8; 139:16; Isa. 65:6; Mal. 3:16 na Ufu. 20:12-13. Hizi ni sitiari kwa kumbukumbu ya Mungu. Mungu atatenda haki kwa Uumbaji wake: wanadamu wanawajibika kwa matendo na sababu zao na ni wenye kuwajibika kwa Mungu (kama vile Gal. 6:7). Kuna hukumu moja tu.
Mada Maalumu: Vitabu viwili vya Mungu (Special topic: The Two Books of God)

◙ **"na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao"** Hukumu inategemea juu ya maisha ya uchaguzi wa mwanadamu (kama vile Mt. 25:31-46). Tunavuna tulichopanda (kama vile Gal. 6:7). Ukweli wa Kitheolojia kwamba wanadamu wote watahukumiwa kwa kadiri ya matendo yao inaweza kuonekana katika Yer. 17:10; Mt. 16:27; 2 Kor. 5:10; Ufu.2:23; 20:13. Kwa orodha kamili ya marejeo tazama maelezo katika Ufu.2:23.

**20:13 "Bahari. . . na Mauti. . . na Kuzimu zikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake"** Hii hairejelei kwa ukweli kwamba wafu watawekwa katika sehemu tatu tofauti: sitiari zenye ufanano zinaonyesha kwamba wafu walisimama mbele za Mungu (kama vile Flp. 2:10-11).

**20:14 "Mauti na Kuzimu zikatupwa katika lile ziwa la moto"** Hizi zilirejelewa mapema katika Ufu. 6:8. Kifo, ni adui mkubwa wa mwanadamu (kama vile Ebr. 2:14-15), kimeshindwa na kuondolewa (kama vile 1 Kor. 15:26,54-55; 2 Tim. 1:10; Ufu. 1:18; 21:4). Mada Maalumu: kuzimu (Special Topic: Hades)

◙ **"mauti ya pili"** Bibli inazungumzia hatua tatu za Kifo:
1. Kifo cha kiroho, kama vile Mwanzo 3; Isa. 59:2; Rum. 5:12-21; 7;10-11; Efe. 2:1,5; Kol. 2:13; Yakobo 1:15
2. Kifo cha kimwili , kama vile Mwanzo 5
3. Kifo cha milele kiitwacho "mauti ya pili" katika Ufu. 2:11; 20:6,14; 21:8, ambacho hurejelea Jehanamu

**20:15 "Na iwapo mtu ye yote"** Sentensi hii ni KAULI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA ambayo husadiki kwamba kutakuwepo na wale ambao hawakuandikwa katika kitabu cha uzima (sitiari kwa wale ambao hawakumuamini Kristo).

◙ **"kitabu cha uzima"** Angalia maelezo katika Ufu.13:8 na 20:12.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa usomaji wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako binafsi ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika nuru tuliyonayo. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumwachia kazi hii mfasiri.

Maswali haya ya kujadili yanatolewa ili kukusaidia kufikiri mambo muhimu yaliyoko katika kipengele cha kitabu hiki. Yanamaanisha kuwa maswali ya kichokonozi, yasio na ukomo.
1. Je! Kwa nini wengi wasiomcha Mungu, watoa maoni wanaoamini Biblia hawakubaliani na fasiri ya sura hii?
2. Kama kitabu hiki kimeandikwa kwa lugha ya ishara (namna ya kiyama), Je! Kwa nini watu wengi wanachukua sura hii kiuhalisia na kihistoria sana?
3. Je! Kwa nini Shetani alifungwa kwa muda mchache? Je ni wapi mataifa yanatoka katika Ufu. 20:3 na 8?
4. Je! Ni makudi mangapi yanahusishwa katika Ufu.20:4 na kwa nini hii ni yenye umuhimu?
5. Je! Kwanini inastajabisha sana kupata ufufuo wa hatua mbili katika sura hii?
6. Je! Ni kwa njinsi gani watakatifu waliofufuliwa waliishi pamoja sanjari na mataifa yaliopo?
7. Je! Nani anahusishwa katika hukumu ya kiti cha enzi kikubwa cheupe katika Ufu.20:11-15?

# UFUNUO 21-22

| MGAWANYO WA AYA WA TAFASIRI YA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Mbingu Mpya na Nchi Mpya | Vyote kufanywa Vipya | Maono ya Yerusalemu Mpya | Mbingu Mpya na nchi Mpya | Yerusalemu ya Mbinguni |
| | | (21:1-22:5) | | |
| 21:1-4 | 21:1-8 | 21:1-4 | 21:1-4 | 21:1-4 |
| 21:5-8 | | 21:5-8 | 21:5-8 | 21:5-8 |
| Yerusalemu Mpya | Yerusalemu Mpya | Kulipima jiji | Yerusalemu Mpya | Yerusalemu ya Ki-Masihi |
| 21:9-14 | 21:9-21 | 21:9-14 | 21:9-21 | 21:9-14 |
| 21:15-21 | Utukufu wa Yerusalemu Mpya | 21:15-21 | | 21:15-22:2 |
| | | Mto na Mti wa Uzima | | |
| 21:22-22:5 | 21:22 | 21:22-22:5 | 21:22-22:3a | |
| | Mto wa Uzima | | | |
| | 22:1-5 | | | |
| | | | 22:3b-5 | 22:3-5 |
| Kuja kwa Kristo | Muda Umekaribia | Hitimisho la kazi | Kuja kwa Yesu | |
| 22:6-7 | 22:6-11 | 22:6 | 22:6 | 22:6-7 |
| | | 22:7 | 22:7 | |
| 22:8-11 | Yesu Kuyashuhudia Makanisa | 22:8-9 | 22:8-11 | 22:8-9 |
| | | 22:10-11 | | 22:10-15 |
| 22:12-13 | 22:12-17 | 22:12-13 | 22:12-13 | |
| 22:14-15 | | 22:14-15 | 22:14-15 | Hitimisho la kazi |
| 22:16-17 | | 22:16-17 | 22:16 | 22:16 |
| | | | 22:17a | 22:17 |
| | | | 22:17b | |
| | | | 22:17c | |
| | Onyo | | Hitimisho | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 22:18-19 | 22:18-19 | 22:18-19 | 22:18-19 | 22:18-19 |
| | Naja Upesi | | | |
| 22:20 | 22:20-21 | 22:20 | 22:20 | 22:20 |
| | | 22:20b | 22:20b | 22:20b |
| 22:21 | | 22:21 | 22:21 | 22:21 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Angalia Semina ya Ukarimani wa Biblia) (Bible Interpretation Seminar)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA.*

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

33. Aya ya kwanza
34. Aya ya pili
35. Aya tatu
36. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Ufunuo 20-22 Unaunda sehemu wa saba za kitengo cha fasihi. Ufunuo 21-22 unahitimisha matendo ya Mungu katika historia ya mwanadamu na kuanzisha ufalme wa milele (kama vile Dan 7: 13-14,27, 1 Kor.15: 27-28). Ufunuo 22: 6-21 ni hitimisho la kitabu chote.
B. Karibu kila kipengele katika sura hizi mbili ni dokezo kwa (1) Mwanzo 1-3; (2) Zaburi 110; au (3) maandiko ya Kiyahudi juu ya matukio ya siku za mwisho kati ya kipindi kati ya agano la kale na agano jipya.
C. Kumekuwako majadiliano mengi kuhusu mambo yasiyo ya kawaida katika sehemu hii ya mwisho.
   1. Kutajwa kwa 'mataifa' - Ufunuo 21:14; 22: 2
   2. Kutajwa kwa 'Wafalme wa dunia' - Ufunuo 21: 24,26
   3. Kutajwa kwa kilicho kinyonge kutoingia ndani yake' - Ufunuo 21:27; 22:15

   Inaonekana kuna sababu kadhaa zinazowezekana katika kuyajumuisha mambo haya:
   1. Yohana anauelezea unabii wa Agano la Kale. Kama mfano wa Injili, ambao wakalimani hawakukusudiwa kutafsiri maelezo yake halisi, lakini kutambua mikazo mikuu.
   2. Lengo la Yohana ni kuonyesha tofauti ya mwisho kati ya waliookolewa na waliopotea.
   3. 'Mataifa' yaliyotajwa katika sehemu hii hutumiwa kwa maana jumla ya kikabila kama 'watu wa Mungu' katika Ufunuo 5: 9; 7: 9; 21:14 na 22: 5.
   4. Kwa sababu ya mambo haya wengine wameona Wayahudi waliookolewa ndani ya mji na Wayahudi waliookolewa nje ya mji. Lakini, kwa sababu ya Wagalatia 3:29 na Waefeso 2: 11-3: 13, hlii haliwezi kuwa chaguo linalofaa la kitheolojia.
   5. Nadhani kuna upatanisho kati ya Ufu. 17-19 na Ufu. 20-22. Hili linaelezea kiini cha kawaida kilichopo katika sehemu hii.
D. Kuna mfululizo mwingine wa 'saba' unaopatikana katika sura hizi mbili. Hivi ni vitu visivyokuwepo tena
   1. Bahari - Ufunuo 21: 1
   2. Mauti - Ufunuo 21: 4
   3. Kuomboleza - Ufunuo 21: 4
   4. Kulia - Ufunuo 21: 4

5. Maumivu - Ufunuo 21: 4
6. Usiku - Ufunuo 21:25
7. Laana - Ufunuo 22: 3

E. Kama hukumu zinazohusiana na Ujio wa Pili wa Kristo zinaonyeshwa kwa namna ya ajabu katika maono matatu (muhuri, baragumu, na bakuli), labda mbinguni kunaonyeshwa kwa namna ya ajabu katika mifano mitatu ya Agano la Kale:
   1. Hekalu, Ufunuo 21: 1-8
   2. Yerusalemu Mpya, Ufunuo 21: 9-26
   3. Bustani ya Edeni, Ufunuo 22: 1-5

Hili linaweza pia kuwa la kweli juu ya utangulizi (Ufunuo 1: 1-8), ambao unasisitiza juu ya
1. Uharaka wa kurudi kwa Kristo
2. Uaminifu wa maneno ya Mungu
3. Utakatifu unaohitajika wa watu wa Mungu

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 21:1-4**
**[1]Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita, wala hapana bahari tena. [2]Nami nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe.[3]Nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema, Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao. [4]Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita.**

**21: 1 'Kisha nikaona'** Kuna kipindi cha muda fulani, muda gani unategemea ufafanuzi wako wa 'miaka elfu' ya sura ya 20.

◙ **"mbingu mpya na nchi mpya"**Neno hili la Kiyunani lenye maana ya *kainos* "mpya", linasisitiza ubora, sio nyakati za majira (kama vile Ufunuo 2:17; 3:12, 5: 9; 14: 3; 21: 1 , 2,5). Hili lilikuwa ni kiini cha Agano la Kale, nchi iliyorejeshwa (kama vile Isaya 11: 6-9, 65:17, 66:22) angalia pia Rum 8: 18-25, 2 Pet 3: 10,12). Waumini wote ni raia wa Ufalme huu mpya (kama vile Filipi 3:20, Waefeso 2:19, Waebrania 12:23) na hushiriki uumbaji huu mpya (kama vile 2 Wakorintho 5:17, Wagalatia 6:15; Waefeso 4:24). Dhana sambamba ya kithiolojia inayofanana itakuwa "mji wa Mungu usiofanywa kwa mikono ya kibinadamu" ya Ebr. 11: 10,16; 12:22; 13:14.

Uumbaji mpya utakuwa kama uumbaji wa awali. Mbinguni inaweza kuwa bustani ya Edeni iliyorejeshwa. Mungu, wanadamu, wanyama, na viumbe vyote vya asili watashirikiana na kufurahi tena! Biblia huanza na Mungu, wanadamu, na wanyama katika ushirika kamili katika bustani (kama vile Mwanzo 1-2). Biblia inamalizia na Mungu na wanadamu katika mazingira ya bustani (kama vile Ufunuo 21-22) na kwa maana ya kinabii, wanyama (kama vile Isaya 11: 6-8, 65:25). Waumini hawaenda mbinguni Yerusalemu mpya inatoka kutoka mbinguni (kama vile Ufunuo 21: 2) na kuja kwenye dunia iliyorejeshwa na iliyosafishwa. Mungu na wanadamu wanakuwa pamoja tena (kama vile. Mwanzo 3:15, Isa 7:14; 8: 8,10, Ufunuo 21: 3).

◙ **"kwa maana mbingu ya kwanza na nchi ya kwanza vimepotea"** Kutakuwa na uumbaji wa kurejeshwa (kama vile Matendo 3:21, Warumi 8:21; Wakolosai 1:20), hawakuathirika tena na dhambi (kama vile II Baruki 37: 6, 2 Pet 3: 10-12; Ufunuo 20:11).

◙ **"na hakuna bahari tena"** Kumekuwa na tafsiri nyingi za maneno haya (angalia maelezo katika Ufunuo 4: 6):
1. kwa sababu bahari imetajwa katika Ufunuo 4: 6 kama njia ya kuzungumza juu ya utakatifu wa Mungu ambayo humtenganisha na Mwanadamu mdhambi, wengine wameuona kusitishwa kwake hapa ni kama kurejeshwa kwa ushirika kamili kati ya Mungu na binadamu
2. kwa sababu katika Ufunuo 20:13 bahari ilionekana kuwa moja ya maeneo matatu yanayowashikilia wafu, ni njia ya kusema kuwa wafu wote wamepewa nafasi moja ya njia mbili za hatima ya umilele.

3. kwa sababu mnyama wa kwanza katika Ufunuo 13: 1 hutoka baharini na kuna mwelekeo wa bahari kama kuwamaanisha watu waovu katika Isa. 57:20, inawezekana ni waovu ambao hawapo tena
4. kwa sababu Ufunuo 17:15 ni nukuu kutoka Isa. 17: 12-13 ambako maji yanasimamia watu, wengi wanasema kwamba inawakilisha mataifa maovu, kama vile Zaburi ya 2. kama # 1 bora.

**21: 2 "Nikauona mji mtakatifu, Yerusalemu mpya"** Yerusalemu katika Palestina inaitwa 'mji mtakatifu' katika Isa. 52: 1 (kama vile. Isa 48: 2, 64:10; Dan 9:24; Neh 11: 1). Yerusalemu mpya hii inaelezwa kwanza katika Ufunuo 3:12 na inaelezewa katika Ebr. 11:10; 12:22; na 13:14. Hii inaonyesha jinsi Yohana alivyoupeba unabii wa Agano la Kale, maneno, vyeo, ahadi na kuvitumia kwa watu wapya wa Mungu. Mji huu sio agano la kale la Yerusalemu huko Palestina kama watu wengine wa milenia wanavyofikiri, bali ni agano jipya la Yerusalemu ya mbinguni.

◙ "**Kushuka kutoka mbinguni"**Hakupo kushuka mara mbili, bali mmoja katika Ufunuo 21: 2 na mwingine katika Ufunuo 21:10. Lugha ya matukio ya siku ya kiyama ni nyepesi na haipaswi kuundwa ki-majira, ki-mantiki, au kwa uasilia.

◙ **"amefanya tayari kama bibi arusi aliyepambwa kwa mumewe"** Mstari huu ni dokezo kwa Isa. 61:10 (kama vile Ufunuo 19: 7). Katika sura hizi za mwisho taswira kadhaa hutumiwa kuwaelezea watu wa Mungu:

1. bibi harusi (kama vile Ufunuo 19: 7; 21: 2)
2. mgeni wa harusini (kama vile Ufunuo 19: 9)
3. mji (kama vile Ufunuo 21:22; 22: 2).

Taswira ya Agano Jipya na YHWH (kama vile hasa Hosea 1-3) kama mume na Israeli kama bwana harusi ndiyo msingi wa sura ya Kanisa kama Bibi arusi wa Kristo (kama vile. Waefeso 5: 21-31).

**21: 3 '' Tazameni, hema ya Mungu iko kati ya wanadamu ''** Maneno haya ya Kiyunani huzirudia ahadi za Agano la Kale za Mungu kuishi na wanadamu kwa njia tatu tofauti:

1. ni dokezo kwa hema, ishara ya uwepo wa YHWH
2. 'Atakaa kati yao' ni kile neno 'Emanuel' kilimaanisha katika Isa. 7:14 (kama vile Yohana 1:14)
3. 'watakuwa watu wake' ni istilahi ya agano; sasa watu wote wanaoamini (kama vile Yohana 10:16) ni watu waliochaguliwa na Mungu (kama vile Law 26: 11-12, Ezek 37: 23,27).

**21: 4 "Naye atawafuta kila chozi katika macho yao"** Mstari huu ni dokezo kwa Isa. 25: 8 (kama vile. Mathayo 5: 4; 7:17). Majira mapya yatakuwa ni wakati wa furaha, amani, ustadi, na sifa!

◙ **"wala mauti hakutakuwapo tena"** Adui huyu wa mwisho (kama vile Ufunuo 20:14) ataangamizwa (kama vile 1 Wakorintho 15:26). Waumini watakuwa na miili yao mpya kama mwili wa Kristo aliyefufuliwa (kama vile 1 Wakorintho 15: 50-57, 2 Wakorintho 3:18, 1 Wathesalonike 4: 15-16, 1 Yohana 3: 2).

◙ **"wala maombolezo,wala kilio,"** Mstari huu ni dokezo kwa Isa. 65:19 na pia huaksi Isaya. 35:10.

◙ **"mambo ya kwanza yamekwisha kupita"** Utaratibu wa kwanza uliotengenezwa uliathiriwa na anguko (kama vile. Mwanzo 3; 6: 5,1-12,13), lakini utaratibu mpya hauwezi kuathiriwa na dhambi (kama vile Waebrania 12: 27-28).

**ANDIKO LA NASB (ILIYOBORESHWA): UFUNUO 21: 5-8**

**5 Na yeye aketiye juu ya kile kiti cha enzi akasema, Tazama, nayafanya yote kuwa mapya. Akaniambia, Andika ya kwamba maneno hayo ni amini na kweli. 6 Akaniambia, "Imekwisha kuwa" . Mimi ni Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho. Mimi nitampa yeye mwenye kiu, ya chemchemi ya maji ya uzima, bure. 7 Yeye ashindaye atayarithi haya, nami nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa mwanangu. 8 Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili."**

**21:5 "Na yeye aketiye juu ya kile"** Mungu anazungumza mara kadhaa katika Ufunuo (kama vile Ufunuo 1: 8 na labda 16: 1,17). Inaonekana kuwa na usawa wa makusudi juu ya nani anayeketi katika kiti cha enzi, YHWH au Masihi (kama vile Ufunuo 22: 3). Angalia maelezo kamili katika Ufunuo 20:11. Kama vile viumbe vya kwanza vilivyoanzishwa na Mungu (yaani, Baba kupitia Mwana) alizungumza (kama vile Mwanzo 1: 3,6,9,14,20,24; Zaburi 33: 6,9), kadhalika, pia kama impendezavyo kuumbwa kupya kutakuwa.

◙**"Nayafanya yote kuwa mapya"** Hii ni ahadi ya Isaya 60-66. Hili linarejea zama mpya za Roho, zama za Masihi, zama zaa haki, ambazo Yesu alizizindua wakati wa ujio wake wa kwanza na atavishinda wakati wa Kuja kwake kwa mara ya Pili. Huu ni mfano wa uhakika wa mapenzi ya Mungu kuwa ukweli (kama vile. Ufunuo 1:19, 14:13; 17:17; 19: 9).

◙ **"Maneno hayo ni amina na kweli"** Maneno haya yalitumiwa ili kuelezea

1. Yesu, kama vile Ufu. 1: 5; 3: 7,14; 19:11
2. Wafuasi wa Yesu, kama vile Ufu. 17:14
3. Neno la Mungu kama vile Ufu. 19: 9; 21: 5; 22: 6
4. Mara nyingi Mungu anaelezewa kama “mwenye haki na kweli” (kama vile Ufunuo 15: 3, 16: 7, 19: 2). Dhana ya Kiebrania nyuma ya kifungu cha maneno cha Kiyunani kingemaanisha uaminifu.

**21:6 "Imekwisha kuwa"** Hii ni KAULI TIMILIFU TENDAJI YENYE KUARIFU. Hii inaweza kuhusisha uhakika wa ahadi za Mungu kuhusu vyote, hasira kwa wasioamini na ukombozi kwa waaminio (kama vile Ufunuo 6:11; 10: 7; 16:17), au asili ya ahadi za Mungu (kama vile Ufunuo 1: 1). , 3: 3:11; 10: 6; 12:12; 22: 7,10).

◙ **"Mimi ni Alpha na Omega"** Hii hutumiwa na Mungu katika Isa. 44: 6 na Ufunuo 1: 8; hata hivyo, ni muhimu sana kwamba maneno haya, ingawa jina la Baba, pia hutumiwa kwa maana ya Masihi katika Ufunuo 1:17 na 22:13. Ni mfano mwingine wa waandishi wa Agano Jipya wanaotumia majina ya Mungu kwa kumaanisha Mwana.

Kuna aina kadhaa ya maneno ambayo yanaelezea umilele, na uwepo wa Mungu wa kipekee:

1. “wa kwanza na wa mwisho,” kama vile Isa. 41: 4; 44: 6; 48:12; Ufu. 1:17; 2: 8; 22:13
2. “mwanzo na mwisho,” kama vile Ufu. 21: 6; 22:13; na KJV 1: 8
3. “yeye aliyepo na aliyekuwapo na ajaye,” kama vile Ufu. 1: 4,8; 4: 8

Yote haya yanahusiana na jina la ki-maagano la Mungu, YHWH, ambalo ni la muundo wa KITENZI cha Ki-ebrania cha neno “kuwa” (kama vile Kut. 3:14, Isa 43: 10,13; 46:41; Zab 90: 2 ; 93: 2).

Mada maalum: Majina ya Uungu D ( Special Topic: Names for Deity, D)

◙**"Nitampa yeye mwenye kiu, ya chemchemi ya maji ya uzima, bure"** Dokezo la Agano la Kale kwa Isaya 55. Mwaliko ni kwa kila mtu na ni wa bure kabisa (kama vile Warumi 3:24, 6:23, Waefeso 2: 8)! Ni mwaliko mkubwa kutoka kwa Mungu Mwenyewe wa upatikanaji wa msamaha. Ukombozi wa wanadamu daima umekuwa katikati ya moyo na akili za Mungu (kama vile Ufunuo 9: 20-21, 14: 6-7, 16: 9,11; 22:17).

Katika chemchemi za maji ya Agano la Kale mara nyingi huhusishwa na Mungu kutoa mahitaji ya kiroho ya wanadamu (kama vile Zaburi 36: 9, Isa 12: 3, 44: 3, 49:10, Yer 2:13; ; Pia Yohana 4:10).

**21:7 "Yeye ashindaye"** Hii ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO, ambayo ni rejea inayoendelea kwa mafundisho ya uvumilivu katikati ya wakati wa mateso makubwa. Kifungu hiki cha maneno hutokea katika nyaraka zote kwa makanisa saba (taz. Ufunuo 2: 7,11,17,26; 3: 3,5,12,21), ambayo inaunganisha sura za ufunguzi za Ufunuo hadi hitimisho.

Mada maalum: Uvumilivu (Special Topic: Perseverance)

◙**"Atayarithi haya"** Tuzo ya urithi katika Ufunuo 21: 7 (kama vile 1 Pet 1: 4,5; Rum 8:17) na onyo la Ufunuo 21: 8 ni kinyume na uasi wa uwezo katika kipindi cha mateso. Mfululizo wa uovu wa uasi (kama vile Ufunuo 21: 8)

ni sawa na ile iliyopatikana katika 1 Kor. 6: 9-10.

Mada maalum: Urithi wa Waumini (Special Topic: Believer's Inheritance)

◙ **"Nami nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa mwanangu"** Hivi ndivyo vifungu vya maneno vya agano (kama vile Ufunuo 21: 3) ambayo ni vya kawaida katika Agano la Kale (kama vile. Kut. 6: 7, 29: 45,46; Walawi 26: 11-12; 2 Sam 7:14; Zab 89: 26-27; Yer 7:23, 11: 4, 30:22, 33:38, Ezekieli 11:20, 14:11, 34:30, 36:28 Hos 2:23; Zekaria 8: 8; 13: 9) na pia hutumiwa katika Agano Jipya (kama vile 2 Wakorintho 6: 16,18).

Dhana ya agano pengine ni dhamira ya umoja wa Biblia. Mwanadamu amekuwa mgeni kutoka kwa Mungu (kama vile Isaya 53: 6; Rum 3: 9-18,23). Mwanadamu hawezi kumtafuta Mungu. Mungu hufikia mbali kwa ajili yetu; Mungu anatufuata! Zawadi yake ya kuungana tena ni mojapo ya agano. Analianzisha (kama vile Jer 31: 3; Yohana 6: 44,65); Anaweka ajenda, lakini wanadamu wanapaswa kujibu kwa njia iliyo maalum. Njia hizi zimetofautiana ki-maudhui (Adamu / Hawa, mti wa marufuku, Nuhu, mashua, Ibrahimu, nchi, mwana, Musa, kanuni ya sheria), lakini aina ya kukubaliwa, imani katika uaminifu wa Mungu, hubakia vilevile (kama vile Warumi 4). Agano la Kale lilikuwa na mahitaji; Ndivyo lilivyo Agano Jipya (kama vile Marko 1:15; Matendo 3: 16,19; 20:21). Wanadamu wanapaswa kujibu mwanzoni na kuendelea katika imani, toba, utii, huduma, ibada, na uvumilivu.

Mada Maalumu: Mwana wa Mungu. (SPECIAL TOPIC: The Son Of God)

Mada Maalumu: Agano  (Special Topic: Covenant)

**21:8** Siyo kawaida kupata mfululizo huu wa dhambi wakati hukumu imekwisha kutokea na waovu wamefikiriwa kuondolewa (kwa ushindi wa Yesu wakati wa Kuja kwake kwa mara ya Pili, kama vile. Ufunuo 19: 5-21 na Kiti cha enzi cha Cheupe, kama vile 20: 11-15). Huku siko kusema kuwa waumini wengine hawajafanya dhambi hizi isipokuwa maisha yao hayajulikani na dhambi hizi (kama vile 1 Yohana 3: 6,9). Hii inaonekana kuwa mbinu ya fasihi ili kuonyesha tofauti ya milele kati ya kuokolewa na waliopotea au kipengele cha tamthilia ya matukio ya siku ya mwisho (mara kwa mara kwa msisitizo). Angalia "Utangulizi wa Ufunuo," Taarifa za Ufunguzi, C.

◙**"Ziwa liwakalo moto na kiberiti. . .mauti ya pili"** Ni wazi kwamba ziwa la moto lina ulinganifu na kifo cha pili au dhana yetu ya Jehanamu, ambayo Yesu aliiita *Gehenna* (neno la Kiyunani ambalo halionekani katika Ufunuo). Angalia Mada Maalumu: Wafu Wako Wapi? (SPECIAL TOPIC: Where Are the Dead?)

**NASB (ILIYOBORESHWA) ANDIKO: Ufunuo 21: 9-14**
**[9] Akaja mmoja wa wale malaika saba waliokuwa na vile vitasa saba vilivyojaa yale mapigo saba ya mwisho, naye akanena nami, akisema, "Njoo huku, nami nitakuonyesha yule Bibi-arusi, mke wa Mwana-Kondoo. "[10] Akanichukua katika Roho mpaka mlima mkubwa, mrefu, akanionyesha ule mji mtakatifu, Yerusalemu, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mwenyezi Mungu; [11] wenye utukufu wa Mungu, na mwangaza wake ulikuwa mfano wa kito chenye thamani nyingi kama kito cha yaspi, safi kama bilauri; [12] ulikuwa na ukuta mkubwa, mrefu, wenye milango kumi na miwili, na katika ile milango malaika kumi na wawili; na majina *yameandikwa* ambayo ni *majina* ya kabila kumi na mbili za Waisraeli. [13] Upande wa mashariki milango mitatu; na upande wa kaskazini milango mitatu; na upande wa kusini milango mitatu; na upande wa magharibi milango mitatu. [14] Na ukuta wa mji ulikuwa na misingi kumi na miwili, na katika ile misingi majina kumi na mawili ya wale mitume kumi na wawili wa Mwana-Kondoo.**

**21:9 "Mmoja wa wale malaika saba"** Haya ni maelezo halisi ya malaika katika Ufu. 15: 1,6-8; 16: 1; na 17: 1 wale waliomimina zile bakuli saba. Kuna destruri katika sheria za dini ya Kiyahudi kwamba kuna Malaika saba wa Uwepo wanaomtumikia Mungu. Hapa, kuna malaika mmoja kwa kila pigo.

**21:10 "Akanichukua katika Roho"** Hii ni mbinu ya fasihi ili kuonyesha maono tofauti (kama vile. Ufunuo 1:10, 4: 2; 17: 3; 21:10).

Mada Maalum: Roho (*pneuma*) katika Agano la Kale ( Special Topic: Spirit (pneuma) in the NT)

◙**"mpaka mlima mkubwa, mrefu"** Wengi wanaamini kwamba hili liko kwenye uelekeo wa moja kwa moja na mchungaji mkuu aliyekuwa mahali pa wazi. Hata hivyo, Yohana anaelezea vifungu vingi vya Agano la Kale, kwa hiyo hapa anaweza kuwa anaurejelea mlima wa ajabu wa kaskazini ambako Mungu anaishi (kama vile Ezek 40: 2, Isa 2: 2, 14:13, Mika 4: 1; 18: 8; 25: 3). Inawezekana kwamba inaelezea jaribu la Shetani kwa Yesu katika Mathayo 4: 8.

◙ **"akanionyesha ule mji mtakatifu, Yerusalemu, ukishuka kutoka mbinguni"** Hii ni Yerusalemu ya mbinguni, mfano wa uwepo wa Mungu (kama vile Ufunuo 21: 2). Yerusalemu yenye dhambi duniani ilizungumziwa katika Ufunuo 11: 1-13. Jiji kuu la Daudi limefanyika la ki-ulimwengu katika makazi ya wakati wa mwisho wa watu wote wa Mungu (kama vile Yohana 14: 2-3).

Mada maalum: Kwa nini ahadi za Agano la Kale zimeonekana kuwa tofauti sana na ahadi za Agano Jipya? (Special Topic: Why Do OT Covenant Promises Seem So Differ from NT Covenant Promises?)

**21:11 "Mwanga wake ulikuwa kama mfano wa kito chenye thamani nyingi kama kito cha yaspi."** Mji (kama vile Ufunuo 21: 11-27) umeelezwa kwa maneno mazuri sana, kimwili, na ki-maadili. Kama kitabu chote cha Ufunuo, sura hii ni kama mfano. Udhambi wa Wanadamu, wenye akili kamili hawana uwezo wa kuelewa furaha na utukufu wa uwepo wa Mungu (kama vile 1 Wakorintho 2: 9). Vyombo vya thamani na jiji la kale vyaweza kuwa mifano mizuri, lakini sio uhalisia wa kweli! Mbingu ni ni kote kweli, mtu (yaani Yesu), na mahali (kwa ushirika na Mungu wa Tatu).

**21:12 "Wenye milango kumi na miwili, na katika ile milango malaika kumi na wawili"** Mstari huu ni dokezo kwa Ezek. 48: 31-34. Hesaabu 'kumi na mbili' hutokea mara kwa mara katika ukunbusho wa sura hii na mistari michache ya kwanza ya sura ya 22. Ni ishara ya kibiblia ya shirika (miezi kumi na miwili, kabila kumi na mbili, au mitume kumi na wawili) au watu wa Mungu. Angalia Mada Maalum: Hesabu Kumi na Mbili.(Speciala Topic: the Number Twelve)

◙ **"na majina yameandikwa, ambayo ni majina ya kabila kumi na mbili za Waisraeli"** Orodha ya kabila kumi na mbili katika Ufunuo 7: 5-8 kwa kiasi kidogo iliubadili Mwonekano wao wa asili. katika hili, ni muhimu sana kutambua kwamba watu wa Agano la Kale wa Mungu, walioelezewa kama milango katika Ufunuo 21:12, wameungana na watu wa Mungu wa Agano Jipya, wakielezewa kama mawe ya msingi, katika Ufunuo 21:14. Siku zote kumekuwa na umoja wa watu wa Mungu, lakini siri hii haikufunuliwa wazi mpaka kuwadia kwa Injili (kama vile Waefeso 2: 11-3: 13).

**21:14 "ukuta wa mji ulikuwa na misingi kumi na miwili, na kaika ile misingi majina kumi na mawili ya wale mitume kumi na wawili wa Mwana-Kondoo "** Sitiari zote hizi zinaelezea Hekalu la wakati wa mwisho wa Ezekieli (Angalia Ezekieli 40-48).Watoa maoni wengi wamesisitiza kwamba mstari huu unaonyesha kwamba mwandishi hawezi kuwa Yohana Mtume. Hata hivyo, Paulo anatumia maneno kama haya sawa na Waefeso 2:20.

**NASB (UPDATED) TEXT: REVELATION 21:15-21**
**[15] Na yeye aliyesema nami alikuwa na mwanzi wa dhahabu, apate kuupima huo mji, na milango yake, na ukuta wake. [16] Na ule mji ni wa mraba, na marefu yake sawasawa na mapana yake. Akaupima mji kwa ule mwanzi; ulikuwa kama maili elfu na mia tano; marefu yake na mapana yake na kwenda juu kwake ni sawasawa. [17] Akaupima ukuta wake, ukapata dhiraa mia na arobaini na nne, *kwa* kipimo cha kibinadamu, maana yake, *cha* malaika. [18] Na majenzi ya ule ukuta wake yalikuwa ya yaspi, na mji ule ulikuwa wa dhahabu**

**safi, mfano wa kioo safi. [19] Na misingi ya ukuta wa mji ilikuwa imepambwa kwa vito vya thamani vya kila namna. Msingi wa kwanza ulikuwa yaspi; wa pili yakuti samawi; wa tatu kalkedoni; wa nne zumaridi; [20] wa tano sardoniki; wa sita akiki; wa saba krisolitho; wa nane zabarajadi; wa kenda yakuti ya manjano; wa kumi krisopraso; wa kumi na moja hiakintho; wa kumi na mbili amethisto. [21] Na ile milango kumi na miwili ni lulu kumi na mbili; kila mlango ni lulu moja. Na njia ya mji ni dhahabu safi kama kioo kiangavu.**

**21:15 "Na yeye aliyesema nami alikuwa na mwanzi wa dhahabu, apate kuupima huo mji"** Upimaji ulitumiwa mapema ili kuonyesha ulinzi na utunzaji wa Mungu (kama vile Ufunuo 11: 1-2; Yer 31: 38-40; Zek 2: 1-5). Unabii wa wakati wa mwisho wa Ezekieli 40 pia unahusisha kupima.

**21:16 " Na ule mji ni wa mraba"** Mstari huu unaweza kuwa dokezo kwa Mtakatifu wa Watakatifu (kama vile 1 Waf 6: 19-20), ambayo pia ilikuwa mchemraba mkamilifu.

Sababu ya kuwa hakuna hekalu (kama vile Ufunuo 21:22) ni kwa sababu Mungu Mwenyewe atakuwa ndilo hekalu. Hii inaweza kuwa njia ya Yohana ya kuonyesha kwamba unabii wa Agano la Kale kama Ezekieli 40-48 ni mfano au umetimizwa kwa namna tofauti.

◙**" maili elfu na mia tano"** Kwa kweli hii ni "stadia kumi na mbili elfu na mia moja na arobaini na nne.' Hii ni makutano ya kumi na wawili; hawaelezei mji wa kweli, lakini vipimo kamili vinavyoonyesha kwamba Mungu anatoa mazingira ya pekee ya furaha ya kudumu na ushirika kati yake na watu wake (kama vile Yohana 14: 2-3) katika ishara kamili ya mchemraba kama ni taswira ya Agano la Kale, Patakatifu pa Patakatifu."

**21:18-20 "Vifaa vya kwa ajili ya ukuta vilikuwa "** Mfululizo huu wa mawe unaweza kutambuliwa kwa

1. Mawe juu ya efodi ya Kuhani Mkuu (kama vile Kut. 28: 17-20), hata hivyo, utaratibu na majina ni tofauti. Hii ilikuwa isiyo ya kawaida kwa sababu majina ya mawe ya kale yalibadilishwa kutoka nchi hadi nchi na karne hadi karne.
2. jiji la vito vya thamani la Isa. 54: 11-17
3. Utukufu wa mfalme wa Tiro (au Shetani) ulitowakilishwa katika vyombo thamani vya mfalme (au mbinguni) katika Ezek. 28: 12-13
4. Mhimili, lakini iliyotolewa kwa utaratibu wa nyuma (Philo na Josephus)

**21:21 "Na milango kumi na miwili ilikuwa lulu kumi na mbili; kila moja ya milango ilikuwa lulu "** Mstari huu ni mfano. Unarudi nyuma hadi kwenye desturi za ki-ualimu za dini ya Kiyahudi (Talmud), '*Sanhedrin*' 100a, ambayo inasema kuwa milango ya jiji litakalokuja siku ya mwisho itatengenezwa kwa jiwe moja la urefu wa miguu 45.

Mada maalum: Hesabu za Ki-maandiko katika Andiko, # 6 (Special Topic: Symbolic Numbers in Scripture, #6)

◙**"Na njia ya mji ni dhahabu safi, kama kioo kiangavu"** Mstari huu ni mfano. Tunapaswa kutambua kwamba mji wa Mungu sio unyenyekevu wa kibinadamu, bali linaashiria thamani na usafi wa uwepo wa Mungu.

**NASB (UPDATED) TEXT: REVELATION 21:22-27**
**[22] Nami sikuona hekalu ndani yake; kwa maana Bwana Mungu Mwenyezi na Mwana-Kondoo, ndio hekalu lake. [23] Na mji ule hauhitaji jua wala mwezi kuuangaza, kwa maana utukufu wa Mungu huutia nuru, na taa yake ni Mwana-Kondoo. [24] Na mataifa watatembea katika nuru yake. Na wafalme wa nchi huleta utukufu wao ndani yake. [25] Na milango yake haitafungwa kamwe mchana; (kwa maana humo hamna usiku). [26] Nao wataleta utukufu na heshima ya mataifa ndani yake. [27] Na ndani yake hakitaingia kamwe cho chote kilicho kinyonge, wala yeye afanyaye machukizo na uongo, bali wale walioandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo.**

**21:22 " Nami sikuona hekalu ndani yake; kwa maana Bwana Mungu Mwenyezi na Mwana-Kondoo, ndio hekalu lake"**Hili silo la kawaida lkilinganishwa na vifungu vingi katika Ufunuo ambapo hekalu la mbinguni linaonyeshwa (kama vile Ufunuo 3:12, 7:15; 11: 1,2,9,19; 14: 15,17; 15: 5 , 6,8; 16: 1,17). Dhana hii ya hekalu mbinguni inafunuliwa katika kitabu cha Waebrania (kama vile Ufunuo 8: 2-5; 9: 11,23-24.)

◙ **"Bwana Mungu Mwenyezi"** Hapa tena pana sifa tatu zinzotumika zaidi za Agano la Kale kwa Mungu (YHWH, Elohim na El Shaddai) yaliyotumika kwa pamoja (kama vile Ufunuo 1: 8, 4: 8, 11:17; 15: 3; 16: 7) ili kuonyesha Utukufu wa Yeye anayeketi juu ya Kiti cha enzi. Angalia uhusiano wake wa karibu na Mwana-Kondoo wa Ufunuo 5. Wanatawala pamoja na kuna Kiti cha enzi kimoja tu (kama vile. Ufunuo 22: 1,3).

Mada maalum: Majina ya Uungu, C. and D. (Special Topic: Names for Deity, C and D )

Mada Maalumu: *Shaddai* (Special Topic*: Shaddai)*

**21:23 " Na mji ule hauhitaji jua wala mwezi kuuangaza, kwa maana utukufu wa Mungu huutia nuru, na taa yake ni Mwana-Kondoo"** Utukufu wa Baba na Mwana ni taa zote zinazohitajika (kama vile Zaburi 36: 9, Isaya 24:23, 60: 19-20, Zak 14: 6-7 na pia Ufunuo 22: 5) . Huu ni uwezekano wa njia ya kukataa kusisitiza ibada ya nyota.

**21:24 "Na mataifa watatembea katika nuru yake. Na wafalme wa nchi huleta utukufu wao ndani yake"** Ni vigumu sana kuelewa kwa nini "mataifa"bado yanasemwa katika hii sehemu ya Kiti cha Enzi-Cheupe cha Ufunuo. Inawezekana tu kuwa mwongozo wa Agano la Kale kwa Zab. 72: 10-11; Isa. 49:23; 60: 3,15,16. Sio kweli, bali ni fasihi! Inawakilisha watu wote kutoka kwa kabila na mataifa yote wanaojengeka kuwa watu wa Mungu.

**21:25 "Na milango yake haitafungwa kamwe mchana; ( kwa maana humo hamna usiku)"** Mstari huu ni dokezo kwa Isa. 60:11 au Zak. 14: 6-7. Dhana ya giza katika Biblia mara nyingi ni mfano wa uovu (kama vile Mathayo 6:23, 8:12, 22:13, 25:30). Mwanga na giza zilikuwa tofauti muhimu za ki-theolojia kwa Yohana (kama vile Yohana 1: 4-5, 7-9, 3: 19-21, 8:12, 11: 9-10, 12: 35-36,46; Yohana 1: 5-7; 2: 8-11). Malango kutokufungwa ni taswira ya uwazi, upatikanaji, kutokuwapo hofu ya mashambulizi.

**21:27 "Na ndani yake hakitaingia kamwe cho chote kilicho kinyonge, wala yeye afanyaye machukizo na uongo"** Mstari huu ni dokezo kwa Isa. 52: 1; Ezek. 44: 9; Zak. 14:21 ambao unaonekana kuwa mbinu ya fasihi inayoonyesha tofauti ya mwisho kati ya watu wa Mungu na wale wa mwovu (kama vile Ufunuo 21:24). Zama mpya ina sifa katika wepesi, mji huru, mji wa haki kamili. Hakuna uovu wowote!

**Wameandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-kondoo"** Kifungu hiki cha maneno cha ki-sitiari "kitabu cha uzima" pia hupatikana katika Ufunuo 20: 12-15, ambapo vitabu viwili vinatajwa:

1. kitabu cha uzima, ambacho kinajumuisha majina ya watu wa Mungu (kama vile Kut. 32:32, Zaburi 69:28, Isa 4: 3, Dan 12: 1, Luka 10:20; Waebrania 12:23, Ufunuo 13: 8; 17: 8; 20:15; 21:27)
2. Kitabu cha matendo au kumbukumbu ambazo zinaandika matendo mabaya na maadili (kama vile Zaburi 56: 8, 139: 16, Isaya 65: 6; Mal 3:16)

Ki-sitiari hizi ni kumbukumbu kamili za Mungu.

Mada Maalum: Vitabu viwili vya Mungu (Special Topic: The Two Boooks of God)

# UFUNUO 22

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 22:1-5**
**[1]Kisha akanionyesha mto wa maji ya uzima, wenye kung'aa kama bilauri, ukitoka katika kiti cha enzi cha**

**Mungu, na cha Mwana-Kondoo, [2]katikati ya njia kuu yake. Na upande huu na upande huu wa ule mto, ulikuwapo mti wa uzima, uzaao matunda, aina kumi na mbili, wenye kutoa matunda yake kila mwezi; na majani ya mti huo ni ya kuwaponya mataifa. [3] Wala hapatakuwa na laana yo yote tena. Na kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo kitakuwamo ndani yake. Na watumwa wake watamtumikia; [4] nao watamwona uso wake, na jina lake litakuwa katika vipaji vya nyuso zao. [5] Wala hapatakuwa na usiku tena; wala hawana haja ya taa wala ya nuru ya jua; kwa kuwa Bwana Mungu huwatia nuru, nao watatawala hata milele na milele.**

**22:1 "Kisha akanionyesha mto wa maji ya uzima"** Hapa hatupaswi kuwa na mgawanyiko wa sura. Dhana ya mto utokao mbele za uso wa Mungu ni dokezo la Agano la Kale (kama vile Zab. 46: 4, Eze. 47: 1-12; Yoe. 3:18, Zek. 14: 8). Maji ni stiari ya kawaida inayomaanisha kwa Mungu kuna utele kikubwa kwa ugavi na mahitaji ya kiroho ya watu wake (kama vile Isaya 12: 3, 44: 3, 49:10, Yer. 2:13; 17:13, Yoh. 4: 10-15; Ufu. 7:17; 21: 6). Ni Yohana pekee yake aliyetumia neno uzima (*zoē)* akirejelea maisha ya ufufuo.

◙ **"Wenye kung'aa kama bilauri"** Hii inazungumzia usafi wa mji wa mbinguni la Mungu (kama vile Ufu. 4: 6).

◙ **"ukitoka katika kiti cha enzi cha Mungu, na cha Mwana-Kondoo"** Kuna Kiti cha enzi kimoja tu (kama vile Ufunuo 21:22). Hii ni lugha ya kumweleza Mungu kwa njia ya ki-binadamu itokanayo na picha za kale za mashariki ya kifalme na sura ya ki-mahakama. Mungu ni roho wa milele; Haishi juu ya kiti cha enzi cha kimwili. Ni mfano wa utawala wake mkuu.

**22:2 "Na upande huu na upande huu wa ule mto, ulikuwapo mti wa uzima"** Mti huo huo unatajwa katika Ufunuo 2: 7. Maono haya yote ni kutoka katika Eze. 47: 1-12 (hapa, Ufu. 22:12). Kuna marejeo mengi katika maandiko ya Kiyahudi ya fasihi juu ya mti wa uzima unaopatikana katika Mwanzo 2: 9; 3:22 (kama vile Inoki 25: 2, IV Esdras 7:53, 8:52, II Enoki 8: 3). Hiyo ambayo Adamu alipoteza kwayo kutoka kwa Mungu (ushirika, ujuzi, uzima wa milele), Mungu sasa anatoa kwa uhuru kuwakomboa wanadamu (kama vile Flp. 2: 6).

◙ **"uzaao matunda*, aina* kumi na mbili"** Angalia MADA MAALUMU: Hesabu Kumi na Mbili. (SPECIAL TOPIC: The Number Twelve)

◙ **"na majani ya mti huo ni ya kuwaponya mataifa"** Hiki ni kitu kisicho cha kawaida kwa sababu haipaswi kuwa na kitu chochote cha kunusuru! Hata hivyo, hii inaweza kuwa tu nukuu kutoka katika Ezek. 47:12; Labda jambo la kawaida la kitheolojia ni kwamba Mungu anataka wote ("mataifa") kuokolewa (kama vile. Isa 2: 3-4; 45: 22-25; 60: 3; 66: 18-19; Zak 2: 11; 8: 20-23).

Mada Maalum: Mpango wa Ukombozi wa Milele wa YHWH (YHWH's Eternal Redemptive Plan)

**22:3 " Wala hapatakuwa na laana yo yote tena"** Mstari huu ni dokezo kwa Mwa 3:17 na Zek. 14:11. Zama mpya imewadia na laana ya Agano la Kale (kama vile Waefeso 2: 15-16; Kol. 2:14) imeondolewa kwa kifo cha Kristo (kama vile Rum. 8: 18,25; Efe. 2: 13,16). Katika Ufunuo bahari angavu ya Ufunuo 4: 6 inaashiria utakatifu wa Mwenyezi Mungu. Wanadamu walioanguka hawakuweza kumkaribia Mungu, lakini sasa bahari imeondolewa (kama vile Ufu. 21: 1).

Inawezekana kwamba neno linamaanisha charam ya Kiebrania, yenye maana iliyoharibiwa au kabisa kuharibiwa (kama vile Zek. 14:11). Ikiwa hii ni tafsiri ya Agano Jipya, basi aya hii inahusu usalama wa Yerusalemu mpya na itakuwa sawa na ahadi za 1 Pet. 1: 4-5.

◙ Angalia mwonekano wa vipengele vya kisarufi vya kifungu hiki. Kuna kiti cha enzi kimoja, lakini viwili vikiwa juu yake (yaani, Mungu na Mwana-Kondoo). Hata hivyo, watumishi wanatumikia 'Yeye' (UMOJA). Hii inahusisha siri ya yule Mungu mmoja na lile umbo la umwili. Mungu mmoja, lakini pia Masihi wa Uungu (na ile nafsi ya Roho Mtakatifu ).

[Mada Maalum: Mungu Mmoja (Special Topic: Monotheism)]

[Mada Maalum: Utatu (Special Topic: The Trinity)]

[Mada Maalum: Utu wa Roho (Special Topic: The Personhood of the Spirit)]

**22:4 "Watauona uso wake"** Katika Agano la Kale kumuona Mungu kulimaanisha kifo. Musa hakuruhusiwa kuuona uso wa Mungu (kama vile Kut. 33:20). Kumwona Mungu au kuishi na Mungu ni zawadi kwa wale walio safi (kama vile Zab. 11: 7, 16:11, 17:15, 140: 13, Mt. 5: 8). Urafiki wa awali uliokusudiwa katika Edeni umerejeshwa kikamilifu (kama vile Zab. 42: 1-2)!

◙ **"na jina lake litakuwa katika vipaji vya nyuso zao"** Kama Shetani alivyowawekea chapa wafuasi wake (kama vile Ufu. 13 1-17; 14 9; 20 4), Mungu huwawekea chapa wale walio wake (kama vile Ufu. 3 12; 7 3; 14 1). Ilikuwa ishara ya umiliki na usalama. Angalia maelezo katika Ufu.7:2.

**22:5 "Wala hapatakuwa na usiku tena"** (kama vile Ufu. 21 23-25; Isa. 60 19-20; Zak. 14 7)

◙ **"nao watatawala hata milele na milele"** Ni nani aongozaye na Kristo wakati wa kile kipindi cha miaka elfu? Ufu. 20: 4-5 inaonyesha Wakristo pekee watakaokuwa wakiishi wakati wa kipindi kile cha mateso ya wakati wa mwisho, lakini Ufu. 2:26 na 5:10 zinaashiria kuwa watakatifu wote watatawala pamoja na Kristo duniani. Hakuna tofauti halisi katiaka Biblia baina ya utawala wa milele (kama vile Dan. 2:44, 7: 14,18; Isa 9: 7, Luka 1:33, 2 Pet 1:11, Ufu. 11:15 ) na utawala ule wa miaka elfu. Katika Taaluma ya Ufasiri wa Biblia si kuchukua mfundisho makuu kutoka katika kifungu cha mafunuo ya matukio ya siku za mwisho. Mstari huu unamaanisha ule utawala wa milele.

Ule mfano wa watu wa Mungu unaokabiliwa na mvamizi mabaya, ambaye ameangamizwa na Mungu kabisa, inachukuliwa kutoka Eze. 37-39. Yohana kamwe hakutazamia hili kutafsiriwa kuwa kweli! Huu ni utumiaji mbaya wa nia ya uandishi ya kugeuza picha za mafunuo ya matukio ya siku za mwisho katika uhalisi wa kihistoria! Upendo wetu kwa ajili ya Biblia na udadisi wetu juu ya siku zijazo umesababisha kanisa la kisasa la magharibi kufasiri unabii na maandiko yahusuyo siku za mwisho kwa njia za kushangaza na za ajabu!

[Mada maalum: Kutawala katika Ufalme wa Mungu ( Special Topic: Reigning in the Kingdom of God)]

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 22:6**
[6]**Kisha akaniambia, Maneno haya ni amini na kweli. Naye Bwana, Mungu wa roho za manabii, alimtuma malaika wake kuwaonyesha watumwa wake mambo ambayo hayana budi kuwako upesi.**

**22:6 "Akaniambia"** Hii inawarejelea kwa malaika waliokuwa na vitasa saba vya hukumu (kama vile Ufu. 21: 9; 22: 1,8,9,10).

◙ **"maneno haya ni amani na kweli"** Kifungu hiki cha maneno hutumika kuelezea
1. Yesu (kama vile Ufu. 1: 5; 3: 7,14; 19:11)2.
2. Wafuasi wa Yesu (kama vile Ufu. 17:14)
3. Neno la Mungu (kama vile Ufu. 19: 9; 21: 5; 22: 6)

Mara nyingi Mungu anaelezewa kuwa "haki na wa kweli" (kama vile Ufu. 15: 3, 16: 7, 19: 2). Nyuma ya kifungu hiki cha maneno cha Kiebrania kinamaanisha uaminifu kamili.

◙ **"Naye Bwana, Mungu wa roho za manabii"** Hili linawezekana:
1. dokezo kwa Ufu. 19:102.
2. rejeo la msukumo wa Agano la Kale (kama vile 2 Tim 3:16, 2 Pet 1: 20-21)
3. rejeo la uongozi wa Agano Jipya (kama vile 2 Pet 3: 15-16)

4. rejeo la wahubiri wa injili katika siku za Yohana
5. rejeo la kitabu cha Yohana (maono)

Maandishi ya Kiyunani ya awali hayakuwa na herufi kubwa. Mara nyingi watafsiri au wakalimani wanapaswa kuamua kama neno "roho" linarejelea kwa Roho Mtakatifu au roho wa binadamu. Andiko hili linarejelea kwa roho ya mwanadamu (kama vile 1 Kor. 14:32, Heb 12: 9).

◙ **"alimtuma malaika Wake**" Mstari huu ni dokezo kwa Ufu.1: 1. Mstari huu uliofungwa umefanana sana katika dhana yao kwa sura ya 1. Muundo wa barua bifsi ulio wa jadi uliyotumiwa katika Ufu.1, unatumiwa tena katika Ufu. 22.

◙"mambo **ambayo hayana budi kuwako upesi"** Kuna mfululizo wa vidokezo vya ukaribu wa kule kuja kwa Bwana (kama vile Ufu. 1: 1,3; 3:11, Ufu. 22: 6 [mara mbili], Ufu.22: 7, 10, 12, na 20) . Kuchelewa kwa miaka elfu mbili hadi sasa ni kugumu sana kwa waumini kuelewa (kuchelewa huku kumefunuliwa katika Wathesolanike 2), lakini ni lazima kuonekana kwamba kila kizazi cha Wakristo kina matumaini ya kuja kwa Bwana katika siku zao. Kuna mvutano halisi katika Agano Jipya kati ya wale wanaotarajia kurudi kwa Bwana kwa wakati wo wote na yale mambo mengine ambayo yanapaswa kutokea kwanza. Waumini wanapaswa kubaki kuwa waaminifu na wachangamfu!

Hapa pana nukuu fupi juu ya suala hili kutoka katika fafanuzi zangu juu ya Mathayo.

"Kuna wasiwasi ya kweli kinzani yak i-theolojia kati ya"

1. Kuna mkinzano wa kitheolojia kati kama vile Mt. 24:27,44) na ukweli kwamba matukio mengine yaliyomo katika historia lazima yatokee
2. Ufalme kama ubaadaye na Ufalme kama usasa.
3. Agano Jipya linaonyesha kuwa matukio mengine yatatokea kabla ya Ujio wa mara ya Pili.
4. Injili ihubiriwayo ulimwenguni kote (kama vile. Mt 24:14: Mk 13:10)
5. Uasi mkubwa (kama vile Mt. 24: 10-13,21, 1 Tim 4: 1, 2 Tim 3: 1, 2 The. 2: 3)
6. Ufunuo wa "mwanadamu alliye na dhambi" (kama vile. Dan 7: 23-26; 9: 24-27; 2 The. 2: 3)
7. kuondolewa kwa mtu azuiaye (kama vile 2 The. 2: 6-7)
8. Uamsho wa Wayahudi (kama vile Zek. 12:10; Rum.11) "

Wale ambao wanaamini kuwa kuna uwiano mkubwa kati ya kweli saba ya uandishi wa kitabu hiki pia husema kwamba kila moja yao huwakilisha kipindi kati ya ujio wa kwanza na wa pili wa Kristo kutokana na vipengele tofauti tofauti (m.f William Hendriksen, *More Than Conquerors*). Ikiwa hii ni kweli basi maandiko yanayotaja kuja kwa Kristo kuwa karibu (kama vile Ufu. 1: 3, 3:11; 22: 7,10,12,20) inahusu uanzishwaji wa unabii huu baada ya kifo na ufufuo Wa Kristo. Mchezo huu wa matukio yahusuyo siku za mwisho unaendelea!

**ANDIKO LA BASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 22:7**
**[7]Na tazama, naja upesi; heri yeye ayashikaye maneno ya unabii wa kitabu hiki.**

**22:7 "naja upesi"** Inaonekana dhahiri kuwa malaika anamnukuu Yesu (kama vile Ufu. 22: 12-15). Hii imenenwa na Yesu kwa upekee katika Ufu. 22:16. Hakika aongeaye katika Ufu. 22:17 na Ufu. 22: 18-19 haijulikani, lakini Yesu anasema tena katika Ufu. 22:20 na Yohana katika Ufu. 22:21.

Mada Maalum: Ujuo wa Mapema (Special Topic: Soon Return)

◙ **"Heri yeye"** Hii ni moja ya heri saba kwa waumini waliopatikana katika sehemu nzima ya kitabu hiki (kama vile Ufu. 1: 3, 14:13, 16:15, 19: 9, 20: 6, 22: 7,14).

◙ **"unabii"** Kitabu hiki ni unabii na lazima kutafsiriwa kwa mfumo wa vitabu vya unabii (kama vile Ufu. 22: 9-10, 18-19; 1: 3; 10:11). Kitabu hiki siyo simulizi za kihistoria! Unabii daima una kipengele cha masharti. Vifungu vya Agano Jipya vihusuvyo matukio ya siku za mwisho vinaonyesha utambuzi wa ndani unabii wa Agano la Kale ambao ulitazamia ule wakati wa mwisho kupitia matukio ya kisasa na miitikio ya imani. Wana taaluma wengi wanaamini kuwa aina ya mafunuo ya matukio ya siku za mwisho yalikuzwa nje ya unabii wa Kiyahudi.

Mada Maalum: Unabii (Agano la Kale) (Special Topic; Prophecy (OT)

Mada Maalum: Unabii (Agano Jipya)  (Special Topic: Prophecy (NT)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 22:8-9**
**[8] Nami Yohana ndimi niliyeyasikia na kuyaona mambo hayo. Na hapo nilipoyasikia na kuyaona nalianguka, ili nisujudu mbele ya miguu ya malaika yule mwenye kunionyesha hayo. [9]Naye akaniambia, Angalia, usifanye hivi; mimi ni mjoli wako, na wa ndugu zako manabii, na wa wale wayashikao maneno ya kitabu hiki. Msujudie Mungu.**

**22:8** Huu ni mstari usio wa kawaida. Hii ndio tatizo halisi ambalo Yohana alikuwa nalo katika Ufu.19:10. Inaonekana kwamba lazima angelifikiri kwamba malaika huyu alikuwa wa ki-Uungu.

**22:9 "na wa wale wayashikao maneno ya kitabu hiki"** Ukristo unauhusisha uamuzi wa awali wa toba, imani, na toba endelevu, imani, utii, na uvumilivu! Ufunuo, ulioandikwa kwa Wakristo walioteswa, unasisitiza uvumilivu. Jaribu la tamaduni zetu leo sio mateso ya kimwili, lakini "uozo mkavu," kutojali, kutokuwepo kwa uaminifu, kupenda mali, Ukristo usio na kina na faida zote na faida bila uwajibikaji!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 10-11**
***[10]* Akaniambia, Usiyatie muhuri maneno ya unabii wa kitabu hiki, kwa maana wakati huo umekaribia.**
***[11]* Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu; na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; na mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa.**

**22:10 "Usiyatie Muhuri"** Hii ni kinyume kabisa na Isa. 8:16; Dan. 8:26 na 12: 4,9. Wakati kamili wa unabii umefika. Maonyo ya Mungu kwa wasioamini na kutiwa moyo kwa waumini ni sasa! Uamuzi wa maamuzi unahitajika sasa! Ufalme umekuwapo.

Mada Malum: Muhuri (Special Topic: Seal)

◙ **"Wakati huo Umekaribia"** Angalia Mada Maalum: Ujio wa Mapema (Special Topic: Soon Return)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 22:12-13**
***[12]* Tazama, naja upesi, na ujira wangu u pamoja nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo.**
***[13]* Mimi ni Alfa na Omega, mwanzo na mwisho, wa kwanza na wa mwisho.**

**22:11** Mstari huu ni dokezo kwa Dan. 12:10.

**22:12 "kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo"** Hiki ni kiini kinachojirudia mara kwa mara katika sehemu zote Biblia (kama vile Ayu. 34: 11,25; Zab. 28: 4, 62:12, Mit. 12:14, 24:12, Mdo. 12:14, Yer 17:10; 32:19, Eze 33:20, Mt. 16:27, 25: 31-46, Rum. 2: 6, 14:12, 1 Kor 3: 8, 2 Kor. 5:10, Gal 6: 7-10; 2 Tim.4:14, 1 Pet 1:17, Ufu. 2:23; 20:12). Mungu atawapa thawabu wale wanaompenda na kumtegemea yeye katikati ya mfumo huu wa dunia ulioanguka

(kama vile 2:23; 20: 12-13). Maisha hufunua ukweli wa kiroho na nguvu ya imani ya ndani (kama vile mt. 7). Watu ni watumishi wa karamaya uzima na wataitoa hesabu kwa mungu!

Hii haimaanishi "kuhesabiwa haki kwa kazi." Mwanadamu amekombolewa kupitia neema ya Mungu kwa njia ya kifo cha Kristo na ufufuo na kurejeshwa kwa Roho! Hata hivyo, ule ushahidi kwamba mtu amekutana na Mungu na kubadilika na kuyabadilisha maisha kuwa yanayomfanana na Kristo! Vipaumbele vya mtu na ugawaji wa rasilimali hufunua moyo!

**22:13** Mstari huu ni dokezo kwa sifa ya Agano la Kale kwa YHWH inayopatikana katika Ufu.1: 8 na 21: 6, lakini hapa panamrejea Kristo. Kuhamishiwa kwa majina haya ya Agano la Kale kwa Yesu ilikuwa njia moja ambayo waandishi wa Agano Jipya, kwayo ilikuwa asili yake ikimwelezea yule Mungu wa milele (kama vile Isa 41: 4; 44: 6; 48:12), lakini sasa hutumiwa kwa Yesu (kama vile Ufu. 1:17; 2: 8)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 22: 14-15**
[14] **Heri wazifuao nguo zao, wawe na amri kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake.** [15] **Huko nje wako mbwa, na wachawi, na wazinzi, na wauaji, na hao waabuduo sanamu, na kila mtu apendaye uongo na kuufanya.**

**22:14 "Heri"** Hii ndiyo heri ya mwisho miongoni mwa zile heri saba kwa waumini zinazopatikana katika Ufunuo (kama vile Ufu. 1: 3, 14:13, 16:15, 19: 9, 20: 6, 22: 7,14).

◙ "**wazifuao nguo zao"** Hii ni stiari ya kuamini katika upatanisho wa Kristo (kama vile Ufu. 7:14). Waumini hukubalika kwa sababu Yeye alikubaliwa (kama vile Efe. 1: 6). Waumini wanaishi kwa sababu Yeye alikufa. Waumini wana ufufuo kwa sababu Yeye anaishi!

Kuna machapicho tofauti ya kKiyunani katika kifungu hiki cha maneno

1. "safisha nguo zao" ni katika MSS א (karne ya nne) na A (karne ya tano), pamoja na lile Toleo la Biblia ya Kilatini. UBS4 inatoa dalaja "A", maana yake ni "yumkini".
2. "yatunze maagizo" iko katika 046, MS herufi kubwa tangu karne ya kumi, MSS herufi ndogo (1 na 94) tangu karne ya kumi na mbili, na toleo ki-Shamu (lile la Kisiria).

◙ **"wawe na amri kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake"** Hizi ni stiari mbili za wokovu wa milele kupitia Kristo. Moja hurejea kwa Mwa. 2: 9; 3:22 (kama vile Ufu. 2: 7; 22: 2,14,19) na nyingine katika Ufu. 21: 2,9-22: 5.

**22:15 "Huko nje wako"** Hili ni gumu sana kutafsiri isipokuwa kama ni stiari ya ziwa la moto (kama vile Ufu. 21: 8).

◙ **"mbwa"** Hikki ni kidokezo kingine cha ajabu kwa sababu haipaswi kuwa na watu waovu walioachwa wakati huu katika kitabu. Katika kumb.23:18 neno hili linarejelea kwa makahaba wale wa kiume Wakanaani waliokuwa wamevuna sana kutokana na rutuba ya ardhi yao. Katika sehemu nyingine za agano la kale na jipya neno hili linamaanisha watu waovu (kama vile. Zab. 22: 16,20, Mt. 7: 6, na Flp. 3: 2). Hebu nimnukuu Robert H. Mounce katika hatua hii kutokana na fasihi yake juu ya kitabu cha ufunuo katika mfululizo mpya wa kimataifa:

"Mstari huu hauna nia ya kufundisha kwamba katika ile hali ya milele kila aina ya watu waovu watakuwa wanaishi nje ya jiji la mbinguni pekee. Kwa kawaida huu unauelezea wakati ujao kwa taswira ya sasa. Tofauti iko kati ya heri ya waaminifu na hatima ya waovu "(uk. 394

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 22:16**
[16] **Mimi Yesu nimemtuma malaika wangu kuwashuhudia ninyi mambo hayo katika makanisa. Mimi ndimi niliye Shina na Mzao wa Daudi, ile nyota yenye kung'aa ya asubuhi.**

**22:16 "'Mimi, Yesu, nimemtuma malaika wangu kuwashuhudia ninyi mambo hayo katika makanisa,"** Tambua kwamba neno "ninyi" liko katika UMOJA na dokezo la ya yale makanisa saba ya Ufunuo 2-3 ambayo yanafanywa maalum sana. Kitabu kinaanza na kumalizia na aina ya barua, ili hali yale maono yaliyopo katikati ni mchanganyiko wa unabii (mwisho unaotazamiwa kwa njia ya ule mwonekano wa mambo yaliyopo) na ile na yale mambo ya mafunuo ya matukio ya siku za mwisho (taswira-picha).

◙ **"malaika wangu"** Mara nyingi mtumaji ni Mungu Baba (kama vile Ufu. 22: 6, "malaika wake"). Hapa mtumaji ni Yesu ("malaika wangu").Kifungu hiki kinapatikana katika Ufu. 1: 1, lakini kitangulizi cha KIWAKILISHI tangulizi ni tatanishi.

◙ **"makanisa"**Angalia Mada Maalum: Kanisa (*Ekklesia*). ( Special Topic: Church (*Ekklesia*)

◙ **"Mimi ndimi niliye Shina na Mzao wa Daudi"** Kuna vidokezo vingi kwenye orodha ya Daudi ya kumuhusu Masihi katika Agano la Kale (kama vile. 2 Sam 7: 12-16 na Isa 11: 1,10) na katika Agano la Jipya (kama vile Mt 1: 1; 15:22; 21: 9, Rum. 1: 3; 2 Tim 2: 8 Ufu. 5: 5). Yesu ni utimilifu wa unabii wote wa Agano la Kale.

MADA MAALUM: Yesu Mnazareti (SPECIAL TOPIC: Jesus the Nazarene)

Mada Maalum: Sifa za Agano la Kale kwa Ujio wa Yule aliye Muhimu ( Special Topic: OT Titles for the Special Coming One)

◙**"ile nyota yenye kung'aa ya asubuhi"** Mstari huu nisifa ya Kimasihi (Kama vile Hesabu 24:17 au Mt 2: 2 au 2 Pet 1:19). Hii unaweza kuwa mchezo fulani kwenye Isa. 14:12 ambapo kifungu kile kile kilimjerejelea Shetani. Katika kitabu cha Ufunuo mara nyingi uovu ni kule kumuiga yule Mungu wa Utatu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 22:17**
*17* **Na Roho na Bibi-arusi wasema, Njoo! Naye asikiaye na aseme, Njoo! Naye mwenye kiu na aje; na yeye atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure.**

**22:17 "Roho na bibi arusi, "Njoo"** Ingawa kuna fafanuzi tofauti za kifungu hiki kutokana na muktadha inaonekana kwamba huu lazima uwe mwaliko wa injili kwa kila mtu anayeona haja na atakayeitikia ile neema ya Mungu katika Kristo. Huu umeendelea kuwa mtazamo wa kitabu cha Ufunuo, si tu kuhamasisha wale waliookolewa bali kuwafanya wale waliopotea waone hatia na kuwa na mwitikio wa neema ya Mungu ya bure katika Mwana Wake. Yale matumizi ya mara kwa mara ya neno "njoo" (yote yanarejelea juu ya wale waliopotea na sio ujio wa pili wa Kristo); Matumizi ya mara kwa mara ya kifungu cha maneno "na yeye"; Na habari njema za kushangaza sana kwamba hii neema inatokea bila gharama (kama vile Isaya 55) hii inapaswa kuwa faraja kwa kila mtu na mtu yeyote yampasa kuuitikia! Kwangu hili linaonekana kuwa mrejesho kwa wale waliokuwa walioishi katika siku zile za Yohana (na kila siku). Hili liinaweza kuelezea mambo yasiyo ya kawaida (uwepo wa waliopotea baada ya Siku ya Hukumu) katika Ufunuo 19-22. Kuna mirejesho kadhaa katika siku za Yohana mwenyewe, ambayo inaweza kuelezewa kwa ufanano miongoni mwa zile kweli saba za Ufunuo. Aliandika kwa kusema "watoto wake wapenzi" huko Efeso akilini (kama vile I, II, na 3 Yohana).

MADA MAALUM: Utatu (SPECIAL TOPIC: The Trinity)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : UFUNUO 22:18-19**
**18 Namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mtu ye yote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki. 19Na mtu ye yote akiondoa lo lote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule**

**mji mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki.**

**22:18-19** Mistari hii kwa uwazi ilihusiana na wasikilizaji wa kwanza wa ujumbe huu pamoja na wasomaji wote wa baadaye /wasikilizaji wa kitabu hiki. Kimaandiko hii ni desturi ya kawaida ya maandishi ya Agano la Kale kuweka maonyo makali kwa wale ambao wanaweza kujaribiwa kupoteza neno la Mungu (kama vile Kumb. 4: 2, 12:32). Hii haikuwa na maana ya kuchukuliwa ki-halisi, bali ni nguvu kubwa ya mashariki ya uharibifu wa kubadilisha ujumbe wa Mungu. Hii haimaanishi wakalimani wanaoamini au waandishi ambao wanaomba kwa bidii na kutafuta mapenzi ya Mungu, lakini kwa mujibu wa Ireneaus katika *Contra-Heresies*, 30:12, inawahusu waalimu wa uongo ambao wanaongeza, wanabadilisha, au kufuta maneno ya Maandiko, ambalo ndilo Suala la kifungu hiki. Kumbuka kwamba hatuwezi kuthibitisha mstari mmoja wa maandishi kwa ajii ya kuhimarisha mafundisho ambayo yanapingana na mafundisho mengine ya Maandiko yaliyo sahihi.

◙ **"aki. . .aki"** Hizi zote ni SENTENSI ZENYE MASHARTI DARAJA LA TATU ambazo zinadokeza tendo lenye umuhimu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 22:20**
[20] **Yeye mwenye kuyashuhudia haya asema, Naam; naja upesi. Amina; na uje, Bwana Yesu**

**22:20 "Naja upesi"** Uharaka wa mwisho, wa ujio wa Mungu katika hukumu ndizo sifa za maandiko ya Kiyahudi na ya Kikristo yahusuyo matukio ya siku za mwisho. Kiini hicho hicho kinaonekana katika Mt. 13:34-36; 24:43; 25:1-13; Luka 12:29; 1 Wathesalonike. 5:2, 4; 2 Pet. 3. Kwa mujibu wa kuchelewa kwa mwaka wa 2000 hii lazima ieleweke katika mtazamo wa kuishi, na sio mtindo wa muda. Anakuja! Tayari kwa kumwona.

Mada Maalum: Ujiowa Mapema (Special Topic: Soon Return)

◙ **"Na uje, Bwana Yesu"** Neno" Njoo 'ni Kiaramu, *Maranatha* (kama vile 1 Wakorintho 16: 22). Inawezekana kufasiri hili kwa njia kadhaa:

1. ikiwa *maranatha*, kumbe ni "Bwana Wetu amekwisha kuja"
2. *marana tha*, kumbe ni "Bwana Wetu, Njoo!"

Nambari 1 inaufaa muktadha huu. Tunajifunza kutokana na *Didach*e 10: 6 kwamba hii ilikuwa kufungwa kwa liturujia kwa huduma ya Meza ya Bwana katika siku zile za Yohana.

MADA MAALUMU: *Maranatha* (SPECIAL TOPIC: *Maranatha*)

Mada Maalum: Kristo Yesu Kama Bwana (Special Topic: Christ Jesus As Lord)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): UFUNUO 22:21**
[21] **Neema ya Bwana Yesu na iwe pamoja nanyi nyote. Amina.**

**22:21** Tambua kwamba "ile neema ya Bwana Yesu Kristo" kuwa na watu wake, ni hitimisho la ukweli unaowasilishwa kwa zama za Wakristo walioteswa na ni matumaini ya kila kizazi cha Wakristo!

## MASWALI YA MAJADILIANO

Haya ni maoni ya mwongozo kwa kujisomea, ikiwa na maana kuwa unawajibika binafsi kwa tafsiri ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mtoa maoni tu.

Maswali haya ya majadiliano yanatolewa ili kukusaidia kufikiri kupitia maswala makuu ya sehemu hii ya kitabu. Yamekusudiwa kuwa chanzo cha uchochezi wa mada, lakini siyo hakika.

1. Je, waaminio wanaenda mbinguni au mbingu ndiyo inarudi katika dunia iliyosafishwa?
2. Ni kwa namna gani Ufunuo 21:3 unahusiana na neno 'Emmanueli'?

3. Kwa nini hakuna hekalu katika Yerusalemu mpya (kama vile Ufu. 21:22)?
4. Je, ni watu gani waliotajwa katika Ufu. 21:24?
5. Ni namna gani waumini 'wanayaendeleza / kuyazingatia' maneno ya unabii huu (kama vile Ufu. 22:7)?
6. Ikiwa hii ndiyo mbingu, nani walio waovu nje ya mji katika Ufu. 22:15?
7. Kwa nini Ufu. 22:17 ni wa muhimu sana?
8. Je, kitabu cha Ufu. 22:18-19 kinapaswa kuchukuliwa kimaandiko? Je! Muumini anayekifasiri kitabu cha Ufunuo visivyo anaweza kuupoteza wokovu wake?
9. Mara Tatu katika Ufunuo 22 inasema "Naja upesi (Kama vile Ufu. 22:7,12:20 imekuwaje tangu miaka 2000?

# TAFASIRI SAHIHI ZA ISTILAHI ZA VISARUFI VYA KIYUNANI

Lugha ya kawaida ya Koine mara nyingi inafahamika kama Kiyunani kilichobobea, ilikuwa ni lugha ya kawaida ya ulimwengu wa Meditarania ilianzishwa na Alexanda mkuu (336-323 B.C) na ikadumu mpaka miaka ya (300 B.C-A.D 500). Haikuwa rahisi, Kiyunani kuwa cha daraja la juu, lakini kwa njia nyingi ni dhana ya Kiyunani ambayo ilikuja kuwa lugha ya pili karibu na mashariki ya kale na ulimwengu wa Mediterania.

Kiyunani cha Agano Jipya kilikuwa ni cha kipekee kwa njia kadhaa kwa watumiaji wake, isipokuwa Luka mwandishi wa kitabu cha Waebrania, yamkini alitumia lugha ya Kiarama kama lugha ya msingi. Kwa hiyo, uandishi wao uliathiliwa na dhana ya muundo wa Kiarama. Pia, walisoma na kunukuu wandishi wa maandiko ya kale (tafasiri ya Kiyunani ya maandiko ya kale) ambayo pia yaliandikwa kwa lugha ya Koine. Lakini maandiko ya kale pia yaliandikwa kwa wasomi wa Kiyahudi ambao lugha yao ya asili ilikuwa sio ya Kiyunani.

Hii ilisaidia kuwa kama kumbukumbu ambayo haiwezi kulipeleka Agano Jipya kwenye muundo mgumu wa kisarufi. Ni wa kipekee na bado una mambo mengi yaliyo pamoja na (1) maandiko ya kale (2) maandiko ya kale kama yale ya Yusufu na (3) mafunjo yaliyopatikana Misri. Kwa hiyo tunakabilianaje na uchambuzi wa visarufi vya Agano Jipya.

Muundo wa kisarufi wa lugha ya Koine na Agano Jipya la lugha ya Koine ulibadilika. Kwa njia tofauti ulikuwa ni urahisishaji wa sarufi. Mazingira ndio yatakuwa mwongozo wetu mkuu. Maneno pekee yana maana katika upanuzi wa mazingira, kwa hiyo, muundo wa kisarufi unaweza tu kueleweka katika mwanga wa (1) aina mahsusi ya mwandishi, na (2) mazingira mahsusi

Hapana hitimisho la fasiri ya dhana na muundo wa Kiyunani unaowezekana. Kimsingi lugha ya Koine ilikuwa ni lugha ya maneno tu. Mara nyingi msingi wa utafasiri ni aina na dhana ya maneno. Mara nyingi vishazi vikuu hutokea kwanza, vikionyesha kushinda vingine vyote. Katika kueleza kitenzi cha Kiyunani, vipande vitatu vya habari lazima vizingatiwe (1) kiini cha msisitizo wa njeo, sauti na dhamira (tukio au umbo); (2) kiini cha maana husika ya kitenzi (usawidi kamusi); na (3) mtiririko wa mazingira yenyewe (isimu ya mpangilio wa maneno)

## I. NJEO

A. NJEO au sura inajumuisha uhusiano wa VITENZI ili kukamilisha kitendo au kutokamilisha kitendo. Mara nyingi huitwa “utimilifu” au “utoutimilifu”
   1. Njeo timilifu zinaangazia juu ya utoaji wa kitendo. Hakuna taarifa nyingine zilizotolewa isipokuwa ya kile kilichotokea! Kuanza kwake, mwendelezo au ukomo wake haukueiezwa.
   2. Njeo zisizo timilifu zinaangazia juu ya mchakato endelevu wa kitendo. Zinaweza kuelezewa dhidi ya unasaba wa kitendo, kudumu kwa kitendo, mwendelezo wa kitendo, n.k.

B. Njeo zaweza kugawanywa kwa jinsi mwandishi anavyoona kitendo kinavyoendelea.
   1. Kimetokea-KITENZI TIMILIFU
   2. Kilivyotokea au matokeo yake-KITENZI CHA WAKATI ULIOPITA
   3. Kilivyokuwa kikitokea nyuma na matokeo yake yakastahimili, lakini sio sasa-KITENZI CHA WAKATI ULIOPITA TIMILIFU
   4. Kinatokea –WAKATI ULIOPO
   5. Kilikuwa kikitokea- WAKATI USIOTIMILIFU
   6. Kitatokea –WAKATI UJAO

Mfano thabiti wa jinsi njeo hizi zinasaidia katika utafasiri ungalikuwa wa neno “okoa.” Lilitumika katika NJEO nyingi tofauti kuonyesha kwa pamoja mchakato na ukomo.

1. KITENZI CHA WAKATI TIMILIFU- “okolewa” (Rum 8:24)
2. KITENZI CHA WAKATI ULIOPITA- “ameokolewa na matokeo yake yanaendelea” (Efe 2:5,8)
3. KITENZI CHA WAKATI ULIOPO- “anaokolewa” (cf. 1Kor 1:18; 15:2)
4. KITENZI CHA WAKATI UJAO- “ataokolewa” (cf. Rum 5:9,10; 10:9)

C. Katika kuzingatia juu ya VITENZI VYA NJEO, mfasiri huangalia sababu za mwandishi wa kwanza alichagua kuelezea yeye binafsi NJEO fulani. Tarajio la NJEO “hakuna madoido” lilikuwa ni la KITENZI CHA WAKATI TIMILIFU. Kilikuwa ni muundo wa KITENZI cha kawaida “kisichoainishwa” “kisichotambulika” “kisichochoka.” Chaweza tumika katika Nyanja pana ambamo mazingira lazima yaelezee. Kwa kawaida kilikuwa kinaelezea kuwa kitu fulani kimetendeka. Sura ya muda uliopita ulikusudia tu katika DHAMIRA ELEKEZI. Kama pana NJEO nyingine zilizotumika, uainishaji wa kitu fulani ulikuwa unasisitizwa. Lakini ni nini?
   1. NJEO YA WAKATI ULIOPITA. Hii inaongelea juu ya tendo lililokwisha tendeka na matokeo yakiendelea kuwepo. Katika namna fulani ilikuwa ni muunganikano wa NJEO ZA WAKATI TIMILIFU na ZA WAKATI ULIOPITA. Mara kwa mara mlengo ulikuwa juu ya matokeo yalioendelea kuwepo au kumalizika kwa kitendo. Mfano: Efe 2:5 & 8, “umekuwa na unaendelea kuokolewa.”
   2. NJEO YA WAKATI ULIOPITA AINISHI. Hii ilikuwa kama njeo ya WAKATI ULIOPITA isipokuwa matokeo yalishakoma. Mfano: “Petro alikuwa akisimama nje mlangoni” (Yoh 18:16)
   3. NJEO YA WAKATI ULIOPO. Hii inazungumzia juu ya kitendo kisichokiwisha au kisichotimilifu. Mtizamo mara nyingi ni juu ya uendelezaji wa tukio. Mfano: “kila mmoja ashikamanae ndani yake haendelei kutenda dhambi”, “kila mmoja aliyesamehewa na Mungu haendelei kutenda dhambi” (1Yoh 3:6 & 9).
   4. NJEO YA WAKATI USIOTIMILIFU. Katika njeo hii uhusiano na NJEO YA WAKATI ULIOPO ni mwendelezo wa uhusiano kati ya WAKATI ULIOPITA na WAKATI ULIOPITA AINISHI. WAKATI USIOTIMILIFU unaongea juu ya kitendo ambacho hakijaisha kutendeka ambacho kilikuwa kinatokea lakini sasa kimekoma au mwanzo wa kitendo awali. Mfano: “kwa hiyo Yerusalemu yote waliendelea kumwacha” au “ Yerusalemu yote wakaanza kumwacha”(Mt3:5)
   5. NJEO YA WAKATI UJAO. Hii inaongelea juu ya kitendo ambacho kawaida kilijitokeza ndani ya muda mwafaka. Inaangazia juu ya umuhimu wa jambo kutokea kuliko utokeaji wa uhalisia. Mara nyingi unazungumzia juu ya ualakini wa tukio. Mfano: “Heri wale….wata...”(Mt 5:4-9).

## II IRABU

A. Irabu inaelezea mahusiano kati ya kitendo cha KITENZI na KIIMA
B. IRABU TENDAJI ilikuwa ni njia ya kawaida, tarajiwa, isiosisitiza utetezi wa kwamba kiima kilikuwa kikitenda kitendo cha KITENZI.
C. IRABU TENDEWA ina maana kuwa KIIMA kilikuwa kikipokea kitendo cha KITENZI kilichotolewa na mtu wan je. Mtu wa nje anayetoa kitendo alionyeshwa katika Agano Jipya la Kiyunani kwa mambo na VIHUSISHI vifuatavyo:
   1. Mtu binafsi wa moja kwa moja wa *hupo* kukiwa na UHUSIKA WA KUONDOA (cf. Mt 1:22; Mdo 22:30)
   2. Mtu binafsi wa kati na *dia* kukiwa na UHUSIKA WA KUONDOA (cf. Mt 1:22)
   3. Mtu wa kawaida asiyehusika na *en* kukiwa na UHUSIKA WA JAMBO
   4. Wakati mwingine ni mtu binafsi au asiyehusika kukiwa na UHUSIKA WA JAMBO pekee.
D. IRABU YA KATI inamaanisha kuwa KIIMA kinatoa tendo la KITENZI na pia moja kwa moja kinahusishwa katika kitendo cha KITENZI. Mara nyingi huitwa irabu ya kurefusha matakwa binafsi. Muundo huu unasisitizia KIIMA cha kishazi au sentesi kwa namna nyingine. Muunganikano huu haupatikani katika

Kiingereza. Una uwezekano mpana wa maana na ufasiri katika Kiyunani. Baadhi ya mifano ya dhana hizi ni;

1. YENYE KUJIREJEA – kitendo cha moja kwa moja cha kiima chenyewe. Mfano: "kajiangika mwenyewe" (Mt 27:5)
2. YENYE KUTIA MKAZO- kiima kinazaa kitendo chake chenyewe. Mfano: "shetani mwenyewe anajifanya kama malaika wa nuru" ( 2Kor 11:14)
3. Kukubaliana – mwingiliano wa viima viwili. Mfano: "walishauliana wao kwa wao" (Mt 26:4)

## III. DHAMIRA (au "NAMNA")

A. Kuna namna nne za DHAMIRA katika lugha ya Koine. Zinaashiria uhusiano wa KITENZI kuwa kweli, haswa ndani ya wazo la mwandishi mwenyewe. DHAMIRA hizi zinagawanyika katika namna pana mbili: ile inayoonyesha ukweli (ELEKEZI) na ile inayoonyesha umuhimu (UTEGEMEZI, KUAMURU/KUSHURUTISHA na HALI Y A UCHAGUZI).

B. DHAMIRA ELEKEZI ilikuwa ni NAMNA ya kawaida ya kuelekeza kitendo ambacho kimekwisha tokea au kilikuwa kinatokea, haswa kwenye wazo la mwandishi. Ilikuwa namna <u>pekee</u> ya Kiyunani ya kueleza ukomo wa muda na hata hapa sura hii ilikuwa daraja la pili.

C. DHAMIRA TEGEMEZI kinaelekeza yumkini kitendo kitakachotokea mbeleni. Kitu fulani ambacho hakijawahi tokea lakini nafasi ya kutokea ingaliwezekana. Ina vitu vingi vinavyofanana na KITENZI CHA WAKATI UJAO ELEKEZI. Utofauti ni kuwa UTEGEMEZI unaelezea kiwango fulani cha mashaka. Katika Kiingereza hii mara nyingi inaelezewa na neno "ingalikuwa", "ingaliweza", "yawezekana" au "yenye uwezo".

D. DHAMIRA YA UCHAGUZI inaelezea utashi ambao kinadharia unawezekana. Ilifikiliwa ni hatua moja mbele kutoka katika ukweli kuliko HALI YA UTEGEMEZI. HALI YA UCHAGUZI inaelezea uwezekano chini ya hali fulani. HALI YA UCHAGUZI ilikuwa ni nadra katika Agano Jipya. Utumikaji wake mara nyingi kilikuwa ni kifungu maarufu cha Paulo. "yawezekana isiwe" (KJV, Mungu anakataza), kimetumika mara kumi na tano ( cf. Rum 3:4,6,31; 6:2,15; 7:7,13; 9:14; 11:1,11; 1Kor 6:15; Gal 2:17; 3:21; 6:14) mfano mwingine unapatikana katika Thes 1:38, 20:16, Mdo 8:20 na 1Thes 3:11

E. DHAMIRA SHURUTISHI inasisitizia juu ya amri ambayo iliwezekana, lakini msisitizo ulikuwa juu ya dhamira ya mnenaji. Inatetea juu ya uwezekano wa hiari na ilishurutishwa juu ya chaguzi za wengine. Kulikuwa na matumizi ya kipekee ya HALI YA KUSHURUTISHA katika maombi na hitaji la mtu wa tatu. Amri hizi zinapatikana tu katika WAKATI ULIOPO na njeo ya WAKATI TIMILIFU katika Agano Jipya.

F. Baadhi ya visarufi vinabainisha VIAMBATA kama moja aina ya NAMNA. Ni vya kawaida katika Agano Jipya la Kiyunani, mara nyingi vikielezewa kama KIVUMISHI CHA TENDO. Vinatafasiriwa kama muunganiko wa VITENZI vikuu ambavyo vinafanana. Tofauti pana iliwezekana katika utafasiri wa viambata. Ni vizuri kuzirejea tafasiri nyingi za Kiingereza. *The Bible in Twenty Six Translation* kilichochapishwa na Baker ni msaada mkubwa hapa.

G. KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI kilikuwa ni njia ya kawaida au "kisichotambulika" cha Kuingiza matokeo. Njeo nyingine, irabu au zilikuwa na ufasiri mahususi ambao mwandishi wa kwanza alihitaji kuwasilisha.

IV. Kwa mtu ambaye hayuko na uzoefu na lugha ya kiyunani, msaada wa usomaji unaofuata utatoa taarifa inayohitajika;

A. Friberg, Barbara na Timothy. Analytical Greek New Testament. Grand Rapids: Baker 1988
B. Marshall, Alfred. Interlinear Greek-English New Testament. Grand Rapids: Zondervan 1976
C. Mounce, William D. The Analytical Lexicon to the Greek New Testament. Grand Rapids: Zondervan 1993

D. Summer Ray. Essential of the New Testament Greek Nashville: Broadman 1950
E. Kitaaluma mtangamano wa kozi ya lugha ya Koine unapatikana kupitia taasisi ya Moody Bible iliyoko Chikago II

## V. NOMINO

A. Ki-isimu, NOMINO zinaainishwa kwa jambo. Jambo ni lile lililoshurutisha dhana ya NOMINO ambayo ilionyesha kuwa na uhusiano na KITENZI na sehemu nyingine ya sentesi. Katika lugha ya Koine kazi nyingi za uhusika zilionyeshwa na VIHUSISHI. Tangu dhana ya uhusika iliweza kutambua tofauti ya mahusiano mbali mbali, VIHUSISHI vilitokea kutoa utengano mzuri wa kazi hizo.
B. Uhusika wa Kiyunani uliainishwa kwa njia nane zifuatazo;
   1. UHUSIKA WA KIIMA ulitumika kwa ajili ya kutaja na kawaida kilikuwa ni kiima cha sentesi au kishazi. Pia ilitumika kwa NOMINO ARIFU na VIVUMISHI vikiunganishwa na VITENZI "kuwa" au "kufaa"
   2. UHUSIKA MILIKISHI ulitumika kwa ajili ya kuelezea na kawaida ulitoa kivumishi au thamani ya nenolililofanana nalo. Ulijibu swali, "aina gani?" mara nyingi ulielezewa na utumiaji wa KIHUSISHI cha Kiingereza "ya/za"
   3. UHUSIKA WA KUONDOA ulitumia dhana ile ile ya kushurutisha kama ya UMILIKISHI, lakini ulitumika kuelezea utenganifu. Kawaida ulidokeza utengano wa alama kwenye muda, nafasi, kiini, chanzo au degrii. Mara nyingi ulielezewa na matumizi ya KIHUSISHI cha Kiingereza "kutoka".
   4. UHUSIKA WA WAKATI ulitumika kuelezea matwaka ya mtu binafsi. Hii ingalidokeza mtizamo chanya au hasi. Mara nyingi hiki kilikuwa si kitu cha moja kwa moja. Mara nyingi ulielezewa na KIHUSISHI cha Kiingereza "ya".
   5. UHUSIKA WA MAHALI ilikuwa dhana shurutishi ya WAKATI, lakini ilielezea mahali au eneo kwenye nafasi, muda au ukomo. Mara nyingi ulielezewa na KIHUSISHI cha Kiingereza "ndani, juu, ni, kati, kwa, juu ya na mbali na"
   6. UHUSIKA WA KUTUMIKA ilikuwa ni dhana shurutishi kama uhusika wa WAKATI na MAHALI. Unaelezea namna au uhusiano. Mara nyingi ulielezewa na KIHUSISHI cha Kiingereza cha neno "kwa" au "enye"
   7. UHUSIKA WA KUSHUTUMU ulihusika kuelezea hitimisho la kitendo. Unaelwzea ukomo. Haswa utumikaji wake ulikuwa kwenye dhana ya moja kwa moja. Ulijibu maswali "kwa umbali gani" au "kwa namna gani"
   8. UHUSIKA WA KAULI ulitumika kuelezea moja kwa moja.

## VI. VIUNGO NA VIUNGANISHO

A. Kiyunani ni lugha sahihi kwa sababu ina viunganishi vingi. Viunganisho fikra ( vishazi, sentesi na aya). Ni vya kawaida kwamba utouwepo wao mara nyingi unakuzwa. Kama jambo la uhakika, viunganisho na viungo hivi vinaonyesha muelekeo wa fikra za mwandishi. Mara nyingi ni vya maana kupima ni kipi haswa anajaribu kukiwakilisha.
B. Hapa pan orodha ya baadhi ya viunganishi na viungo na maana zake (taarifa hizi zimekusanywa haswa toka kwa H.E Dana na Julius K. Mantery. A Manual Grammar of the Greek New Testament
   1. Viunganishi vya wakati
      (a) *epei, epedē,hopote, hōs, hote, hotan (*TEGEMEZI)- "lini"
      (b) *heōs- "*wakati"
      (c) *hotan, epan (*TEGEMEZI)- "kila, wakati wowote"
      (d) *heōs, achri, mechri (*Tegemezi)- "mpaka"
         a. *priv (*kitenzijina)- "kabla"

b. *hōs-* “tangu”, “lini”, “kama”.

2. Viunganishi venye mantiki
   a. Kusudi/dhumuni
      1) *hina* (TEGEMEZI) *hopōs (*TEGEMEZI) *hōs-* “ya kwamba”, “kuwa”
      2) *hōste(*KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO)- “kuwa”
      3) *pros(*KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO) au *eis* (KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO)- “kuwa”
   b. Tokeo (kuna uhusiano wa karibu kati ya kusudio la dhana ya kisarufi na tokeo)
      (1) *hōste(*ISIYO NA KIKOMO, hasa hiki ni cha kawaida)- “ili kwamba”, “hivyo”
      (2) *hiva(*TEGEMEZI)- “ya kwamba”
      (3) *ara-* “kwa kiasi hicho”
   c. Chanzo au sababu
      1) *gar(*chanzo/athari au sababu/hitimisho)- “kwa”, “kwa sababu ya”
      2) *dioti, hotiy- “*kwa sababu ya”
      3) *epei, epeidē, hōs-* “tangu”
      4) *dia(*ikiwa na SHUTUMA) na (ikiwa na KIUNGO KISICHO NA UKOMO)- “kwa sababu ya”
   d. Maamuzi
      (1) *ara, poinun, hōste-* “kwa hiyo”
      (2) *dio(*KIUNGO HITIMISHO chenye nguvu)- “kwa sababu ipi”, “kwa nini”, “kwa hiyo basi”
      (3) *oun- “*kwa hiyo basi”, “kwa kiasi hicho”, “hatimaye”, “hivyo basi”
      (4) *tinoun-* “kufuatana na”
   e. –a kinyume au tofauti
      (1) *alla(* yenye KINYUME thabiti)-“lakini”, “isipokuwa”
      (2) *de- “*lakini”, “ingawa”, “bado”, “kwa upande mwingine”
      (3) *kai- “lakini”*
      (4) *mentoi, oun- “ingawa”*
      (5) *plēn-* “hata hivyo” (haswa katika Luka)
      (6) *oun- “ingawa”*
   f. Ulinganifu
      (1) *hōs,kathōs (*ingiza vishazi linganifu)
      (2) *kata(*kwa muunganiko, *katho, kathoti, kathōsper, kathaper)*
      (3) *hasos(*katika Kiebrania)
      (4) *ē- “kuliko”*
   g. Enye mlolongo au mtiririko
      (1) *de- “*na”, “sasa”
      (2) *kai- “*na”
      (3) *tei-* “na”
      (4) *hina, oun- “*kile”
      (5) *oun- “*kasha”(katika Yohana)

3. Matumizi yenye mkazo
   a. *alla- “*kwa hakika”, “naam”, “kwa kweli”
   b. *ara- “*hakika”, agharabu”, “kweli”
   c. *gar- “*lakini kweli”, “agharabu”, “hakika”
   d. *de- “*hakika”
   e. *ean- “*hata”

f. *kai*- “hata”, “hakika”, “kweli”
g. *mentoi*- “hakika”
h. *oun*- “kweli”, “kwa hali zote”

VII.

A. SENTESI SHURUTISHI ni ile iliyo na kishazi kimoja au zaidi. Muundo huu wa kisarufi unaongeza utafasiri kwa sababu unatoa amri, sababu au chanzo kwa nini kitendo cha KITENZI kikuu kimetokea au hakikutokea. Palikuwa na aina nne za sentesi shurutishi. Zilitoka kwa zile zilizofikiriwa kuwa kweli toka kwa mtizamo wa mwandishi au kwa kusudio lake kwa lile alilokuwa na utashi nalo.
B. SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA ilielezea kitendo au kile kilichofikiliwa kuwa kweli toka kwa mtimamo wa mwandishi au kusudio lake. Ingawa ilielezewa kwa neno “kama.” Katika mazingira tofauti lingeweza kutafasiriwa “tangu”(cf. Mt 4:3, Rum 8:31). Ingawa hii haimaanishi kudokeza kuwa MADARAJA YA KWANZA yote ni ya kweli. Mara nyingi yalitumika kuweka alama kwenye hoja au kuangazia kosa(cf. Mt 12:27)
C. SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA PILI mara nyingi huitwa “inayopingana na ukweli”. Inaelezea kitu ambacho kilikuwa ni cha uongo kwenye ukweli wa kufanya jambo. Mfano:
   1. “kama kweli alikuwa nabii, ambapo sio, alikuwa sasa nani na mwanamke wa tabia gani anaye mng’ang’ania yeye, lakini hawezi (Thess 7:39)
   2. Kama kweli Musa, lakini hamkumwamini, mngaliniamini na mimi lakini hamkuniamini (Yoh 5:46)
   3. Kama ningalitaka kuwapendezesha wanadamu lakini sivyo, nisingalikuwa mtumwa wa Christo hata sasa(Gal 1:10)
D. DARAJA LA TATU linaongelea juu ya tukio lijalo ambalo laweza kutokea. Mara nyingi unafikirika uwezekanao wa kitendo kutokea. Kawaida inaashiria tahadhari. Kitendo cha KITENZI kikuu ni tahadhari juu ya tendo la kishazi “hiki”. Mfano toka 1Yoh 1:6-10; 2:4,6,9,15,20,21,24,29; 4:20; 5:14,16
E. DARAJA LA NNE ni daraja la mbali lililoondolewa kwenye uhakika. Ni adimu katika Agano Jipya. Kama jambo la kweli, hakuna SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA NNE lililokamilika ambamo pande zote za jambo zinastahili maelezo. Mfano wa DARAJA LA NNE ni ufunguzi wa kishazi katika 1Pet 3:14. Mfano wa sehemu DARAJA LA NNE ni katika kuhitimisha kishazi katika Mdo 8:31.

## VIII. VIZUIZI

A. KITENZI CHA KUAMURU CHA WAKATI ULIOPO kikiwa na KIAMBATA MĒ mara nyingi (lakini hakitengwi) kina msisitizo wa kusimamisha tendo ambalo liko kwenye mchakato. Baadhi ya mifano: “msijiwekee hazina yenu duniani…………”(Mt 6:19); “msisumbukie maisha yenu……….” ( Mt 6:25); “wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi…….”(Rum 6:13); “wala msimhuzunishe Yule Roho Mtakatifu wa Mungu (Efe 4:30) na “tena msilewe kwa mvinyo…………………”(Ef 5:18)
B. KITENZI TEGEMEZI TIMILIFU kina mkazo wa “udhahanifu au mwanzo wa kutenda kitendo” baadhi ya mifano: “msidhani ya kuwa……..”(Mt 5:17); “msisumbuke………”(Mt 6:31); “msiuonee haya………..”(2Tim 1:8)
C. KITENZI HASI CHENYE JOZI kikiwa na DHAMIRA TEGEMEZI ni chenye msisitizo hasi. “kamwe, katu” au “kwa hali yeyote ile”. Baadhi ya mifano: “kamwe, hataonja mauti………”(Yoh 8:51); “hakika, kamwe………..”(1Kor 8:13)

XI

A. Katika lugha ya Koine, KIBAINISHI CHA WAZI cha neno “wale, Yule,ile” kina matumizi mfanano na kwenye Kiingereza. Kazi yake kuu ilikuwa ni ya “muonyeshwaji”, ni njia ya kukamata hisia ya neno, jina au kirai. Utumiaji unatofautiana kati ya mwandishi na mwandishi kwenye Agano Jipya. KIBAINISHI CHA WAZI pia chaweza kutenda
   1. Kama chombo cha kutofautisha mfano cha kuonyesha
   2. Kama alama ya kurejea KIIMA kilichowekwa awali au mtu
   3. Kama njia ya kutambua kiima kwenye sentesi kikiwa na KITENZI kinchounganisha. Mfano: “Mungu ni Roho” Yoh 4:24, “Mungu ni nuru” 1Yoh 1:5; “Mungu ni upendo” 4:8,16

B. Lugha ya Koine haina KIBAINISHI KISICHO CHA WAZI kama ilivyo kwenye Kiingereza cha neno “a” herufi ya kwanza ya alfabeti au “an” mbadala wa “a” kwenye irabu zinazoanza na herufi kama “e”, “h”. Kutokuwepo na KIBAINISHI CHA WAZI chaweza kumaanisha;
   1. Mlengo juu ya tabia au thamani ya kitu
   2. Mlengo juu ya aina ya kitu

C. Waandishi wa Agano Jipya walitofautiana sana kwa jinsi KIBAINISHI kilivyotumiwa.

## X NJIA ZA KUONYESHA MKAZO KWENYE AGANO JIPYA LA KIYUNANI

A. Mbinu za kuonyesha msisitizo zinatofautiana toka kwa mwandishi mmoja hadi mwingine kwenye Agano Jipya. Waandishi waendelezaji na warasimishaji walikuwa ni Luka na mwandishi wa Waebrania.

B. Mwanzo kabisa tumesema ya kuwa KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI kilikuwa ni kipimo na kisichoangaliwa kwenye msisitizo, lakini njeo nyingine, irabu au dhamira zina umuhimu wa ufasiri. Hii sio kumaanisha kuwa KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI mara nyingi hakikutumika kwenye umakinishaji wa kisarufi. Mfano: Rum 6:10 (mara mbili)

C. Upangiliaji wa neno kwenye lugha ya Koine.
   1. Lugha ya Koine ilikuwa ni lugha ngumu isiyo tegemezi, kama vile Kiingereza, kwenye mpangilio wa maneno. Kwa hiyo mwandishi angaliweza kutofautiana kwenye mpangilio wa kawaida aliotegemea kuonyesha.
      a. Kile mwandishi alihitaji kusisitiza kwa viongozi
      b. Kile mwandishi angalikishangaza kwa viongozi
      c. Kile mwandishi alichosikia toka ndani
   2. Mpangilio wa kawaida wa neno kwenye Kiyunani bado ni jambo ambalo halijatulia ingawa mpangilio wa kawaida unaokusudiwa ni
      a. Kiunganishi cha VITENZI/Vitenzi unganishi
         (1) KITENZI
         (2) KIIMA
         (3) SIFA
      b. VITENZI elekezi
         (1) KITENZI
         (2) KIIMA
         (3) KISHAMILISHI
         (4) KISHAMILISHI KISICHO DHAHIRI
         (5) KIRAI HUSISHI
      c. Virai vya NOMINO
         (1) NOMINO
         (2) KIVUMISHI

(3) KIRAI HUSISHI

3. Mpanglio wa neno waweza kuwa muhimu mno kwenye upangiliaji wake. Mfano:
   a. “walinipa mimi na Barnaba mkono wa kuume wa shirika” (Gal 2:9) kirai “mkono wa kuume wa shirika” imegawanyika na kuwekwa mbele kuonyesha umuhimu wake.
   b. Pamoja na Kristo (Gal 2:20), iliwekwa kwanza kifo chake kilikuwa kiini.
   c. “ni sehemu nyingi na kwa njia nyingi” (Ebr 1:1), iliwekwa kwanza. Ilikuwa ni kwa namna Mungu alivyojidhihilisha mwenyewe kwa tofauti na sio ukweli wa mafunuo.

D. Kawaida kwa kiasi fulani cha degrii ya msisitizo ulionyeshwa na
1. Urudiaji wa KIWAKILISHI ambacho tayari kilikuwepo katika KITENZI kilichonyambulika. Mfano: “mimi mwenyewe, hakika nitakuwa nawe…….”(Mt 28:20)
2. Ukosekanaji wa KIUNGO tarajiwa, au kitu kingine cha kuunganisha maneno, virai, vishazi au sentesi. Hii inaitwa (isiofungamana). Kitu unganishi kilikuwa ni
   a. Ibada ya kubarikiwa kwa Kristo, Mt 5:3 ff(ikisisitizia orodha)
   b. Yohana 14:1 (maada mpya)
   c. Rumi 9:1 (kifungu kipya)
   d. 2Kor 12:20 ( inasisitizia orodha)
3. Urudiaji wa maneno au virai vilivyomo katika mazingira tajwa. Mfano: “usifiwe utukufu wa neema yake” (Efe 1:6, 12 & 14). Kirai hiki kilitumika kuonyesha kazi ya kila mtu wa utatu.
4. Utumiaji wa nahau au neno (sauti) unakaa kati ya istilahi.
   a. Tasifida- maneno mbadala kwa viima vyenye miiko kama “lala” kwa kifo (Yoh 11:11-14) au “nyayo” kwa viungo vya uzazi vya kiume (Ruth 3:7-8; 1Sam 24:3)
   b. Maneno ya kuzunguka- mbadala wa maneno kwa jina la Mungu, kama “ufalme wa mbingu” (Mt 3:21) au “sauti toka mbinguni” (Mt 3:17)
   c. Maumbo ya hotuba
      (1) Kutowezekana kuyakuza (Mt 3:9; 5:29-30; 19:24)
      (2) Upole wa maelezo (Mt 3:5; Mdo 2:36)
      (3) Mfano halisi wa (1Kor 15:55)
      (4) Kejeli (Gal 5:12)
      (5) Dondoo za kishairi (Flp 2:6-11)
      (6) Mvumo unaokaa kati ya maneno
         (a) “kanisa”
            i. “kanisa” (Efe 3:21)
            ii. “Kuitwa” (Efe 4:1,4)
            iii. “Kuitwa” (Efe 4:1,4)
         (b) “huru “
            i. “Mwanamke huru” (Gal 4:31)
            ii. “uhuru” (Gal 5:1)
            iii. “huru” (Gal 5:1)
   d. Lugha ya kinahau- ni lugha ambayo mara nyingi ni ya kitamaduni na lugha bayana
      (1) Hii ilikuwa ni matumizi ya kistiari ya neno “chakula” (Yoh 4:31-34)
      (2) Hii ilikuwa ni matumizi ya kiistiari ya neno “hekalu” (Yoh 2:19; Mt 26:61)
      (3) Hii ilikuwa ni nahau ya Kiebrania ya kuonyesha huruma, ya neno “chukia” (Mwa. 29:31; Kumb.21:15; Thess 14:36; Yoh 12:25; Rum 9:13)
      (4) “wote” dhidi ya “wengi”. Linganisha Isa. 53:6 (“wote”) na 53:11 & 12 (“wengi”). Istilahi hizi zina maneno sawa kama Rum 5:18 na 19 kama inavyoonyesha.

5. Utumiaji wa kifungu cha isimu moja kwa moja badala ya neno moja. Mfano: “Bwana Yesu Kristo”.
6. Utumiaji maalumu wa neno *autos*
    a. Wakati likiwa na KIFUNGU (nafasi ya kivumishi angama) kilichofasiliwa “sawa”
    b. Wakati bila KIFUNGU (nafasi ya kuarifu) kilitafasiliwa kama KIWAKILISHI CHENYE MKAZO CHA KUJIREJEA- “mwenyewe jinsia ya ME” “mwenyewe jinsia ya KE” au “yenyewe/chenyewe”

E. Wanafunzi wa Biblia wasio weza soma Kiyunani waweza kutambua mkazo katika Nyanja tofauti:
1. Utumiaji wa misamiati ya kichambuzi na andiko nasaba la Kiyunani/ Kiingereza.
2. Mlinganyo wa fasili za Kiingereza, hasa toka kwa nadharia za fasiri zinazotofautiana. Mfano: ufasiri mlinganyo wa “neno kwa neno” (KJV, NKJV, ASV, NASB, RSV, NRSV) na “mfanano wa karibu” (William, NIV, NEB, REB, JB, NJB, TEV)
   Msaada mzuri hapa ungalikuwa ni ule toka *The Bible in Twenty-Six Translation* kilichochapishwa na Baker.
3. Utumiaji wa *The Ephasized Bible* cha Joseph Bryant Rotherham (Kregel, 1994).
4. Utumiaji wa tafasiri yenyewe.
    a. *The American Standard Version* ya mwaka 1901
    b. Young’s Lateral Translation of the Bible cha Robert Young (Guardian Press, 1976)

Usomaji wa kisarufi unachosha lakini unafaa kwa ufasiri mzuri. Maelezo hasa sahihi, maoni na mifano inahamasisha na kuwaamusha watu wasiojua Kiyunani kutumia mihitasari ya kisarufi iliyotumiwa kwenye juzuu hii. Hakika maana hizi zimerahisishwa zaidi. Zisingaliweza kutumika katika hali madhubuti nay a kulazimisha, lakini kama ngazi ya kupandia kwenda kwenye uelewa mkubwa wa isimu za Agano Jipya. Kimatumaini maana hizi zitawawezesha wasomaji kuelewa maoni ya msaada mwingine wa usomaji kama vile maoni ya kiufundi juu ya Agano Jipya.

Ni lazima tuweze kuthibitisha ufasiri wetu uliolenga kwenye habari iliyopatikana kwenye maandishi ya Biblia. Sarufi ni moja ya msaada mkubwa wa vipengere hivi, vipengere vingine vingalijumuisha muundo wa kihistoria, maandishi ya kifasihi, utumiaji wa neno la wakati ule ule na dondoo zinazorandana.

# Uhakiki wa Tofauti za Kiuandishi

Somo hili litajikita kwa namna moja kutoa maelezo yanayopatikana katika maoni haya.
Mhutasari ufuatao utahusika

I. Vyanzo vya maelezo ya Biblia zetu za Kiingereza
   A. Agano la Kale
   B. Agano Jipya
II. Maelezo mafupi ya matatizo na nadharia ya "maoni dhaifu" pia yanaitwa "uhakiki wa maandiko"
III. Vyanzo vilivyopendekezwa kwa ajili ya usomaji wa badaye

I. Vyanzo vya maandiko ya Biblia yetu ya Kiingereza

A. Agano la Kale
1. Machapisho ya kale ya Kiebrania ya karne ya kumi na tisa (MT)-maandiko ya konsonanti za Kiebrania yalipangwa na Rabbi Aquiba miaka 100 Baada ya Kristo. Nukta za irabu na lafudhinukuu za pembeni, vituo vya uandishi na alama za nukta zilizoongezwa katika karne ya sita Baada ya Kristo na vilihitimishwa katika karne ya tisa Baada ya Kristo. Yalifanywa na familia ya wasomi wa Kiyahudi wajulikanao kama Wana-maandiko ya Kale ya Kiebrania. Muundo wa maandiko walioutumia ulikuwa sawa na ule katika Mishnah, Talmud, Targums, Peshitta, na Vulgate.
2. Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale la Kiebrania (LXX) –Utamaduni unasema Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale la Kiebrania ilitengenezwa na wasomi wa Kiyahudi 70 katika siku 70 katika maktaba ya Alexandria chini ya ufadhili wa Mfalme Ptolemy wa II (285-246 K.K). Tafsiri ilidhaniwa kuwa matakwa ya kiongozi wa Kiyahudi aliyeishi katika Alexandria. Utamaduni huu unatokana na "Herufi Aristeas." Mara kwa mara Tafsiri ya Agano Kale(LXX) ilijikita katika kutofautiana kwa utamaduni wa maandishi ya Kiebrania kutoka katika maandishi ya Rabbi Aquiba (MT).
3. Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (MBC)-Michoro ya Bahari ya Chumvi -iliandikwa huko Ruma kipindi cha K.K(200 Kabla ya Kristo hadi Baada ya Kristo 70) na madhehebu ya Kiyahudi waliojitenga waitwao " Esene". Machapisho ya Kiebrania, yalikutwa katika sehemu nyingi kandokando ya Bahari ya Chumvi yakionyesha baadhi ya zile tofauti za machapisho ya familia za Kiebrania nyuma ya Machapisho ya Kale ya Kiebrania (MKK)na Tafsiri za Kale za Kiebrania (70).
4. Baadhi ya mifano ya mahususi ni kwa namna gani ulinganifu wa maandishi haya imewasaidia wakalimani kulielewa Agano la Kale.
   a. Tafsiri za Kale za Kiebrania zimewasaidia watafsiri na wasomi kuyaelewa maandishi ya Kale ya Kiebrania.
      (1) Tafsiri za Kale za Kiebrania za Isa. 52:14, "Kama vile wengi watakavyo shangazwa <u>Naye</u>."
      (2) Maandishi ya Kale ya Kiebrania ya Isa. 52:14, "Bado kama vile wengi walivyo staajabishwa <u>Nawe</u>."
      (3) Katika Isa. 52:15 tofauti ya kiwakilishi cha Tafsiri za Kale za Kiebrania imehakikishwa
         (a) Tafsiri za Kale za Kiebrania, "hivyo mataifa mengi yatashangazwa naye"
         (b) Maandishi ya Kale ya Kiebrania, "hivyo yeye ameyatapakaza mataifa mengi"
   b. Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (DSS) yamewasaidia watafsiri na wasomi kuyaelewa Maandishi ya Kale ya Kiebrania
      (1) Mafunjo ya Bahari ya Chumvi ya Isa. 21:8, "ndipo akalia Karibu na mlinzi wa mnara nilipo simama."
      (2) Maandishi ya Kale ya Kiebrania (MT) ya Isa. 21:8, "ndipo akalia kama simba, Ee Bwana, mimi nasimama daima juu ya mnara wakati wa mchana……"
   c. Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (DSS) zote zilisaidia kuichuja Isa. 53:11
      (1) Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na Mafunjo ya Bahari Chumvi (DSS), "Baada ya kutaabika sana, mtumishi wangu atafurahi. Kwa kuwajibika kwake kikimilifu, atatosheka na matokeo hayo.''

(2) Maandishi ya Kale ya Kale ya Kiebrania (MT), "Ataona —ya taabu ya nafsi yake, na kuridhika. Kwa maarifa yake mtumishi wangu mwenye haki Atawafanya wengi kuwa wenye haki."

B. Agano Jipya

1. Maandishi yapatayo 5,300 yote au sehemu za Agano Jipya la Kiyunani yapo hadi leo. Yapatayo 85 yameandikwa katika karatasi za mafunjo na 268 ni maandishi yaliyoandikwa yote kwa herufi kubwa (maandiko adimu) Baadaye, mnamo karne ya tisa B.K., maandishi yaliyo somwa (madogo sana) yalikuzwa. Maandishi ya Kiyunani yaliandikwa kutoka namba zipatazo 2,700. Pia tunazo nakala zipatazo 2,100 za orodha ya Machapisho ya maandiko Matakatifu yalitumika katika kuabudu ambayo tunaiita misale ya waumini.
2. Machapisho ya Kiyunani yapatayo 85 yaliyokuwa na sehemu za Agano Jipya zilizoandikwa katika karatasi za mafunjo yamejengewa katika makumbusho. Baadhi yao yamewekwa katika kipindi maalumu kutoka karne ya pili A.D., yaliyo mengi ni kuanzia karne za tatu na nne A.D. Hakuna kati ya machapisho ya kale. Hizi zilizo na Agano Jipya Kamili. Hii ni kwa sababu hizi ni nakala za kale za Agano Jipya hazimaanishi kuwa sio ya kujiendesha yenyewe zina tofauti chache. Zilizo nyingizilinukuliwa kwa kasi kwa matumizi ya kawaida. Utunzaji haukuzingatiwa katika utendaji. Hivyo, zina utofauti mwingi.
3. Kitabu cha miswada ya kale chenye maandishi ya Kale ya Kiyunani ya karne ya nne B.K. kinachojulikana kwa herufi ya Kiebrania א (*aleph*) au (01), iliyokutwa katika nyumba ya Mt. Katarina juu ya Mlima Sinai na Tischendorf. Tarehe yake imeandikwa kuanzia karne ya nne B.K. iliyokuwa na zote Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na za Agano Jipya la Kiyunani. Ni aina ya"Maandishi ya Kialekzandria."
4. Kitabu cha miswada ya Kale cha Alexandrianus, kijulikanacho kama "A" au (02), machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano ambayo ilipatikana katika Alexandria, Misri.
5. Kitabu cha miswada ya Kale cha Machapisho ya Kiyunani cha karne ya nne, kijulikanacho kama "B" au (03), iliyopatika katika maktaba ya Vatikani katika Roma na imeandikiwa tarehe kuanzia katikati ya karne ya nne B.K. Ina zote Tafsiri za Kale za Kiebrania za Agano la Kale na Agano Jipya la Kiyunani. Yalikuwa aina ya "Maandishi ya Kialekzandria."
6. Kitabu cha miswada ya kale cha Ephraemi, kijulikanacho kama "C" au (02), machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano ambayokwa makusudi yaliaribiwa.
7. Kitabu cha miswada ya Kale cha Bazae, kijulikanacho kama "D" au (05), machapisho ya Kiyunani ya karne ya karnre ya tano au sita. Ni mwakilishi mkuu wa kile kinachojulikana kama "Maandishi ya Magharibi." Ina maongezeko mengi ulikuwa ushahidi mkuu wa tafsiri ya Mfalme James.
8. Agano Jipya la machapisho ya kale yanaweza kuwekwa katika makundi matatu, kadria nne, familia ambazo zimeshiriki sifa fulani.
   a. Maandishi ya Kialekzandria kutoka Misri
      (1) $P^{75}$,$P^{76}$ ( yapata 200 B. K.), ambayo inachukua kumbukumbu ya Injili.
      (2) $P^{46}$ (yapata 225 B. K.), ambayo ilichukua kumbukumbu ya barua za Paulo
      (3) $P^{72}$(yapata 225-250 B. K.), ambayo ilichukua kumbukumbu ya Petro na Yuda
      (4) Kitabu cha miswada ya Kale B, kiitwacho Viticanus (mnamo 325 B. K), ambacho kimebeba Agano la Kale zima na Agano Jipya
      (5) Origen alinukuu kutoka aina hii ya maandiko
      (6) Machapisho ya kale mengine ambayo yanaonyesha aina hii ya maandishi ni א,C, L, W, 33
   b. Maandishi ya Magharibi kutoka Afrika ya Kaskazini
      (1) alinukuu kutoka wakuu wa kanisa wa Afrika ya Kaskazini, Tertullian, Cyprian, na tafsiri za Kale za Kilatini
      (2) yalinukuliwa kutoka Irenaeus
      (3) ilinukuliwa kutoka Kilatini na tafsri za kale za Kisiria
      (4) Andiko D la Machapisho ya kale "Bezae" ilifuata aina ya maandishi haya
   c. Byzantine Mashariki kutoka Constantinople
      (1) aina ya maandishi inaakisiwa katika 80% ya 5,300 MSS

(2) ilinukuliwa na kanisa la mapadre wa Antiokia ya Silia, Cappadoceans, Chrisostom, natherodoret
(3) Andiko A la machapisho ya kale, katika Injili tu
(4) Andiko E la machapisho ya kale, (karne ya nane) ya Agano Jipya

d. aina ya nne iwezekanayo ni ya "Kikaizari" kutoka Palestina
(1) kwanza inaonekana katika Mrko tu
(2) baadhi ya shuhuda zake ni $P^{45}$ na W

II. Matatizo na nadharia ya "ukosoaji dhaifu."

A. Ni kwa namna gani tofauti zilitokea

1. isio angalifu au bila kukusudia (matukio mengi mno)
   a. makosa madogo madogo ya macho katika kunakili kwa mkono ambapo ulisomwa mfano wa pili wa maneno yanayofanana na pale ambapo yanaondoa maneno yote katikati (mfanano wa maneno)
      (1) makosa madogo madogo ya macho katika kuondoa maneno ya herufi jozi au vifungu (urudiaji wa maneno)
      (2) makosa madogo madogo ya kumbukumbu katika kurudia kifungu au msitari wa maandishi ya Kiyunani (mshabaha ule ule)
   b. makosa madogo madogo ya masikio katika kunakili maneno ya imla ambapo makosa ya kiuandishi hutokea (itacism). Mara nyingi makosa ya kiuandishi hudokeza au kutaja herufizenye mfananowa sauti za maneno ya Kiyunani.
   c. maandishi ya Kiyunani ya kale hayakuwa na sura au mgawanyo wa mistari, chache au alama za uandishi na hakuna mgawanyo kati ya maneno. Inawezekana kuzigawa herufi katika nafasi kuunda maneno tofauti.
2. makusudi
   a. mabadiliko yalifanywa ili kufanikisha muundo wa kisarufi wa maandishi yaliyo nakiliwa
   b. mabadiliko yalifanywa ili kuyaleta maandiko katika ulinganifu na maandiko mengine ya kibiblia (mlinganyosambamba)
   c. mabadiliko yalifanywa kwa kuuunganisha masomo mawili au zaidi yaliyokuwa tofauti katika muungano mmoja wa maandishi marefu (conflation)
   d. mabadiliko yalifanywa kusahihisha makosa yaliyotambuliwa katika maandishi ( cf. I Kor. 11-27 na I Yohana 5:7-8)
   e. baadhi ya taarifa za nyongeza kama mpangilio wa kihistoria au ufafanuzi sahihi wa maandishi uliwekwa pembezoni kwa nakala moja lakini zilihamishiwa katika maandishi kwa kuzinakili mara ya pili ( Yohana 5:4)

B. Mafundisho muhumu ya ukosoaji wa maandiko (mwongozo wa kimantiki ili kubainisha usomaji halisi wa maandishi wakati tofauti inapojitokeza)

1. maandishi ambayo hayakuwa na ustadi zaidi au ambayo hayakuwa muhimu kisarufi yamkini ni halisi
2. maandishi mafupi zaidi yamkini ni halisi
3. maandishi ya kale yamepewa uzito zaidi kwa sababu ya ukaribu wake kihistoria katika uhalisia, kila kitu kuwa sawa zaidi
4. Machapisho ya kale ni namna mbali mbali ya kijiografia mara nyingi yana usomaji halisi
5. Kimafundisho maandishi ya wanyonge, hasa yale yanayohusiana na majadiliano makuu ya kitheolojia ya kipindi cha mabadiliko ya machapisho kama Utatu katika Yohana 5:7-8, yanapaswa kupendelewa.
6. maandishi ambayo yanaweza kuelezea zaidiasili ya tofauti zingine
7. nukuu mbili ambazozinzsaidia kuonyesha usawa katika tofauti zinazotaabisha
   *a.* kitabu cha J. Harold Greenless, *Inroduction to New Testament Textual Criticism*, "Hakuna mafundisho ya Kikristo yanayoning'inia juu ya maandishi yenye kujadiliwa; na mwanafunzi wa

Agano wa Jipya anapaswa kuyatambua maandiko yake anayoyataka kuwa mwenye imani zaidi au kuwa mwenye nguvu kimafundisho kuliko msukumo asilia" (uk. 68).

*b.* W. A. Criswell alimwambia Greg Garrison ya *The Birmingham News ambayo yeye* ( Criswell) haamini kila neno katika Biblia ni la kutia moyo "angalau si kila neno ambalo limekwisha kutolewa kwa alaiki ya kisasa kwa karne za watafsiri." Criswell alisema "Mimi ni mwamini sana katika ukosoaji wa maandishi. Kama vile, Nafikiri, nusu ya sura ya 16 ya Marko ni uasi: haitii moyo, imebuniwa…Unapolinganisha machapisho hayo kwa kurudi huko nyuma, hakukuwa na kitu kama hicho kama lilehitimisho la Kitabu cha Marko. Mtu fulani alikiongeza…" Mababa wa uzao wa SBC wasio wakosaji walidai kuwa "kutia maneno yasiokuwepo katika kitabu" pia ni dhahiri katika Yohana, uwajibikaji wa Yesu katika bwawa la Bethesda. Na alijadili tofauti mbili za uwajibikaji wa kujinyonga kwa Yuda ( Mt. 27 na Matendo 1): "Ni maoni tofauti ya kujinyonga," Criswell alisema "Kama iko katika Biblia, kuna maelezo yake. Na hatia mbili za kujinyonga kwa Yuda ziko katika Biblia."Criswell aliongeza, "Ukosoaji wa Maandishi nisayansi ya ajabu ndani yake yenyewe. Si ya muda mfupi kupita, si isiyo husiana.Ni yenye nguvu na kuu…"

III. Matatizo ya machapisho (ukosoaji wa maandishi)

A. Vyanzo vilivyopendekezwa kwa ajili ya kusoma zaidi

1. *Biblical Critcism, Historical, Literary and Textual*, na R. H. Harrison
2. *The Textual of the New Testmemt: Its Transmission, Corruption and Restoration*, na Bruce M. Metzger
3. *Introduction to New Testament Txtual Critism*, na J. H Greenlee

# FAHARASA

**Uasilishaji.** Hili ni moja kati ya maoni ya kale ya uhusiano wa Yesu na Uungu. Kimsingi inadai kwamba Yesu alikuwa mwanadamu wa kawaida kwa kila namna na alichukuliwa na Mungu kwa kazi maalumu katika ubatizo wake (Mt. 3:17; Marko 1:11) au katika ufufuo Wake (cf. Rum.1:4).Yesu aliyaishi maisha haya kama mfano ambao Mungu, kwa kiasi chake, (ubatizo, ufufuo) uliyomuasilisha Yeye kama "mwana" Wake (Rum.1:4 Flp. 2:9). Hili lilikuwa kanisa la mwanzo na maoni ya watu wa karne ya nane. Badala ya Mungu kuwa mwanadamu (umbo la kibinadamu) akalirejeresha hili na sasa mwanadamu anakuwa Mungu!
Ni vigumu kusema namna gani Yesu, Mungu Mwana, Uungu uliokuwepo kabla alivyozawadiwa au kuwa mbadala kwa ajili ya maisha yenye mfano. Kama Yeye alikuwa tayari ni Mungu, ni kwa namna gani Yeye alitolewa kama zadiwa? Kama Yeye alikuwa na utukufu wa Kiungu wa awali ni kwa namna gani Yeye angeliheshimiwa zaidi? Ingawa ni vigumu kwetu sisi kutambua, kwa namna Baba alivyomuheshimu Yesu katika dhana maalumu ya ukamilifu Wake wa kuyatimiza mapenzi ya Baba.

**Shule ya Alexandria.**Njia hii ya ukalimani wa kibiblia ilikuzwa katika Alexandria, Misri katika karne ya pili B.K. Inatumia misingi ya kanuni za ukalimani ya Philo, ambaye alikuwa mfuasi wa Pilato, mara nyingi inaitwa njia ya kiistiari. Ilitawaliwa katika kanisa hadi wakati wa Marekebisho. Watetezi wake zaidi walikuwa Origen na Augustine. Tazama Moisea Silva, *Has The church Misred The Bible?* (Academic, 1987)

**Ufuasi wa Alexandria.**Haya ni machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano kutoka mji wa Alexandria, Misri ikijumuisha Agano la Kale, lililothibitishwa, pamoja na Agano Jipya. Ni moja ya ushahidi wetu mkubwa katika Agano Jipya zima la Kiyunani (isipokuwa sehemu za kitabu cha Mathayo, Yohana, na II Wakorintho). Wakati ambapo machapisho haya, ambayo yanapewa alama "A, na machapisho ya alama "B" (ya Vatican) yanaafiki juu ya usomaji unaofikiriwa kuwa ya mwanzo na baadhi ya wasomi.

**Istiari.** Hii ni aina ya ukalimani wa kibiblia ambayo kiasili ulianzishwa ndani ya dini ya Kiyahudi huko Alexandria. Ilienezwa na Philo wa Alexandria. Msukumo wake wa msingi ni shauku ya kufanya uhusiano wa Maandiko na utamaduni wa mtu au mfumo wa kifalsafa kwa mpangilio wa historia ya Biblia na/ au muktadha wa maandishi. Inatafuta uficho au kweli ya kiroho nyuma ya kila kifungu cha maandiko. Inapaswa kukubaliwa kwamba Yesu, katika Mathayo 13, na Paulo, katika Wagalatia 4, alitumia istiari kuiwasilisha kweli. Kwa hali yoyote, hii, ilikua katika muundo wa taipolojia (uanishi), na si istiari halisi.

**Uchanganuzi wa misamiati.** Hii ni aina ya chombo cha utafiti ambacho kinamruhusu mtu kutambua kila muundo wa Kiyunani katika Agano Jipya. Ni mkusanyiko, katika mpangilio wa alfabeti za Kiyunani, wa kimuundo na maelezo ya msingi. Katika muunganiko kwa tafsiri mbalimbali, unaruhusu usomaji wa wasio Wayunani kuchambua visarufi vya Agano la Kale la Kiyunani kimsamiati na kimuundo.

**Ushabihiano wa Maandiko.** Hiki ni kifungu kinachotumika kueleza wazo kwamba Biblia nzima imefunuliwa na Mungu, na ni, kwa hiyo sio mkanganyiko bali ukamilifu. Ukubalifu wa dhanio hili ni msingi kwa matumizi yanayo fanana na vifungu vya maneno katika kufasiri maandiko ya biblia.

**Utata.**Hii inarejea juu ya mashaka ambayo yanaleta matokeo katika nyaraka zilizoandikwa ambapo kuna maana mbili ziwezekanazo au zaidi au wakati vitu viwili au zaidi vinakuwa vikirejewa kwa wakati mmoja. Inawezekana kwamba Yohana anatumia utata huu kwa makusudi.

**Elimu ihusuyo tabia ya mwanadamu.** Inamaanisha kuwa na "tabia zinazohusiana na wanadamu." neno hili linatumika kueleza lugha zetu za kidini kumuhusu Mungu. Linatokana na neno la Kiyunani kumuhusu mwanadamu. Inamaanisha kwamba tunazungumza kuhusiana na Mungu kana kwamba Yeye alikuwa mwanadamu. Mungu anaelezwa katika umbo la mwili lionekanalo, kijamii, maneno ya kisaikolojia ambayo

yanahusiana na wanadamu (cf. Mwa. 3:8; II Wafalme 22: 19-23). Hii, hakika ni mshabihiano pekee. Hata hivyo maarifa yetu kumhusu Mungu, ingawa ni kweli, lakini yamewekewa mipaka.

**Shule ya Antiokia.**Hii njia ya ufasiri wa kibiblia ilianzia huko Antiokia, Syria katika karne ya tatu B.K. kama kuonyesha hisia juu ya utaratibu wa kiistiari wa Alexandria, huko Misri. Msingi wa msukumo wake uliangalia maana ya kihistoria ya Biblia. Ilitafasiri Biblia kama fasihi ya kawaida ya mwaadamu. Shule hii ilikuwa imejumuishwa katika ubishi kumhusu Kristo kama alikuwa na asili mbili (mafundisho kuhusu uwili wa Yesu) au asili moja (Mungu kamili na mwanadamu kamili). Ilitambuliwa kama maoni ya kupinga Ukristo kwa Kanisa Katoriki la Rumi na kuhamishiwa Uajemi lakini shule ilikuwa na umuhimu mdogo. Misingi ya kanuni zake za ufasili wa kibiblia baadaye ikawa kanuni za ufasili wa watu walioleta mageuzi kwenye dini ya Kiprostanti (Luther and Calvin).

**Kutabaini.** Hii ni moja miongoni mwa njia tatu za uwasilishaji wa neno uliotumika kudokeza uhusiano kati ya misitari ya ushairi wa Waebrania. Unahusiana na misitari ya ushairi yenye kukinzana kimaana (cf. Mit. 10:1; 15:1).

**Fasihi ya mafunuo.** Hii ilikuwa ni namna tanzu ya Wayahudi wenye nguvu, hata kuonekana ya kipekee. Ilikuwa ni aina ya uandishi wenye mafumbo uliotumika nyakati za uvamizi na umiliki dola yenye nguvu ya Kiyahudi. Inafikiriwa kwamba mtu, muumbwaji aliyekombolewa na Mungu na kuyatawala matukio ya ulimwengu, na kwamba Israeli ina upendeleo maalumu na uangalizi kutoka Kwake. Fasihi hii inahaidi ushindi mkuu na kupitia juhudi pekee za Mungu.

Ni ishara kuu na ya ubunifu sana yenye maneno ya mafumbo. Mara nyingi ilieleza ukweli katika rangi, tarakimu, maono, ndoto, upatanishi wa kimalaika, alama za siri za maneno, mara nyingi uwili wa vitu kati ya mema na mabaya.

Baadhi ya mifano tanzu hapa ni (1)katika Agano la Kale, Ezekieli (sura ya 36-48), Danieli (sura ya 7-12), Zekaria; na (2) Katika Agano Jipya, Mathayo 24;Marko 13; II Wathesalonike 2 na Ufunuo.

**Mtetezi.**Hili linatoka katika mzizi wa neno la Kiyahudi "ulinzi wa kisheria." Haya ni mafundisho ndani ya theolojia ambayo yanatafuta kutoa ushahidi na uwiano wa hoja za kifikra kwa imani za Kikristo.

**Haki ya kutangulia.**Kimsingi huu ni ukaribu wa maana ya neno "dhanio." Inahusisha ufikiliaji wa wa maana za awali zilizokubalika, kanuni au nafasi iliyosadikika kuwa kweli paspo uchambuzi au uchunguzi.

**Ufuasi wa Arius.**Arius alikuwa mhudumu ndani ya kanisa huko Aexandria, Misri katika karne ya tatu na mwanzoni mwa karne ya nne. Alikubali kwamba Yesu alikuwepo hapo kabla lakini si kwa Uungu (si sawa na asili ya Baba), huenda kwa kufuata Mithali8:22-31. Alipingwa na askofu wa Alexandria, ambaye alianza (B.K. 318) mabishano yalidumu kwa miaka mingi. Ufuasi wa Arius ulikuja kuwa kanuni rasmi katika Kanisa la huko Mashariki. Baraza la Nicaea katika 325 B.K.walimshtumu Arius na kuutetea usawa na Uungu kamili wa Mwana.

**Jamii ya watu wakuu.** Alikuwa mmoja wa wanafalsafa wa kale wa Ugiriki, mwanafunzi wa Pilato na mwalimu wa Iskanda Mkuu.Ushawishi wake, hata sasa, umefika maeneo mengi yanayofundisha mafunzo ya kisasa. Hii ni kwa sababu alisistiza maarifa ni kupitia uchunguzi na upambanuzi. Hii ni moja ya itikadi ya njia za kisayansi.

**Miandiko binafsi.** Hili ni jina lililotolewa kwa maandishi ya mwanzo ya Biblia. Maandiko haya asilia yaliyoandikwa kwa mkono yote yamepotea. Baadhi tu ya nakala zimesalia. Hiki ndio chanzo cha utofauti wa maandishi mbalimbali katika machapisho ya Kiebrania na Kiyunani.

**Maandiko ya asili ya karne ya sita.** Haya ni machapisho ya Kiyunani na Kiratini ya karne ya sita B.K. Yanasanifiwa na alama "D." Imejumuisha Injili na Matendo na baadhi ya Nyalaka za Jumla. Inabainishwa na nyongeza nyingi za maandishi yenye ueledi. Inaunda msingi wa "uundaji wa maandiko"ambayo ni tamaduni za machapisho makuu ya Kiyunani nyuma ya toleo la King James Version.

**Upendeleo.** Hili ni neno linalotumika kueleza maelezo yenye nguvu kuhusiana na jambo au mtazamo fulani. Ni mtizamo ambao uadilifu ndani yake hauwezekani kungalia kitu au maoni Fulani. Ni madhara ya kieneo.

**Mamlaka ya Kibiblia.** Ni neno lililotumika katika maana maana ya kipekee. Linaelezwa kama uelewa wa kile alichokisema mwandishi asilia katika siku zile zake na kutumia ukweli huu katika siku zetu. Mamlaka za Kibiblia mara nyingi zinaelezwa kuitazama Biblia yenyewe kama kiongozi chetu chenye mamlaka. Hata hivyo, katika hali ya sasa, utafasiri sio sahihi. Nimeweka mipaka juu a dhana ya Biblia kama ilivyotafsiriwa na kanuni za njia ya historia ya kisarufi.

**Orodha ya vitabu vya Agano Jipya.**Hili ni neno linalotumika kuelezea maandishi yanayosadikiwa kuvuviwa kipekee. Limetumika kuangalia maandiko yote ya Agano la kale na Agano jipya.

**Kristo kama kitovu.**Ni neno lililotumika kuonyesha Kristo kama kitovu cha mambo yote. Na lilitumiwa kuunganisha dhana ya kwamba Yesu ni Bwana wa Biblia zote, Mawazo ya Agano la Kale dhidi yake na utimilifu wa malengo yake.

**Fasiri.**Hii ni aina pekee ya utafiti wa kitabu. Inatoa kwa pamoja usuli wa kitabu cha Biblia. Pia inajaribu kuelezea maana ya kila kipengele cha kitabu. Baadhi inatazamisha matumizi, wakati mwiingine zinahusiana na andiko katika hali ya kiufundi. Vitabu hivi ni vya manufaa, lakini lazima vitumike baada ya mtu kufanya uchunguzi wake wa awali. Tafsiri za watoa maoni lazima zisikubalike kuhakiki. Ukilinganisha fasiri nyingi toka kwa mitizamo ya wanathiolojia tofauti utaona inasaidia.

**Itifaki.** Hii ni aina ya chombo cha utafiti kwa usomaji wa Biblia. Inaorodhesha kila utokeaji wa neno katika Agano Jipya na la Kale. Inasaidia katika njia tofauti: (1) kubainisha maneno ya Kiebrania au Kiyunani yaliyoko nyuma ya maneno ya kiingereza: (2) kulinganisha kurasa ambapo neno lile lile la Kiebrania au Kiyunani limetumika: (3) kuonyesha mahali ambapo maneno mawili tofauti ya Kiebrania au Kiyunani yametafasiriwa kwa neno lie lile la kiingereza: (4) kuonyesha mwendelezo wa kutumia maneno fulani katika vitabu fulani au maandishi: (5) inasaidia mtu kupata somo katika Biblia (cf. Walter Clark's *How to use New Testament Greek Study Aids*. kurasa za 54-55).

**Magombo ya Bahari ya Chumvi.** Inarejerea mlolongo wa maandiko ya kale yaliyoandikwa katika Kiebrania na Kiarama ambayo yalipatikana karibu na Bahari ya Chumvi mwaka 1947. Palikuwepo na maktaba za kidini ya Kiyunani ya karne ya kwanza. Msukumo wa umilikaji toka Rumi na vita ya kinazi vya miaka ya sitini viliwasababisha wao kuficha magombo yaliyokuwa yamefungashwa ndani ya vyungu kwenye mapango au mashimo. Inatusaidia sisi kuelewa muundo wa kihistoria wa palestina ya karne ya kwanza na kuthibitisha maandiko ya mossoretes kuwa yako sahihi kwa kiasi fulani enzi ya awali kabla ya Yesu B.C.

**Mambo yaliyofasiliwa.** Njia hii ya kimantiki au ufikiliaji inatokana na kanuni ya pamoja ya matumizi maalumu kwa njia ya wazo. Hii ni kinyume toka ufikiliaji wa mambo yaliyofasiriwa, ambayo yanaangazia njia ya kisayansi toka kwenye uchunguzi maalumu kwenda hitimisho la pamoja (nadharia)

**Mbinu pembuzi.**Hii ni njia ya kufikilisha ambapo kile kinachoonekana kuleta mkanganyiko au mafumbo huwekwa pamoja katika hali ya mkazo, ikitafuta jibu la pamoja ambalo linajumuisha pande zote za fumbo. Mafundisho mengi ya Biblia yana upembuzi unaofanana, kuamuliwa kabla-mapenzi huru, ulinzi-ustahimilivu, imani-kazi; uwamuzi-ufuasi; uhuru wa Mkristo-uwajibikaji wa Mkristo

**Wayahudi waliotawanyika katika mataifa mengine.**Hili ni neno la kiufundi la Kiyunani lililotumiwa na wapalestina wa Kiyahudi kuelezea wayahudi wengine walioishi nje ya mipaka ya kijiografia ya nchi ya ahadi.

**Mlinganyo wa nguvu.** Hii ni nadhalia ya ufasili wa Biblia. Tafasili ya Biblia inaweza kuangaliwa kama mwendelezo toka ushirika wa "neno kwa neno", mahali ambapo neno la Kiingereza lazima liwekwe kwa kila neno la Kiyunani au Kiebrania, kwenye "ufasili" ambapo tu wazo limetafasiliwa kwa angalizo la chini ya neno au kifungu cha awali.

Katika nadharia hizi mbili ndipo pana "mlinganyo wa nguvu" unaojaribu kuchukua neno la mwanzo kwa umakini wake, lakini limefasiliwa katika miundo ya visarufi vya kisasa na nahau. Majadiliano mazuri ya kweli ya hizi nadharia mbali mbali za fasili zinapatikana katika makala ya Fee na Stuart *How to Read the Bible For Its Worth,* uk. 35 na katika Robert Bratcher's utangulizi katika Biblia ya TEV.

**Kutofuata mfumo.** Neno hili linatumika katika mahusiano ya uhakiki wa maandiko. Unarejerea kitendo cha kuchagua usomaji toka machapisho tofauti tofauti ya Kiyunani ili kufika kwenye neno linalotakiwa kuwa karibu na maandiko ya mwanzo.

**Kupotosha maana.** Hili neno ni kinyume cha neno fasili ya maandiko. Kama fasili ya maandiko ni "kuondoa" kulingana na kusudio la mwandishi wa awali, basi neno hili litamaanisha "kuingiza" wazo la kigeni.

**Elimu ya asili na historia ya neno.** Hii ni dhana ya usomaji wa neno unaojaribu kuyakinisha maana ya awali ya neno. Kutokana na chanzo cha maana hii, utumiaji wa kipekee unaotambulika kirahisi katika ufasili, elimu ya asili na historia ya neno sio kiini cha mtizamo, mbali na maana ya wakati ule ule na utumiaji wa neno.

**Fasili ya maandiko.** Hili ni neno la kiufundi kwa utendaji wa kutafasili kifungu maalumu. Inamaanisha "uondoaji nje" (wa neno) ukidokeza kwamba dhumuni letu ni kuelewa kusudi la mwandishi wa mwanzo katika uelewa wa muundo wa kihistoria, mazingira ya kifasihi, sintaksi na maana ile ile ya neno.

**Namna ya Uwasilishaji.** Hili ni neno la Kifaransa ambalo limedokeza aina mbali mbali ya fasihi. Msukumo wa neno hili ni mgawanyiko wa miundo ya fasihi katika namna mbali mbali ambazo zinashirikishana tabia za aina moja. Usimuliaji wa kihistoria, mashairi, mithali, ufunuo na uandikishaji.

**Maarifa ya utambuzi/mafunuo.** Zaidi ya maarifa tulionayo kuhusu imani potofu yameletwa toka maarifa ya utambuzi wa maandiko katika karne ya pili. Ingawa mawazo ya awali yalikuwepo katika karne ya kwanza (na kabla). Baadhi ya maelezo ya mafunuo ya kinazi ya Valentino na Cerinthin ni (1) mwili na roho vyote vilikuwepo kabla. mwili ni mwovu, na Roho ni nzuri. Mungu, ambaye ni Roho hawezi kuhusishwa moja kwa moja na mwili mwovu (2) kuna asili (*eons au* daraja la kimalaika*)* kati ya Mungu na mwili. Wa mwisho au wa chini alikuwa YAHWE wa Agano la kale, ambaye aliuumba ulimwengu (*kosmos*); (3) Yesu alikuwa mwanzilishi kama YAHWE lakini akiwa juu ya viwango, karibu na Mungu wa kweli. Wengine walimweka juu zaidi lakini bado yu chini kuliko Mungu na hakika asiye na mwili wa Kiungu (cf. 1:14). Kwa vile mwili ni mwovu, Yesu asingelikuwa na mwili wa kibinadamu na bado akawa na hali ya Kiungu. Alikuwa ni nafsi ya kufikirika (cf. 1Yoh 1:1-3; 4:1-6); na (4) wokovu ulipatikana kupitia imani katika Yesu pamoja na maarifa maalumu, yaliyojulikana na watu maalumu. Maarifa (maneno ya siri) yalihiiitajika kupitia ulimwengu wa kimbingu. Washikiliaji sana wa kisheria za Kiyahudi nao pia walihitaji kumfikia Mungu. Walimu wa uongo wenye maarifa ya utambuzi walitetea miundo miwili kinzani ya kimaadili (1) baadhi ya stadi za maisha hazikuhusiana na wokovu. Kwao wokovu na utakaso ulifumbwa kwenye maarifa ya siri (neno la siri) kupitia ulimwengu wa kimalaika (*eons)*; au (2) kwa wengine stadi ya maisha ilikuwa muhimu katika wokovu. Walisisitiza miundo ya maisha kama kielelezo cha utakaso wa kweli.

**Kanuni za ufasili.** Hili ni neno la kiufundi kwa kanuni zinazoongoza ufasili wa maandiko. Ni seti ya mwongozo maalumu na sanaa/kipawa. Kibiblia, au takatifu, kanuni za ufasili zimegawanyika kwa namna mbili; kanuni za ujumla na kanuni maalumu. Hizi zinahusiana na aina tofauti za fasihi zinazopatikana katika Biblia. Kila aina tofauti (tanzu)zina mwongozo wake wa kipekee lakini zinashirikiana na baadhi ya dhana na namna ya utafasili.

**Uhakiki juu ya maandiko.** Hii ni namna ya utafasili wa kibiblia ambao unatazamisha kwenye muundo wa kihistoria na umbo la fasihi hasa hasa katika kitabu cha Biblia.

**Nahau.** Neno hili linatumika kwenye vifungu vinavyopatikana katika tamaduni tofauti zenye maana maalumu na sio vilivyohusiana na maana ya kawaida ya maneno binafsi. Maana ya mifano ya kisasa ni: "ilikuwa ni vizuri sana" au "umeniua". Biblia pia inajumuisha aina hizi za vifungu.

**Nuru.**Hili ni jina lililotolewa kwenye dhana kuwa Mungu aliongea na mwanadamu. Dhana nzima kwa kawaida imeelezewa kwa namna tatu: (1) ufunuo-Mungu ametenda kwenye historia ya binadamu: (2) uvuvio-ametoa utafasili sahihi wa matendo yake na maana yake kwa watu fulani waliochaguliwa kuweka kumbukumbu ya mwanadamu: na (3) nuru –ametoa roho wake kumsaidia mwanadamu kuelewa mafunuo yake.

**Kudukiza.** Hii ni njia ya kimantiki au kufikiria inayotoka sehemu Fulani na kuenea sehemu yote. Ni njia ya kutegemea majaribio ya kisasa. Kimsingi, huu ni mjongeo wa watu wenye hadhi ya juu.

**Unasaba.** Hii ni aina ya chombo cha uchunguzi kinachoruhusu wale wasiojua lugha za kibiblia kuchunguza maana yake na muundo. Inaweka tafasili ya kiingereza kwenye ngazi ya neno kwa neno chini ya lugha ya awali ya kibiblia. Chombo hiki kinajumuishwa na "misamiati ya kiuchunguzi" ambayi inatoa miundo na maelezo ya msingi ya Kiebrania na Kiyunani.

**Uvuvio.**Hii ni dhana ya kwamba mungu aliongea na mwanadamu kwa kuwalinda waaandishi wa kibiblia kwa usahihi na uwazi ili kuweka kumbukumbu ya mafunuo yake. Dhana nzima imeelezewa kwa namna tatu: (1) ufunuo-Mungu ametenda katika historia ya mwanadamu (2) uvuvio-ametoa utafasiri wasahihi wa matendo yake na maana yake kwa watu Fulani waliochaguliwa kuweka kumbukumbu ya mwanadamu: na (3) Nuru-ametoa roho wake kumsaidia mwanadamu kuelewa mafunuo yake.

**Lugha ya maelezo.** Hii inatumika pamoja na nahau pale Agano la Kale lilipoandikwa. Inaongelewa juu ya dunia kwa namna jinsi vitu vinavyotokea kwenye milango mitanmo ya fahamu. Sio maelezo ya kisayansi hata yakamaanisha kuwepo.

**Ushikiliaji sana wa sheria.** Mwenendo huu umeainishwa kwa msisitizo zaidi juu ya sheria au matambiko. Unajaribu kutegemea juu ya utendaji wa mwanadamu kama njia ya ukubalifu kwa Mungu. Unajaribu kushusha uhusiano na kuinua utendaji, mwote ambamo dhana muhimu ya mahusiano ya kimaagano kati ya Mungu mtakatifu na mwanadamu mtenda dhambi.

**Tafasili sisisi.** Hili ni jina jingine la mlengo wa kimaandiko na njia za kihistoria za za kanuni za ufasili toka Antiokia. Ina maana kwamba utafasili unahusika katika maana dhahili za lugha ya mwanadamu, ingawa inaendelea kutambua uwepo wa lugha za kitamathali.

**Fasihi tanzu.** Hii inarejerea kwenye miundo ya utofauti ili kwamba mawasiliano ya uwanadamu yanaweza kuchukuliwa kama vile ushairi au simulizi za kihistoria. Kila aina ya fasihi ina nji/namna yake maalumu ya kanuni ya ufasili kwa kuongezea kwenye kanuni za pamoja kwa fasihi zote zilizoandikwa.

**Sehemu ya fasihi.** Hii inarejerea mgawanyo wa lengo kuu la kitabu cha Kibiblia. Inaweza kuundwa na misitari, aya, au ibara chache. Ni kijumuishi pekee chenye kiini cha somo.

**Lower criticism- Uhakiki wa kawaida wa maandiko.**

**Maandiko ya asili.** Neno hili linahusiana na nakala mbali mbali za Agano jipya la Kiyunani. mara nyingi limegawanyika katika aina tofauti kwa (1) nyenzo iliyotumika kuandikiwa kwayo (mafunjo, ngozi) au (2) muundo wenyewe wa uandishi. Limefupishwa kwa neno "MS" (umoja) au "MSS" (wingi).

**Andishi la kidesturi la Kiebrania la Biblia ya Kiyahudi.** Hii inarejerea karne ya nane A.D. maandiko ya asili ya Kiebrania ya Agano la kale yalitolewa na vizazi vya wasomi wa Kiyahudi ambayo yalijumuisha alama za irabu na mihtasari mingine ya maandiko. Yanatengeneza msingi wa neno kwa Agano letu la kale la Kiingereza.

**Mshabihiano wa neno.** Huu ni namna ya msemo ambao jina la kitu linatumika mbadala wa kitu kingine kinachofanana nacho. Kwa mfano " birika linachemka" ki uhalisia inamaanisha "maji yaliyeko kwenye birika yanachemka".

**Orodha ya vitabu vya Agano jipya.** Hii ni orodha ya vitabu vya sheria za kanisa la Agano jipya. Iliandikwa huko Rumi kabla ya mwaka 200 A.D. Inatoa vitabu ishirini na saba kama vile vile vya Agano Jipya la Waporostanti. Hii wazi kabisa inaonyesha makanisa madogo madogo ya mahali katika sehemu mbali mbali za milki ya Rumi kulikuwa "kiutendaji" pamewekwa sheria za kanisa kabla ya baraza kuu la kanisa la karne ya Nne.

**Ufunuo wa asili.** Hii ni namna ya Mungu mwenyewe kujifunua kwa mwanadamu. Unajumuisha utaratibu wa kiasili (Rum 1:19-20) na dhamila adilifu (Rum 2:14-15). Umeongelewa katika Zaburi 19:1-6 na Warumi 1-2. Unatofautishwa toka kwenye mafunuo maalumu, ambayo kwa mungu mwenyewe ni muhimu kujifunua katika Biblia na mwanae pekee Yesu wa Nazareti. Uangaliaji huu wa kithiolijia unasisitizwa tena na mwenendo wa "dunia ya zamani" kati ya wanasayansi wa Kikristo (cf. maandishi ya Hagh Ross) wanatumia uangaliaji huu kwa kuthibitisha kuwa kweli yote ni kweli ya Mungu. Ulimwengu ni mlango ulio wazi wa maarifa ya kumjua Mungu; ni tofauti toka kwa ufunuo maalumu (Biblia); unawapa wanasayansi uhuru wa kufanya uchunguzi juu ya utaratibu wa kiasili. Kwa maoni yangu , hii ni fursa mpya ya ajabu kushuhudiwa juu ya wanasayansi wa ulimwengu wa magharibi.

**Ufuasi wa Nestory.** Nestory alikuwa ni mkuu wa familia ya Constantino kwenye karne ya tano. Alifundishwa huko Antiokia ya Syria na kuthibitisha kwamba Yesu ana asili mbili, moja ni mwanadamu kamili na nyingine ni Mungu kamili. Maoni haya yalichepushwa toka kwenye mtizamo wa asili wa mtu mmoja wa Orthodox kutoka Alexandria. Kusudio kubwa la Nestory lilikuwa ni cheo cha "mama wa Mungu" alichopewa Maria Magdalena. Nestory alipingwa na Cycil wa Alexandria na, kwa kuwekwa matatani juu ya mafundisho yake huko Antiokia. Antiokia yalikuwa makao makuu ya mtazamo wa kihistoria wa visarufi vya maandiko kwa utafasili wa Kibiblia, wakati Alexandria yalikuwa makao makuu ya shule Nne zilizotengwa kwa ajili ya utafasili. Nestory hatimaye aliondolewa toka ofisini na kukimbilia mafichoni.

**Mwandishi wa awali.** Hii inarejerea wandishi halisi wa maandiko

**Mafunjo/Magombo.** Haya yalikuwa aina mojawapo ya nyenzo toka Misri zilizotumika kuandikiapo maandiko. Yalitengenezwa kwa majani au magome ya miti. Ni nyenzo ambazo nakala za zamani Agano la Kale la Kiyunani zilihifaziwapo.

**Vifungu Mlinganyo**. Ni sehemu ya mtazamo kuwa yote yaliyomo kwenye Biblia yametoka kwa Mungu na, kwa hiyo, ni ufafili wake mahsusi na mlinganyo wa kweli wa kimafumbo. Hili pia ni la msaada pale mtu anapojaribu kutafasili kifungu kisicho wazi au kigumu. Pia inamsaidia mtu kupata kifungu kilicho wazi juu ya somo husika vile vile mtazamo wote wa kimaandiko juu ya somo husika.

**Ufafanuzi/fasili.** Hili ni jina la nadhalia ya utafali wa Biblia. Utafasili wa Biblia unaweza kuangaliwa kama mwendelezo wa mahusiano wa "neon kwa neon" ambapo neon la Kiingreza laweza kuweka kwa kila neon la Kiebrania au Kiyunani kwenye "fasili" ambapo tu wazo limetafasiliwa kwa mtizamo wa kawaida wa neon au kifungu cha awali. Kati ya nadhalia mbili hizi "mlinganyo wa nguvu" ambao unajaribu kuchukuawa kwa umakini andiko la awali lakini likatafasiliwa katika muundo wa kisasa wa kisarufi na nahau. Kweli kabisa mjadara mzuri wa nadhalia hizi mbali mbali za utafasili zinapatikana katika chapisho la Fee na Stuart *How to Read the Bible For All Its Worth, Uk. 35.*

**Aya.** Huu ni msingi wa ufasili wa fasihi moja kinadhalia. Unajumuisha wazo moja kuu na mwendelezo wake. Tukibaki na musukumo wake mkuu hatutatazama juu ya udogo wake au uzuri wa kusudi la mwandishi wa awali.

**Uparokia.** Hii inahusiana na mapendeleo yaliyofungiwa kwenye muundo wa tamaduni/ thiolojia ya kawaida. Haitambui asili ya mapokeo ya kweli yaliyobadilika ya Kibiblia au matumizi yake.

**Fumbo.** Hii inarejerea kweli zile zinazoonekana kuleta mkanganyiko, nab ado zote zikabaki kuwa kweli, ingawa bado zinakinzana. Zinaunda kweli kwa kuwakilisha toka pande zilizo kinyume. Kweli nyingi za Kibiblia zinawakilishwa kimafumbo (au kiupembuzi). Kweli za Kibiblia sio kama nyota zilizotengana, zimetengenezwa kwa ukilimio wa sehemu za nyota.

**Pilato.** Alikuwa ni mmoja ya wanafalsafa wa Ugiriki ya kale. Falsafa yake kwa kiasi kikubwa ulisababisha kanisa la mwanzo kupitia wasomi wa Alexandria, Misri na baadaye, Augustino. Alituma ujumbe kuwa kila kitu duniani ni kiini macho na ni mfano tu wa kielelezo asili wa vitu vya rohoni. Baadaye wanathiolojia wakasawazisha "mtizamo/mawazo" ya Pilato na ulimwengu wa kiroho.

**Dhanio.** Hili linarejerea uelewa wa jambo tulilowaza kabla. Mara nyingi tunaunda wazo au hukumu kuhusu mambo hata kabla hatujatazamisha maandiko yenyewe. Uelekezaji huu vile vile hujulikana kama upendeleo, kujitanguliza mbele, kudhania au kuelewa kabla.

**Uhakiki wa maandishi.** Hiki ni kitendo cha kutafasili maandiko kwa nukuu za kifungu bila kuangalia mazingira ya haraka au ukubwa wa mazingira katika fahisi moja. Hii inaondoa vifungu toka kwa kusudio la mwandishi wa awali na mara nyingi unahusha jaribio la kuhakiki maoni binafsi wakati huo likithibitisha mamlaka ya Kibiblia.

**Ualimu wa dini ya Kiyahudi.** Ngazi hii ya maisha ya watu wa Uyahudi yalianza walipokimbilia Babel (586-538 B.C). kama ushawishi wa makuhani na hekalu ulivyoondolewa, masinagogi ya kawaida yakawa mtizamo wa maisha ya Kiyahudi. Hivi vitovu vya kawaida vya tamaduni za Kiyahudi, ushirika, kuabudu na elimu ya Biblia ikawa mtizamo wa maisha ya kidini kitaifa. Katika siku za Yesu, hii "dini ya wandishi" ilikuwa sambamba na ile ya makuhani. Katika kuanguka kwa Yerusalem mwaka wa 70 A.D muundo wa kiandishi, ukitawaliwa na mafalisayo, walidhibiti mwelekeo wa maisha ya kidini ya Kiyahudi. Inachagizwa na utafasili wa kiutendaji, na wa kisheria wa Torah kama ulivyoelezwa katika tamaduni za Talmud.

**Ufunuo.** Hili ni jina lililopewa kwenye dhana ya kwamba Mungu amesemezana na mwanadamu. Wazo zima mara nyingi limeelezewa katika maneno matatu- (1) Ufunuo-Mungu ametenda katika historia ya mwanadamu (2) Uvuvio-Ametoa tafasili sahihi ya matendo yake na maana yake kwa mtu Fulani aliyemchagua kuweka kumbukumbu ya mwanadamu (3)Nuru-Amempa Roho wake kumsaidia mwanadamu kuelewa ukaribu wake.

**Elimu-maana.** Hii imerejerea kipimo halisi cha maana kinachohusiana na neno. Kimsingi ina vidokezo mbali mbali vya neno katika mazingira tofauti.

**Maandiko ya kale ya Kiyunani.** hili ni jina lililopewa tafasili ya Kiyunani ya Agano la kale la Kiebrania. Mafundisho ya zamani yanasema kuwa yaliandikwa kwa siku 70 na wasomi sabini wa Kiyahudi kwa ajili ya maktaba ya Alexandria, Misri. Tarehe ya kimapokeo ilikuwa 250 B.C (kiukweli yawezekana ilichukua zaidi ya miaka Mia kumaliza kuandika). Tafasili hii ni muhimu kwa sababu (1)inatupatia andiko la kale kulinganisha na andiko la Kiebrania (2) inatuonyesha sisi hali ya utafasili wa Kiyahudi katika karne ya pili nay a tatu B.C (3) inatupatia uelewa wa umasihi wa Kiyahudi kabla ya kumkataa Yesu. Kifupi chake ni "LXX".

**Machapisho ya asili.** Haya ni machapisho ya asili ya Kigiriki ya karne ya Nne A.D. Yalivumbuliwa na msomi wa Kijerumani, Tischendorf, katika nyumba ya mtawa Catheline, kwenye eneo la kimila la mlima Sinai. Maandishi haya yameundwa na herufi ya kwanza ya Kiebrania ya alfabeti inayoitwa "*eleph*" (א). Yanajumuisha Agano la Kale na Agano Jipya kwa pamoja.

**Kujitakasa.** Hili neno ni kisawe chenye istiari katika maana kuwa linakwenda mpaka kwenye historian a mazingira ya fasihi ya kifungu na kulifasili katika msingi wa jambo lingine.

**Visawe.** Hii inarejerea maana yenye kariba au mfano wa maana moja (ingawa kiukweli hakuna maneno mawili yenye elimu-maana kamili iliyopishana). Kwa karibu sana yanahusiana kiasi kwamba moja linaweza kuwa mbadala wa lingine katika sentesi bila kupoteza maana. Pia yanatumika kuunda moja kati ya miundo mitatu ya mlinganyo wa ushairi wa Kiebrania. Kwa maana hii inarejesha mistari miwili ya ushairi ambayo inaelezea kweli ile ile (cf. Zab 103:3).

**Sintaksi.** Hili ni neno la Kiyunani linalirejeresha muundo wa sentesi. Inahusiana na namna ya sehemu ya sentesi zinaweza wekwa pamoja kuleta maana kamili.

**Usanisi.** Hii ni moja ya maneno matatu yanayohusiana na aina ya ushairi wa Kiebrania. Neon hili linaongelea juu ya mistari ya ushairi uluojengwa juu ya mwingine katika maana moja, wakati mwingine huitwa "taaluma ya mabadiliko ya hali" (k.v. Zab 19:7-9).

**Thiolojia mpangilio.** Hii ni hatua ya utafasili ambayo inajaribu kuhusisha ukweli wa Biblia katika hali ya pamoja na mlingano. Ina mantiki zaidi kuliko historia tupu, ni uwasilishaji wa thiolojia ya Kikristo kwa namna ( Mungu, mtu, dhambi,wokovu).

**Buku la taratibu na kanuni za Kiyahudi.** Ni wadhifa uliokuwapo kwa ajili ya upangaji wa simulizi za kanuni na taratibu za Kiyahudi. Wayahudi wanaamini ulitolewa kwa Musa kwa kusimuliwa na Mungu kwenye mlima Sinai. Ki-ukweli inaelekea kuwa ni mkusanyiko wa hekima za walimu wa Kiyahudi kwa miaka mingi. Kuna matoleo mawili tofauti yaliyo andikwa juu ya Talmud: ya Babel na fupi la kiparestina ambalo halikwisha.

**Uhakiki wa tofauti za kiuandishi.** Huu ni usomaji wa maandiko wa Biblia. uhakiki wa maandiko ni muhimu kwa sababu hakuna maandiko ya mwanzo yaliyopo na nakala zilizopo zinatofautiana toka moja hadi nyingine. Unajaribu kuelezea utofauti na kufika (karibu iwezekanavyo) na maneno ya awali kabisa ya miandiko ya Agano la kale na jipya. Mara nyingi unaitwa "uhakiki wa asili ya neno".

**Upokeaji wa Maandiko.** Usanifishaji huu ulianzia kwenye toleo la Elzevir la Agano jipya la Kiyunani katika mwaka wa 1633 A.D. Kimsingi ni muundo wa Agano jipya la Kiyunani lililozalishwa toka kwenye maandiko machache ya asili ya Kiyunani na matoleo machache ya Erasmo ya Kilatini (1510-1535), Stephano (1546-1559) na Elzevir (1624-1678). Katika *An Introduction to the Textual Criticism of The New Testament uk. 27 cha A.T Robertson* anasema "andiko la Byzantine kiutendaji ni aina ile ile ya uundaji wa maandiko. Andiko la Byzantine ni la thamani ya chini kati ya familia tatu ya maandiko ya awali ya Kiyunani (Kimagharibi, Alexandria na Byzantine). Inajumuisha mkusanyiko wa makosa ya karne nyingi za maandiko na nakala za mkono. Hata hivyo, A.T Robertson alisema uundaji wa maandiko umetunza kwa ajili yetu andiko sahihi kimalidhawa (uk.21). Mapokeo haya ya maandiko ya asili ya Kiyunani (hasa Erasmo, toleo la tatu la 1522) yanatengeneza msingi wa toleo la King James la mwaka 1611 A.D.

**Sheria za Musa.** Hili ni neno la Kiebrania lenye maana ya "ufundishaji". Lilitokea kuwa wadhifa rasmi wa maandishi ya Musa (Mwanzo mpaka Kumbu kumbu la Torati). Kwa Wayahudi ulikuwa ni mgawanyo wa kimamlaka wa kanuni za kanisa la Kiebrania.

**Uanishaji.** Hii ni aina ya urasimishaji wa wa utafasili. Mara nyingi unahusisha kweli ya Agano jipya inayopatikana katika vifungu vya kale kwa njia ya analojia. Namna hii ya kanuni za ufasili ilikuwa ni dalili kubwa ya njia za Alexandria. Kwa sababu ya matukano ya aina hii ya utafasili, mtu lazima aweke ukomo wa matumizi yake kwa mfano mahsusi ulioandikwa katika Agano jipya.

**Maandiko ya Vatican.** Haya ni maandiko ya asili ya Kiyunani ya karne ya Nne A.D . Yalipatikana kwenye maktaba ya Vatican. Uwasili wake unajumuisha vitabu vyote vya Agano la kale, ufunuo na Agano jipya. Hata hivyo, sehemu

zingine zilipotea( Mwanzo, Zaburi, Waebrania, Filemon na Ufunuo). Inasaidia maandiko ya asili kubadilisha miandiko ya maneno ya awali. Tena yameundwa kwa herufi kubwa “B”.

**Tafasili ya Biblia ya Kilatini.** Ni jina la tafasili ya Biblia ya Kilatini ya Jerome. Ilikuwa ndio msingi au utafasili wa “kawaida”wa kanisa Katoriki la Rumi. Lilifanyika mwaka 380 A.D.

**Hekima ya Fasihi.** Hii ni fasihi tanzu iliyozoeleka enzi za kale karibu na pande za Mashariki (na ulimwengu wa kisasa). Kimsingi lilikuwa ni jaribio la kuelekeza kizazi kipya juu ya mwongozo wa maisha ya ushindi kupitia ushairi, mithali, au insha. Ilielezewa zaidi kwa watu binafsi kuliko kwenye jumuiya iliyoungana. Haikutumia viini macho kuweka historia, lakini ilisimamia uzoefu na uchunguzi wa maisha katika Biblia, Ayubu kupita Wimbo ulio Bora, anasadiki uwepo na ibada ya YAHWE, lakini mtizamo huu wa ulimwengu wa kidini sio wa wazi kwa uzoefu wa kila mtu kila wakati.

**Picha ya ulimwengu na Mtizamo wa Kidunia.** Haya ni maneno mwandani. Yote yana dhana ya kifalsafa kuhusiana na uumbaji. Neno “picha ya ulimwengu” inarejerea “kwa namna gani” juu ya uumbaji wakati “mtizamo wa kidunia” unahusiana na “nani.” Maneno haya yote ni muhimu kwenye utafasili pale mwanzo 1-2 inaposhughulika hasa hasa na nani, na sio kwa namna gani juu ya ulimwengu.

**YAHWE/YEHOVA.** Hili ni jina la Agano la Mungu katika Agano la kale. Linaelezewa katika kitabu cha Kutoka 3:14. Ni muundo wa KISABABISHAJI wa neno la Kiebrania “kuwa” ambalo Wayahudi waliogopa kulitamka jina hili ili wasilitamke bure; kwa hiyo, walitumia jina lingine badala yake yaani “Adonai” likimaanisha “Bwana”. Hivi ndivyo jina la Agano limetafasiliwa katika Kiingereza.

# MAELEZO YA KIMAFUNDISHO YA BOB

Mimi siangalii hasa habari za imani au kanuni za imani. Napendelea kuthibitisha Biblia yenyewe. Ingawa, natambua kuwa habari ya imani itawaleta wale tusiojuana ili kupima mtizamo wa mafundisho yangu. Katika siku zetu za leo zenye makosa mengi ya kithiolojia na upotofu, natoa muhtsari mfupi wa thiolojia yangu kama ufuatavyo.

1. Biblia, yote katika Agano la Kale na Agano Jipya, ni neon la Mungu lililovuviwa, lenye uhakika, lenye uzima na lenye mamlaka. Ni ufunuo pekee wa Mungu ulioandikwa na watu chini ya uongozi wa nguvu za ajabu (Angalia MADA MAALUM: UVUVIO[SPECIAL TOPIC: INSPIRATION). Ni kiini pekee cha ukweli sahihi kuhusu Mungu na Kusudi Lake (Angalia Mada Maalum: Mpango wa YHWH wa Ukombozi (Special Topic: YHWH's Eternal Redemptive Plan). Pia ni kiini pekee cha imani na utendaji wa kanisa lake.
2. Kuna Mungu mmoja tu wa uzima, uumbaji na ukombozi (Angalia MADA MAALUM: UWEPO WA MUNGU MMOJA (SPECIAL TOPIC: MONOTHEISM). Yeye ndiye muumbaji wa vitu vyote, vionekanavyo na visivyo onekana. Amejidhihilisha mwenyewe kama Mungu wa upendo na anayejali ingawa pia ni Mungu asiye na upendelea. Amejidhihilisha mwenyewe katika nafsi tatu tofauti: Baba, Mwana na Roho; haswa wanatengana lakini wanafanya kazi moja (Angalia MADA MAALUM: UTATU(SPECIAL TOPIC: TRINITY).
3. Muda wote Mungu yuko hai kuangalia ulimwengu huu. Kuna mpango wa ndani wa uumbaji wake usiobadilika na mtazamo wa kipekee unaomfanya binadamu kutenda mapenzi huru. Hakuna kinachoweza kutokea pasipo ruhusa na maarifa ya Mungu, bado anaruhusu uchaguzi kwa wote malaika na wanadamu. Yesu ni chaguo la Baba na wote kimanufaa wamechaguliwa katika Yeye. Ufahamu wa mbele wa Mungu kuhusu matukio hayampunguzii binadamu kubainisha maandiko yaliyoandikwa kabla. Wote tunahusika kwa mawazo yetu na matendo (Angalia Majaaliwa (Calvinism) Dhidi Ya Mapenzi Huru Ya Kibinadamu (Arminianism) Predestination (Calvinism) vs Human Free Will (Arminianism)
4. Binadamu, japo aliumbwa kwa sura ya Mungu na mbali na dhambi, aliamua kumwasi Mungu. Ingawa alijaribiwa na kitu chenye nguvu ya ziada (Angalia MADA MAALUM: UOVU BINAFSI (SPECIAL TOPIC: PERSONAL EVIL). Adamu na Hawa waliwajibika kwa utashi wao wenyewe kuamua. Uasi wao umeathiri utu wa uumbaji. Watu wote tunahitaji rehema na huruma ya Mungu yote kwa hali ya ushirika katika Adamu na uasi binafsi wa hiari.
5. Mungu anatoa aina ya msamaha na urejesho kwa binadamu aliyeanguka. Yesu Kristo, Mwana pekee wa Mungu Baba, akawa mwanadamu, akaishi maisha yasio na dhambi, na kwa kifo chake mbadala, akalipa malipo ya dhambi ya mwanadamu. Ndiyo njia pekee ya kurejesha ushirika wetu na Mungu. Hakuna njia nyingine ya wokovu isipokuwa kupitia imani ya kazi yake aliyoimaliza.
6. Kila mmoja wetu binafsi yampasa kupokea ahadi ya msamaha na urejesho katika Kristo. Hilo linatimizwa kwa njia ya imani ya hiari katika ahadi za Mungu kupitia Kristo Yesu na kugeuka kwa mapenzi huru kwa dhambi inayojulikana Tazama Mada Maalum:Ina Maana Gani "Kupokea" "Kusadiki" "Kukiri/Kutubu" na "Kusihi"? (Special Topic: What Does It Mean to "Receive," "Believe," "Confess/Profess," and "Call Upon"?)
7. Sisi sote tumesamehewa jumla na urejesho umelenga juu ya kuamini(Mada Maalum: "Kuamini" Katika Agano Jipya(Special Topic: "Believe" in the NT)katika Kristo na toba toka dhambini (MADA MAALUM: TOBA[AGANO JIPYA] SPECIAL TOPIC: REPENTANCE (NT) Ingawa, ushahidi wa mahusiano mapya unaonekana katika mabadiliko na badiliko endelevu. Dhumuni la Mungu kwa wanadamu sio tu kwenda mbinguni siku moja, lakini kufanana na Kristo kwa sasa. Wale wote ambao wanakombolewa kweli ingawa wakati mwingine wanatenda dhambi, wataendelea katika imani na toba siku zao zote za maisha.

8. Roho Mtakatifu ni “Yesu mwingine”(Mada Maalum: Yesu na Roho(Special Topic: Jesus and the Spirit) Yuko duniani kuwaongoza wale wote waliopotea katika Kristo na kujenga ufanano wa Kristo katika kuokolewa. Karama za rohoni zinapewa toka kwenye wokovu. Ni maisha na huduma ya Yesu yaliyogawiwa katika mwili wake, yaani kanisa. Vipawa 358 ambavyo kimsingi ndio mwelekeo na msukumo wa hitaji la Yesu likihamasishwa na tunda la Roho. Roho yu hai katika siku zetu kama alivyokuwa katika enzi za Biblia.
9. Baba amemfanya Yesu Kristo aliyefufuka kama mwamuzi w vitu vyote. Atarudi duniani kuhukumu wanadamu wote. Wale wote walioamini Yesu na majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima cha mwanakondoo watapata mwili na utukufu ataporudi. Wataishi nae milele. Ingawa, wale wote walioikataa kweli ya Mungu watatengwa milele toka katika furaha ya ushirika wa Mungu wa Utatu. Watahukumiwa pamoja na shetani na malaika zake. Hii hakika haijaisha au kukamilika lakini natarajia itakupa ladha ya kithiolojia ya moyo wangu, nafurahia maelezo:

“Katika mambo ya msingi-umoja, mambo yaliyo ukingoni-uhuru, katika mambo yote-upendo.

# MITAZAMO TOFAUTI JUU YA UJIO WA MARA YA PILI

## UTANGULIZI

A. Mada hii imesababisha mabishano makubwa
B. Kwa namna gani haijulikani, ni lini haijulikani, lakini tukio ni la uhakika
C. Umekipata wapi kile unachokiamini
D. Ni nini dhumuni la ujio wa pili
E. Je? Biblia inafundisha hatua kwa hatua mambo ya kiama
F. Kwa nini watu wa enzi hii wako na shauku juu ya ujio wa pili
G. Nadharia zote zinazohusu ujio wa Yesu kimwili ni zile zenye mitizamo ya kale

## KANISA LA MWANZO KABLA YA UTAWALA WA MIAKA 1000 (Utawala wa miaka 1000 kabla kihistoria)

Kufanyika Binadamu kupalizwa

Uumbaji Miaka 6000 ↓ † ↑ ↓ Miaka 1000 ℓ Hukumu

Siku 6 za Uumbaji Ujio wa pili siku 7 za uumbaji

**Matarajio**

1. Historia ya dunia inafanana Na siku 7 za uumbaji (waraka Wa Barnaba, Ireneus, Methodius)
2. Siku moja inawakilisha miaka 1000 (2 Petro 3:8; Zab.90:4)

**Wathibitishaji**

1. Papius Irenius, Justine Martyr, Tartullian Hippolytus, Methodius
2. George Ladd(utawala wa miaka 1000 kabla kihistoria

**Kulifanya dhabiti**

1. Matukio Fulani lazima yatok ee kabla ya ujio wa pili
   a. Injili kwa mataifa yote (Mat.24:14)
   b. Kuongoka kwa Israel (Rum. 11:25 na kendelea)
   c. Uasi mkubwa (Mat.24:10; 2 Thess. 2:3)
   d. Dhiki kuu (Mat. 24:21)
   e. Kumdhihilisha mwana mwana wa uasi-mpinga Kristo (2 Thess. 2:3) Kuonekana,unyakuo wa Wote, na ujio

## UTAWALA WA MIAKA 1000 (unatambuliwa au kuanzisha miaka 1000)

Kufanyika binadamu kupalizwa

Uumbaji ↓ † ↑ ↓ ℓ Hukumu

Kalvary Ujio wa mara ya_pili

**Matarajio**

1. Kanisa ni Israel ya kiroho (Gal. 3:9,29; 6:16; Rum.2:5,9 28-29, Ufu.1:6; 1Petr.3:6)
2. Agano moja (Agano la Klae na Jipya, Rum.4-Ibraham ni mfano

**Wathibitishaji**

1. Baadhi ya makasisi wa kanisa la mwanzo
2. Augustino

**Kulifanya thabiti**

1. Ushindi ulioshinda pale kalvary
2. Shetani bound now

| | | |
|---|---|---|
| Paulo kwa kuhesabiwa haki Kwa imani) | | |
| 3. Ufalme wa Kristo sio wa muda (Yoh. 18:36) | 3. Zwingli | 3.Umoja wa mpango wa Mungu Wa ukombozi |
| 4. Ujio mmoja wa mara ya pili | 4. Calvin (mshirika wa Presbytarian | |
| Ufufuo mmoja | 5. Ray Summer (Baptist) | |
| Hukumu moja | 6. Jay Adamu(aliyeongoka) | |
| Ufalme wa milele | 7. Mengi ya makanisa ya Wakristo) | |

**UTAWALA WA YESU BAADA YA MIAKA 1000 (**Miaka 1000 sasa)

Kufanyika binadamu kupalizwa

Uumbaji † ℓ Hukumu

Kalvary ujio wa pili

(Miaka 1000)

| Matarajio | Wathibitishaji | kulifanya thabiti |
|---|---|---|
| 1. Juhudi za mwanadamu zitatimizwa Kama huko mbinguni | 1.Jonathan Edward | 1.Uchukulie ujio wa mara ya pili kwa umakini |
| 2. Mambo yanaendelea kuwa sawa | 2. A.H. Strong | 2. Mwanadamu ana sehemu katika mpango wa Mungu |
| | 3. W.T. Conner | 3. Kuwa na tumaini kuhusu Tamaduni ya wakati ule ule |
| | 4.Wasomi wengi wa karne ya 19 | |

**MPANGO WA MUNGU WA YESU KURUDI KABLA**

Majuma 69 ya Daniel

Unyakuo wa siri/ Kutwaliwa (2 Kor.5:10

Hukumu ya waaminio

Hukumu ya mataifa Ufu.20:7-10 Mat.25

Kipindi kifupi cha shetani

Maagano kadhaa (Adamu na Musa)

† (kipindi cha kanisa)

Kufanyika Mwanadamu

Kalvary

kuja kwa siri

Majuma 70 ya Danieli

Kuja kwa wazi

Hukumu ya Mwisho

1. Kuna mitazamo 3 juu ya huu ujio wa siri
   1) Wale wanaoamini unyakuo utatokea kabla ya dhiki kuu
   2) Wale wanaoamini unyakuo utatokea wakati wa dhiki kuu
   3) Wale wanaoamini unyakuo utatokea baada ya dhiki kuu
2. Hukumu ya waaminio(2 Kor. 5:10)
3. Hukumu ya mataifa (Mat.25

**Matarajio**

1. Biblia imegawanyika katika Migawanyo 7 tofauti
2. Utimilifu wa wazi wa kila Unabii wa agano la kale Kwa Israel
3. Kanisa na Israel moja kwa moja Vinatengana, kanisa ni mpango B wa Mungu pindi wayahudi Walipomkataa Yesu kama Masihi
4. Kanisa litanyakuliwa kwa siri Kabla ya dhiki kuu. Kitabu Cha ufunuo, baada ya sura Ya 5, inahusu Wayahudi
5. Agano Jipya linafasiliwa Katika mwanga wa unabii Wa agano la kale


**Wathibitishaji**

1. John Darby(Plymouth Brethren)
2. Clarence Larkin
3. D.I. Moody
4. C.I. Scofield(reference Bible)
5. Dallas Seminary (Pentecoste, Ryrie, Walvoord)
6. W.A. Criswell (Southern Baptist)
7. Hal Lindsay
8. Tim LaHaye
9. Bible Churches (Dallas Seminary)

**kulifanya thabiti**

1. Kuuchukulia unabii wa Biblia kimakini
2. Ujio wa wakati wowote (Mat. 24:40-42)

## <u>HOJA YA MAJARIBIO YA BOB</u> (Kutawala kwa Yesu kabla/baada/kutokuwepo kwa miaka 1000 kihistoria)




**Matarajio**

1. Mpango mmoja (Mwa. 3:15)
2. Umoja wa watu wa Mungu (Rum 2:28-29; 4; Gal.3:29; 6:16)
3. asili ya matukio ya siku ya mwisho Daniel, Ezekiel, na Ufunuo (namna ya uwasilishaji wa fasihi)
4. agano la kale linatazama kwenye ujio wa mara moja (Enzi mbili/Nyakati mbili) Enzi moja ni ujio wa wazi
5. Ujio mmoja wa wazi

Unyakuo mmoja (1Thes.4:13-18)
Ufufuo mmoja
Hukumu moja (Mat. 25, ufu 20)
Ufalme wa milele

**Mvutano wa kipembuzi**

1. Kati ya mifano ya agano la kale na mifano ya Kitume ya agano jipya
2. Kati ya wale wenye kuamini uwepo wa Mungu mmoja(Mungu mmoja kwa wote) na uchaguzi wa Israel
3. Kati ya kipengere cha kimasharti cha maagano ya kibiblia na ahadi (kama………tena) na waaminifu wasio na masharti
4. Kati ya fasihi ya Mashariki ya karibu na mifano ya fasihi ya Magharibi ya leo
5. Kati ya ufalme wa Mungu wa sasa na ule ujao
6. katikati ya imani ujio wa Kristo u-karibu na imani Kuwa baadhi ya matukio lazima yatokee kwanza

**Hitimisho**

1. John Calvin alisema juu ya kitabu cha ufunuo Kuwa Mungu pekee ndiye anayejua hili linamanisha Nini
2. Hakuna maoni ya wengi yaliyothibitisha juu ya Ujio wa mara ya pili
3. Kila kizazi cha waaminio wanalazimisha Biblia kwenye Miundo yao ya kihistoria na kitamaduni
4. Hakuna mpangilio sahihi wa mambo yajayo ya kiyama Katika agano jipya. Lakini ukweli umethibitishwa "kuwa tayari" na "kuwa katika utendaji"
5. Ni wale tu wasiopenda mabadiliko ndio wanapingana Na jambo hili
6. Ni kila kizazi cha waaminio wenye tumaini, kutiwa moyo, Wenye hamasa watarajiao ujio wa pili katika maisha yao

Haki miliki © 2000 na Bob Utley
Marshall, TX, BIBLE LESSON INTERNATIONAL
Haki zote zimehifadhiwa

# *UFUNUO*

*Uliniogopesha kiasi Fulani,*
*Huu ufunuo wa kutatanisha,*
*Lakini baadaye tena uliupelekea udadisi wangu*
*kuwa juu na kuchochea fikra zangu.*
*Lakini nimejifunza kuwa lazima niwe mwangalifu,*
*Kwa namna ninavyoutizama ujumbe,*
*Ili kuhakikisha siwi katika mfumo wa imani Fulani,*
*Na kuufafanua kwa uangalifu.*
*Nafahamu lugha iliyotumika ni ya kiishara,*
*Kwa hiyo siwezi kurupuka na kuwa huru na*
*ufasiri wangu ili kuondoa utata uliopo.*
*Namna ya uwasilishaji ni wa muhimu.*
*Lazima nikumbuke kuwa,*
*Kamwe nisifikiri majibu yangu ndiyo majibu pekee yaliyo sawia,*
*Lakini natumai kuwa niweze kuyasikia*
*Maneno yale Baba yampasayo kunena,*
*Angalia ujio wa Kristo kurudi tena,*
*Inaonyesha wengine kuwa Yeye ni njia, kweli na uzima,*
*Na baadaye nitakumbuka vile nijitahidivyo kila siku,*
*Katika wajibu wangu hapa duniani,*
*Kwamba Mungu apate kushinda,*
*Hutawala juu sana,*
*Yuko katika uthibiti.*
*Pat Bergeron 7/21/1999*